


Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

HISTORIA KUU YA AFRIKA •

Juzuu
Lililofupishwa

IV Afrika Kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi Karne ya Kumi na Sita

WAHARIRI J. KI-ZERBO • D.T. NIANE



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · IV

Afrika Kuanzia Karne ya Kumi na Mbili Hadi ya Kumi na Sita

MHARIRI J. KI-ZERBO na D. T. NIANE

Toleo Lililofupishwa

Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL IV

© UNESCO 1999

ISBN 9976 911 416

Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.

Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.

Toleo la Tafsiri ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.

Historia Kuu ya Afrika · IV

Afrika Kuanzia Karne ya Kumi na Mbili Hadi ya Kumi na Sita

Toleo Lililofupishwa

UNESCO Historia Kuu ya Afrika

- Juzuu I *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*
Mhariri J. Ki-Zerbo
- Juzuu II *Saarabu za Kale za Afrika*
Mhariri G. Mokhtar
- Juzuu III *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja*
Mhariri I. Irbek
- Juzuu IV *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*
Mhariri J. Ki-Zerbo na D.T. Niane
- Juzuu V *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*
Mhariri B.A. Ogot
- Juzuu VI *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi miaka ya 1880*
Mhariri J.F. Ade Ajayi
- Juzuu VII *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*
Mhariri A. Adu Boahen

Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi


- Juzuu VIII *Afrika Kuanzia 1935*
Mhariri A.A. Mazrui
Mhariri Msaidizi C. Wondji

**Toleo lililofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO
Limechapishwa na:**

**Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam, Tanzania**

**Pamoja na:
UNESCO Publishing
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris**

**Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha
Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.**



YALIYOMO

Dibaji na Amadou-Mahtar M'Bow aliyekuwa Mkurugenzi wa UNESCO (1974-87)	vii
Wasifu wa Mradi na B.A. Ogot, aliyekuwa Mwenyekiti, Kamati ya Kiyansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika	xii
Maelezo ya Wendo	xv
Wanakamati wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika	xvi
Orodha na Wasifu wa Waandishi waliochangia kwenye juzuu kuu	xviii
<i>1 Utangulizi</i>	<i>1</i>
<i>2 Kuunganishwa kwa Maghrib chini ya Wamohadi</i>	<i>10</i>
<i>3 Kuenea kwa ustaarabu Maghrib na athari kwa ustaaratu wa magharibi</i>	<i>29</i>
<i>4 Kusambaratika kwa umoja kisiasa katika Maghrib</i>	<i>41</i>
<i>5 Jamii katika Maghrib baada ya kuondoka Wa-Mohadi</i>	<i>54</i>
<i>6 Mali na Upamukaji wa pili na Wamande</i>	<i>62</i>
<i>7 Kuanguka kwa Himaya ya Mali: Karne ya kumi na tano hadi kumi na sita</i>	<i>86</i>
<i>8 Wasonghai tokea karne ya kumi na mbili hadi ya kumi na sita</i>	<i>94</i>
<i>9 Watu wa Falme za pindi ya Mto Niger na Bonde la Volta</i>	<i>107</i>
<i>10 Falme na watu wa Chad</i>	<i>120</i>

11	<i>Wahausa na Majirani zao katika Sudani ya Kati</i>	131
12	<i>Watu wa Pwani kuanzia Kasamansi hadi kwenye nyangwa za Cote d'Ivoire</i>	148
13	<i>Kuanzia Wangwa wa Cote d'Ivoire hadi Volta</i>	160
14	<i>Kutoka Volta hadi Kameruni</i>	167
15	<i>Misri Dunia ya Kiislamu kutoka karne ya 12 hadi mwanzoni mwa karne ya 16</i>	183
16	<i>Nubia toka miaka ya mwishoya Karne ya 12 hadi utamalaki wa Wafunji</i>	196
17	<i>Pembe ya Afrika: Wasulemani katika Ethiopia na madola ya Pembe ya Afrika</i>	208
18	<i>Maendeleo ya Ustaarabu wa Waswahili</i>	222
19	<i>Kati ya Pwani na Maziwa Makuu</i>	234
20	<i>Eneo la Maziwa Makuu</i>	243
21	<i>Mabonde ya Zambezi na Limpopo (1110-1500)</i>	255
22	<i>Afrika ya Ikweta na Angola: Uhamiaji na kujitokeza kwa madola ya awali</i>	268
23	<i>Kusini mwa Afrika: Watu wake na muundo wa jamii</i>	282
24	<i>Bukini na visiwa vya jirani kuanzia karne ya 12 hadi ya 16</i>	292
25	<i>Mahusiano na mabadilishano kati ya majimbo mbalimbali</i>	300
26	<i>Afrika katika mahusiano na mabara mengine</i>	310
27	<i>Hitimisho</i>	320
	<i>Bibliografia</i>	
	<i>Faharasa</i>	
	<i>Sherche</i>	



Dibaji

AMADOU - MAHTAR M'BOW

Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni niwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya

bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, miechepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendeka haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokezaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za “mweupe” na “mweusi” zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imbadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya junuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kichukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika*, ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya

Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kumpeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa*) kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia*; kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihansa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa

kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika*, na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepokana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza ulhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweh na umakini ambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii. Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele

fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*¹ yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

Historia Kuu inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazama vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

Historia hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika


¹ Majuzuu kumi na mbili yafiatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu:

Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.

Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoclezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango waliutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.



Wasifu wa Mradi

B.A. OGOT¹

*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi
kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.
- (b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya schemu zote za bara ambazo mara nyingi liutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na inabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande

¹ Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wavya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

- (c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.
- (d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahususi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulimgana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya niwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa inwisho. Inapooona kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapohititisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imekataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda unoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu nichango mkubwa kwa maclewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.



Maelezo kuhusu Wendo


Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

- (i) 230 KS = - 350
- (ii) 2900 KK = - 2900
1800 WK = + 1800
- (iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo
Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.



Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za wanachama.

Profesa J.F. Ade Ajayi
(Nigeria), tangu 1971
Mhariri Juzuu VI

Prof. F.A. Albuquerque Mourão
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971-8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa D. Chanaiwa
(Zimbabwe), tangu 1975;
alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa M. Difuiila
(Angola), tangu 1978

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

Hayati H.E.M. El Fasi
(Moroko), tangu 1971; alifariki 1991
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971- 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland
(Ujerumani Magharibi), tangu 1971;
alifariki 1992

Dakta Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampaté Bâ
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu); alifariki 1991

Dakta I.S. El-Hareir
(Libya), tangu 1978

Hayati Dakta I. Ĥrbek
(Chekoslovakia), tangu 1971; alifariki 1993
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal), 1971- 86; alifariki 1986

Hayati Abbé Alexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975
Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa Bethwell A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary
(Madagascar), tangu 1971

Dakta (Bibi) A. Jones
(Liberia), tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E.
Williams (Trinidad na Tobago),
1976-8; alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo Mwanakamati

Profesa C. Wondji (Côte d'Ivoire)
Mhariri Msaidizi Juzuu VIII
Siyo Mwanakamati


*Ukatibu wa Kamati ya
Kimataifa ya Kisayansi*
Schemu ya Ushirikiano wa Kinataifa wa Utamaduni
Hifadhi na Ukuzaji wa Utambuzi wa Tamaduni
UNESCO
1, rue Miollis, 75015 Paris

Wasifu wa waandishi waliochangia makala katika nakala kuu

*Toleo lililofupishwa lilitayarishwa kutokana na matini za
toleo kuu lililoandikwa na waandishi wafuatao:*

- UTANGULIZI D.T. Niane (Guinea); Mtaalamu wa Mandingo; amechapisha kazi nyingi kuhusu Afrika Maghaibi wakati wa himaya kuu, kuanzia karne ya kumi na moja hadi ya kumi na sita; alikuwa Mkurugenzi wa Mfuko wa L.S. Senghor, Dakar, mchunguzi.
- SURA 2 O. Saidi (Tunisia); mtaalamu wa historia ya Waalmohad; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya zamani ya Maghrib, na hususan Tunisia, anafundisha historia kwenye Kitivo cha Sanaa na *Ecole Normale Superieure* ya Chuo Kikuu cha Tunis.
- SURA 3 M. Talbi (Tunisia); mtaalamu wa Uislamu; amechapisha kazi nyingi na makala kwenye maeneo mbalimbali ya dini ya Kiislamu na Utamaduni, anafundisha kwenye Kitivo cha Sanaa, Tunis.
- SURA 4 I. Hrbek (Jamhuri ya Czech); mtaalamu wa kumbukumbu za Kiarabu za historia ya Afrika, hususan Afrika Magharibi; pia ni mtaalamu wa Uislamu; amechapisha kazi nyingi na makala katika nyanja hizi; ni mchunguzi katika Taasisi ya Taaluma za Mashariki, Prague.
- SURA 5 R. Idris (Ufaransa); mtaalamu wa lugha na fasihi ya Kiarabu; alifundisha historia ya Magharibi ya Uislamu; amefariki.
- SURA 6 D.T. Niane
- SURA 7 M. Ly-Tall (Mali); mtaalamu wa historia ya Mali; amechapisha kazi zinazohusu himaya za Mali, anafundisha kwenye *Ecole Normale Superieure*, Bamako; Mchunguzi.
- SURA 8 S.M. Cissoko (Senegal); mtaalamu wa historia ya Timbuktu ya Kale; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Afrika Magharibi; mhadhiri msaidizi kwenye Kitivo cha Sanaa, Dakar.
- SURA 9 M. Izard (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya bonde la Volta na hasa lile la falme za Mossi; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi kabla ya ukoloni; historia ya ukoloni na historia ya kisasa ya eneo hili; Mchunguzi Mwamamizi katika Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kisayansi, Paris.
- SURA 10 D. Lange (Ujerumani); mtaalamu wa historia ya Sudan ya kati kabla ya ukoloni; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi hiki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha Niamey.
- SURA 11 M. Adamu (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Wahausa; amechapisha kazi zinazohusiana na sono hili; Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Utamaduni wa Nigeria cha Chuo Kikuu cha Ahmadu Bello, Zaria.
- SURA 12 A. Salifou (Niger); mtaalamu wa historia ya Wahausa; amechapisha kazi nyingi kuhusu Niger na Nigeria; anafundisha Niger.
- SURA 13 Y. Person (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Afrika, hususan Mandingo; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Afrika; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Paris 1, Pantheon – Sorbonne; amefariki.
- SURA 14 P. Kipre (Côte d'Ivoire); mtaalamu wa historia ya kisasa na ya sasa ya Côte d'Ivoire; amechapisha makala mengi kwenye masimulizi; anafundisha *Ecole Normale Supérieure*, Abidjan.
- SURA 14 A.F.C. Ryder (Uingereza); mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi kabla ya ukoloni na wakati wa ukoloni wa eneo hili; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Bristol.

- SURA 15 J.C. Garcin (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Misri ya Kiislamu; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Misri chini ya Mamluki na Misri ya Juu ya Waislamu; anafundisha Chuo Kikuu cha Provence, Aix-en-Provence.
- SURA 16 L. Kropáček (Jamhuri ya Czech); mtaalamu wa historia ya jamii, siasa na dini ya Sudan, amechapisha kazi nyingi kuhusu Darfur, anafundisha katika Idara ya Taaluma za Asia na Afrika ya Chuo Kikuu cha Charles, Prague.
- SURA 17 T. Tamrat (Ethiopia); mtaalamu wa historia ya kale ya Ethiopia; amechapisha kazi nyingi juu ya kipindi hiki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha Addis Ababa.
- SURA 18 V. Matveiev (Muungano wa Urusi); mwanahistoria na ethnolojia; amechapisha kazi nyingi juu ya kumbukumbu za Kiarabu za historia ya Afrika; Mchunguzi Mwandamizi kwenye Taasisi ya Ethnolojia, Akademia ya Sayansi ya Urusi, St. Petersburg.
- SURA 19 C. Ehret (Marekani); mwanaisimu na historia ya Afrika Mashariki; amechapisha kazi nyingi na makala kuhusu historia ya kabla na wakati wa ukoloni wa Afrika Mashariki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha California. Los Angeles.
- SURA 20 B.A. Ogot (Kenya); mtaalamu wa Afrika na hususan historia ya Afrika Mashariki; amechapisha kazi nyingi na makala juu ya historia na akiolojia ya Afrika Mashariki; mwalimu, mchunguzi; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Kumbukumbu ya Louis Leakey kuhusu Historia ya Awali ya Afrika; Mkurugenzi, Taasisi ya Utafiti na Taaluma za Uzamili, Chuo Kikuu Kishiriki cha Maseno, Kenya.
- SURA 21 B.M. Fagan (Uingereza); mwanaanthropolojia, mwanaakiolojia; amechapisha kazi nyingi kuhusu tamaduni za Enzi ya Chuma na Enzi ya Mawe Afrika Mashariki na Kusini; Profesa wa Anthropolojia katika Chuo Kikuu cha California, Santa Barbara.
- SURA 22 J. Vansina (Ubelgiji); mtaalamu wa simulizi; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Ikweta ya Afrika na Afrika ya Kati; anafundisha Chuo Kikuu cha Wisconsin, Marekani.
- SURA 23 L. Ngeongco (Botswana); mtaalamu wa historia ya Kusini mwa Afrika kabla ya ukoloni; amechapisha kazi nyingi kuhusu Botswana kabla ya ukoloni; alifundisha Chuo Kikuu cha Botswana; Mkurugenzi wa Taasisi ya Taifa ya Uchunguzi Gaborone.
- SURA 24 J. Vansina.
- SURA 24 F. Esoavelomandroso (Madagascar); mtaalamu wa historia ya Madagascar; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Madagascar kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane; anafundisha kwenye Kitivo cha Sanaa, Antananarivo.
- SURA 25 D.T. Niane
- SURA 26 J. Devisse (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Kaskazini Magharibi ya Afrika kuanzia karne ya nne hadi ya kumi na sita; mwanaakiolojia; amechapisha makala mengi na kazi juu ya historia ya Afrika. Profesa wa Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha Paris 1, Pantheon – Sorbonne.
- S. Labib (Misri); mtaalamu wa historia ya kale ya Afrika; amechapisha makala mengi kuhusu historia ya jamii na uchumi ya kipindi hiki; anafundisha Chuo Kikuu cha Utah (Marekani) na Chuo Kikuu cha Kiel (Ujerumani).
- SURA 27 D.T Niane



Utangulizi

Ijapokuwa mgawanyo huu mdogo wa kipindi kati ya karne ya kumi na mbili hadi karne ya kumi na sita hauna umuhimu sawa katika kila sehemu ya Bara hili, unaweza ukachukuliwa kuwa wa maana, kwani karne hizi chache zinaonyesha aina fulani ya mshikamano wa jumla kwa Bara zima. Kilikuwa ni kipindi muhimu ambacho Afrika ilitawisha tamaduni zake za asili na kuingiza athari za kigeni, wakati huohuo ikidumisha upekee wake hadi kipindi cha pigo kubwa la biashara ya watumwa ya Atlantiki ambayo ilifungua kipindi kipya (Juzuu la V).

Juzuu lililotangulia lilizungumzia kipindi ambacho kinaonyesha kufahamika zaidi kwa bara la Afrika, hasa kutokana na waandishi wa Kiarabu. Kilikuwa ni kipindi cha ugunduzi wa Nchi ya Weusi (Sudani) Kusini mwa Sahara, ambako idadi kadha ya dola na falme zilizojiimarisha zilijitokeza. Katika Sahara Magharibi, kulikuwa na milki ya Soninke ya Ghana ambayo ilitawala eneo hilo kutoka Ghuba ya mto Niger hadi mlango wa bahari wa Senegal. Al-Bakri anatoa maelezo mafupi lakini muhimu kuhusu dola hii. Upande wa pili wa Sudani, katika eneo la bonde la Chad, kulikuwa na Falme za Kāneni-Borno. Kati ya kanda hizi mbili, falme nyingine kama vile Songhai zilikwisha stawi. Baada ya karne ya kumi na moja, na hasa baada ya karne ya kumi na nne na kumi na tano, rekodi za maandishi zikawa nyingi: kutokana na kuongezeka kwa maandishi ya Kiarabu, na pia, mwishoni mwa kipindi hiki, kutokana na mchango wa maandishi ya Wareno juu ya falme za Pwani na Bara za Afrika ya Magharibi, Kati, Kusini na Mashariki.

Mada tatu kuu

Mada tatu kuu zilitawala kipindi hiki katika Afrika: ushindi wa Uislamu juu ya maeneo makubwa; kupanuka kwa ubadilishanaji (wa bidhaa), hasa katika mahusiano ya biashara; na mwisho, kuundwa kwa madola makubwa ambayo yalikuwa yamejengwa madhubuti.

Ushindi wa Uislamu

Uislamu, uliokuwa umcenea pembezoni mwa Bara la Afrika, katika kipindi hiki ulipenya ndani zaidi na kujikita zaidi. Nafasi za wafanyabiashara Waarabu wa Kiislamu waliokuwa wamcunganishwa ndani ya mtandao wa mabara mengi zilichukuliwa na Wafanyabiashara Waafrika ambao waliingia ndani sana kwenye maenco ya misitu.

Bara likawa limezingirwa kutoka pande mbili — upande wa Sudani na upande wa pwani ya mashariki.

Katika kipindi kilichopita, Afrika ya Kaskazini ilikuwa tayari imekwishaingiliwa sana na Uislamu. Katika karne ya kumi na moja chama cha Wamoravi, kikitokea kwenye kingo za Senegal, kilikwishaingia na kurejesha tena imani halisi na kali za Kimāliki katika Maghrib na Hispania; kisha kukaribia mwaka 1076, chama hicho kilikwisha teka Kumbi Salch, mji mkuu wa Ghana. Tukio hili muhimu karibu liwapite kando wana Tarehe, wakati njia za kupitia Sahara kuunganisha Afrika ya Kaskazini na Sudani zikiendelezwa na madola yaliyofuatia Ghana: Takrur, Mande, Songhai, n.k. Uislamu, ambao ulipokelewa ulivyo na wakati mwingine kufanyiwa markebisho na Waberiberi na watu wa Sudani, ulienca kwa amani kutoka mijini na makazi ya wafalme, hasa kwa njia za biashara, bila kuharibu miundo ya kijadi.

Mashariki mwa Bara la Afrika, Uislamu ulijipenyeza, wakati mwingine kwa kutumia nguvu, kuanzia Misri na tawala za Kiislamu zilizoambaa Bahari ya Sham, Ghuba ya Aden na Pembe ya Afrika, kadhalika kutoka kwenye makazi au vituo ya biashara vya Kiislamu katika Bahari ya Hindi (Sofala, Kilwa, Zanzibar, Pate, Mogadishu, n.k.) kuelekea Nubia, Sudani Mashariki, Nyanda za juu za Ethiopia na maenco makubwa ya Mashariki na Kusini mwa Afrika. Huko Ustaarabu wa Waswahili ambao ni zao la Afrika, ukastawi na kurutubishwa na Uislamu. Lugha ya Kiswahili, yenye mfumo wa Kibantu na iliyotajirishwa na maneno ya Kiarabu, ilisambaa Afrika Mashariki nzima na Afrika ya Kati hadi kufikia Maziwa Makuu na lango la mto Kongo (Zaire).

Vipingamizi vikuu viwili dhidi ya upanuzi huu usioepukika vilikuwa, ukubwa wa Ethiopia na, kwa kiasi fulani katika kipindi hiki, ukubwa wa cneo la Bara la Wabantu.

Ufalme wa Ethiopia unajitokeza sana katika kipindi hiki kupinga Uislamu. Hii ilitokana na nguvu ya Ukristo wake uliokuwa na uasili wa miundo na ujenzi; michoro na miundo yake ya kitawa. Ingawa kanisa hili la Ethiopia lilikuwa likitengwa mara kwa mara na mkuu wake, askofu mkuu wa Aleksandria, lakini lilikuwa na mafanikio mengi. Mengi katika hayo yalitokana na makazi ya kitawa yaliyojengwa katika miinuko ya nyanda za juu. Katika schemu hizo,

climu ilitolewa na historia ya wafalme na marekebisho ya kidini yaliandaliwa. Aidha athari za zamani za *Kikushi* na zile za kabla ya Ukristo zikiingilia waziwazi taratibu za Kikristo za ibada, sherche, ngoma na sadaka za wanyama. Hapa kama ilivyokuwa kwa Uislamu, Uafrika ulijitokeza. Katika Afrika ya Mashariki na Kati, lugha ya Kiswahili na ustaarabu wa Waswahili wenye tabia za Kiafrika ambazo kimsingi zilirutubishwa na mikopo ya Kiarabu, ilienca kutoka pwani ya mashariki hadi sehemu za bondeni za mto Kongo katika Bahari ya Atlantiki kupitia nchi zinazozunguka Maziwa Makuu.

Ushindi wa Uislamu kwa kiasi kikubwa huenda ulitokana na kufanana kwa taratibu za maisha za waenzaji wake wa awali na zile za Waafrika weusi wengi au Waberiberi. Aidha baada ya matukio ya kivita yaliyofanywa na Wamoravi; dini hii ya Kiislamu ilienezwa kwa amani na wakazi wa miji, wafanyabiashara, na watu maarufu katika mabaraza ya wafalme, bila kuharibu mila au kuomba chochote mbali na kodi kutoka kwa watu walioshindwa na kutawaliwa.

Maendeleo ya mahusiano ya biashara

Upanuzi wa mahusiano ya biashara unaambatanishwa kwa karibu sana na ule wa Uislamu. Uislamu ulienca katika Mabara kutoka Bara Hindi hadi rasi ya Iberia, vilevile kutoka visiwa vya Mediterania hadi Bukini. Muungano wa lugha na dini, pamoja na usalama wa uhakika uliokuwepo katika eneo hili, usingeshindwa kukuza biashara za aina zote. Afrika ambayo ilipakana na Asia na Ulaya kwa upande mmoja na bahari ya Mediterania na bahari ya Hindi kwa upande mwingine, isingeweza kukwepa athari za mifumo hii ya biashara.

Mahusiano ndani ya Afrika yalikuwa katika kiwango ambacho taaluma za akiolojia, toponimia na Isimu zinaendelea kutufunulia. Jangwa la Sahara lilikuwa likivukwa mara kwa mara na misafara mikubwa ya ngamia hadi kufikia 12,000. Na misafara hii iliendelezwa na maelfu ya wachuuzi kuelekea kusini hadi kwenye misitu minene na pwani. Biashara hizi zilisambaza mazao ya chakula (hasa yale yaliyotokea Bahari ya Hindi) mbinu na tabia za kijamii zilizodhihirisha umoja wa kitamaduni wa msingi wa bara hili ukiondoa tofauti ndogo za kimaskani

Kusini mwa Ikweta, kama zinavyoonyesha, sura zinazoshughulikia nchi zinazozunguka maziwa makuu na mabonde ya mto Kongo, Zambezi na Limpopo, pamoja na Kusini mwa Afrika, athari za Uislamu hazikujipenyeza sana katika kipindi hiki.

Ni bidhaa za aina gani zilibadilishwa? Afrika ya kusini mwa Sahara iliua nje hasa dhahabu, pembe za ndovu, sanaa za ufundi, na mazao ya kilimo (nafaka, ngozi na bidhaa za pamba, n.k.). Aidha Afrika ilipeleka watumwa Maghrib, Mistri, na

Mashariki ya Karibu: wanawake kuwa masuria na wanaume kuwa watumishi wa nyumbani na mashambani, na walenzi wa watawala. Miji Mikuu na miji ya biashara kusini mwa Sahara iliagiza hasa bidhaa za anasa: Silaha na vyombo vya chakula vilivyonakshiwa sana, nguo za kifahari, farasi, mikuo ya chuma, na shaba, n.k. Zaidi ya haya, kulikuwa pia na watumwa wachache mafundi wa sanaa walioletwa kutoka Kairo na matajiri wa Kisudani baada ya kukamilisha hija zao kwenye miji mitakatifu ya Kiislamu.

Kukua kwa falme na milki

Jambo la tatu katika kipindi kinachozungumziwa hapa lisiangaliwe kama matokeo ya mambo yale mawili ya kwanza, ijapokuwa katika enco la watu weusi la Sudani, kwa hakika Uislamu na biashara vilikuwa na athari ya namna fulani katika macdelco ya kisiasa, hata kama kimsingi havikuwa chanzo chake. Kwa upande mwingine, kwa mfano, Falme za Kongo, Zimbabwe, na Mwenemutapa, hazikuchangiwa chochote na athari za Uislamu.

Kama tulivyokwishaona, ukweli ni kwamba vituo vya biashara pote katika pwani ya Bahari ya Hindi, Bahari ya Sham na Mediterania, na katika pande zote mbili za Sahara, vilikuwa vituo ambamo climu na tamaduni za kidini vilitolewa. Lakini katika viwango vya kisiasa, kisosiolojia na hata za kitamaduni, Waberiberi na Wasudani waliendelea kujing'ang'aniza kwenye asasi zao na kuukubali Uislamu bila kuupokea utamaduni wa Kiarabu.

Ni katika kipindi hiki ambapo Misri ilikuwa kituo kikuu cha utamaduni cha ulimwengu wa Kiislamu, ikichukua nafasi ya Baghdad, Damasko, na miji ya Uarabu; na Maghrib nayo kwa kupitia Andalusi na Italia ya kusini, ilikuwa ikieneza huko Ulaya urithi wa heshima wa kifasihi, kiufundi na kisayansi uliojengwa na Uislamu. Kadhalika, ilikuwa ni katika Baraza la Mfalme wa Kikristo, Roger wa Sisilia, ambapo al-Idrisi alipotolea *Jiografia* yake mashuhuri ambayo iliamsha hamu ya matabaka ya wakwasi raha kujishughulisha na Bara la Afrika.

Kwa upande wa kisiasa, baada ya ushindi mkubwa wa Yusuf Ibn Tāshūn huko Hispania dhidi ya Wakristo, hasa mjini Zallaka (1086), chama cha Wamoravi kilisambaratika katika makundi yaliyopingana, yaani kati ya makabila ya Maghrib na yale ya Sahara, na pia kutokana na upinzani wa majimbo ya Ghana, baada ya kifo cha AbuBakr mwaka 1087.

Mfalme Roger II wa Sisilia alitumia mwanya huu wa udhaifu wa Wamoravi kujasurisha kuishambulia Afrika ya Kaskazini na kutoza kodi katika baadhi ya bandari zilizokuwa zinatembelwa sana na maharamia wa Kiberiberi. Lakini, kabla ya muda mrefu kupita, pwani yote ya Afrika ya Mediterania ilitakwa na Wamohadi kwa upande wa Magharibi, na Waayubi, na hasa Mamluki, kwa upande wa

Mashariki, mnamo karne ya kumi na tatu na kumi na nne. Mamluki waliyazima mashambulizi ya Wakristo ya vita vya msalaba, katika Mashariki ya Karibu, na kuwalazimisha wapiganaji hao kukimbilia kwenye ngome ili kujinusuru bila kuukamata mji wa Yerusalemu.

Ilikuwa katika kipindi hiki ambapo madola ya magharibi na ya kati ya Sudani yalipofikia upeo wake. Ingawa karne ya kumi na mbili haifahamiki vizuri kwa enco hili, maandishi ya al-Adrisi's pamoja na mapokezi simulizi, vinawezesha kusimulia upya mapambano makali ya kuwania madaraka yaliyopiganwa kwenye magofu ya Ghana katika maeneo ya Wagadu, Takrir na Mandé. Baada ya kipindi cha utawala wa kabila la Soso, ambalo ni kundi dogo la Soninke-Mandé lililoukataa Uislamu, karne ya kumi na tatu ilishuhudia kuinukia kwa Mali, na Sundiata akiwa mshindi dhidi ya Sumaoro-Kante, mfalme wa kabila la Soso huko Kirina, mnamo mwaka 1235. Mababu wa Sundiata walisilimishwa katika karne ya kumi na moja; naye akarudisha tena uhusiano na wafanyabiashara wa Kiislamu na wasomi, na kuanzisha asasi ambazo zilikuja kutawala milki ya Mali kwa karne nyingi. Biashara ya kuvuka Sahara, ambayo iliguzwa kuelekea zaidi Misri, sasa ilivuma sana, wakati huohuo idadi kubwa ya wafanyabiashara wa Dyula walielekea kusini kwenye nchi za misitu zilizozalisha kola, dhahabu, pembe za ndovu, mafuta ya mawese, na mbao za thamani, walipeleka huko samaki wakavu, bidhaa za pamba, na bidhaa za viwandani. Mfumo huo wa biashara uliambatana na uanzishwaji na upanuzi wa milki au falme za Songhai, Kānem-Borno, Mossi, Dagomba, n.k.

Madola ya watu weusi yalikuza mahusiano ya kibalozi kwa kuweka ofisi za kibalozi katika nchi za Afrika ya Kaskazini (Moroko, Tunisia, Libya, Misri) na wakati mwingine kwa safari fashifashi za hija zilizofanywa na watawala. Waandishi wanne wa Kiarabu wametuachia maelezo yenye manufaa ya maeneo haya kwa kipindi hiki. Wa kwanza ni Ibn Khaldun (1332-1406), mwana historia mwenye maarifa sana na mfikirifu ambaye alihusika na maguzi ya maisha katika majumba ya Kifalme ya Fez, Tunis, na Andalusia. Kitabu chake maarufu kitiwacho Historia ya ulimwengu (*Universal History*) pamoja na schemu iliyotafsiriwa kama "Historia ya Waberberi" (*History of the Berbers*), kina maelezo muhimu juu ya Himaya ya Mali. Aliweka orodha ya watawala hadi mwaka 1390. Kitabu chake kitiwacho *Mukaddima (Prolegomena)* kimweka msingi wa taaluma za Sosiolojia na historia ya kisayansi.

Ibn Battuta, msafiri asiyechoka, katika karne ya kumi na nne, alisafiri schemu zote za magharibi, kaskazini, Afrika ya mashariki na Bahari ya Hindi hadi kufika India na China. Alipendelewa sana na kila kitu: vyakula, asasi za kisiasa, mila za ndoa, dawa na vilevile njia za biashara. Alibahatika binafsi kutembelea jumba la maliki wa Mali aliyecitwa Mansa Musa I. Anahadithia, kwa mfano, kuwa aliona

kauri katika makao makuu ya mfalme na kule Gao kama zile alizoziona katika visiwa vya Maldiva na ambazo zilitumika kama fedha - kauri 1150 kwa dinari moja ya dhahabu.

Al-Umari anatupa taarifa muhimu aliyopata kutokana na wadhifa wake kama katibu wa baraza la mfalme wa Mamluk kati ya mwaka 1340 na 1348. Nafasi hiyo ilimwezesha kuingia kwenye hifadhi ya nyaraka za kifalme, na pia kupata habari kutoka kwa mabalozi wa Sudani walioko Kairo, na kwa kupitia watu ambao waliwahi kukutana na wafalme wa Kisudani katika safari zao za hija za kuzuru Schemu Takatifu. Makala yake yaitwayo "Maelezo ya Afrika bila Misri" yana usahihi wa hali ya juu na uhalisi.

Mwisho, mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, Leo Africanus alitembelea Sudani mara mbili na kurejea na habari kemkemu juu ya maeneo hayo, mwanzoni tu mwa wakati-matumizi ya meli ndogo nyepesi zilizoitwa *Karavele* yalipoanza, wakati ambao Sudani ya Magharibi ilianza kudidimia.

Aidha, licha ya mapokezi ya mdomo na maandishi, eneo hili limeelezwa kwetu bayana na wanaakiolojia. Baada ya kufukuliwa Kumbi Saleh, mji mkuu wa Ghana, mnamo mwaka 1914, ilifuata zamu ya Awdāghust kufukuliwa na maprofesa J. Devisse na Robert mwaka 1965. Viwango mbalimbali vya makazi ya wakati huo viliweza kutambuliwa na hazina kugunduliwa. Ugunduzi huo ulithibitisha ukweli wa kauli ya al-Bakri kuwa Awkār katika kipindi hiki ilikuwa ni "Nchi ya Dhahabu". Kusini zaidi huko Nyani, mji mkuu wa Mali, kikosi cha wataalamu wa kutoka Guinea na Poland kinekuwa kikichimbua makaburi ya zamani kwenye eneo hilo, kazi ambayo imepelekea kupatikana kwa mabaki mengi yenye habari nyingi.

Mbele zaidi Afrika ya Magharibi, upande wa pili wa Afrika ya weusi, mabaki mengi makubwa ya kumbukumbu za mawe zilizoitwa zimbabwe na mapungobwe (kwa Kishona) ni dalili ya ustadi wa kiufundi, ongezeko la watu na mfumo wa kisiasa katika kiwango kikubwa.

Baada ya nadharia tete za kijinga zilizotolewa na wanahistoria wa kikoloni, sasa ukweli umedhihirika kuhusu chanzo cha majengo ya kuvutia ambayo awali yalisemekana kutokana na Wafoeniki, miongoni mwa watu wengine. Mnamo mwaka 1905 mtaalamu wa mambo ya Misri, David Randall Maclver, alitangaza bayana kuwa kumbukumbu hizo za mawe ni zenye asili ya Kiafrika:

Hakuna dalili ya intindo wowote wa Asia au Ulaya wa kipindi chochote... Hali ya makazi yaliyofunikwa na vifusi vya mawe, na ambayo ni sehemu yake, kwa hakika ni ya Kiafrika... Sanaa na inbinu ... ni za Kiafrika.

Baada ya maneno ya mtaalamu huyu, wasomi wengine walisema vivyo hivyo, kama vile Dkt. Gertrude Caton Thompson na Basil Davidson. Profesa B.M. Fagan anajenga hoja hiyo katika juzuu hili.

Kwa hakika, mnamo karne ya kumi na tano, wakati Wareno walipoingia mashariki mwa Afrika, na kufika Sofala, walisikia habari kuhusu himaya ya Kiafrika yenye nguvu huko bara, na hata kukutana na wakazi wa dola hii ambao walikuja kufanya biashara na Waarabu. Wao waliuita Ufalme huo Benametapa. Da Goes anauandikia ifuatavyo:

Katikati ya nchi hii kuna ngome iliyojengwa kwa mawe makubwa na mazito ndani na nje... jengo la kustajibisha na lililojengwa imara, kwani inasemekana kuwa hakuna madongo yanayoweza kuonekana yakishikilia mawe pamoja... Mfalme wa Benametapa anaishi kifahari na kuhudumiwa kwa hesiuna kubwa, kwa kupigiwa magoti.

De Barros anaongeza kusema kuwa "wananchi wa nchi hii wanayaita majengo yote haya makubwa "Symbaoc", ikimaanisha jumba la mfalme kwa lugha yao. Jitihada za pamoja za wanaisimu, wanaakiolojia na wanaanthropolojia zimekwishatoa mwangaza wa kutosha juu ya majengo haya na kuhusu mfumo imara wa kijamii na wa kisiasa wa wajenzi wake. Kama alivyokuwa *Kaya maghan*, *Mwenemutapa* jina la Cheo cha kifalme linaloamaanisha "bwana wa metali" alikuwa na ukiritimba wa dhahabu. Eneo lote hili katika bonde la Zambezi (Zambia ya leo, Zimbabwe na Malawi) lilijaa shaba, dhahabu na chuma. Kwa mujibu wa Basil Davidson, "maelfu ya machimbo ya zamani kiasi cha 60,000 au 70,000" yamekwishagunduliwa. Ijapokuwa tarehe ya ustaarabu huo wa miaka haijathibitishwa kabisa, kilicho na uhakika ni kwamba Wareno walipofika, ingawa *Mwenemutapa* na Zimbabwe ilikuwa bado inaonekana yenye nguvu kubwa, lakini usambaratikaji wake ulikwishaanza na hali hii ilizidishwa na uharibifu na unyang'anyi wa Wacno na Wazungu wengine. Watu wa nchi hizi walishiriki sana katika kilimo cha matuta ya ngazi. Walikuwa ni Wabantu waliojisimika na kuchukua maeneo ya wakazi wa zamani na kuwafukuzia misituni na kwenye majangwa Mbilikimo na makabila mengine madogo.

Kuwepo kwa falme nyingine nyingi kati ya Afrika Magharibi na milki za Afrika ya kati na kusini, kumerekodiwa kwenye kumbukumbu nyingi.

Wareno walivutiwa sana na falme za Kiafrika walizokutana nazo tangu walipofika kwenye mlango wa bahari wa mto Senegal mnamo karne ya kumi na mbili. Nchini Senegambia, walisikia habari za Maliki au Mansa wa Mali, na

walianzisha uhusiano na wafalme wa Wolof.

Kutoka Senegambia hadi delta ya Niger pametanda eneo ambalo kumbukumbu zake za kimaandishi ni za kubabia. Lakini tunajua ya kutosha kutuwezeshwa kutamka kuwa mazingira ya misitu hayakuzuia kabisa maendeleo ya kisiasa-jamii. Miji ya Benin na sanamu nzuri za kuchonga za Wayoruba ziliendelezwa katika mazingira haya ya misitu. Hapa tena, uzushi wa waandishi wengi wa Ulaya ulibuni wasanii wa sanaa hizi bora wasio Waafrika hadi hapo asili yake ya Kiafrika ilipoonyeshwa, na uhusiano wa asili kati ya vyombo vya udongo vya Nok (miaka 500 kabla ya Ukristo) na shaba nyeusi ya Benin (Karne ya kumi hadi kumi na nne) kuthibitishwa.

Pitio hili fupi limeonyesha kuwa kulikuwa na mifumo ya aina mbalimbali ya kisiasa-kijamii katika Afrika wakati wa kipindi hiki. Katika makundi mengi ya watu, kuwa na ukoo au nasaba zinazodai kutokana na babu mmoja ilikuwa ni kitu cha kawaida, na waliishi chini ya utawala wa mzee wa heshima au chifu ambaye kazi yake muhimu ilikuwa ni kuhakikisha mgawanyo sawa wa mapato ya jamii. Pato lilipoongezeka sana na kuzalisha ziada kubwa uwezo na nguvu za chifu ambazo mwanzoni zilikuwa ndogo ziliongezeka zaidi na zaidi. Ukoo hasa ulikuwa kundi la kibiojia lililodai kuwa na eneo la makazi lililofahamika waziwazi. Hata hivyo, katika mabadiliko ya polepole ya ukoo, eneo la makazi (balada ya uhusiano wa kibiojia) likawa ndilo kitu cha kujitambulisha nacho.

Ufalme ulikusanya pamoja koo mbalimbali; chifu mmojawapo wa koo hizo akajisimika na kutawala wenzake wa cheo kimoja kama ilivyotokea kwa ukoo wa Keita uliounda Mali. Mfalme alitawala kwa msaada wa baraza ambalo wajumbe wake aliwatunza. Ijapokuwa kila ukoo ulidumisha desturi zake maalumu na ibada za kidini, koo hizi ziliunganishwa katika ufalme kwa utii ulioonyeshwa kwa njia ya kulipa kodi (aghalabu kwa kutoa mazao). Mfalme alibaki na mamlaka yake kama mkuu wa kidini lakini kwenye eneo kubwa zaidi la ufalme. Nafsi yake ilikuwa tukufu kama ilivyokuwa kwa Mali, Kongo, Mwenemutapa, n.k.

Himaya ilimaanisha jimbo kubwa zaidi lililojumuishia falme nyingi. Hali hii ni kama ile ya himaya ya Wamohadi ambayo sultani wake mkuu, japo alitoka kwenye ukoo (kabila) fulani, alitawala masultani wengine waliokuwa wamesambaa kwenye sehemu kubwa ya Maghrib. Hali hii ilitokea pia kwa maliki (mansa) wa Mali ambaye alikuwa na majimbo kumi na mawili, ikiwa ni pamoja na falme mbili chini ya utawala wake. Baraza la Maliki, kama lile la mfalme, lilifanya kazi kwa kutumia katiba isiyoandikwa au desturi na hivyo ikasaidia kudhibiti tabia za utawala wa mtu mmoja. Kulikuwa pia na falme ndogo ndogo ambazo zilikuwa kama *dola-miji*, ambazo zilitawala pia maeneo yaliyozizunguka. Falme hizi ni kama zile za miji ya

Hausa na miji ya Yoruba ya Benin, ambayo ilitawaliwa kwa kanuni ngumu na tata, na ikiwajibika kwa miji mama kimila. Daura ukawa mji mama wa miji ya Hausa, na Ife ukawa mji mama kwa miji ya Yoruba. Licha ya kuwepo kwa vita vya hapa na pale, miji hii iliendelea kuwepo ikiwa imeunganishwa na utamaduni mmoja.

Kama inavyojidhihirisha, tumekataa istilahi kama zile za "jamii iliyomeguka" na "jamii isiyo na dola". Kazi za dola zinaweza kutckelezwa kwa njia nyingi zinazotofautiana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Vile vile tumcondolca mbali maneno kama vile "kabila" (tribe) na "ushirikina" ambayo yana maana dhalilishi. Tutazungumzia sasa juu ya "watu" au "mbari" ijapokuwa istilahi hii ya mwisho ina utata wake pia. Dini ya asili ya Kiafrika ilikuwa sio ya "kishirikina" au "kinyama"; kwa sababu ya utata wake kinyume na vile inavyoonekana kijuujuu, ni bora kuielezea kuwa ni "dini ya kiasili". Zaidi ya hayo, neno *Hamitic* ambalo lilijadiliwa sana katika juzuu la I, linakataliwa. Ijapokuwa neno hili limetokana na Ham (Babu wa Biblia wa watu weusi); maana yake imekenguliwa ili kutaja watu wasio weusi, ambao walidaiwa kuwa walifika Afrika kama wafugaji bora ambao walileta mbinu mpya na bora za maendeleo ya kijamii. Hii ilikuwa ni itikadi potofu iliyokusudiwa kuhlalisha ukoloni. Njia ya kuondoa ukoloni katika historia ni kuzitupilia mbali nadharia hizi za uongo na udhalilishaji unaoambatana nazo.

2

Kuunganishwa kwa Maghrib chini ya Wamohadi

Kuanzia katikati ya karne ya kumi na mbili hadi katikati ya karne ya kumi na tatu, utawala wa Wamohadi uliashiria hatua ya juu kabisa ya juhudi za kuunganisha eneo la Maghrib na hata eneo lote la Magharibi ya Waislamu. Umoja ulioletwa na Wamohadi ulizidi ule ambao walijaribu kuuleta. Hii ilitokana na mabadiliko ya kidini yaliyoongozwa na mtu maarufu aliyeitwa Mahdi Ibin Tumart na kuendelezwa na jumuiya ya Muwahidun (Wamoja). Hatimaye juhudi hizi zilikuwa na kuwa mpango kamili wa kisiasa, ambao viongozi wake walikuwa masultani wa nasaba iliyoanzishwa na mmoja wa masahibu wa mwanzo wa Mahdi. Wamumiwidi walikita nguvu zao kwenye nguzo mbili za uchumi ili kuunda umoja wa eneo la magharibi la Waislamu. Kwanza, walidhibiti misafara ya biashara ya kuvuka jangwa la Sahara, na inasoko ya kaskazini ya dhahabu ya Sudani. Pili, waliunganisha vituo muhimu vya ukuaji wa uchumi.

Hali ya kidini katika Maghrib na juhudi za Wamohadi za utafuta

Dini ya Asili na Uislamu


Mnamo katikati ya karne ya kumi na moja madhehebu ya Shia yalikuwa bado yanaendelea na juhudi za kujieneza, ijapokuwa utawala wa Wafatini wa Misri ulikuwa umeporomoka. Aidha vuguvugu la kuwaunganisha Waislamu ilikuwa bado imesambaratika. Zilikuwapo njia tatu zilizodai kuelekeza jamii kwenye umoja. Ya kwanza ilikuwa ni utakasaji wa mila za Kisumi ambao wakati mwingine ulikuwa na hatari ya kuingiza msimamo mkali wa Kisufii. Ya pili, ni kutungwa kwa sheria zenye kuzingatia desturi rasmi na ada ya kimila. Na ya mwisho ni kufanywa kwa utafiti wa kina wa maswala ya kidini na kufanya usanidi wenye mwelekeo wa fikra za al-Ashari. Mikondo miwili ya fikra iliyoshindana, na ambayo ilipingwa na

wanafikra wengine, ni itikadi ya sura na falsafa. Lakini huko Maghrib Uislamu ulipambana na matatizo zaidi. Uzushi wa Wahariji uliokataa mamlaka na kuhubiri usawa wa watu wote uliwavutia wahamaji na jamii za vijijini. Hususan Waberberi waliuona uzushi huo kama kielezo cha upinzani wao wa asili na wa muda mrefu dhidi ya kugeuzwa Waarabu kulikoashiriwa na kusilimishwa. Ukharija ulipinga kanuni ya kurithi Ukhalifa na kanuni iliyodai kuwa kabila fulani ni tukufu kuliko mengine. Kudumu kwa muda mrefu kwa sheria za mila za Waberberi kuliamsha hisia zilizolala za ukinzani wa kiroho ambao Wa-Almoravi na Wa-almohadi ndio hatimaye walifanikiwa kuopunguza.

Tatizo jingine la Uislamu huko Maghrib lilitokana na UMaliki wenyewe. UMaliki ulijipenyeza mapema sana kwa njia ya mahubiri ya wafuasi wa Malik Bin Anas kama vile Daktari wa Sheria Ibn al-Kasim na Imam Sahnun (776-854) ambao walifanya Kayrawan kuwa kituo kikuu cha Umaliki. Lakini Umaliki uliandamwa na upotofu wa kusikitisha. Madaktari wa sheria waliohodhi ardhi kubwa, waliacha kuyazama kiroho mafundisho ya misingi ya dini (Kurani na Hadithi), inambo ambayo yalithaminiwa sana na Waislamu wa Mashariki, na badala yake walijishughulisha na furutu (vitabu vya sheria-matumizi). Kwa kutofanya juhudi ya kutafsiri (kufafanua) vitabu vya msingi kwa kufanya wokovu utegemee matendo ya ibada yanayoonekana kubeza imani ya kiroho kujaribu kujilinganisha na Mungu kuchonganisha na kutesa waumini, wanasheria wa KiMaliki walionekana kuwa watu wenye mawazo finyu na ya kikasuku kuwa mfano wa yanayomgeuza Mungu kuwa binadamu kwa umbo. Ulipopambanishwa na msako kiakili na ya kiroho wa Wamutazili, mtazamo wa WaMaliki uliojikusisha zaidi na sheria na ibada tu, na ujanja wa kutumia matendo na sifa za binafsi kujipatia kufanya inatendo mema yatakayompatia masilahi ulionekana kuwa muflisi na kapa. Ni rahisi kuelewa kwa nini maulama kama al-Ghazali na Ibn Hazm walikosoa mtazamo huu wa Imani na pia matendo ya wanasheria wengi ambao walilipwa vizuri sana ili kusimamia misingi ya dini, wakati ambapo upotofu na ujanja uliokithiri uliwafanya vibaraka wa watawala. Katika maandishi yake yaitwayo "Uhuishaji wa mafunzo ya Dini" al-Ghazali, ambaye mwelekeo wake wa imani kali ya kiroho ulipingwa vikali sana na WaMaliki, alitetea kurejewa matumizi ya "inaji ya uzima," yaani chemchemu za Kurani na *Sunna*.

Elimu ya Ibn Tumart

Habari za Ibn Tumart ambaye sifa zake zimetufikia zikiwa zimechanganyika na visakale, zinafahamika kidogo sana. Inafikiriwa kuwa alizaliwa mwaka 1075 hako



2.1 Maghrib kutika karne ya kumi na mbili — Shughuli za kiuchumi (J. Devisse, kulingana na O. Seidi na C. Vanacker)

katika milima ya Anti-Atlas nchini Moroko. Wazazi wake walitokana na makabila mawili ya Masmuda yanayofahamika siku hizi kama Shiluh. Baadaye iliyumishwa kuwa alitokana na ukoo wa Masharifu ili kukidhi malengo yake. Baba yake alikuwa tajiri na hali hii ilimwezesha kwenda Mashariki kupata elimu, na kwa mujibu wa Ibn Khaldun, hadi akapewa katika lugha ya jina asafu ("yaani utaa" ya Shluh) kutokana na juhudi zake.

Ibn Tumart hakuwahi kukutana na al-Ghazali, japokuwa sifa za al-Ghazali hatimaye alizitumia kuhamasisha watu wakubali mahubiri yake. Ibn Tumart alifanikiwa kutekeleza dhima mbalimbali: alikuwa mkaguzi wa maadili, mwanathiolojia aliyejitokeza huko Marrakesh; mkuu wa shule mpya iliyoanzishwa Aghmat; na kiongozi wa kikundi cha Wanajumuiya wa Tinmallal. Pasi na papara, lakini kwa ushupavu mkubwa, alieleza malengo yake. Aliporejea kutoka Mashariki akielekea Moroko, alisimama kwa muda mrefu Bidjaya (Bougie) cneo la Ifrikiya, ambapo alikaa faraghani kwa muda akisali, kusoma na kufanya taamuli. Hapo ndipo alipokutana na mrithi wake wa baadaye Abd-al-Mumin, mtu ambaye alikuwa katika safari ya kielimu kuelekea Mashariki. Ibn Tumart alimshawishi Abdi-al-Mumin akatishie safari yake na aungane naye. Baada ya mkutano huu safari yake kuelekea magharibi iliandaliwa vyema zaidi kwa kuwa na vituo, katika miji mbalimbali na kukutana na wanazuoni wa dini, na kufaragua au kuandaa mikutano ya majadiliano. Idadi ya wafuasi wake iliongezeka sana. Alipokuwa kati ya Sale na Marrakesh alifanya ishara ya kukataa kulipa ushuru, na alipokuwa kauka mji mkuu wa Almoravi, aliendesha majadala maarufu baina yake na wanasharia wa kitawala, mbele ya Ibn Yusuf, mtawala wa Waalmoravi. Katika kufanya hivyo wapinzani wa Ibn Tumart ambao walikuwa wanamdhibiti mtawala wa Waalmoravi, walinyamazishwa na nguvu za hoja zake. Kutokana na hali hii alionekana kuwa tishio kwa wanasiasa na waziri alishauri auawe; lakini kiongozi mwingine alimshauri kuondoka, na akamsaidia kutoroka.

Awamu mpya ilianza. Alienda Aglimat na kuupinga waziwazi utawala wa Waalmoravi; kwa mfano alikataa kwenda Marrakesh alipoamriwa na Amir (mtawala wa mji huo). Tangu wakati huo akawa anaongoza jeshi kubwa ambalo liliupinga utawala uliokuwapo kutokana na chuki za kiukoo dhidi ya Waalmoravi na wala sio kwa sababu ya kutaka kuleta mageuzi ya kidini. Mapambano yalikuwa hayacupukiki.

Mageuzi ya Wamohadi yaliyofanywa na Ibn Tumart


Hatimaye Ibn Tumart na wenzake walijisctiri katika pango lililokuwa katika kijiji cha Igilliz alikozaliwa. Hoja zake kuhusu imani za kidini, maadili na sheria ambazo zilikuwa zikijengeka taratibu, na kuimarishwa, ziliunganishwa katika kanuni chache

za kimsimamo.

Kanuni ya kwanza bila shaka ilikuwa ni kukiri kuwa Mungu ni mmoja (*tawhid*) kanuni hii iligeuzwa kuwa nguzo ya kiroho ya imani yenye athari ya mafundisho ya al-Ghazali. Jina la Almohadi linatokana na imani hiyo. Wafuasi wa Ibn Tunart walikuwa waumini wa umoja (wa Mungu) (*al-Muwahhid*), na kutokana na hali hiyo wakapata jina la Almohadi (waumini wa Mungu mmoja). Wamona walidhihirika kwa unyofu wa maadili yao ambayo yalisifiwa na Waberiberi waliokuwa wakiishi vijijini, hususani wakati Mahdi alipohubiri kwa Kiberiberi na kukitumia kwenye maandishi yake mengine. Aidha kwa kuzingatia desturi za kabila la Washlah, Ibn Tumart alitegemea ushauri wa baraza la watu mashuhuri. Kwa kufuata fikra za Wamutazali na kukana fasiri linganishi za Wamohadi zinazoshabihisha sifa za Mungu na hali halisi ya binadamu, Ibn Tumart alitamka kwa dhati kuwa Mungu alikuwa ni 'roho tu, kwa hivyo baadhi ya aya za Kurani zilipaswa kutafsiri kama istiaru. Kwa upande mwingine, Waalmoravi walionekana kuwa na kosa la ushirikina. Kosa hili lilihusishwa na Wamohadi pekee kwa sababu waliwajibika kwa waliowatawala, na kwa maoni ya Ibn Tumart walistahili kutengwa.


Imani ya pili ilikuwa, Uungu wa milcle: Mungu kama muumba ndiye wa mwanzo na ndiye wa mwisho, na ataendelea kuwapo maana hatakuwa na mwisho. Imani ya tatu ni enzi ya Mungu. Kuhusu imani ya nne, uthibitisho wa ujumbe wa mtume kwa ishara za ajabu, na ushuhuda (*ayat*), msimamo wa Ibn Tumart ulifanana na ule wa Wasunni. Kuhusu imani ya Mahdi (Kiongozi asiye na dosari) anayecongozwa na Mungu, alitofautiana sana na Wasunni, ambao kwa upande wao Mahdi angetokea karibu tu na mwisho wa dunia. Lakini Ibn Tumart alikiweka chanzo cha utume wake mara tu baada ya kifo cha Ali katika mwaka 661. Katika kufanya uamuzi huu alivutia kwake matlaba ya watu kuelekea kwenye "zama za haki" ambazo waliamini Mahdi angeanzisha; na ambazo Ibn Khaldun ameshuhudia kuhusiana na kipindi hiki. Kwa sababu hii ilikuwa ni lazima kumtii Mahdi bila kufikiri, na kuelekeza uchunguzi wa kina wa kithcolojia katika imani kwenye lengo la kuendeleza mipango muhimu ya Mahd ya kuiondoa serikali ya kidhalimu iliyokuwa madarakani.

Akiwa anatambua Kurani na sunna kuwa ni vyanzo muhimu vya sheria ya dini, Ibn Tumart hata hivyo katika mazingira maalum alikubali muafaka (*idjima*) ambao uliwahusu tu masahaba wa Mtume, na tafakuri zilizofanywa kwa kurejelea mifano halisi bila kuingiza mambo ya uzushi. Kwa upande mwingine, alikataa kabisa kufuata maandiko ya kisheria pekee pamoja na ulaghai bila kurejea moja kwa moja kwenye vyanzo vyenyewe.



2.2 Kibla, au ukuta wa mashariki, wa msikiti ulioko Timmaltal (Moroko). Ukiwa kama mahali pa kwanza muhimu pa kusalia pa jumuiia ya Wamohadi, msikiti huu ni kielelezo cha usanifu majengo na upambaji wa vitu ambao Wamohadi walitaka kuulazimisha ufanvike.

2.3 Sehemu ya ndani ya uga wa msikiti wa Timmaltal¹



Muundo wa jumuiya ya Wamohad:

kikundi cha propaganda, kueneza itikadi na mapambano

Baada ya kwenda Aghmat, Ibn Tumart alikipa kikundi chake malengo ya kisiasa mbali na yale ya kidini. Kama alivyokuwa amekusudia kumwigiza Mtume kwa kwenda kuishi pangoni, aliendeleza tabia hii kwa kuwataka masahibu wake kumi akiwemo Abd Al-Mumin wamtangaze kuwa Mahdi akiwa chini ya mti. Vivyo hivyo, kukimbilia kwake Tinmallal kuliitwa pia hijra, na kampeni zake kama zile za mtume ziliitwa *maghazi*.

Mara yalitokea mapigano madogo madogo baina ya wafuasi wake na majeshi ya Wamohadi. Akisaidiwa na kabila la Masmuda, alifanikiwa kutwaa sehemu kubwa ya Anti-Atlasi. Wamohadi walifanya shambulio kali dhidi yake na kumlazimisha akimbilie Tinmallal mwaka 1123. Mbali na migogoro iliyokuwepo katika kundi lake ambayo ilisababisha wafuasi wake wa kabila la Masmuda kugawanyika, Wamoravi nao walipigwa na kushindwa na Wahispania. Ibn Tumart alitumia fursa hii ya kushindwa kwa Wamohadi kuanzisha muundo wa asasi ambao sehemu zake kuu zilikuwa mabaraza ya watu kumi, watu hamsini na *talaba*.

Baraza la Watu Kumi

Baraza hili lilijulikana kama “watu wa jumuiya” (*Ahl-al-Jamaa*). Idadi yao ilikuwa ikibadilikabadilika, na iliitwa hivyo kwa kulinganisha na masahaba wa Mtume. Hili lilikuwa baraza la washauri, “baraza la nyumba” (*Ahl al-Dar*) ambalo liliongozwa na Abd al-Mumin baada ya al-Bashir. Wajumbe wa baraza la kumi walikuwa kwa namna fulani mawaziri wa Mahdi ambao walimsaidia kuandaa na kutekeleza maamuzi muhimu katika nyanja za kiraia, kiutawala na kijeshi.

Baraza la Watu Hamsini

Idadi ya baraza hili nayo ilikuwa inabadilikabadilika. Hili lilikuwa baraza la ushauri lililokuwa na wawakilishi kutoka katika makabila. Wajumbe saba muhimu walitokana na makabila muhimu matatu: Waharga, ambalo ni kabila la Mahdi, Watinmallal na Wajanfisa.

Talaba

Hawa walikuwa wanafunzi waliokusanywa na Mahdi alipokuwa katika ziara zake za mafundisho.

Al-Kaffa

Usemi huu ulielezea kundi kubwa la Wafuasi waliopangwa katika makabila (vikundi vya kisiasa - kijamii na kidini) yaliyogawanywa zaidi katika vikundi vya watu kumikumi (nakib) (rutba) na kupangwa kidaraja. Utaratibu huu uliwezesha watu watiwe kasumba ya itikadi mpya, kujenga hisia ya utambulishi, na tabia ya uhasama mkali dhidi ya watu wengine, hususan Wamoravi. Wamohadi walitafautishwa na watu wengine hata kwa mavazi yao na waliepukana na wasioamini umoja mtakatifu na kuungana na waumini wenzao. Imani ya *tawhid* ilifunzwa kwa utaratibu maalum kwa njia ya vijitabu kwa Kiberiberi na Kiarabu, kwa kuoanisha maarifa na vitendo (*ilm* na *amal*). Mafunzo haya makali yalizia utii wa kikondoo miongoni mwa wafuasi kiasi kwamba walikuwa tayari kuwaua hata ndugu zao kama hapana budi. Hii ilisababisha umwagaji mkubwa wa damu. Baada ya kifo cha Ibn Tumart, baraza la watu kumi na hile la watu hamsini lilitajwa tu wakati wa kiapo cha utii (*bay'a*) kwa Abd al-Mumim. Kusema kweli Abd al-Mumin ahona ni busara kufanya kazi na wajumbe binafsi wa baraza badala ya kupitia baraza zima. Kuanzia wakati huo baraza la mashehe wa Wamohadi lilielekea kushika nafasi ya yale mabaraza mawili yaliyoundwa wakati jumuiia hii ilipoanzishwa. Hii ilileta wasiwasi mkubwa sana. Mashehe walijitwalia mamlaka yaliyokuwa karibu sawa na yale ya makhalifa. Mamlaka ya mashehe yaliondolewa kabisa hasa na Khalifa al-Nasir mapema kabla ya vita vya Les Navas de Tolosa, na huenda jambo hili lilichangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kwa Wamohadi. Kwa upande mwingine, kuporomoka kwa mamlaka ya makhalifa kulisababisha mamlaka zaidi kwa mashehe. Mashehe waliungana na kujiundia namna fulani ya ukoo wa watawala ambao Khalifa al-Mamun hakuweza kuuvumilia. Mashehe waliokuwa wengi na wenye umashuhuri mkubwa walikuwa watoto wa wajumbe wa baraza la watu kumi au la watu hamsini, isipokuwa tu wawakilishi wa kabila la Mahdi hawakushika nafasi muhimu katika utawala, jambo ambalo baadaye lilisababisha ndugu wa Mahd kuasi. Kusema kweli baraza la mashehe lilianza kupanua taasisi za awali za uongozi ili kuhusisha sekta mpya zilizoanzishwa, hali ambayo ilipelekea kuundwa kwa baraza la mashehe wa Kiarabu na baraza la mashehe wa Kiandalusia wa Jund. Kwa upande wa kikundi cha *talaba*, Abd al-Mumin alikijahi sana kutokana na nafasi yao kama waeneza propaganda.

Hata hivyo walipewa majukumu mengine katika maeneo mbalimbali kama vile elimu, utawala, na ukamisaa katika jeshi. Wajibu wao ulikuwa kuhimiza matendo mema na kukataza maovu.

Madhehebu ya kundi hili yaliendelezwa kwa muda mrefu; ila nguvu zake za kisiasa zililipungua al-Mumin alipoacha itikadi ya umahdi.

Kuunganishwa kwa Maghrib na Makhaliifa wa Wamohadi wa Kimumin

Uhasama wa awali uliofanywa dhidi ya Wamohadi uliambatana na matukio matatu tofauti: Wamohadi walishindwa katika vita vya Aghmat; Mwaka 1122 Wamohadi walishinda vita vya Kik na halafu kuzingira mji wa Marrakesh. Lakini askari wa farasi wa Wamoravi waliliangamiza jeshi la Wamohadi kule al-Buhayra na kumuua al-Bashir, sahib mkuu wa Mahdi. Abd al-Mumin aliyekuwa amejeruhiwa aliwarejesha Timmallel askari waliokuwa wamesalia. Ulikuwa ni wakati huu huu ambapo Ibn Tumart mwanzilishi wa kundi hili alifariki dunia mwaka 1130.

Kipindi cha Abd Al-Mumin na kuundwa kwa himaya (1133-63)

Kipindi kirefu cha mgogoro kihohofuatia kifo cha Ibn Tumart na kuisha baada ya Abd al-Mumin kutwaa madaraka na kujiimarisha katika utawala hakiwezi kuelezwa kwa misingi ya ukabila pekee. Hali hii ilisababishwa na kupanuka kwa lenigo la awali la kuimarisha dini katika eneo dogo kuwa mradi mkubwa zaidi wa kuunganisha upya Maghrib kwa nia ya kuimarisha Uislamu, na kwa masilahi ya familia ya Abd al-Mumin. Katika kipindi chake cha miaka thelathini ya utawala, al-Mumin alidhihirisha uwezo wake mkubwa kama mpangaji mikakati ya kijeshi na kiongozi wa nchi. Hatua kuu za shughuli hii kabambe zilikuwa kama ifuatavyo: kuiteka Moroko, kuiteka Maghrib ya kati, kuimarisha mamlaka yake, kuiteka Ifrikiya na kuanza kuivamia Andalusia.

Kutekwa kwa Moroko

Funzo alilolipata Abd al-Mumin kutokana na maafa ya al-Bulyra ni kwamba mapambano ya nchi tambarare yaliwafaa zaidi askari wa farasi wa Wamoravi, hivyo aliamua kwenda kuitwaa milima ya Waberiberi kutokea upande wa kusini. Hii ilimwezesha kudhibiti madini na njia ya biashara ya kuelekea Sudan, ambayo pamoja na kutwaa nehi za Sus na Draa, vyote vilimpatia mapato makubwa. Kisha jeshi la Wamohadi lilifuata njia inayopita kwenye kingo za milima kuelekea kaskazini mashariki ili kuhitenga eneo la kati la Wamohadi. Walilitwaa eneo la Atlas ya Kati na oasisi za Tafilalet baina ya mwaka 1040-41 na hatimaye wakatokea Moroko Kaskazini na kuzitwaa ngome katika eneo la Taza na kuungwa mkono na makabila ya kusini mwa Mediterania. Askari wa Wamoravi walizingirwa. Abd al-Mumin akiwa na idadi ya kutosha ya askari na zana, alishaka hadi tambarare ambako mazingira mazuri yalifaa kwa mashambulizi yake. Mazingira hayo yaliyomsaidia ni kuwepo kwa chuki baina ya chifu wa Walemtuna na Chifu wa Wamasufa baada ya kifo cha Amir Ali ibn Yusuf Ibn Tashfin mwaka 1143; kifo

cha Mkatalan aliyerudia dini yake ya awali (*al-Ruburtayar*) na aliyekuwa kiongozi wa wanamgambo wa Kikristo wa Wamoravi, kilichotokoa 1145; na kujiunga kwa Waberiberi wa Zenata katika vuguvugu la Ki-tawhid (Kimohadi). Baada ya Wamoravi kuiteka Tilimsan, mtawala wa Waberiberi Tashfin Ibn Ali alikwenda Oran ambako alifariki ghafla. Moroko ilitokwa karibu yote na Wamohadi ambao walidhibiti njia kuu za biashara zinazounganisha Sudan na Mediterania. Katika hali hiyo uasi ndani ya nchi kama ule uliofanywa na al-Harghi wa kabila la Ibn Tumart, au uasi kutoka nje uliochochewa na wafuasi wa Wamohadi wa Sus, na wale waishio kati ya Sabta na Agadir, usingeweza tena kuwa tishio kwa utawala mpya, ambao ulizima uasi wowote uliotokoa kwa umwagaji mkubwa wa daniu. Maana Wamoravi, kwenye jumuiia yenye muundo nyumbufu na yenye kufuata madhehebu ya Maliki ambayo walikwisha jinasibisha nayo kwa urahisi, hawakuonekana kuwa sio wacha Mungu. Hii ndio sababu, ukiachilia mbali milima ya Masumuda, Wamohadi hawakupokelewa kama wakombozi. Hivyo palikuwa na matukio mengi ya kukataliwa kwa Wamohadi na jamii zilizohisi kuwa jumuiya ya kibaguzi na yenye moyo mgumu ya Wamohadi ilikuwa ni tishio kwao.

Kuishinda Maghrib ya kati

Abd al-Mumin sasa aliweza kusonga mbele na kuishinda Maghrib yote. Kabla ya kuanza vita hivi aliitikia ombi la Waandalusia ambalo lilieleza kuwa wasingeweza tena kuvumilia utawala wa kidhalimu wa Wamohadi na kwamba walihofia hatari inayozidi kuongezeka kutoka Kastile. Baadhi ya miji kama vile Seville na Gardove ilijisalimisha na kupokelewa na kikosi cha wavamizi cha Wamohadi. Majimbo ya mashariki yalifanya tahadhari; na mwaka 1150 ujumbe wa Waandalusia ulipowasili kula kiapo cha utii kwa Abd al-Mumin, kiongozi huyo wa Wamohadi hakuona haja ya kuendelea mbele hadi Hispania, na badala yake alipendelea kwanza kuelekea mashariki kwa lengo la kuiunganisha Maghrib.

Na huko Ifrikiya kwenyewe kulikuwa pia na tishio la Wakristo: Wanorma wakiongozwa na Roger II wa Sisilia walianza kutwaa maeneo ya pwani na kujiimarisha ilihali koo za ufalme za Kisanhaja, Wakayrawan na Wabijaya (Bougie), zilikuwa zinatishiwa na tawala za Kisanhaja na Kiarabu upande wa bara.

Mwaka 1152 Abd al-Mumin pamoja na jeshi lake walitembea hadi Maghrib ya kati kwa kushtukiza. Aliteka miji ya Algiers na Bijaya. Mji wa Konstantini aliutwaa bila mapigano baada ya Waziri wa mtawala wa Wahamadi kujisalimisha. Kwa ukatili mkubwa aliwasambaratisha Wasanhaja, Watuwata, na Wakutama. Marafiki au wateja wao wa Kiarabu ambao hadi wakati huo walikuwa na tahadhari, walijitosa katika mapambano na kushindwa vibaya sana kauka mbuga za Setif

mwaka 1153 baada ya kupambana kishujaa. Khalifa wa Wamohadi aliwapa msamaha usio wa kawaida. Huenda baada ya kuonyesha nguvu zake alikuwa tayari anafikiria kupanua misingi ya himaya yake na kuwafanya Waarabu marafiki kwa kisingizio cha jihad ili kuishambulia Andalusia. Ndiyo maana aliacha nyuma walinzi wa ngome na magavana huko Maghrib ya kati na kurejea Moroko.

Kuimarisha mamlaka ya Wamumini

Kwa kuhofia kuwa ushindi wa hivi karibuni ungeweza kuimarisha nguvu ya khalifa, nduguze Mahdi Ibn Tumart, miongoni mwa Wahargha na watu wa Tinmallal waliasi. Uasi huu ulizimwa na wakahamishwa kutoka nchini kwao. Ili kuwapoza watu, khalifa alikwenda kuhiji kwenye maziwara maeneo ya kumbukumbu ya Mahdi Ibn Tumart. Aliwagawia watu zawadi na kupanua msikiti wao. Lakini mwaka 1156-57 alipiga kambi Sale na kuwafanya watu wantambue mwanac mkubwa kuwa, ndiye atakayemrithi kama mtawala wa himaya yake. Wanae wengine aliwafanya magavana wa miji mikubwa na kuwapa cheo cha *sayyid*. Kila mmoja wao alikuwa na naibu ambaye alikuwa Sheikh Mmohadi akiwa na wadhifa wa waziri na mshauri wake. Kuanzishwa kwa utawala huu wa kinasaba kuliwezekana kutokana na kuungwa mkono na majeshi mapya ya himaya: Waarabu wa Hilal na makabila ya Sanhaja kwa upande wa mashariki.

Lakini kwa mara nyingine mfumo huu mpya ulizusha maasi huko kusini mashariki miongoni mwa Walamta na Walamtuna. Huko Marrakesh ndugu wawili wa Mahdi Ibn Tumart walifanya njama dhidi ya serikali; njama hizo ziliutikisa utawala vibaya sana, na zilizimwa kwa akatili usio na huruma.

Matokeo ya majaribu yote haya yalikuwa ni kumfanya Abd al-Mumin kuwa mkuu wa himaya ya kurithisha utawala kiukoo, badala ya kuwa kiongozi wa jumuiya ya waumini waliokuwa wamepatwa na misukosuko mingi kama alivyokuwa hapo awali. Aliacha kutegemea ukoo-tawala pekee, ukoo wa Wamasmuda, akaanza kufikiria namna ya kupanua misingi ya himaya kwa kuungwa mkono na makabila ya Maghrib ya kati na Waarabu wa Hilal. Badala ya kutegemea ukoo na dini, sasa mamlaka yakawa ya kisiasa yenye kuhusisha makabila mengi.

Kutekwa kwa Ifrikiya

Baada ya kushinda upinzani mbalimbali uliokuwa umemkabili, mwaka 1159, Abd al-Mumin alianza kampeni yake ya pili kuelekea mashariki jambo ambalo hatimaye lingefanya Maghrib yote kwa mara ya kwanza iungane chini ya mamlaka moja. Watu wa Ifrikiya waliomba msaada mara kwa mara ili kukabili uvamizi wa Wakristo.

Akiongoza jeshi kubwa la ardhini na la majini, yote yakienda sambamba kuelekea mashariki, Abd al-Mumin aliuzingira mji wa Tunis ambao baada ya muda mfupi ulitekwa. Hata hivyo iliwachukua miezi saba kuuzingira na kuuteka mji wa Mahdiyya uliokuwa chini ya Wanorma wa Kikristo kwa miaka kumi na miwili. Miji ya Gabas, Gafsa, Sifaksi na Tripoli ilitakwa mmoja baada ya mwingine. Nchi iliyokuwa bara ya Ifrikiya ilishambuliwa na majeshi ya baharini na askari wa farasi upande wa kusini na hatimaye kutekwa. Tawala za wanamfalme zilizorithi ufalme wa Kiziri zilisambaratishwa, Wanorma walifukuzwa kutoka pwani na Maghrib ikaunganishwa.

Matayarisho ya kuingilia Andalusia na mwisho wa utawala wa Abdu al-Mumin
Mamwinyi wa Andalusia, wawakilishi wa nasaba tawala ya Wamoravi, na vikundi vya Kikristo, walipinga mamlaka ya makhalifa, na kufanya mashambulio ya mara kwa mara dhidi ya Andalusia kaskazini. Abd al-Mumin alipeleka kwanza vikosi ambavyo vilipata ushindi kama ule wa Badajoz. Lakini wakati huo huo khalifa alifariki huko Sale alipokuwa anajiandaa kuivamia Hispania. Alizikwa Tinmallal karibu na kaburi alimozikwa Ibn Tumart. Alikuwa kiongozi hodari sana wa majeshi na mpangaji mzuri ambaye hakupuza masuala ya kiuchumi. Kwa mfano alihamisha kituo cha mwisho cha njia ya biashara ya kuvuka sahara katika pwani ya Atlantiki ya Moroko kutoka Draa na kukipeleka Oran. Kwa kufanya hivi liwaondoa Wamoravi katika biashara ya dhahabu kutoka Sudan na nafasi yao ikachukuliwa na Wamohadi. Khalifa alilazimika kila wakati kuyaweka majeshi yake upande wa kaskazini katika peninsula ya Iberia ili kuzuia mashambulizi ya Wakristo na upande wa mashariki kuelekea Ifrikiya ili kuulinda muungano wa Maghrib uliopatikana kwa gharama kubwa. Hata hivyo ilikuwa vigumu sana kufanikiwa kutimiza malengo yote mawili kwa wakati mmoja.

Wamohadi walikuwa wameongeza umoja wa kisiasa na kiutawala katika umoja ulokuwepo wa kichumi na kiutamaduni. Abd al-Mumin alivunja desturi ya Wamoravi ambayo ilitokana na mfumo wa Wahispania na Waumayya na kuanzisha mfumo wa utawala uliozingatia mahitaji ya himaya kubwa na ya wafuasi wake wa Kiberiberi. Kwa upande wa ufundi aliwatumia Waandalusia ili kuhakikisha kunakuwepo na kiwango cha kuridhisha cha ufanisi. Kisiasa aliwatumia *sayyid* wa Kimumini na shekhe wa Kimohadi ili kuhakikisha uwiano mzuri wa madaraka. Katika uwanja wa itikadi aliwatumia *matalaba* kama makamisiaa wa kisiasa ili kuhakikisha utiifu kwa utawala. Athari ya mfumo huu bado inaonekana katika baadhi ya Makhzen katika Moroko ya sasa.

Gharama za kuendesha utawala huu mpya zililipiwa na mfumo mpya wa kodi.

Alipokuwa akirejea kutoka Ifrikiya mnamo mwaka 1160 Khalifa aliagiza ardhi yote ya Maghrib kutoka Tripol hadi Moroko Kusini ipimwe. Ukiachilia mbali theluthi moja ya ardhi ambayo ni milima na isiyo na rutuba, ardhi yote iliyobaki ilitozwa kodi ya ardhi, *haraji*. Kulikuwa hakujawa na urajisi wa ardhi tangu enzi za Warumi. Yawezekana pia kuwa huenda katika kuanzisha kodi hii aliathiriwa na kodi ya Wahilali. Raslimali nyingi zilikusanywa, kwani watu wote walipaswa kulipa kodi isipokuwa Wamohadi waumini wa Mungu mmoja, (*muwahhidun*.)

Maghrib ya kati na Ifrikiya zilichukuliwa kana kwamba sio nchi za Kiislamu. Jambo hili liliwafanya wakazi wa maeneo hayo kuuchukia umoja uliokuwa umepatikana hasa ikizingatiwa kuwa Wamohadi wenye kutukuza dhehebu lao pekee hawakujaribu kuwatoa wasiwasi. Aidha, japokuwa kodi hii mpya iliwezesha kujenga majeshi ya nchi kavu na ya majini ambayo yalikuwa maarufu katika eneo lote la Mediterania, majeshi haya hayakuwa na sifa za jeshi moja, jambo ambalo lilionekana kuwa siku moja lingesababisha hatari kubwa. Ama kuhusu kuwahamisha Wahilali na kuwapeleka Maghrib, hakukuwa na hali ya maangamizi makubwa kama anavyoclezea Le Toureau.

Kipindi cha ulinganifu

Abu Yusuf Yakub (1163-84)

Baada ya kufariki Khalifa Abd al-Mumin kulitokea wasiwasi mkubwa. Kulikuwepo na sababu kadha zilizofanya hali hii kuwapo: Sababu ya kwanza ilikuwa uhasama kati ya Muhammad, mrithi aliyetarajiwa kuchukua madaraka kwa upande mmoja, na ndugu zake, kwa upande mwingine. Mmoja kati ya hawa ni Abu Yusuf, ambaye hatimaye alikuwa mshindi. Baadaye Waghumara wa Moroko kaskazini waliasi. Uasi huu unafikiriwa kuwa ulisababishwa na kuvunjwa kwa jeshi ambalo liliundwa kwa ajili ya safari ya kwenda kuwashambulia Waandalusia. Hatimaye upinzani wa Wamaliki huko Sabta huenda pia ulikuwa unaunga mkono uasi ulitokea. Uasi huu ulizimwa kwa umwagaji mkubwa wa damu na khalifa mpya, ambaye alijipa jina la Amir al-Muminin (1158), na kumteua kaka yake kuwa gavana wa Sabta na kumpa wajibu na kusimamia Rif.

Kampeni ya Andalusia

Mwaka 1165 khalifa na ndugu zake walimshinda mwanamfalme Ibn Mardanish wa Andalusia pamoja na askari wa kukodiwa wa Kikristo, lakini alishindwa kuteka Mursia, makao yake makuu. Hata hivyo majeshi ya khalifa yalinasurika katika shambulio dhidi ya jeshi lililokuwa likiongozwa na kapteni maarufu aliyicitwa Giraldo Sempavor kwenye eneo la Badajoz, kwa msaada wa rafiki yao Mhispania

Ferdinand II wa Leon. Baada ya mapigano ya muda mfupi, jeshi la Ibn Murdanish lilisambaratika na askari wake wengi walijiunga na jeshi la khalifa, lakini jeshi la Wakastilia lilipoingilia kati, Wamohadi walilazimika kujiengua na kurudi Mursia ambapo jeshi lilivunjwa. Khalifa alirejea Marrakeshi mwaka 1181-2.

Abu Yusufu Yakubi Al-Mansur (1184-99)

Alipoteuliwa na Wamohadi kama mrithi wa utawala wa baba yake, kulikuwepo na upinzani kadha; lakini kutokana na ukweli kwamba alikuwa waziri katika Serikali ya baba yake, mtu aliyekuwa karibu sana na baba yake, na kwamba alikuwa mtu mwenye mawazo mazuri na shujaa, baraza kuu la uteuzi wa mrithi halikuwa na hiari bali kumteua. Hata hivyo mwanzo wa utawala wake ulishuhudia upinzani mkubwa kutoka kwa washiriki wapya katika historia yao ya Maghrib: Wabanu Ghaniya.

Wabanu Ghaniya wa Maghrib ya Kati

Watu hawa walipata jina hili kutokana na jina la binti mfalme wa Wamohadi aliyeyitwa Ghaniya, ambaye aliozwa na Mmoravi Yusuf Ibn Tashfin kwa Ali Ibn Yusuf al-Masufi na kumzalika wana wawili, Yahya na Muhammad. Wakati mamlaka ya Wamohadi yalipoisha, Mohammad alikuwa gavana wa Wabaleari. Mwanawe Ishak aliigeuza bandari ya Ubaleari kuwa ufalme uliostawi kutokana na uharamia. Mjukuu wake aliapa kuwa angewashinda Wamohadi, kuvihami visiwa dhidi ya Wamohadi na hata kuviendeleza vita hivyo hadi Maghrib kwa sababu za kibiashara. Wakitambua ukweli kuwa Wahammad Sanhaja wa Bijaya bado walitarajia kutwaa tena madaraka, Wamohadi wa Majorka waliwasaidia kwa kuwapatia vikosi 20 na askari 4,200 wakaingia Bijaya na kuuteka mji; na kisha walichukua nafasi yao. Ali Ibn Ghaniya akisaidiwa na Waarabu wa Riyah aliutwaa mji wa Algiers, na kisha Konstantini na alitoka tu katika mji huo mara jeshi la Wamohadi lilipokuja.

Ijapokuwa walishindwa, ujasiri liuu wa Wamoravi ulisababisha msukosuko mkubwa. Majeshi yaliyokuwa yakiwapinga Wamohadi sasa yalikuwa yamempata kiongozi wao. Ibn Khaldun anadai kuwa miongoni mwa majeshi haya, Waarabu walionyesha ari ya kuyaunga mkono yale yaliyoongozwa na Wabanu Ghaniya. Akitokea Sabta, khalifa mpya alifanya shambulio la nehi kavu na baharini ili kutwaa tena Algiers, na wakati huo huo Ibn Ghaniya alitoroka na kukimbilia kusini kuelekea Mzab.

Wabanu Ghaniya katika Ifrikiya.

Baada ya jeshi lao la majini kuangamizwa na kituo chao cha Bijaya kuchukuliwa

tena na Wamohadi, Wabanu Ghaniya walibadili mbinu ya mapambano na kuanzisha vita vya msituni wakitumia jangwa, ambako kulikuwa na uasi wa kudumu, kama kituo cha kukimbilia wanapozidiwa nguvu, na kujikusanya tena. Ali Ibn Ghaniya aliungana na Walemtuna na Waberiberi wa Masufa, Waarabu wa Banu Sulaym na Mwarmania aliyelitwa Karakush aliyeachwa huru na mpwa wa Salah al-Din (Saladini). Ali alituma hata ujumbe wa utii kwa Khalifa al-Nasir wa Ki-Abbas (Baghdad), ambaye aliahidi kumsaidia wakati ambapo Mwarmania, mkuu wa Tripolitania aliutwaa mji wa Gabes. Ali Ibn Ghaniya alianzisha kituo chake kikuu luko Jarid kusini magharibi mwa Tunisia.

Abu Yusuf Yakub aingilia Ifrikiya

Mwaka 1186 khalifa aliamua kwenda Tunis na jeshi lenye askari wa farasi 20,000. Ibn Ghasniya ahondoa majeshi yake na kuyarejesha Jarid ambapo alikirubuni kikosi cha wapanda farasi 6,000 na kukiangamiza karibu na Gafsa mwaka 1187. Baada ya shambulio hili, khalifa aliamua kushiriki katika mapambano mwenyewe. Ibn Ghaniya alisliindwa na kujeruhiwa kule al-Hamma na akatowekea jangwani. Khalifa alimshinda na kumteka Karakush huko Gabes, na kuyafagia majeshi yote katika eneo lote la bonde lenye rutuba la Jarid, akutwaa tena Gafsa, akawaadhibu vikali sana maofisa wa Kimoravi na kuwahamisha kwa wingi Waarabu waliokuwa wakishirikiana nao kutoka katika eneo hilo na kuwapeleka Tamasna huko Moroko.

Kutokea tena kwa Wabanu Ghaniya

Yahya Ibn Ghaniya alipomrithi kaka yake Ali, naye pia aliendesha mapambano dhidi ya himaya ya Wamohadi kwa ukali akihujumu jimbo la mashariki la Ifrikiya na udhoofisha mamlaka yake. Yahya alifanya tena mapatano ya kushirikiana na Karakush ambaye hakuwa amenyongwa. Alikwenda Ifrikiya ambapo washiriki wao wa Kiarabu hawakuwa wengi tena, akashambulia Maghrib ya kati. Akishirikiana na Mwarmania (Karakush), walidhibiti eneo lote la bara ya Tunisia baada ya muda mfupi. Wahipogombana wao kwa wao, Karakush akashindwa na kufukuzwa, akarudi Jabal Nafusa. Ndipo Yahya kadhibiti eneo kubwa kuanzia Tripolitania hadi Jarid. Aliweza kutwaa eneo kubwa kiasi hiki kutokana na mfarakano uliozuka miongoni mwa Wamohadi, na kuungwa mkono na Wakhariji wa Jaba Nafusa. Kwa hivyo hatimaye Ibn Ghaniya alikuwa mtawala wa nusu ya eneo lote la Maghrib upande wa mashariki.

Kampeni ya Al-Arak (Alarcos) na mwisho wa utawala wa Yakub

Wakati huo huo matatizo makubwa sana yalitokea huko Hispania na kudhihirisha mikinzano mikubwa ndani ya sera ya Wamohadi: kuingilia kati Hispania kutokea

katika sehemu mbili, yaani peninsula ya Iberia na Maghrib. Tangu mwaka 1194 Khalifa aliitelekeza Ifrikiya kwa Hispania. Mnamo Julai 1195 aliwashinda Wakastilia huko al-Arak, tukio ambalo lilimpatia jina la *al-mansur billah* (mshindi kwa mapenzi ya Mangu!). Kuhitilafiana kulikotokea miongoni mwa Wahispania kulimwezesha kuendesha kampeni ya kuwaangamiza hadi Madrid ambapo alikubali ombi la suluhu kutoka Kastilia, ambayo ilikuwa ikishirikiana pamoja na Aragon dhidi ya Leon. Alipata maradhi na kurudi Moroko, ambako alifariki dunia.

Abu Abdallah Muhammad Al-Nasir (1199-1214)

Muhammad alirithi hali ngumu; Ifrikiya na Hispania ziliendelea kutishiwa. Khalifa mpya aliipa umuhimu mkubwa Ifrikiya ambako Ibn Ghaniya alikuwa anapanua miliki yake kuelekea magharibi na kuwataka watu wanaposali wataje jina la khalifa wa Ki-Abbasi wa Baghdad. Lakini huko Moroko kwenyewe alilazimika kuzima uasi wa Sus ulioongozwa na Abu Kasaba aliyedai kwamba alikuwa “kahtani” mtarajiwa - hii ikimaanisha kuwa Umahdi ulikuwa unatumiwa dhidi ya Wamohadi ambao walikuwa wameutumia kuanzisha mamlaka yao. Hili lilikuwa jambo la kutia uchungu sana. Isitoshe miongoni mwa washauri wa khalifa, ni mmoja tu ambaye alimshauri asifanye mapatano ya amani na Mmoravi Ibn Ghaniya.

Mashambulizi ya Al-Nasir dhidi ya Wabanu Ghaniya na marekebisho ya mamlaka ya Wamohadi huko Ifrikiya

Akitumia mbinu mpya, khalifa alitwaa kwanza Majorka mwaka 1203 ili kuwakosesha Wabanu Ghaniya mahali pa kukimbilia katika Baleari ambapo waliwahi kupatumia kama kituo cha kijeshi na biashara. Kituo hiki kiliwawezesha kuendeleza uhusiano na Aragon, Genoa na Pisa dhidi ya Wamohadi. Hata hivyo Wabanu Ghaniya walijibu shanbulio hili kwa kutwaa Tunis. Khalifa alifanikiwa kuuchukua tena mji wa Tunis pamoja na Malidiyya. Ibn Ghaniya ambaye mpwa wake alikwisha kujisalimisha alikimbizwa hadi Barka. Abu Muhammad abd al-Wahid aliyeshauri kufanyika kwa kampeni hii aliteuliwa gavana na kaimu mtawala wa Ifrikiya, akabaki tunis wakati khalifa alipoondoka kurudi Moroko mwaka 1207. Ibn Ghaniya alikusanya vikundi kadha vya Waarabu miongoni mwao wakiwa Wariyah, Wasulaym na Wadawawida ambao kwa pamoja walijaribu na kushindwa kuuzuia msafara wa Khalifa ulipokuwa ukuejca Moroko. Halafu akalichakaza eneo la Tilimsan na Maghrib yote ya kati ambao mnamo karne ya kumi na nne kwa mujibu wa Ibn Khaldun athari zake hadi zilikuwa zinaonekana.

Mapambano makali yalitokea baina ya Abd al-Wahid, gavana mpya, na Ibn Ghaniya, akiungwa mkono na washiriki wake wa Kiarabu. Mapigano yalitokea

Jabal Nafusa mwaka 1210. Pale Mmohadi huyo na vikosi vya marafiki zake, Waarabu na Wazenata, waliwashinda vibaya sana. Hapo Ibin Ghaniya aliendelea kusini hadi Waddan na hatimaye kutekwa mwaka 1233 na mrithi wa gavana Abd al-Wahid.

Kipindi cha msukosuko wa Wabanu Ghaniya hakiwezi kushambuliwa kama mfululizo wa maafa ya Waarabu wa Hilal yaliyochukuliwa na Wamajorika hadi Maghrib ya kati kama anavyodai Georges Marcais. Kwa nusu karne mgogoro huu uhigeuka sehemu ya mkakati (wa utawala), kwa namna ulivyounganisha, katika hatua za mwanzo za matendo ya kishujaa ya Wamoravi, suala la udhibiti wa Sahara ya wahamaji na lile la udhibiti wa njia za bahari. Kipindi hiki kilionyesha uimara na upatanifu wa hali ya juu, na haiwezi kufikiwa kuwa huu ulikuwa ni uasi tu usiokuwa na malengo mazito ya kisiasa.

Ukweli ni kwamba huu ulikuwa ni mvutano wa madaraka ambapo Wabanu Ghaniya walijaribu kujionyesha kuwa wangekuwa bora kuliko mamlaka ya Wamohadi. Katika mapambano haya vipengere vya kiitikadi na kisiasa vilikuwa muhimu sana kwani viliunganisha wote waliokuwa wakimpinga khalifa: tawala za kinasaba za zamani zilizokuwa zimeondolewa madarakani, Wamaliki, Wanomadi wa Kiarabu na Waberiberi wa huko Tripolitania. Vipengere vya kijiografia, kisiasa na kiuchumi vyaweza pia kutusaidia kuelewa mafanikio ya wastani ya harakati hizi: Kwanza, ni umuhimu wa kisiwa cha Majorika kama kituo cha kibiashara na kidiplomasia; pili, ukweli kwamba eneo la himaya ya kikundi hiki lilienea kutoka Waddan na Tripolitania kusini hadi makazi ya Khariji ya zamani katika Maghrib ya kati. Ukanda huu ulijumuisha Maghrib kutoka Tripoli hadi mipaka ya Moroko, na kukusanya makabila pinzani ya milimani na oasisi zenye rutuba ambazo zipo katika matokeo ya njia kuu za kuvuka jangwa la Sahara. Vita vya Wabanu Ghaniya vilikusudiwa kurejesha urithi wa Wafatimi, Waziri na Wamoravi wa kudhibiti biashara kati ya Mediterania na Sudani. Mradi wa Wamohadi, mbali na kuvutiwa na Hispania, kwa upande wake ulielekezwa katika kuidhibiti nchi za mashariki hadi magharibi kupitia Maghrib, bila kuhusha eneo la Sudan na Sahara ambalo lilisafirisha dhahabu ya Afrika iliyokuwa muhimu kwa uchumi wa Mediterania.

Kushindwa kwa Al-Ikab (Las Navas De Tolosa) na Mwisho wa enzi ya Al-Nasir

Kushindwa kwa Wakristo kule Alarcos mwaka 1195 kuliwatahadharisha na kuwafanya wajandae tena, ijapokuwa kulikuwa na mapatano ya kusimamisha vita. Mwaka 1200 Wakristo walianzisha tena vitendo vya uhasama wakiongozwa na Alfonso VIII wa Kastilia, na Pedro II wa Leon wakiwa wametiwa nguvu na moyo wa mapambano wa askofu maarufu Toledo Rodrigo Jimenez de Rada, ambaye alimshawishi Papa Innocent III kutangaza vita vitakatifu. Wamohadi hawakuwa na umoja. Khalifa al-Nasir alipoamua kujibu mapigo kwa kushambulia Hispania,

alilisafisha jeshi lake kwanza kwa kuwanyonga maofisa wake waandamizi. Tarehe 16 Julai 1212 al-Nasir alishindwa vibaya sana katika vita vya Las Navas de Tolosa, ushindi ambao Wakristo waliutia chumvi mno. Hata hivyo huu ulikuwa ushindi mkubwa wa kwanza wa Wakristo walioungana dhidi ya Waislamu wa Hispania na Maghrib wakiongozwa na khalifa mwenyewe. Jambo hili liliwafadhaisha sana Waislamu, kwani hii haikuonekana tu kama ni kushindwa katika mapambano, bali ni kushindwa kisiasa kutokana na askari kukata tamaa. Ni jambo la kushangaza kwamba dalili hii ya kusambaratika kwa utawala wa Wamohadi haikuwachochea Waislamu wa Magharibi kuasi tena. Kulikuwepo na hali ya kutokujali. Tunaweza basi kuelewa ni kiasi gani khalifa alisononeka aliporejea Marrakesh haraka, jambo ambalo lilimhuzunisha hadi alipofariki mwaka 1213.

Kusambaratika kwa mfumo wa Wamohadi

Khalifa al-Mustansir aliyemrithi al-Nasir alikuwa kijana mdogo, na mamlaka yake yalidhibitiwa na viongozi wa Wamohadi; kwa mfano hakuweza kuliweka jeshi lake katika nchi ya adui kadri alivyopenda. Zaidi ya hayo, utulivu uliojidihirisha katika enzi yake ulivurugwa na mashambulizi ya Wakristo, kuimarika upya kwa Wabanu Ghaniya, na mashambulizi ya ghafla ya Wabanu Marin ambao hadi wakati huo hawakuweza kuvuka mipaka ya Sahara. Mawaziri nao walijitwalia mamlaka zaidi na zaidi. Baada ya al-Mustansir kufariki, nguvu za kuisambaratisha himaya ziliongezeka zaidi ijapokuwa juhudi za dhati za kuinusuru zilifanywa na al-Mamun (1227-32) na al-Said (1242-8). Jeshi lisilokuwa na umoja lilikuwa linajihami dhidi ya vita vitakatifu vya Wakristo. Ulikuwepo uhasama wa kimya kimya baina ya Wamumini na mashehe wa Kimohadi. Mashehe hawa wakiwa wameshindwa kuwa katika mstari wa mbele kutoa mafunzo ya dini, walianza kujifanya watetezi wa watu dhidi ya mkusanya kodi. Katika mapambano makali ya wenyewe kwa wenyewe yaliyofuatia, wapenda madaraka walishindana wenyewe kwa wenyewe kugombania ukhalifa. Katika hali hii, dhima ya Wakristo na makabila ya Kiarabu iliongezeka. Al-Mamun, mmoja wa wagombea ukhalifa, alifanya mkataba na Ferdinand III wa Kastilia uliomwezesha kuajiri wanamgambo wa Kikristo ambao walimsaidia kumshinda mpinzani wake aliyekuwa amejitangaza khalifa kule Marrakesh. Akiwa mkuu wa himaya, alifanya maamuzi mawili muhimu: uvumilivu kwa Wakristo na kuikana itikadi ya Wamohadi ambayo ni pamoja na kanuni ya Kimohadi na imani kuwa Mahdi hakosei. Tabaka tawala la Wamohadi lilichanganyikiwa kuhusu hatua hii, ambayo ilikuwa ni ishara ya kujipendekeza ili kuleta amani na Wamaliki. Hata hivyo ukweli ni kwamba mbinu hii iliharibu kabisa uhalali wa itikadi ya utawala.

Kuanzia 1230 na kuendelea, al-Mamun aliwategemea kabisa askari wa kukodiwa wa Kikristo, na kulazimika kutoa upendeleo zaidi wa biashara kwa Wakristo na Waarabu wa Hilal ili kumdhibiti mpinzani wake ambaye bado hakuwa

amekata tamaa ya kutwaa ukhalifa. Mwana wake al-Rashid alitawala kutoka mwaka 1232 hadi 1242 kutokana na msaada wa mama yake Habbada, ambaye kwa asili alikuwa mtumwa wa Kikristo, na msaada wa kiongozi wa wanamgambo wa Wakristo.

Vikundi vya Wazungu na Wabanu Marin vilinufaika sana na hali hii. Mnamo mwaka 1242, al-Said, mwana wa al-Mamum na mtumwa mweusi, alipotwaa madaraka, nguvu za kusambaratika ziliongezeka. Baada ya al-Said, Wabanu Marin walitwaa Marrakesh. Ifrikiya ilijitenga katika hatua mbili. Kwanza kuasi na kujitenga kulikofanywa na Yahya Ibn Ghaniya ambaye alitekwa na Abu Zakariyya, mwana wa Mhafsi, Abd al-Wahid. Abu Zakariyya alitwaa madaraka mwaka 1228, na mwaka 1233 alijitangazia uhuru, na hata kudai haki ya kuwa khalifa.

Wakati huohuo Hispania ya Wamohadi ilikuwa inasambaratika. Magavana waliwaachia madaraka Waandalusia, ambao hatimaye walijisalimisha kwa wafalme wa Kikristo. Tawala za kiukoo za wenyeji zilizokuwepo kabla ya Wamohadi, kama vile Beni Mardenish, zilitokeza wakati mwingine, lakini kwa muda mfupi tu na hatimaye kuwa vibaraka wa watawala wa Kikristo. Kufikia mwaka wa 1230, mamlaka ya Wamohadi ilitoweka huko Hispania, na badala yake utawala wa mbali wa Wabbasi, na utawala uliokuwa karibu wa Wahafsi wa Ifrikiya, zikachukua nafasi yake. Hali hii mpya iliwapa wafalme wa Kastilia na Aragon nguvu mpya ya kujipanua.

3

Kuenea kwa ustaarabu Maghrib na athari kwa ustaarabu wa Magharibi

Karne ya Wamohadi

Kilele

Je, kilele cha ustaarabu wa Maghrib kilifikiwa karne ya tisa chini ya utawala wa Waaghlabi wakati majeshi ya Ifrikiya yalipokuwa yakitawala Mediterania na kutishia jiji la Roma? Au karne ya kumi wakati Wafatimi walipoufanya mji wa Mahdiyya makao ya khalifa mpinzani wa khalifa wa Baghdadi? Au ilikuwa katika karne za kumi na mbili na kumi na tatu, wakati Wamohadi wakiongozwa na ukoo wa mfalme wa Waberiberi walipounda himaya iliyotanda Ulaya na Afrika kutoka Tripoli hadi Seville? Kipindi hiki cha mwisho kwa kila hali ndicho kilichozindaka sana kuliko vipindi vingine vyote. Uhusiano kati ya Hispania na Maghrib ulifanana na ule wa Roma na Ugiriki. Mara mbili Hispania iliwashinda washindi wake Waberiberi waliokuwa "washenzi" na kuwateka Wamoravi na kuwafanya wajenzi wa ustaarabu wa Hispania na Maghrib uliovuka mipaka ya Mediterania. Wasudani weusi waliokuwapo kwa wingi katika eneo lote la Maghrib walichangia kwa kiasi fulani katika kuujenga utamaduni huu wa mseto kama walivyofanya watu wenye asili mchanganyiko ambao ndio zao la kizazi cha sasa. Hivi ndivyo pia walivyofanya huko Hispania, hususani Seville na Granada, ambapo waliingiza mila za Waafrika weusi, na wakati mwingine kufanya kuwepo kwao kufahamike katika mazingira ya kitaaluma kama alivyodhihirisha Jean Latin, Profesa wa Chuo Kikuu.

Sanaa

Nusu ya Maghrib ya magharibi ndiyo hasa sehemu ambapo sanaa ya Kimohadi ilionekana, kwani Ifrikiya ilikwishadhoofika sana. Zaidi ya hayo, enzi za utawala wa Wamoravi na Wamohadi zinaunda kipindi kimoja, kwani sanaa ya Wamoravi

ilikuwa ndio kilele eha sanaa iliyoanza katika kipindi kilichotangulia. Wamohadi walikuwa wajenzi maarufu. Majengo yao ya kiraia na ya kijeshi (ikulu na ngome, kazi za umwagiliaji n.k.) yalikuwa mazuri sana, lakini mengi ya hayo yamekwisha haribiwa. Hata hivyo majumba ya makumbusho ya kidini yalihifadhiwa vizuri zaidi, hasa kule Algeria. Hivyo msikiti mkuu wa Marrakesh umetoweka, ila msikiti mkuu wa Algiers uliojengwa 1096 haukuathiriwa sana na marekebisho uliyofanyiwa baadaye. Msikiti Mkuu wa Tilimsan bila shaka ndio unaonyesha kuwa sanaa na usanifu majengo wa Wamohadi ulikuwa wa hali ya juu sana. Msikiti huu likamilika kujengwa mwaka wa 1136. Ni jengo kubwa na la kifahari lililochanganya madhubuti na umakini wa majengo ya Sahara pamoja na uangalifu wa hali ya juu wa sanaa ya Waandalusia. Kuba yake yenye kingo ambayo ni kiwakilishi kizuri cha sanaa ya Kiandalusia, inahusishwa na sanaa ya Kiajemi.

Kwa kulinganisha wingi na utajiri wa nakshi zake, sanaa ya Wamohadi iliongeza ubora na uzuri wa mtindo uliotangulia. Upeo wa sanaa hii unadhihirika zaidi katika *Djamir al-Kutubiyyin* ¹(Msikiti wa wauza Vitabu) ulioko Marakesh, ambao ni mojawapo ya johari za sanaa ya Kiislamu, uliojengwa na Abd al-Mumin mwenyewe. Mnara wenye ghorofa sita wa msikiti huu una urefu wa mita 67. Mukuba matano ya mawemaji ambayo yanafikiriwa kuwa kazi iliyoboea kwa namna ya mtindo wake yanapamba akumbi unaokingamana nayo. Matao yaliyopambwa kwa vijitao yalipita juu ya kumbi kumi na saba na baraza saba na kuipanua nafasi hiyo vizuri sana. Msikiti mkubwa wa Seville, tunu nyingine ya sanaa ya Wamoravi ulijengwa na Abu Yusuf Yukub (1163-84), mrithi wa Abu al-Mumin. Uligeuzwa na kufanywa kanisa kuu, na leo hii mnara wake maarufu uitwao Giralda ndio tu pekee uliobakia. Jengo jingine la fahari sana lilikuwa Msikiti wa Hasan ulioanza kujengwa Rabat na al-Mansur, lakini haukuisha, isipokuwa mnara wake wa ukumbusho (Mnara wa Hasan) ndio uliosalia na kuwa kivutio kikubwa hivi leo. Ni majengo machache ya kiraia ya enzi ya Wamohadi ambayo yanalipo, kati yao ni malango makuu mawili ya Al-Mansur yaliyoko Rabat, kambi (*kasaba*) ya Badajoz, mnara maarufu uitwao Mnara wa Dhahabu, ambao ukiziangalia kwa juu meli zilizokuwa Guadalquivir. Sanaa ya Wamoravi ilikolezwa zaidi kwa kutiwa madoido na rangi nyingi, hasa kutokana na matumizi ya vyombo vya udongo vilivyorembwa kwa rangi nyingi. Hii ilikuwa ni sanaa iliyopevuka, imara na ya kifahari.

Fasihi

Kustawi kwa kazi ya fasihi baada ya kipindi kifupi cha kujishauri mwanzoni mwa utawala wa Wamoravi kanatokana na ukweli kwamba kwa kawaida watawala wa Kiarabu walikuwa kwa asili ni walezi wa sanaa. Katika uwanja huu na kwa kipindi

tunachohusika nacho, Ifrikiya haikung'aa sana kifasihi. Hata hivyo itafaa kumtaja yule mshairi maarufu Ibn Hamdis ambaye alizaliwa Sisilia, na kuishi muda mrefu sana huko Ifrikiya.

Maeneo ambayo yalikuwa na utajiri mkubwa wa wasanii wenye vipaji vikubwa bila shaka yalikuwa Maghrib ya mbali, na hasa hasa Andalusia. Ibn Baki (aliyefariki 1150) aliyatumia maisha yake akisafiri kati ya maeneo haya mawili; Ibn Dihya ambaye alitoka Hispania na akasafiri eneo lote la Maghrib na kufariki Kairo; na mwisho, Ibn Sabl (aliyefariki 1251), mwenyeji wa Seville na mwenye asili ya Kiyahudi, walikuwa wanafasihi wa vipaji vya juu. Lakini wanafasihi wawili wanajitokeza na vipaji vya pekee: Ibn Khafaja (1058-1139) na Ibn Kuzman (ambaye alifariki 1160). Aliyetajwa kwanza alikuwa mshairi wa mazingira mwenye kipawa asiye na kifani aliyestahili kupewa jina la kupanga la al-Jannan (mtunza bustani) kwa sababu ya upya, raha na mahaba katika mashairi yake ambayo hueleza uzuri wa mazingira na furaha ya maisha. Anakumbukwa kuwa ni mmoja wa washairi bora wa Kiarabu hadi sasa.

Ibn Kuzman alikuwa 'mwanamfalme wa ushairi pendwa' (*imam al-Zadajalin*). Aliacha kutumia lugha fasaha na badala yake akalimbua Kihispania-Kiarabu cha mitaani kwa umahiri wa hali ya juu sana.

Alikuwa na sura mbaya sana na aliishi maisha ya kiuasherati na kufanya ufsadi waziwazi. Kila mara alikuwa hana fedha, alifungwa jela mara kadha, na alinusurika adhabu ya kifo. Katika tenzi fupi alizotunga alibuni mizani na mpangilio mpya wa vina, akawa anasifu mapenzi na mvinyo, starehe za hali ya juu zilizojaa wanawake wazuri na wakati mwingine akitumia matusi ya nguoni yaliyokaribia kuwatia watu kinyaa. Mshairi wa nchini kwake Madghalis, na wengine wengi, hata huko Mashariki, walijaribu sana miaka mingi baadaye kufikia tenzi za kipawa cha Ibn Kuzman.

Katika uwanja wa uhakiki wa kazi za fasihi anaweza kutajwa Ibn Bassam (aliyefariki 1148), ambaye alikusanya mashairi mengi yenye busara katika diwani yake, *Dhakhira*, ili kupinga madai ya ubora wa wanafasihi wa Mashariki. Kazi hii iliendelezwa na Ibn Bashkuwal (aliyefariki 1183) ambaye alikusanya mashairi pamoja na wasifu wa watu maarufu 1,400 wa Hispania ya Kiislamu.

Hatuna budi kumtaja pia Ibn Mada'al-Kurtubi (aliyefariki 1195), bingwa wa filolojia, ambaye zama hizo alitetea kuwa sarufi ya Kiarabu itahisishwe; na zaidi ya wote hao ni mtaalamu maarufu wa historia na jiografia, al-Idrisi (1099-1166), ambaye aliishi katika jumba la mfalme Roger wa Pili wa Sisilia.

¹ Kutokana na *Kitab*, neno la Kiarabu lenye kumaanisha 'kitabu'

Falsafa, Tiba na Sayansi

Falsafa ilisitawi sana wakati wa enzi ya Wamohadi, ambao walikuwa wa walezi mkusanyiko wa wanazuoni maarufu kama vile Ibn Bajja (Avenpace aliyefariki 1139), Ibn Rushd (Averroes 1126-1152), Ibn Maymun (Moses Maimonides 1135-1204). Wanazuoni hawa walijishughulisha na sayansi ya vitendo, pia, kama vile tiba, hisabati, na unajimu. Kutoholewa kwa majina yao katika Kilatini unadhihirisha kuwa yalitumika Ulaya wakati wa enzi za kati. Na hivi ndivyo ilivyokuwa kwa Ibn Rushd ambaye alikuwa maarufu kuliko wote. Baada ya kuwa *kadhi*, aliandika kitabu cha tiba na kisha kujishughulisha na unajimu, kabla ya kukaribishwa na Khalifa Abu Yakub Yusuf ili kufafanua mafumbo yaliyomo katika kazi za Aristotle, mwanafalsafa maarufu wa Kiyunani. Hapo Ibn Rushd akaonyesha kipaji chake chote. Lakini wanateolojia walipinga ufafanuzi wake, akalaumiwa na ufedheleshwa, kisha akafukuzwa kutoka nchini na kazi zake kuehomwa moto. Tumeweza kuzipata kazi zake nyingi katika tafsiri za Kilatini na Kiebrania. Ukiachilia mbali ufafanuzi aliofanya wa kazi za Aristotle, ipo pia kazi yake iitwayo *Fasl al-Makal* (Maandiko Dhahiri) ambayo inachambua tatizo kubwa la mgongano kati ya hoja na imani, na nyingine ikiwa ni *Tahafut al-Tahafut* ambamo anakanusha kwa dhati kabisa tasnifu za al-Ghazali, mwanathelolojia maarufu wa Uislamu mkongwe.

Fikra za Ibn Rushd zinakinzana. Hususani, baadhi ya watu wameshambulia utata wa fikra za Ibn Rushd zinazochanganya uyakinifu wa urazini ulio maalumu kwa wasomi, na mjadala unaozingatia misingi ya imani kongwe unaolenga watu wa kawaida. Ukweli ni kwamba mawazo ya Ibn Rushd yanaakisi mazingira alimoishi. Hii inayapa mawazo yake utajiri na kina ambacho hakijawahi kuelezwa. Mawazo yake hakika yameathiriwa sana na Aristotle, kwani alikuwa mchambuzi mkuu wa kazi zake, lakini pia alijihusisha na falsafa yote ya Kiarabu ambayo aliikubali baada tu ya kuihakiki kwa kutumia vikali vipaji asilia vya teolojia, sharia au falsafa menyu (*Tahafut*). Katika enzi ya Wamohadi, hasa mnamo karne ya kumi na mbili, kulikuwa na mabingwa waliobobea katika sayansi za vitendo kama vile mwanabotania Ibn al-Baytar, na zaidi ya wote wanajimu na wanahisabati, Jabir Aflah na al-Zarkali.

Utukufu wa jua linalokuchwa

Baada ya maafa yaliyotokea Las Navas de Tolosa (1212), himaya ya Wamohadi ilisambaratika na nafasi yake kuchakuliwa na falme nne; moja ilikuwa Hispania, na tatu zilikuwa Maghrib.

Granada au usitawi bora na wa mwisho

Ufalme mdogo wa Granada ulikuwa kilele kizuri cha usitawi wa historia kuu na yenye matukio mengi ya ukhalifa wa Kordova. Utawala wa nasaba ya Nasri wa Granada, uliacha majengo mengi ya kihistoria, ya kijeshi na ya kiraia. Majengo haya hayakuwa na usanifu majenzi wowote mpya; isipokuwa usanifu wake uliweza kuoanisha vizuri uwiano stadi wa ukubwa na umbo ambao unavutia sana kwa nje, na mapambo maridhawa na ya fahari sana: jozi pacha za milango na madirisha, safu ya matao ya mawe iliyobebwa juu ya mihimili myembamba ya marumaru, vidaka vya kuingiza mwanga na mabaka ya vivuli. Kuta zake zikiwa zimefunikwa na nakshi za motifu za maua au maandishi au michoro ya kijiometria zinazolingiana kutoka kila upande kama vile muziki usioeleweka na usioisha, pamoja na ulinganifu wa rangi hafifu au zinazong'aa, sanaa ya Granada ni wimbo wa mwisho wa ajabu na wa kupendeza wa sanaa ya Hispania ya Maghrib iliyochokea. Sanaa yake bora kuliko zote inabakia kuwa ile ya Jengo la Alhambra.

Utamaduni ulihipuka katika ruwaza ile ile: wakati ambapo falsafa ilidorora na sayansi za vitendo kusita au kukwama (japokuwa hatuna budi kuwataja tabibu Ibn Khatima na mwanahisabati Al-Kalasadi (1412 - 86)), washairi, wanafilolojia na wanamitindo walitoa kazi nzuri sana, nathari nzuri ziliendelezwa kama zamani, hususani mabingwa wawili kauka tanzu za ushairi na riwaya. Wa kwanza alikuwa Lisan al-Din Ibn al-Khatib (1313-75) ambaye hakuwa na mshindani katika kumudu elimu ya binadamu; alikuwa amebobea katika historia, tiba, na theolojia ya kiroho. Alikwisha kufikiriwa na rafiki yake, Ibn Khaldun, na hata sasa anafikiriwa, kuwa mmoja wa maandishi bora na maarufu wa Kiarabu sanifu. Hata hivyo alizuliwa mashtaka ya uwongo na watu maarufu wenye mamlaka, ikiwa ni pamoja na mfuasi wake, Ibn Zamrak, ambaye pia alichukua nafasi yake kama waziri, akanyongwa akiwa gerezani na mwili wake kuehomwa moto. Lakini Ibn Zamrak, ambaye usanii wa maandishi yake ulishindana na wa Ibn al-Khatib, naye aliuawa kwa amri ya sultan. Kwa ufupi Granada ilikuwa inapembea kati ya utamaduni wa sanaa nzuri sana na matendo ya kishenzi ya mamlaka potovu.

Warithi wa Wamohad huko Maghrib


Tatizo la kutokuwa na nguvu liliwapata pia warithi wa himaya ya Maghrib: Wamarini wa Moroko, Waabd al-Wadi wa Maghrib ya kati na Wahafsi wa Ifrikiya, hali ambayo ilidumu hadi mwishoni mwa karne ya kumi na sita.

Wakati ambapo idadi ya watu ilikuwa inaongezeka sana katika eneo la Magharibi walimoishi Wazungu, watu walikuwa wanapungua sana katika eneo la Magharibi walimoishi Waislamu. Hali hii ilikuwa mbaya zaidi mnamo katikati ya karne ya kumi na nne. Ibn Khaldun ambaye alidhani kuwa kupungua kwa idadi ya

watu ilikuwa sababu mojawapo iliyofanya ustaarabu usambaratike alizingatia hali hii na mambo yote yaliyofuata: kufikia kwa kilimo, na kuenea kwa Wanomadi. Mji wa Kayrawan uliokuwa na wakazi malaki kadha mnamo karne ya tisa ulibadilika na kuwa mji mdogo mnamo karne ya kumi na nne. Kwa mujibu wa Leo Africanus, idadi ya watu wa Bijaya ilipungua hadi kufikia theluthi moja ya wakazi wa awali. Idadi ya wakazi wote yaelekea ilipungua kwa theluthi mbili. Maradhi ya milipuko yalikuwa ndiyo sababu na matokeo ya mabadiliko haya ya kutisha ambayo, kama Ibn Khaldun alivyosema, yaliitumbukiza pwani ya kusini ya Mediterania katika machweo wakati ambapo pwani ya kaskazini ilikuwa inaona mapambazuko ya *kipindi cha mwamko*.

Katika usanifu majengo, athari ya Granada ilijitokeza zaidi Moroko na Algeria ya magharibi. Wamarini walikuwa ni wajenzi maarufu pekee. Mnamo karne ya kumi na tatu aina mbili mpya za majengo zilijitokeza. Kwanza kulikuwa na madrasa, chuo cha elimu ya juu ambacho ujenzi wake uliigwa kutoka Mashariki. Sehemu ya ndani ya uga wa jengo hili imezungukwa na roshani zenye vyumba vya wanafunzi vinavyotokezea nje, na upande mmoja kuna chumba kikubwa chenye *mihra bu* ambacho hutumiwa kama darasa na chumba cha kusalia. Jengo lililokuwa kubwa kuliko yote ni Abu Inaniyya lililopo Fez. Jengo jingine lilikuwa *zawiya* ambalo lilikuwa likitumiwa kama ukumbi wa jumuiya ya watu, na ziyara (maziko) takatifu ya mwanzilishi wake.

Mtindo wa majengo haya unaonyesha ustadi kamili usiokuwa na ubunifu wowote mpya. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa upande wa utamaduni pia, kama Ibn Khaldun alivyosema, "maendeleo ya kujifunza yalivia kabisa." Sayansi razini ndizo hasa zilizodhibitiwa na wanateolojia wasiopenda mabadiliko. Mmoroko, Ibn al-Banna (1256-1321) alikuwa mwanahisabati wa mwisho, wakati Mwifrikiya Ibn al-Kammad alikuwa mnajimu wa mwisho. Mmoroko, Ibn Battuta (1304-1377) msafiri maarufu aliyewahi kuzuru Afrika, Mashariki ya Kati, India na China, alikuwa bingwa wa jiografia elezi iliyokuwa katika masimulizi ya safari (*rihla*). Mwisho, kati ya wanahistoria mabingwa, Ibn Khaldun (1332-1406), Mwanahistoria aliyefunzwa na al-Abidi wa Tilimsan ndiye aliyekuwa maarufu kuliko wote. Kwa jumla ulimwengu wa wasomi ulikuwa umelasisirika sana. Tondozi na hotuba zilizotolewa wakati wa mazishi zilidhihirisha hila na unafiki. Uchapwa na hata tungo kauleni za kiasherati zilichukua nafasi ya tungo adhimu za wakati uliotangulia. Hata hivyo umbo la nje la kazi hizo chache za fasihi lilijengwa vizuri sana. Hata hivyo, kazi hizi za kisanaa zilishuhudia kuwepo kwa wasomi mabwanyenye, miongoni mwao wakiwemo wanawake, wa utamaduni uliorithiwa na kufunzwa badala ya kuwa zana ya ubunifu wa kiakili na kisani. Walipenda sana muziki ambao ulikuwa na athari kubwa ya Waandalusia, wakafurahia sana kucheza dansi; kama Leo



3.1 *Alhambra ya Granada: chumba kilichoshikana na Kitala cha Simba, sanaa ya kuchongwa yenye urembo, karne ya kuu na tne*

Africanus anavyosema, kuhusu watu wa jamii ya juu huko Bijaya: "Ustaarabu wa wapokea riba ulikuwa unafuata ule wa enzi kakamavu zaidi ya waanzilishi na wabunifu."

Athari ya Maghrib kwa ustaarabu wa Magharibi (Ulaya)

Ingawa Waislamu wa Magharibi na Wakristo wa Magharibi walichukua njia tofauti na zinazokinzana, hawakuwahi kuacha kuhusiana katika namna nyingi tofauti.

Kubadilishana vitu

Biashara baina ya Maghrib na Hispania na nchi nyingine za Ulaya ziliendeshwa kwa mikataba ambayo pia ilidhibiti makazi ya watu binafsi. Kwa hivyo Wazungu walidhibiti makazi yaliyoitwa *Funduk* katika miji mikuu iliyokuwa Maghrib (Tilimsan, Marrakesh n.k.). Makazi hayo yalijumuisha mikahawa, mahali pa kuabudia na ofisi za biashara zilizoendeshwa na balozi aliyeteuliwa na mamlaka zenye madaraka. Bali kinyume chake hakikutokea: Wafanyabiashara wa Maghrib hawakuweza kuendesha usafiri wao wa baharini au kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi kwa ajili ya kuuza nje. Kodi zilizolipwa na wageni zilitumiwa hasa kutunisha hazina ya dola.

Muundo wa biashara vilevile ulionyesha ukosefu huo huo wa uwiano wa kibiashara. Kinadharia, hapakuwa na kikomo cha bidhaa zilizoingizwa nchini kutoka nje kwa kila upande; ilihali katika kusafirisha bidhaa nje baadhi ya bidhaa nyeti zilipigwa marufuku au kiasi fulani tu kiliruhusiwa kama vile silaha, chuma,

mbao n.k. Licha ya kanuni hizi rasmi, Waiberia waliuzia Magrib metali, mbao, bidhaa za ehuma, viungo vya chakula, mvinyo, karatasi na hasa nguo. Kutoka Maghrib, walinunua sufu, ngozi, nta (hata mji wa Bijaya uliipa lugha ya Kifaransa neno *Bougie* likimaanisha mshumaa wa nta), tende na mazulia na bidhaa nyingine za mikono. Ufalme wa Aragon ulijitahidi kudhibiti njia ya biashara ya Barselona-Majorjka-Tilimsan-Sijilmasa ambayo ilitumiwa kusafirishia dhahabu ya Sudan hadi bonde la Mediterania.

Maghrib ilipata nakisi katika biashara hii ya kubadilishana bidhaa. Hata hivyo ilikuwa msafirishaji nje mkubwa wa mafanikio ya urithi wa utamaduni wake ambao haikuweza tena kuuendeleza.

Kubadilishana utamaduni

Katika kipindi hiki Maghrib ilihamisha urithi wa utamaduni wake na pia kuwa kama njia ya kusafirishia maadili ya Uislamu kutokea Misri na Mashariki.

Muktadha na motisha

Mnamo karne za kumi na mbili na kumi na tatu, Wakristo wa Magharibi walikuwa wavumilivu wa mambo mbalimbali kutoka Maghrib na waliendelea kuwa hivyo hadi Granada iliposambaratika mwaka 1492, wakati baraza la kudhibiti wazushi wa dini lilipoleta mabadiliko katika mwelekeo wa watu.

Kulikuwepo na sababu mbili kuu zilizofanya kuwepo kwa uwazi huu wa asili: udadisi au huruma wa kweh, na mkakati wa kiroho. Roger II wa Sisilia (1105-54) na Frederick II (1194-1250) walizungukwa na wasomi wa Kiarabu. Petro I wa Aragon (1094-1104) alitia saina barua zake kwa Kiarabu na kupiga chapa sarafu zake kwa mtindo wa Kiislamu. Lakini Wadominika na Wafransiska walitamani kupata ushindi wa kiroho. Ramon Llull (1235-1315) alitumia muda wa maisha yake kufanya mazungumzo na Waislamu, kuandika makala kwa Kiarabu, kuhubiri huko Maghrib na kujaribu kutumia falsafa na vita vya msalaba ili kukomesha Uislamu. Aliwahimiza mapapa na wafalme wa Ulaya kutumia mbinu zake. Katika kikao cha Baraza la Vienna cha mwaka 1311, alipendelea kuanzishwe vyuo vya Taaluma ya Kiarabu, na kuundwe mamlaka ya kijeshi itakayoangamiza Uislamu. Jambo la ajabu ni kwamba Roman Llull aliathiriwa sana na Ibn al-Arabi (1165-1240) Mwislamu sufu maarufu zaidi wa Hispania, kiasi cha kufahamika hapo baadaye kama "sufii wa Kikristo".

Taaluma kuhusu Waarabu

Athari ya Waislam na Waarabu ilienea kupitia njia kuu mbili: njia ya Wataliani inayopitia Sisilia, na njia ya Waiberia inayopitia kusini mwa Ufaransa. Ikilinganishwa na njia hizi, vita vya msalaba vilielekea kuwa finomena nyepesi zenye kutokea kinyumenyume.

Athari ya tapo la Kiitaliano ilienea kutoka Salerno ambako Konstantini Mwafrika (Constantinus Africanus), aliyekuwa tabibu na mfanyabiashara kutoka Tunis alibatizwa na kuwa mkristo na hatimaye kufanywa mkuu wa nyumba ya watawa ya Monte Kassino. Lakini hasa ilikuwa ni Palermo, luoko Sisilia, ambapo kutokana na kutiwa moyo na Frederiki II (1194-1250) na watawala wa mwanzo wa Angevin kipindi maarufu cha kazi ya kutafsiri kutoka Kiarabu kwenda kwenye Kilatini kilianzishwa na watu kama mnajimu Theodori, na hasa Msikochi Michael Scot na Myahudi Faraji bin Salim wa Agrigento.

Huko Hispania vuguvugu hili la tafsiri lilianza mnamo karne ya kumi huko Katalonia katika makazi maarufu ya watawa ya Ripoll. Hata hivyo ilikuwa katika karne ya kumi na mbili ambapo Barcelona ilikuwa kituo maarufu cha shughuli za tafsiri, ambapo Plato Tiburtinus na Myahudi wa Andalusia Savasorda (Sahib al-Shurta) walitafsiri kazi mbalimbali za unajimu na elimu ya nyota, ikiwa ni pamoja na jedwali muhimu zilizotayarishwa na al-Battani (Albatenus). Toledo palikuwa mahali pengine palipowavutia wanazuoni kutoka Ulaya yote, pakitimiza dhima ileile katika kuweka misingi ya utamaduni wa Wakristo wa Magharibi, kama ilivyofanya Baghdad mnamo karne ya tisa ilipokusanya urithi wa Kiyunani kwa ajili ya ulimwengu wa Waarabu. Alfonso X Mwenye Hekima (1252-1284), alishabihiana na al-Mamun (813-33), aliyetamani kuwa kama Aristotle. Maaskofu wakuu wawili, Raymond, na kisha Rodrigo Jimenez de Rada (1170-1247), walikuwa wakuu wa taasisi ya Toledo ambayo waanzilishi wake wa mwanzo walikuwa Wayahudi na Wamozarabi. Kwa hakika tafsiri za mwanzo zilikuwa katika Kiebrania kabla ya kuwa katika Kikastilia na Kilatini.

Miongoni mwa wafasiri maarufu walikuwa mwanafalsafa maarufu Dominicus Gondisalvius wa Segovia, na Mwingereza Robert wa Ketton ambaye alimtafsiria Petro Mstahiki, mwanamageuzi wa Kluny, Kurani ya kwanza katika Kilatini. Lakini zaidi ya wote ni Gerald wa Kremona (1114-87) ambaye raghba yake isiyo kikomo ilimwezesha kutafsiri si chini ya kazi 70. Kipindi cha pili cha tapo la Toledo kilitawaliwa na Michael Scot.

Mfano huu ulikuwa na matokco makubwa sana. Taaluma kuhusu Waarabu ziliongezeka. Mwaka 1250 Ibn Rashiq wa Mursia alikutana na Wadominika katika makazi ya watawa ya jiji lile wenye kufahamu vizuri Kiarabu na Kurani. Zaidi ya hayo Alfonso X ahiweka shule ya Mursia chini ya uongozi wa mwanafalsafa wa Kiislamu wa eneo lile. Aidha mwaka 1250 Taaluma kuhusu Waarabu iliyoanzishwa Tunis na Wadominika ilinufaika kutokana na mchango wa Ramon Marti ambaye alitunga kamusi ya Kiarabu - Kilatini. Mwaka 1276 Mfransiska Ramon Llull alianzisha huko Majorka chuo maarufu cha Miramar ambako watawa walianzishwa kujifunza Kiarabu kabla ya kusafiri kwenda nchi za Waislamu kueneza injili. Hatimaye, kufuatia pendekezo la Baraza la Vienna, Taaluma za Kiarabu

zilianzishwa Oxford, Paris, Roma na Bologna ambapo Leon Africanus alikuwa bado anafundisha mnamo karne ya kumi na sita. Huko Marseilles familia moja ya Kiyahudi kutoka Granada, familia ya Ibn Tibbon, ilijipambanua kama wafasiri wazuri wa kazi za Kiarabu katika Kiebrania.

Tafsiri za kazi kutoka Andalusia na Maghrib na athari zake

Falsafa

Enzi za Kati za Ukristo ziligundua, zikaelewa na kutambua fikra za kale kupitia kwa wanafalsafa wa Maghrib na Andalusia ya Waislamu. Ibn Bajja (Avempace) na Abubakar walifahamika katika Enzi za Kati za Walatini, japokuwa ni tafsiri za Kiebrania pekee za kazi zao ndizo zimebakia kutoka katika kipindi hiki. Tafsiri ya kwanza ya Abubakar inayoitwa *Philophus Autodidactus* ilichapwa takribani katika mwaka wa 1671. Lakini bingwa kushinda wote bila shaka yoyote alikuwa Ibn Rushd (Averroes), ambaye vitabu vyake vingi vimetufikia vikiwa katika tafsiri za Kilatini au Kiebrania. Alijadiliwa kwa undani. Miongoni mwa wafasiri wengi na waenezaji wa kazi zake ni muhimu kumtaja Msikoehi Michael Scot (aliyefariki 1235) na Watibboni wa Provence. Ibn Rushd, mpinzani wa al-Ghazali na mwandishi wa *Tahafut*, iliyotafsiriwa kwa jina la *Destructio destructionis*, alionekana kama bingwa wa urazini na *mpinga dogma*. Kwa hivyo makundi mawili yasiyoweza kupatana yalitokea. Katika kundi la Averroes alikuwepo Siger wa Brabant wa Chuo Kikuu cha Paris. Lakini Averroes alipodai kuwa dunia haitakwisha na kukanusha kuwa roho ya binadamu inaishi milele alipingwa kwa nguvu sana na Albertus Magnus (1206 - 80) na Ramon Llull. Mawazo ya Averroes yaliwagawanya wanazuoni maarufu ambao kwa hamaki waliamua kujiunga na mojawapo ya kambi hizi. Siger alitengwa na kufungwa, na akafariki mwaka 1281.

Wachoraji walimwonyesha Averroes katika picha zao: kwa mfano kule Pisa, Andrea Orcagna anamweka (Averroes) kando ya Muhamadi pamoja na Mpinga Kristo katika jehanamu yake. Mnamo 1340 Fransisko Traini alimchora akiwa kichwa chini miguu juu, chini ya miguu ya Mt. Thomas Aquinas. Iliwahi kusemwa kuwa Mt. Aquinas "alikuwa kwa wakati huo huo mpinzani mkali na mfuasi mkubwa sana wa Averroes" (Ernest Renan). Madondoo mia tano na tatu kutoka kwa Ibn Rushd yamehesabiwa katika maandishi ya Mt. Thomas Aquinas. Akiwa amesahihishwa au kueleweka vizuri zaidi, Ibn Rushd alishinda kwa mara nyingine mnamo karne ya kumi na nne. Mnamo karne ya kumi na tano Louis XI wa Ufaransa alipounda upya ufundishaji wa falsafa alipendkeza mafundisho ya Aristotle na ya mhakiki wake Averroes ambayo kwa muda mrefu sana yalitambuliwa kuwa yenye

manufaa na ya uhakika. Katika Chuo Kikuu cha Padua, mawazo ya Averroes yalipata matokeo mazuri sana ambayo yalidumu hadi kufikia karne ya kumi na nane.

Sayansi

Maandishi ya tiba aliyoandika Ibn Rushd yalifasiriwa mjini Padua na Myahudi Bonaeossa. Hali kadhalika maandishi bora ya shule maarufu ya tiba ya Kayrawan (Ishak ben Imran) yalifasiriwa na Constantinus Africanus mnamo karne ya kumi na moja na kutumiwa kufundishia huko Salerno. Maandishi ya tiba ya Ishak al-Israili yaliendelea kupendwa sana hadi karne ya kumi na sita. *Kitab al-Tarif* kilichoandikwa na Mwandalusia Abu al-Kasim (Abulcasis 936 - 1013) kilipendwa sana katika kipindi chote cha enzi ya kati japokuwa sio kama maandishi ya Avicenna, *Misingi ya Tiba (The Canon of Medicine)*, ambayo yalifikiriwa kuwa ni Biblia ya Tiba na matabibu wote wa zama hizo. Hali kadhalika famakolojia ya zama ya kati inayo mambo mengi yanayotokana na kazi za Mwandalusia Ibn Wafid (Abenguefit (988 - 1074). Maandishi yake yalitafsiriwa na kuitwa *De medicamentis simplicibus*. Mchango wa Andalusia na Maghrib kwa hisabati na sayansi ya unajimu ulikuwa muhimu pia. Adelard wa Bath alitafsiri *Jedwali za Unajimu* za Maslama al-Majriti ambazo ziliandikwa yapata mwaka 1600 kufuatia kazi ya Al-Khuwarizmi.

Karne ya kumi na tatu ilishuhudia pia kutafsiriwa kwa saiklopedia nyingi za unajimu za Mwifrikiya Ibn Abi al-Rijal zilizotafsiriwa na Yehuda ben Moshe. Gerald wa Kremona naye alitafsiri Jedwali ya Al-Zarkali (Azarquiel) ambayo ilifahamika sana Ulaya ya enzi ya kati yote kama *Tablas Toledanas*. Baina ya karne ya kumi na tatu na kumi na sita, *Makala Juu ya Unajimu* ya al-Bitruji (Alpetragius) ilitafsiriwa mara kadha, jambo linalodhihirisha kuwa ilifanikiwa sana. Mintarafu mwanahisabati mwenye kipaji cha hali ya juu sana, Leonardo wa Pisa (aliyezaliwa takriban mwaka 1175) ambaye aliishi kwa muda mrefu Bijaya (Bougie), alikopa mengi kwa Waarabu katika aljebra na mfumo wa tarakimu ambao aliuanzisha Ulaya.

Lugha, Fasihi na Sanaa

Suala la athari ya fasihi katika Kiarabu kwa Ulaya ya enzi za kati limekuwa likijadiliwa kwa shauku kubwa.

Je ushairi wa manju watembezi wenyec dhamira za mapenzi ya heshima uliotungwa karne ya kumi na mbili na kumi na tatu ukitumia arudhi mpya, ulikuwa ni wa asili ya Kiarabu? Jean Anglade anasema, *hapana*. Waandishi wengine kama

vile Ramon Menendez Pidal wanasema *ndiyo*. anaonyesha ushabihiano ulio wazi kabisa kati ya ushairi wa Ibn Kusman na ushairi wa Languedoc uliowakilishwa na Guillaume IX wa Poitiers. Aina hii ya athari inaonekana kuwa ni matokeo ya kawaida ya uhusiano wa kutegemeana wa jamii hizi mbili, wenye chimbuko lake Andalusia, ambao kabla ya karne ya kumi na mbili ulitawala mahusiano ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

Kwa upande mwingine, athari za Waarabu Waislamu kwa kazi ya Dante *Komedia Takatifu* zinatambulika kila mahali; hasa baada ya kugundulika kwa tafsiri ya *Miraji*, hadithi pendwa kuhusu kupaa mbinguni kwa Muhammad. Hadithi hii ilipendwa sana na Waislam wa Hispania. Imethibitishwa kuwa Dante aliifahamu, japo hili haiathiri kwa namna yoyote ile kipaji chake.

Urafiki wa muda mrefu baina ya Waislamu wa Magharibi na Wakristo wa Magharibi uliacha alama nyingi katika lugha za Ulaya. Maneno kama "algebra," "logarithm," "azimuth," "algebra," "alcohol," "cipher," "Ushuru," "syrup," "sukari" na mamia mengine yanayohusiana na hisabati, unajimu, tiba, kemia, botania n.k. yana asili ya Kiarabu. Katika Kihispania maneno kama hayo yanafika takribani elfu nne. Athari ya kisani ilivuka usanifu majengo wa Andalusia na kuathiri sanaa ya usanifu majengo ya Kirumi, kama alivyoeleza Male. Halikadhalika sanaa ya mapishi ya Ulaya ya enzi ya kati iliathiriwa.

Hitimisho

Kwa kupitia madaraja mawili ya Sisilia na Hispania, utamaduni wa Kiafrika ukiwa katika umbo la Andalusia - Maghrib ulipenya utamaduni wa Ulaya Magharibi, hadi karne ya kumi na nne. Hali hii iliendelea hadi utamaduni huu ulipokoma kuwa na nguvu katika nchi yake ya asili kutokana na kusambaratika kwa utawala na kupungua kwa watu katika nchi hiyo. Hapo utamaduni huo ulitekwa nyara na Ulaya iliyokuwa na ongezeko kubwa la watu, baada ya kutambua thamani ya maarifa yasiyo na kifani iliyoyapata, ambayo, iliyageuza nyenzo ya ustawi wake wa kihistoria.



*Kusambaratika kwa
umoja kisiasa
katika Maghrib*


Kuanguka kwa Wamohadi

Baada ya kushindwa katika vita vya Las Navas de Tolosa, utawala wa Wamohadi uliendelea kusambaratika polepole lakini kwa uhakika. Nchi za kwanza kujitenga zilikuwa katika Afrika na al-Andalus na kisha katika Maghrib ya kati (Tilimsan). Mwishowe ilifuatia Moroko na kumalizia na kitovu cha kusini cha asili cha utawala wa Wamohadi ambacho mwaka 1269 kilitakwa na Wamarini.

Sababu zilizochangia kuanguka huku ni kwanza, ukubwa wa himaya yenyewe ambayo ilitapanya nguvu za makhalifa waliosambazwa kati ya Maghrib ya Mashariki na Hispania na kufanya utawala wowote wa kutoka makao makuu kuwa mgumu. Pili mazingira mabaya ya kijiografia ya mahali palipokuwa mji mkuu, Marrakesh, yaliongezea matatizo yaliyokuwepo.

Hali hii ndiyo kisa cha kuwepo kwa uasi mwingi kutoka kwa Waarabu wa Kinomadi, Wa-Banu Ghaniya na wakazi wa mijini. Zaidi na zaidi, ufalme ulibidi kuomba msaada kutoka kwa Waarabu, Waberiberi, na hata askari wa kukodiwa wa Kikristo, na hivyo kuharibu fikra za mwanzoni za umoja. Aidha, mamwinyi wa Kimohadi waliazimia kubaki na marupurupu yao na waliwaona Waislamu wasio Wamohadi kuwa ni makafiri. Lakini, manwinyi wenyewe hawa waligawanyika katika koo mbili. Kwa upande mmoja kulikuwa na Wazawa wa 'Abd al-Mu'min, waliojulikana kama *Ma-Sayyid*. Kwa upande wa pili kulikuwa na Wamohadi wa Masmuda na mashehe wa dini. Kundi hili la pili, lilipambana na urasimu wa Waandalusi uliotambua anri ya khalifa.

Mwaka 1230 ugomvi kati ya ufalme na mashehe ulidhihirika pale mwana mmoja wa mfalme aitwaye Ya'kub al-Ma'mun alipokuja kutoka Hispania akiongoza jeshi la wapanda farasi wa Kikristo na kulipiga jeshi la khalifa



4.1 Ugawanyikaji wa himaya ya Waalmohadi (J: Hrbek)

aliyekuwa anatawala.

Alijitangaza kama *Amir al-Mu'minin* na kuwaua mashehe na kisha akatupilia mbali kuungama kwa Kimohadi. Mrithi wake, al-Rashid (1232-42), alipojaribu kurudisha tena itikadi ya Mahdi kwa kukubaliana na mashehe, mambo yalikuwisha chelewa. Machafuko ya utawala yalikuwisha kuwa hayatibiki. Khalifa wa mwisho wa Kimohadi aitwaye Al-Wathik alipinduliwa na Wamarini mwaka 1269.

Migawanyo mitatu ya Maghrib

Migawanyo hii mitatu iliirudisha Maghrib kwenye hali iliyokuwa nayo kabla ya utawala wa Wafatimi: hali ya kuwa na madola matatu ambayo yalidhoofishwa na vurugu za ndani zisizokwisha, na pia mashambulizi ya kutoka nje yaliyofanywa na maadui wa Kikristo. Madola haya matatu baadaye yakawa Tunisia, Algeria na Moroko. Madola yote matatu yalitawaliwa na falme zenye asili ya Waberiberi zilizoathiriwa sana na Uarabu. Tawala hizo zilidhibiti miji na makundi yaliyostakimu kwenye mbuga. Maeneo ya milimani na mbugani yalikuwa ndiyo makazi ya Waberiberi na Waarabu wa milimani, ambao walikuwa tayari kushambulia miji wakati wowote mamlaka kuu ilipolegalega.

Masultani wa falme mbili kuu (Wahafsi na Wamarini) kwa nyakati tofauti walipigania cheo cha ukhalifa. Lakini hata wakati Al-Mustansir, mtawala wa Wahafsi, alipotambuliwa na masharifu wa Maka na Mamluki wa Misri katikati ya karne ya kumi na tatu, hali hii ambayo haikudumu kwa muda mrefu, haikurudiwa tena katika enzi ya ukhalifa wa Kiabbasi huko Kairo.

Aidha madola haya matatu yalipata matatizo kutokana na ongezeko la shinikizo la kijeshi, kisiasa na kiuchumi la madola ya Kikristo yaliyozunguka Mediterania; madola haya matatu yalishindwa kuzuia kuanguka kwa Granada, mabaki ya mwisho ya Hispania ya Kiislamu; ni kuzuka tu kwa utawala mpya wa Kiislamu wa milki ya Ottoman kulikozuia uwiano wa nguvu kuhamia kabisa kwenda upande wa nchi za Kikristo za Ulaya. Kazi hii ya kuhifadhi uwiano wa nguvu kati ya madola ya Kikristo na Kiislamu ilisaidiwa pia na sera ya nchi za Iberia wakati huu ya kuwekeza rasilimali na nguvukazi kubwa zaidi katika mabara mengine ng'ambo ya bahari ya Hindi na Atlantiki.

Falme tatu ambazo sasa zilikuwa zinatawala Maghrib zilikuwa: Wahafsi (1228-1574) huko Tunis, wa Abd al-Wadidi au Wazayyani (1235-1554) huko Tilimsan, na Wamarini (1230-1472) huko Moroko.

Wahafsi

Mwanzilishi wa ufalme huu alikuwa rafiki mpenzi wa Mahdi Ibn Tumart aliyetitwa Shehe Hafs Ibn `Umar. Mtoto wake alikwisha tawala Ifrikiya kwa madaraka kamili, na mjukuu wake, Abu Zakariyya, aliacha kutaja jina la khalifa katika hutuba ya swala ya Ijumaa na badala yake akajitaja mwenyewe mara tu baada ya kupata cheo cha Amir mwaka 1229. Alirudisha kawaida za kale za Wamohadi na hatimaye kukomesha maasi ya Wabanu Ghaniya, akateka miji ya konstatini, Bijaya na Algiers na kulazimisha utawala wake juu ya Wazayyami, Wamarini, na Wanasri wa Granada. Mji Mkuu wa Tunis ulifunguliwa tena kufanya biashara na Ulaya ingawa ilibidi ulipe kodi kwa Mfalme Frederick II, mtawala wa Sisilia kwa kibali cha kuanzisha tena biashara za bahari na uhuru wa kuagiza ngano ya Sisilia. Almustansir (1249-77) alipochukua kiti cha baba yake, Abu Zakariyya, alirithi ufalme uliostawi na utawala usiotishika. Hivyo ilikuwa ni jambo la kawaida kwa al-Mustansir kuchukua cheo cha *Amir almu`minin* mwaka 1259 na kutambuliwa kwa kipindi kifupi tu kama khalifa Misri na Maka. Khalifa wa mwisho wa Kiabbasi wa Baghdad alikuwa ameuawa karibuni na Wamongoli mwaka 1258 na kiti cha ukhalifa kilikuwa bado kiko wazi. Hata hivyo, mnamo mwaka 1261, Sultani wa Kimamluki aitwaye Baybars, alimtawaza khalifa kibaraka wa Kiabbasi chini ya udhibiti wake huko Kairo. Hata hivyo, Al-Mustansir aliimarisha sifa yake katika ulimwengu wa Kiislamu kutokana na matokeo mabaya (kwa Wakristo) ya mapambano ya kidini dhidi ya Tunis yaliyoongozwa na mfalme Louis IX wa Ufaransa.

Kama Mfalme Louis alipotoshwa katika kuamini kuwa mtawala wa Kihafsi alikusudia kuritadi (kuingia Ukristo), au alishawishiwa na baadhi ya wafanyabiashara wa Provençal waliokuwa na nia ya kukomboa madeni yao, huu ulikuwa ni ushauri potovu wa kusikitisha. Kaka yake aitwaye Charles wa Anjou, Mfalme wa Sisilia, akaharakisha kutafuta amani na Tunis. Hivyo Tunis ikakubali kuendelea kulipa kodi na uhusiano wa kibiashara ukaanza tena na kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, chini ya tawala hizi mbili za Abu Zakariyya na al-Mustansir, utawala wa Wahafsi ulitambuliwa toka Hijaz hadi AndalusiA.

Baada ya utawala wa al-Mustansir kulikuwa na machafuko kwa karibu karne moja yaliyoambatana na kuuana wenyewe kwa wenyewe, maasi ya Waarabu na upinzani wa mara kwa mara, hasa katika miji ya Konstantini na Bijay. Ilikuwa ni katika vipindi hivi ambapo harakati za kujitana zilijitokeza na Wamarini wa Moroko kushikilia eneo la Wahafsi mara mbili (mwaka 1348 na 1357) pamoja na Tunis.

Ilikuwa ni Abu al-'Abbas (1370-94) aliyerudisha heshima ya ufalme kwa kuiunganisha na kuipanga nchi upya. Chuki ya wazi iliyokuwepo baina ya WaTilimsan na Wamarini wa Moroko ilimwondoshea wasiwasi kabisa kwa upande wa magharibi. Wakati wa utawala wake mwanae, Abu Faris (1394-1434), ambaye alitawala kipindi kirefu, aliimarisha kazi hii na kuchagua magavana miongoni mwa watumwa huru. Utawala wake ulikubalika hadi sehemu za mbali kama Tilimsan nchini Moroko na hata Andalusia. Abu Faris alipata mafanikio yake kutokana na kujali haki, kwa mfano, miongoni mwa jamii nyingi katika ufalme (Wamohadi, Waarabu, na Waandalusia), uvumilivu wake kwa Wayahudi, ukarimu wake kwa viongozi wa dini *Maulama* au *Masharifu*, na pia kwa kujenga kumbukumbu nyingi, kukataza kodi haramu na tamasha kubwa za maadhimisho ya sherehe za Kiislamu.

'Uthman, mjukuu na mrithi wake (1443-88) alikuwa na kipindi kirefu sana cha utawala. Alisumbuliwa tu na ghasia za baadhi ya watoto wa mfalme, baa la njaa na milipuko ya tauni.

Baada ya utawala wake, kipindi hiki cha pili cha utawala wa Wahafsi kiliporomoka haraka kama kile cha kwanza, na kutoa mwanya wa fujo baada ya kumalizika kwa karne ya kumi na tano, na hivyo kufanya ufalme kushindwa kutumia fursa ya mapambano makubwa kati ya Hispania na milki ya Ottoman ili kuitawala Mediterania.

Wamarini

Kwa asili, Wamarini walitoka Mzab na walitokana na watu watukufu miongoni mwa Wazenata. Hawakujua pesa wala kilimo, wala biashara. Walithamini ngamia, farasi na watumwa tu. Matatizo yao ni kielelezo kizuri cha nadharia ya Ibn Khaldun kuhusu umuhimu wa "moyo wa udugu" (*asabiyya*) katika kuiteka nchi na kuanzisha madola. Baada ya kupigwa kule Las Navas de Tolosa (1212), Wabanu Marin wakastakimu katika mbuga zinazokaribia Sahara. Kutoka hapo walifanya uvamizi wa sehemu za kaskazini mashariki mwa Moroko na uanzisha utawala wao wakitoza kodi toka kwa wakulima au mijini kama vile Fez na Taza. Tamaa za kisiasa zikafuata. Muda mrefu waliochukua kukamilisha utekaji wa utawala, tangu mwaka 1240, wakati waliposhindwa na jeshi la Wamohadi kabla ya Mekues, hadi mwaka 1269 walipoukamata mji wa Marrakesh, bila shaka huweza kuelezeka kutokana na ukosefu wa msukumo wa kidini kati yao. Ilikuwa mi katika utawala wa Abu Yusuf Ya'qub (1258-86) ambapo mji wa Fas al-Jadid (Fez Mpya) ulifanywa kuwa mji mkuu.

Kabla ya muda mrefu kupita, Wamarini, ambao ni watu wakao jangwani, walitekwa na mazigazi ya kaskazini pamoja na mbuga za kijani za Andalusia,

kama ilivyokuwa kwa Wamoravi na Wamohadi kabla yao. Hapa tena, kama ilivyokuwa kwa Wahafsi, kulikuwa na vipindi viwili virefu. Kipindi cha kwanza kilianzia mwaka 1258 hadi 1307 chini ya utawala wa Abu Yusuf Ya'kub na mtoto wake aliyeitwa Abu Ya'kub Yusuf. Kipindi cha pili kilikuwa chini ya utawala wa Abu al-Hasan (1331-48) na kisha mtoto wake aliyeitwa Abu 'Inan Faris (1349-58). Ilikuwa wakati wa kipindi hiki cha pili ambapo kwa muda tu Wamarini walidai kuitawala Maghrib.

Mojawapo ya maendeleo inuhimu chini ya utawala wa Wamarini ni kukua kwa umaarufu wa Waarabu. Wamarini walifanya tathmini ya kisiasa na kuona kuwa wasaidizi wao wa Zenata ni kundi dogo sana. Kwa hiyo, waliungana na Waarabu ambao walikuwa wamekwisha changanyika nao sana. Waarabu wa Kinomadi walihimizwa kuhamia nchini. Vikundi vingi vya Kiberiberi vilirithishwa utamaduni wa Kiarabu. Kiberiberi, ambayo ndiyo ilikuwa lugha ya majeshi ya Wamoravi, na Wamohadi kilitoa nafasi kwa Kiarabu ambacho ndicho kilichofanywa lugha rasmi. Hatua hii ambayo iliwanufaisha Waarabu wa Kinomadi, iliwafanya waingilie ardhi ya wakulima. Mashamba, bustani, na misitu ikageuzwa sehemu za Malisho. Ukazaliwa mfumo wa kudumu wa makundi inatatu ya kijamii, yaani wanomadi, wakazi wa mijini, na wakazi wa milimani. Miji na viunga vyake pekee vilikuwa chini ya utawala wa Sultani moja kwa moja ambapo *Wamakhzan kabila*, Waarabu na Wazenata, kwa kiasi kikubwa walijitawala wenyewe. Lakini, Waberiberi wa Atlas, Warif na Wajabal, walibaki nje ya madaraka ya aina yoyote, hata yale yasiyokuwa ya moja kwa moja, na kila serikali kuu ilipolegalega, Waberiberi hawa walivamia *Bilad al-Makhzan* na kuiweka hata kama ni kwa kipindi kifupi, chini ya "nchi ya upinzani" (*bilad al-siba*). Ili kupambana na balaa zote hizi, sultani alitumia sana mfumo wa majeshi ya kukodiwa ya watumwa ambayo yaliwekwa mijini.

Sambamba na mmininiko wa Wanomadi, kulikuwa na mehango wa wahamiaji wa Kiandalusia ulioingiza sanaa na ufundi bora sana pamoja na mila za miji inikubwa. Mji wa Fez ukachukua nafasi ya mji wa Marrakesh uliokuwa unashuka hadhi, na kuwa Kituo kikubwa cha utamaduni. Mji huu ulijengwa kuzunguka Chuo Kikuu, al-Karawiyyn, na madrasa mengi ambamo chini ya malezi ya sultani madhehebu ya Miliki asilia yalishamiri. Kwa upande wao wakazi wa inashambani walivutiwa sana na udugu wa Kisufii (*Tarika*), wazawiya na mawalii wenyeji (marabout). Wamohadi walikwishaingiza itikadi ya Kisufii ya al-Ghazali (kafariki 1111) kwenye mafundisho yao, na utawala wa Wamarini ulishuhudia kuibuka kwa vikundi vingi vya Kisufii ambavyo kwa kiasi kikubwa vilikuwa ni vizalia vya Kadiriyya. Ilikuwa ni kwa njia hii maarufu ambapo Uislamu ulifika sehemu za ndani kabisa za Moroko.

Kuhusu tishio la upanuzi wa Ukristo, Abu Yusuf Ya'kub alilishughulikia mara nne, akishuka Hispania na kuwapiga Wakastile waliokuwa nchi kavu na baharini. Hii ilisaidia kudhibiti tishio la Ukristo kwa muda. Kampeni ya nne ilimalizika mwaka 1285 kwa kuweka mkataba ambao ulimtaka mfalme wa Kastile asiingilie masuala ya Kiislamu nchini Hispania. Vilevile alitakiwa arudishe miswada yote ya Kiarabu iliyokuwa imekamatwa awali.

Sultani Abu Ya'kub aliugawa muda wake kati ya kufanya kampeni dhidi ya maasi ya ndani, na kampeni dhidi ya Tilimsan na Mfalme wa Kastile ambaye alivunja mkataba wa mwaka 1285. Baada ya kuuawa kwake, kulikuwa na kipindi cha vurugu iliyoambatana na maasi ya mwanamfalme, aliyefaulu kudhibiti biashara ya kuvuka Sahara, na kukomesha upanuzi wa ufalme wa Hispania na wa Maghrib. Abu al-Hasan pkee ndiye aliyefaulu kukomesha maasi haya. Akikabiliwa na mashambulizi ya Kastile juu ya Granada, aliungana na Amiri wa Kinasri wa Granada na kukomboa Algesiras; na pia kuitishia Kastile ambayo iliamua kushirikiana na Aragon. Mbali na ushindi mkubwa wa majini lililoupata jeshi la majini la Wamarini likisaidiwa na baadhi ya meli za Wahafsi, vita vikali vya Rio Salada (1340) vilimalizika kwa kushindwa vibaya. Ndipo Sultani wa Moroko akaacha ndoto zake kuhusu Hispania na kuutelekeza ufalme wa Granada.

Wamarini, kama Wazayyani, walitumia udhaifu wa Wahafsi katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nne kupanua eneo lao. Abu al-Hasan alichukua nafasi hii kuitaka Tilimsan, mji mkuu wa Wazayyani baada ya kuuzingira mji huu kivita kwa muda mrefu, na baadaye Tunis (1347), na kuanzisha utawala wa Kimarini katika eneo lote la Maghrib. Hata hivyo, tendo la kuingilia masuala ya makabila ya Waarabu wa Ifrikiya, lilizua ghasia nchi nzima. Ghasia hizo ziliteketeza jeshi la Abu al-Hasan pale Kayrawan na kisha kumzingira katika mji wake mkuu, ambako aliweza kutoroka lakini akajikuta anakabiliwa na uasi wa mtoto wake mwenyewe, Abu 'Inan, ambaye aliudai ufalme. Ukuu wa Abu al-Hasan wakati wa ustawi wake, na mwisho wake wa kuhuzunisha milimani ulikuwa kama marudio ya onyesho la filamu kuhusu historia ya nasaba za kifalme za wa Maghrib: Mkusanyiko wa polepole wa majeshi, kuvuka na kuingia kwenye kipindi cha mafanikio, na maangamizi ya ghafla. Na siku zote zilikuwa ni sababu zile zile: Kusambaa kwa raslimali ndogo katika eneo kubwa mno, kushindwa kuzingatia tafouti za kienyeji, na hali mbaya ya fedha.

Wakati Abu 'Inan mwenye tamaa ya ukuu alipomrithi baba yake, alijipa cheo cha ukhalifa na kuitaka tena miji ya Tilimsan na Tunis. Hata hivyo, kipigo toka kwa Waarabu kilimfanya aikimbie miji hiyo na baadaye akauawa na


mmoja wa mawaziri wake.

Kutoka wakati huo, machafuko na uozo ukatawala. Mawaziri, na hasa ukoo wa Wazenata wa Wabanu Wattas baada ya mwaka 1420, ukashikilia madaraka imara na kuwaingiza na kuwatoa watawala hadi mwaka 1472, wakati Muhamamad al-Shaykh alipotangazwa kuwa sultani, baada ya mapambano makali dhidi ya masharifu waliojijhusisha na madhehebu ya watakatifu na baraka za waswalihina. Masultani wa kwanza wa Kiwattasi walifanikiwa katika kudhibiti vuguvugu la masharifu. Hata hivyo, hawakufanikiwa kudhibiti kupanuka kwa Wareno katika mwambao wa Atlantiki. Punde wakabaniwa kwenye eneo la Fez, na sehemu ya kusini ya nchi kuwa nje ya mamlaka yao. Kutoka hapa jeshi la umma lililokusanywa na familia ya masharifu likaandama jihadi dhidi ya Wareno, na kuupigia mbiu ya kifo ufalme wa Kiwattasi.

Wa-Zayyani (Wa-Abd Al-Wadid)

Yaghmurasan Ibn Zayyan, gavana wa Kinohadi wa Tilimsan, ambaye alitoka kwenye tawi dogo la ukoo wa Wazenata, aliuasi utawala wa sultani na kuanzisha ufalme wake. Ufalme huo ulidumu kwa karne tatu, licha ya shinikizo kutoka kwa majirani wa magharibi au mashariki na mashambulizi ya Waarabu kutoka upande wa kusini. Mafanikio haya yalitokana na siasa niwanana za watawala wengi ambao kwa kawaida walikuwa kwenye hali ya kujihami. Kadhalika mafanikio yao yalitokana na kuweza mara nyingi kwenda na kufanya mashambulizi dhidi ya Fez huko magharibi na bonde la Shelif huko mashariki. Chini ya utawala wao, kazi ya kuwarithisha Uarabu Waberiberi wa Zenata iliendelea kwa nguvu sana, kiasi cha kuifanya Algeria ya magharibi ipoteze tabia yake ya awali ya Kiberiberi.

Ufalme wa Wazayyani uliandamamwa na ghasia na vita visivyokwisha vya ndani kwa ndani. Hali hii ilitokana na misingi tepetevu ya uchumi wa ufalme uliojengwa katika sehemu ya Tell yenye rutuba haba, uchache wa wakazi wastakimu, na wingi wa wanomadi wanaosumbuliwa na Waarabu. Pamoja na hayo, dola hili lilidumu hadi liliposhindwa na himaya ya Ottoman katikati ya karne ya kumi na sita. Raslimali kubwa ya dola hili ilikuwa mji wake mkuu wa Tilimsan ambao ulichukua mahali pa Táhart kama kituo kikubwa cha biashara cha Maghrib ya kati. Mji huu ulijengwa mahali ambapo njia ya mashariki magharibi iliyokuwa inaunganisha Fez na Ifrikiya inakatiza njia ya kaskazini kusini ambayo ilianzia Ulaya hadi Sudan kupitia Oran na Oasisi za Sahara. Mji huu pia uliunganishwa moja kwa moja na mji wa Sijilmasa ambao ulitekwa



4.2 *Msikiti wa Karawiyyin huko Fez: ulikarabatiwa wakati wa enzi ya WaAlmohavidi; katika baraza ni mlango mkuu wa chumba cha kusalia (J.L. Arbey)*

mwaka 1264. Miaka kumi kuanzia hapo, na kwa mara ya kwanza, mji wa Tilimsan uliziweka njia hizi kuu mbili za biashara ya kuvuka Sahara chini ya utawala mmoja. Falme mbili zilizopingana za Wamarini na Wazayyani pamoja na Wahafsi zilipigana mara kwa mara kudhibiti biashara hii. Kati ya mwaka 1299 na 1307, Abu Yusuf Ya'kub aliuzingira kijeshi mji wa Tilimsan na kujenga mji mpya ulioitwa *Tilimsan al-Jadid* (Tilimsan mpya) kando yake. Mji huu mara tu ukanyakua biashara karibu zote hadi ulipoharibiwa baada ya mji wa Tilimsan kuachiwa huru.

Methali ya zamani na maarufu itumikayo Tilimsan yasema: "Dawa bora ya umasikini ni Sudan". Hivyo ufalme, kwa ufundi kabisa ulivitumia vizuri vipindi vya udhaifu wa jirani zake wenye nguvu. Kwa upande mwingine, wakati Marini Abu al-Hasan alipoupiga mji wa Tilimsan mwaka 1337, alizikamata njia za biashara za kutokea na kuvuka Sahara. Utajiri ukarudi katika nusu ya mwisho ya karne ya kumi na tano, wakati wa utawala wa Abu Hammu Musa II (1359-89), mtawala mwenye uwezo. Hata hivyo kulikuwa na matatizo yaliyotokana na vipindi viwili vya kutawaliwa na Wamarini na machafuko ya Waarabu Wanomadi. Ni katika matukio haya ya mwisho ambapo mwanahistoria maarufu Ibn Khaldun aliingilia kati kwa niaba ya Abu Hammu; kitu ambacho kilimfunua macho kuhusu chemchemi za siasa za vurugu za Maghrib. Alitoa ushahidi kuhusu utamaduni wa Wazayyani kwa kusema: "Hapa [katika Tilimsan] sayansi na sanaa vimekua kwa mafanikio. Hapa palizaliwa wanazuoni na watu maarufu ambao mafanikio yao yalipenya hadi kwenye nchi nyingine." Kumbukumbu nyingi za kuchonga bado zipo kuonyesha ushahidi wa mafanikio haya. Lakini wakati Abu Tashfin alipomnyang'anya ufalme baba yake aliyetitwa Abu Hammu mwaka 1389 ikawa ndiyo mwanzo wa kipindi kirefu cha kuporomoka. Mji wa Tilimsan ukawa kwa vipindi vipindi kibaraka wa Tunis au Fez, na baada ya karne ya kumi na tano ukawa chini ya Aragon hadi kuingia kwa himaya ya Ottoman iliyokomesha ufalme wa Zayyani mwaka 1554.

Changamoto ya Ulaya ya Kikristo

Kama Maghrib ilikuwa imegawanyika, basi mahasimu wake wa Kikristo wa upande wa kaskazini waligawanyika zaidi. Falme za Kastile na Aragon, miji ya Italia ya Pisa, Genoa na Venisi, Sisilia na Ureno iliendesha siasa za mashindano. Baada ya masaibu ya St. Louis, Ufaransa ikajitoa kwenye mashindano na kuanza kuangalia mambo yake yenyewe. Kila njia ya kidiplomasia na ya kibiashara ilijaribiwa. Hali hii ilionyesha kuwa mapambano havakuwa ya kidini tu kati ya makundi mawili ya kiitikadi. Kwa hakika masuala

ya kiuchumi ndiyo yalisababisha kuundwa kwa kundi la mshikamano kati ya Waislamu na Wakristo dhidi ya kundi lingine la mshikamano wa Waislamu na Wakristo.

Hata hivyo, kipindi cha katikati cha karne ya kumi na tatu kilishuhudia mageuzi thabiti, wakati karibu miji yote katika peninsula ya Iberia na visiwa vya Baleariki ilipoingia chini ya utawala wa Kikristo. Uamiri mdogo wa Granada uliachwa huru kwa muda hadi mwaka 1492. Mizania ya nguvu za utawala ilihamia Mediterania ya Magharibi. Hii ni wakati ambao kwa hakika Maghrib ililazimishwa kujihami.

Mambo ya ndani ya nchi yalichangia sana hali iliyokuwepo, na hasa msukumo wa kudumu wa nguvu za utengano katika madola ya Kiislamu uliowakilishwa na wana wa wafalme wapinzani, viongozi wa makabila ya Kinomadi, majeshi ya kukodiwa ya Kikristo, na viongozi wa kidini (mashehe au masharifu). Vikundi vyote hivi vilijali sana maslahi yao. Pamoja na makundi haya, kulikuwa na uhasama kati ya maeneo ya mashambani kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine miji ambayo ilijizatiti kwenye biashara na kutafuta pesa, bila kujali maslahi ya taifa au dini. Vilevile kulikuwa na uadui kati ya Wanomadi na jamii zilizostakimu, n.k.

Zaidi ya hayo kulikuwa na upunguaji wa kiwango cha ongezeko la watu, uliozidishwa zaidi na "Kifo Cheusi" katikati ya karne ya kumi na nne; hali ambayo ilirekebika kidogo kutokana na kuingia kwa kundi kubwa la wakimbizi Waislamu wa Kiandalusia pamoja na kuondoka kwa wakazi wa vijijini kutokana na kubanwa na utawala wa kimwinyi na kuharibika kwa udongo kulikosababishwa na kutumiwa na makundi ya Wanomadi. Orodha ya matukio inaonyesha kuwa kulikuwa na mambo mengi mabaya ndani ya nchi.

Kwa upande wa nje ya nchi, ni vema kuelewa kwamba, biashara ya kuvuka Sahara ambayo kwa karne nyingi ilichochea ustawi wa kiuchumi, kuanzia miaka ya 1350 na kuendelea ilielekezwa Misri, hivyo kugeuza mkondo wa faida nyingi za kiuchumi na kifedha (kama vile ushuru wa forodha) za biashara hii.

Lakini wakati huo huo, dola za Kikristo zilikuwa zinaimarisha nguvu zao. Hata utawala wa Wahafsi uliokuwa mbali sana nao, haukuepuka kuingiliwa na kuvamiwa na vituo vyake vya majini kutekwa na Aragon, Sisilia, Genoa na Venisi. Mji wa Jarba ulibaki mikononi mwa Wakristo hadi mwaka 1335, na katika kipindi chote cha karne ya kumi na tano, bandari nyingi kati ya Tripoli na Algiers zilikuwa maeneo ya kushambuliwa, na hivyo kuzorotesha uhusiano kati ya Wahafsi na madola ya Kikristo.

Hali katika Maghrib ya kati na ya magharibi ilikuwa tatanishi zaidi. Wakati

Aragon, ilidumisha uhusiano mzuri na Moroko kama mbinu ya kulinda himaya yake hadi katikati ya karne ya kumi na tano, Kastile, pamoja na Ureno, ziliendeleza vita vya kidini na hamu ya kutokomeza vitendo vya uharamia wa baharini.

Uharamia katika Mediterania umekuwepo tangu zama ya zama, lakini utekaji tena wa Hispania uliofanywa na Wakristo uliipatia nchi hiyo mwelekeo wa kidini. Maharamia wa Kiislamu, hasa wale waliofukuzwa kutoka Andalusia, walichukulia tendo lao la kulipiza kisasi kama namna fulani ya jihadi. Walianzisha mashambulizi kutoka kwenye vituo vya wanamaji walivyoviita "Jamhuri", vilivyokuwa nje ya udhibiti wa utawala. Zaidi ya hayo, Wamarini kama Wawattasi na Wahafsi, walikuwa na msimamo wa kutatanisha dhidi ya maharamia, walijipongeza kwa ujasiri wao dhidi ya changamoto la Kikristo japo walikuwa dhaifu kukabiliiana nalo, na wakati huohuo wakiwa makini kutochokoza mashambulizi kutoka kwa maharamia au madola ya Kikristo.

Maharamia wa Kiislamu, kama walivyokuwa masharifu na mawalii wa Moroko, katika karne ya kumi na tano na kumi na sita, ambao walichochea chuki dhidi ya Wareno, walikana suluhu na Wakristo. Lakini kabla ya muungano wa Kastile na Aragon (1479) haikuwezekana Ulaya kufanya kitendo cha pamoja dhidi ya Maghrib. Kitendo cha kuiua Granada (1492) ndicho tu kilichodhihirisha kuwa muungano huo unawezekana. Ureno, kwa upande wa pili, ikishawishiwa na hisia zake za kidini, kisiasa au kiuchumi, iliendelea kufanya mashambulio.

Mnamo mwaka 1415 kutekwa kwa Sabta kulikofanywa na watoto wawili wa mfalme, ambao mmoja wao baadaye ndiye aliyekuja tambuliwa kama Mwanabaharia Henry, kulikuwa ndio mwanzo upanuzi wa Wakoloni wa Ureno na hata wa Ulaya. Huu ulikuwa ni utangulizi katika sura mpya ya historia ya dunia, licha ya vita vya kidini vilivyotangulia, ambavyo kwa hakika vilikuwa ni mashambulizi ya hapa na pale kuzunguka Mediterania tu. Kuanzia wakati huu, Bahari ya Atlantiki ikaingizwa ulingoni pamoja na mabara yote.

Wareno walishindwa kwa mara nyingine tena katika vita vya Tangiers mwaka 1437, na Mfalme Duarte wa Ureno alipendelea kumwacha kaka yake Fernando, ambaye alikamatwa mateka, afie huko Fez kuliko kuirudisha Sabta kwa Moroko. Ureno ilihitimisha kuwa haingeweza kuipiga Moroko ili iweze kufika kwenye dhahabu za Sudan kwa njia ya kuvuka Sahara kwa mashambulizi ya uso kwa uso. Hii inaelezea kwa mini kulikuwa na mpango wa kuizunguka Moroko kwa kupitia Atlantiki. Tangu katikati ya karne ya kumi na tano na kuendelea, miji mingi ya pwani ilitawaliwa na Wareno: 'Anfa, Arsila, Massat na Agadir, na hatimaye mji wa Tangiers nao ukaangukia mikononi

mwao mwaka 1471.

Pwani ya Afrika ya Magharibi ilikuwa tayari imekwisha pelezwa. Licha ya ngawira iliyopatikana kutokana na mashambulizi ya pwani na miji ya Moroko, Wareno walianzisha biashara ya mzunguko ya kununua bidhaa za nguo za sufu, nafaka na farasi nchini Moroko na kuzipeleka Afrika ya Weusi kubadilishana na watumwa pamoja na dhahabu.

Wakati Ureno iliyokuwa inamtafuta “Presta Yohana,” wa visakale, ilikuwa inatafuta njia ya kuiteka dunia ya Waislamu kwa kuivizia, ndoa ya Ferdinand wa Aragon na Isabella wa Kastile ya mwaka 1469 ilifuatiwa na kuanguka kwa Granada mwaka 1492, na safari ya kwanza ya Kristofa Kolumba kuvuka Atlantiki, katika mwaka huo huo.

Mnamo mwaka 1494, Papa aliidhinisha mkataba wa kuigawa Maghrib kati ya falme mbili za Iberia. Wahispania walipata bandari nyingi schemu za kati na mashariki ya Maghrib (Melilla, Oran, Bijaya, Tripoli) bila kuingia bara.

Mwisho wa karne ya kumi na tano ulishuhudia kutokomea kwa utawala wa Kiislamu katika Maghrib. Utawala huu uligawanyika, na kuhujumiwa na migogoro ya ndani kwa ndani na kunyonywa nguvukazi yake kiuchumi na katika idadi ya watu, wakati ambapo mazingira mazuri ya mshikamano wa kisiasa na kupanuka kiuchumi, yalikuwa yanaisaidia Ulaya.

Karne ya kumi na sita ilishuhudia kuibuka upya kwa Maghrib. Upande wa magharibi kulikuwa na vyama vya umma na upande wa mashariki kulikuwa na mashambulio ya maharamia wa Kituruki, na baadaye himaya ya Ottoman. Lakini kipindi cha utawala wa Kiislamu kilichoanzishwa na Wamoravi, Wamohadi na watawala wa mwanzo wa Kihafsi na Kimarini kilikuwa kimekwisha kabisa.



5

Jamii katika Maghrib baada ya kuondoka Wa-Mohadi

Kushadidi kwa Unomadi: Maisha mijini

Wanomadi

Baada ya karne ya kumi na moja mlingano kati ya Wanomadi na watu waliostakimu ulivurugwa kwa manufaa ya Wanomadi kutokana na kuwasili kwa Wa-Banú Hilál, ambao walifuatiwa na Wa-Banú Sulaym katika karne ya kumi na mbili. Kwa sababu za kimkakati, Wamohadi waliwaachia Wanomadi mbuga za Atlantiki, ambapo Wa-Banú Ma'kil walikaa sehemu za kusini na Mashariki ya safu ya milima ya Atlas upande wa Moroko. Kwa hiyo, upande wa Magharibi wa Maghrib ulitengwa na Mashariki na kurudishwa nyuma kuelekea pwani ya Mcditerania.

Watu wa vijijini

Wakulima walikuwa ndio wengi zaidi kati ya watu walioishi kwa kutegemeana na watu wa mjini. Unyarubanja haukuwepo, mashamba madogo ya kifamilia ndiyo yaliyotawala katika muktadha wa ubia au ushirika, ijapokuwa kulikuwepo na mashamba makubwa. Maeneo mengi yalikuwa yamewekwa wakfu na waliogawiwa waliyalima kwa utaratibu wa kupanga. Aina mbalimbali za mikataba ziliwafunga wenye kumiliki maeneo hayo kwa wakulima, kwa mfano kugawana mavuno kwa kutoa kodi ya moja ya tano ya mazao. Lakini wakodi mashamba (*khammas*) mara nyingi walikuwa wenye hali mbaya. Masoko ya vijijini mara kwa mara yalikuwa na kuwa miji ya masoko; vituo vya kukutania kati ya wakulima na Wanomadi.

Maeneo ya mbali ya watu wazungumzao Kiberiberi ndiko ambako aina mbalimbali za mifumo ya kale ya maisha ilidumu kwa muda mrefu.

Watu wa mijini

Kwa jumla, jamii ya Kiarabu ya Kiislamu katika Maghrib ilikuwa na sifa za familia inayoongozwa na wanaume, utengano wa kijinsia, utengano kati ya watu huru na watumwa, na kati ya Waislamu na watu wengine.

Mpango wa kiasili wa mji ulijumuisha msikiti mkuu katikati ya mitaa ya kandokando (*souk*), na hamamu (mabafu ya maji moto), na boma lenye milango mikubwa iliyoelekea nje ya mji na makaburini. Maeneo yaliyokuwa kandokando ya bandari (*funduk*) yalikalikiwa na wafanyabiashara wa Ulaya na maharamia wa baharini waliorudi na watumwa.

Wayahudi walitoa mchango mkubwa sana, kutokana na mtaji wao, stadi zao, na uhusiano wao na Ulaya. Idadi yao iliongezeka kutokana na kuingia kwa wakimbizi waliokimbia kuuawa. Kwa jumla walipokelewa vizuri nchini Moroko na mara nyingi walipata vyeo vya juu, lakini hawakuweza kuepuka chuki na mauaji yaliyofanywa dhidi yao na wenyeji, hasa mwanzoni na mwishoni mwa nasaba ya ufalme wa Ki-Marini na pia katika oasisi ya Tuat mwishoni mwa karne ya kumi na tano.

Lakini, kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na tatu hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tano, mchango muhimu zaidi ulitolewa na Waislamu wa Kihispania. Watu hawa (Wa-Andalusia) walikaa katika makundi makundi, na waliweza kuonekana kuanzia ngazi za juu katika mfumo wa kijamii, mpaka chini. Walikuwepo masahibu wa Sultani, watunza bustani na mafundi waashi, pamoja na waandishi, wanamuziki, makatibu, wafanyabiashara na wanajeshi.

Tabia ya kuwafanya masuria wanawake weusi ambao walikuwa wengi miongoni mwa watumwa, ilisababisha kuchanganyika sana kwa makabila. Hata hivyo, kiwango kikubwa cha kuingiliana kati ya Waarabu na Waberiberi katika miji hakikuvunja "ukabila".

Ushindi wa Umaliki: Mwelekeo wa Kisufi

Chini ya utawala wa Wa-Marini na Wa-bd-al-adidi, itikadi ya dini ya Umohadi ya utawala uliopita, ilibadilishwa na Umaliki asilia ambao ulikuwa haujapotea na ambao ulikuja fufuka upya kwa msaada wa Waandalusia kupitia katika madrasa mengi. Kwa upande wa Wahafsi, ambao kwa muda mrefu walikuwa Wamohadi, walijaribu bila mafanikio kushikilia itikadi ya nasaba ya kifalme miongoni mwa Waifrikiya, walioendelea kushikilia itikadi ya Umaliki ambayo madaktari mashuhuri waliifufua upya katika nusu ya pili ya karne ya kumi na moja kwa njia ya madrasa, mahakama na asasi za dini. Wahafsi walikubali

kushiriki (katika kueneza Umaliki), na kwa msaada wa Ibn 'Arafa mashuhuri, Umaliki ulishinda katika karne ya kumi na nne.

Pamoja na Umaliki asilia, ambao mtazamo wake finyu wa kushikilia sheria, wakati wa utawala wa Wamohadi ulisababisha kupigwa marufuku kwa kazi za al-Ghazali, watu wa Moroko, ambao walikuwa wanatafuta imani yenye mvuto zaidi, walijiunga na Usufii wa Kiandalusia ambao uliamsha tena maisha ya utawa na kujinyima anasa. Viongozi wengi wa Kisufii wakawa Mawalii maarufu. Abú Madyan al-Andalusi, Mwiberia alivuka Moroko na kwenda kusharabu ndani ya chemchemi ya elimu ya Usufii ya mashariki. Baadaye aliishi Bijayā na kufia Tilimsan mwaka 1198, akiacha wafuasi, ikiwa ni pamoja na al-Dahmani na al-Mahdāwi. Al-Shādili aliyezaliwa karibu na Tetuan, alianza mahubiri yake katika eneo alikochepekua la Tunisia la Jabel Zaghouān. Alidai kuwa yeye ni Sharifu na alifia sehemu za mashariki, akiwa ameacha wafuasi wengi walioshiba Usufii wenye hamasa lakini ulio rahisi. Ushādili ulikuwa hasa wa madhehebu ya Mawalii (Umarabuti, baraka na maombi makali ya miujiza) na ulihusishwa na vikundi vya udugu na Uzawiya. Miongoni mwao, mwanamke aliyeitwa Lāllā Mānubiyya (karne ya kumi na tatu), alipata umaarufu sana kutokana na tabia yake ya kupagawa wazimu, na uwezo wake wa kuwafanya watu wa Ifrikiya wamwogope na kumheshimu sana. Kwa upande wa Wa-Al-Murjani, tabia hizi zilizoenea miongoni mwa umma zilikubalika hata miongoni mwa wanateolojia katika Jumba la Mfalme.

Kisha akaja Mwi-Ifrikiya, Sidi Ben "Arus" (kafariki 1463), Mmarabuti wa Kisufii mtembezi asiye na simile ambaye hatimaye aliweza kumshawishi kila mtu na akafa na heshima ya uwali. Katika karne ya kumi na sita, wafuasi wake waliunda udugu wa Waarusiyya.

Hata hivyo, nchini Moroko ambako muasisi wa Ushadili alitokea, ndiko maarifa mengi ya ki-Shadili yalikozaishwa, hasa katika Aghmat na Marrakesh miongoni mwa *Wāzawiya* wa Ragra. Mwishowe, mnamo karne ya kumi na tano, Al-Jazuli, Mberiberi kutoka kusini ambaye alikuwa wa ukoo wa Mtume kwa mujibu wa visakale aliunganisha pamoja Usufii, madhehebu ya marabuti na madhehebu ya Masharifu. Wakati huo Masharifu wa Kiidrisi waliunda makundi yenye nguvu yaliyoruhusiwa na Wamarini. Al-Jazuli mfuasi wa Shadili, alifundisha Wamarabuti wengi ambao baadaye walisambaa kwa makundi sehemu za kaskazini na mashariki hadi Tripolitania. Baada ya kifo chake, kulikuwa na matukio ya fujo kwenye jeneza lake ambalo kwa miaka mingi lilikuwa linazungushwa huko na huko kabla ya kuhamishwa na al-A'raj, Sharifu wa Ki-Sadi, mwaka 1524 kwenda kwenye kaburi lile lile alilozikiwa baba yake. Jambo hili liliimarisha muungano kati ya nasaba mpya ya ufalme mpya na itikadi ya Ujazuli na kuihakikishia ushindi wake.

Ilikuwa tena nchini Moroko ambapo Maulidi, yaani karamu ya kuzaliwa kwa Mtume, ambayo yalikuwa tayari yakiadhimishwa huko mashariki tangu mwanzoni mwa kame ya kumi na tatu yalipoenea miongoni mwa Waberiberi. Karamu hii ilirasimishwa na Abu Ya'kub mnamo mwaka 1292. Baada ya kipindi cha kukinzwa na wanasharia wa Tunisia, Ifrikiya ikiwa chini ya uongozi wa Abu Faris (1394- 1434) ilikubali kusherehekea Maulidi kwa mapambo, kughani mashairi na kasida. Kila mahali masharifu na makundi ya udugu yalikusika kwenye kuandaa shughuli hizi, yakaziendesha na kupata fahari kubwa kwa kufanya hivyo.

Nguvu za nasaba za kifalme na muundo wa kijamii

Kimadharia, jumuiya ya Maghrib iliundwa na makundi makuu mawili. Watamalaki wa Kiberiberi (Wamarini, Wa-Abd al-Wadidi, Wahafsi) ambao walihusishwa na dola (*makhzan*), na wengine wote waliobaki; au *Wakhassa* (mamwinyi, wasomi, na wanaojua kusoma) na *waamma* (watu wa kawaida, umma, wasiojua kusoma). Lakini mgawanyo huu wa pili haukuwa sawa na ule wa kwanza. Aidha watu wa tabaka la kati walivuruga mgawanyo huu: tabaka la vibwanyenye waliojaribu kupanda ngazi za kijamii kwa njia ya bahati tu, au elimu au uchaji Mungu, huku wakijiegemeza kwa watu wakubwa.

Wamarini

Wapanda farasi wa Kimarini na mamwinyi wa Zenāta, waliotoa mawaziri na viongozi wa vita, waliungwa mkono na watu mbalimbali wa Kiturko, Kifranki, Kiandalusia na askari wa kukodiwa walioasi. Familia mashuhuri ya Banu Wattas ikajitokeza mwishoni mwa nasaba ya Ufalme wa Marini. Ofisi ya Mkuu wa Jumba la Mfalme ilikabidhiwa Makatibu (Katib). Wahajib walikuwa watunzaji wa jengo. Hawa walikuwa watumwa walioachwa huru bila mamlaka yoyote isipokuwa kwa Myahudi mmoja ambaye alikuwa mkuu wa Serikali chini ya utawala wa Abu Yakub Yusuf. Wapambe wengi na wakuu wa itifaki walisimamia kaida zinazotakiwa katika ukumbi wa Baraza wa Jumba la Umma (*dar al-umma*).

Mrithi Mtarajiwa alikuwa anahusishwa kwa karibu zaidi na utawala. Magavana maarufu wa mikoa waliteuliwa kutoka kwenye familia ya kifalme na jamii ya Wazanata au Waarabu. Eneo la Atlas takriban lilikuwa huru; makabila ya Kiarabu yaliruhusiwa kutoza kodi (*ikta*), kodi ambayo makundi ya kidini ya Udugu yalisamehewa kulipa; wakati Masharifu na wacha Mungu walimegewa sehemu ya kodi hii. Wamarini waliondoka Marrakesh, mji mkuu wa Wamoravi,

wakaenda Fez, mji ambao katika karne ya kumi na nne ulikuwa umekwishafikia kilele cha maendeleo. Mji huu ulikuwa na maeneo maalumu ya makazi ya mfalme, makazi ya Wakristo, na makazi ya Wayahudi, yaani *Mallah*. Hata hivyo; wengi wa Wamarini hawakupendelea kuishi mjini humo, bali walipendelea kwenda kufanya biashara. Katika karne ya kumi na nne, Abu Yusuf Ya'kub alianzisha *Madrasa* maarufu ya Wamarini katika mji wa zamani kwa msaada wa mali wakfu ya *Habou*.

Kulikuwa na biashara kubwa kati yao na Ureno, Hispania, Genoa na Venisi. Wafanyabiashara Wakristo na Wayahudi walikuwa na miundo yao huru na walikuwa wanadhibitiwa na *muhtasib*; sawa sawa na *kadhi* kwa shughuli za biashara. Baada ya kuanguka kwa nasaba ya ufalme, Fez ikarudi nyuma na mji wa Marrakesh, ambao uliteuliwa kuwa mji mkuu na Wasa'di, ukahuishwa tena.

Wa-'Abd al-Wadid

Mwanzilishi, Yaghmurāsān (1235-83), Mnomadi wa Zenāta ambaye aliishi Tilimsan, alikuwa bado anaishi kwenye hema akiwa na miaka 30 na alikuwa anazungumza Kiberiberi tu. Hapo awali, uwaziri ulikuwa unapewa ndugu za wafalme, lakini baadaye ulitolewa kwa familia ya Kiiberia ya wabadilishaji pesa. Myahudi akawa Waziri wa Fedha. Mhasibu Mkuu alichaguliwa kutoka miongoni mwa wanasharia, ambapo Abu Tashfin (1318-1337) alimteua mtumwa huru Mwaandalusia kuwa Mkuu wa Jengo la Mfalme. Wakurdi pamoja na wanajeshi wa kukodiwa wa Kikristo walitumiwa katika jeshi lakini Wabanu Hilal ambao walipewa unafuu muhimu wa kifedha waliunda sehemu kubwa ya jeshi. Yangmurasan alijenga minara juu ya misikiti mikuu ya Tilimsan na Agadir, na ngome ya mfalme. Wafalme waliomfuatia walijenga madrasa. Wakati huo mji wa Tilimsan ulikuwa umefikia kilele cha ustawi. Hivyo, chini ya uongozi wa Abu Hammu II (1359-89), ambaye aliweka misingi ya kidini, na kujenga kaburi zuri la familia na madrasa, sherehe za usiku za Maulidi zilifana sana; na saa kubwa yenye maumbo yanayozunguka ilivutia watu sana.

Wakati, Wamarini walipotwaa Tilimsan mara mbili mnamo karne ya kumi na nne, waliongeza majengo yao pia. Kwa mfano, waliongeza msikiti na madrasa kwenye kaburi la Abu Madyan na kulinakishi. Kwa ufupi, mbali na magomvi ya kisiasa, Tilimsan ilifurahia mafanikio ya mfululizo. Bidhaa zilizotokana na biashara ya nje iliyoshamiri zilipangwa kando kando ya Msikiti Mkuu. Wasanii wa kazi za mikono walitengeneza nguo za sufu, mazulia, vyombo vya udongo, lijamu na vigwe vya kuongozea farasi na kusheheneza vyombo vya baharini ambavyo mara nyingi vilisafiri kupitia Oran. Dhahabu na

watumwa kutoka Sudan walikuja kupitia Sijilmasa hadi Tilimsan, mji unaoonekana kuwa ulishikilia biashara karibu zote za kuvuka Sahara badala ya Marrakesh. Nao mji wa Bijaya, ukiwa pamoja na bandari yake ya biashara, kituo chake cha maharamia wa baharini na kiwanda cha kutengenezea meli ulikuwa hasa kituo cha taaluma na dini cha Wakabye na Waandalusia kikishindana na Tilimsan. Mji wa Konstantini ulikuwa na harakati nyingi pia, na ulikuwa na tabaka kongwe la mabwanyenye tajiri ambalo lilishirikisha Wayahudi wengi.


Wahafsi

Wahafsi waliendeleza utawala wa Wamohadi kwa kupitia maamiri wake. Maamiri walikuwa magavana wa majimbo ambapo watoto wao pamoja na wale wa Sultani walifanya kazi kama wahudumu (*sibyan*) katika Jumba la Mfalme. Askari wa kukodiwa ambao hapo awali walikuwa watumwa na waasi, walikuwa na majukumu makubwa jeshini na katika ngazi za juu za uongozi. Mashehe walitawala makabila mbalimbali ya asili ya Wamohadi. Katika kujenga usawa, Mashehe walilipwa mishahara sawa na ule wa sultani. Lakini umaarufu wao ulipungua na kuchukuliwa na watu huru na Waandalusia waliokuwa wajumbe wa Baraza (*shura*) pamoja na makhalifa ambao walisimamia ukomeshaji wa ukatili.

Chini ya uongozi wa Abu Zakariyya (1228-49), kulikuwa na mawaziri watatu: mmoja wa jeshi, ambaye alikuwa pia Waziri Mkuu, mwingine wa fedha, na wa mwisho kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Mahakama. Mwishoni mwa karne ya kumi na tatu kulianzishwa ofisi ya Mkuu wa Jengo la Mfalme (*Hajib*), ambaye katika karne ya kumi na nne alikuja kuwa ndiye Waziri Mkuu. Mwangalizi wa Jumba la Kifalme mwishowe akawa mhibiti wa fedha za Umma, ambapo *mazwār* (mtumishi mkuu na mkuu wa walinzi wa jumba la mfalme) akawa wa pili katika wadhifa akishikilia utawala wa jeshi. Makatibu ambao awali walikuwa Waandalusia polepole walikuwa wakitwaliwa mahali pao na Waifrikiya.

Mashehe wa Kimohadi ambao walikuwa magavana wa majimbo walitoa nafasi zao kwa watumwa huru na ndugu wa karibu wa sultani. Mashehe wa "kikabila" walitawala makabila yao na walipatiwa unafuu wa kifedha.

Jeshi lilikuwa la mchanganyiko wa makabila, na liliundwa na Wa-mohadi, Waarabu wa Kinomadi, Waberiberi wa Kiifrikiya, Waasia, Waandalusia, Wafranki, n.k. na majemadari wake mara nyingi walikuwa watumwa huru, au askari watoro. Maharamia wa baharini walitumwa na watawala au wafanyabiashara. Mijini, jeshi la mgambo la Kiandalusia liliishi karibu na jeshi



5.1 Msikiti wa Kasaba huko Tunis. (B. Nantet)

la mgambo la askari wa farasi wa Kikristo ambao walifanya kazi kama walenzi wa Sultani, na wanajeshi wa kukodiwa wa Kituruki.

Wahafsi waliuacha mji mkuu wa zamani, Kayrawan, ambao ulitelekezwa na Wabanu Hilal, na kujiingiza katika shughuli za kibaharia.

Tunis lilikuwa jiji linalostawi. Abu Zakariyya alibadili *kasaba* Wamohadi kuwa makao ya serikali. Kisha mnamo mwaka 1240, karibu na Msikiti Mkuu wa Zāytuna, akajenga madrasa kongwe kabisa katika Afrika ya Kaskazini. Kulikuwa na wingi wa *zawiya*, *funduku*, bustani na viunga vya matunda yaliyotunzwa na Waandalusia. Kulikuwa pia na bustani za burudani, majumba ya wana wa mfalme pamoja na jengo la mfalme la Bardo (1420).

Ilikuwa mjini Tunis ambapo Ibn Khaldun (1332-1406) aliyekuwa mtu mashuhuri kabisa wa wakati huo, alizaliwa. Asili ya familia ya Khaldun ni Yemeni na waliishi Hispania. Waliondoka Hispania baada ya Ukristo kushinda tena. Mababu wa Ibn Khaldun walikuwa wanasiasa wakitumikia Wahafsi. Yeye pia alijiunga na kazi zao, lakini akakimbia kabla ya uvamizi wa Ifrikiya uliofanywa na Amir wa Konstatini. Ibn Khaldun akaajiriwa na Mmarini Abu 'Inān huko Fez. Huko alijihusisha na uhaini akafungwa miaka miwili jela. Njama za kisiri siri na mabadiliko ya kisiasa yalifululiza sana huko Granada, Seville, Bijayā, Konstantini, Tunis na Tilimsan. Wakati fulani Ibn Khaldun

alikuwa akiajiri askari wa kukodiwa kwa ajili ya Wamarini wa Fez. Baadaye alikwenda mafichoni karibu na Tiaret kwa miaka minne kutunga kitabu chake maarufu kilichoitwa *Mukaddima*.

Ilikuwa mjini Tunis, mwaka 1378, ambapo alikamilisha kitabu chake kiitwacho "Historia ya Ulimwengu." Alipogundua amewekewa njama za siri, alitoroka kwenda kuhiji Maka mwaka 1382. Baadaye alirudi na kuishi Kairo ambapo alikuwa mwalimu na Kadhi Mkuu wa Kimaliki. Huko Damasko, uliokuwa umezingirwa na Tamerlane, alipata fursa ya kukutana na mtiishaji huyo maarufu wa Mongolia kabla ya kifo chake.

Kutokana na uzoefu wake katika Maghrib, Ibn Khaldun aliibuka na fikra asilia ajabu. Aliunda falsafa ya kisayansi ya historia yenye kuzingatia kanuni za matukio yenye duru zinazolingiliana; makundi ya kinomadi yenye mwamko wa ujumii (*asabiyya*) yaliteka mbuga, miji na mamlaka. Lakini, baada ya kustakimu walisalimu kipaji chao hicho kwa makundi mengine ya kinomadi yaliyochukua nafasi yao. Kwa maoni yake Ibn Khaldun, Wa-Banu Hilāl, na baa la "Kifo Chcusi" viliumaliza utomvu wa uhai wa Maghrib inayokabiliana na Magharibi yenye idadi ya watu inayoongezeka.

Kwa mujibu wa nadharia yake, utawala hudumu kwa vizazi vinne tu. Katika kitabu chake *Historia ya Ulimwengu "Universal History"* alichunguza kwa undani makabila ya Waarabu na Waberiberi na tawala zao za kifalme. Ibn Khaldun ni mtu muhimu kwa sababu mbili: kwanza anatoa habari zenye ubora wa hali ya juu ambazo zinatokana na nafasi yake kama shahidi wa wakati wake. Lakini zaidi ya hayo, nadharia zake nzito zinazozingatia uhalisia razini wenye ushahidi thabiti, na hata wenye kuzingatia kanuni za ulazima wa matukio, ziliwezesha kufafanua kanuni za mabadiliko ya kihistoria ambazo zilisababisha aonekane kama mwanzilishi wa falsafa ya uyakunifu wa historia (*historial materialism*).



Mali na upanukaji wa pili wa Wamande

Leo hii, wazungumzaji wa Kimande (Wamandingo, Wamandenka, Wamanden) wanapatikana kuanzia Atlantiki hadi Air, pamoja na vikundi vikundi vya makazi hadi kufikia Ghuba ya Benin. Katika karne ya kumi na mbili makazi haya yalikuwa hayajapanuka kiasi hiki. Wakati huo makundi matatu makuu yaliweza kuainishwa, kutoka kaskazini hadi kusini: Wasoninke (au Wasarakolle), waanzilishi wa Ghana huko Wagadu, Bukhumi na Kaniaga, Wasoso, na Wamalinke katika bonde la juu la mto Niger. Wakati ambapo Wamohadi walikuwa wanashinda himaya ya Ghana, Wasoninke kadhaa, hasa Wamarka au Wawakore (Wawangara), labda kwa kutafuta dhahabu, walikuwa wakianzisha makazi mapya kusini zaidi. Mfano mmojawapo wa makazi hayo ni mji mkuu wa nchi ya Jenne. Machimbo kwenye eneo la Jenne-Jeno yameonyesha makazi ya kutokea karne ya tatu kabla ya enzi ya Ukristo. Kwa hivyo, maendeleo ya mji huo hayakusababishwa na biashara ya kupitia Sahara bali yalitokana na mahusiano baina ya wenyeji wafugaji, wavuvi, wakulima na wahunzi.

Ilipofika mwanzoni mwa enzi ya Ukristo mchele wa Kiafrika (*Oryza glaberrima*) ulikuwa ukipandwa kwenye tope lenye rutuba katika makutano ya Niger na Bani ambapo ndipo ulipokuwa mji wa Jenne-Jeno, katikati ya vijiji vingi vikubwa.

Kuwepo kwa vitu vya shaba mwanzoni mwa karne ya sita ya enzi ya Ukristo, bidhaa ambazo zingeweza kuwa zimekuja kutoka kwenye migodi ya Sahara huko Takedda, ni ushahidi wa hali ya kushamiri kwa biashara ya kupitia Sahara. Uhamishaji wa Jenne-Jeno kwenda kwenye eneo lake la sasa huko Jenne labda ulihusishwa na haja ya Waislamu na wafanyabiashara ya kujitoa kutoka kwenye wakazi wengi ambao bado walifuata dimi ya asili. Shaba ilipelekwa

pande za kusini na kubadilishwa kwa dhahabu, kola na pembe.

Ugunduzi wa shaba huko Jenne na Igbo-Ukusu kwenye *delta* ya Niger unaonyesha kuwa biashara iliyopitia Sahara haikuanza na Waarabu, bali muda mrefu kabla yao, ilianzishwa na Wawangara (au Wadiola) ambao walieneza kuelekea kusini, wakati mwingine kwa kutumia nguvu za kijeshi. Kuna nyaraka chache za kuhusu kipindi kati ya kuanguka kwa Kumbi Saleh, mji mkuu wa Ghana mnamo mwaka 1076, na kuanzishwa kwa Mali baada ya ushindi wa Sundiata dhidi ya Wasoso mnamo mwaka 1235. Kipindi hiki kiliashiria mwanzo wa upanukaji wa pili wa Wamande ambao ulihamisha koo za Wamalinke kutoka Niger ya juu na kuwapeleka pwani ya Atlantiki huko Senegambia. Zaidi ya hayo, wafanyabiashara na mawalii wa Kimandenka walielekea upande wa mashariki hadi nchi ya Hausa na upande wa kusini ambapo vituo vya biashara kama vile Begho vilianzishwa kuelekea kwenye maeneo yenye dhahabu nyingi kama vile nchi za Akan.

Kwanza tutawaelezea watu na falme za Sudani Magharibi mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili, halafu mwanzo wa maendeleo ya upanukaji wa Wamande; hatimaye sifa kuu za utamaduni waliouunda.

Falme na majimbo ya Sudan magharibi mnamo karne ya kumi na mbili

Kabla ya Kumbi Saleh kutekwa na Wamohadi mnamo mwaka 1076, al-Bakri anatoa taarifa muhimu kuhusu Sudan magharibi; taarifa hizi zinajazilizwa na al-Idrisi mnamo katikati ya karne ya kumi na mbili. Taarifa hizi za kimaandishi ziliongezeka tokea wakati huo na kama zile za *Ta'rikh* za karne ya kumi na saba, zilikuwa na msingi wa mapokeo simulizi. Kazi za kiakiolojia zilizofanyika huko Kumbi Saleh, Awdaghost na Nyani nazo pia zinathibitisha kile ambacho mapokeo simulizi yameelezea, na kutoa ushahidi ambao unafanya iwezekane kupata picha pana zaidi ya Sudan magharibi ya wakati huo.

Takrur

Mnamo katikati ya karne ya kumi na moja, Warjabi, mfalme wa Takrur ambaye alikwishasilimu, na mwanac Labi, walikuwa wamekwisha jitenga na Ghana. Hata walikwishachangia kuanguka kwa Ghana kwa kuungana na Wamohadi.

Waliudhibiti mto Senegal ambao ulikuwa unatumika kusafiria hadi Gondiuru (jimbo la Kayes) ambapo chumvi ilisafirishwa kutoka kwenye migodi ya Awlii iliyokuwa chini ya mamlaka yao kama ilivyokuwa migodi ya dhahabu ya Galam. Wakati vita vya wenyewe kwa wenyewe vilipopamba moto katika majimbo ya Soninke ya Wagadu, Bakhumu na Kaniaga, Takrur ilikuwa inateka

Barissa kwenye sehemu ya mto, na hivyo, kama anavyodhihirisha al-Idrisi, kuwa ufalme wenye nguvu sana ambao jina lake lilichukua nafasi ya jina la Ghana kwenye karne ya kumi na mbili na lilitumiwa na Waarabu kuielezea Sudan magharibi yote. Kama vile Kumbi Saleh, mji wa Takrur ulijumuisha eneo la makazi ya Waarabu Waberiberi, lakini eneo lake la mamlaka na taathira liliishia kwenye bonde la Senegal.

Songhai

Mwanzoni mwa karne ya kumi na moja, ufalme huu wa zamani kabisa, ambao ulikuwa nje ya uga wa Ghana, ulikuwa na wafalme wa Kiislamu na uliwakaribisha wafanyabiashara na wasomi Waarabu wa Kiberiberi. Mji mkuu ulihamishwa kutoka Kukya kwenda Gao. Timbuktu, zilipokutana njia za mto na barabara, ulianzishwa mnamo mwaka 1100. Muda haukupita athari ya utawala wa Songhai ikaenea kote kuzunguka Ghuba ya mto Niger.

Majimbo ya Soninke

Mnamo karne ya nane kulikuwa na uhusiano wa kibiashara baina ya Kumbi Saleh na ukingo wa Kaskazini ya Sahara: Waislamu Waarabu wa Kiberiberi walishika nyadhifa za juu kule; na ingawa idadi kubwa ya wakazi iliendelea kuamini dini yao ya asili, kusilimu kulikuwa kumeifikia hata familia ya mfalme Beei; kama vile mwanae Kanmer, ambaye hata hivyo "alificha dini yake." Wale walioikataa dini mpya walikimbilia jimbo la Mema. Matatizo hayo hayo yaliikumba pia Kaniaga (Diafunu) ulipokuwa mji mkuu wa zamani ulioitwa Sain Demba; Mahmud Ka'ti anasema kuwa mji huo uliharibiwa baada ya kuanguka kwa Ghana, na badala yake ukaanzishwa mji wa Zara. Baadhi ya wakazi wa himaya hiyo, Wakussa, walihamia Kussata. Wengine walikwenda Zara ambayo nayo baadaye ilitakwa na mtawala Kaniaga (*Kaniaga fren*) aliyepanua ufalme wake kuelekea jangwani ambako alipambana na Wasoso.

Umaarufu wa Wasoso

Umaarufu wa Wasoso ulidumu kwa kiasi cha nusu karne baada ya mwaka 1180. Mji mkuu wa Wasoso labda ulikuwa karibu na Kulikoro (kaskazini ya Bamako), kwenye milima iliyokaliwa na ukoo wa Wamaninka, wahunzi waliouchukua Uislamu. Tunaambiwa kuwa ukoo wa Wasoninke wa Wajariso ulikuwa umejikomboa kutoka Ghana hata kabla ya kuanguka kwa Kumbi Saleh. Kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na mbili mfalme Kemoko wa Wasoso alikuwa ameunganisha Kaniaga na Soso ambazo alizitawala hadi 1200 wakati.

mwanac Sumaoro Kante au (Sumanguru) aliposhika madaraka. Baada ya kuteka majimbo ya Soninke Sumaguru aliishambulia Mande ambayo iliweka upinzani mkali wa mashambulizi mara tisa mfululizo.

Mansa Dankaran Tuman alimrithi baba yake, Nare Fa Maghan, lakini alipendelea kupatana na Sumaoro ambaye alimuoza dada yake Nana Triban.

Hivyo Sumaoro alikuwa kwenye kilele cha madaraka yake ambayo aliyapanua hadi kwenye majimbo yote ya Wasoninke na kupata utii kamili wa Wamaninke. Alikuwa anatisha kiasi kuwa tunaambiwa watu hawakuthubutu kukutana kuandaa upinzani kwa kuogopa kuwa upepo unaweza kuyachukua maneno yao na kuyafikisha kwa mfalme. Alifikiriwa kuwa mganga na mchawi mashuhuri. Lakini vilevile amesifika kwa kuvumbua marimba na *dan*, gitaa la nyuzi nne ambalo lilitumiwa na mayeli (Yeli) wa wawindaji au waimbaji sifa za mfalme. Ushahidi kutoka kwa wahunzi wa Kikante unatupa sababu nyingine iliyomfanya apingane na Wamande na Wasoninke. Alikuwa mpinzani mkali wa biashara ya watumwa pamoja na Uislamu. Wamande waliasi dhidi ya utozaji kodi wake na wakamwomba mfalme wao Dankaran Tuman aanzishe tena mapambano; lakini yeye aliamua kukimbilia kusini alipoanzisha mji wa Kisidugu (mji wa wokovu). Wafuasi hao walimwomba kaka yake, Sundiata Keita, ambaye alikuwa akiishi ukimbizini huko Mema, aanzishe mapambano hayo.


Mande kabla ya Sundiata

Kumbukumbu za Maandishi

Kwanza al-Bakri, halafu al-Idrisi, wote wanataja falme mbili za Malel (Mali) na Do; wanagusia wafanyabiashara wa Nungharmata (Wangara) walioshika watunwa katika nchi ya Wa-Lem-Lem, wenyeji waliotoja nyuso zao na kubeba vumbi la dhahabu kutoka Irseni [Barissa] hadi nchi nyinginezo. Kufuatana na al Bakri, Mfalme wa Malel alikuwa na cheo cha *al-Muslimani*.

Taarifa za Mdomo

Kuna vituo vingi na shule zenye kutoa mafunzo ya mapokeo simulizi ya nchi ya Wamandenka, ikiwa ni pamoja na Keyla, karibu na Kangaba, ambacho ni kituo kilichomilikiwa na mayeli wa ukoo wa Diabate wenye uhusiano na familia ya kifalme ya Keita. Lakini pia vipo vituo vingine kama Nagassala, Jelibakoro, Kita, Fadama, n.k. Vituo hivi, ambavyo ni nyumba za makumbusho ya simulizi za kihistoria na vyo ambamo mayeli (*maYelii*) wa baadaye walifundishwa, viko chini ya mamlaka ya *Belentigi* (Mabingwa wa Kusema)



● Niani, Soso: miji mikuu na falme
 □ Bamako, Kankan, Siguiri: Miji mipya
 DODUGU } Majimbo
 BURE }
 BAKO }

6.1 Mande ya kale (D. T. Niane)

ambao wanaimudu historia ya Mali inayojiegemeza kwenye jina la Sundiata Keita. Hoja muhimu za hadithi hizi zinapatana sana.

Mwanzoni kulikuwa na falme mbili. Upande wa kaskazini mashariki, karibu na Soso, kulikuwa na ufalme wa Do (Dodugu), na upande wa kusini-magharibi, karibu na machimbo ya Bure kulikuwa na ufalme wa Kiri au Mande (Manden) ambayo baadaye ilikuja kuwa jina la nchi nzima ya Maninka. Dodugu ilikaliwa na ukoo wa Wakonde ambao inasemekana ulijumuisha miji kumi na miwili. Wakonate na Wakeita waliishi nchi ya Kiri, pamoja na Watraore. Polepole Wakamara wa Sibi na Tabon walikalialia eneo la ukingo wa kulia wa Mto Niger (au Bako).

Hatimaye, Wamalel ndio walioliunganisha jimbo hilo. Al-Bakri anasema kuwa mfalme wao alisilimishwa kabla ya kuanguka kwa Ghana. Kufuatana na Ibn Khaldun, mfalme huyu alikuwa Beremundana, ambaye anaweza kuhusishwa na Beremun wa mapokezi ya Kita. Alikwenda kuhiji Maka. Kati ya karne ya kumi na moja na ya kumi na mbili akina Keita tayari walikuwa wameziunganisha *tawala* zote za eneo hilo kuwa ufalme mmoja. Waliadini kuwa wametokana na nasaba ya Bilali au Bilal Ibn Rabah, sahaba yake Mtume na muadhini wa kwanza wa jumuiya ya Kiislamu, ambaye mwanae, Lawalo, inasemekana alikuja Mande (Manden) na kuanzisha mji wa Kiri au Ki (kazi). Mjukuu wa Beremun, Mamadi Kani, alikuwa *simbon* au “bingwa wa kuwinda” na aliutumia udugu huu wa siri, ambao uliimarishwa na kushehenezwa siri za msituni, ili kuiunganisha miji ya Do, Kiri, Bako na Bure kuwa kundi moja la kisiasa chini ya koo za Kamara, Kcita, Konate na Traore. Hii ilikuwa mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili. Karne moja baadaye, mmoja wa vizalia wake, Maghan Kon Fatta, alitawala; wakati huo Wasoso walikuwa katika kilele cha kujipanua kabla ya kumwachia utawala Dankaran Tuman, mwanzilishi wa Kisidugu.

Kwa hiyo, ngano zote zinasisitiza uanzilishi wa mapema wa Uislamu kwa Wamande (Wamanden) na dhima kuu ya wawindaji katika kupanuka kwake; hata mama yake Sundiata aliozwa kwa baba yake, Maghan, na wawindaji wa ukoo wa Traore.

Sundiata Keita

Kati ya mwaka 1220 na 1235 palitokea mapambano ya kihistoria baina ya Wasoso na Wamande (Wamanden) ambayo yaliongozwa na Sundiata. Ibn Battuta na Ibn Khaldun wanayataja mapambano hayo. Kwa kusisitiza Ibn Khaldun anamwelezea Mari-Diata kuwa: 'neni (Mari) lina maana ya *amiri* na (Diata) lina maana ya simba. Alielezea zaidi kuwa “Mfalme, ambaye nasaba

yake bado haijagundulika, alitawala zaidi ya miaka ishirini.” Taarifa ndogo hii ya kimaandishi inaakisi wingi wa mapokezi simulizi. Kulingana na mapokezi simulizi, Sundiata alikuwa na matatizo utotoni na alilemaa kwa muda mrefu. Kwa sababu hiyo, mama yake alikuwa kichekesho kwa wake wenzie. Alipoanza kutembea katika hali ya ajabu, alitokea kuwa kiongozi wa vijana wa rika lake na alionewa sana na kaka yake, Dankaran Tuman. Aliamua kuhama, na ukimbizi (*bori*) huo ulichukua miaka mingi, na kumfikisha Ghana na Mema ambako Mfalme wa Mema alivutiwa na ujasiri wake na kumpa wadhifa mkubwa. Hapo ndipo matarishi wa Kimande walipomkuta, na alikubali kuandamana nao pamoja na jeshi la askari aliopewa na mfalme wa Mema.

Kurudi kwake kulileta msisimko mkubwa baina ya Wamaninka. Watemi wa vita, ambao walikuwa wa rika moja na Sundiata walikuwa tayari kuungana: Tabon-Wana (Ghana), Kamadian Kamara wa Sibi, Faony Konde, Bara Kuman Konate na Tiramaghan Traore. Waliungana na Sundiata kwenye uwanda wa Sibi. Kwenye ukingo wa kulia, uasi dhidi ya Sumaoro Kante uliongozwa na Mansa Kara Noro ambaye askari wake walivaa deraya. Uasi huo ulizimwa tu kwa ufundi na ujanja wa Fakoli, kiongozi wa jeshi la Sumaoro. Lakini wakati wa kusherehekea ushindi huu, Sumaoro aliehukua fursa hiyo kumtongoza Keleya, mke wa Fakoli. Fokoli alichukua na akavuka mto Niger na jeshi lake kuungana na kikundi kilichopo Sibi. Licha ya kipingamizi hiki, Sumaoro aliendelea na mashambulizi. Baada ya mapambano mawili ya wasiwasi, pambano mkataa lilitokea huko Kirina. Sumaoro alifika na askari wake wapanda farasi maarufu akiwa anasaidiwa na marafiki wawili wakuu, Jolofing, mfalme wa Jolof, mchawi mashuhuri, na mtemi wa Tunkara wa Kita. Sundiata alijiamini zaidi kwa sababu dada yake, Nana Triban, ambaye hapo awali alilazimishwa kuolewa na Sumaoro, alitoroka kwa kusaidiwa na yeli wa Sumaoro, Balla Fasseke Kuyate, akichukua kikwaruzo cheupe chenye siri ya kizimu (*tana totem*) cha mumewe wa zamani. Hivyo, Sumaoro alikwenda vitani akiwa amedhoofika kisaikolojia. Alishindwa vibaya sana. Sundiata alimfuata hadi Kulikoro, ingawa hakufanikiwa kumteka. Kulikoro ilitakwa na baada ya muda mfupi Soso iliteteketewa. Ushindi wa Kirina haukuwa tukio la kupita, bali wenye mafanikio ya kudumu: ulileta muungano baina ya koo zilizokusanyika Sibi; ulihakikisha kuwa Mali ilirithi uhalali wa himaya ya Ghana upande wa Sudan magharibi; na mwishowe ulifungua njia ya kueneza Uislamu kusini.

Kuenea kwa Uislamu kuelekea kusini ndiyo hoja ya mwisho ambayo waandishi wa Kiarabu kama vile Ibn Battuta wanaitaja; lakini hawavitaji vita vya Kirina ambavyo viliwezesha usilimishaji wa Wabilad al-Sudan kwa wingi. Kama kwingine kote, taarifa za simulizi zinajaza mapengo, taarifa za maandishi.

Mafanikio ya Sundiata Keita

Ushindi wa Kijeshi

Sundiata alitiisha nchi za Ghana akisaidiwa na majenerali hodari. Tiramaghan Traore alipelekwa magharibi kupambana na Mfalme wa Wawolof, Jolofing, ambaye aliuingilia kati msafara wa wafanyabiashara waliotumwa na Sundiata kununua farasi. Baada ya kumshinda Jolofing, Tiramaghan alianzisha vita katika mabonde ya Senegal na Gambia, akawatiisha Wakasamansi na nyanda za juu za Guinea-Bissau ya leo, na kuanzisha himaya kubwa ya Senegambia ya Kaabu au Gabu.

Fakoli Koroma alitumwa kusini na kutamalaki eneo la mto Senegal ya juu na maeneo yaliyopakana na msitu. Sundiata mwenyewe aliitaka Diafunu na Kita. Baada yake, kwa mara ya kwanza kutiishwa kwa Gao na Takrur kulikamilisha umoja wa Sudan ya magharibi.

Katiba ya Mali

Mapokezi Simulizi yanamsifia Sundiata kwa uwekaji wa maadili ya kijamii na kisiasa ambayo bado kwa kiasi fulani yanawatawala Wamande. Sundiata alipewa majina mengi: *Simbon Salaba* (Mwindaji Mkuu, ambaye kichwa chake kinastahili heshima), *Mari Diata* (Mfalme Simba) na huko Soninke alitwa *Maghan Sundiata* (Mfalme Sundiata). Kufuatana na simulizi, ilikuwa ni kwenye uwanda mkubwa karibu na Kangaba, huko Kurukanfuga, ambapo *Gbara* au mkutano mkuu ulifanyika, mkutano ambao kwa hakika ulikuwa ndio baraza la koo zote za Wamandenka.

- (a) Sundiata Keita alitawazwa kuwa mfalme mkuu pale (*mansa au magha*); viongozi wengine wakawa *farin* magavana katika majimbo yao isipokuwa watemi wa Mema na Wagadu ambao walipewa cheo cha ufalme.
- (b) Mkutano huo pia ulikubali kuwa hapo baadaye mfalme atachaguliwa kutoka kwenye ukoo wa Sundiata kwa upande wa udugu wa kiume. Mfalme huyo alitambuliwa kama jaji mkuu na baba wa wote, na kwa hivyo alipewa cheo cha Noa Mansa (baba yangu, mfalme wangu).
- (c) Koo kumi na sita za watumwa wabeba podo waliopewa uhuru, ziliundwa.
- (d) Koo tano za mawalii, mashabiki wa mwanzo wa Sundiata, ikiwa ni pamoja na Sise Kisse wa Wagadu, Ture (*Toure*) na akina Berete, walitawazwa kuwa walezi watano wa imani.
- (e) Watu waliokuwa na ujuzi maalum waligawanywa katika koo nne-mayeli (*maYelii*), washona viatu, wahunzi na wafumaji.

- (f) Majina ya koo hizo yaligunduliwa kuwa yalilingana na majina ya koo za makabila mengine, na hivyo kuunda *sanankuya*, udugu uliozaa umoja na pia uhusiano wa utani. Huu ndio muundo uliosaidia kupunguza mvutano.
- (g) Wasomono na Wabozo ambao walikuwa mabingwa wa mitumbwi walipewa “ubabe wa maji.”

Kwa kifupi Sundiata “aliigawa dunia,” kila mmoja akiijua haki na jukumu lake. Ujuzi wa kazi za mikono ulirithishwa, hali ambayo haielekei kuwa ilikuwa hivyo nyakati za Ghana.

Serikali ya Sundiata

Marafiki zake Sundiata ndio waliounda serikali. Zaidi ya wao kulikuwa na wanazuoni weusi wa koo za mawalii na labda wafanyabiashara wachache Waarabu. Kufuatana na Ibn Battuta, mnamo karne ya kumi na nne, Mari Diata alisilimishwa na mtu fulani aitwaye Mudrik ambaye dhuria wake aliishi kwenye jumba la kifalme la Mansa Sulayman. Zaidi ya falme za Ghana na Mema, tawala za kitemi zilizotekwa zilijumuishwa kwa urahisi, na kuongezewa gavana (*farin*) sambamba na mtemi wa asili. Hivyo himaya hiyo ilikuwa kama shirikisho la falme na tawala za kitemi, na majeshi ya Wamandenka katika majimbo makuu yakihakikisha usalama na kiasi fulani cha muungano. Himaya hiyo iligawanywa kwenye majimbo makubwa mawili ya kivita. Moja kwa ajili ya upande wa kaskazini chini ya *sura farin* (mkuu wa eneo la kaskazini) na jingine kwa ajili ya kusini.

Nyani Mkuu wa Mali

Mji wa Niani, ulioko Sankarani, ni eneo la Kamara. Sundiata alipendelea eneo hili ambalo lilikuwa na chuma na dhahabu tele kuliko Narena au Dakadiala ambako akoo wa Keita uliishi mwanzoni.

Ukweli ni kwamba ukoo wa nasaba moja mara chache uliweza kujenga mazingira ya kutegemea kama inavyoshuhudiwa na ugomvi baina ya Dankaran Tuman na kaka yake. Zaidi ya hayo, eneo la Dakadiala milimani lilikuwa gumu kufikika; wakati eneo la Nyani kwenye sehemu za tambarare pembezoni mwa Sankarani, lilikuwa na usafiri wa majini mwaka mzima, na pia lilizungukwa na vilima vingi vilivyokuwa na kilele cha jabali, hivyo lilijumuisha faida za uzuri wa mawasiliano na ulinzi.

Zaidi ya hayo, Nyani ilikuwa pembezoni mwa msitu, ambapo palikuwa chanzo cha dhahabu, *kola*, mafuta ya mawese, na pembe za ndovu ambazo wafanyabiashara wa Kimaninka walizinunua kwa kubadilishana na pamba,

bidhaa za shaba na chuinvi. Eneo hili, lililokuwa mbali sana na maeneo ya Sahel kaskazini ambayo yaliweza kuvamiwa na wanomadi lilikuwa salama zaidi. Kwa hivyo liliendelea haraka kama mlango wa njia kuu mbili — moja kuelekea kaskazini, ambayo iliitwa “njia ya Wamande,” nyingine kuelekea kusini, iliyofahamika kama “njia ya Wasarakolle.” Ibn Battuta, ambaye alipitia huko kwenye karne ya 14, aliliita eneo hili Malli. Lakini Al-Umari alikuwa tayari amekwihalipatia jina la Nyeni (Nyani) akiendelea kuisisitiza kuwa ndilo jina rasmi la Mali - kwani ndio mji mkuu wa majimbo ya ufalme huu.

Ni maandishi haya ya Al-Umari ambayo yalimwezesha Maurice Delafosse, baada ya mabishano mengi ya awali, kulionyesha eneo la Nyani sehemu ya Sankarani katika mpaka wa hivi sasa baina ya Mali na Guinea.

Eneo la Nyani lilitambuliwa kwenye miaka ya 1920, lakini uchimbaji wa makini ulifanyika baada tu ya mwaka 1968 na watafiti Waguinea na Wapoli. Makazi ya Waarabu na mji wa kifalme vimetambuliwa kutokana na misingi ya nyumba za mawe, *kibla* ya msikiti na kuta zilizozunguka mji wa kifalme. Majengo yalikuwa ya matofali ya tope, kama Al-Umari alivyoandika, akiongezea kuwa: Dari zilitengenezwa kwa nguzo na matete. Zinakaribia umbo la kuba (yaani umbo la pia au nundu ya ngamia), kama tao lenye zege. Sakafu za nyumba hizo zilikuwa na udongo uliochanganywa na mchanga... Mfalme alikuwa na ikulu nyingi zilizozungukwa na ukuta wa duara. Wanaakiolojia wamelinganisha maandishi haya pamoja na mapokeo simulizi na mambo yanayoonekana. Magofu yametapakaa hivi leo kuanzia Nyani hadi Sidikila, umbali wa km 25, na kulikuwa na vijiji vingi vya koo zenye ufundi anuwai.

Sundiata alitangaza Nyani eneo la kifalme, makazi ya watu wake wote. Watu walioishi humo walikuwa mchanganyiko. Kama ilivyokuwa wakati wa wafalme wa Ghana, watoto wa kiume wa *mafarin* na wafalme vibaraka walilelewa huko.

Kifo cha Sundiata

Hapa tunaweza tu kuzungumzia kinadharia kwa sababu kuna mapokeo tofauti na kwa sababu ni mwiko katika nchi ya Mande kutoa siri ya makaburi ya wafalme wakuu. Kufuatana na Maurice Delafosse, Sundiata aliuawa kwa bahati mbaya na inshale wakati wa sherche; inawezekana zaidi kuwa alizamishwa kwenye maji marefu ya Sankarani, kwani km 10 juu kutoka Nyani ni sehemu inayoitwa Sundiata-dun (maji marefu ya Sundiata). Sehemu hii ya mto ina mizingo mingi. Katika kingo kwenye sehemu hii, makafara mengi hufanyika mara kwa mara na wazao wa karibu wa mtamalaki huyu. Huko Kirina, “wanajadi” Wamamissoko hutoa kafara kwenye msitu wa ibada. Huko

Tigan, kati ya Wakamara, kuna lundo la majivu liitwalo *bundalin* ambamo ndani yake inaaminika kuwa kuna viatu, kisu na deraya za Sundiata. Mwisho, kuna sherehe kila baada ya miaka saba karibu na sehemu ya ibada iitwayo *Kamablon* huko Kangaba: huko nako yasemekana kuna vitu vya Sundiata.


Muziki sanifu wa Wamande ulianza wakati wa Sundiata (*Sundiata tele*). Hekaya ya mtamalaki huyu iliyoitwa *Sundiata fassa* na iliyotungwa na yeli wake, Balla Fasseke, iliandamana na muziki maalum. Sundiata aliufanya wimbo ulioitwa *Boloba* (muziki kabambe), uliotungwa na mayeli wa Sumaoro Kante, muziki wa kila mpiganaji wa Kimaninka aliyeuomba. Duga (*tai*) ni muziki ulitengwa kwa ajili ya wapiganaji mashuhuri tu. Na *Janjon* (utukufu kwa mpiganaji) iliwekwa kwa ajili ya Fakoli Koroma na *Tiramaghan fasa*, mshindi wa majimbo ya magharibi.

Warithi wa Sundiata Keita

Katika maandishi yake maarufu ya *Historia ya Waberiberi* na *Utangulizi* Ibn Khaldun anakiri umaarufu wa kisiasa na kiuchumi wa Mali katika dunia ya Waislamu ya karne ya 14. Alipata taarifa zake kutoka kwa wafanyabiashara wa Kiarabu na balozi za Mali huko Kairo. Maelezo yake yanalingana katika sehemu nyingi na taarifa zilizotolewa kwenye simulizi.

Kanuni ya zamani ya urithi wa udugu (wa kiume) ilikuwa haifuatwi baada ya kifo cha Sundiata. Mwana mkubwa, Mansa Oulin alitawala kuanzia 1250 hadi 1270. Wamande walijizatiti huko Tukrur na Senegambia na kuanzisha makazi huko. Baada ya kifo chake, hila za kiikulu zilitishia umoja wa himaya hiyo. Sakura, jenerali mkakamavu, alizima ghasia zote hizi kwa ushindi wake huko kaskazini dhidi ya Watuareg na katika bonde la mto Niger hadi Gao; aliua alipokuwa anarudi nyumbani kutoka hija na alizikwa kwa heshima za kifalme huko Mali. Baada ya kipindi cha watawala hafifu, mpwa wa Sundiata, Kanku Musa I, alitawala kuanzia 1307 hadi 1332. Kipindi hiki kilikuwa ni kilele cha ufanisi wa Mali, na hija yake ilielezewa kwa upendo na maandishi wengi.

Baada ya mwanae, Maghan I, ilikuwa ni kaka yake, Mansa Sulayman, ambaye aliweza kuulinda ukubwa wa himaya hiyo. Hatimaye, "koo" za kisiasa zilianzisha tena mapigano ya wao kwa wao. Mtoto wa Mansa Sulayman, Fomba, alitawala kwa mwaka mmoja tu. Aliondolewa kitimi na Sundiata II ambaye alikuwa dhalimu aliyeharibu himaya hiyo na kufilisi hazina, na hata, kwa kufuatana na Ibn Khaldun, akauza dhahabu nyingi yenye kilo 25 kwa bei rahisi kwa wafanyabiashara wa Misri. Alikufa kwa ugonjwa wa malale na



6.2. *Shajara ya nasaba ya mansa wa Mali kidingana na Ibn Khalidun.*

*Angalia : majina yaliyopatikana kwa mapokezi yako kwenye mabano (D.T. Niane)

kurithiwa na mwanac, Mansa Musa II (1374-87) ambaye chini yake madaraka halisi yalikuwa kwenye mikono ya jenerali ambaye alizima maasi ya Takadda, mji wa shaba. Kisha hila zilizochochewa na mabinti wa mfalme zilitingisha himaya hiyo lakini hazikuizuia kufurahia hadhi yake ya kudumu.

Ushindi wa Uislamu chini ya Mansa Musa

Mansa Musa I (1307 - 32)

Ilikuwa ni Mansa Musa ambaye aliifanya Mali ifahamike Afrika Kaskazini na Mashariki ya Karibu kwa kutoa dhahabu nyingi sana kiasi cha kuifanya thamani ya dhahabu ianguke. Kutoka wakati huo Sudan iliwasumbua watu vichwa, kama ilivyofanya Eldorado baadaye. Ili kuimarisha mamlaka kuu, alipata msaada wa jenerali mmoja mwenye uwezo sana, Saran Mandian, ambaye aliweza kuwadhibiti Wanomadi wa Sudan, waliokuwa na tabia ya kupora, na kuipanua himaya yake hadi kwenye bonde la Niger kupita Gao.

Ili kutayarisha hija yake Mansa Musa alitoza mchango maalum kwa kila mji wa biashara na kila jimbo. Wafuasi wake walikuwa wengi: wapagazi 60,000, watumishi waliopambwa na dhahabu 500, kila mmoja akiwa amebeba mkuo wa dhahabu. Sifa hizi zilizotiwa chumvi zinatoa sura fulani ya kiwango cha utajiri.

Huko Kairo Mansa Musa I alikuwa kama mfalme mmojawapo wa hadithi za Kiarabu.

Al-Makrizi aliacha picha iliyojaa sifa zake: Alikuwa kijana mwenye ngozi ya maji ya kunde, uso wa kuvutia na umbo zuri, aliyefunzwa madhehebu ya Kimaliki. Zawadi zake zilivuta macho kwa uzuri na ufahari wake. Kufuatana na mapokeo, alinunua ardhi na nyumba huko Kairo na Maka ili wakae mahujaji kutoka Sudan. Kwa ufupi, mahusiano mazuri yalikuwa sasa yameanzishwa baina ya nchi alizopita na Sudan.

Mansa Musa, mjenzi na mlezi

Mfalme alirudi na msanifu majengo mashuhuri, Ishak al-Tuejin, ambaye alijenga msikiti mkuu wa Gao, msikiti mkuu wa Timbuktu, ambao pia ulifahamika kama *jingereber*, na jumba la kifalme au *madugu*. Lakini alionyesha ufundi wake wote kwenye chumba maarufu cha hadhira kwenye "Uwanja wa Nyani, wenye kuba juu yake, ambayo aliipiga lipu na kuipamba kwa michoro ya majani yenye rangi za kuvutia." Kulingana na Ibn Khaldun, ulikuwa mnara wa kuvutia. Huko Sudan, kutokana na ukosefu wa mawe, tope huimarishwa kwa miti ambayo huchomoza kwenye majengo.

Ibn Amir Ajib, gavana wa Kairo ambaye sultani wa Mamluk alimtea kumwangukia hujaji huyu mashuhuri anatumia kuwa rangi za bendera yake zilikuwa njano juu ya nyekundu: "Akiwa juu ya farasi walimpungia bendera za kifalme, yaani bendera kubwa juu ya kichwa chake." Akieleza idadi ya watu wa dola lake, Mansa Musa alizungumzia "watu wengi sana," akiongeza kuwa kwa kufananisha na kusini mwa Sahara, idadi ya watu wa Mali "ilikuwa ni kama doa dogo jeupe kwenye ngozi ya ng'ombe mweusi." Kuhusu uchumi alisisitiza kuwa ni Tigidda (Takedda) "ambako kuna mgodi wa shaba nyekundu. Hakuna kitu katika himaya yangu ambacho ni chanzo kikubwa cha kodi kama uingizaji wa shaba hii ghafi ... Tunaipeleka kwenye nchi za wapagani weusi ambako tunauza moja ya shaba hii kwa dhahabu yenye theluthi mbili ya uzito wake."

Katika ngazi ya siasa na ufundi, Mansa Musa I alieleza wazi kuwa aliyemtangulia alifia baharini. "Kwani mfalme huyu hakutaka kuwasikiliza wale waliomwambia kuwa ilikuwa haiwezekani kuivuka bahari na alicndelea kukaidi katika lengo lake" hata akatayarisha safari ya merikebu 200 ambayo ilihariki; kisha akatayarisha meli 2,000 ambazo aliziongoza yeye mwenyewe ... asirudi tena.

Kuhusu hoja hii waandishi wengi, kama vile Wiener na Jeffreys, wamejadili tatizo la kufika kwa watu weusi Marekani kabla ya Kristofa Kolumba, na kwa kweli kufanana kwingi kumeonekana baina ya vitu fulani kwenye ustaarabu wa

Mexico na vitu kwenye Afrika ya watu wesci. Angalau tukio lililotajwa na mfalme wa Mali linaonyesha kuwa mwanzoni mwa karne ya kumi na nne viongozi wa Sudan walijihusisha na matatizo ya safari za baharini.

Wakati aliporudi Mali, Mansa I, ambaye alikuwa akifahamu Kiarabu vizuri sana, lakini kila wakati akitumia wakalimani alipokuwa akizungumza na Waarabu, alilita maktaba ya Kiarabu na makarani wa Kiarabu, *makadhi* na waalimu. Hata hivyo wataalamu hawa walishindwa kubadilisha vyombo vya kiutawala na kisiasa. Makundi ya kitaalamu na kibiashara yaliyohusiana na shughuli hizo yalianzishwa na uhusiano huo ulifanya Walata, Jenue na Timbuktu kuwa miji ya biashara na vyuo vikuu sawa na miji ya aina hiyo Afrika ya Kaskazini, kwani mnamo karne ya kumi na tano na kumi na sita waliweza kuchapisha fasihi kamili ya watu wesci kwa lugha ya Kiarabu.

Mahusiano ya kidiplomasia yalianzishwa na kulikuwa na, kwa mfano, mabadilishano ya mabalozi na zawadi baina ya Mali na Wamarini wa Fez.

Mansa Sulayman


Ilikuwa ni wakati wa utawala wake (1336-58) Ibn Battuta alipotembelea Mali na kukaa katika mji mkuu kwa miezi tisa. Maoni yake yanaoana na taarifa zilizotolewa na al-Umari zenye kutoa picha nzuri na ya undani kuhusu jumba la *Mansa* na utawala wake.

Mansa na Baraza lake

Kama alivyokuwa mfalme wa Ghana, mansa alikuwa kwanza kabisa ni mtoa haki na baba ambaye watu wote walifikisha malalamiko yao kwake. Aliwaondoa madarakani inagavana ambao walipatikana na kosa la madai ya vitisho. Watu wake walimsujudia, wakiwa wamejipaka vumbi na kusema *N/a* Mansa (“Bwana wangu”, “baba yangu”).

Mansa alikutana na watu kwenye chumba cha faragha kilichojongwa na Musa I, au chini ya mti mkubwa kwenye kiti cha enzi kilichotonwa kwa dhahabu na pembe za ndovu. Luteni-jenerali (*Kankoro Sigi*), waheshimiwa, magavana, wahubiri na wataalamu wa sharia walikaa kwenye nafasi zao na *yeli*, ambaye alikuwa kama msemaji au mwongozo sherehe, alisimama mbele ya kaumu kwenye chumba cha faragha: “Kilemba cha mfalme kilipambwa kwa matamvua, ambayo watu hawa waliyapanga kwa ufundi mkubwa. Shingoni kulikuwa kumening'inia kijambia chenye ala ya dhahabu ... Alishikilia mikuki miwili ... mmoja wa fedha na mwingine wa dhahabu.”

Kazi ya *yeli* ilikuwa ni “kusimulia” historia na kuyakumbuka majina na matendo ya kishujaa ya wafalme. Watu waliapa kwa jina la mfalme *Mansa Sulayman Kib*.



6.3 Himaya ya Mali 1325 (D. T. Niane)

Sikukuu za Kiislamu zilikuwa ndizo siku za sherehe za kuvutia, ingawa ibada za asili zilikuwa bado hazijatoweka kwenye maenco ya mfalme, kama Ibn Battuta alivyogundua kwa mastajabu.

Kuhusu waheshimiwa, kufuatana na al-Umari, walivalia vizuri sana na kupambwa kwa dhahabu. "Waungwana wa podo" ambao ni wazao wa rafiki za Sundiata walitofautishwa na "Waungwana wa kilemba" ambao walitokana na koo tano za mawalii.

Ustaarabu'wa Wamande (Wamandinka)

Katika kilele chake cha ustawi Mali iliwakutanisha watu mbalimbali wa enco la Sudan - Sahel.

Wanomadi na wafugaji


Wamesufa, Wanomadi wakuu wa Sahara, walikuwa ndio wengi kutoka kwenye mashimo ya chumvi ya Toghazza hadi mji mkuu wa biashara wa Walata. Walikuwa mawakala wa biashara kwenye biashara ya chumvi na pia viongozi wa misafara. Upande wa magharibi Walamtuna, Wasanhaja na Waberiberi wa Godala waliishi pwani ya Atlantiki, wakati Watuareg walikuwa kati ya Walata na Kuruba ya Niger. Watu wote hawa walikuwa ndani ya mstari wa ngome za kijeshi.

Watu wa Sahel

Sahel ilikuwa na majani mengi ya kulishia wanyama nyakati zile. Miji ya kaskazini ilikuwa imejengwa huko: Takrur, Awdaghost, Kumbi, Walata na Timbuktu. Enco hili lilikuwa enco la Wafulbe wa maisha ya kinomadinomadi, wafugaji ng'ombe ambao waliwahamisha wanyama wao kulingana na misimu; walikuwapo pia kwa kiasi fulani makundi ya watangulizi waliofanya makazi ya kudumu kusini zaidi. Wakuliina - Watukuloor (Toucouleur), Wasoninke na watu wa Songhai - walikuwa wamekwisha silimishwa mapema (karne ya kumi na moja na kumi na mbili). Waliishi kwenye miji mikubwa ambayo baadaye ilikuja kuwa majiji.

Watu wa Savana

Kutoka magharibi hadi mashariki watu walioishi huko walikuwa Wawolof, Wasereer, Wamande na Wasoninke; lakini hata kabla ya karne ya kumi na tatu wafanyabiashara na mawalii wa Kisoninke na Kimande waliweza kupatikana Senegambia. Pwani, kati ya Gambia na Rio Grande, ziliishi jumuiya za wakulima na wavuvi wa Kibeafada, Kibalante, Kidiola, Kifelupe na Kibaininke. Jumuiya hizo zilisifika kwa kilimo cha mpunga. Wareno walifika



6.4 Pégué: Gwanda wa pamba la Tellem kwenye pango C (awamu ya pili ya Tellem, karne ya kumi na moja hadi ya kumi na mbili). (R M A. Bedaun, 1977)

katika enco hilo mnamo karne ya kumi na tano na ni kutokana nao ndipo tunafahamu kuwa enco hili liliathiriwa sana na Wamande.

Mali ilikuwa na watu wengi sana, hasa kandokando ya mto na kuzunguka vituo vikuu vya kilimo na biashara. Kwa mfano, kufuatana na *Ta'rikh al-Sudan*, enco la Jenne lilikuwa na vijiji 7,077 ambavyo vilikuwa karibu karibu sana kiasi kwamba mfalme alipohitaji kumwita raia ujumbe huo ulisemwa kwa sauti kubwa kwenye mojawapo ya milango ya boma na uliweza kurudiwa kijiji hadi kijiji mpaka kuwafikia walengwa. Mahmud Kati aliandika kuwa Mali "ilikuwa na kiasi cha miji 400" na kuwa udongo wake ulikuwa na rutuba sana. Kati ya falme za watawala wa ulimwengu, Shamu pekee ndiyo inayoizidi Mali kwa uzuri. Wakazi wake ni matajiri na wanaishi vizuri. Mji mkuu wa Nyani ulikuwa na wakazi kiasi cha 100,000 katika karne ya kumi na nne. Zaidi ya hayo, watawala wa Gao walipenya hadi ukingo wa Niger na kumweka gavana huko Hombori, chini ya milima ya nchi ya Wadogon.

Wadogon

Watu hawa, ambao kazi zao za sanaa zinapatikana katika hazina ya kazi zilizokusanywa huko Ulaya na Amerika, wamechunguzwa sana kichthonolojia na kitakvimu, lakini ni hivi karibuni tu ambapo wamechunguzwa na R.M.A.

Bedaux katika muktadha wa uhusiano wao kihistoria na watu wengine wa Kuruba ya Niger. Kutoka kwenye majabali ya Niger kama yale ya Bandiagara ambayo yalivikinga vijiji vyao vilivyojengwa juu kuepuka wavamizi; Wadogon wanasemekana kuwa wamehama kutoka Mande mnamo karne ya kumi na nne; na kuhamia kwenye milima ambapo watu, waliotangulia, waliowaita *Tellem* (ikimaanisha “tuliwakuta hapo”), iliwabidi washuke chini kwenye nyanda za Yatenga. Mfananisho wa vyombo vya udongo vya Wadogon na vile vya Wamanika wa Nyani unaonyesha uhusiano wa karibu baina yao.

Kwa jumla, muundo ulioundwa na himaya hiyo uliclekea kuisitiza tofauti baina yao, kwa kutumia mfumo wa majina yanayofanana na uhusiano wa utani, kwa mfano baina ya Wamande na Wafulbe, Wafulbe na Wawolof, na Wamande na watu wa pwani n.k.

Mfumo wa kisiasa na kiutawala

Serikali Kuu

Muongano wa Mali uliwekwa chini ya mamlaka ya Mansa aliyesainiwa na baraza la waheshimiwa waliotokana na marafiki wa Sundiata. Katika ngazi za mwanzo, huko Mande, kulikuwa na vijiji vilivyounghanishwa kufanya majimbo au *kafu (jamana)*.

Sambamba na mtawala kulikuwepo na unashuhuri wa yeli msemaji wa mfalme (ambaye alizungumza kwa upole) na ambaye pia alikuwa msemaji wa watu, na wa wajumbe waliopokelewa kwenye jumba la mfalme; aidha alikuwa mwalimu wa watoto wa mfalme, mwendeshaji sherche na kiongozi wa beni ya mfalme.

Katika karne ya kumi na nne, Mansa alikuwa na makarani ambao walitumika tu wakati ujumbe ulipokuwa unatumwa kwa watawala wenzake. Wakati inwingine wote ujumbe ulitumwa au kupokelewa kwa ndomo.

Kama “baba wa watu wake” na mtoa haki, mfalme kama hakutembea alikaa ikulu. Katika majimbo aliwakilishwa na *makadhi*.

Maafisa

Licha ya yeli anatajwa luteni-jenerali, mkuu wa majeshi, na *santigi* (huyu mwanzoni alikuwa mkuu wa ghala za nafaka na baadaye mkuu wa hazina). Mwanzoni kazi hii ilifanywa na mtumwa wa mfalme. Koo zote za mali ziliwakilishwa mbele ya Mansa na ‘watemi’ walioteuliwa.

Serikali ya Jimbo

Katika karne ya kumi na mbili, dola hilo lilikuwa na majimbo kumi na mawili,

kila moja likiwa linaongozwa na gavana (au *farin*). Majimbo muhimu zaidi yalikuwa Takrur, ukingoni mwa Senegal ya kati na ya chini; Bambugu, iliyokuwa maarufu kwa migodi ya dhahabu, Dia au Diafunu kwenye Niger ya kati, Gao au Songhai, ambayo ilijipatia uhuru mwishoni mwa karne ya kumi na nne; Sanagana, ambayo ilitajwa na Al-Umani, nchi ya Wasanhaja na Wagodala. Kila jimbo lilikuwa na tarafa ndogo, ambazo mara kwa mara zilikuwa ni vitengo vya koo, na zilikuwa na ikulu ndogo ya *farin* iliyokuwa ni mfano wa ikulu ya Mansa.

Ghana na Mema zilikuwa falme mbili za kirafiki zilizokiri mamlaka ya Mali.

Mali ilipata uimara kutokana na mfumo huu nyumbufu, uliohakikisha usalama wa bidhaa na watu kwa kuwepo na jeshi ambalo kwa muda mrefu halikuweza kushindwa.

Jeshi

Nyaraka za Kiarabu zinataja watu 100,000 wenye silaha. Nguvu hizi za kijeshi zilikuwa zinatokana na Wamande ambao walikuwa wapiganaji na watu wenye nidhamu. Kwa kawaida jeshi lilikuwa limejengewa maboma kwenye miji mingi, na majukumu yake yalisambaa hadi Tegahazza. Hata watoto wa mfalme wa Maghrib walioondolewa madarakani waliomba msaada wa Mansa Musa kupata tena viti vyao vya enzi.

Askari wapanda farasi ambao walikuwa kikosi cha waali, walitokana na watu wa koo bora za *watontigi* (wabeba podo na pinde), lakini pia walijua namna ya kutumia mikuki na majambia. Walikuwa chini ya amri ya Mansa moja kwa moja.

Mwanzoni farasi walitoka Takrur na Jolof; lakini uzalishaji farasi ulistawi ghafla katika bonde la Niger. Askari wa miguu walikuwa chini ya amri ya waungwana wadogo. Wale wa kutoka Sahara walipigana kwa ngao maarufu za ngozi. Vikosi vya watumwa vilitokea baadaye kabisa.

Hali ya Kiuchumi

Kilimo

Ingawa Mali ilifahamika nje kwa ajili ya “dhahabu ya Sudani” ilikuwa hasa ni nchi ya kilimo na ufugaji. Nyaraka zote za kimaandishi zinataja wingi wa vyakula; mpunga ulipandwa kwenye mabonde ya mito na hasa hasa Kaabu. Mtama, zao kuu, ulipandwa kwenye maeneo makame zaidi. Pia kulikuwa na maharagwe, viazi na mboga nyingine nyingi. Ibn Battuta anatumia kuwa msafiri hakuhitaji kubeba chakula chochote kwani kila kijiji kilikuwa na chakula cha kutosha.

Raslimali kama hizo zilikuwa ni njia mojawapo ya kulidumisha jeshi na



6.5 *Humayo ya Mali: Sanamu ya mpanda furasi, ilipatikana katika eneo la Bamako (makadiriwa kuwa ya miaka 680±105 kabla wa 1979, 1194-1404) (B. de Grunne, 1980).*



6.6. *Itimaya* ya Mali: Sanamu ya mama na mtoto (unakadiriwa kuwa ya miaka 690 ± 105 kabla ya 1978; 1184-1394) (B de Graine, 1980).



6.7 *Himaya ya Mali* - *Sawamu ya mtu alyepiga magoti, kutoka eneo la Bankou*
(mukali wa kiwa ya maka 680 ± 105 kabla ya 1979 (1396-1586)
(B de Gume 1980)

ufalme. Mansa alikusanya mazao ya mwanzo ya mavuno. Kukataa mchango huu kulikuwa sawa na kuasi.

Katika karne ya kumi na tano, mabaharia wa Kireno waliarifu kuwa pamba ilikuwa ni mojawapo ya raslimali kuu za Wakasamanse.

Ufugaji na Uvuvi

Ufugaji ilikuwa ndiyo kazi kuu ya Wafulbe, lakini wakulima wa bondeni pia walishughulika na kazi hiyo, hasa mifugo midogo.

Uvuvi ilikuwa ni kazi maalum ya makabila fulani kama vile Wasomono wa Niger ya juu, Wabozo wa Niger ya kati na Wasorko kati ya Timbuktu na Gao. Samaki waliofukizwa au waliokaushwa walipakiwa kwenye vikapu vikubwa na kuuzwa sehemu za mbali hadi kufika sehemu za msitu.

Mafundi

Shughuli za ufua chuma na ngozi pamoja na ufumaji zilikuwa ni za koo fulani tu. Chuma kilikuwa kingi kwenye milima ya Wamande na wafuaji ambao walikuwa na karakana kubwa Nyani walitengeneza zana na silaha.

Wafumaji waliuza majora ya pamba; nguo zilizowekwa rangi ya buluu iliyokoza ilikuwa ndiyo kazi kuu ya Watukulor na Wasoninke, hususan wa ukoo wa *Mabo*.

Ndoa kati ya ndugu ilikuwa ndiyo kanuni baina ya mafundi ambao majukumu yao na haki zao zilielezwa wazi wazi.

Biashara

Dhahabu, chumvi, shaba, kola, nguo na samaki ni kati ya bidhaa zilizosafirishwa kwenye barabara za Mali.

Dhahabu, ambayo ilikuwa inapatikana zaidi Mali kabla ya kugunduliwa kwa dunia mpya, ilitoka kwenye machimbo ya Bure katika Niger ya juu, Bambuk na Galam katika Senegal ya juu. Nyani ilikuwa pembezoni mwa maeneo yenye dhahabu ya Bure. Mansa kama mtawala wa Ghana, alikuwa na haki zote za kupata mawe ya dhahabu. Lakini maeneo mengine yaliyokuwa kusini zaidi (Volta, Nchi ya Akan) pia yaliipatia Mali dhahabu.

Chumvi ya baharini kutoka Senegambia na chumvi ya mawe zaidi kutoka Teghazza na Ijil, iliuzwa Afrika Magharibi yote. Vivyo hivyo kwa shaba ambayo ilichuuzwa kutoka kaskazini hadi nchi ya Akan na ufalme wa Benin.

Uuzaji wa kola ulileta uhusiano baina ya wafanyabiashara Wadiula na Wawangara na wale wa Waakan na Waguro wa maeneo ya msitu.

Kwenye njia hizi kuu za biashara, Wamande walijenga vituo vya kupumzikia

ambavyo kati yavyo vilikuja kuwa miji mikuu ya biashara kama vile Kong na Begho. Walitangaza Uislamu hadi nchi ya Hausa. Walituma misafara ya punda na watumwa waliobebeshwa chumvi, bidhaa za pamba, samaki na vifaa vya shaba kila walipoclekca eneo la msitu na walirudi na dhahabu, pembe za ndovu na kola.



*Kuanguka kwa
Himaya ya Mali: karne ya
tano hadi kumi sita*


Utangulizi: vyanzo

Baada ya karne ya kumi na nne, iliyotawaliwa na utukufu wa Mansa Kanku Musa, Mali ilipitia kipindi kirefu cha kushuka pole pole, kikiasliiriwa na shughuli zake muhimu *kuhamishiwa* magharibi. Ukiritimba wa Waislamu katika biashara ya kuvuka sahara uliendelea kuimarishwa katika Songhai na Kanem, ambapo biashara ya Mali, iliyokwisha poteza masoko ya Timbuktu na Jenne hadi Songhai, ilielekezwa Sutuko na pwani ya Senegambia ambako Wazungu walikuwa wanaanza kuwasili.

Kipindi hiki kina kumbukumbu chache. Baada ya Ibn Khaldun, ilipita zaidi ya karne moja kabla ya kutokea maandishi ya Leo Africanus yaitwayo *Africae Descriptio*, ambayo ndiyo ushahidi wa mwisho wa Kiarabu juu ya himaya hiyo. Kwa upande mwingine, idadi ya maelezo ya Warcno ilikuwa ikiongezeka. Ca da Mosto na Diego Gomes walikuwa wa kwanza kuuabiri mto Gambia kati ya 1455 na 1456. Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita tunaona Duarte Pacheco Pereira na Valentim Fernandes. Muhimu zaidi, mwishoni mwa karne tunakuta kitabu kiitwacho *Tratado Breve dos Vios de Guine* cha Alvares d' Almeida, Mreno aliyezaliwa katika kisiwa cha Santiago do Cabo-Verde na kufanya biashara katika eneo analolielezea.

Tarihi za Sudan za kuanzia karne ya saba zinafaa kwa kuijua Mali ya kipindi hiki, japo zina upendeleo kwa namna fulani.

Mwisho, mapokeo simulizi ya wakazi wa Mali ya Magharibi, hususa wale wa ufalme wa Kaabu au Gabu, yanatupa mwanga wa dhima ya uchumi ya maeneo haya, ambapo mapokeo ya Futa Toro na Futa Jallon yanatupatia taarifa juu ya mahusiano kati ya himaya ya Mande na taifa la Fulani la Futa Toro.



7.1 *Situa ya Kanabha (kusini-magharibi ya Kangaba, Mali) kutoka kwenye Safari za Mungo Park katika Maeneo ya Ndani ya Afrika (1790). (Maktaba ya Tanja, Paris)*

Himaya ya Mali yapoteza udhibiti wa biashara ya jangwani

Ilikuwa ni wanomadi, kabla ya Songhai, walioitikisa Mali

Watuareg na Waberiberi

Mali ilikuwa na vikundi kadha vya Waberiberi, kwa mfano Wa-Kal Antasar na Wa- Lamtuna, katika utawala wake. Walikwishaanza kuishi maisha ya maskanini na walilipa kodi kwa Mansa. Lakini Mabedui katika Air na Andrar des Ifogha waliendelea kupinga na waliweza kudhibitiwa barabara chini ya tawala za watawala imara kama Kanku Musa na Sulayman. Musa II alipofariki, mgogoro wa urithi ulitokea kati ya aila za Sundiata na wale wa ndugu yake mdogo Mandé Bory. Watawala waliuawa na nguvu ya kifalme kudhoofishwa. Hatimaye katika karne ya kumi na tano, Watuareg walizitaka Timbuktu, Walata na Nema. Jambo hili liliathiri mahusiano ya Mali na maeneo mengine ya jangwani. Kuibuka kwa Songhai chini ya Sonni Ali kulikuwa kikwazo kikubwa kwa ueneaji wa Watuareg na utamalaki wa Mali, ambayo ilipata uhai mpya kutokana na biashara kati yake na Wareno.

Majimbo ya Magharibi ya Mali

Kufika kwa Wareno kuliyafanya majimbo ya magharibi, ambayo hapo awali hayakuwa na umuhimu wa haja, yachukue nafasi muhimu. Baada ya uhusiano wa kibiashara kuanzishwa, Mali na Ureno zilianzisha uhusiano wa kibalozi.

Biashara

Mali ilimiliki machimbo ya dhahabu ya Bure na pia ilipata dhahabu kwa biashara toka hata nchi za kusini hadi Asante. Misafara ilipeleka dhahabu hii hadi pwani ya Gambia na kuibadilisha kwa shaba, bidhaa za pamba toka India na nguo za anasa. Wawangara walikuja na vipimo vyao na mizani; na ingawa mara nyingine walilazimika kurudi na sehemu ya dhahabu yao makwao, aghalabu waliweza kujipatia faida kutokana nayo.

Wazungu waliutanua utaratibu huu wa biashara, mathalan kwa kununua farasi Futa na kuwauza Gambia kwa mgavana wa Mali na pia Jolof. Punde watumwa waliingizwa katika mzunguko huu, kwanza kwa kubadilisha watumwa wanane na baadaye watumwa kumi na watano kwa farasi mmoja. Jeshi la Mali lilitoa watumwa zaidi na zaidi, wengi wao wakipelekwa kuishi Ureno.


Alvares d'Almeida alipatia kwa kuandika (kuwa) 'ni katika Gambia ambako kuna biashara kubwa kabisa katika enco lote la Guinea.'

Kilimo na Ufugaji

Idadi kubwa ya wenyeji walijishughulisha na kazi hii. Gambia ni jito kubwa ambalo mafuriko yake wakati mwingine yaliweza kuhamisha mashua kutoka kwenye mkondo wake na kuitelekeza msituni. Udongo wa kinamasi kutoka mito kadha ulitengeneza makonde mazuri ya mpunga na pamba. Kwenye misitu ya kandokando ya mito uwindaji uliotegemea ujuzi wa mazingira kwa kiasi fulani na siri za kiganga ulishamiri, hususani kutokana na makundi makubwa ya tembo yaliyoimarisha biashara ya pembe. Pamoja na wafugaji wa Ki-Fulbe wakulima wadogo waliweka mifugo michache. Biashara ya ngozi ilistawi hasa mwishoni mwa kipindi hiki.

Maisha ya Kijamii

Urithi ulikuwa wa upande wa mama, kama ilivyokuwa katika Ghana, kufuatana na al-Bakri. Uhakikishaji kuwa uhusiano wa damu unabaki upande wa mama ulizaa upendeleo wa wapwa. Hivyo Farin Songoli, Mangi Mkuu wa Gambia, aliwakilishwa na mmoja wa wapwa zake huko Niumi. Mwanamfalme aliyeteuliwa kurithi, wakati mwingine alitakiwa kutawa kwa mwaka mzima ili



7.2 Dola za Sudan kwenye karne ya kumi na sita (baada ya Madina Ly-Tall)

ajitakase. Hapo ufalme ulisimamiwa na jenerali wa mfalme aliyepita. Utaratibu huu ulizusha mizengwe mingi.

Kushikilia dini ya jadi hakukuondosha ukiukwaji wake. Hivyo kadhia nyingi za 'ulozi' ziliamuliwa na jaribio la maji mekundu, maji hayo yakiwa ni kinywaji kilichotokana na mizizi ya *mcailedra*. Mshinde alifanywa mtumwa. Mila hii ilitumiwa vibaya na baadhi ya machifu kujiongezea watumwa. Zaidi ya hayo, Uislamu mara nyingi ulitumiwa kama pambo. Kwa hiyo, kabla ya kuandama vita, mfalme wa Kiislamu wa Kasamansi aliunfanya imam mwenyewe kutaka ushauri wa wapiga ramli,

na alimwaga vinywaji kwa wafu. Mashambani, fito zilizopakwa unga wa mchele au mahindi uliochanganywa na damu ya mbuzi zilisimikwa kuhakikisha mavuno mazuri. Imani za kishamba ziliendelea kuhuishwa.

Hata hivyo, Uislamu ulikuwa unapiga hatua, hata kama machifu hawakusita kuritadi (kuhama Uislamu na kuingia Ukristo). Mawalii waliendelea na kazi yao bila kukata tamaa. Ule utulivu wa kale ukapinduliwa na athari zote zilizokuja na mkondo wa biashara na dini mpya. Zaidi, mamlaka ya kisiasa ya Nyani yalikuwa mbali. Yalisaidiwa na baadaye kung'olewa pole pole na mfalme wa Kaaba ambaye alijiita *Kaab Mansaba* (Mfalme Mkuu wa Kaabu). Kwani tishio jipya la kisiasa na kijeshi lilikuwa likiinyemelea Senegambia: tishio kutoka kwa Wa-fulbe wa Denianke.

Kuibuka kwa Wa-fulbe

Watengella (1490-1512)

Tangu karne ya kumi na tatu wafugaji wahamaji wa Kifulbe wamekuwa wakielekea kusini kutafuta majani na maji. Wakaja kukutana katika Futa Toro, Bundu, Masina na Futa Jallon, ambako, baada ya kipindi cha kuishi na wenyaji au chini ya mamlaka yao, waliendelea kujenga mataifa yenye nguvu.

Hiyo ndiyo iliyokuwa historia ya mapokeo ya Tegella na mwanawe Koly katika Futa Toro. Je, watu hawa walihusiana hasa na Sundiata, au hadithi liyo ilikuwa ni kisakale tu? Je, watu hawa asili yao ni Futa Toro au ni Futa Jallon? Vyovyote vile iwavyo, mgongano na Wamande ulikuwa hauna budi.

Mgongano huo ulitokea kati ya mwaka 1481 na 1514. Karne moja baadaye, Alvare d' Almeida alihadithiwa juu ya idadi kubwa ya wapanda farasi waliokuwa nao; lakini aliambiwa pia juu ya kundi kubwa la mifugo yao, jambo ambalo linaleta fikra kwamba Koly Tengella alifanya maskani kwenye nyanda za juu zenye nyasi nyingi za Futa Jallon; kutoka hapo alielekea kaskazini, kutoka kwenye miamba ya milima, kwenye uchochoro ulio katikati ya Mali na

majimbo yake ya magharibi. Sasa ilichukua miezi sita kwa wafanyabiashara waliotumwa na Mansa kufika Sutuko ndani ya Gambia.

Majeshi ya Koly na baba yake Tegella, yakishehenezwa na vikosi vilivyochangiwa na wakazi mbalimbali wa Fulbe, yalimiminika katika Futa Toro baada ya kuvuka mto Gambia na kutwaa Bundu. Halafu Tengella akaelekea kwenye Ufalme wa Jara (Diara) na mwanawe, Koly, akaanza kutamalaki Futa Toro.

Ndani ya Ufalme wa Jara

Ufalme huu ulioshikwa na mwana mfalme Omar Komzagho wa Songhai ulikuwa bado unagombaniwa na wapinzani wa Kimali. Ni wakati huu huu ambapo Tengella alitokea, lakini akauawa mnamo 1511-12. na jeshi la Gao. Jimbo hili lilikuwa muhimu kwa himaya ya Songhai kama njia ya kufikia machimbo ya dhahabu ya Bambuk.

Kushindwa kwa Futa Toro na Jolof

Katika Futa, machifu wadogo, waliokuwa chini ya mamlaka ya Mali hapo awali kupitia Jara, waliutumia ushindi huu wa Songhai kujikomboa. Koly, hata hivyo, alizishinda kwa urahisi tawala hizo zilizogawanyika na kujenga makao mkuu yake hapo Anyam-Godo.

Kufuatana na simulizi za mapokeo zilizokusanywa na Raffeneil mwaka wa 1846, Koly aliteka nchi kutoka kwa Waberiberi na Wajolof; Wajolof walitimuliwa kutoka mabonde ya mto na mikondo yake. Utawala huu juu ya nchi jirani ulidumu hadi mwanzo wa karne ya kumi na nane. *Silatigi* mtawala wa Futa, aliitwa "Fulo-Mkuu" na Wareno. Lakini mamlaka ya Mali yalifika hadi nchi za Kasamansi na Gambia kwa kilomita kama 1500 kuzunguka Sutuko.

Hatima ya himaya ya Mali

Pamoja na tishio la Songhai upande wa mashariki na nguvu ya Denianke upande wa magharibi, Mali ilibidi ikabili pia usumbufu wa Wareno. Baada ya jaribio la kutumia mabavu kwa wenyeji wa pwani kushindikana, Wareno walitumia njia ya kidiplomasia mwishoni mwa karne ya kumi na tano, kwa kupelcka mabalozi kwa mfalme wa Futa, Mansa wa Mali na Koi wa Timbuktu kutoka kwa Mfalme John II wa Ureno.

Kufuatana na umuhimu wake Mali ilipelekewa tume mbili, tume moja ikipitia mto Gambia na nyingine ikitokca katika ngome hapo El Mina. Katika barua yake kwa mfalme wa Ureno, Mansa Mahmud III aliilinganisha himaya

yake na zile za Kairo na Baghdad. Ujumbe wa Kireno uliotumwa mwaka 1534 toka El-Mina ulikwenda kujadiliana juu ya masuala kadha kuhusiana na biashara katika mto Gambia.

Lakini Wareno walikwisha anza kuingilia kati magomvi ya ndani ya nchi hizi za pwanipwani. Mnamo 1482, walijaribu kumtawaza Bemoy, ambaye alikuwa anakaimu ufalme. Zaidi ya hayo, kwa kupitia ziara za kirafiki, walikuwa wakikusanya taarifa, na walikuwa wakitumia biashara kujaribu kuwatenga machifu wa pwani na utawala wa Mali.

Takio mahsusi ambapo jambo hili lilitendeka ni Ufalme wa Salum, ulioanzishwa mwishoni mwa karne ya kumi na tano na M'Began N'Dur, mfalme wa Sine. Ufalme huu ulitwaa kaskazini ya mto Gambia mnamo 1556. Mfanyabiashara Alvares d'Almeida anaelezea juu ya muundo wake imara wa kijeshi na makapteni - jenerali wawili ambao waliidhinishwa na Mfalme kukusanya majeshi, pindi panapotokea mzozano. Machifu wa vijiji vya Kimande, walitoa vikosi vya wapanda farasi ambao farasi wao walinunuliwa kutoka kwa Wafulbe na Waberiberi. Polepole, ufalme huu ulijikomboa kutoka Gambia na kukua kwa kuididimiza Gambia, hata kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba Gambia, jimbo la mbali la Mali, ikawa haitajwi tena; nafasi yake ikachukuliwa na falme tatu: Salum, Wuli na Kantor. Lakini huu ndio uliokuwa mlango peke wa Mali wa kutokea nje (duniani).

Tapatapa ya mwisho ya Mali

Mahmud IV alijaribu kuyatumia maafa yaliyojitokeza katika delta ya Niger ya ndani kutokana na uvamizi wa Wamoroko. Akiungwa mkono na karibu machifu wote wa

Fulbe na Bambara, aliongoza jeshi hadi Jenne. Hapo, mmoja wa marafiki zake akamkimbia dakika ya mwisho na kujiunga na Wamoroko, ambao, kwa kutumia ushauri wake, licha ya kufadhaishwa na ukubwa wa majeshi ya Mali, walifanikiwa kuyashinda baada ya milipuzo mikali.

Lakini hata kama alishindwa, mansa alipokea heshima anayostahili kuipata. Washirika wa Wamoroko kufuatana na *T'arikh al Sudan*, walikutana naye mahala pa usalama, wakamwamkia kama sultani na kumvulia kofia kumpa heshima yake, kama ilivyokuwa ada yao. Majimbo ya Mali yakajitoa moja baada ya moja na kufanya falme ndogo tano. Ufalme uliokuwa na matumaini sana kati ya falme hizo ni ule uliunganisha pamoja vituo na vikundi vya wahamaji wa Kibambara kwenye maeneo ya delta ya Niger ya ndani. Huu ndio ulizaa falme za Kibambara za Segu na Kaarta; Mali yenyewe ilibakia kuwa ufalme mdogo schemu za Kaabu na Kita.

Hitimisho

Baada ya kunyang'anywa majimbo yake ya kaskazini katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na sita, kwa manufaa ya Watuareg na Wasonghai, Mali iliponapona kwa karne moja na nusu nyingine, kutokana na nguvu za uchumi za majimbo yake ya magharibi ambako ushahidi wa Wareno unaonyesha miundo ya kisiasa na ya kijamii ambayo ilikuwa bado imara.

Wafarin waliowawakilisha *Mamansa* waliwadhibiti barabara machifu wengi wa vijiji: waliojulikana kama *njoni mansa*, *bati mansa*, *kasa mansa* na kadhalika. Kwenye masoko yaliyotapakaa kingo za mto Gambia, kama Sutuko, Jamnam Sura, n.k. Wareno walibadilishana farasi mvinyo, vitambaa, mapambo ya vioo/gilasi, na bangili kwa vyakula, dhahabu, watumwa, pembe na vifa vya kazi za mikonosanaa.

Kuanzia karne ya kumi na sita Kaabu ukawa ufalme huru wenye nguvu (kuliko Mali). Msukosuko mkubwa wa harakati za Wadenianke, pamoja na kuwako kwa Wareno sawia, yote haya yalidhoofisha sana misingi ya himaya ya Mali ambayo ilielekeza mamlaka yake Worodugu (nchi ya Kola, msituni).

Baada ya pambano la mwisho na Wasonghai, Mali ilibakia na sehemu ndogo tu ya ardhi mwanzoni mwa karne ya kumi na saba.



Wasonghai tokea karne ya 12 hadi ya 16

Baada ya kipindi kirefu cha kujiandaa na ambacho kilichukua karne nyingi, Wasonghai, waliokuwa wamekaa katika kingo zote mbili za mto Niger, waliunda serikali mnamo karne ya kumi na tano. Serikali hii iliunganisha sehemu kubwa ya Sudani ya magharibi na kuwa msingi wa kuanzishwa kwa ustaarabu mpevu.

Ufalme wa Gao kutoka karne ya 12 hadi majilio ya Sonni Ali Ber mnamo 1464


Kipindi cha kwanza hakijulikani wazi. Ingawa yapo maandishi machache ya kihistoria au napokco simulizi, lakini vyanzo hivyo havitoi taarifa za kutosha zaidi ya nadharia tete za kufanyia utafiti.

Ufalme wa Gao katika karne ya 12

Kulingana na nafasi yake kijiografia katika Pindo la mto Niger kwa kukabiliana na pande la Sudan ya Kati, katika karne ya kumi na mbili, Gao ikawa mji mkuu wa serikali mpya ya Wasonghai, na kuishia kuugubika mji wa kale ulioitwa Kukya na maandishi wa Kiarabu.

Chumvi kutoka jangwani, bidhaa kutoka Misri, Libya na Ifrikiya, zilizopitia Tadmekka na Turat, ziliifanya Gao kuwa soko kubwa na la mseto wa watu. Al-Bakri na Al-Idrisi wamethibitisha kuweco kwa Gao na Kukya, mji ambao katika karne ya kumi na mbili ulikuwa umezungukwa na ukuta.

Ufalme huu, uliosambaa katika kingo zote mbili za mto kutoka Dendi hadi Gao, ulikuwa unatawaliwa na Joa au Zaa ambao pengine walikuwa ukoo wa Wasonghai waliooana na Waberiberi. Uislamu uliingizwa katika jumba la



8.1 Himaya ya Songhay kueleka mwishoni mwa karne ya kumi na sita (D.T. Niane)

ufalme mnamo mwaka wa 1019 wakati wa utawala wa mfalme Jaa Kosoy. Hata hivyo umma uliendelea kuamini dini zao za jadi. Mawe ya kaburi yaliyoandikwa habari za marehemu na ambayo ndiyo ushahidi wa kuwepo kwa Uislamu yaonekana kama yaliletwa kutoka nje.

Utawala wa Mande na nasaba ya kifalme ya Sonni

Katika mwisho wa karne ya kumi na tatu, Wamali waliwashinda Wagao na Kanku Musa, akirejea kutoka hija, akajenga msikiti na kumteua gavana. Hata hivyo Wagao hawakusita kujitoa katika utawala wa Nyani pindi nafasi ilipojitokeza.

Katika karne ya kumi na tatu nasaba mpya ya Wasonni iliyoanzishwa na Ali Kolon ilijikomboa.

Kufuatana na Boubou Hama, Wasonni au Wasii au Washi walikuwa mashujaa wa vita kutoka Kukya, ambao waliitaka Masina, Mkoa wa Soninka wa Mema, na hata Nyani, mji mkuu, ambapo Sonni Madawu alileta koo 24 za watumwa ambazo ziliongezea nguvu uwezo wa kifalme.

Ufalme wa Wasonghai katika karne za 15 na 16

Sonni Ali aliacha uvamizi wa mara kwa mara na kuamua kuitawala nchi. Alilipanga upya jeshi lake, ambalo lilipewa merikebu za kupitia mto Niger. Jeshi hilo liliamriwa na *hi-koy*, na kikundi cha askari wa miguu kilichowachukua wapiganaji bora zaidi kutoka kwa washinde. Zaidi ya yote kulikuwepo na kikosi cha wapanda farasi ambacho kutokana na kasi yao, pamoja na ushupavu wao vitani katika eneo lote la Niger, kilijigeuza jeshi kuu kuliko yote katika Sudan.

Kwa kusifiwa kuwa mchawi aliyicitwa *daali* (Mtukufu kabisa), Sonni Ali alitia hofu mioyoni. Aliitaka Jenne na sehemu mojawapo ya Masina ambamo Wafulbe wengi waliuliwa. Baadaye, mnamo 1468, ikawa zamu ya Timbuktu.

Watuareg wa Kaskazini, Wadogon na Wabariba wa kusini walishambuliwa. Mnamo mwaka wa 1483 alimshtukiza na kumshinda mfalme wa Wamossi, Nasere I, katika vita vya karibu na Jenne, alipokuwa anarudi nyumbani kutoka Walata akiwa ameshehenezwa na ngawira za thamani. Kutokana na ushindi huu, Sonni Ali aliyakomesha mashambulizi ya Wayatenga katika bonde la Niger.

Ufalme wa Wasonghai ulisambaa kutoka Dendi hadi Masina. Ulikuwa umepangwa vizuri na kuwekwa chini ya magavana walioitwa *fari*, *farma* katika lugha ya Kimande, na *Koy*, *mondzo* katika lugha ya Kisonghai. Sonni Ali

alimteua kadhi mjini Timbuktu, lakini alishindwa katika mipango yake ya kujenga mfereji baina ya Niger na Walata. Hata hivyo alijenga mabwawa yaliyotumika kuendeleza kilimo.

Katika mambo ya dini maandishi ya miaka ya baadaye ya wanazuoni wa Kiislamu wa Timbuktu, yamemwelezea Sonni Ali kuwa dhalimu, katili na asiye na murua. Kwa kweli Sonni Ali, ambaye alilelewa Sokoto, nchi ya mamake, aliendelea kushikilia mila za kabla ya Uislamu. Aliwapinga Maulama kwa urafiki wao na Watuareg, watu ambao alijaribu sana kuwashinda. Kwa hiyo zilikuwa pingamizi za kiitikadi na kisiasa ambazo zilimngonganisha na wanasharia wa miji mikuu ya eneo la mto Niger.

Maaskiya (miaka ya 1492 - 1592)

Mtawala wa mwisho wa Kisonni ambaye aliukataa Uislamu alifukuzwa kutoka utawala na *Hombori-Koy Toure* au *Sylla*, aliyekuwa Muislamu mwaminifu na ambaye alianzisha cheo cha kifalme cha *askiya*.

Hombori-Koy Toure, aliyekuwa mwanazuoni wa asili ya Soninke na Takrur, alikuwa mwadilifu na wa wastani. Aliziunganisha juhudi za Waislamu ili kuimarisha na kutilia nguvu mafanikio ya Waislamu wa Sunni.

Akichukua dinari 300,000 alikwenda Maka, akiandamana na kundi la wapanda farasi na maulama 800. Alikutana na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar mjini Kairo. Katika Maka alipata kibali cha upendeleo kwa mahujaji wa kutoka Sudan na pia kupata cheo cha Khalifa wa Sudan kutoka kwa Sharifu wa Maka. Kwa hiyo, baada ya kuhalalishwa utawala alirudi nyumbani na kufanya kazi pamoja na nduguye, Umar Komdiagho, katika kuipanua milki yao hadi Masina na Diara, mashimo ya madini ya Tehazza, Agades na miji ya Wahausa ya Katsina na Kano ambako Tengella aliuawa. Hata hivyo kwa upande wa kusini mipaka ya milki haikubadilika, licha ya mashambulizi dhidi ya Wadogon, Wamossi na Wabariba.

Umar Komdiagho, ambaye alichaguliwa kuwa *kurmina fari*, alijenga mji wa Tendirma. Katika mikoa mipya *askiya* aliwateua magavana waliokuwa waaminifu kwake na pia akateua makadhi katika miji yote ya Waislamu. Aliunda upya serikali na baraza la kifalme na kuyapa hadhi mamlaka ya kidini.

Ili kuhimiza biashara, aliimarisha kikosi cha polisi wa masoko na usimamizi wa mizani na vipimo. Katika kuhamasisha kilimo, alianzisha mashamba kwa watumwa waliotekwa vitani na akapunguza kodi kwenye mavuno. Uendelezaji wa elimu ulihakikishwa kwa heshima na zawadi nyingi walizopewa ma'ulama. Askia Muhammad alizeeka na kuwa kipofu. Aliondolewa uongozimi katika njama zilizoongozwa na mwanawe mkubwa, Musa.

Warithi wa Askiya Muhammad

Watoto wa kiume wa Askiya Muhammad walikuwa hawana tena nchi za kuteka, bali walifanya mashambulio tu na kuliana njama za kupinduana ndani ya nyumba ya ufalme. Wakati huohuo matatizo ya mashimo ya chumvi ya Tegahazza, yaliyotamaniwa sana na Wamoroko yalisababisha mwisho wa utawala wao.

Tutaona baadaye jinsi matatizo haya yalivyojitokeza katika tawala za maaskiya watatu wawakilishi wakuu wa kipindi hiki.

Ishak wa Kwanza (miaka ya 1539-49)

Wakati wa utawala wa mwanamfalme dhalimu huyu, sultani wa Kisadi Muhammad Al-Shaykh, alidai umilikaji wa mashimo ya chumvi ya Tegahazza. Ishak wa Kwanza aliyajibu madai hayo kwa kutuma kikosi cha farasi cha Watuareg kuwatimua Wadraa wa Moroko.

Dawud (miaka ya 1549-83)

Utawala huu wa muda mrefu na wenye ujiri uliongozwa na mtawala msikivu na aliyejipatia werrevu kutokana na hila za tawala zilizotangulia na pia wadhifa wake mkubwa ulikuja wakati himaya hiyo inafikia kilele cha ufanisi. Kulikuwa na ustawi mkubwa wa kiuchumi na usomi. Misafara ya kibiashara iliyovuka jangwa la Sahara ilifanikiwa zaidi kuliko biashara za bahari ya Atlantiki. Uchungaji mzuri wa raslimali iliyotokana na shughuli za kiuchumi ulimwezesha mtawala (*askiya*) kuhodhi hazina ya sarafu na maghala ya nafaka, Mali nyingi hii ndiyo iliyohudumia, kwa kiasi, wasomi, maskini na misikiti. Pamoja na kufanya mashambulizi dhidi ya Wamosi na Masina, Askiya Dawud alifanikiwa kupata masikizano na Sultan Ahmad Al-Mansur ambayo yalihakikisha umilikaji wa Wasonghai wa mashimo ya Tegahazza. Lakini chini ya utawala wa mrithi wake, Askiya Muhammad wa Tatu (miaka ya 1583-86), kutwaliwa kwa mashimo ya Tegahazza na Wamoroko kuliwafanya Watuareg kuhamia upande wa kusini ili kuitumia chumvi kutoka mabwawa ya Taudeni. Baada ya hapo Tegahazza ilididimia na kuwa maghofu.

Kuchaguliwa kwa Muhammad wa IV, Bano, kuwa *askiya* Mnamo mwaka wa 1586 kulizusha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika mwaka wa 1586 ndugu zake wengi, akiwemo *balama* (amiri jeshi) Al-Saddik, waliuvamia mji wa Gao wakiyaongoza majeshi kutoka upande wa magharibi. Maasi hayo yalikomeshwa kwa ukatili na himaya ikagawanyika. Schemu ya magharibi ilivunjika moyo na kuacha kujishughulisha na mambo ya Gao. Hivyo mnamo

mwaka wa 1591 hawakusita kuwakaribisha wavamizi kutoka Moroko. Himaya hiyo ikajiletea maangamizi yake yenyewe.

Ustaarabu wa Wasonghai

Utawala msonge chini ya mamlaka unganifu ya kiimla uliupa ufalme wa Gao sifa za kisasa ambazo zinautofautisha na utawala nyumbufu wa kimajimbo uliokuwepo katika Ghana na Mali.

Ufalme

Mfalme aliheshimiwa kama baba mwenye mamlaka tukufu na mwenye kuhakikisha ustawi kwa watu wote. Njia ya pekee ya kumkaribia mfalme ilikuwa ni kwa kumsujudia. Pamoja na mila za Kisudan, kulikuweco na zile za Kiislamu zilizowekwa shinikizo na Askiya Muhammad na Askiya Dawud.

Baraza la kifalme la Gao lilijumuisha ndugu za mfalme, wakuu, na mayeli walioitwa *gesere* na *mabo*. Mfalme aliketi kwenye jukwaa lililokuwa limeinuliwa huku akizungukwa na matowashi mia saba. *Wandu* au yeli mkuu ndiye aliyetangulia. Kwa kanuni mfalme akiaga dunia ndugu yake mkubwa ndiye aliyemrithi. Mrithi alitangazwa na nyumba ya mfalme na kutawazwa hapo Kukya. Hata hivyo mazoea yalionyesha kuwa jambo la muhimu katika urithi lilikuwa ni uwiano wa madaraka baina ya wale waliodai uongozi.

Serikali ya Kifalme

1) Serikali kuu iliundwa na walioshikilia vyeo vya juu wakikaa kama baraza la himaya.

Mwandishi wa baraza alishughulikia mawasiliano, kumbukumbu za mikutano na mikataba au mapatano ya ndani na ya nje. Kwa sababu ya ukosefu wa upambanuzi wa kazi maandishi ya kihistoria (Tarehe) hutoa tu orodha ya kazi na waliozisimamia.

Bwana mkubwa wa majini au *hi-koy* ndiye aliyekuwa jemadari wa kikosi cha majini. Alikuwa ni kama waziri wa mambo ya ndani na mwenye mamlaka juu ya magavana, pengine, kwa sababu ya umuhimu wa mto katika maisha ya himaya.

Aliyeshikilia uwaziri wa kilimo aliitwa *fari mondzo*. Afisi hii muhimu, iliyosimamia mashamba makubwa ya himaya, kwa kawaida ilishikiliwa na watawala wa damu ya kifalme au hata wana wa mfalme mwenyewe. *Saw farma* alikuwa ndiye kamishina wa misitu na kazi zake zilifanana na za *fari mondzo* lakini zilikuwa za kiwango cha chini zaidi.

Kalisa farma au “waziri wa fedha” ndiye aliyesimamia hazina ya

ufalme. Huyu alisaidiwa na *werney farma*, afisa aliyesimamia mali ya ufalme, *bana farma* ambaye alisimamia mishahara, na *doy farma* aliyesimamia ununuzi. Mkuu wa majeshi alitwa *balama*; mamlaka yake yalipunguzwa baadaye, akaachiwa usimamizi wa kikosi cha askari waliokuwa katika mkoa wa Kabara-Timbuktu. Hata hivyo afisa huyu huenda wakati huo alimtegemea zaidi makamu wa mkuu wa nchi aliyeitwa *kurmina fari*. Waziri aliyesimamia shughuli za wageni weupe alitwa *korey farma*. Zaidi ya hawa kulikuwepo na idadi kubwa ya makamishina wa serikali walioteuliwa inara kwa mara ili kutekeleza kazi maalum.

(2) Serikali ya mikoa ilikuwa na pande mbili:

(a) Upande mmoja ulijumuisha mikoa iliyotekwa ambayo ilitawaliwa moja kwa moja na askiya, ambaye aliwateua magavana (walioitwa *fari, farba* na *farma*) kuisimamia. Machifu wa viwango vya chini waliitwa *koy* au *mondzo*. Mambo yaliyohusu sheria yalisimamiwa na kadhi peke yake.

Himaya ilikuwa na mikoa mikubwa miwili yaani Kurmina uliokuwa upande wa magharibi na Dendi ambao ulikuwa upande wa kusini-mashariki. *Kurmina fari* au *kanfari* alishika cheo cha pili katika serikali na mara nyingi cheo hicho kilishikiliwa na mwana mfalme mrithi. Huyu aliishi mjini Tindirma na yaonekana kama alisimamia sehemu yote ya nchi ambayo ilikuwa magharibi mwa Timbuktu, hasa kufikia mwisho wa karne ya kumi na sita. Wakati huo alikuwa na jeshi lenye nguvu la kuweza kukabiliana na jeshi la Gao. Majoribio ya kulikabili Jeshi la Gao yalifanywa mara kadha.

Dendi Fari alikuwa msimamizi wa mkoa wa kusini-mashariki. Alikuwa wa tatu kwa cheo katika serikali ya nchi na ndiye aliyesimamia mipaka ya nchi ya upande wa kusini.

Baadhi ya mikoa maalum ilipewa madaraka ya kujisimamia yenyewe chini ya machifu waliochaguliwa na *askiya* kama vile *Hombori Koy* na *arabinda farma*. Mipango kama hiyo ilitekelezwa kwa miji mikubwa kama

vile Timbuktu, Jenne, Walata na Teghazza, ambayo ilikuwa na uhuru wa utawala chini ya usimamizi wa *koy* au *mondzo*. Huyu alisaidiwa na maajenti wengi maalum kama vile *asara mondzo*, aliyekuwa kamishina aliyesimamia sera ya inasoko na pia utekelezaji wa hukumu za kadhi, mainspekta wa mizani na vipimo, wakaguzi wa kodi masokoni, maafisa

wa forodha kutoka Kabara, wakuu wa mashirika ya uzalishaji, machifu wa makabila na wengineo.

(b) Nchi huru zilizokuwa chini ya ulinzi wa himaya zilitawaliwa chini ya sheria za kienyeji. Machifu walioteuliwa na wenyeji walitambuliwa na askiya lakini palipotokea ugomvi baina ya walioudai au maasi *askiya* aliingilia kati na kumpachika chifu wake kutawala. Nchi hizi zilikuwa ni pamoja na Masina, jamii za Wahausa katika Kano na Katsina, ufalme wa Waagades na muungano wa Watuareg Kel Antassar. Utiifu wao kwa askiya ulionyeshwa kwa ulipaji wa kodi, kutoa vikosi vya majeshi vilivyohitajika na mfalme, ziara za kumtembelea mfalme, zawadi na ndoa.

Kwa kuzingatia utaratibu huu wa kanuni na taasisi za ndani na za asili ya Kiislamu, serikali ya Songhai ilihakikisha usalama wa Mali na wa watu na, pia, udumishaji wa mamlaka yasiyo ya mtu binafsi, katika nyakati zote, kukiwa shida au la. Tajiriba hii ya kipekee ya ustawi wa dola hili la Kiafrika ilikatizwa kikatili kwa ushindi wa Wamoroko.

Vyombo vya Dola

Dola lilikuwa na jeshi la kudumu lililohakikisha usalama wa ndani na wa nje. Wingi wa utajiri wake uliisaidia kudumisha uhuru. Uhuru wa kisheria waliokabidhiwa makadhi na machifu wa kijadi ulisaidia kulinda uhuru na haki za watu.

Jeshi

Malodi (watu wa nasaba bora) ndio waliokuwa uti wa mgongo wa kikosi cha wapanda farasi waliovalia deraya kifuani chini ya nguo zao za vita. Farasi walikuwa ghali kununua (kama mateka kumi kwa farasi mmoja). Kwa hivyo kikosi cha wapanda farasi kilikuwa ni cha waungwana waliopendelewa zaidi.

Jeshi la askari wa miguu liliundwa kutokana na watu huru na mateka. Walitumia mikuki, mishale na ngao za ngozi au shaba. Muziki wa kijeshi ulipigwa na mistari mirefu ya wapiga tarumbeta ndefu (*kakaki*), na bendera kubwa ziliyatangulia majeshi. Kufuatana na maandishi ya *Ta'rikh al-Fattash*: "Wanaume mashuhuri wa Songhai walikuwa na ujuzi mwingi wa vita. Walikuwa mashujaa jasiri na wataalam katika matumizi ya mikakati ya kijeshi."

Jeshi lililokusanyika katika vita vya Tondibi, mnamo mwaka wa 1591, lilikuwa na askari wa miguu 30,000 na wapanda farasi 10,000, baadhi yao

wakiwa walinzi wa mfalme. Hili lilikuwa ndilo jeshi kubwa zaidi lililoundwa katika Sudan ya Magharibi. Lilikuwa chombo cha kisiasa na pia cha kiuchumi hasa kwa sababu ya idadi kubwa ya nyara lilizoteka.

Raslimali ya kifedha

Kulikuwa na namna nyingi za kujipatia fedha, kwa mfano, mapato kutoka mashamba ya serikali, malipo ya zaka kwa ajili ya maskini, kodi ya mavuno, mifugo na uvuvi, pia kodi na ushuru wa forodha juu ya biashara, kodi maalum kwa wafanya biashara mijini; na nyara kutokana na vita vya karibu kila mwaka. Mapato haya yaligharamia matumizi ya nyumba ya mfalme, utawala, majeshi na pia zawadi na sadaka.

Sheria

Kulikuwa na aina mbili za hukumu, ambazo zilienda sambamba katika milki. Moja ilikuwa ni hukumu chini ya sharia za Kiislamu za madhehebu ya Maliki. Kadhi ndiye aliyekuwa jaji mkuu huru, wa maisha, aliyeteuliwa na mfalme. Hiki kilikuwa ni cheo ambacho hakikutamaniwa sana na kwa hivyo baadhi ya watu walilazimishwa kukichukua. Katika Timbuktu cheo hiki kilishikiliwa kwa muda wote wa karne ya kumi na sita na familia mashuhuri ya kadhi Mahmud ben Umar al-kit. Kadhi alisaidiwa na makatibu, makarani wa mahakama na mawakili. Alifanya kazi kama msajili: aliweka rekodi za watumwa walioachiliwa huru, mirathi, uhalalishaji wa mikataba ya watu binafsi na mengineyo. Alilinda haki fulani za kimsingi. Alikuwa ndiye mkuu hasa wa Timbuktu.

Sheria za kimila, ambazo ndizo zilizoenea kwa wingi katika himaya, zilisimamiwa vizuri na maajenti wa kimila. Baraza la kifalme likiketi kama korti ya kisiasa lilitoa uamuzi juu ya mambo ya dola.

Maendeleo ya Kiuchumi

Sehemu za mashambani

Mbinu za kufanyia kazi hazijabadilika sana tangu wakati huo. Jembe (jepesi au zito), sanadi, kilimo cha mboga katika mabonde, na ulimaji wa kuhamahama nyikani, zilikuwa ndizo mbinu za kilimo. Bonde la Niger lilikuwa na watu wengi zaidi wakati huo. Mashamba makubwa yaliyoliniwa na watumwa yalikuwa ya mamwinyi. Askia ndiye aliyemiliki ardhi kubwa zaidi ambapo mashamba yake yalisimamiwa na *fanfa*.

Samaki walikuwa wengi na uvuvi ulifanywa na Wasorko, Wado na Wabozo. Ufugaji wa wanyama ulifanyika kwa wingi katika baadhi ya mikoa kama vile Masina na Bakhunu. Wanyama walitoa nyama, maziwa na ngozi, hasa kwa matumizi ya wakaaji wa mijini. Nao walioishi mashambani walijipatia bidhaa za viwandani na chumvi kutokana na ubadilishanaji huu wa bidhaa.

Sekta ya biashara

Njia za kuvukia jangwa la Sahara zilikuwa ni hizi zifuatazo: kutoka Timbuktu kupitia Teghazza hadi Tilimsan, kutoka Timbuktu kupitia Walata, Tishit, Wadan na Draa hadi Fez; kutoka Gao hadi Tunis, Tripoli na Kairo kwa kupitia ama Tuwat au Fezzan. Pia kulikuweco na njia ya upande wa mashariki kupitia ama nchi ya Wahausa au Kanem na kwenda hadi Nili ya chini.

Biashara ya kuvuka jangwa la Sahara ilifanywa na Waarabu wa Kiberiberi. Wasudani (Wawangara), Wawakore (Wasoninke), Wamossi, Wahausa na Wasonghai waliendesha biashara katika miji iliyopakana na jangwa, ambapo mawakili walifanya biashara ya kufana hasa kutokana na kupanda na kushuka kwa bei. Pia walijiunga ili kutumia usafiri uliokuwepo, yaani mashua katika mto, ngamia, maksai wa kupakia mizigo, na punda. Alipofika Kabara, Leo Aficanus alieleza kuwa bandari ya Timbuktu ilikuwa na mlundikano wa bidhaa za kila aina.

Biashara ilifanywa kwa ubadilishanaji wa bidhaa au kwa kutumia bidhaa za kulipia kama vile kauri, dhahabu, chumvi na shaba. Wasudan waliingiza chumvi ya mawe kutoka jangwani, vitambaa, zana za vita, shaba, bidhaa za voo, sukari na bidhaa za kifundi kutoka Afrika ya Kaskazini. Himaya iliua nje dhahabu, pembe za ndovu, viungo, kola, watumwa na bidhaa za pamba, zote zikitoka sehemu zilezile kama nyakati za Himaya ya Mali. Biashara ya ndani iliingiliana na ile ya mbali, kwa mfano, ile ya nafaka, samaki waliokaushwa ama kwa moto au kwa jua, na bidhaa za kifundi. Katika mfumo huu wote mji wa Jenne ulikuwa kituo kikubwa cha usambazaji bidhaa na uhamasishaji wa biashara.

Hata hivyo biashara hii, ambayo iliwatajirisha baadhi ya wakazi wa mijini, iliathiri uzalishaji sehemu hizi kwa kiasi kidogo tu. Kwa kiasi kikubwa biashara ilishughulika na bidhaa za madini na za ukusanyaji. Kwa hivyo biashara ya kuvuka jangwa la Sahara ilihusu zaidi ubadilishanaji wa bidhaa za ndani na zile za kutoka nje kuliko uchumi halisi wa soko uliotegemea uzalishaji wa ndani. Hali hii inaelezea kwa nini kulikuwa na mabadiliko madogo sana katika muundo wa jamii na mbinu za kazi licha ya mabadiliko katika mijengo ya nyumba, chakula na mavazi miongoni mwa waungwana mijini.

Muundo wa jamii ya Niger

Jamii yote ya Songhai ilidhihirisha umuhimu wa uhusiano wa udugu. Koo zilikuwa za asili mbalimbali. Kabila la Wasoninke, (Wature, Wasylla, Watunkara, Wasisse, Wajakhite, Wadrume na Wajawara), kabila la WaSonghai (Wamaiga), Wamande (Watraore, Wakeita na Wajamara) n.k. Zaidi ya hawa kulikuwa na watu wa mchanganyiko wa damu ambao walitokana na mchanganyiko wa jamii iliyoishi mijini ambamo kulikuwa na Waberiberi.

Kuweko kwa tofauti za kikabila kulimaanisha tofauti za kikazi kwa Wafulbe au mateka wa vita walioajiriwa katika jeshi kwa lazima au katika kazi za kilimo. Hali hii ya kuweko kwa tofauti za kikazi iliyoambatana na tofauti za kidaraja inaweza kuonekana pia katika tabaka za jamii kama vile mamwinyi au waungwana, watumwa walioachiwa huru, wanachama wa mashirika ya uzalishaji, na watumwa. Watu huru walikuwa wakulima wenye kujitegemea, watumwa walikuwa wafanyakazi wasiojitegemea, wanachama wa mashirika ya uzalishaji walibobea katika ufundi wa kienyeji, ambapo waungwana walijitengea kazi za utawala, mamlaka na vita.

Jamii ya mashambani

Watu wengi waliishi vijijini kama ilivyo katika falme na himaya za Afrika ya siku hizi. Mafundi, kama wavuvi, walijishughulisha na kilimo pia. Pengine watu hawakuwa na dhiki kama Leo Aficanus anavyodai. Usalama ulikuwa jambo la kawaida, na njaa ilikuwa nadra. Hapatajwi popote maasi ya wakulima. Orodha ya Mali ya msimamizi wa serikali katika Dendi yaonyesha kuwa kulikuwa na waliomiliki ardhi kubwa katika sehemu za mashamba. Kuweko kwa masoko mashambani kunathibitisha kuweko kwa mazao ya ziada kati ya wakulima.

Miji na jamii ya mijini

Upanukaji mkubwa wa biashara uliwezesha ustawi wa ustaarabu halisi wa mijini katika sehemu ya Sahel ya Sudan. Miji ilikuwa na sehemu ya kati ambayo ilikuwa na nyumba za mawe zilizojengwa kwa mtindo wa Kisudan, sehemu iliyotengwa kwa soko na nyingine iliyotengewa msikiti; ambapo viungani kulikuwa na mahema na vibanda vya nyasi kwa ajili ya wakazi wa muda mfupi.

Miji mitatu inajitokeza: Timbuktu, Jenne na Gao. Timbuktu, ambao ulitekwa na Sonni Ali Ber katika mwaka wa 1468, ulikuwa ndiwo lulu ya Sudan katika karne ya kumi na sita, kama mji wa wasomi na watawa na pia kama mji mkuu wa uchumi. Jenne, ambao kidini na kiuchumi, uliunganishwa na Timbuktu, ulijulikana zaidi kwa msikiti wake ambao ulikuwa mojawapo ya johari za

Sudan ya mashariki. Pia ulikuwa ndio kituo kikuu cha uhusiano na ulimwengu mpana wa nyika na misitu. Gao, makao makuu ya kisiasa, ulikuwa na wakazi zaidi (100,000) na ulihusiana sana na Sudan ya kati, Libya na Misri.

Katika miji hii Kisonghai ndiyo iliyokuwa lugha kuu ya wakazi wa mijini hali Kiarabu kilikuwa lugha ya wasomi. Kigezo cha kuzitenganisha jamii kitabaka kilikuwa zaidi ni uchumi, kigezo hiki kiliwahusu wote — wanasiasa, wafanyabiashara, mafundi na wasomi (wote, waalimu na wanafunzi). Ustaarabu uliotokana na mchanganyiko wa jamii pamoja na utajiri ulijitokeza katika ulegelege wa uadilifu katika koo bora na uongezekaji wa idadi ya malaya. Tofauti baina ya jamii ndogo ya mijini na jamii kubwa nchini iliendelea kuongezeka.

Maendeleo ya kidini na kisomi

Maisha ya Kidini

Uislamu ulienea kwa namna mbalimbali kutengemeana na sehemu lakini haukushika sana au kwa vingi katika kipindi hiki. Katika sehemu za mijini kundi dogo la waliopendelewa liliuchukua Uislamu na kutokea kuwa wasomi wa dini hiyo wenye heshima na sifa katika ulimwengu wa wakati huo. Hawa walifadhiliwa na ukarimu wa watawala kama vile Askia Muhammad, mwanzilishi wa ufalme huo. Hata hivyo watu wengi waliendelea na imani zao za kijadi.

Wasonghai waliabudu mizimu waliyoita *hole*, na pia mizimu ya kimaumbile iliyohitaji kutulizwa. Mizimu miwili iliyokuwa muhimu zaidi ni mizimu wa mto au Harake Dikko na mizimu wa radi au Dongo. Wasonianke, makuhani waponyaji ambao walifikiriwa kuwa wa asili ya nasaba ya Sunni, walikuwa bado wanaheshimiwa sana, na ndio walioilinda jamii dhidi ya pepo wabaya na wachawi au *tierkei*. Matambiko ya wafu yalidumishwa na machifu wa kila ukoo. Kwa hivyo Uislamu kwa watu weusi ulilazimika kujirekebisha na kuvumilia imani zilizokuwepo ili uenee.

Uislamu ulikuwa ni dini ya watawala na wakazi wa mijini, na ulisaidiwa na watawala kama Askia Muhammad ambaye kwa kuzingatia ushauri wa madakatari, Al-Maghili wa Tuwat, na Al-Suyuti wa Kairo aliharibu "hirizi" na kuwaangamiza wafuasi wa Sonni. Alilazimisha kufuatwa kwa madhehebu ya Maliki na kupigana vita vya jihadi dhidi ya wafuasi wa dini za kijadi za upande wa kusini, hasa Wamossi. Wafanyabiashara, kwa kutumia mbinu zao, waliueneza Uislamu mpaka ndani ya misitu.

Kwa njia hizi Uislamu uliingizwa katika mazingira ya mamlaka mijini.

Kutokana na hali hii Timbuktu ikawa kielezo kwa misikiti yake mikubwa mitatu, yaani Jingereber, Sidi Yahya na Sankore, na, pia, kwa umaarufu wa madaktari na watakatifu wake (hasa Sharif Sidi Yahya, ambaye alikufa mwaka wa 1464; na Kadhi Mahmud). Timbuktu ukawa jiji takatifu la Sudan.

Maisha Kisomi

Wasomi wa Kisudan waliosomea katika vyuo vikuu vya Karawiyyin katika Fez na al-Azhar mjini Kairo walikuwa huru na kwa jitihada zao walifikia kilele cha usomi wa Kiislamu. Kuweko kwa mali ya ziada katika uchumi kulisaidia ustawishaji wa tabaka la wasomi walioshikilia ibada na uanazuoni. Hali hii vilevile iliwavutia wanazuoni kutoka Sudan, Afrika ya Kaskazini na hata Mashariki ya Kati. Vitabu viwili vya Tarehe vilivyotolewa na wasomi wa Songhai vinadhihirisha kiwango kilichofikiwa na vyuo hivi ambavyo havikuwa vimeandaliwa kwa kanuni kali kama vile vya Afrika ya Kaskazini. Vilikuwa vyuo huru na pia misikiti huria.

Katika karne ya kumi na sita Timbuktu ilikuwa na shule za Kurani 180 zenye maelfu ya wanafunzi kutoka kila mahali. Waalimu ambao hawakulipwa, lakini waliokidhiwa kila hitaji, walifanya kazi usiku na mehana. Elimu ilikuwa katika viwango viwili, kile cha shule ya Kuran kilichozingatia ukariri wa matini na kile cha "madrasa" na chuo kikuu ambacho kilizingatia ufafanuzi na ubunifu wa maandishi. Hapa, kama ilivyokuwa kwingineko, elimu ya Kiislamu ya kijamii ilikuwa na masomo kama haya: elimu ya teolojia (*tawhidi*), elimu ya tafsiri, elimu ya mapokeo (*hadith*) elimu ya sharia (*fikh*), sarufi, ufasaha, mantiki, astrolojia, unajimu, historia na jiografia. Uzingativu mwingi wa sharia za Kimaliki, na utaratibu wa kufafanua matini kwa ufupi kwa kuzingatia mbinu za usomi za Wanasharia wa Kisudan haukutoa nafasi kubwa ya kuzingatia masomo ya sayansi.

Kati ya waalimu mashuhuri wa karne ya kumi na tano ni lazima kuwataja Shaykh Sidi Yahya na Muhammad Al-Kabari (kutoka Kabara). Katika karne ya kumi na sita, familia mbili kubwa za Kiberiberi zilitoa wengi wa wasomi, yaani akina Akits na akina Anda Ag Muhammad. Kati ya hawa alikuwepo msomi mashuhuri Abbas Ahmad Baba ambaye alisifika katika ulimwengu wa Kiislamu wote hata Mashariki. Hata hivyo alimnukuu na kumheshimu mwalimu wake mwenye sifa, Baghayogho, kutoka Jenne.

Juhudi hii ya kisomi na kiimani haifai kupuuzwa. Hata hivyo, kwa kuwa iliwahusu wasomi wachache huko mijini, na kwa kuwa iliandikwa kwa lugha ambayo haikutilia maanani lugha na tamaduni asili za wenyeji, ilibakia kandoni mwa jamii, na kwa hivyo ikaporomoka pamoja na miji ambamo ilistawi.



Watu na Falme za pindi ya Mto Niger na Bonde la Volta kutoka karne ya 12 hadi ya 16

Wamossi wa pindi ya mto Niger

Kwa sababu mbili muhimu katika pindi ya mto Niger tutashughulikia jamii za Wamamprusi, Wadagomba na falme za Wamossi. Sababu ya kwanza ni kuwa katika sehemu hii jamii hizi zinajulikana zaidi kuliko jamii nyingine kama vile ya Wagurma ambazo hazikuwa na utawala wa serikali moja kuu. Sababu ya pili ni kuwa tatizo la kuitambua jamii ya Wamossi, ambayo imerejewa na maandishi ya *Tarikh al-Sudan* na yale ya *Tarikh al-fattash*, hujitokeza na, hivyo, kuwa uanishaji ufaao wa mpangilio wa kihistoria wa eneo hili lote hutegemea utatuzi wa tatizo hili.

Maandishi ya *Tarikh al-fattash* huelezea juu ya mashambulio dhidi ya ufalme wa Wasonghai, mnamo katikati ya karne ya 13, wakati wa *Za Baray* ambaye anahusianishwa na *Za Beirafoloko*. Ilikuwa ni katika utawala wa mrithi wake, *Za Asibay*, ambapo ufalme wa Wagao ulitwaliwa na Mali ambayo wakati huo, ilitawaliwa na Mansa Wali (1260-1277).

Maandishi haya hutumia tamko la "*Mossi Koy*" kwa maana ya chifu au mfalme wa Wamossi.

Haya hayakuwa makundi ya wachafuzi, bali vikosi vya jamii za kijeshi zenye utaratibu na ambazo zilikuwa tayari kukabilia na tawala kuu zilizomiliki Pindi la into Niger. Ukweli kuwa mji wa Timbuktu ulikuwa mojawapo ya malengo yao waonyesha hamu ya Wamossi kuisimamia biashara ya Afrika ya Magharibi.

Kufuatana na maandishi ya *Tarikh al-Sudan* ilikuwa ni katika utawala wa mmojawapo wa warithi wa Mansa Kanku Musa (1312-37), ambapo Wamossi waliingia kwa ghafla katika schemu hii: "Sultani wa Wamossi aliingia mjini, akauteka, akautia moto, akauangamiza, na baada ya kuua kila aliyemshika na kutcka mali yote aliyoweza kuipata, alirudi nchini kwake."

Pengine, matukio haya yalitokea katika miaka iliyofuata kifo cha Kanku Musa, yaani karne moja baada ya mashambulizi yaliyoitajwa na maandishi ya *Tarik al-fattash*. Tukio hili laonyesha kuweco kwa utawala thabiti na wenye

uwezo wa kuandaa mashambulizi kama haya katika umbali mkubwa na kwa kipindi kirefu. Maandishi ya *Tarikh al-Sudan* yamerekodi shambulio la tatu la Wamossi dhidi ya Wabenka muda mfupi kabla ya mwaka wa 1433.

Ama kuhusu utawala wa Sonni Ali tunazo taarifa zifuatazo za kurejea. Katika kipindi cha 1464-5 mfalme Komdao wa Wamossi alishindwa vita na Sonni Ali ambaye aliongoza shambulio dhidi ya nchi ya Wamossi katika miaka ya 1471-2. Katika miaka ya 1477-8 Wamossi waliingia katika nchi ya Wasonghai ambamo walikaa kwa muda wa miaka minne, baada ya kuiteka miji ya Sama na Walata. Mwishoni mwa shambulizi hili Wamossi walizingirwa, wakashindwa na kusakwa na Wasonghai walioitaka “*smala*” ya mfalme na ngawira.

Ni jambo gani ambalo lilitokea baina ya katikati ya karne ya kumi na nne, wakati wa shambulizi dhidi ya Wabenka, na katikati ya karne iliyofuata, ambapo paonekane kama kilele cha uenezaji wa milki ya Wamossi hadi kufikia Walata? Jambo lililodhahiri ni kuwa kwa Sunni Ali adui mkubwa alikuwa ni Wamossi aliopigana nao vita vikali vilivyoendelezwa na warithi wake.

Askiya Muhammed (1493-1529) aligeuza vita vya Wasonghai dhidi ya Wamossi kuwa jihadi, kwa sababu Wamossi walifuata dini za kijadi, kama wakazi wa Gurma. Majeshi ya Wasonghai yalivishinda vita dhidi ya Sultani Naasira na kuteka kina mama wengi na watoto wao.

Wakati wa shambulio la pili lililoongozwa na Askiya Dawud (1549-82), chifu wa Wamossi na majeshi yake, aliihama nchi. Shambulio jingine laonekana kama liliangukia patupu kwa sababu majeshi ya Wasonghai yalirudi bila kuteka chochote.

Hivyo kwa kipindi cha karne tatu, jamii shindi ya kijeshi ilipigana dhidi ya Wasonghai kwa nia ya kusimamia mto Niger, baada ya kulimiliki pindi la mto Niger. Mwishowe Wamossi walishindwa. Baada ya utawala wa Muhammad, uhasama wa kisiasa ulitiliwa nguvu na uhasama wa kidini.

Wamossi wanaozungumziwa na maandishi ya *Tarikh* walikuwa watu wa aina gani? Kwa sababu ya ukosefu wa mapokeo simulizi juu yao, ni lazima tutegemeee ushahidi utokanao na ufukuzi wa kiakiolojia.

Kufuatana na Boubou Hama, ambaye anayanukuu maandishi ya Kiarabu yaliyoandikwa na Uld Audar (bila shaka maandishi ya *Tarikh* ya Say), Wamossi waliotoka mashariki, waliunda dola yao ya kwanza katika upande wa kushoto wa mto Niger na kuita Dyamare. Mji mkuu wa dola hiyo uliitwa Rozi. Baada ya karne tano (ya nane hadi ya kumi na mbili), kutokana na shinikizo la Waberiberi, Wamossi walihamia Minji, ambao ulikuwa mji mkuu wa dola yao ya pili au Dyamare ya pili. Mara baada ya kuhamia Minji waliondoka wakavuka mto na kuanzisha dola yao ya tatu, yaani Dyamare ya tatu, baada ya

kuzishinda jamii za wenyeji wa sehemu ile, yaani Wakurumba na Wagurmank-yeba.

Kufuatana na Al-Umari, mfalme wa Wamali, Mansa Musa, alipokuwa akizungumza na watu mashuhuri wa Kairo alinukuliwa akisema, "Tunaye adui mgumu ambaye, kati ya watu weusi, yeye kwetu ni kama walivyo Watartar kwenu. Wao ni hodari kwa kupiga mishale na wanao farasi waliohasiwa wenye pua zilizopasuliwa." Pengine hawa walikuwa wapanda farasi kutoka sehemu za kaskazini mwa nchi ya Wamossi.

Mfanyabiashara wa Kigenoa, Antonio Malfante, ambaye aliitembelea Towat katika mwaka wa 1447, anazungumzia juu ya kuzingirwa kwa Vallo (pengine Walata) na mfalme mshirikina, akiwa na watu elfu mia tano. Kwa mujibu wa Yves Person, huyu huenda akawa ndiye mfalme wa Wamossi wa Kaskazini. La mwisho, katika maandishi yake ya *Decadias da Asia* (1553), Joao de Barros, anazungumzia juu ya Wamossi waliotajwa na mwana mfalme Bemoy wa Wawolof mnamo mwaka wa 1488 alipozuru nchi ya Ureno. Kufuatana na Barros, nchi ya Wamossi ilienea upande wa mashariki kutoka Tinibuku. Mfalme wa Ureno alifurahishwa na habari hizi na kumtambua mfalme wa Wamossi kuwa ndiye Presta Yohana wa visakale, ambaye alidhani alikuwa akipigana dhidi ya uongozi wa Kiislamu wa Mansa wa Mande.

Alipokuwa akikusanya mapokeo simulizi, Claude Meillassoux aligundua msitari wa visima baina ya Nyamina na Nara (katika Jamhuri ya Mali) ambavyo vyasemekana kuwa vilichimbwa na Wamossi. Wamossi wanasemekana kuwa waliwashinda Wasumare lakini koo za Wajariso (Dyariso) zilikabiliana na Wamossi na kuwashinda. Katika Hodh, Wamossi wanasemekana kuwa waliunda kikosi eha jimbo kiliehokuwa na makao yake katika Gara, na kuwavamia Daole-Gilbe karibu na Kumbi Saleh.

Wamossi wa pindi la mto Niger na bonde la Volta-tasnifu rasmi

Waandishi wa kale zaidi waliuweka uhabuzi wao juu ya mapokeo simulizi ambayo hudai kuwa tawala zote za kifalme za Wamossi, zilitokana na mzazi mmoja, Naaba Wedraogo, na kuonyesha uhusiano wazi baina ya chanzo cha falme za Wamossi na zile za Wamaprusi-Wanamumba-Wadagomba.

Katika masimulizi ya kisasa ya Wamossi, hakuna maelezo ya mashambulio dhidi ya Wasonghai. Hata hivyo, kutokana na maandishi ya *Tarikh*, wataalamu, Delafosse, Probenius na Tauxier, wanafahamu sana kuweco kwa Wamossi wa kaskazini tangu kale katika nchi za ndani ya delta ya Mto Niger na hata nje ya delta yenyewe. Kwa kutumia vidokezo vyovyote vile, kwa mfano, kufanana kwa Naasira inayozungumziwa katika maandishi ya *Tarikh* na jina la mtawala wa

Yatenga, waandishi wa kwanza wa historia ya Wamossi waliwaunganisha Wamossi wa pindi la mto Niger na wale wa mto Volta Mweupe. Kwa njia hii waandishi hawa wakaipa historia ya falme za kisasa za Wamossi kina kirefu zaidi kuliko inavyodhihirishwa na uchambuzi wa mapokeo simulizi ya Wamossi na pia kuliko matukio ya kihistoria ya majirani wao. Tasnifu hii inadokeza nadharia tete ifuatayo: kuwa Wamossi walikuwa tayari tu kuanzisha mashambulizi makubwa ya kijeshi baada ya kufaulu kuwatala wenyeji wa sehemu ya Volta. Kwa hivyo matendo yaliyorekodiwa katika *Tarikh* ni lazima yafikiwiwe kuwa yalitokea katika historia ya baadaye lakini yakasukumwa nyuma katika nyakati za kale, ambazo zimewekwa na Delafosse katika karne ya kumi. Nadharia tete hii yaweza kutetewa tu ikiwa vipindi vya tawala za wafalme vielezwavyo katika masimulizi vitarefushwa zaidi ama ikiwa itafikiwiwa kuwa orodha ya watawala haikukamilika.

Katika mwaka wa 1907 Kapteni Lambert alikosoia uainishaji wa Wamossi wa siku hizi na Wamossi wa maandishi ya *Tarikh*. Hata hivyo utafiti wake haukuchapishwa na hii ndiyo sababu iliyofanya ukosoaji mkali wa John Fage dhidi ya tasnifu ya Delafosse uonekane kama ufasiri mpya kabisa wa historia ya Wamossi. Yeye aliwatenganisha kabisa Wamossi wa pindi la mto Niger na wale wa bonde la Volta japo hakuondoa kabisa uwezekano wa uhusiano baina yao. Uamuzi wake huu ulimfanya kuiweka tarehe ya chanzo cha falme za siku hizi kuwa ya karibuni zaidi. Kwa mfano, anaitaja tarehe ya mwanzilishi wa ufalme wa Wadagomba kuwa kama mwaka wa 1480. Kulingana na John Fage ni lazima Wamossi wa Kaskazini wawe walianza kujitokeza kabla ya kuweko kwa mfumo wa dola. Naye Nehemia Levtzion, akitumia ulinganishi wa jinsi madola ya bonde la Volta yalivyokua, anafikia hatima hiyohiyo, baina ya miaka ya 1380 na 1480. Michel Izard alichambua historia ya vizazi vya Wamossi ili kulinganisha falme za kisasa hasa za Wagadugu na Yangenga. Alianza kwa kuitambua tarehe muhimu ya kuanzishwa kwa Yatenga kuwa mwaka 1540. Kutoka hapa alirudi nyuma hadi mfalme wa kwanza wa Wagadugu, Naaba Wubri, mnamo mwaka 1495. Akirejea nyuma zaidi, aliuweka wakati wa mtawala wa kwanza wa nasaba hii (Na Bawa) kati ya miaka ya 1375 na 1420.

Chanzo cha tawala za bonde la Volta: hali ya sasa ya maarifa yetu kuhusu kipindi hicho

Kizazi cha Wamossi wa kale wa Dyamare ya pili (Minji) kiliuvuka mto katika sehemu ya Say mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tatu na kuanzisha Dyamare ya tatu katika pindi la mto Gurma. Kuanzia wakati huo hadi kufikia

mwaka wa 1575 kulikuwa na majaribio mengi ya kuuchukua usimamizi wa utajiri wa njia za kupitishia biashara ya kuvuka jangwa la Sahara. Hata hivyo sehemu hii ilikuwa tayari imetwaliwa na himaya mbili kubwa katika Sudan, yaani za Mali na Gao.


Je, kuna uhusiano baina ya kizazi hiki cha Wamossi wa kale wa Kaskazini na ufalme wa Maprusi, ambao ulizalisha Wananumba na Wadagomba, Wamossi wa siku hizi na milki ya sasa ya Nungu (Fada Ngurma)? Jambo lililokuwa likitokea hasa lilikuwa ni hali ya ueneaji wa utaratibu fulani wa kisiasa kutoka Bornu hadi mfalme Bawa wa Wamaprusi kupitia nehi ya Wahausa ya Zamfara.

Kufuatana na masimulizi yaliyorekodiwa na E. Tamakloe, Tohajiye, aliyeitwa mwindaji mwekundu, na baadaye mwanawe Kpogonumbo, walikuwa washirika wa mfalme wa Wamali. Baadaye Kpogonumbo aliondoka kuelekea magharibi hadi Gurma ambapo mwishoni alimuoa Soyini, mmojawapo wa mabinti za mfalme. Huyu ndiye aliyemzaa mfalme wa baadaye, Na Bawa (Gbewe) wa Wamaprusi ambaye alijulikana na Wadagomba na Wamossi kama Na Nedega aliyekaa Pusuga, alipoimarisha mamlaka yake kwa kupigana dhidi ya Wakusasi na Wabisa. Mwanzoni mwana mkubwa wa Na Bawa, Zirili, alizuiliwa kuuchukua ufalme na babake lakini hatimaye aliuchukua baada ya kumuua ndugu yake na pia kumuondoa dadake aliyekuwa amekabidhiwa uongozi badala yake. Zirili aliupanga upya utawala wa Maprusi. Baada ya kifo chake, ndugu zake wadogo watatu waliuchukua uongozi wa falme tatu za kisasa za Maprusi, Namumba na Dagomba.

Kuna aina nyingi za masimulizi haya ya jumla. Lakini, kama kuna uhusiano baina ya Wamossi wa pindi la mto Niger na wazazi wa Wamaprusi ni lazima uwe ulianzia katika wakati wa Dyamare ya pili (katika sehemu ya ukingo wa Wahausa wa mto Niger) na Dyamare ya tatu (katika sehemu ya ukingo wa Wagurma). Pengine ni katika nyakati hizo ambapo vikosi vya mashujaa mamluki viliondoka na kuhamia sehemu za Pusuga.

Ushirikiano na Wamali, ambao umetajwa katika mojawapo ya masimulizi yaliyogusiwa hapo juu, unahusu Wamali wa upande wa mashariki ambao wanazungumziwa na Wamossi wa Yatenga na ambako ndiko kulikokuwa na nchi ya chanzo ya Wakurumba wa Lurum; ushirikiano huo hauwahusu Wamossi wa Magharibi wanaozungumziwa katika maandishi ya *Tarikh*.

Kutokana na uhusiano baina ya Yenenga na mwanamfalme Ryale alizaliwa Naaba Wedraogo ("farasi dume") ambaye ndiye alitokea kuwa mzazi wa Wamossi wote. Lakini Ryale alikuwa baba mzazi tu. Asili halisi ya Wedraogo, kijamii na kisiasa, ilitokana na Yenenga na nyuma zaidi ilitokana na babu yake



9.1 Kuaruba ya Niger na Bonde la Volta, 1100-1600.

Chanzo M. Izard in 'Introduction à l'Histoire des Royaumes Mossi' (tasnifu, Chuo Kikuu cha Paris, 1970)

wa upande wa mama, Na Nedega ambaye alimchagua kusimamia kikosi cha wapiganaji. Haya yalitokea katika karne ya kumi na tano.

Kwa hakika utawala wa Wagurma ulikuwa tayari upo, ingawa siyo kama serikali kuu moja, bali kama serikali ya muungano wa tawala mbali mbali za machifu ambazo zilikuwa huru kiasi. Maandishi ya *tarihi* hutaja mashambulizi ya watawala wa Wasonghai dhidi ya wafuasi wa dini ya kijadi ya Wagurma. Ibn al-Mukhtar, mjukuu wa Mahmud Karti, hata anasimulia juu ya kuingia kwa Askia Ishak katika Bilanga, makao makuu ya mfalme wa Gurma. Nayo mapokeo yanayokubalika zaidi ya Wamossi yanasema kuwa *Nunbado* (mfalme wa Nungu) wa kwanza, Dyaba, mzazi wa Wa-lompo, alikuwa mwana wa Naaba Wedraogo. Mapokeo mengine yasiyo ya kiitikadi mno yanasema kuwa Dyaba alikuwa mwana wa Na Nedega lakini Gurma kwenyewe, mfalme wa kwanza wa Nungu alishuka kutoka mbinguni.

Mwanzo wa historia ya falme za Wamossi

Katika karne ya kumi na sita, vizazi vya Naaba Wedraogo vilianzisha mamlaka yao juu ya watu wa bonde la Volta Nyeupe na katika upande wa magharibi wakavuka Volta Nyekundu. Katika bonde la Volta Nyeusi, Boromo ulikuwa ndio mwisho wa usambaaji huu wa mamlaka yao.

Ingawa mapokeo ya Tenkudugo yamegubika baadhi ya mapokeo ya zamani zaidi, haya yalikusanywa na Junzo Kawada mnamo mwaka wa 1971 na yanaonyesha mchango wa Pusuga katika ukuaji wa poleple wa kisiasa kabla ya ushindi. Kuanzia hapo ufalme wa Mamprusi ulijitokeza pamoja na tawala za machifu za Durtenga na Komin-yanga ambazo machifu wake walikuwa wa Gurmankyeba.

Vivyo hivyo, inasemekana kuwa kutokana na Zambarga, tawala za machifu za Wargay, Largay na Tenoagen ziliibuka, na Tenkudugo ilijitenga kutokana na Tenoagen.

Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tano watu wawili mashuhuri Naaba Rawa na Naaba Zungrana, walimfuata Naaba Wedraogo, na walidhaniwa kuwa walikuwa wanawe.

Naaba Rawa, ambaye wanamuziki ya Yatenga humwita chifu wa Po (Pugo), Zondoma, Sanga n.k, ndiye hasa aliyeanzisha utawala uliosambaa kaskazini-magharibi mwa nchi ya Wamossi na ambao ulilitumia jina lake (yaani Rawatenga au nchi ya Rawa). Utawala huu ulikuwa ni mkusanyiko wa tawala za machifu, ambazo zilisambaa katika sehemu kubwa ya milki. Lakini utawala huu haukuwa na udhibiti wala mshikamano wa haja, hivyo utii wa makabila ya wenyeji haukuwa thabiti, na utawala ukasambaratika.

Naaba Rawa alimalizia ushindi wake katika nyika ya Gondo alipowatimua Wadogon kutoka Yatenga na kuwaelekeza kwenye majabali ya Bandiagara. Mshindi (Naaba Rawa) aliunda vikosi vingi wilayani vilivyosimaniwa na watu wa familia yake. Lakini sehemu ya utawala wake ambayo ilibakia kama utawala halisi ilikuwa ufalme wa Zondoma ambao kwa sasa ni kijiji kimoja tu ambao mna kaburi la Naaba Rawa.

Ukweli ni kwaniba utawala wa Yatenga ulipanuka katika karne ya kumi na sita, kwa kujimegea maeneo ya ufalme wa Zondoma. Jina la Naaba Zungrana, ambaye hajulikani sana, linahusishwa na falme ndogo za Ratenga na Zitenga, kusini mashariki ya Yatenga.

Katika kipindi hicho kulikuwa na mikondo mitano ya Wamossi walioingia katika sehemu ya kati ya bonde la Volta Nyeupe huku wakianzisha tawala za machifu kila upande: kwa mfano, magharibi, katika sehemu za Kombisiri na Manga; katika sehemu za Kugupela (Koupela); kingoni mwa ziwa Bani (Ratenga na Zitenga); sehemu ya Bulsa, na Naaba Gigma; na sehemu muhimu ya Wubritenga, mji ulioanzishwa na Naaba Wubri, mwana wa Naaba Zungrana. Watu wawili wanajitokeza katika kipindi hiki, nao ni Naaba Gigma na Naaba Wubri. Naaba Gigma aliongoza upanuzi wa utawala kuelekea pande za mashariki na kaskazini hadi kufikia mipaka ya sasa ya Liptako. Wakati huo sehemu kubwa ya utawala huu ilipakana na nchi ya Wagurma waliokuwa na utawala ulioandaliwa vya kutosha kukabiliana na Wamossi. Naaba Wubri, aliyeanzisha ufalme wa Wagadugu ambapo mtawala huitwa *Moogo Naaba*, Chifu wa Mossi (nchi iliyofikiwa kuwa ndiyo ulimwengu) aliishi katika miaka ya mwanzo ya karne ya kumi na sita.

Kutoka sehemu ya Zinyare (jina la mwanzo la Wubritenga) Naaba Wubri aliisambaza manilaka yake kuelekea mashariki na kaskazini-mashariki huku akianzisha tawala za machifu kama vile Lay, Yako na mwishowe Kudugo ambako alifariki. Mwili wake ulizikwa Gilougu na Lumbila. Warithi wake waliendeleza kazi yake kwa kuusanbaza utawala wa Wamossi upande wa magharibi.

Baadhi ya vizazi vyake walielekea upande wa Yatenga, kwa mfano, Naaba Wumtane, mwanzilishi wa ufalme wa Giti ambao uliendeleza mapambano dhidi ya Wadogon na kuwafanya wahunzi kuwa watumwa wao. Kutawazwa kwa Naaba Kudumye, mjukuu wa Naaba Wubri, kulipatana na kuondoka kwa Naabu Yadega, mjukuu mwingine wa Naabu Wubri, kuelekea Gursi. Wanamfalme hawa wawili walikuwa wanawania ufalme wa Wagadugu.

Baada ya kushindwa na mpinzani wake, Naaba Yadega aliondoka akiandamana na dada yake mkubwa, Pabre, ambaye alimwibia (Naaba Yadega)

nembo za kifalme zilizokuwa zimewekwa chini ya usimamizi wake (Pabre). Maoni yetu ni kuwa haya yalitokea kama mwaka wa 1540.

Naaba Kudumye alitoa mchango mkubwa katika kuziandaa tawala za siku hizi za Konkistenga, Yako, Tcma, Mane na Busuma. Pia aliweza kuingia ndani ya nchi ya Gurunsi, hata ingawa ilikuwa kwa muda mfupi. Naaba Kuda, mwanawe Naaba Kumdumye, aliipa sehemu ya kati ya nchi ya Wamossi umbo lililodumu kwa karne nyingi.

Katika Gursi, Naaba Yadega, alianzisha mfululizo wa vituo vya kivita chini ya uongozi wa Wamossi, ambapo kituo kikuu kilikuwa kile cha ufalme wa Zondoma. Kutoka Gursi hadi mipaka ya nchi ya San (Samo) Naaba Yadega aliimarisha mamlaka yake kwa haraja ya babake mlezi, Naaba Swida. Mwishowe aliishi mjini Lago. Wakati wa utawala wa mwanawe wa pili, Naaba Geda (mwishoni mwa karne ya kumi na sita), ufalme mpya wa Yatenga ulivunja uhusiano wake wote na ufalme wa Wagadugu. Kuanzia hapo hizi zilikuwa dola mbili kuu za utawala wa Wamossi.

Awamu tatu muhimu zinajitokeza katika historia ya Wamossi: awamu ya kujitayarisha (nusu ya pili ya karne ya kumi na tano); awamu ya ushindi (nusu ya kwanza ya karne ya kumi na sita); na mwisho awamu ya uimarishaji (nusu ya pili ya karne ya kumi na sita).

Mfumo wa siasa ya Wamossi

Jambo la msingi hapa ni kule kutafautisha baina ya wale waliomiliki ardhi (*tengsobondo*) na wale ambao walishikilia mamlaka (*naam*) ya utawala. Waliomiliki ardhi (wana wa nchi) walikuwa ni wenyeji wenyewe. Wenye mamlaka ya utawala, kwa kawaida, walikuwa Wamossi lakimi neno hili (*naam*) liliishia kumaanisha wote waliosimilishwa mathalan, mateka wa mfalme waliopewa madaraka. Kwa hivyo sambamba na naaba aliyeshikilia mamlaka ya kisiasa, kulikuweco na *tengsoba* (bwana wa ardhi). Uwili huu ulijitokeza pia katika itikadi ya kidini kwa sababu *tengsoba* walihusishwa na ibada ya mungu-mke wa ardhi, ilihali machifu walimwabudu mungu wa jua (naaba Wende). Muungano wa hawa wawili ndio uliodhibiti umoja wa nchi.

Wenyeji wanaweza kuwekwa katika makundi matatu makubwa. La kwanza ni lile la wale wanaojiita kundi la Wagurunsi, kundi la watu wanaoongea lugha za Kivolta au Kigur ambalo laweza kuwa ni pamoja na Wakurumba (Fulse); Kundi la pili ni lile la Wadogon ambao walidhulumiwa sana; kundi la tatu ni la Wasan (Wasamo) na Wabisa ambao sasa wanaishi katika nchi tofauti.

Wenyeji ndio waliokuwa na jukumu la kufanya ibada ya uzazi ya kila mwaka. Ilikuwa tu baada ya kafara maalum katika madhabahu ya ardhi

ambapo mfalme mpya aliyechaguliwa (akiitwa naaba tu) angeweza kutawazwa na kupewa cheo cha *rima* kilichomruhusu kuzikwa katika makaburi ya kifalme na mwanawe kuchukua uongozi baada yake.

Katika Yatenga walioshikilia mamlaka ya ufalme wanaweza kuwekwa katika makundi matatu: watu wa nyumba ya mfalme (*niyiridemba*), wakuu wa vita (*tasobanamba*); na watu wa ukoo wa kifalme (*nakombse*). Makundi mawili ya kwanza yalijumlisha Wamossi au mateka wa mfalme au watu wenye hadhi waliotokana na familia kuu za kabla ya Watenga. Hawa ndio waliokuwa watu wa karibu sana na mfalme. Hata hivyo mfalme aliwashuku Wanakombse ambao walikuwa karibu sana naye kwa damu.

Katika kila makao manne ya mfalme kulikuwa na makundi manne ya watumishi na kila kundi liliongozwa na mheshimiwa. Makundi haya yalikuwa ni: *watogo naaba*, *wabalum naaba*, *waweranga naaba* na *warasam naaba*. Waheshimiwa waliowaongoza waliitwa nesomba. Hawa walikuwa na majukumu mawili: kwa upande mmoja walifanya kazi za serikali kuu chini ya amri za mfalme, na kwa upande wa pili baada ya kifo cha mfalme, walifanya baraza la ya uchaguzi. Baada ya muda utaratibu wa urithi kutoka ndugu hadi mwingine uliingiliana na utaratibu ambamo ndugu mkubwa kati ya wana wa mfalme mmoja angedai uongozi. Kwa sababu ya ukosefu wa utaratibu madhubuti, mara nyingi, ugomvi uliotokea baina ya makundi yaliyopingana ulileta vita vya wenyewe kwa wenyewe, licha ya kuweko ulundikaji wa mamlaka zaidi mikononi mwa mfalme, jambo ambalo lilipunguza uwezo wa wale waliowania ufalme.

Hata hivyo umoja ulipatikana kutokana na lugha moja, na kutokana na kuukubali utaratibu wa utawala kiutamaduni, kijamii na kisiasa.

Watu wasiokuwa na mifumo unganifuserikali kuu

Utawala wa jamii za aina hiyo kwa kawaida haujihusishi na mapokeo ya kina kuhusu watawala na enzi zao na matendo yao. Hii ndiyo sababu inayowafanya watu kama hao kutokuwa na historia yenye kina kirefu hata ingawa wamekuwepo kwa muda mrefu zaidi. Kwa hivyo ni machache sana yanayojulikana juu ya watu kama hao baina ya 1200 na 1600.

Lugha za Kigur zimechambuliwa na wataalam wengi, kama vile, Gabries Manessy, De Lavergne de Tressan, Westermann na Bryan, Greenberg na Kohler kati ya wengine. Uanishaji wao wa lugha hizi pamoja na vigezo vya misingi yake vinahitilafiana, hata bila kutaja matatizo ya uhusiano wa lugha hizo kinasaba, ambao una utata mwingi zaidi. Kwa muhtasari tunaweza kutafautisha (1) kundi kubwa la Wamossi linaloundwa na makundi madogo matatu ya Wamossi (Moore), Wadagomba na Wa-Birifor-Dagari-Wile,

(2) kundi la Wagurunsi (yaani Mashariki, Magharibi na Kaskazini), (3) kundi la Wagurma.

Mahusiano haya ya kitamaduni hayamaanishi ulinganifu wa utaratibu wa kijamii na kisiasa kati ya watu wenye serikali kuu moja wanaopakana na wengine wanaozungumza lugha zenye uhusiano na yao, bali waliosambaa zaidi na wenye mifumo ya kijamii inayojitawala yenyewe. Hii ndiyo hali ya Wamossi na Wadagari. Hata hivyo inaonekana kuwa idadi ya lahaja za lugha moja hubadilika kulingana na kiwango cha ukiritimba wa mamlaka ya serikali kuu.

Swali muhimu linalojitokeza ni hili: Ni upande gani maendeleo ya kitamaduni yalielekea? Je washindi waliwalazimisha washinde kuitumia lugha yao? Ama hawa walisimilishwa kitamaduni kama ilivyotokea mahali kwingine? Lakini katika kiwango hiki ni lazima ieleweke kuwa maeneo ya kitamaduni na yale ya kilugha hayaandamani moja kwa moja. Kwa mfano, Wabwa huzungumza lugha ya Kigur lakini utamaduni wao ni wa Kimande kama majirani zao Wabobo wanaozungumza lugha ya Kimande.

Kwa kutumia mbinu za kiantropolojia katika kuzitalii jamii za bonde la Volta, Guy Le Moal anatafautisha makundi yafuatayo: Wamossi, Wagurunsi, Wabobo, Wamande na Wasenufo. Anawaweka pamoja chini ya kiekwa kimoja cha habari, watu wa sehemu ya Kusini-Magharibi mwa Burkina Faso ya Leo.

Pamoja na Wamossi, ni lazima wahusishwe Wamossi, watu waliowatangulia Wamossi, kwa mfano Wakurumba, ambao katika ufalme wa Lurum, walikuwa na muundo wa kisiasa wenye sifa za mamlaka kuu ambayo mwanzoni ilijengwa juu ya dhana ya ufalme mtakatifu. Katika Yatenga, Wakurumba (Fulse) walikuwa katika makundi ya "watu wa ardhi", sawa na Wamaranse ambao walikuwa wa asili ya Kisonghai au Wayarse au Wakambosi ambao walikuwa wa asili ya Kimande.

Wagurunsi wamegawanyika katika vijikundi sita vifuatavyo:- Lela, Nuna, Kasena, Sisola, Ko na Puguli. Wanahusishwa na Watalensi, Wakusasi na Wanakansi. Ingawa kitamaduni na kitaifa jamii hizi zilikuwa huru, majirani zao waliwafikiria kuwa tawala zilizokuwa chini ya milki yao. Jamii ya Wabobo huundwa na Wabwa (Bobo-Wule) na Wabobo halisi (Bobo-Fing). Katika jamii hizi, jando iliyohusiana na ibada ya *Wado* ilikuwa ya muhimu sana. Na utaratibu wa kisiasa ulijikita katika jamii huru vijijini.

Wadafing (Wamarka) walisambaa kutoka bonde la Suru kaskazini hadi sehemu ya Bobo-Dyulaso upande wa kusini. Wadafing walikuwa wafanyabiashara na wapiganaji. Walikuwa Waislamu, japo kundi kubwa miongoni mwao walishikilia dini yao ya jadi. Waliunda dola nyingi ndogo ndogo zenye mfumo wa utawala wa serikali kuu moja.

Wakaraboro, Watusya, Waturka, Wagwe na Wawara walikuwa na uhusiano na Wasenufo. Kwa hiyo Watusya walikuwa na jumuiya ya kisiri iliyoitwa *lo*, ambayo ilifanana na *poro* ya Kisenufo. Katika upande wa Kusini-Magharibi Wawile, Wadagari, Wabirifo, Walobi na Wadya waliingia kwa mfululizo kutoka Ghana ya leo, kuanzia karne ya kumi na sita. Wawile, ambao ndio waliowasili kwanza, waliwafukuza Wapuguli. Walifuatwa na Wadagari ambao walikuwa na uhusiano na Wawile lakini ambao asili yao ilikuwa na pande mbili, yenye kufanana na asili ya Wabirifo.

Wawile, Wadagari na Wabirifo walikuwa na lugha ambayo ilitokana na kundi la Kimossi. Jambo moja lililowashirikisha kijamii lilikuwa ni umuhimu wa sherche ya siri ya kuingizwa katika *bagre*. Wabirifo na Wadya walikuwa na uhusiano wa karibu kiutamaduni na Walobi ambao wengi wao walizingatia mfumo wa koo za mama, na kwao sherche ya mpito ya *poro* ilikuwa yenye umuhimu katika udhibiti wa jamii. Jamii hizi zote, kinyume na Wagurunsi, hazikuwa na mifumo ya mamlaka unganifu.

Wafulbe walioishi katika bonde la Volta Nyeusi, bonde la Suru, nyika ya Gondo, Jelgoji na Liptako, waliunda tawala nyingi za kichifu kama vile Barani, Jibo, Barabulle, Tongomayel na baadaye ufalme wa Liptako.

Mwelekeo wa uchumi


Katika nyika, kilimo kilitawaliwa na mtama ambapo katika upande wa kaskazini aina mbalimbali za fonio zilichukua nafasi ya mtama na upande wa kusini mazao ya viazi. Pamba ilikuwa ikilimwa kwa muda mrefu; na wakati wa kuanzishwa kwa falme za kwanza za Wamossi, ufumaji ulikuwa umeenea sana, na kanzu ndefu kutengewa machifu. Inasemekana kuwa mfumaji mmoja alimfumia Naaba Wubri kanzu kama hizo. Wayarse waliotoka Mande walihusishwa na ufumaji. Utiaji rangi, ambao ulikuwa maalum kwa Wasonghai, ulikuwa umeandaliwa vizuri hasa kutokana na miti ya aina ya mnili na pia miti ya aina ya *Anogeissus* au *leicarpus* (mti wa mswaki), ambayo ilitoa rangi ya aina ya khaki.

Ufugaji wa ng'ombe ulikuwa ni kazi ya Wafulbe. Wayatenga waliuza punda kwa Wamossi wa sehemu za kati na za kusini. Sehemu za mashariki zilisifika kwa ubora wa farasi wao wa aina ya *Dongolawi*, ambao waliingizwa mapema zaidi kutoka Misri ya Juu. Jamii tano za farasi zimetambuliwa, nazo zikiwa ni zile za Yatenga, Jelgoji, nchi ya Kurumba, nyika ya Gondo na Barani. Ufuaji wa chuma, ambao ulisaidiwa na wingi wa mawe ya chuma, na pia, viwanda vya ufinyanzi, viliendeshwa kiushirika. Kwa upande wa biashara inaonekana kuwa Wamossi walipofika biashara ilikuwa inaendeshwa na Wayarse; uundaji wa

falme ulisaidia tu katika kuistawisha zaidi.

Ufumaji ulifungamanishwa na maendeleo ya biashara. Wafumaji na wafanyabiashara wa Kiyarse walitumia vipande virefu vya vitambaa vya pamba kama bidhaa za kuuza na pia kama bidhaa za kulipia katika biashara kati ya kaskazini na kusini. Upande wa kaskazini ulileta chumvi ya mawe kutoka jangwa la Sahara na pia samaki waliokaushwa, na mikeka, hali upande wa kusini uliuza zaidi kokwa za kola na dhahabu. Zaidi ya ubadilishanaji wa bidhaa, sarafu ya kulipia ilikuwa ni kauri na vipimo vingine kama vile dhiraa au mkono wa kitambaa cha pamba. Farasi walilipiwa mateka.

Wahunzi wenyewe waliendesha biashara ya bidhaa zilizokamilika (vyombo na zana za vita) au matufe ya chuma. Historia ya makazi inafichua umri wa baadhi ya vituo vya biashara. Lakini katika hali ya ukosefu wa data ya kiakiolojia, mapokeo simulizi, maelezo katika *Tarikh* za Kiafrika, na habari zitokanazo na maandishi ya Wazungu waliosafiri Afrika zimebakia kuwa vyanzo vikuu katika kuijenga upya historia ya bonde la Volta.



Falme na watu wa Chad

Katika karne ya kumi na mbili sehemu kubwa ya eneo la Ziwa Chad ilikuwa chini ya utawala wenye nguvu wa ufalme wa Kanem. Falme nyingine zilizuka lakini wenyeji wengi waliishi katika koo na makabila tofauti. Ufalme wa Kanem, ambao ulijulikana zamani sana na wasafiri na wanajiografia wa Kiarabu, ulikuwa ndio wenye nguvu katika eneo lililokuwa baina ya Wanuba wa bonde la mto Nili na Wakaw-kaw wa Kuruba la mto Niger. Kuna marejeo mengi juu ya himaya hii, ambayo ndiyo itakayokuwa mada kubwa ya sura hii. Hata hivyo ni muhimu kufikiria juu ya makundi mengi ya watu ambayo hayakushughulikiwa na wanaTarehe.

Rejeo kuu la ndani ni *Diwani* ya masultani wa Kanem-Borno, ambayo mwanzo wake inarudi nyuma hadi nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tatu na ambayo iliongezewa taarifa mara kwa mara hadi kufikia mwisho wa utawala wa Wasefuwa, mnamo karne ya kumi na tisa. Katika muswada huu mfupi wenye kurasa kama sita hivi mnapatikana historia ya nasaba ya Kanem-Borno. Pamoja na haya kuna rekodi za Al-Idrisi (1154), Ibn Saidi (kafariki 1286) na Al-Makrizi (kafariki 1442). Rekodi hizi mbili zinachangiana, ambapo Waafrika wanajishughulisha na mambo ya nyakati hali wanajiografia wa Kiarabu wanajishughulisha na mambo yaliyohusiana na jiografia ya eneo hilo.

Nasaba ya Wasefuwa

Wazaghawa walitawala Kanem hadi kufikia mwisho wa karne ya kumi na moja. Nao Wasefuwa walipewa jina hilo kutokana na madai yao kuwa wao walikuwa wa kizazi cha shujaa wa Kiyemeni, Sayf ben Dhi Yazan. Mwanzilishi wa utawala, Hummay (1078-80) yaelekea alikuwa wa kizazi cha familia ya Kiberiberi. Wakati wa Al-Idrisi wakazi wa Kawar walivaa *litham (mulaththamun)*. Madai ya asili ya Kiyemeni – yanaeleweka; yamekusudiwa kuwatofautisha watu wanaodai kuwa Waberiberi wa Afrika ya Kaskazini na

Waarabu wa sehemu ile, ambao walidai kuwa wa asili ya Kihimyar. Hata hivyo kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tatu mtindo ulibadilika, ambapo Hummay haikujinasibisha tena na Waberiberi bali na vizazi vya Wakurayshi wa kabila la Mtume. Hapa lengo lilikuwa ni kuonyesha imani yao ya muda mrefu katika Uislamu.

Kwa upande mwingine, haja ya kuonekana kuwa na misingi yao katika Kanem ilimaanisha kuwa wanaTarehe wa karne ya kumi na tatu waliandika kuwa Salmama b. Abd Allah (k. 1182-1210) alikuwa "mweusi sana," ambapo Ibn Said anaandika "Sultan wa Kanem... ni Muhammadi ben Jabl, wa ukoo wa Sayf... Mji mkuu wa wahenga wake makafiri, kabla ya kusilimishwa ulikuwa Manan." Lakini Muhammad lilikuwa jina tu, ambalo kwalo mfalme mashuhuri Dunama Dibalami (t. 1210-48) alijulikana duniani. Wakati huo Wasefuwa walifikiriwa kuwa wa kizazi kimoja na Wa duguwa (wafalme wa Zaghawa) licha ya kubadili dini na kubadilisha mji wao mkuu. Ukweli ni kuwa utawala huu, ambao ulikuwa na muundo kamili unaothibitishwa na maandishi ya *Diwan*, pengine ulianzia huko nyuma katika karne ya sita na kuwa na mji wake mkuu katika Manan, chini ya Waduguwa kwa muda usiopungua karne moja na pia katika Jimi, chini ya Wasefuwa, kwa muda wa karne tatu.

Ubadilishaji huu wa mji mkuu bila shaka uliakisi mabadiliko ya uwiano wa nguvu kati ya watu wenye makazi ya kudumu, ambao nguvu yao ilikuwa inaongezeka, na wa nusu-nomadi wa sahel, ambao nguvu yao ilikuwa inapungua. Hali ya kuuondeva mbali Uberiberi katika utawala mpya yaweza kuonekana katika mabadiliko ya asili za kikabila za mama-Malikia.

Inaweza kuonekana kuwa Watomaghra, ambao waliweza kutoa mama Malikia wawili katika kipindi cha Waduguwa, hawatajwi popote chini ya utawala wa Wasefuwa. Hata hivyo koo hizi za Kitubu zingalipo hadi sasa katika Tibesti na Kawar.

Kinyume na hali ilivyo kwa Watomaghra, Wakay wametajwa kuhusiana na nasaba zote mbili, jambo ambalo linamaanisha kuwa hadhi yao kisiasa ilibaki bila mabadiliko. Siku hizi Wakay (Koyam) huishi katika ukingo wa Borno karibu na Komadugu Yoo. Watubu wanatokea katika *Diwan* wanapohusishwa na Wasefuwa tu. Mke mkubwa wa Hummay alikuwa Mtubu, na inawezekana kuwa Watubu walichangia katika kuanguka kwa Waduguwa. Walikuwa na uhusiano gani na Wazaghawa, ambao waandishi wa Kiarabu waliwaweka kati ya Kanem na Nubia? Baadhi ya Watubu (Wadaza au Wagorban) wangali wanaishi katika sehemu hii. Lakini Watubu halisi wanaishi katika milina ya Tibesti. (Neno tu-bu huehukuliwa kuwa na maana ya "mkazi wa mlimani").

Wadabir (Wadibbiri) na Wakunkuna wanaotajwa katika *Diwan* hawako tena. Walitajwa na Nachtigal na Bath katika karne ya kumi na tisa kama Wakanembu wa kale wasiohamahama.

Kundi la mwisho ni la Wamagomi, ambao walikuwa ndio kitovu cha watu (Wakanuri) ambao polepole walijitokeza kutokana na nasaba ya Wasefuwa; lakini hili linamaanisha kuwa asili ya dola la Karem-Borno imatangulia asili ya watu ambao siku hizi ndio sehemu kubwa ya dola hilo.

Kabla ya kuibuka kwa Wakanuri, wafalme wa Kanem walipata mamlaka kutokana na makundi tofauti ya makabila ya wanomadi na walowezi waliozungumza lugha za kusini mwa jangwa la Sahara (Kitubu, Kizaghawa, Kikanuri) au lugha za Kichad. Makundi ya wazungumzaji wa lugha za Kiberiberi ambao mara nyingine (mathalan katika karne ya kumi na tatu) walichanganywa na kundi hili, waonekana kuwa kila wakati walikuwa wachache. Kufuatana na maandishi ya *Diwan*, kulikuwepo na awamu tatu zilizofuatana katika maendeleo na uimarishaji wa misingi ya kikabila ya wafalme wa Wasefuwa.

Awamu ya kwanza ilienea kutoka mwanzo wa mtawala Hummay mpaka katikati ya karne ya kumi na tatu na ilishuhudia utawala wa makundi mawili ya Wanomadi, yaani Watubu na Wakay. Katika awamu ya pili walowezi, yaani Wadabir na Wakunkuna, walijitokeza kuwa washirika wakuu wa Wasefuwa. Katika awamu ya tatu, kuanzia wakati wa Magomi, mama yake Dunama Dibalami (t.1210-48), mamlaka ya kisiasa katika ukoo wa ufalme wa Wamagomi yaliimarishwa zaidi. Karne moja baadaye *Diwan* iliacha kuonyesha asili za akina mama Malikia, jambo ambalo linaleta fikra kuwa mnamo mwanzoni mwa karne ya kumi na nne Wamagomi walikuwa wameyameza makundi mengine ya Wakanem walowezi. Jambo hili linaweza kuelezea kwa nini Dunama Dibalami, ambaye katika utawala wake Wamagomi walijitokeza kuwa wenye uwezo, alianza vita vya muda mrefu dhidi ya Watubu. Pia jambo hili linaweza kuelezea ni kwa nini kipindi cha kurithishana kwa amani kiasi kiti cha enzi kati ya baba na mwana kilimalizika wafalme wa Wasefuwa walipoacha kuwaoa wake zao wakubwa kutoka ugenini na kuanza kuoa kutoka koo zao wenyewe.

Ufalme wa Kanem katika kilele chake

Tangu nyakati za utawala wa Warumi, sehemu iliyoko kati ya Ziwa Chad na bahari ya Mediterania ilikuwa na njia ya moja kwa moja iliyopitia Fezzan na chemchemi za Kawar. Upande wa mashariki kulikuwepo pia njia mbaya sana iliyopitia chemchemi za Kufra na kwa upande wa magharibi kulikuwa na njia iliyopitia Takedda au Agades. Bila shaka njia hizi za biashara ya kuvuka jangwa la Sahara zilichangia ukuaji wa Kanem.

Muundo wa kisiasa

Hadi kufikia utawala wa Duama Dibalami ukoo wa Kifalme ulishikilia nafasi kuu katika nchi. Kuanzia karne ya kumi na tatu, wakati ambapo kulikuwapo na migongano ya wazi kati ya masultani na wana wao, wana hawa walitengwa na wageni au machifu wenyeji wakapendelewa katika mgawo wa madaraka. Vyeo vya *yerima* (gavana wa kaskazini) na *kayghamma* (gavana wa kusini) pengine vilianza wakati wa Waborno.

Mama-Malikia na ukoo wake walikuwa na nafasi kubwa katika uteuzi wa sultani mpya. Baadaye mke wa kwanza wa mfalme (*gumsu*) alitokea kuwa mke muhimu sana, kwa sababu mfalme alimteua mrithi wake (*shiroma*) kutokana na watoto wa kiume wa mke huyu.

Kufikia mwisho wa karne ya kumi na tano Wasefuwa walikuwa wakitawala, falme kumi na mbili za vibaraka. Utawala wa moja kwa moja, ambao mara kwa mara uliwekwa chini ya usimamizi wa watumwa wa mfalme, ulishughulikia sehemu ndogo tu ya milki. Maandishi yanatenganisha baina ya *jumud* (askari wa mgambo) na *asakir* (askari mweledi wa kuajiriwa).

Licha ya jitihada za kuanzisha sheria ya Kiislamu (*Sharia*) kama ilivyokuwa katika wakati wa Idrisi Alawoma, utendaji haki waonekana kuwa lilikuwa jukumu la mfalme kama ilivyokuwa kwa Mansa wa Mali.

Muundo huu wa kisiasa uliziathiri jamii za nchi majirani kama vile Wahausa, Wabaghirmi na wengineo.

Uchuuzi na Biashara

Sehemu ya magharibi mwa Ziwa Chad ilikuwa muhimu kwa Kanem ambayo ilikuwa mashariki mwa ziwa. Lengo kuu lilikuwa ni kudhibiti biashara kutoka Kawar. Biashara hii ilikuwa na pande mbili: uuzaji chumvi nje kwa wingi, kutoka Bilma na Agram kwenda katika nchi za Sahel kwa upande mmoja; na kwa upande mwingine, kulingana na Al-Idrisi, biashara yenye faida kubwa ya kuuza (*alum-shabu*: bidhaa iliyotumiwa kwa kutia nguo na ngozi rangi) Misri na nchi za Maghrib.

Lakini kwa biashara ya kuvuka jangwa la Sahara Fezzan ilikuwa na umuhimu zaidi ya Kawar. Fezzan ilikuwa mahali pazuri katika njia panda ya kutoka kaskazini hadi kusini baina ya Kanem na Afrika ya kaskazini, kwa upande mmoja; na kwa upande mwingine ilichunga njia zilizounganisha himaya zilizokuwa kwenye mipaka ya kusini mwa jangwa la Sahara na nchi za Misri na Mashariki ya Kati. Usalama katika njia hizo na udhibiti wa vituo vya kufanyia biashara hiyo yalikuwa malengo muhimu ya Kanem-Borno.

Muundo wa biashara hii haukubadilika sana baina ya mwanzo wa kuingia

kwa Uislamu na karne ya kumi na tisa. Al-Yakubi amerekodi kuwa wafanyibiashara wa Kiberiberi walileta idadi kubwa ya watumwa weusi kutoka Kawar hadi Zawila, mji mkuu wa Fezzan.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, Leo Africanus anatuambia kuwa wafanyibiashara wa Afrika ya Kaskazini walisafiri hadi Borno ili kubadilisha farasi kwa watumwa. Mashambulizi ya sultani wa Borno dhidi ya watu wasiokuwa Waislamu wa kusini, hayakutosheleza mahitaji ya watumwa. Aidha raia wa Kanem-Borno wenyewe wakati mwingine waliathiriwa vibaya na jambo hili, hasa ufalme ulipopungukiwa na nguvu. Katika barua aliyomwandikia Sultan Baybar wa Misri mwishoni mwa karne ya kumi na nne, Bir ben Idrisi alilalamika kuwa Waarabu walikuwa wakiwafanya watumwa raia zake Waislamu.

Bidhaa nyingine zilizouzwa kutoka Kanem zilikuwa pembe za ndovu, manyoya ya mbuni na wanyama kama vile twiga ambaye Ibrī Khaldum anasema alitumiwa sultan wa Ki-Hafsi Al-Mustansir, na "mtawala wa Kanem na bwana mkuu wa Borno." Madini ya bati kutoka uwanda wa juu wa Nigeria yalisafirishwa hadi Tripoli kupitia Borno hasahasa katika karne ya kumi na saba na pengine hata mapema zaidi.

Kwa kweli Kanem-Borno ilijipatia utajiri wake mwingi kutokana na shughuli zake za kilimo, ufugaji, na uchimbaji wa madini, kuliko kutokana na mapato ya biashara ya watumwa; aidha kulikuweko na bidhaa za kiufundi kama vile mavazi yaliyotiwa nakshi ambayo yanatajwa na Ibn Battuta.

Bidhaa zilizoingizwa kutoka nje zilikuwa ni farasi wa vita ambao waliongezwa wale wa Kanem ambao Al-Makrizi anawaelezea kuwa walikuwa wadogo. WanaTarehe wanasema kuwa kikosi cha farasi cha Dunama Dibalami (k.1210-48) kilikuwa na farasi 41,000.

Bidhaa za viwandani kama vile mavazi na silaha za chuma ziliingizwa kutoka nje. Al-Muhallabi anatwambia kuwa mfalme wa Wazaghawa alivalia mavazi ya sufu na hariri kutoka Sus (Sousse), ingawa ufumaji wa vitambaa vya pamba, ambavyo vilitumiwa kama viwango vya thamani, ulikuwa umeendelea sana nchini.

La mwisho ni kuwa, hapa, kama ilivyokuwa katika Mali, shaba kutoka Takedda iliuzwa hasa upande wa Kusini.

Kiwango cha biashara kilitegemea usalama katika njia za kufanyia biashara. Usalama huo ulihakikishwa na tawala tatu tu; ufalme wa Fezzan upande wa kaskazini uliokuwa unaongozwa na Waberiberi wa Banu Khattab; tawala za kichifu za Waberiberi wa Kawar sehemu ya kati, na utawala wa Kanem upande wa kusini. Hata hivyo mnamo mwaka wa 1172 kiongozi wa kivita wa

Wamamluk Sharif al-Din Karakush aliangamiza Fezzan. Ili kurudisha amani Dunama Dibalami (karne ya kumi na tatu) aliteka Kawar na Fezzan. Jambo hili limethibitishwa na Al-Umari katika karne ya kumi na nne. "Ufalme wa Kanem unaanzia upande wa Misri katika mji unaoitwa Zella (kaskazini mashariki mwa Fezzan) na kuishia upande mwingine katika mji uitwao Kaka; safari ya miezi mitatu inatenganisha miji hii miwili." Ibn Said anadhihirisha kuwa mfalme wa Kanem alishikilia mji wa Takedda katika upande wa magharibi na aliwatawala Watajuwa na Wazaghawa upande wa mashariki. Hata hivyo itakuwa ni uamuzi wa haraka kuona ndani ya mamlaka haya ya watawala wa Kanem juu ya schemu za mbali za mipakani mwa nchi muundo thabiti wa utawala. Kwa mfano, pengine Watubu wa Bahr al-Ghazal walikuwa watu huru. Pia watu walioishi kuzunguka ziwa Chad na wale walioishi visiwani ambao baadhi yao wametajwa na Al-Makrizi (Wabadi, Waankazar na Wakuri), waliendelea kuulinda uhuru wao kwa mafanikio.

Wafuasi wa dini za jadi kama vile Waafnu (Wahausa kama wanavyoitwa na Wakanuri) na Watokoto waliathiriwa vibaya sana kwa kushikwa mateka, kutokana na kuvamiwa na wafalme wa Kanem. Kwa ufupi halikuwa jambo la manufaa kwa Wafalme wa Kanem kusaidia katika kuusanibaza Uislamu kuvuka inipaka fulani kwa sababu watunwa walikuwa ni mchango muhimu sana, wa Sudan ya kati, katika biashara ya kuvuka jangwa la Sahara.

Hata Kanem kwenyewe Uislamu haukushika mizizi kabla ya karne ya kumi na tatu. Kinyume na yanayosemwa na Al-Makrizi, Dunama Dibalami hakuwa mfalme Muislamu wa kwanza wa Kanem, kwa sababu kulingana na *Diwan Wasefuwa* wote walikuwa Waislamu. Pia, mtawala wa pili wa milki, Dunama b. Hummay (t.1086-1140), anasemekana kuwa alikwenda hija mara mbili. Inawezekana kuwa katika utawala wa Dunama Dibalami Uislamu rasmi uliota mizizi na watu wengi wakasilimu. Alikuwa kiongozi mashuhuri katika mageuzi ya Kiislamu. Alivunjilia mbali mune, yaani dude lililoabudiwa na ufalme kabla ya Uislamu. Kulingana na waandishi wa *Diwan*, Imamu Furtu alimlaumu kwa kitendo chake ambacho inasemekana kuwa kilileta mfululizo wa machafuko, vikiwepo vita virefu dhidi ya Watubu. Dunama Dibalami, akiwa na wanasheria wengi wa Kiislamu, alianzisha *Madrassa* mjini Kairo kwa ajili ya watu wa Kanem, na pia alipigana vita vikali vya jihadi dhidi ya Waberiberi na watu weusi waliofuata dini ya kijadi.

Katika kipindi cha utawala wa Bir ben Dunama (1277-96) imetajwa ziara nchini Kanem ya masheikh wavili wa Kifulbe (felbata) kutoka Mali. Al-Umari ametaja uhaba wa mali wa ufalme huu, lakini akawasifu kwa imani yao kubwa na haki iliyotawala nchini kote.

Pengine Fezzan ilikuwa bado ni sehemu ya eneo la Kanem, lakini Takedda ilikuwa imejikomboa.

Kwa kweli kufikia nusu ya pili ya karne ya kumi na nne machafuko ya kudumu yalikuwa yameanza. Kwa hiyo kufikia mwisho wa karne hiyo Wabulala walifanikiwa kuiteka Kanem na kuuvunja ukiritimba wa ufalme huo juu ya biashara ya kuvuka jangwa la Sahara, na huo ulikuwa ndio mwanzo wa kipindi kibaya cha kuanguka kwa Wasefuwa.

Kutoka Kanem hadi Borno

Kufikia karne ya kumi na mbili, uhamaji mkubwa wa watu kutoka mashariki kuelekea magharibi mwa ziwa Chad, yaani kuenda Borno, ulikuwa umeanza. Hawa walikuwa ni pamoja na Watomaghra, Watura, Wakay (Wakoyam), ambao ndiyo makundi ya zamani zaidi ya Wamagomi. Uhamaji huu uliendelea hadi karne ya kumi na sita, hasa baada ya kufaulu kwa kampeni za kivita za Idrisi Alawoma na pia kutokana na kuhama, kutoka Kanem, kwa Watubu na Waarabu wengi waliovutiwa na ardhi yenye rutuba na yenye usalama zaidi katika upande wa magharibi.

Katika eneo hilo wenyeji walowezi, na ambao waliitwa kwa jina moja la jumla la Wasao, waliishi na kuongea lugha zao za Kichad. WanaTarehe wamerekodi kuwa katikati ya karne ya kumi na nne wafalme wanne wa Kisefuwa waliuliwa katika vita dhidi ya Wasao. Katika karne ya kumi na sita Leo Africanus ametaja kuweko kwa Wasao magharibi mwa Ziwa Chad na kusini mwa Borno. Idrisi Alawoma (1564-96) alianzisha mfululizo wa mashambulizi makali dhidi yao ambayo yaliwalazimisha kuyahama makao yao ya asili na wengine wao kujisalimisha katika visiwa vya Ziwa Chad.

Kuanzia mwisho wa karne ya kumi na tatu utawala wa Borno ulianza kupata umashuhuri. Yawezekana kabisa kuwa utawala huu ulikuwepo, kama ufalme huru, hata kabla ya wakati huo, na kuwa na mji wake mkuu katika Jaja, ambao umetajwa na Ibn Said. Isitoshe, waandishi wa Kiarabu kila mara wanatenganisha tawala hizi mbili. Al-Makrizi anaandika kuwa Ibrahim ben Bir (1296-1315) alishikilia falme za Kanem na Borno. Ibn Khaldun anazungumza juu ya “milki ya Kanem na bwana mkubwa wa Borno.”

Katikati ya karne ya kumi na nne al-Umari anataja kuwa masultani wa Kimamluk wa Misri walibadilishana barua na wafalme wote wawili, wa Kanem na wa Borno. Ushahidi huu wote unaleta fikra kuwa Kanem na Borno zilikuwa falme mbili tofauti, lakini kuanzia karne ya kumi na tatu ziliwekwa chini ya utawala wa Wasefuwa ambao utawala wao juu ya Waborno haukuwakataza Waborno kuwa na kiasi fulani cha uhuru.

Hali hii ilibadilika kabisa wakati mashambulizi ya Wabulala na Waarabu

yali Powellazimisha Wasefuwa kuondoka Kanem na, mwishowe, kuhamia Borno.

Wabulala, ambao walikuwa wafugaji, waliokaa mwanzoni kwenye eneo la Ziwa Fitri na kuwatawala Wakuba, wanaonekana kuwa walisukumwa kuelekea magharibi na uhamaji wa Waarabu kufuatia kuondolewa kwa ufalme wa Kikristo wa Nubia mwanzoni mwa karne ya kumi na nne. Lakini pia walivutiwa kwenda upande wa magharibi kwa kudhoofika kwa utawala wa Wasefuwa kutokana na magomvi ya kinasaba, hasa kati ya Dawud ben Ibrahim Nikale (karne ya kumi na nne) na wana wa nduguye na mtangulizi wake Idrisi. Dawud na warithi wake watatu waliuawa katika vita dhidi ya Wabulala. Umar ben Idris (1382-87) alilazimika kuuhama mji wa Jimi, na tishio la adui hawa wenye kuogofya halikuondolewa mpaka mwanzoni mwa karne ya kumi na tano lilipodhibitiwa na Wasefuwa.

Al-Makrizi anakariri matukio haya anaposema kuwa mnamo 800 mwaka (1400) raia wa Kanem waliasi dhidi ya wafalme hawa na kuikana dini yao. Waborno walidumisha imani yao katika dini na walipigana vita vya jihadi dhidi ya watu wa Kanem. Hata hivyo Diwan haithibitishi kuwa Wabulala walikuwa "makafiri". Kinyume na hayo, himaya mpya ya Waborno, chini ya Wasefuwa, na mji wake mkuu Kaka, iliashiria hali mpya na halisi ya kisiasa katika Sudan ya kati.


Wabulala walianzisha himaya mpya yenye nguvu katika Kanem ililojulikana na Leo Africanus kwa jina la Gaoga. Ilishirikiana na Watubu na Waarabu na kudumisha uhusiano mzuri sana na makhalifa wa Misri. Ilikuwa ni katika mwisho wa karne ya kumi na sita tu ambapo Waborno waliuteka tena mji wa Jimi kutoka kwa Wabulala, ambao mwishowe walipondwa na Idris Alawoma.

Migogoro ya kinasaba na kisiasa

Diwan inatambia kuhusu mfuatano wa tawala katika Kanem-Borno na uhusiano wa kiukoo kati ya wafalme mbaliinbali. Ni dhahiri kuwa kuchaguliwa kwa mtawala kulitegemea, kwa kiasi fulani, uwiano muwafaka wa madaraka. Zaidi ya yote, kuchaguliwa kwa mtu kuwa mfalme kuliamuliwa na uhalali anaopewa na sheria ambazo hazikuandikwa, mifano ya watangulizi wake na desturi kuliko sheria zilizoandikwa. Sheria hizi zilibadilishwa tu baada ya vipindi virefu au kutokana na machafuko makubwa.

Lakini wafalme sita wa kwanza walirithiana kwa utaratibu wa baba na mwana. Utaratibu huu wa urithi unaelekea kutokana na machifu wa Kawar wanaomkinika kuwa wazazi wa Hummay, aliyeanzisha milki mpya ya Wasefuwa.

Ilikuwa ni chini ya utawala wa mwanawe Dunama Dibalami ambapo urithi wa kwanza wa mtu kumrithi nduguye ulitokea. Kaday na Bir, ambao



10.1 Watu na falme za Chad kwenye karne ya kumi na mne (D. Lange)

wote wawili walikuwa wana wa Dunama, lakini kutokana na mama wawili tofauti kwa mara ya kwanza walizusha ugomvi kama tunavyoelezwa kwenye *Diwan*. Pengine, ugomvi huu ilikuwa ni ushindani kati ya ukoo wa ufalme wa Wamagomi na koo za Wakanem walowezi. Zaidi ya haya, yafaa kufahamika kuwa Kaday alikufa katika vita dhidi ya mmoja wa mabarakala wakubwa wa himaya. Baada ya utawala wa nduguye Bir, mwanawe (Bir) Ibrahim Nikale (t. 1296-1315) alirithi uongozi kufuatana na sheria ya zamani, lakini alikufa akipigana na barakala mwingine mkubwa.

Alifuatwa na mwana wa Kaday, Abd Allah, ambaye alirithiwa na mwanawe. Hivyo, hadi kufikia mwanzoni wa karne ya kumi na nne kanuni ya zamani ya urithi wa moja kwa moja ilikiukwa kwa kutumia nguvu tu.


Baadaye urithi wa sambamba (wa ndugu kwa ndugu) ulitokea kwa wingi. Wana wanne wa Abd Allah walifululiza katika uongozi mmoja baada ya mwingine kabla ya kumwachia uongozi mjukuu wa Bir, Idris ben Ibrahim Nikale, ambaye alifaulu kuwasuluhisha Wasao wenyeji. Baada ya kifo chake mmoja kati ya ndugu zake, Dawud, alichaguliwa kuongoza lakini wanawe (Nikale) walipigana vita vikali dhidi ya ami yao. Kulikuweco na vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilisaidia upanuzi wa utawala wa Wabulala. Makundi mawili yaliyopingana, yaani lile la wana wa Dawud na lile la wana wa Idris yalirithiana madaraka zaidi kwa misingi ya usambamba na pia kwa kutegemea hali ya kisiasa ya wakati wa urithi. Ilikuwa ni katika muktadha huu ambapo Said (k. 1387-88) asiye kuwa Msefuwa alimrithi Umar baada ya yeye (Umar) kuhama kutoka Kanem hadi Borno.

Wana-Idris na Wana-Dawud walijiri kuondolewa uongozini na watu kutoka nje ya ukoo wa ufalme, hasa maafisa wakuu kama vile *kayghamma* (mkuu wa majeshi) na *yerima* (gavana), ambao hawakusita kupindua na kufanya hila ili kuutumia uongozi jinsi walivyopenda.

Zaidi ya haya ilikuwa ni katika utawala wa Bir Uthman (t.1389-1421), na baada ya Wabulala kurudishwa nyuma na majeshi, ambapo *kayghamma* aliamua kuonyesha uwezo wake wa kisiasa. Machafuko yaliyoanzishwa hivyo yakaendelea, baadhi ya wafalme wakashindwa kukaa kwenye kiti cha enzi zaidi ya mwaka mmoja.

Ilikuwa ni katikati ya karne ya kumi na tano tu, na baada ya karne moja ya zahama, ambapo ukoo wa Dawud uliondoshwa kabisa. Lakini kanuni ya urithi wa sambamba ambao sasa ulikuwa umejijenga, ilileta ugomvi katika ukoo wa Idris wenyewe. Hivyo Ali Ghjideni (1465-97), ambaye alishinda vita dhidi ya ukoo wa Dawud, alilazimika kuwaachia ndugu zake uongozi kabla ya yeye mwcnnyewe kuuchukua. Alijenga makao makuu mapya ya Wasefuwa, katika mji wa Gazargamo ambao ulikuwa kati ya Kano na Ziwa Chad, na uliodumu kama

mji mkuu kwa karne tatu. Lakini baada ya kifo chake utaratibu wa urithi wa moja kwa moja, kutoka kwa baba hadi mwanawe, ulirejeshwa, jambo ambalo liliurudisha utawala wa Borno pale ulipoanzia kwenye siku za kale kabisa za utawala wa Wasefuwa.



Wahausa na majirani zao katika Sudani ya Kati

Nchi ya Wahausa imeenea kutoka milima ya Air kwa upande wa kaskazini hadi uwanda wa juu wa Jos kwa upande wa kusini, na kutoka Borno upande wa mashariki hadi bonde la Niger kwa upande wa magharibi. *Kasar hausa* (nchi ya Kihausa) ndilo jina lililopatiwa eneo hili japokuwa watu wasiokuwa Wahausa kama vile Watuareg, Wazabarma (Wajerma) na Wafulbe pia waliishi hapo. Ustaarabu wa hali ya juu uliostawi hapa ulitokana kwa kiasi kikubwa na mwingiliano huu wa kitamaduni kwa njia ya lugha ambao uliwezesha kuzifanya mila na asasi za kisiasa kuungana na kuwafanya Wahausa moja ya makabila muhimu kabisa ya Afrika.

Asili ya Wahausa

Kuna nadharia nne zinazoeleza asili ya Wahausa:

Nadharia ya kwanza ambayo sasa imekwishatupiliwa mbali inatokana na tafsiri potofu ya kisakale cha Wabayajida (au Wadaura) inayodai kwamba mababu wa Wahausa walikuwa Waarabu kutoka Baghdad. Kwa mujibu wa Abdullahi Smith, iwapo kisakale cha Wabayajida kina maana yoyote, basi itakuwa ni athari za Waborno kwa asasi za kisiasa za Wahausa kama inavyodhihirishwa na maneno ya Kikanuri katika msamiati wa Kihausa. Nadharia ya pili inaeleza kuwa Wahausa kwa asili waliishi Sahara ya kusini na walielekea Kusini zaidi nchi yao ilipogeuka jangwa; na kuwasukuma nyuma watu wa asili wa sehemu hiyo hadi kwenye uwanda wa juu wa Bauchi ambapo lugha inayoongewa ni tofauti na ya Kihausa. Maelezo haya yanaweza kuwa kweli lakini hayana ushahidi wa data ya uhakika. Hii ni nadharia tete tu.

Nadharia ya tatu inadai kwamba mababu wa Wahausa walikuwa wanaishi pwani ya magharibi ya Ziwa Chadi, na ziwa lilipokauka waliamua kusalia katika ile ardhi iliyokauka maji ya ziwa na kuwa wakulima, kisha walisambaa kuelekea kaskazini na magharibi kutokea mahali ambapo ndipo palikuwa kitovu

cha falme za Daura, Kano, Rano na Garun Gobas, na kujumlisha Katsina, Zazzau, Gobir Zamfara na Kebbi. Hata hivyo hakuna ushahidi kamili unaoweza kuthibitisha tasnifu hii.

Nadharia ya nne iliyopendekezwa na Mahdi Adam, inasisitiza sifa ya uasili wa Wahausa kwa kudai kuwa hapana kikundi cha Wahausa chenye masimulizi ya uhamaji. Inadaiwa kuwa "mababu walitoka mashimoni ardhini." Baadaye makundi ya awali yalinufaika sana, bila shaka kutokana na uhamiaji wa Wangarawa (Wangara, Joola) na Wafulbe. Bila shaka mchakato wa kuzuka kwa watu hawa ni vigumu kuujenga tena, lakini hapana namna ya kuukanusha. Aidha inawezekana kwamba, zama za zamani sana nchi ya Wahausa ilijumlisha sehemu za Sahara, hasa Air (Azbin), ambayo ilitakwa na Watuareg mnamo karne ya kumi na nne na kumi na tano ambao waliwarudisha nyuma Wahausa kuelekea Gobir. Neno Hausa lienezwa kutumika takribani mnamo karne ya kumi na sita. Mpaka wakati huo wakazi wa eneo hili walijulikana kwa njajina ya falme zao: Katsinawa, Kanawa, Gobirawa n.k. Mmisri Al-Suyut (1445-1505) alitumia neno "Hausa" katika maandishi aliyoyaita *Barua kwa Wafalme wa Sudan, Hausa na al-Takrur*. Waandishi wa *Tarikh* ya Timbuktu walitumia neno hili kutaja ukingo wa magharibi wa mto Niger kwa kutofautisha na Gurma.

Awali neno Hausa lilitumiwa kutaja lugha, watu wenyewe walijiita "Hausawa" ikimaanisha wazungumzaji wa Kihausa. Baadaye, kwa lengo la kuweka mipaka ya matumizi, neno hili lilitumiwa kuwataja wale wote wanaoishi karibu na dola la Songhai ambao waliwakilisha Wahausa kwa pamoja, yaani falme za zamani za Zamfara, Kebbi na Gobir. Watu wasiokuwa Waislamu lakini walioongea Kihausa waliitwa Wamaguzawa au Waazna, yaani "Wapagani" (kutokana na neno la Kiarabu majus). Hii inaonyesha kuwa kuundwa kwa Uhausa ni kwa hivi karibuni. Tutatumia istilahi Hausa kuwataja wazungumzaji wote wa Kihausa bila kubagua.

Chimbuko na ukuaji wa nchi za WahausaWahausa

Kwa mujibu wa kisakale maarufu, mwana mfalme Bayajida alikuja kutoka Baghdad na kupata mapokezi ya utatanishi kutoka kwa *mai* (mfalme wa Kanem-Borno), jambo lililomfanya akimbilie magharibi. Alifika katika mji wa Daura uliotawaliwa na Malikia; mji huo ulikuwa ukisumbuliwa sana na nyoka Bayajida. Baada ya kumwua yule nyoka alimwoa malkia, akamzalia mwana aliyeitwa Bawogari, kisha kimada wake akamzalia mwana mwingine aliyeitwa

Karbogari.

Bawogari alizaa wana sita ambao walikuwa machifu wa Kano, Daura, Gobir, Zazzau (Zaria), Katsina na Rano, kwa mfuatano huo. Ukichanganya na Biram iliyokuwa ikitawaliwa na mwana wa binti mfalme wa Borno, nchi zote saba ziliitwa *hausa bakwai*. Wana wa Karbogari walianzisha nchi nyingine saba: Kcbbi, Zamfara, Gwari, Jukun (Kwararafa) Yoruba, Nupe na Yawuri, *banza bakwai* (wanaharamu saba).

Hadithi hii maarufu kwa hakika inatoa picha ya hali halisi - hali iliyokuwapo karne ya kumi na sita ambapo nchi hizi saba zilinusurika mapigano yaliyokuwa yanawazunguka na kujihalalisha kwa hadithi inayodai kuwa zilitokana na ukoo mashuhuri sana wa mashariki. Lakini kuwapo kwa malkia wakati Bayajida alipowasili Duara ni ushahidi kuwa mfumo wa serikali kuu haukuletwa na shujaa mstaarabishaji. Aidha ukaribu wa hadithi hii unatokana na ukweli kuwa ndani yake unatajwa na mgawanyo wa shughuli miongoni mwa miji ya Wahausa.

Kano na Rano ilikuwa *sarakunan babba* (wafalme wa buluu), Katsina na Daura *sarakunan kasuwa* (wafalme wa soko) Gobir *sarkin yaki* (mfalme wa vita) na mwisho Zaria alikuwa *sarkin bayi* (mfalme wa watumwa) kwa mujibu wa majukumu ambayo yalitekelezwa na miji hii katika utengenezaji rangi, biashara, ulinzi au kutoa wahadimu. Majina haya yalieleza hali ya jumla (ya nyakati za karibumi).

Kutokea kwa madola yenye serikali kuu kunaelekea kuhusishwa na kuanzishwa kwa miji yenye ngome iliyoitwa *birane* (umoja ni *birni*).

Kano

Historia ya Kano inafahamika sana kwa sababu ya Tarehe zake na utajiri mwingi wa mapokeo simulizi. Awali kulikuwepo na tawala ndogo za tambiko, mathalani ule wa Dala. Inakadiriwa kuwa kuingia kwa Bagauda katika eneo la Kano kulitokea mwaka 999. Mjukuu wake, Gijimasu (1095-1134), alianzisha mji wa Kano chini ya kilima cha Dala. Alianza kujenga kuta za mji ambazo zilikamilishwa na mwanae Tsaraki (1136-94).

Chini ya utawala wa Yaji (1349-85) kazi ya kuzitwaa nchi zilizoizunguka Kano na kuziunganisha ilikamilika, japokuwa ilikabiliwa na matatizo. Hata Rano ilitakwa na haikupata tena uhuru wake kamili. Upinzani wa Santolo ulizimwa hasa kwa msaada wa Wangarawa Waislamu anbao walikuwa ndio kwanza wamewasili pale. Kituo hiki cha dini cha asili kiliteketezwa. Upinzani dhidi ya utawala wa Kano anbao unaonyeshwa kama upinzani dhidi ya Uislamu, uneleweka vyema zaidi ukionekana kama upinzani wa watu maarufu

au vikundi vya umma dhidi ya ukiritimba dhalimu wa madaraka. Upanuzi wa Kano ulielekezwa kusini, na hii ilisababisha mapambano ya kwanza na majeshi ya Kwararafa/Jukun. Katika vita hivi hapana aliyetokea kuwa mshindi. Wajukun walikataa kulipa kodi, lakini walipeleka shehena moja ya watumwa.

Kananeji (1390-1410), aliendeleza sera ya kupanua himaya na kuitwaa Zaria. Mawasiliano na nje yalizidishwa kama inavyodhihirishwa kutumika kwa *lifidi* (kinga ya farishi kwa ajili ya farasi wa vita), kofia za chuma na dereya. Wakati wa utawala wa Dauda (1421-38), kuwasili kwa mwanamfalme wa Borno ambaye alikuwa mkimbizi kulileta dhana za hali ya juu za utawala, ikiwa ni pamoja na matarumbeta na bendera. Vyeo vya Borno kama vile *galadima*, *chiroma* na *kaigama* vilianza kutumika Kano.

Kuanzia wakati huu shughuli za biashara za Kanawa zilizidi kuwa muhimu zaidi kuliko vita. Njia ya kuvuka mataifa ya Afrika ilianzishwa baina ya Borno na Gonja. Misafara ya ngamia waliobeba chumvi, kola na matowashi kutoka Sahara iliongezeka zaidi na zaidi. Ustawi na maendeleo ya Uislamu yaliwavutia viongozi wa dini. Mnamo 1450 Wafulbe kutoka Mali walileta vitabu vya dini, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo vitabu vilivyohusu sharia na hadithi tu ndivyo pekee vilivyokuwapo. Mwishoni mwa karne waliwasili masharifu kadha, wakifuatiwa na mwanamageuzi asiyetetereka, Al-Maghili.

Tarihi ya Kano inamnasibisha Muhammad Rumfa (1463-99) na uvumbuzi kadha muhimu: utanuzi wa kuta za jiji, uteuzi wa inatowashi kushika nyadhifa za kisiasa, kuanzisha soko kubwa na kuteuwa baraza la maofisa tisa maarufu wa serikali (*tara-ta-Kano* "Tisa wa Kano") ambao waliunda namna ya baraza la mawaziri. Baadhi ya mavumbuzi haya yanadokeza kuwa yaliigwa kutoka yaliyokuwa yakifanywa katika nchi ya jirani ya Borno: k.m. ujenzi wa ikulu mpya (*gidan Rumfa*), inatumizi ya matarumbeta marefu na vipepeo vya manyoya ya mbuni, ujenzi wa harimu iliyokuwa na inasuria 1,000 na shamra shamra za sherehe za kuadhimisha kumalizika kwa Ramadhan (*Id al-fitr*). Hata hivyo, Kano iliendelea kudhalilishwa kwa kuilipa kodi Borno, na ilipigana vita kwa miaka mia moja na Katsina.

Katsina

Maendeleo ya Katsina yanaelekea karibu kulingana na yale ya Kano japokuwa kwa wakati tofauti. Hapa pia, tawala ndogondogo ikiwa ni pamoja na ule wa Durbi, ziliungana na kuunda dola ya jiji. Kuanzia wakati wa Sarki (Mfalme) Muhammad Korau (1445-95) tunapata taarifa za historia. za uhakika zaidi. Korau alijenga mji wa Katsina uliozungushiwa ukuta (*birni*) kwenye makutano ya njia kadha za biashara, karibu na machimbo ya chuma na mahali patakatifu

palipojulikana kama Bawada. Watawala wa nchi jirani walikuja kulipa kodi ambayo ilikuwa mikuo ya chuma, na huu ndio uliokuwa mwanzo wa *haraji* au kodi ya kichwa.

Kutoka kwenye makazi haya, Korau, ambaye alikuwa mtawala wa kwanza wa Kiislamu, alifanya mashambulizi ya kupanua nchi yake kuelekea Kusini, alijenga msikiti wa Gobarau ulioiga misikiti ya Gao na Jenne, na kumpokea Al-Maghili.

Tarihi ya Katsina imerekodi hasa vita dhidi ya Nupe. Kati ya warithi wa Korau, Ibrahim Sura (1453-99) alipigana na waliokataa kuukubali Uislamu, na aliandikiana na Al-Suyuti. Baada yake alitawala Ali ambaye kipindi chake kirefu cha utawala kilijumlisha robo ya kwanza ya karne ya kumi na sita. Aliitwa *murabit*, labda kama kumbukumbu kwa kuujengea mji ngome.

Zaria

Hapa kuna ushahidi kidogo sana wa kihistoria. Kwa kipindi kilichodumu zaidi ya miaka karibu elfu moja, kuanzia Turunku, machifu waliyaunganisha au kuyatwaa maeneo yaliyokuwa jirani kabla ya kuselea mahali ambapo Zaria sasa ipo, labda mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Haya ndiyo maoni ya Abdullahi Smith. Murray Last ana maelezo tofauti. Anadai kuwa mwishoni mwa karne ya kumi na tatu palikuwa na shirikisho la Kangoma lililojumuisha vikundi visivyokuwa Wahausa. Hawa walikuwa warithi wa utamaduni wa Wanok waliojishughulisha na biashara ya metali. Shirikisho hili lilipovunjika, ufalme wa Kangoma ulitwaa eneo hili la Turunku. Na ilikuwa ninamo karne ya kumi na saba tu ambapo Wahausa walikuja kuitawala Zaria. Hii ni nadharia tete ya kijasiri sana.

Abdullahi Smith anatetea msimamo wake kwa kusema kuwa karibu na mwishoni mwa karne ya kumi na nne miji mingi miongoni mwayo ikiwa Turunku na Kufena ilizuka katika eneo hili. Ilibakia huru hadi Bakwa wa Turunku alipotwaa madaraka kule. Kufena na kujenga makao makuu mapya karibu na hapo na kuyaita Zaria kwa heshima ya binti yake. Zaria Amina, dada yake *Bakwa*, ambaye alikuwa mwanamke mrefu na mwenye nguvu, ndiye aliyeyaongoza majeshi ya Zaria hadi kufika nchi ya Waupe na Kwararafa. Katika Tarehe ya Kano, inaelezwa kwamba "*Sarkin Nupe* alimpelekea binti mfalme huyu matowashi arobaini na kola 10,000. Alikuwa mtu wa kwanza katika nchi ya Wahausa kumiliki matowashi na kola." Inasemekana pia kuwa Amina alijengea ngome miji ya Zaria na Kufena. Alikuwa *gimbya* (binti mfalme) maarufu, lakini hakuwahi kuwa malkia.

Gobir

Gobir ilikuwa nchi ya kaskazini kabisa ambayo eneo lake la awali lilikuwa ni pamoja na vilima vya Air. Wagobirawa walirudishwa nyuma na Watuareg hadi kufika maeneo tambarare ya Adar na kuelekea eneo la sasa la Gobir wakichukua pamoja nao chumvi kama bidhaa ya kawaida na mahindi. Kabla ya karne ya kumi na sita, Wagobirawa waliselea katika ufalme uliokuwa katika eneo la sasa la Niger na makao yake makuu yakiwa Marandet. Kituo hiki cha biashara na viwanda kilichotegemea biashara ya kuvuka Sahara kinafahamika tangu karne ya tisa. Gobir ulikuwa bila shaka kinga ya mipaka ya kaskazini ya nchi ya Wahausa.

Rano

Ufalme huu unaelezwa kuwa ulikuwapo tangu karne ya kumi na moja kabla ya kutwaliwa na Kano. Kwa kweli Tarehe ya Kano haitaji nchi hii kabla ya karne ya kumi na tano. Kulikuwapo na utawala wa Kihausa wa Zamnagaba, ambao labda ulihusiana na Santolo na ulitekwa vitani mwishoni mwa utawala wa *Sarkin Yaji* (1349-85). Pengine Zamnagaba ingechukua nafasi ya Rano katika orodha ya *hausa bakwai*.

Zamfara

Nchi hii ilijitokeza waziwazi mnamo karne ya kumi na sita. Mwanzoni kulikuwa na tawala chache miongoni mwazo zikiwa Dutsi, Togno na Jata, ambazo makao yake ya tawala yalikuwa karibu na madini ya chuma na vilima vyenye madhabahu ya kijadi. Dutsi iliongoza katika kuunda serikali kuu. Birnin Zamfara ilianzishwa katikati ya karne ya kumi na sita, wakati dola hii ilipotuma misafara mbalimbali, kwa mfano, hadi Yawuri katika bonde la Niger.

Kebbi

Muhammad Bello anadai kuwa watu wa Kebbi wametokana na mama Mkatsina na baba MSonghai. Wakati wa Sunni Ali (1464-92), katika eneo hili lililokuwa limetwaliwa na Songhai, kulikuwa na watawala wa ukoo (magaji) ambao walishindwa na mhamiaji kutoka Katsina Muhammadu Kanta. Alikuwa kiongozi hodari wa kijeshi ambaye alijiunga na jeshi la Songhai na kisha kuwa mkuu wa jimbo hili. Aliporejea kutoka vitani dhidi ya Sultani wa Agades, akiwa hakuridhika na mgao wake wa nyara iliyopatikana, alijitenga na kuhimiza upinzani dhidi ya Songhai kwa kujenga ngome nyingi ambazo hatimaye zilifanya ngome ya Birnin Kebbi na kuanzisha nchi ya Kebbi.

Aliitwa Air (Agades) kutoka utawala wa Songhai. Kwa mujibu wa Muhammad Bello, aliteka nchi yote ya Wahausa na sehemu za Borno, na pia alilivamia eneo la Kusini hadi Nupe. Eneo lote hili halikuwekwa chini ya himaya kuu moja bali lilibakia kama mtanduo wa nchi zilizolipa kodi tu. Mnamo karne ya kumi na sita Kebbi lilikuwa taifa kubwa lililokuwa na nguvu sawa na Songhai upande wa magharibi na Borno upande wa mashariki. Borno ilishindwa ilipojaribu kuishambulia Kebbi. Lakini Kanta alifariki alipokuwa akirejea kutoka katika vita vya ushindi mwaka 1556. Ndipo Nchi za Wahausa zikajikomboa na kuisaidia Agades kujikomboa. Kebbi ikarudia hadhi yake ya awali ya kuwa ufalme wa kienyeji.

Kwa ufupi baina ya miaka 1200 na 1600, Wahausa walijiundia dola za miji zilizokuwa na nguvu sana, zenye dhima muhimu na wakati mwingine ya msingi katika mwenendo wa kijeshi, kisiasa na kiuchumi wa Sudani ya Kati.

Mahusiano ya Wahausa na mataifa ya jiranijirani

Miongoni mwa watu ambao hawakuwa Wahausa waliokuwa washirika na maadui wa Wahausa wafuatao wanapaswa kutajwa: Wajukun, Wakwararafa, Wayoruba, Wanupe na Wayawuri, na bila shaka majirani zao wakubwa, Waborno na Wasonghai.

Wahausa waliwaita wakazi wa Kanem Borno (Wakanembu, Wakanuri) *Waberiberi*. Kupitia kwa viongozi wao, wafanyabiashara na viongozi wa dini, utamaduni wa Kanem-Borno umepenyeza vitu vingi katika ustaarabu wa Wahausa ambavyo leo hii havitenganishiki nao. Athari hizi zilipata mashiko zaidi baada ya utawala wa Sefuwa kuhama kutoka Kanem na kwenda kwa Borno, kurejea kwa utangamano huko Borno, na kuanzishwa kwa Ngazargumu kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na tano. Uthman Kalnama, mkimbizi toka Borno aliyeishi Kano, alikuwa na dhima muhimu huko mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tano. Borno ilikabiliana na hali hii kwa kupunguza hadhi ya miji mbalimbali ya Wahausa na kuifanya iwe "makoloni" yenye kulipa kodi tu, ijapokuwa uhusiano huu unahitaji utafiti zaidi.

Lakini njia kuu ya kupitishia athari ya Waborno ilikuwa Kano, ilihali Kebbi ikiwa chini ya Kanta, iliongoza mapambano ya Wahausa dhidi ya Waborno, hata kuweza kuikomboa baadhi ya miji ya Wahausa kutoka kwa udhamini wa Waborno.

Kwa upande wa magharibi kulikuwa hasa na Songhai, kwani kwa wakati huu Mali iliendeleza shughuli za kidini na za biashara pekee. Kwa muda mrefu wanahistoria waliainini kuwa Askiya Muhammad (1492-1528) aliivamia na

kuitawala nchi yote ya Wahausa. Chanzo pekee cha tukio hili kilikuwa maelezo ya Leo Africanus. Hata hivyo Tarehe ya Kano haisemi lolote kuhusu hoja hii, ilihali inakiri waziwazi juu ya uvamizi wa nchi ndogondogo. Zaidi ya hayo Tarehe za Timbuktu zinazoeleza hadithi hii kwa mtazamo wa Songhai hazisemi lolote kuhusu uvamizi huu unaodaiwa. Hivyo kuna sababu za msingi za kuyakataa maelezo ya Leo Africanus.

Wajukun waliishi kusini mashariki mwa nchi ya Wahausa katika eneo la Benue ya Kati. Katika Wakati huo walifanya mambo mengi muhimu kuliko idadi yao ya sasa inavyoyumkinisha. Baadhi ya watu wanadai kuwa Wajukun walitoka katika bonde la Nili na Kordofan wakati mmoja na Wakanuri. Lakini kuna uwezekano kuwa walikuja kutoka nchi ya karibu zaidi wakipita kati ya Ziwa Chad na nyanda za juu za Mandara. Lakini kwa mujibu wa lugha yao wao ni sehemu ya familia ndogo ya lugha za Benue-Kongo kama vile Waibibio na Waefik, jambo ambalo laelekea zaidi kudai kuwa asili yao ni kusini. Kwa ufupi, inawezekana kuwa walikuwa kundi la mwisho kati ya makundi mengi yaliyokuwa yakihama mfululizo kutoka kaskazini mashariki.

Baadhi ya watu wanadai kuwa nguvu kubwa ya Wajukun ilikuwa kusini katika Benue ya Kati. Magofu ya Kwararafa yanaonekana hapa hadi leo kama yalivyo yale ya Wukari iliyofuatia Kwararafa mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Wajukun walitokea hapa na kuelekea kaskazini, hususa Kasar Chiki ambapo mapokezi simulizi yake yanadhihirisha kuwa asili yao ni kusini.

Lakini nadharia nyingine inadai kuwa nguvu ya kisiasa ya Wajukun ilianzia katika bonde la Gongola na la Benue ya juu kabla ya kuelekea kusini.

Hizi nadharia mbili hazisigani iwapo itakubaliwa kwamba Wajukun walikuwa na vituo viwili vya nguvu za kisiasa. Baadhi ya mashambulio dhidi ya nchi za Wahausa kutokea bonde la Gongola huenda yaliambiwa na *aku* (mfalme wa Wajukun) wa upande wa kusini ambapo ndipo ilipokuwa nguvu kubwa ya Wajukun. Inawezekana pia kwamba kulikuwa na dola mbili za Wajukun, moja ya kaskazini ikiitwa Kwana na Wakanuri, na nyingine ambayo inatajwa katika *Tarehe ya Kano* ya karne ya kumi na nne, ambayo ilikuwapo kusini zaidi. Jambo la hakika ni kwamba baina ya miaka ya 1200 na 1600 Wajukun waliishi Benue ya kati na katika bonde la Gongola. Walikuwa na nchi yenye nguvu ambayo ilifikia kilele chake mwishoni mwa karne ya kumi na sita; lakini athari ya utamaduni wake iliwafikia watu wa makabila mengi kama vile Waigala, Waidoma na mengine mengi.

Nupe ilikuwa ukingoni mwa msitu na kuwa kama daraja kuelekea msitu katika mukutano ya mito Niger na Benue. Kwa hali hii ilikuwa ni dhahiri kuwa Nupe palikuwa ni mahali pa kukutania. Mwanzilishi wa Nupe katika visasili

aliitwa Tsoede, lakini kabla yake kulikuwa na shirikisho la Wabeni lililoundwa na koo tano miongoni mwao zikiwemo Wacbe, Wabini n.k. Bila shaka walikuwapo wafalme wengine kabla ya Tsoede ambaye anaonekana kuashiria ujenzi wa mamlaka kuu ya kifalme, ambao pengine ulitokea karne ya kumi na sita, japokuwa kumbukumbu za Wahausa kuhusu Nupe zinaanza karne ya kumi na tano. Utamaduni uliovuka mipaka ya kabila uliokuwa ukibwia tamaduni za nje zilizokuwa zimetokea nchi ya Yoruba, Borno na Igala ulijidhihirisha kuwa ulikuwa na nguvu sana. Wafalme wa Nupe walianzisha mawasiliano ya kibiashara na kidiplomasia na nchi jirani, na hasa miji ya Wahausa. Wakazi wa Bauchi, nchi iliyokuwa kusini mwa nchi ya Wahausa, walikuwa washirika muhimu wa Wahausa. Wakazi wengi, ukiachilia mbali Wakambari, walikuwa ni makabila madogo madogo. Mahusiano yalielekea kuwa hasa ya wahamiaji wa Kihausa walioingia katika maeneo haya kama wakimbizi au kwa ajili ya kufanya biashara au kwa sababu za kijeshi. Wahausa wengi waliishia kuusharabu utamaduni wa watu hawa na kumezwa nao. Eneo hili lilitumika pia kusaka watumwa. Walikuwa Wakambari na Wakannuku pekee miongoni mwa watu wa Bauchi ambao walianzisha serikali kuu. Wakambari walifanya hivyo kule Maginga mnamo karne ya kumi na tatu ambapo utawala wa Wahausa ulifika hapo mwishoni mwa karne ya kumi na nne. Mintaarafu Wakamuku, inawezekana kuwahusisha na ufalme wa Kankuma uliotajwa na Al-Makrizi.

Matukio Makuu katika Nchi ya Wahausa

Uhamiaji

Wahamiaji waliingia nchi ya Wahausa wakitokea zaidi kaskazini kutoka Borno kwa upande wa mashariki na kutoka Mali na Songhai kwa upande wa magharibi. Hawa walikuwa wafugaji, wavuvi, wakulima, wafanyabiashara, wanazuoni (*mallam*), viongozi wa dini na wanamfalme.

Wafugaji walikuwa ni Wafulbe wakifuatiwa na Watuareg. Wafulbe (Wafulani) walitoka magharibi. Kwanza walifika Katsina mnamo karne ya kumi na tano. Muda mfupi baadaye *Tarehe ya Kano* inarekodi kuwasili kwao kwa maelezo yafuatayo:

Wakati wa utawala wa Yakubu (1452-63) Wafulani walikuja katika nchi ya Wahausa kutokea Melle, wakileta pamoja nao vitabu vya dini na etimolojia... Wafulani walipita na kuelekea Bornu, wakiwaacha watu wachache katika nchi ya Wahausa, pamoja na watuina na watu waliokuwa wamechoka kusafiri.

Kwa kweli wengi wa hawa Wafulbe walikuwa wafugaji kondoo waliokuwa wakitafuta malisho; waliendelea na dini yao ya kijadi. Walikuwa wengi sana hasa eneo la kati la Kano, kaskazini mwa Katsina na kwenye bonde la Rima (Kebbi). Viongozi wa dini ya Kiislamu walijishughulisha zaidi katika miji.

Watuareg waliwasili kutoka Air mwishoni mwa karne ya kumi na nne wakiwasukuma Wahausa wa asili kuelekea kusini na kuanzisha usultani wa Agades. Kwa kuwa Watuareg ni waliamhamaji, hawakufanya makazi hapa, walibadilisha ngo'mbe au sanaa za ufundi mazao ya kilimo na kufanya uvamizi wa mara kwa mara kwa watu walio na makazi ya kudumu.


Uhamiaji kutoka Borno ulianza mapema sana, lakini mnamo karne ya kumi na tano ndipo unapoanza kutajwa katika nyaraka. Uhamiaji uliongezeka sana kabla ya 1600 na ulifanywa na mamwinyi wakimbizi, wanazuoni na wafanyabiashara walioselea hasa Kano, Katsina na Zaria. Wangarawa (WaDiula) waliwasili pia kutoka magharibi mnamo karne ya kumi na nne na ya kumi na tano. Wengi wao walikuwa ni wafanyabiashara na waliselea Kano, Yandoto na Kuyambana, na hatimaye wakamezwa na mfumo wa kijamii wa Wahausa.

Makundi ya wavuvi wa Songhai yalikuja kutoka magharibi na kuselea katika sehemu ya chini ya bonde la Rima. Walikuwa na zana bora zaidi. Lakini hatimaye waliungana kabisa na Wahausa na kufanya ukanda wa magharibi wa Uhausa.

Hatimaye, waliwasili wafanyabiashara na wanazuoni wa Kiarabu na Kiberiberi waliotoka Timbuktu au Afrika ya Kaskazini mnamo nusu ya pili ya karne ya kumi na tano ambao waliselea hasa Kano wakiwa wamevutiwa na utajiri na dini ya Kiislamu.

Uhamaji

Lakini watu walikuwa pia wanaihama nchi ya Wahausa, wakielekea kusini na magharibi, na walikuwa wanafanya hivyo tangu zamani sana. Mwelekeo wa kusini ulikuwa, kwa mfano, ukihusishwa na kampeni za kivita zilizoanzishwa na Kano na Katsina dhidi ya watu wasio Wahausa wa Bauchi, Gongola, Jukum na Yawuri. Operesheni za kuizingira miji na "kuleta amani" zilichukua muda. Wahausa wengi wasio wanajeshi waliyafuata majeshi kwa ajili ya biashara au kwa sababu mbalimbali za kidini au huduma za jamii. Wengi wao hawakurudi tena nyumbani. Kwa hiyo, eneo la Kuyambane lililoko kusini mwa Katsina likaanzisha utawala wa Kihausa huko Yawuri katika nusu ya pili ya Karne ya kumi na nne. Wakanawa pia walifika Borno mnamo karne ya kumi na tano.



11.1 Wahausa na mataifa mengine ya Nigeria Kaskazini (M. Adamu).

Lakini, upanuzi mkuu wa Wa-Wahausa ugenini katika Afrika Magharibi ulikuja mara baada ya karne ya kumi na sita.

Kuenea kwa Uislamu

Tarihi ya Kano linasema kuwa Uislamu ulianzishwa na Wangarawa kutoka Mali katika karne ya kumi na nne wakati wa utawala wa Sarkin Yaji. Lakini kuenea kwa dini hii kwa hakika kulianza siku za nyuma zaidi kwani ilikuwa tayari imekwishafika Kanem-Borno tangu karne ya kumi na moja.

Maneno mengi ya Kiarabu yanayohusiana na dini yalikwishaingizwa kwenye Kihausa kupitia Kikanuri. Kwa hiyo Uislamu ulitokea mashariki, na mapokezi yanathibitisha ukweli huu. Zaidi ya hayo njia ya biashara kutoka Fezzan hadi Gao, ambayo ilikuwepo tangu karne ya tisa, ilikwenda hadi Gobir kupitia Marandet; uanzishwaji wa uislamu ni lazima utakuwa umekuja kwa kupitia njia hii pia, mapema kabla ya karne ya kumi na nne. Kwa kumalizia, hata kabla ya *Sarkin Yaji*, kulikwisha kuwa na Wahausa wengi waliokuwa na majina ya Kiislamu kama vile: Daud, Abdullahi, Salamata, *Uthman*, n.k.

Muswada uliogunduliwa hivi karibuni *Tarihi ya Wangarawa* ya mwaka 1650-1, umevuruga mambo zaidi kwa kutaja kufika kwa Waislamu wa Ki-Wangarawa miaka ya baadaye wakati wa utawala wa Sarkin Rumfa (karne ya kumi na tano). Lakini kupingana kwa taarifa zilizomo ndani ya maandiko haya kunamaanisha kuwa umuhimu wa kwanza upewe maelezo yaliomo kwenye *Tarihi ya Kano*, na itafsiriwe tu kuwa kinachotajwa katika *Tarihi ya Wangarawa* ni kuwasili kwa wasomi wa Kiislamu, ijapokuwa Uislamu ulikwishaletwa mapema zaidi na wafanyabiashara ambao walikuja kutoka Kanem, Gobir au hata Mali.

Zaidi ya hayo, Uislamu huu ulikuwa hasa ni dini ya watu wachache wa mjini wenye hali nzuri, yaani wafanyabiashara, wanasheria na mamwinyi. Umma mkubwa wa watu uliendelea kufuata imani zilizokuwepo kabla ya Uislamu. Lakini ilikuwa ni katika karne ya kumi na tano ambapo utamaduni wa Kiislamu wenye nguvu ulianza kupata mashiko. Wasomi wa Kiwanganarana na Kifulbe walishiriki kwenye jambo hili kama walivyofanya Waberiberi wengi wa Kiarabu; mtu maarufu zaidi miongoni mwao alikuwa Al-Moghili wa Tuwat. Yeye alikuwa msomi, mbishi, na mtesaji wa mayahudi na mnano miaka ya 1490 alitembelca Agades, Takedda, Kano, Katsina na Gao. Alikuwa na athari kubwa kwa watu wa kawaida, na kwa tabaka tawala, labda baada ya kumsilimisha *Sarkin* ambaye alimwandikia insha juu ya "Wajibu wa Wana Mfalme." Katika barua zake za baadaye alizomwandikia mfalme, alieleza fikra zake kuhusu serikali adilifu. Sio rahisi kuamini kuwa Rumfa alifuata ushauri huu, kwani *Tarihi ya Hausa* ilimlaumu kwa kufanya vitendo visivyo vya

Kiislamu.

Watu wengine maarufu waliacha athari zao. Al-Tazakhti (karne ya kumi na sita), msomi kutoka Timbuktu, aliporudi kutoka hija aliteuliwa kuwa kadhi wa Katsina. Ahmed Ibn Umar Akit, babu wa Ahmad Baba, alifundisha Kano katika karne ya kumi na tano.

Mwanahistoria wa Moroko. Abd al-Ratiman Sukkayn na mwenziwe Al-Balbali pia walifundisha katika nchi ya Wahausa. Kano ilianza kujitokeza kama mji wa Kiislamu; mageuzi yake yaliashiriwa kwa kukata miti mitakatifu enzi za Rumfa.

Uislamu ulikuwa pia unasonga mbele katika dola nyingine za Wahausa kipindi hiki. Kwa mfano, huko Zaria na katika Kebbi ambako Muhammad Kanta alikuwa kiongozi katika jeshi la mcha Mungu Askiya Muhammad. Watawala wengine waliofuata wana majina ya Kiislamu, ijapokuwa Kebbi ilibaki imejiegemeza kwenye dini ya kiasili.

Mji wa Yawuri, ambao uko kwenye njia ya zao la kola kati ya Gonja na Borno, huenda nao ulikuwa na vikundi vidogo vilivyosilimishwa. Zaidi ya hayo, kwa kiasi fulani, Uislamu huu ulijirekebisha na kujumuisha mawazo ya kidini na desturi za awali za kitamaduni na kijamii za Wahausa. Haya ndiyo yaliyokuwa malipo ya kuufanya Uislamu ukubalike na kusonga mbele. Hii ndiyo maana ijapokuwa wasomi na wanafunzi wao walifuata Uislamu safi, kulikuwepo pia mifumo mseto mbalimbali miongoni mwa jamii.

Katika uwanja wa siasa, Uislamu umechangia katika kujenga mfumo wa mamlaka kuu moja, kwa kubomoa miundo ya kijadi iliyojikita kwenye udhibiti wa sehemu za kijadi za kuabudia. *Tarihi ya Kano* ambayo inatoa maoni rasmi ya watawala wa Kiislamu, ina hadithi nyingi zinazoelezea upinzani wa machifu wa kijadi waliotambuliwa kama "makafiri". Viongozi hawa, ambao walipinga kuwekwa kwa madaraka yote mikononi nwa watawala wa Kiislamu wa Kano, ilibidi washuhudie uharibifu mkubwa wa sehemu na vifaa vyao vya kuabudia. Santolo ilikuwa ya mwisho kuharibiwa miongoni mwa sehemu hizi takatifu.

Hatimaye, kujaa kwa wasomi wa Kiislamu kulimaanisha kuwasili kwa mawazo mapya, kuenea kwa stadi ya kujua kusoma na kuandika kwa Kiarabu (mfumo wa *Kiajami*). Uongozi wa biashara na utawala ulinufaika sana na maendeleo haya.

Mfumo wa kisiasa na kiutawalawa

Sura mbili za msingi za kimuundo ambazo ni za kawaida kwa tawala za

Wahausa zilikuwa kwanza, msingi unaofanana wa kijamii na kiutamaduni unaotambulishwa na lugha moja, na pili, athari za Kanem-Borno ambazo kwa muda mrefu zimekuwa ndizo kielezo cha ustaarabu. Licha ya mashambulizi ya Borno na kodi ilizotoza, haikuonekana ni adui kama ilivyokuwa Songhai au Kwararafa.

Wahausa pia walijenga umoja wa kutegemeana uliotokana na upekee wa mazingira yao. Kwenye shina la muundo wa kijamii kulikuwa na ukoo wa kifamilia (*gida*). Juu yake kulikuwa na kijiji na chifu wake (*sarkin gari*) kileleni kulikuwa na mji uliojengwa ngome unaotawaliwa na chifu wa nchi (*sarkin kasa*). Miji hii iliyojengewa ngome na ambayo ilitapakaa karibu nchi nzima ilikuwa na dhima ya chachu ya maendeleo ya kijamii na kisiasa kutokana na kuwepo kwa raslimali nyingi za kilimo na ufundi; kuwepo kwa biashara ya mbali, na mwishowe kuwepo kwa ulinzi wa uhakika patokeapo machafuko.

Mchanganyiko wa watu wake wa mjini ulikuwa ni kichocheo cha ugunduzi. Mfalme (*sarki*) ambaye alikuwa mtukufu aliwajibika kwa ustawi wa watu wote na alikuwa na mamlaka yote ambayo alishirikiana na maafisa wachache wa ukoo wake au ukoo wa karibu. Baraza la nchi liliwajibika kumshauri mtawala na kumchagua mtu atakayemithi. Huko Gobir baraza hilo liliitwa "tisa wa Gobir" (*tara ta Gobir*) na huko Kano liliitwa "tisa wa Kano" (*tara ta Kano*). Watumwa wa Mfalme walijishughulisha zaidi na zaidi kutunza kaya ya mfalme na ofisi za serikali.

Ofisi ya *galadima* ambayo ilikuwa kama ofisi ya waziri, wakati mwingine ilishikwa na mfalme mtarajiwa. Galadima mwenye nguvu aliweza kumfanya mfalme kikaragosi wake; ndiye aliyewadhibiti viongozi maarufu na maafisa wa ngazi mbalimbali za utawala.

Ilikuwa ni karibu mwaka 1530 ambapo ukuaji wa ukiritimba wa madaraka uliongezewa kasi na Uislamu pamoja na kukua kwa biashara ya watumwa na athari za watumwa wa Mfalme katika vyombo vya serikali. Mambo haya yalidhoofisha mamlaka ya kinasaba yaliyokuwepo kabla. Taratibu mpya alizozianzisha Rumfa (kukamatwa kwa mali na wanawake, na haki ya kukusanya wananchi kwa kazi za shurti) zinadhahirisha mabadiliko haya makubwa katika mfumo wa jamii.

Maendeleo ya kiuchumi

Nchi ya Wahausa ilikuwa na raslimali nyingi za kiuchumi
Madini ya chuma yaliyokuwa karibu na cncu lenye msitu yalichimbuliwa ili

kuhakikisha kuni zinazohitajika zinapatikana kwa urahisi. Utafiti wa kiakiolojia unathibitisha ripoti zilizomo ndani ya *Tarehe ya Kano* kuhusu suala hili. Udongo wenye rutuba ulikifanya kilimo kiwe shughuli muhiinu sana kwenye falme zote za Wahausa. Licha ya kukosekana kwa takwimu za kihistoria, idadi ya vijiji na miji inaashiria kwamba nchi ya Wahausa ilikuwa na watu wengi sana na kwamba idadi ya watu ilisambaa sawasawa nchi nzima. Zaidi ya hayo, sehemu ilipo nchi ya Wahausa katika Sudan (kati ya mashariki na magharibi ya eneo hili kubwa, na kati ya jangwa na msitu), imeipa fursa nzuri kwa aina zote za biashara kuelekea pande zote. Hii ndiyo sababu biashara na ufundi ulistawi mapeina katika eneo hili.

Lakini ijapokuwa Mhausu alikuwa na hali bora katika eneo hili, kabla ya yote, kila Mhausu kwanza alikuwa mkulima. Ardhi ilimilikiwa na jamii na haikuuzwa. Kila mmoja alinufaika na haki ya kutumia ardhi chini ya uangalizi wa chifu wa jamii. Kutokana na kukua kwa utawala mkuu pamoja na madaraka kubinafsishwa, Mfalme (*sarkin*) alianza kugawa ardhi kwa watu binafsi. Wakulima waliwekwa chini ya madaraka ya chifu wa mazao (*sarkin noma*) ambaye wajibu wake ulikuwa ni kufuatilia mienendo ya majira na kufanya matambiko yanayotakiwa ili kuhakikisha mavuno mazuri.

Mwishowe, aina tatu za mashamba zilijitokeza: Shamba la mfalme (*gandum sarkin*) ambalo lilitambulika kwa ukubwa wake; shamba la familia (*gandum gide*); na mwisho, shamba la mtu binafsi (*gayauna*). Kazi za watumwa zilitumika sana katika shamba la mfalme, kadhalika katika mashamba makubwa ya maafisa wa serikali. Wakati wa utawala wa mfalme wa Kano Abdullah Burja (1438-52), maelfu ya watumwa waliishi Kano na vitongoji vyake na wengi wao walitunikishwa katika kazi za kilimo. Mazao makuu yalikuwa mtama, ulezi, fonio na mpunga (hasa kule Kebbi na wilaya za magharibi). Pamba na nili zilipandwa kama mazao ya biashara.

Kazi za ufundi wa mikono zilikuwa ni sekta ya pili muhimu katika uchumi wa Wahausa na zilifikia kiwango cha juu sana cha ubobezi. Fani iliyokuwa inaongoza ni ya viwanda vya nguo na utiaji rangi, ikifuatiwa na kazi za ugozi ambazo zilizalisha vitu vya aina mbalimbali vilivyozwa hadi Afrika ya Kasikazini.

Wahunzi waliosifika kwa ujuzi wao walitengeneza silaha na zana na vyombo vya nyumbani vilivyohitajika kutokana na mawe ya chuma (*marmara*). Ufundi wa vyombo vya udongo ulifanya hivyo hivyo.

Kazi nyingi za ufundi ziliongozwa na ushirika wa uzalishaji na kila ushirika ulikuwa na kiongozi aliyechaguliwa na Mfalme, mara nyingi miongoni mwa waliopendekezwa na wanachama. Ushirika ulidhibiti mbinu za uzalishaji,

vivango vya ufundi, bei na uingizaji wa wanachama. Mahali palipopendelewa kufanyia biashara palikuwa ni gulioni (*kasuwa*) na mtu aliyekuwa mfawidhi wa gulio (*sarkin kasuwa*) na wasaidizi wake walidumisha utulivu, waliamua ugomvi, na walikusanya kodi ikiwa ni fedha au bidhaa. Gulio lilikuwa pia mahali pa maisha ya kijamii na mahali pa mikutano ya kijamii.

Wahausa walipambanua wazi kati ya biashara za maskanini, biashara ya kanda na biashara za masafa ya mbali, zilizounganishwa na watu wa kati baina ya wauzaji wa jumla na wale wa rejareja. Zaidi ya hayo, kulikuwa na mgawano wa shughuli kufuatana na bidhaa: Nyama, nafaka n.k.

Dalali, ambaye alikuwa anapata kamisheni kwa huduma zake, alikuwa mtu muhimu sana kwa vile alikuwa anajua bei zinazotumika katika kila soko, katika kanda, na aliweza kutabiri mabadiliko ya upatikanaji wa bidhaa, mahitaji na bei, na kufanya ulanguzi kutokana na ujuzi wake. Lakini shughuli muhimu mara nyingi ilifanyika nje ya soko: viwandani, au nyumbani kwa wafanyabiashara au kwa mamwinyi kwenye jumba la mfalme, kwani watu hawa kutokana na vyeo vyao wasingaliweza kufika sokoni. Wanawake pia walichangamkia masoko wakishughulika zaidi na vyakula.

Biashara ya kubadilishana bidhaa ilishamiri pia. Majora ya nguo za pamba, chumvi, na watumwa vilitumika kama fedha. Kwa upande wa kauri ambazo zilikwisha kuwa zinatumika huko Mali na Songhai, zilianza kutumika Kanem katika karne ya kumi na tisa; kwa mujibu wa chapisho la hivi karibuni, kauri zilitumika Katsina katika karne ya kumi na sita kwa biashara ndogondogo.

Kutokana na kasi ndogo ya kuchipuza serikali kuu katika nchi ya Wahausa ukilinganisha na majirani zao wa upande wa mashariki na magharibi, nchi hii ilichelewa kushiriki kwenye biashara ya masafa ya mbali. Mchango wa Wangarawa kwenye biashara hii umetiwa chumvi mno, kwani walikuwepo pia Waafrika wa Afrika Kaskazini, Watuareg, Wakanuri na, kuanzia karne ya kumi na tano, Wahausa wenyewe ambao walidhibiti njia fulani fulani, hasa zile zilizoelekea kusini. Kano na Katsina vilikuwa ni vituo vikuu vya biashara katika biashara ya Kaskazini-Kusini.

Lakini Wahausa walifanya biashara sehemu mbalimbali kama orodha ya bidhaa inavyoonyesha:

Bidhaa za Wahausa: nguo za pamba, ngozi, mazao ya kilimo, manyoya ya mbuni, gundi na shanga za kioo.

Bidhaa za Afrika Kaskazini na Ulaya: Vyombo vya metali, silaha, farasi, shanga, na vitambaa vya fahari.

Bidhaa za Sahara: mikuo ya bati kutoka machimbo ya Takedda, chumvi na natroni kutoka Bilma iliyouzwa hasa kupitia Agades na Gobir.

Bidhaa za Kusini: watumwa, kola, meno ya tembo na dhahabu.

Ingawa ni kweli kwamba wafanyabiashara wa Afrika ya kaskazini waliitawala biashara upande wa kaskazini wa mtandao huu, tabaka tawala na lenye kumiliki mali la dola za Kihausa nalo lilipata faida kutokana na hali hiyo kuanzia karne ya kunii na tano. Faida hiyo ilichochea ustawi uliomwezesha Rumfa, kwa mfano, kuanzisha programu kabambe ya ujenzi pamoja na mageuzi mengi.

12

Watu wa Pwani kuanzia hadi kwenye nyangwa za Cote d'Ivoire Makutano ya mwanzo na Wareno

Sifa za jumla za eneo hili

Kwa mabaharia wa mwanzo wa Kireno, nchi ya Guinea ilidhaniwa kuwa ndiyo Ethiopia, na ilianzia Gambia hadi delta ya mto Niger (unapoingilia baharini); Guinea ya Juu ilijumuisha eneo kati ya Gambia na Bandama. Eneo hili sio la msitu lakini pia sio nyika tena. Watu walitawanyika na kugawanyika katika makundi mengi ya kikabila. Wamande walivutiwa na eneo hili kwa sababu ya kola, dhahabu na watumwa.

Shauku juu ya pwani hii ilizidishwa sana na ujaji wa Wazungu mnamo karne ya kumi na tano. Pwani ya Atlantiki iliacha kuwa sehemu iliyo nyuma kimaendeleo na ikawa ndiyo mlango wa kukaribisha ulimwengu wa Ulaya na Marekani. Kwa bahati mbaya ulikuwa mlango ambao baada ya muda mfupi tu biashara ya watumwa ikawa ndiyo shughuli yake kuu. Katikati ya mikingamo hii wenyeji walijitahidi kutunza utu wao na kuyamiliki maisha yao wenyewe.

Eneo la msitu lilihusishwa na biashara ya masafa marefu inapema mno tangu karne ya kumi na mbili, kwani wakati huo kola tayari zilikwisha kuwa zinafika Afrika ya Kaskazini. Katika eneo hili la msitu bidhaa kutoka kaskazini zilichukuliwa na makundi ya koo bila kutumia wafanyabiashara maalum. Biashara ya pilipili (ya) *malaguetta*, ambayo awali ilipelekwa kuuzwa Ulaya kupitia Maghrib, ilichepushwa baadaye na kuelekezwa pwani.

Mfumo wa makazi ya watu katika eneo hili unaonekana kwenye Tarche za Wareno za wakati huo. Maeneo ya pwani yenye kinamasi yalikuwa na sehemu zenye tope ambazo zilifaa kwa ulimaji mpunga. Bahari yenyewe haikuwaathiri sana watu wa pwani ambao kimsingi walikuwa wakulima ambao pia walijihusisha na utengenezaji chumvi kwa ajili ya kuuza kwa watu wa bara. Bidhaa kuu mbili za biashara ya kuvuka Sahara ambazo pia, kwa kiasi fulani,

zilichepushwa na kuelekezwa sehemu hii ya pwani, zilikuwa dhahabu na watumwa.

Maendeleo ya nchi za Guinea ya juu

Hali ya Utafiti

Hapa tutatoa maelezo ya awali tu ya historia ya maeneo haya, kwani masimulizi ya mapokeo hayarudi kwenye tarehe za nyuma sana katika eneo hili, na utafiti wa kiakiolojia ndiyo kwanza unaanza. Kwa hivyo, inatubidi tutumie mbinu ya kurejelea, tukianza kwenye hali ya sasa ya kiantropolojia na kujaribu kukisia hali ilivyokuwa hapo nyuma.

Kuanzia Kasamansi hadi Mlima Kakulima

Karibu sana na kusini mwa Senegambia kwenye mwingiliano wa hori za Kasamansi na Rio Kacheu wanaishi Wabalante, Wajoola, na Wafelupe. Wabainuk wanachukuliwa kuwa ndio wenyeji; ambapo Wabiafada na Walanduma walikuwa chini ya utawala wa mansa wa Kimande liadi katikati ya karne ya kumi na sita ambapo walikuwa tawala zenye kujitegemea. Wabiafada walipambana na Wabijago ambao waliishi kwenye visiwa vilivyojengewa ngome na waliishambulia bara hadi karne ya kumi na tisa. Mashua zao kubwa ziliweza kubeba hadi watu 120.

Huko bara, kuanzia Gambia ya Juu hadi chini ya vilima vya Futa Jallon, waliishi Watenda (Wabassani, Wakoniagi na Wabadiaramke). Watu hawa waliishi katika jumuiya luru za vijijini na kwa ukaidi walipinga kutawaliwa na askari wa Kimande na Kifulbe.

Nchi za Walanduma, Wabaga na Wanalu zilianzia Rio Grande hadi Rio Pongo. Hawa walikuwa wakulima wa mpunga na wavuvi ambao waliishi kwenye vijiji vilivyojengwa katikati ya kinamasi au wakati nwingine kwenye mifereji.

Mabaharia wa Kireno wanatoa taarifa kuwa pwani liizi zilikuwa na watu wengi; lakini "wafalme" ambao wanawataja bila shaka walikuwa kwa kiasi fulani kama wazee wenye heshima au wakuu wa koo. Valentim Fernandes aliandika kuhusu msaada wa bure waliopewa "wafalme" na raia wao kwenye kazi za shambani na ujenzi. Lakini ilipofikia suala la kwenda vitani baraza la wazee liliweza kusesitiza juu ya amani kama liliona kuwa "vita hivyo havina uhalali au kama adui ana nguvu zaidi." Kwa hali hiyo, hizi zilikuwa ni jamii za kidemokrasia za vijijini.

Dini ya asili ndiyo iliyotawala bila upinzani. Watu waliabudu "mizimu"

iliyowakilishwa na sanamu zilizotengenezwa kwa miti na sanamu kuu iliitwa Kru. Wanyama walitolewa kafara kwa wafu ambao walitengenezwa sanamu ndogo kwa kutumia mawe maalum ya mapambo au miti. Mizimu hii ilijulikana kama *nomoli* au *pomta*.

Kuanzia Mlima Kakulima hadi nchi ya Kru

Watemne walitawala eneo la kusini mwa mlima Kakulima; ambapo majirani zao walikuwa Wabulom na pia Wakissi upande wa bara. Makundi haya mawili yalizungumza lugha ya Kisherbro. Watu hawa waliishi kwenye vijiji vilivyojitawala yenyewe (miongoni mwa Wabulom, kila kijiji kilikuwa na wakazi kiasi cha 3,000) chini ya mamlaka ya jamii za siri za (majuso) ambazo zililusika na shughuli za jando; kama vile jamii ya *Wasimo*. Ulimaji mpunga ulitoa chakula cha ziada ambacho Wareno walikinunua. Wabulom, ambao walikuwa wavuvi maarufu waliotumia mashua kubwa sana, walikuwa pia ni wasanii bora sana ambao walichonga sanamu za miti na pembe za ndovu; waliziuza kazi zao za sanaa kwa Wareno.


Utamaduni wa Watemne, ambao unaanzia karne ya kumi na tatu au kumi na nne, ulikuwa umecenezwa bara Wareno walipofika. Lakini Wasoso, waliowatangulia Wamande, tayari walikuwa wanaanza kuwasukuma kuelekea kusini. "Himaya ya Wasape" ambayo Wareno wanaitaja kuhusiana na Watemne haikuwa kitu kingine zaidi ya temi na koo nyingi zilizounganishwa na utamaduni mmoja uliosonga mbele kwa kujieneza polepole badala ya kutegemea uhamaji wa ghafla kwa makundi ya watu.

Kusini zaidi, walikuwepo Waku hadi Bandama kwenye kanda ya msitu. Hawa walikuwa wavuvi zaidi, kwani mpunga ambao ulikuwa umetokea nchi ya Wamande ulikuwa haupandwi sana. Hivyo eneo lao lilipanuka hadi Seguela, ambako walifukuzwa na Wamaninka mnamo karne ya kumi na sita.

Athari ya Savana

Watu ambao hasa walihusika katika eneo hili walikuwa Wamande na Wafulbe. Wamande walijikusanya kwenye vijiji vilivyowekwa pamoja kufanya *kafu* (tarafa), kisha katika falme, na hatimaye kuwa himaya ambayo haielekei kuwa mamlaka yake ya kisiasa yalivuka mpaka unaoanzia Kurusa kupitia Kankana hadi Odienne. Lakini watawala walielekea wakati wote kuhimiza uhusiano mzuri na watemi wa eneo la msituni.

Upande wa mashariki wa Futa Jallon ambapo mamlaka ya Mali yanaelekea kuwa hayakuwepo, upanuzi wa taratibu wa mamlaka uliongozwa na wakuliina



12.1 Poryolano ya Mecia de Viladestes, 1413
(ramani ya rangi iliyocharwa kwa mkono)



12.1 (Maendeleo)



12.2 Pembe za ndovu wa Afrika zilizochongwa meli na askari wa Kireno
(W.Fagg, *Afro-Portuguese ivories*, 1970, London. Picha © Warner Forman Archive)

walioungwa mkono na askari. Kisha koo kuu za kifalme zililazimisha utawala wao, kama vile Wakonde kutawala Niger ya Juu, na Wakuruma na Wakonate kutawala kuanzia Kankan hadi Odienne mnamo karne ya kumi na nne na ya kumi na tano.

Kusini zaidi, inaelekea watu waliokuja mwanzo walikuwa Wajoola ambao walifika Ghuba ya Guinea. Magomvi yao na wenyeji wa asili yalisababisha wawaite askari wa Kimaninka ambao waliingiza wakulima na kuwawekwa wenyeji wa asili (Wakuranko, Wakoninke n.k.) utaratibu wa kiutawala. Baadhi yao, kama vile Wavai na Wakono, walifika baharini mapema sana mnamo karne ya kumi na tano. Yaelekea kuna hakika kwamba Wakamara wa Konianke ndio waliohusika na uvamizi wa Wasomba ambao ulifika pwani mnamo 1550.

Lakini kikosi tangulizi hiki cha Wamaninka hakikuelekezwa pwani, bali kilielekezwa kwenye maisha ya kibiashara na kisiasa ya Sahel na kaskazini. Ilikuwa ni mwishoni mwa karne ya kumi na saba tu ambapo biashara ya watumwa iliifanya pwani kuwa muhimu zaidi na kuanzisha mlipuko wa watu wa Niger ya Juu kuwavuruga watu wa pwani, na hatimaye Wamande wengine wa bara.

Nchi za Wamande au majimbo ya pwaniya pwani

Mnamo karne ya kumi na tatu, mfuasi wa Sundiata, Tiramaghan Traore, alilazimisha utawala wa himaya ya Mali, ambao ulimiliki maeneo yenye dhahabu ya Senegal ya Juu na Niger ya Juu katika Senegambia. Umiliki huu ulijikita hasahasa kuanzia Gambia hadi chini ya vilima vya Futa Jallon. Dola hili kubwa la Kaabu lilidumu hadi karne ya kumi na tisa. Liliipatia Mali njia ya kutokea baharini, liliunganisha chini ya himaya yake falme nyingi ambazo mara nyingi zilikalwiwa na watu ambao hawakuwa Wamande (Wakokoli, Wabafada, Waniumi, Wabadibu, Wavuli n.k). Wabalante waliendelea kuwa wakaidi. Utamaduni wa Kimande ulitawala katika eneo hili lakini uhuru wa ufalme huu ulikuwa halisi na ukoo wa kifalme ulichukua mfumo wa urithi kwa upande wa mama. Wagelowa wa falme za Sereer walitokea kwenye ukoo huu wa kifalme kabla ya kufika kwa Wareno.

Katika Kasamansi ya chini Wabainuk-Kassanga, ambao jina lao la kifalme (*Kasa-Mansa*) ndilo lililotolewa kuwa jina la mto huo, walihifadhi utambulisho wao hadi waliposambaratishwa na Wabalante mnamo karne ya kumi na tisa.

Tukio ambalo lilikuwa na athari kubwa hapa lilikuwa lile la kufika kwa Wareno katika Gambia mwaka 1446 na huko Rio Grande mwaka 1456. Tukio hili liliashiria kuifungulia Mali milango ya dunia mpya, hasa kwa vile mto Gambia ulikuwa njia ya maji yenye kupitika kwa urahisi, hivyo ikawa njia

mojawapo kuu ya kuingia bara. Hii ndiyo iliyokuwa njia ambamo dhahabu na watumwa kutoka Mali walipitishwa na kuuzwa nje, na ambamo mabalozi wa Kireno huko Mali walipitia mnamo karne ya kumi na tano. Kadiri ufalme wa Sereer wa Salum ulivyopata nguvu mnamo karne ya kumi na saba, ndivyo ulivyoweza kuziingiza falme za Wamaninka chini ya himaya yake kuelekea kaskazini mwa mto Gambia (Niumi, Nyaani). Wakati huo biashara ya watumwa ilitawala kila kitu.

Kuhusu Kaabu, ambayo bado ilikuwa inatii himaya ya Mali, ilibanwa kwenye kingo za kusini za mto Gambia (Kantora) na ilifanya mawasiliano na Wareno kwenye mito ya Rio Kacheu na Rio Grande. Bambugu ilibakia chini ya utawala wa Mali hadi iliposhindwa kabisa mkabala na Jenne mnamo 1599. Machimbo ya madini yalitekwa na mamluki wa Kireno wakiongozwa na Myahudi aliyelitwa Ganagoga kwa niaba ya Wadenianke wa Futa Toro (iliyofahamika kama "himaya ya Ful kuu"). Tangu wakati huo, Kaabu ilitengwa na Mali kadiri ilivyocndelea kudidimia (t.1600).

Kusini zaidi, kwenye uwanda wa juu wa Futa Jallon, waliishi Wajallonke na Wasoso ambao walizungumza lahaja za Kimande. Wajallonke walikuwa kwenye temi ndogo ndogo zilizokuwa ndani ya himaya ya Mali. Wasoso hawakuwa na muundo kamili kama wenzao. Walikuwa na jumuiya ya *simo* ambayo ilikuwa na asili ya Kitemne au Kibaga. Wabaga na Wanalu bado walikuwa wengi kwenye mabonde ya Futa Jallon; baadaye walitimuliwa huko na *jihadi* ya Wafulbe mnamo karne ya kumi na nane.

Wafulbe na Watu wa Futa Jallon Jallon

Ilikuwa mnamo mwaka 1450 ambapo Dulo Demba, ambaye alikuwa kwenye kundi la

Wafulbe lililotokea Futa Toro, aliwashambulia Wabiafada ambao bado walikuwa raia wa Mali. Ilikuwa ni kwenye nchi ya Jallonke alikokuwa anaishi ambako Tengella alianza kupigana na majeshi ya Kaabu na kisha Songhai, kabla ya mwanae Koly kuanzisha nasaba ya ufalme wa Denianke huko Futa Toro.

Futa Jallon ilikuwa imeunganishwa kiishara tu na himaya ya "Ful Kuu", lakini Wadenianke hawakuwachukua Wafulbe wote wakati walipoondoka. Wengi waliselea baina ya Wasoso na Wajallonke. Waliungana na Wasoso kuzuia uyamizi wa Wamane ambao walikuwa wameyashinda macneo yote ya kusini. Wafulbe hawa waliendelea kuelukua nafasi yao duni hadi majilio ya Waislamu yaliyowawezesha kuwatiisha Wajallonke mnamo karne ya kumi na saba baada ya *jihadi*.

Hali ya Wasoso ilibadilika kabisa kwanza kutokana na wingi wa biashara mpya ya dhahabu iliyofanywa na misafara ya Wadiakhanke wa Bure na merikebu za Wareno. Wasoso, kwa kufuatia nyendo hizi, waliwafukuza Wabaga na Watemne kuelekea Rio Pongo. Uislamu haukuwa na athari kubwa kiutamaduni hadi mwishoni mwa karne ya kumi na saba.

Mkabala wa msitu kuanzia Niger ya juu hadi Sassandra ulikaliwa na Wamande wa kusini kama vile Wakuranko (Wakonianke na Wamau). Wajuula, wakiwa kama madalali, walianzisha biashara ya kola, ambayo wazalishaji wake waliwaona kama "washenzi", iwe walizungumza Kimande — kama vile Waguro, Wadan au Watoma — au lugha ya Kimel kama vile Wakissi. Wenyaji hawa ama walimezwa ama walifukuzwa. Wakati huo huo, makazi ya askari, wakulima na wafanyabiashara yalianzisha muundo wa sasa wa mchanganyiko wa watu kuanzia karne ya kumi na tano, yaani wakati ambapo kuondoka kwa Mali kuelekea kaskazini kuliwafanya wengine waelekeze nguvu zao kusini.

Wamande wakiingiliana na Wakissi na Watoma walitamakani Sankaran na Toron, mashariki ya Niger ya juu, mapema mnamo karne ya kumi na nne. Mwishoni mwa karne ya kumi na moja, eneo la Konianke na Tuba ambalo ni uwanda wa juu na lililokuwa mahali pazuri pa kuweza kuitawala pwani, likawa chini ya utawala wa koo za Kamara na Dyomande. Koo za Wafulbe zilizofika katika karne ya kumi na saba zilianza kuzungumza lugha ya Kimaninka.

Wamande walijaribu mara mbili kuvuka mpaka wa msitu.

Wakono na Wavai

Huenda katika kiu ya kutaka chumvi na samaki, Wamande waliotamakani katika kanda ya msitu kabla ya kufika Wareno, wakiongozwa na kina Kamara, walisogea kusini kuelekea baharini, kwenye mpaka wa sasa kati ya Liberia na Sierra Leone. Baadhi yao walibaki katika nyanda za juu baada ya kumsubiri bila mafanikio mjumbe kutoka kundi lililotangulia, na kwa sababu hiyo wakaitwa Wakono (kutokana na neno *kono*, "subiri"). Wengine wakiongozwa na Kamara mdogo, wakawaratibu Wavai waliokuwa pwani. Walikuwa na kuku wengi sana hata Wareno wakawapa jina la *Galinhas*. Wanaonekana kuwa waliendelea na muundo wa siasa wenye mamlaka kuu.


Vamizi la Mane au Mandela

Uvamizi wa Mane-Sumba na Kwoja-Karu ni schemu ya mihamo ya watu iliyozikumba kanda zote za bara la Afrika, kama ile ya Wajaga katika Angola
Mchoro 12.3



12.3 Kijiji cha Kiafrika (Makumbusho ya Uingereza, London)

12.4 Mfalme wa Sestro (katiba ya kumi na saba)
(Makumbusho ya Uingereza, London)



au Wazulu katika karne ya kumi na tisa. Lakini haikubadili ramani ya kijami-kiisimu.

Uvamizi wa Mane unahusika na kuenea kwa lugha ya Mande na hata kwa uundwaji wa kundi la Loko, lakini, zaidi ya yote, ulichangia katika usambazaji wa asasi unganifu za kisiasa na katika upanuzi wa mtandao wa biashara ya masafa marefu ya Sudan.

Inaonekana kuwa upanuzi wa Mane ulikuwa ni jitihada za Wamande ambao tayari walikuwa na uzoefu katika biashara ya dhahabu. Kwa kuwa tayari Wareno walishakuwapo kwa miaka themanini, hamu ya kuanzisha njia ya biashara ya moja kwa moja kwenda pwani ilikuwa dhahiri. Kundi hili dogo likiwa na utaratibu bora wa kisiasa na kijeshi lilifanikiwa katika kuwahamasisha wenyeji, kundi moja baada ya jingine, na hivyo kuendelea mkumbo mmoja hadi pwani.

Visiwa vya Cape Verde

Visiwa vikame vya Cape Verde vilianza kukaliwa mnamo 1462 kwa mtindo wa Madeira na baadaye kurejea kwa utawala wa Ureno katika mwaka 1484. Makao makuu yalianzishwa Santiago, kisiwa kilichokuwa karibu sana na bara, ambacho kilikuwa makazi ya gavana na askofu ambao mamlaka yao yalinea hadi pwani ya eneo la bara.

Kwa haraka visiwa hivi vikakaliwa na watumwa walioletwa kutoka bara. Katika mwaka 1582, visiwa viwili vikuu, Fogo na Santiago, vilikuwa na wakazi 1,600 weupe, watu weusi huru 400 na watumwa 13,700. Msingi wa uchumi ulikuwa ufugaji, kilimo cha pamba na ufumaji, kwa kutumia mbinu za Kiafrika.

Baadaye, watumwa waliingizwa kisiwani kwa ajili ya kusafirishwa tena kwenda Marekani ya Hispania katika karne ya kumi na sita, kwa kiasi cha kama watumwa 3,000 kwa mwaka, kwa kubadilishana na nguo za pamba kutoka Cape Verde.


Ukoloni wa Wareno ulikuwa umckitwa kwenye misingi ya ukiritimba wa ufalme kwenye biashara, ambao ulitolewa kwa wenye vibali kwa vipindi na maeneo maalum. Mkataba wa 1466 uliwapatia wakazi wa visiwa hivi haki ya kufanya biashara na pwani ya Senegambia, lakini kanuni ya 1514 ilizuia uhusiano wowote na bara. Sababu ilikuwa ni kusimamisha shughuli zote za *Lançados* (kutokana na *Lançar*: kuanzisha safari za kijasiri), ambao walifikia mapatano na watawala wa Kiafrika kulowea bara, kuiga desturi za wenyeji na kuanza kuishi kama wafanyabiashara huru.

Na ilikuwa kweli kuwa wengi wa malanzado hawa walitokana na matabaka ya chini ya jamii, hasa "Wakristo wapya", yaani Wayahudi ambao waligcuzwa

kuwa Wakristo kwa nguvu.

Hitimisho

Kutokana na kufunguliwa hivi karibuni kwa hifadhi za Lisbon na kuanza kwa taaluma za akiolojia, historia ya eneo hili ni wazi itatajirishwa. Tayari ni dhahiri kuwa eneo hili halikuwa limetengwa au kuwa pkee. Uvamizi wa Wamande na Wafulbe, biashara ya kola na bidhaa zingine za msituni, himaya za pwani zenye nguvu kama zile za Kaabu na Konianke, shughuli za Wareno kuanzia karne ya kumi na tano — haya yote ni mambo yaliyohusisha eneo hili na dunia jirani ya Afrika na Ulaya. Baadhi ya jamii, kama vile Wanalu, Wabago na Wabulom, zinafahamika kwa umaarufu wao katika uchongaji. Ubingwa wa kulima mpunga wa baadhi ya jamii ulifanya eneo hili kuwa ghala la nafaka kwa eneo la savana ambalo wafalme wake kwa kawaida waliendeleza uhusiano mzuri na machifu wenycji.



Kuanzia Wangwa wa Cote d'Ivoire hadi Volta.

Nchi

Kutoka rasi ya Palmas, pwani imepinda kutoka Kusini Magharibi hadi Kaskazini Mashariki katika umbo la nusu duara ambalo linauuda Ghuba ya Guinea. Sura nyingine ni kuwepo kwa wangwa kwenye mwambao wa pwani. Hali ya hewa ni ya kiikweta, yenye mvua nyingi isipokuwa sehemu inayoelekea mlango wa mto Volta ambapo mbuga za majani zinaehukua nafasi ya msitu.


Matatizo ya vyanzo

Vyanzo vya Maandishi

Kutoka mwaka 1471, nehi iliyopo kati ya rasi ya Palmas na mlango wa mto Volta ilipelelezwa na Wareno ambao waliacha taarifa kuhusu safari zao. Mnamo mwaka 1481, walianza kujenga ngome ya El Mina, mahali madhubuti palipodhibiti biashara kwenye mwambao wote wa pwani. Maandishi ya Duarte Pacheco Pereira yaitwayo *Esmeraldo de Situ Orbis* (karne ya kumi na sita) na baadaye maandishi ya Dapper yaitwayo *Description of Afrika* "Maelezo kuhusu Afrika" ambayo ni mkusanyiko wa taarifa za kale, ni nyaraka za thamani kubwa kwa wanahistoria.

Kwa mfano, watu ambao Pacheco Pereira anawaita *Eguorebo* ni Wagrebo wa Rasi ya Palmas. Mito imerekodiwa kwa uangalifu. Mto Santo Andre au Sassandra una mashamba ya mpunga "harrari", na mto Rio Laguo a unaweza kutambuliwa kama *Lahu Kuu*.

Nje ya eneo hili, Pacheco Pereira aliwatambua watu wajulikanao kama Kru kuwa ni watu wabaya, na adui kwa mabaharia. Ugunduzi wa dhahabu katika eneo hili ndio uliochochea ujenzi wa El Mina ambapo mfalme wa Ureno alituma



13.1 Bangili la kuvaa mkonoi lililopatikana huko Séguié (Taasisi Ya Historia, Sanuu na Akiolojia ya Afrika, Abidjan).

meli tisa zilizojaa mawe na chokaa. Ngome ilijengwa bila kujali kuwepo kwa vitisho vilivyoendelea vya wenyeji ambao walichukia kujengwa kwake. Lakini ngome hii ikawa kitovu cha biashara; Waattie (Atty), Wahakanyi (Akan), Wagoroe (Abron) na Wamandingo (Mande) walileta na kuuza dhahabu hapo.

Eneo kati ya Bandama na Rasi ya Three Points liliitwa Pwani ya Pembe (za Ndovu) au *Ivory Coast*. Eneo lililjulikana kama Pwani ya Dhahabu *Gold Coast* lilianzia Rasi ya Three Points hadi mto Volta. Vijiji vingi hutajwa na Wareno ambao pia wanatoa taarifa muhimu kuhusu mila za watu wake.

Vyanzo vya Kiakiolojia

Ufukuaji wa Begho kwenye nchi ya Bron, katika ukingo wa Kaskazini wa msitu, unaonyesha kuwa vitu vingi vya kiutamaduni vimetoka Jenne. Mtaalamu Posnansky anadhani kwamba uhusiano mkubwa wa biashara wa muda mrefu ulikuwepo kati ya msitu na savana. Kuwepo kwa koloni kubwa la Juu la katika eneo hili ni ushahidi wa uhusiano huo. Kwa mujibu wa vitu vilivyochimbuliwa katika eneo la Nyarko huko Begho, inaonyesha kuwa eneo hili limeanza kukaliwa karibu mwaka 1100. Eneo hili lilikuwa moja ya masoko yaliyokuwa yakiongoza kwa biashara ya kola na dhahabu ambayo ilikuwa inauzwa kwa wingi jinsi Mali ilivyokuwa inazidi kuendelea. Upande wa magharibi katika nchi ya Guro, kuwepo kwa Wamande tokea zamani zaidi kulihusishwa na biashara ya kola kwenye eneo la makutano kati ya savana na msitu lenye kufuata lalitud

ya 80. Kulikuwa na vituo vingi vya biashara kufuata msitari huu; na katika baadhi ya vituo kama vile Segue (nchini Cote d' Ivoire) kuna mashimo yenye umbo la yai yanayofanana na maeneo ya kujihami. Kwa mujibu wa Waabe, mashimo haya yalikuwepo hapo wakati walipowasili hapo kabla ya uhamaji mkuu wa Akan katika karne ya kumi na nane. Utafiti unatakiwa uelckezwe kwenye vituo vilivyotajwa na mabaharia. Hata hivyo, uchimbaji katika eneo la wangwa na vituo vya mikoko ambapo kuna mkusanyiko mkubwa wa majani yaliyokufa ni mgumu sana. Visiwa vitatu katika wangwa wa Aby vimetoa marundo ya simbi, makaburi, mifupa, shanga na bangili za enzi za neolithi.

Vyanzo Simulizi

Vyanzo hivi ni vingi kwa sababu kila watu wana mapokeo au visasili vya usuli. Hata hivyo, matatizo makubwa bado yanabaki. Kwanza, kumbukumbu zote kwa pamoja hazirudi nyuma zaidi ya karne ya kumi na nane. Zaidi ya hayo, baadhi ya vikundi vya makabila hudai kuwa mababu zao wametokea mbinguni, na wengine hudai kuwa wametokea kwenye shimo katika ardhi wakisema hivyo kwa sababu za wazi kabisa za kupotosha au kwa sababu hawajui. Vilevile, kuna kuingiliana kati ya kumbukumbu moja na nyingine. Kwa mfano, Waavikam wanawachukulia Waalladi kuwa ni ndugu zao. Mihamo pia hutwajwa. Kwa mfano, Waadiukru wanaamini kuwa walitokea magharibi kwa makundi manane yaliyofuatana. Waakan wanadai kuwa asili yao iko Jamhuri ya Ghana. Mapokeo ya Waakwamu yanasema kuwa asili yao inapatikana kwenye mbuga huko Kong. Vilevile, Waafanti wa pwani wanasema kuwa mababu zao walitokea Tenkiyiman kaskazini-magharibi ya Ghana. Kukusanya na kulinganisha data kutoka fani mbalimbali ndiyo njia pekee ya kuibua nadharia tete za kuelezea hali hii.

Ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Abijani na Chuo Kikuu cha Ghana huko Legon ulizaa semina ya Bonduku mwaka 1974 kuhusu "Watu wa asili ya Cote d'Ivoire na Ghana." Hitimisho la Semina hii kwa kuzingatia data zinazotokana na fasihi simulizi, akiolojia na anthropolojia ni kwamba uko uwezekano wa kuunda upya mchakato wa kihistoria.

Mtengano wa watu katika vikundi inawezekana umefanyika kati ya karne ya kumi na saba na kumi na tisa. Hata hivyo, Wakan, Wakru, na Wabron inaonekana walikwisha selea mahali walipo ilipofika karne ya kumi na tano. Kwa mujibu wa Wandenye, babu yao aliyeitwa Ano Asena alitokea mashariki katika nchi iliyoitwa Anyanya. Inasemekana aliwahi kufundisha kilimo kwa kuanzisha kilimo cha viazi vikuu na ndizi. Ulinganishi wa mapokeo mbalimbali unaiweka shughuli hii karne ya kumi na saba. Utafiti wa Claude Perrot kwenye hifadhi ya nyaraka umeonyesha kuwa asili ya Wandenye inaweza kutajwa kuwa

ni karibu na mwaka 1690.

Lakini inawezakana kilimo kiwe katika tarehe za karibuni kama hizi? Kilichotokea ni kwamba mwishoni mwa karne ya kumi na saba, kufuatia mfarakano katika ukoo wa mfalme katika Ufalme wa Aowin nchini Ghana, Ano Asena aliondoka na watu wake na kustakimu maeneo ya Assini (Côte d'Ivoire). Wandenye baadaye wakaunda upya visasili vyao na kumhusisha Ano Asena na maendeleo yaliyotokea mapema zaidi, kama njia ya kufutilia mbali kila kitu kilichotokea kabla ya uhamaji wao ambao ulilipa kabila hilo umbo lake la sasa. Ni kwa njia ya kuweka pamoja vyanzo mbalimbali na kwa fani mbalimbali kufanya kazi pamoja ndipo itakapowezekana kuunda upya ruwaza ya kihistoria kutoka data zote zilizotapanywa au zinazopingana.

Watu wa pwani na bara


Nadharia inayowatofautisha watu wa wangwa na msitu kwa upande mmoja na wale wa savana kwa upande mwingine haiwezi kuhimili udadisi. Wengi ni wa kabila la Kwa. Wareno waliita sehemu ya pwani hii "Pwani ya Waquaqua".

Kwa mujibu wa Profesa Boahen, Waakan ambao hufanya asilimia 45 ya watu wa Ghana na asilimia 33 ya watu wa Côte d'Ivoire wana umoja thabiti wa kilugha. Hali hii inayahusu makundi haya: Waasante, Waakyem, Wawasa, Watwifo, Waakwamu, Wasefwi, Wanzima, Wafanti na wengine nchini Ghana; Waabron, Waagni, Wasanwi, Wabaule, Waattie, Waabe, Waabure, Waalladi na wengine nchini Côte d'Ivoire. Kabla ya karne ya kumi na saba, mgawanyo uliopo katika lugha tofauti labda ulikuwa bado haujatokea. Lakini watu wa wangwa walikuwa wa kabila hilo hilo la *Wakwa* kama ilivyo kwa Waakan. Inawezekana wote wametokea eneo la Chad-Benue kwa awamu, wakivuka mkono wa chini wa mto Niger na kisha nchi zijulikanazo leo kama Benin na Togo huku wakijiundia asasi zao wenyewe. Makundi mengi ya wahamaji yalianzia Adansi na kuchanganyika na watu wa wangwa na kuunda makabila ya Wabaule, Wanzima, Waagni na mengineyo.

Kwa upande wa Wabron, tayari walikuwa Begho mwanzoni mwa karne ya kumi na nne na wakiwasiliana na Wamande.

Watu wa Wangwa

Watu wa wangwa wamestakimu mahali walipo sasa kabla ya karne ya kumi na mbili. Mnamo karne ya kumi na tano, Wakru walikuwa tayari wamekwishaunda jamii za kiukoo zinazojitegemea; Wareno walisifu ubora wao, kuwa ni jamii za mabaharia na wavuvi. Wareno waligundua pia kuwa pwani ilikuwa na vijiji vingi vikubwa na vyenye watu wengi, machifu wakiwa na hadhi ya juu kuliko viongozi wa kidini. Uhuru wa kujitawala wa Wakru ulidumishwa hasa kutokana na kinga ya wangwa na msitu.



13.2 Ramani ya eneo kati ya boude la Nîger na ya Guînea (M. Posnansky, Warsha ya Bonduku, 1974)

Wareno wanaripoti pia kuwepo kwa mahusiano ya kibiashara kati ya Waku na watu wa Bara; watu wa Rio Lahou waliuza chumvi kwa watu wa bara ambao pia walifanya nao biashara kubwa ya nguo. Zaidi ya nguo, biashara ilihusu samaki, dhahabu na shaba. Waku walikuwa ni uzao wa asili uliotoa makundi ya Waadiukru na Waebric-Abia. Katika karne ya kumi na sita, utawala uliendelea kupewa sura ya kisiasa na hivyo kupunguza nguvu ya mahusiano ya kiukoo.

Niger valley and the gulf of guinea

Asili ya Jamii ya Akanya Kwa mujibu wa Profesa Harris, usawa wa kiantropolojia uliopo kwenye eneo la msitu unatokana na ukweli kwamba hapo awali uzao wa aina tatu ulitoa makundi ambayo yaliingiliana: Uzao wa Waakan, Waku na mwishowe jamii zilizojijenga kwa muda mrefu: Waewotie, Waagwa n.k. Hata hivyo, ni wakati gani makundi hayo matatu ya uzao yalitengana na lini asasi na utamaduni wa Waakan ulitokea bado inabaki ni kitendawili.

Posnansky anadhani kwamba karne ya kumi na saba ilikuwa ya mageuzi, kwa mfano kulikuwepo na mitindo mipya ya uundaji vyombo vya udongo. Kwa upande mwingine, kazi za shaba na dhahabu zilianza mapema sana. Utafiti wa kina unahitajika kuziba mapengo yaliyopo kati ya kuwasili kwa Wareno katika karne ya kumi na tano na upanuzi wa falme za Waakan katika karne ya kumi na saba.

Lakimi mnamo karne ya kumi na tano, falme hizi za Waakan zilikuwa tayari zinaanza kupata mashiko, wakati watu wa pwani kama vile Wafanti walikuwa wamejiimarisha kwa kazi na biashara ya dhahabu. Vilevile, Begho, mji mkuu wa ufalme wa Bron, ulikuwa tayari una mawasiliano na Sudan magharibi kwa kupitia Wangara.

Misingi ya Jamii ya Waakan

Vita vya karne ya kumi na saba na kumi na nane viliyasukuma makundi kadha ya Waakan kuelekea magharibi. Kama Profesa Wondji alivyogundua, ni kwamba neno *Akan* linatumika kwa maana za kisiasa na neno *Twɔ* linatumika kutaja kundi la lugha ambalo hujumuisha lugha zote za Waakan.

Sifa kuu za kitamaduni-Kijamii na kisiasa za Waakan ni kama ifuatavyo:

- (1) Utaratibu wa urithishaji wa utawala kwa upande wa kuukeni.
- (2) Utaratibu wa kuwapa watoto majina mawili, jina moja la siku ya Juma alipozaliwa na jingine linalochaguliwa kutoka ukoo wa baba.
- (3) Kalenda ya siku 42 inayozingatia masuala ya kidini ambayo uhusiano wake na ile ya Kiislamu bado ni suala la malumbano.
- (4) Sherche zinazohusiana na mavuno ya viazi vikuu.

- (5) Kuwepo kwa koo 8 za kuukeni na koo 12 za kuumeni, koo za kuukeni zikihusika na damu na zile za kuumeni zenye kukamilishana; zikihusika na tabia na nafsi ya mtu.
- (6) Udhibiti wa hali ya juu wa madaraka anaopewa malkia au mfalme akisaidiwa na Kuhani ambaye huendesha sherehe za kitaifa au za kiukoo na shughuli za ibada.

Kwa mujibu wa Profesa Diabate, hapo awali madaraka yalikuwa yakishikwa na malkia na hali hii iliendelea hadi karne ya kumi na tano wakati koo zilipotengana na kuwa huru. Kufuatia hapo jinsi magomvi ya silaha yalivyoongezeka, walipendelea mtawala ambaye atakuwa tayari kwa vita.

Hitimisho

Ukanda wa wangwa tangu karne ya kumi na mbili hadi karne ya kumi na tano, ulishuhudia maendeleo ya jamii huru za kiukoo, miongoni mwao kiwango fulani cha mgawanyo wa kazi kilichipuka, hususani katika uhusiano wao na watu wa bara. Hawa, wakati mwingine walitokea Sudan ya Magharibi ili kufanya biashara pembezoni mwa msitu. Washirika wao wakuu walikuwa Waakan ambao falme zao zilianza kuundwa tangu karne ya kumi na tano.



Kutoka Volta hadi Kameruni

Ekolojia na lugha


Sura ya ukanda wa pwani wa eneo hili haikuwa tofauti sana na ilivyo leo, isipokuwa sehemu zilizosafishwa zilikuwa chache zaidi. Tayari kulikuwa na mabwawa kwenye delta ya Niger, kanda za msitu wenye mvua nyingi na uwazi kwenye msitu kwenye eneo la Benin na Togo ya hivi sasa. Matumizi ya chuma katika karne za mwanzo za enzi ya Ukristo yaliwezesha watu kupenya ndani zaidi katika eneo la msitu na kuongeza wingi wa makazi ya watu. Uchanganuzi wa lahaja za lugha ya Kiyoruba unaelekea kuonyesha kuwa uhamiaji ulikuwa ni wa kutoka kwenye msitu na kuelekea savana, jambo ambalo linapingana na mapokezi ya historia. Maelezo ya hali hii ni kwamba, kulingana na wakati unaoangaliwa, hajira mara nyingine zilikuwa kutoka kaskazini kwenda kusini au mara nyingine kinyume chake.






Makundi makuu matatu ya lahaja za Kiyoruba yametambuliwa. Makundi mawili ya kale zaidi ni kundi la kati (Kiife na Kiilesha) na kundi la kusini mashariki (Kiowo na Kijebu). Katika karne ya kumi na mbili, makundi haya yalikuwa kwenye maeneo ya msitu. Kundi la kaskazini magharibi (Kioyo na Kiibadan) ni la karibuni zaidi. Mahitimisho haya ya uchanganuzi wa kiisimu yanathibitisha mapokeo yanayodai mwanzo wa kuumbwa kwa ardhi kuwa ni Ile-Ife na asili ya Wayoruba kuwa mashariki ya Oyo.

Uchanganuzi wa lugha za Kiedo unatenganisha makundi mawili: moja la kaskazini na moja la kusini, lenye kuwakilisha lahaja ya ufalme wa Benin, kitovu cha maendeleo ya siasa na utamaduni; lakini unuhimu wa kihistoria wa ugunduzi huu wa kiisimu bado haujawa bayana.

Ingawa uchanganuzi wa lahaja ya lugha ya Kiigbo haujaenda mbali, unaelekea kuonyesha mtawanyiko kutoka mahali pa asili karibu na Owerri na Umuahia.

14.1 Ramani ya eneo kati ya Volta na Camerooni, 1100-1500 (A.F.C. Ryder)



-  Kanamasi cha maji-chunvi
-  Kanamasi cha maji safi
-  Msitu mwele
-  Msitu mkame
-  Savana

Isitoshe, kwenye karne ya kumi na mbili lugha zilikaribiana zaidi kuliko ilivyo sasa, na pia zilikuwa nyingi zaidi, kabla ya kuenea kwa haraka kwa baadhi yake na kuzifuta nyingine ambazo sasa pengine zinazungumzwa katika kijiji kimoja au viwili tu. Kipindi kinachoanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita ndicho hasa kilishuhudia kuenezwa kwa utawala na lugha za baadhi ya vikundi juu ya eneo kubwa katika mfumo wa madola makubwa ya Oyo, Benin na Ife. Hata hivyo vikundi vingine havikufuata mkondo huo.

Jumuiya za kiukoo

Hizi zilikuwa ni koo huru chini ya wakuu wa ukoo waliokuwa na mamlaka ya kidini na ya kisiasa, wakizungukwa na mabaraza ya wazec. Katika kipindi hiki, ongezeko la idadi ya watu lilihusishwa moja kwa moja na maendeleo ya kiufundi na lische bora. Kwa mfano, kilimo shadidi cha viazi vikuu na michikichi kinaonyesha dhahiri sababu za kupanuka kwa Waibo. Kati yao, koo na vijiji vingi viliongozwa na mamlaka yaliyokuwa na muundo thabiti. Waakposo wa Togo waliweza kuhifadhi miundo yao ya ukoo, labda kwa sababu ya kutokalika kwa mazingira ya eneo walimoishi. Lakini mara nyingi walijijumuisha kupigana na adui aliyewakabili kwa pamoja. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hali ya Waigbo (wasichanganywe na Waibo wa leo) walipopambana na Waife.

Walivyohama kutoka kwenye delta ya maji baridi na kwenda kwenye mabwawa ya maji chumvi, baadhi ya Waijo waliacha kulima na kuvua samaki. Kadhalika waliachana na muundo wa jamii wa kijamaa uliotawaliwa na wanaume na wazee, lakini ambamo uwezo ulichukua nafasi ya umri kama kigezo cha kupatia madaraka. Katika utaratibu mpya waliouanzisha, marika yaliyoarikwa pamoja, na vyama vya siri vilivyohudumia jumuiya ya kijiji kizima, polepole viliwawezesha watu kuvuka mipaka ya familia au ukoo na kufuata vigezo vya nchi badala ya maumbile. Madhahabu mapya ya kidini kama yale ya Amakiri na Amatemesuo ya Waijo yalichukua nafasi ya matambiko ya kifamilia.

Uchunguzi unaoangalia desturi za uhamaji au asasi za kidini umewezesha kuonyesha kuwa mtawanyiko wa Waijo kuvuka delta ya mto Niger haukuendelea zaidi ya mwisho wa karne ya kumi na mbili. Ingawa ni vigumu zaidi kufikia makadirio ya namna hiyo, mara nyingine yanatoa habari za kuaminika zaidi kuliko utoaji wa tarehe kwa uchimbuaji, kwani asili ya mabaki ya kale huwa na utata.

Huko Ile-Ife, utoaji wa tarehe kwa kutumia radiokaboni umconyesha miaka ya kati ya 560 na 980, ambapo huko Yelwa kwenye kingo za mto Niger,

mabaki ya kiakiolojia yanaonyesha makazi ya muda mrefu tangu mwaka 100 hadi 700 katika enzi ya Ukristo.

Makazi ya muda mrefu, mchakacho wa kukabiliana na mazingira, na mabadiliko ya ndani, yanaelezea vyema zaidi kuliko kitu kingine chochote mageuzi ya kuelekea kwenye tawala kuu, bila kutafuta sababu kutoka nje, hata kutoka Sudan. Polepole, uongozi ulipoteza hali yake ya mpito, na koo asisi zilipata mamlaka zaidi, kumbukumbu kuhusu makazi na sheria za pamoja zilikubaliwa na zilitumiwa kama msingi wa kanuni za utawala.

Falme na miji

Njia na mabadilishano ya kibiashara ni lazima yalichangia sana katika maendeleo ya miji, hata kwenye maeneo ya misitu. Miji maalumu ilitawi zaidi kutokana na ushindani, hata uadui. Lakini miji iliyostawi zaidi ilitwaa mamlaka ya moja kwa moja kwenye maeneo machache tu; nje ya hapo, kulikuwa na mfumo wa vituo vya vibaraka, na koo ziliendelea kuwa na nguvu. Hata hivyo, athari kutoka nje katika maendeleo ya mfumo wa dola katika maeneo ya msitu haziwezi hupuuzwa moja kwa moja: inawezekana dola lilichukua kutoka nje vipengee vya itifaki yake, au vifaa vya sherehe (panga za sherehe) au vyeo vya uchifu au hata viongozi. Uhusiano baina ya Sahel na maeneo ya misitu, ambao umeshuhudiwa tangu kuwepo kwa himaya ya Ghana, haukuishia katika usafirishaji wa kola, pembe na watumwa; ulichukua pia amali za kiutamaduni na kidini, na kwa hali hiyo kuhusisha amali za kisiasa na kiasasi. Kwa mfano, mtu anaweza kuona jinsi watu wa kijiji cha Waijo cha delta ya Niger mashariki walivyolazimika kuza samaki na chumvi ili wabadilishane na chakula ambacho hawakuweza kukizalisha, kisha biashara hiyo ikaongezeka kwa umuhimu na muundo huru wa awali ukabadilika ili kuruhusu kubinafsisha na kuhodhi mamlaka, na hatimaye chifu kujipa cheo muhimu cha *amanyamabo* (mmiliki mji).

Wayoruba

Mkusanyiko muhimu zaidi wa madola ulikuwa ni ule uliohusishwa na watu waliozungumza Kiyoruba; madola hayo yalienea kutoka Atakpame magharibi hadi Owo iliyo Mashariki. Madola mawili kati ya hayo - Ife na Oyo - yameathiri mapokeo ya madola mengine kwa kiasi kwamba inakuwa vigumu kubaini mfuatano wa matukio yaliyounda mfumo mzima kihistoria. Madai ya watu au nasaba za kifalme kuwa na asili ya Ife hayawezi kukubalika haraka haraka kama vile yasivyokubalika niadai kuwa madola mengi ya Ijo yana asili ya Benin. Pale ambapo kikundi hakikumbuki tena chimbuko lake, mara nyingi

kikundi hicho hujihusisha na dola kongwe na maarufu zaidi lililopo sasa, na ambalo liko mbali kiasi cha kutokuwa tishio kwa njia yoyote ile kwa kikundi hicho.

Kumbukumbu za kiisimu zinazolinganisha lahaja za Kiyoruba cha kati na zile za kusini mashariki zinaonyesha kuwa waundaji wa dola la mwanzo la Yoruba ambao ishara na "mzazi" wao ni Oduduwa walikuwa katika maeneo ya Ife, na hakuna kisakale kingine kinachopingana na hiki. Tarehe za radiokaboni kutoka kwenye machimbo ya Ita-Yemoo unaanzia mwaka 960 hadi 1160, na hivyo kuthibitisha habari zinazotolewa na mapokeo. Mwisho kuwepo kwa Ife kaskazini, karibu na savana, kumeiwezesha kufikiwa mapema zaidi ya madola mengine, na shinikizo zilizoharakisha utaratibu wa ulinganifishaji.

Asili

Kufuatana na mapokeo ya Ife, kundi la kwanza la madola lilitokana na wajukuu wa Oduduwa, ambao walihama kutoka Ife; Kctu, Benin, Popo, Sabe na Oyo. Lakini haiyumkini kuwa zote zilianza wakati mmoja, kutokana na tofauti kubwa ya idadi ya watawala katika orodha ya wafalme, kutoka 27 huko Sabe hadi 52 huko Ijebu, ambayo hairodheshwi miongoni mwa madola ya awali.

Madola ya mji ya asili ya Kiyoruba yalikuwa na mji mmoja na vijiji vilivyozunguka, na yalikuwa na eneo dogo. Miji ilikaa mbalimbali au iliunda makundi ya mashirikisho, kama ilivyokuwa kwa Waegba na Waijebu. Kulikuwa na vikundi vya ukoo pia.

Aina ya dola la "himaya" kama vile Oyo, ilitokea mnamo karne ya kumi na saba tu, na hata hivyo bado inaweza kuelezwa kuwa ilitokana na hali ya kipekee ya ekolojia ya kisavana iliyowezesha mahusiano ya ndani, na mahusiano na madola ya jirani kama vile Borgu na Nupe. Na kusema kweli, dola la Nupe lilivamia Oyo mnamo robo ya mwisho ya karne ya 16 na halikutwaliwa tena na wenyewe hadi mwishoni mwa karne hiyo.

Ife

Ni kitendawili kwamba ingawa Ife inachukuwa nafasi kubwa kwenye historia ya Wayoruba, kutokana na taarifa nyingi zinazomhusisha Oduduwa, mhenga wa visakale aliyeanzisha dola hilo, na warithi wake, bado mapokeo yana mapengo mengi. Kwa bahati njema, kumbukumbu za uehimbuzi zimejaribu kuyajaza.

Awamu ya kwanza ya historia ya dola hilo inaanza mnamo karne ya kumi na moja. Awamu hii inadhihirishwa na kuwepo kwa makazi yaliyokuwa mbalimbali, utengenezaji wa shanga za vioo, matumizi ya sakafu zenye uzio wa nakshi za vyungu, sanaa nzuri za kiasilia za udongo mwekundu na sanamu



14 2 Kichwa cha Terra cotta (Owo, Nigeria)

(Nigeria, akioloju na historia yake, London, Thames and Hudson, 1978)

zinazofanana na zile za utamaduni wa Kinok, lakini hasa zinazohusiana na sanamu kama hizo zilizogunduliwa katika nchi yote ya Wayoruba, kwa mfano huko Ire karibu na Osogbo, huko Idanre, na Owo ambako sanamu za udongo mwekundu zilichimbuliwa katika mazingira ya karne ya kumi na tano. Mtindo huu wa sanaa ulioenea sana na kufikia miji yote ya Wayoruba, na ambao asili yake haijulikani, unaelekea kufungamana na matambiko fulani ya kidini kuliko mamlaka ya kisiasa. Kwa hali hiyo, Ife, badala ya kuwa pekee ilikuwa ni mojawapo ya madola mengi yaliyohodhi sanaa hii iliyoshamiri. Sakafu za vyungu, kwa mfano, zinaonekana hadi mbali kufikia Ketu iliyo katika Jamhuri ya Benin, na pia kaskazini mwa Togo na huko Daima karibu na Ziwa Chad. Huko Ife sanaa hii ilionekana baina ya karne ya kumi na mbili na kumi na sita. Kupotea kwake kwa ghafla kunaelekea kuhusishwa na maafa fulani yaliyougharikisha mji mnamo karne ya kumi na sita. Lakini labda kabla ya tukio hilo, vichwa ishirini na tano vya "shaba nyeusi" vya Ife (lakini hasa vilikuwa vya shaba nyeupe na shaba nyekundu) ambavyo vinaiga barabara mtindo wa uasilia wa sanaa za udongo mwekundu, vilikwishafuliwa. Kuvunjika kwa dola la Ife katika karne ya kumi na sita kunaweza kuelezwa tu kwa kubadilika kwa ufalme. Kwa hali hiyo utawala wa sasa unatokana na nasaba mpya iliyojenga kasri na kuta za awali karibu na eneo la kati ya mji. Utawala huo unawezekana ulibakisha baadhi ya asasi za kisiasa na kijamii za ufalme wa zamani. Hii ina maana kuwa haiwezekani kueleza kwa undani mfumo uliokuwepo katika kipindi cha awali, na wala kuamua kuwa uhusiano baina ya miji mingine ya Kiyoruba na Ife ulianza katika kipindi cha pili au cha kwanza cha historia ya Ife.

Kwa hiyo, taratibu za kutawaza wafalme na nembo za kifalme zinafanana katika nchi yote ya Yoruba, lakini zinatofautiana sana na nembo zilizovaliwa na watu mashuhuri ambao labda walitokana na familia za kifalme za nasaba ya mwanzo iliyoangushwa.

Athari ya madola ya Sudan ya kaskazini zaidi (ya karibu zaidi yakiwa Borgu na Kwararafa) iko wazi. Wanupe waliwafukuza Wayoruba kutoka Oyo ya zamani mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, na kiukoniboa mji wao mkuu. Waoyo waliunda upya majeshi yao na kutoa umuhimu kwa askari wa farasi, ambao ndio kikosi cha dafurao katika madola ya Savana. Waoyo walikopa madhehebu ya wahenga ya *Egungun* kutoka kwa Wanupe.

Ufalme wa Benin

Hili ndilo lililokuwa dola la kwanza la pwani kuwapokea Wareno na kuanzisha uhusiano wa kibiashara na kibalozi na Wareno.

Ikiwa ipo kusini mashariki mwa Ife, Benin labda ilikuwa ufalme mnamo karne ya kumi na mbili. Inaelekea ilipitia mabadiliko makubwa mnamo karne ya kumi na tano yanayofanana na yale yaliyoikumba Ife kwenye karne ya kumi na sita. Lakini kwa uhakika uanzishaji wa ufalme huo ulikwishatokea mwanzoni mwa karne ya kumi na nne; watu wa Benin, kufuatana na mapokeo, walimwomba mfalme wa Ife, Oduduwa, awapatie mwanamfalme na aliwapelekea Oranyan. Tunaelezwa kuwa madaraka ya watawala wa mwanzo yalidhibitiwa na machifu wa kienyeji waliojulikana kama Ozama; lakini inawezekana kuwa madaraka ya machifu wa kienyeji wa baadaye yalipangwa na ufalme wenyewe. Kwa kweli hapa tuna mfano wa majukumu ya kisiasa ya machifu ya kienyeji, yanayofanana na yale ya *oyomesi* saba wa Oyo; na, kwa upana zaidi, huu ni mfano wa ruwaza iliyoenea sana Afrika ya mgawanyo wa madaraka baina ya mfalme na machifu wazawa wa makundi ya kiukoo.

Baada ya mapambano ya silaha na *ozama*, mtawala wa nne wa ufalme wa Benin anasemekana kuwa alifanikiwa kubadilisha mizania ya madaraka kwa manufaa yake. Baada ya hapo alijenga kasri kubwa zaidi ambamo washika vyeo vikubwa hawakupata vyeo hivyo kutokana na urithi bali kwa kutunukiwa na ufalme. Licha ya yote hayo madaraka ya *ozama* hayakuvunjwa kabisa; mtawala alibakia kama mtu wa kati. Mnano karne ya kumi na tano, machafuko makubwa yalisababisha kusimikwa kwa utawala wa kibinafsi wa mabavu chini ya mfalme Ewuare, ambaye alitwaa kiti cha ufalme baada ya kumwua kaka yake. Lakini inawezekana sana kuwa masimulizi haya yanaficha tukio la mabadiliko ya ufalme, labda yaliyotokana na kuingilia kwa nguvu kutoka nje.

Serikali ya Ewuare

Ewuare alijenga mji wake kwa ramani mpya na aliupa jina la Edo. Ulizungukwa na handaki kubwa na maboma. Barabara pana ilitenganisha kasri na nyumba za mafundi na wakuu wa kimila, Kasri ilikuwa na sehemu ya mavazi, wapanibe wa mtawala na harimu, kila idara ikiwa na madaraja matatu yaliyofuata umri ambayo yalifanana na marika ya vijiji vya Edo. Kila ushirika wa uzalishaji mjini vilevile ulikuwa na muundo wa marika, na kila rika liliunganishwa na idara mwafaka ya kasri. Wajumbe wa ngazi za juu katika jumba la mfalme walikuwa na vyeo binafsi walivyoshika kwa maisha yao yote. Inadhaniwa kuwa Ewuare alimhusisha kila raia wake aliyezaliwa huru na shughuli za kasri.



14.3 Benin. Mpiga jilimbi ya shaba nyeusi (W. Forman, B. Forman na P. Dak 1960)

Baada ya kumaliza huduma zao, wengi wa wanaume walirudi vijiji kwao, baada ya kuchanjwa usoni ili kuwatambulisha kwamba ni "watumwa wa Oba" watawala wa kijadi yaani *maozama*, machifu wa jumba la mfalme, ambao walikuwa karibu naye, na aina mpya ya machifu wa "mji". Hawa waliunda baraza la dola, na kila mmoja alisimamia ushuru kutoka sehemu moja ya ufalme. Ewuare alianzisha pia kanuni ya urithi wa mtoto wa kwanza kwa kiti cha ufalme, ambapo mrithi-mtarajiwa aliketi miongoni mwa *maozama* akiwa na cheo cha *edaiken*. Ewuare anakumbukwa kama mganga mkuu, na aliimarisha nguvu zake za ajabu kwa kuanzisha sherehe ya kila mwaka ya Igwe ambapo nguvu zake za uzima zilipata uhai mpya.

Ewuare pia alianzisha vita kubwa baina ya Waedo, Waibo na Wayoruba. Hatimaye himaya ilionekana kama mlolongo wa maduara yenye kitovu ki moja. Katika duara la kipenyo cha kilometa 60 kuzunguka mji mkuu, kulikuwa na utawala wa moja kwa moja ambapo ni mfalme tu aliweza kutoa adhabu ya kifo. Sehemu nyingine za nchi zilitawaliwa na wanamfalme wenye damu ya kifalme na muundo wa utawala wao ulilingana na ule wa Edo. Mbali zaidi, falme zilizoilipa kodi serikali ya Benin zilikamilisha ramani ya kisiasa ya Benin.

Siri ya mafanikio hayo inaweza kuwa ilitokana na mafanikio ya Ewuare katika kuwaunganisha raia wake na kuwafanya wawe na moyo wa utaiifa. Warithi wake waliendelea na matendo ya kivita, ambayo mgawira na ushuru wake ulitumiwa moja kwa moja katika kukimu jeshi. Kwa njia hii, karibu nchi yote ya kaskazini mwa Edo iliingizwa Benin, kama ilivyokuwa nchi nyingine za Wayoruba kama vile Owo na Ijebu. Waitsekiri walipewa mjukuu wa Ewuare kama mtawala wao, na kusababisha wakubali kuwa chini ya Benin kwa karne kadhaa.

Tumesisitizia muundo wa kijamii na kisiasa wa Benin kwa sababu ni moja ya nchi chache zenye taarifa za uhakika za asasi zilizokuwepo kabla ya karne ya kumi na sita, na uchimbuzi wa kiakiolojia umethibitisha masimulizi yaliyopo. Aidha, dola hili lilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Waedo na majirani zao. Uchimbuzi pia umetoa mwanga kuhusu mabadiliko ya sanaa maarufu ya Benin. Vifaa vyote vya shaba nyeupe vilivyotengenezwa kabla ya karne ya kumi na sita vimedhihirisha kuwa vimetengenezwa kwa uhunzi na sio kwa kumimina. Ingawa ufundi huo wa kuyeyusha nta ulikuwa ukijulikana hapo awali, ulishamiri tu idadi kubwa ya shaba nyeupe ilipoingizwa kutoka Ulaya.

Sanaa ya Ife na tatizo la sanamu za shaba nyeusi

Ustaarabu wa Ife-Benin unatuwezesha kuiweka sanaa ya Kiafrika katika muktadha wa kihistoria na kijamii wala sio katika muktadha wa kiujumi tu. Uchongaji wa miti ulioenea kwingineko Afrika unatoa vipande vya sanaa vya

hivi karibuni. Ustaarabu wa Ife-Benin na sanaa yake ya udongo mwekundu na shaba nyeusi ni johari tofauti na ya pekee.

Tumekwishataja uhusiano wa kihistoria na ule wa kinasaba baina ya sanaa za udongo mwekundu za Nok, ziliyoanza tangu enzi ya chuma (karne ya tano kabla ya Kristo), sanamu ndogo za udongo mwekundu za Ife, na mwishowe vifaa vya shaba nyeupe vilivyofuliwa au kumiminwa kwa ufundi wa kuyeyusha nta. Hiki ni kipengee na ushahidi wa mahusiano ya muda mrefu baina ya nchi za savana (kwa hapa ni uwanda wa juu wa Bauchi) na zile za misitu.

Tutaacha kando nadharia za waandishi wa Kizungu waliokataa kutambua Uafrika wa sanaa liizi aali zisizo na kasoro. Mjerumani Leo Frobenius kwa bahati alikusanya na kufasiri kwa haki baadhi ya sanaa hizi huko Ife mnamo 1910. Lakini tasisahau kwamba Ife ilitakwa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na jeshi la Waingereza na kuporwa sanaa nyingi aali.

Lundo muhimu la sanaa hizi liligunduliwa 1939 si mbali sana na kasri ya *Oni* wa Ife. Tangu hapo, ugunduzi mwingi umcfuata.

Sifa na Maendeleo ya Sanaa ya Benin

Ndani ya kaburi huko Abiri, Bernard Fagg aligundua vichwa vitatu vya udongo mwekundu kimoja kikiwa ni mfano wa mtindo halisi na asilia wa Ife, wenye utulivu mwanana na mlingano wa ndani unaoupa sura yenye kina cha hisia, ambapo vile yiwili vingine vilikuwa vya mtindo wa kikaida kabisa ambao ulikaribia sanaa dhahania: inatundu mawili yakiwakilisha macho, mkato wa mlalo ukionyesha mdomo. Vyote vilikuwa na asili moja na vilitengenezwa kwa mbinu ileile ya uchomaji.

Ni ajabu na kwa kiasi kikubwa ni tukio la kipekee katika historia ya utamaduni wa dunia kukuta katika utamaduni mmoja aina mbili za sanaa zinazotafautiana. Hakuna haja ya kutafuta watu wa nje kuelezea njia hizi mbili tofauti za kujieleza kisanaa: kinachotakiwa ni kuelewa jamii iliyounda sanaa hizi aali, hasa maisha yake ya kidini.

Ukweli ni kwamba sanaa hizi, ambazo kwa kawaida humwakilisha *Oni*, chifu wa kisiasa na kidini, zilitengenezwa baada ya kifo chake, ili ziwekwe katika kaburi lake. Kwa hiyo haishangazi kuwa mazingira haya ya miviga yangeamsha mikabala aina mbalimbali ya kiujumi. Nia ilikuwa kuendeleza, katika mahekalu mia ya Ife, kumbukumbu ya wale (wahenga) wanaoendelea kuwachunga watu wanaoishi.

Inasinuliwa kwamba *Oba* wa Benin aliomba na alipata kutoka kwa *Oni* wa Ife mchongaji mwenye ujuzi aliyewafundisha wasanii wa Benin. Hivyo, Ife ilikuwa kweli jiji mama mlimozuka dini na sanaa inayotumiwa kuwatukuza wahenga.

Tatizo la sanaa ya shaba nyeusi

Nje ya eneo la Ife-Benin, sanaa nyingi za shaba nyeusi zimegunduliwa kutoka kwenye delta hadi mipakani mwa Nupe. Kwenye eneo la Igbo-Ukwu, ambapo palichimbuliwa mwaka 1959, na panawakilisha mji uliojengwa kuzunguka jumba la mfalme na mahekalu, kumechimbuliwa karibu sanaa 800 za shaba nyeusi katika mtindo ambao ni tofauti kabisa na ule wa sanaa za shaba nyeusi za Ife-Benin.

Majengo yaliyogunduliwa ni chumba kikubwa ambamo hazina zilitunzwa, cheinba ya kuzikia kuhani mkuu, na shimo la takataka.

Sifa kuu inayoonekana katika sanaa hii ni uhusiano wake na ufalme wenye kufungamana na miviga ya kidini. Uwezo wa wasanii wa Kiigbo-Ukwu ni wa hali ya juu: Kwa mfano katika maumbo maalum ya wanyama yaliyofanywa kwa ubingwa wa kushangaza ambayo yanapamba mabakuli ya shaba nyeusi na magudulia ya udongo. Hapa teknolojia na ujumi vilidhibitiwa kwa ufundi mkubwa. Huenda Igbo-Ukwu palikuwa makao makuu ya kidini ya ufalme mkubwa, na ilikuwa hapo ambapo hazina zilihifadhiwa chini ya uangalizi wa mfalme kuhani. Lakini tarehe zilizopatikana kwa kutunia mbinu ya radiokaboni zinaonyesha kuwa tayari utamaduni huu wa hali ya juu ulikuwapo katika karne ya tisa, karne mbili kabla ya utamaduni wa kusifika wa Waife. Aidha utamaduni huu ulistawi miongoni mwa Waibo, watu wanaosemekana kuwa walikuwa "wamegawanyika" katika vikundi vidogo vidogo na hawakuwa na dola!



Hii ndiyo sababu suala la jedwali ya miaka na hata tatizo la kuaminika kwa tarehe za radiokaboni linahojiwa tena na baadhi ya waandishi. Kwa ufupi, Igbo-Ukwu ni fumbo jingine katika historia ya Afrika.

Sanaa za Shaba za Nupe


Hizi ziligunduliwa kati ya Busa na makutano ya Benue. Hi ni sanaa maarufu zijulikanazo kama "shaba za Tsoede" zinazoelezwa kuwa zililetwa katika karne ya kumi na sita na muasisi wa ufalme wa Nupe. Vilevile alileta kutoka Igala kundi la wahunzi ili kuwafundisha watu wake mbinu ya uhunzi wa kuyeyusha nta.

Maswali mengi bado hayajajibiwa; bado kuna haja ya kuchunguza kwa makini mahusiano ya kaskazini na kusini baina ya eneo la Niger ya chini, ambalo ni la watumiaji wakuu wa shaba nyekundu na shaba nyeupe, na nchi zinazoweka kuwa vyanzo vya metali hizi kaskazini zaidi, katika Afrika (Takedda) au mahali pengine.

14.5 *Chungu chenye kamba ya shaba nyensi*
(T. Shaw, 1970)




14.4 *Mchoro maalum wa chungu chenye kamba ya Shaba nyensi* (na T. Shaw, 1970)



14.6 *Bakuli kubwa la shaba nyensi, likionekana toka juu (T. Shaw, 1970)*

14.7 *Bakuli kubwa la shaba nyensi liltofunikwa, likionekana toka pembeni (T. Shaw, 1970)*





14.8 Ukarabati wa kiakioleja wa mazishi ya mtawala wa Igbo-Ukuvu (T. Shaw, 1970)

Katika delta ya Niger

Hapa jamii za kiukoo kama vile za nusu Wabantu Waekoi (angalau kabla hawajamezwa na Waefiki) au Waibo, ziliishi sambasamba na makundi mengine kama vile Waijo ambayo yalikuwa katika mchakato wa kuunda mfumo wa serikali kuu. Dola za Okrika, Bonny na Nembe zilizoanzishwa kama katikati hivi ya karne ya kumi na tano, zinaonyesha uwezo huu wa kujongea katika maeneo, kumeza makundi mengine kama Waitsekiri na kutumia desturi mpya za kitamaduni kama zinazohusu miungu na matambiko ya kidola. Hata hivyo katika uhamaji wao kupitia sehemu ya mashariki ya delta, Waijo waliwazindua Waibibio na Wandoki. Kuundwa kwa dola ya Kalabar katika karne ya kumi na saba katika Mto Cross kulikuwa ni jitihada za tawi la Waefiki wa Ibibio.

Hitimisho

Mwishoni mwa karne ya kumi na tano, wakati Wareno walipofika pwani, Oyo na Benin zilikuwa ndizo dola muhimu sana. Mchakato wa kuunda dola uliharakisha kasi ya mwingiliano wa kitamaduni baina ya watu, ukihimiza kuenea kwa asasi, ada, madhehebu ya dini na teknolojia, pamoja na mbinu za ufuaji kwa kuyeyusha nta ambazo hapo awali zilikusishwa na falme tukufu.

Kutokana na mahitaji yake makubwa, wafalme walichochea uzalishaji wa ndani na biashara kwa kukusanya na kusafirisha mazao, na kuhakikisha usalama. Dola za biashara za Ijo zilikuwa zikipeleka majahazi yao makubwa yakiwa yamesheheni chumvi mbali kabisa ndani ya nchi. *Oba* wa Benin alikuwa akiratibu biashara kubwa ya pembe, pilipili na watumwa. Kutokana na kuwa mpakani kati ya dola za misituni na za savana, Oyo ilidhibiti sehemu kubwa ya biashara iliyopitishwa baina ya kanda mbili. Hivyo, Wareno walipofika, walikuta dola ambazo tayari zilikwishaimarika zikiwa na uchumi uliolingana na mahitaji ya biashara ya kimataifa.

15

Misri na Dunia ya Kiislamu kutoka karne ya kumi na mbili hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na sita

Umuhimu wa Misri katika maisha ya kisiasa na kiuchumi kwenye kipindi hiki

Katika kipindi hiki, inaweza kuonekana kwamba Misri iliipiga kisogo Afrika. Waayyubi na baadaye, himaya ya Wamamluk ambayo ilienea hadi kufikia Efurata na Anatolia, walichukua nafasi ya ukhalifa wa Wafatimi ambao asili yake ilikuwa Maghrib.

Na isitoshe, kilikuwa pia kipindi cha hija kuu za wana wa wafalme wa Kanem, Mali na Songhai waliopitia Kairo wakiwa njiani kwenda kwenye Schemu Takatifu za Kiislamu. Vilevile kilikuwa kipindi ambapo njia za kuvuka Sahara zilikuwa kwenye upeo wa matumizi yake kuelekea Misri na kurudisha katikati ya Afrika, bidhaa, kanuni za mwenendo na mifumo ya fikra. Zaidi ya hayo kutoweka kwa ukhalifa wa Kishi'a kutoka bonde la Nili kulizileta karibu Maghrib ya Wamaliki, Misri na Mashariki, na kuchangia kujenga upya kipengee cha umoja wa Uislamu ambacho Kairo ndipo palikuwa kitovu chake.

Uhuisho wa Misri baada ya kuanguka kwa Wafatimi (Salah Al-Din na kuinukia kwa nchi mpya ya kisiasa)

Kila kitu kilionyesha kuwa Salah al-Din Yusuf ibn 'Ayyub (Saladin) ndiye mtu wa kuongoza mapambano ya Uislamu dhidi ya vita vya msalaba vya Kizungu. Si ukhalifa wa Kiabbasi wa Baghdad, uliokuwa chini ya utawala wa maamiri wa Ki-Seljuk, wa Kituruki ambao waliwasili muda si mrefu kutoka mbuga za Asia, wala si ukhalifa wa Kifatimi wa Kairo chini ya ushawishi wa wakuu wake wa kijeshi na huku ukitishiwa na khalifa wa Baghdad, uliohubutu kukabili

changamoto ya Wazungu waliojipandikiza huko Palestina na Efurata ya juu.

Amiri aliyetawala Mosul, Nur al-Din, alifaulu kukomesha uvamizi huu wa Wakristo kuelekea mashariki kwa kuteka tena ukanda wa Efurata ya juu na schemu za ndani ya nchi ya Shamu.

Hata hivyo, khalifa wa Kairo alikuwa akizidi kuchezeza na wakuu wake wa kijeshi ambao katika mashindano yao ya kuwania cheo chake, walianza hata kuwaomba Wakristo kuwaunga mkono. Ndipo hapo khalifa alipokubali kusaidiwa na vikosi vya kijeshi vilivyotumwa kutoka Damasko pamoja na Mkurdi, Shirkuh, ambaye, baada ya kifo chake, nafasi yake ilichukuliwa na mpwa wake Salah al-Din. Mnamo mwaka 1171, huyu Salah al-Din alitangaza kuondolewa kwa ukhalifa wa Kishi'a na utii kwa ukhalifa wa Kiabbasi wa Baghdad uliodhibitiwa na Nur al-Din. Pengine mgogoro ungezuka baina ya viongozi hawa wawili wenye nguvu wa Uislamu wa mashariki. Lakini kifo cha Nur al-Din mnamo mwaka 1174 kiliacha njia wazi kwa Salah al-Din, ambaye aliteka tena nchi zilizobakia kwenye Efurata na kisha, mnamo mwaka 1187, akaiteka Yerusalemu kutoka kwa Wakristo. Kutokana na ushindi huo umoja wa dunia ya Kiislamu ya mashariki ukajengeka ukiwa na kitovu chake katika Misri.

Itikadi ya mamlaka mpya

Lengo la kidini na kisiasa lilikuwa ni uundaji upya wa Misri ya Kiislamu. Ushia ulikuwa haujaenea sana miongoni mwa umma isipokuwa huko Misri ya juu. Ushia huu ulilaumiwa kwa udhaifu wa Uislamu ulipokabiliwa na watu kutoka nchi za Magharibi. Kilichohitajika ni kuujenga upya kwa uimara Uislamu wa mapokeo na wa jumuiya, yaani Uislamu wa Kisunni. Makhirifa wa mbali huko Baghdad wakawa wamepata tena heshima kiasi. Safari za hija kwenda Makka ambazo zilikuwa zimezuwa na ufalme wa Kikristo wa Yerusalemu, zilianza tena kwa kiwango kikubwa na kukuza sifa za Salah al-Din hata kufikia huko Moroko.

Huko Misri kwenyewe, mamlaka yaliunda tabaka la watu waliobobea kwenye fani za kidini na kisharia ili kudumisha Usunni. Mfumo wa *Madrassa*, ulioigwa kutoka katika Uislamu wa Seljuk, uliendelezwa wakati wote katika kiwango kikubwa ili kutoa wanazuoni na watumishi wa kidini waliohitajika ili kuweka kiungo cha kijamii na kiutamaduni baina ya watawala na watawaliwa. Kutoka Mashariki hadi Maghrib waliwasili waumini wa Kisufii waliokalia majumba ya watawa (*khankah*) au katika upweke kwenye *maribati* ya Misri ya Juu. Hawa walikuwa na dhima kubwa ya kufundisha na kuamsha hisia za umma. Mnamo mwaka 1244, sufii wa Maghrib Abu al-Hassan al-Shadhili alifanya maskani yake Aleksandria.

Amani ya Waayubi

Ujenzi wa Misri ya Kisuni ulisaidiwa na ufanisi wa kiuchumi uliotokana na kumalizika kwa uhasama. Lakini mashambulizi mengine ya Wazungu katika sura ya Vita vya Tatu vya Msalaba yaliwawezesha watawala wa kizungu kuteka tena Yerusalemu, bali hayakuselea kabisa yaliwawezesha kwa mara nyingine kwenye pwani za Shamu na Palestina. Kuwepo kwao huku kungeweza kuwa kwa manufaa kibiashara kwa madola ya Waayubi. Baada ya kifo cha Salah al-Din mnamo mwaka 1193, warithi wake walitumia kwa faida yao nia njema ya Wakristo na kutia sahihi makubaliano ya maridhiano nao. Kilifuata kipindi cha ustawi mkubwa wa kiuchumi.

Kilimo cha miwa nacho kikaongezwa kwenye jumla ya mazao asilia. Licha ya vikwazo vya biashara ya vitu vya kivita, wafanyabiashara wa Venise na Genoa walianza tena kuingiza chuma, mbaao za kuundia vyombo na bereu — vitu ambavyo vilikuwa muhimu kwa mashua za kivita. Misri kwa upande wake iliua shabu kwa ajili ya viwanda vya nguo na inazao ya thamani ya Afrika Mashariki na Asia. Dola la Kiayyub liliinufaika kutokana na juhudi za Wafatimi za kurejesha katika njia za Bahari ya Shamu na bonde la Nili biashara ya kihistoria ya Bahari ya Hindi. Kwa karne tatu kutoka nusu ya pili ya karne ya kumi na moja, bidhaa zilizoteremshwa katika bandari ya Aydhab kwenye pwani ya Bahari ya Shamu zilihamishwa na misafara kwenda kwenye bandari ya Kusi katika Nili na kutoka hapo kupelekwa hadi Aleksandria ambako wafanyabiashara wa Kizungu walilazimika kuzingoja kwa kuwa walikuwa wamefungiwa kufika Kairo kwenyewe na Bahari ya Shamu. Mwanamfalme wa Kiayubi aliitawala Yemen. Na, Wakarimi ambao walikuwa mabingwa wa biashara hii ya masafa marefu, walitumia njia hii yenye faida kubwa ambayo Misri ilikuwa imeishika kabisa na ambayo ilihangia katika ustawi na umoja wa bonde la Nili.

Dola na mundo wake: tabaka la kijeshi mamlakani

(Warithi wa Salah Al-Din)

Hakukuwa na mabadiliko kutoka utawala wa Kifatimi, ambamo Wakristo wa Kikhufu, warithi wa mbinu za kirasimu zilizojaribiwa na kujaribishwa, waliendelea kuwa na dhima kuu. Madiwani waliendeleza shughuli zao chini ya masultani wa Kiayubi ambao hapo awali walikuwa mawaziri wa Khalifa na mara zote walitajwa kwa cheo cha *Malik*.

Lakini Salah al-Din kama amiri wa Kikurdi aliyezoea taratibu za Maseljuk ambao familia yake iliwafanyia kazi, alinua kulinufaisha jeshi lake, kama

ilivyofanywa jeshi la Kifatimi, kwa kutumia mfumo wa *ikta*, yaani kila amiri kupewa mapato ya kodi ya maeneo fulani.

Lakini Wakurdi na Waturuki walionufaika na kodi hii walitazamwa kama wageni na Wamisri. Zaidi ya hayo, mtazamo wa kifamilia wa mamlaka aliokuwa nao Salah al-Din ulimfanya awape jamaa zake mamlaka ya majimbo au miji, hata kufanya himaya ijiunde katika shirikisho la mamlaka za wanamfalme, Misri ikiwa katika nafasi ya katikati ikiongoza familia nzima. Lakini muda si mrefu ushindani ulizuka miongoni mwa wale waliowania vyeo hivyo, ambao hawakusita kuwatafuta marafiki hata miongoni mwa Wakristo. Tokea wakati wa kifo cha Salah al-Din mnamo mwaka 1193, kulikuwa na mapigano ndani ya familia na ni baada ya matukio makubwa ya mashambulio ya Kikristo ya Vita vya Tano vya Msalaba, ndipo al-Malik, mpwa wa mpwa wa Salah al-Din mwishowe akajiimarisha huko Kairo mnamo mwaka 1240. Uzoefu ulikwishamfundisha kwamba ni jeshi eledi lililoundwa vema na lililojitolea kutetea nafsi na jaala ya mtawala tu ndilo lingehakikisha utulivu, walau wa kiwango cha chini kabisa. Akaamua kuwachukua watumwa wa Kituruki: Mamluki au Wabahri, walioitwa hivyo kwa sababu ya kuwekwa katika kisiwa kwenye mto Nili (*Bahr*).

Mamluki wa Kituruki

Mamluki waliwakilisha asasi, iliyokuwa juu ya jamii, ya tabaka la kijeshi lenye nguvu lililochagua masultani kutoka miongoni mwa makundi yake kutawala juu ya jamii, bila kujali mwendelezo wa ukoo tawala. Utengano baina ya watawala na watawaliwa ukakamilika.

Asili ya mamlaka yao ilikuwa ni hatari kubwa iliyosababishwa na uvamizi wa Wamongol kuelekea magharibi, na mvuvumko wa majeshi ya Kikristo ya wazungu. Kukaliwa kwa bonde la chini la Volga na Hungary na wimbi la kwanza la Wamongol kulitoa idadi kubwa ya watumwa wa Kituruki ambao Waayubi walikimbilia kuwachukua, hao ndio waliunda kikosi cha Bahri cha Kairo. Kisha, mnamo mwaka 1249, jeshi la Vita vya Msalaba vya Sita, likiongozwa na Mfalme Louis wa IX wa Ufaransa mwenyewe, lilitua Damietta. Tukio hili lilitokea sambamba na kifo cha al-Malik al-Salih, wakati mrithi wake, Turan Shah, akiwa safarini huko Efurata. Kikosi cha Bahri ndicho kilichoiokea Misri kwa kunshinda Louis wa IX na kumteka.

Turan Shah aliporudi na kutaka kulazimisha mamlaka yake juu yao, Mamluki walimuua. Huyu ndiye alikuwa mtawala wa mwisho wa Waayubi, ingawa mjane wa al-Malik al-Salih alipewa usultani na mamluk kama ada tu. Wakati Mamluki wanakaribia kuraruana, wimbi la pili la Wamongol lilitwaa Baghdad mnamo mwaka 1258, wakamuua khalifa wa Kiabbas na kuteka milki


za Waayubi hadi huko Gaza. Kutokana na mfarakano wa ndani kati ya Wamongol, Mamluki walifaulu kuwarudisha nyuma hadi kuvuka Efurata. Mamluku pekee walikuwa wameuokoa Uislamu dhidi ya matishio mawili ya Wakristo na Wamongol, ambao kwa bahati nzuri, hawakujiunga kufanya shambulio la pamoja. Walinufaika pia kutokana na ukweli kwamba Wamongol walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili: kundi la Wailkhan wa uzao wa Hulagu, mjukuu wa Ghengis Khan, lililokuwa na makao yake Persia, na kundi la Wakhan, wa Kipchak waliokwisha silimu.

Mamluk wa Bahri walitumia fursa hii ya mazingira yaliyowapendelea kugeuza mamlaka yao halisi waliyonyakua kutoka kwa Waayubi kuwa mamlaka halali. Walifanya hivyo kwa kujipatia sultani ambaye bila shaka alikuwa hodari mno kijeshi na kisiasa, aliyeitwa Baybars (1260-77). Huyu aliharibu ngome kuu za Wakristo huko Shamu (Syria) na Palestina na kuongoza majeshi yake hadi Anatolia dhidi ya Wamongol. Warithi wake waliendeleza kazi hiyo hiyo. Kutwaliwa kwa ngome ya mwisho ya Wakristo kwenye pwani ya Palestina ya Mt. Yohana wa Akre, mnamo mwaka 1291, kulikuwa jibu kwa tishio jipya la ushirika baina ya Wamongol na wafalme wa Ulaya. Wailkhan wa Kiajemi nao waliposilimu kukapatikana muda wa amani; lakini uislamu wa Kishia wa Wamongol wa Kiajemi ndio pengine ungekuwa tishio kwa Uislamu wa Kisunni ambao ulikuwa umetawala huko Mashariki ya Kati na Misri. Kuporomoka kwa dola la Wailkhan mnamo mwaka 1323, na kwamba Waturuki wa Kiottoman upande wa kaskazini walijishughulisha zaidi na vita dhidi ya masalio ya himaya ya Bizante, na walikuwa hawajawa na nguvu, ndiyo mambo yaliyowezesha dola la Mamluk kujitokeza kama nguvu kuu ya Uislamu.

Mamlaka ya Mamluk barani Afrika

Utajiri wa Mamluk ulitokana na bara la Afrika. Biashara kubwa na Mashariki ya Mbali iliendelea kupitia Bahari ya Shamu na bonde la Nili. Misri iliimarisha nafasi yake kwenye njia hii kwa kutawala Yemen na kushirikiana na maamiri wa Dahlak. Wakati fulani Wamongol walijaribu kuzirejesha njia za biashara za Bahari ya Hindi na za Mashariki kwenye Ghuba ya Uajemi, na kwenye njia za bara zinazodhibitiwa na Wamongol. Lakini, mnamo katikati ya karne ya kumi na nne, bandari kuu za Ulaya zilikiri kwamba njia ya Bahari ya Shamu na bonde la Nili haikuwa na ushindani. Wafanyabiashara wa Kikarimi walioidhibiti njia hii walijenga mawasiliano hadi kufikia Timbuktu.

Mahusiano ya kisiasa na kitamaduni baina ya Misri na Afrika yalikuwa yanasitawi. Ilikuwa ni wakati huu ambapo Al-Umar aliandika kitabu chake cha maarifa yote ya jiografia. Watu wa Kairo walishuhudia misafara ya mamwinyi



15.1 Kaburi la Keyi Bay la Cairo (1472-4) (Usanii majengo)
(G. Wiet na L. Hautecoeur, 1932)


wa Kisudani ambao ukarimu wao mkuu ulivuma mno. Mtawala wa Kanem alianzisha madrasa huko Fustat, ambapo mnamo mwaka 1324, mfalme mkuu wa Mali, Mansa Musa, aligawa kiasi kikubwa cha dhahabu. Dhahabu ya Sudan ilitumiwa na watengeneza sarafu wa Kimisri. Nguo za thamani, vitabu na mila za utawala wa Mamluk na bidhaa nyingine nyingi za viwanda na za kitamaduni zilipelekwa Sudani na mahujaji maarufu.

Lakini mtazamo wa Misri kwa jirani zake wa Kiafrika ulikuwa wa kikatili mno: mnamo mwaka 1275, sehemu ya kaskazini ya ufalme wa Kikristo wa Nubia ilitwaliwa, na wanamfalme vibaraka kusimikwa. Katika uharibifu wake wa Nubia dola la Misri liliungana na Mabedui wa makabila ya Banu Kanz na Wajuhayna, Wabali na wengine ambao walikuwa wakijongea kuelekea Darfur na Afrika ya Kati. Misri ilifarijika mno kuona makundi haya ya zahaina na vurumai yaliyosaidia kuondoa kikwazo cha Nubia yakisogea mbali.

Uislamu Misri

Uislamu uliendelezwa kufuata mila ya Waayubi ya mafunzo ya Kisunni yenye *madrasa* ya fahari au ya kawaida, ongezeko la kushiriki kwa wasomi kutoka mikoani katika maisha ya mji mkuu, na mkondo wa kiwalii uliotokana na kazi ya Al-Ghazali na vikundi vyake vya udugu au *mashadili*. Nafasi za juu za utawala zilifufua utukufu wa ukhalifa wa Kiabbasi, hasa ziliposhikwa na Washamu kama vile Al-Umari, au kuelekea mwisho wa karne ya kumi na nne, kutokana na kazi bora ya mtu kama Al-Kalkashandi.

Hata hivyo wanasharia waliendelea kuwakosoa Mamluk; licha ya umaarufu wao kama watetezi wa imani dhidi ya Wamongol: mapigano haya yalitokea mbali, ambapo anasa ya kifedhuli ya maamiri, ambao walielewa zaidi Kituruki kuliko Kiarabu; ilikera hisia ya Uma wa Wamisri, na wanazuoni wake kuilalamikia. Lakini watu wa kawaida pia walimaizi ushindi mkuu, majengo ya kifahari ya masultani kama Baybars au Kalaun, vishindo vya masultani, na viviga vya ajabu vya jumuiya za udugu kutoka Mashariki ya Mbali. Katika hili watu wa kawaida na tabaka la kijeshi walikubaliana, hasa kwa kuwa Baybars alikuwa amepokea kutoka kwa khalifa wa Kiabbasi hati rasmi iliyomhalalisha kama sultani. Makhhalifa walipoanza kukimbilia Kairo kama ilivyokuwa mwaka 1262, sala zilizosaliwa kwa majina yao zilizusha mvutano hadi khalifa alipowekwa chini ya ulinzi; lakini hata ishara ya kuwepo kwake tu iliimarisha utukufu wa sultani katika dunia nzima ya Kiislamu ambayo Kairo ilikuwa ndiyo kituo chake kikuu cha kisiasa na kitamaduni. Ngano za *Alfu Lela Ulela* zilikuwa zinakaribia kuisha. Ni dhahiri utamaduni huu mpya wa kikakamavu ulikuwa umepungukiwa ubora na utajiri kuliko ulivyokuwa ule wa Baghdad,



15.2 *Taa ya Kimisri iliyopambwa kwa glasi (enzi ya Mamluk)*
(G. Wiet and L. Hautecoeur, 1932)

lakini ulikuwa ukifasiri upya urithi mkubwa wa ukhalifa ili kujinasibisha na mazingira ya wakati huo. Hapo ndipo ulipokuwa umuhimu wa kazi kubwa ya kihistoria ya Ibn Khaldun, ambaye kwa mara kadhaa alikuwa *kadhi* mkuu wa Kimaliki wa Misri, ambako aliwasili mnamo mwaka 1382, na ambako kama wengine wengi, alifundisha katika *madrassa* ya Kairo.

Mfumo wa Kisiasa wa Mamluk

Tabaka la Mamluk wa Kituruki lilitoka zaidi kwenye fuko za Black Sea, likiwa na watumwa wachache wengine, wakiwemo Wamongol. Waliuzwa na wafanyabiashara wa Kignoa au wa Kiarabu. Ilikuwa ni miongoni mwa makumi ya maelfu haya machache ya wanajeshi ambamo mchezo wa kisiasa ulichezwa. Mshikamano wa kundi hili ulitegemea elimu ya namna moja, ya kijeshi na ya kidini. Masultani na maamiri waligawana mapato ya kodi ambazo ziliwawezesha kuweka majeshi tayari chini ya amri ya maamiri wao kuitikia amri yoyote toka kwa sultani. Uchaguzi ulikuwa wa kikatili na usioweza kutabirika. Na kila *amiri* aliyepata usultani alijihusisha tu na uimarishaji wa kundi jipya la Mamluk waliojinaki na jina lake na kujihusisha na maajaliwa yake, kama hakuondoka duniani kwa kufa au kwa kushambuliwa na kundi jingine lililowania kutwaa mamlaka.

Katika hali kama hizi, uendelezaji wa ukoo tawala unaoonekana katika baadhi ya majina ya masultani wa familia ya Kalaun, mathalan, haukuwa halisi. Ni kweli kwamba baada ya Baybars (1260-77) Kalaun alifaulu kumkabidhi mwanawe mamlaka, lakini mwanawe huyo aliondoshwa na ami yake aliyetitwa Muhammad ambaye alirjea mamlakani mara tatu. *Maamiri* wakuu kama Usun na Taz walikaimu utawala na kuchangia kwa hali ya juu mno katika usanifu majengo wa mji wa Kairo, ukiwemo msikiti wa fahari wa Sultani al-Nasir Hassan (1356-62). Kutokana na kipindi cha usirisiri kilichofuata, *Amiri* Barkuk alijitokeza na kuwa sultani hadi mwaka 1399 kutokana na jitihada za watu wa kabila lake, Wasirkassi.

Misri hadi mwisho wa karne ya kumi na tano: mawasiliano na Afrika (Mamluk wa Kisirkassi)

Hii ilikuwa hatua mojawapo kuu katika historia ndefu ya Misri: serikali ya Mamluk wa Kisirkassi iliiondoa Misri katika Enzi za Kati.

Mabadiliko makubwa

Mamluk wa *Kikhana* wa Kipchak hawakuwa tena wakifika Misri kwa wingi kama ilivyokuwa hapo kabla. Nafasi yao ilichukuliwa na Wasirkassi kutoka Kaukasus, ambao walianza kutawala kutokana na nguvu ya mshikamano wao wa kifamilia, ambao ulikuwa kama mshikamano wa kirangi uliohodhi njia za kufikia usultani kwa kupendelea kundi dogo zaidi kuliko hapo awali — kundi la Mamluki walipojiuza kwa mwenye nguvu kuzidi wote.

Lakini raslimali iliyotokana na mabaki ya kodi (*ikta*) ilikuwa ikipungua: Misri ilikuwa ikidhurika na magonjwa makubwa ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na ule ugonjwa uliojulikana kama *Black Death* ("kifo cheusi") mnamo mwaka 1349. Magonjwa haya yalipunguza sana idadi ya watu tokca kwa masultani kwenda chini na kupunguza mapato ya *ikta*.

Cha mwisho na kilicho muhimu pia, "makabila" ya Kibedui ambayo yalikuwa yameruhusiwa kizembe kuangamiza Nubia yalipata nguvu huko Misri ya Juu pia na yakawa hayawezi kudhibitiwa kiasi cha kufanya barabara kati ya Aydhab na Kus isipitike mnamo miaka ya 1360. Kwa hiyo kwa muda bandari ilikopitia biashara ya viungo iliamishwa kwenye pwani ya musoma wa Sinai ili kuepuka kutozwa kodi. Kwa muda, mamlaka ya Barkuk (1382-99) yalidhibiti na kubadilisha uffiaji huu kwa kuwagonganisha Waberiberi na makabila ya Kiarabu huko Misri ya Juu na kuzidisha udhibiti wa majimbo. Hii yaelekea ilirejesha kipindi cha ufanisi wa masultani.

Mgogoro wa mwanzoni mwa karne ya kumi na tano

Lakini baada ya kifo cha Barkuk mgogoro ulizuka. Ulikuwa mgogoro wa nje na wa ndani. Kwa nje, utawala wa Mamluk ulitishiwa huko Anatolia na mwana wa mfalme wa Kituruki wa Maottoman aliyekuwa akiwashambulia Wazungu huko Balkans. Lakini kilichokuwa kibaya zaidi huko Asia ya Kati, ni Tamerlane, afisa wa wanamfalme wa Wamongol aliyekuwa akijaribu kurejesha himaya kuu. Kwa kasi alishambulia hadi Damasko na kisha, kama muujiza, badala ya kushambulia Misri, alielekea Anatolia kuwamaliza Maottoman. Hatari mbili zilizokuwa zikiikabili Misri zikamalizana.

Kutokea wakati huo Mamluk ambao walitazama bila uwezo makabiliano kati ya mamlaka kuu mbili mpya, walitumbukia kwenye inigogoro ya ndani ya wenyewe kwa wenyewe.

Baada ya kushindania uhamishaji wa mamlaka kwa mwana wa Barkuk aliyecitwa Faraji, tabaka la kijeshi lilianza kujirarua lenyewe katika mapambano makali. Kwa muda, usultani ulipata hata kukabidhiwa kwa khalifa bandia wa

Kiabbasi. Lakini wakati huo huo maafa yalikuwa yakijilimbikiza: mafuriko ya mto Nili hayakutokea; palikuwa na njaa na tauni mnamo mwaka 1405; Waberiberi na Wanomadi wa Kiarabu walikuwa wakifanya uporaji na uharibifu katika Misri ya Juu. Yakiwa yamekabiliwa na migogoro kama hii ambayo ilikuwa haijawahi kutokea ilibidi madola ya Kimamluk yabadilike au yaangamie.

Misri dhidi ya hatari ya Wakristo: mapambano dhidi ya Wareno: Misri mpya

Ilikuwa ni Mamluk kutoka kundi la Barkuk, hasa Shayh na Barsbay (1422-39) ambao walirejesha amani katika mambo ya Misri, na kufanikiwa kuwatumia Waberiberi wa Kihauwara kuituliza Misri ya Juu. Ili kujaziliza hazina za taifa zilizopungua sana kutokana na vifo vya tauni. Barsbay aliamua kuchukua miliki yote ya biashara viungo ambavyo sasa vilikuwa vinatokea Aden kupitia Misri kwa kutumia njia fupi zaidi ya kutoka El Tur kwenye rasi ya Sinai hadi Aleksandria au Damicitta, au kwenda kwenye bandari ya Shamu. Barsbay alihalalisha mzunguko huo kwa kudai bidhaa zipitie bandari ya Jeddah (wakati huo ikiwa bandari ya Misri) ambapo zilitozwa kodi na kisha kuuzwa kwa kupitia njia halali. Hii ilikuwa na athari mbaya kwa wafanyabiashara binafsi wakubwa, hususan Wakarimi ambao walitoweka; Wavenetia, ambao ndio walikuwa wanunuzi wakuu, Wakatalan na Wagenoa ambao ilibidi apigane nao vita. Katika uhusiano huu Kupros ilivamiwa na mfalme wao kuchukuliwa mateka. Kuhodhi huku kulimpatia Barsbay na warithi wake msingi imara zaidi wa kiuchuni wakati ambapo maamiri walididimizwa hadi kuishi kwa kutegmea mapato kidogo yaliyopatikana kutokana na Madaraka yote yalikuwa sehemu moja. Tatizo lilikuwa tu kwamba askari wapya walioandikishwa kwenye jeshi walikuwa ni mamluki tu waliopambana na kundi lenye hadhi la Wakirassi. Zaidi ya hayo, ilikuwa si maamiri vijana tena ambao, kwa msaada wa watu wao, walishika madaraka, bali watu wazima na wazce zaidi, ambao waliona zaidi kama wanasiasa kuliko wanajeshi. Usultani, ukiwa umehalalishwa wakati huu, ukawashinda makhalifa wa Kiabbasi wakati uwiano wa Waislamu na Wakristo ukiwa unaongezeka, na kuifanya Misri ya Kiislamu kuzidi kuwachukia Wakristo, maharamia na wafanyabiashara, pamoja na sarafu zao za dhahabu na nguo zao za bei ghali. Hivyo, wakiwa wamekabiliwa na njama za Wazungu, jamii ya Kimamluk ilionekana imara kiuchumi na kidini lakini hafifu ilipokabiliana na mvuvumko wa kibiashara wa Wakristo na wanio lao kubwa la kuiepa Misri ili ikiwezekana washirikiane na Negus (mfalme) wa

Ethiopia. Wasafiri kadhaa wa kizungu waliacha maelezo ya thamani ya safari zao.

Hata hivyo, wagcni wengi zaidi walikuwa mahujaji wa Kiafrika kutoka Sudan wakiwa njiani kwenda hija kwenye Sehemu Takatifu za Uislamu. Usunni ulioenezwa Afrika kusini mwa Sahara kutokea Misri na Makka ulizaa matunda kama *Tarikh al-Fattash na Tarikh al-Sudan* zinavyoonyesha. Na wakati wa hija watawala wa Kisudani nyakati zingine walipewa mamlaka rasmi na khalifa wa Kiabbasi, kama ilivyomtokea Askiya Muhammad mnamo mwaka 1496. Wamisri waliona Sudan hasa kama chanzo kikubwa cha dhahabu. Misri ya Juu ilichangia sana katika biashara hii hasa kwa kuwa wakati huo maamiri wa Kibedui walikwisha kuwa Waislamu na wafanyabiashara, wakiuza farasi waliowazalisha watumwa waliowapata kutoka Sudan ya Kati.

Lakini Misri ya Juu, ikiwa haina viungo, ilianza kuonekana maskini zaidi na maisha huko yalisogea kwa kasi ndogo kuliko ilivyokuwa huko Misri ya Mediterania iliyokuwa imejaa biashara na majumba makubwa ya mtindo mpya, hasa wakati wa usultani uliodumu muda mrefu wa Khayt Bay (1468-96). Hiki kilikuwa kilele cha mamlaka ya Mamluk, walioipatia Kairo sura ambayo imehifadhi hadi leo hii.

Licha ya dalili za kufifia, mwisho wa karne ya kumi na tano bado ulidhihirisha athari kubwa ya Misri katika utukufu wa dola na utamaduni uliokuwa ukichanua, hususan kama ulivyodhihirishwa na tapo la wanahistoria cha Misri, wakiwemo akina al-Makrizi na msomi maarufu al-Suyuti, ambao sifa zao zilienea hadi Takrur.

Muktadha mpya wa Kimataifa

Kutoka kwa Watimuri — warithi wa Watamerlane — waliogeuka kuwa Waislamu wenye amani na walinzi wa sanaa, Mamluki walioimarika hawakuwa tena na chochote cha kuhofia, upande wa mashariki. Kwa kuingia Anatolia, wangeweza hata kuwa na dhima ya upatanishi baina ya Waturuki. Lakini upanuzi huu wa mamlaka yao hatimaye ulichokoza utawala wa Waottoman, moja ya makundi ya makabila ya Kituruki.

Waottoman, hapo awali wakiwa wamegawanyika na kushindwa, walijizatiti upya, na chini ya Mehmed II (1451-81) walitwaa Konstantinople mnamo mwaka 1453, na kujitokeza kama watetezi wapya wa uislamu. Hii ni wakati nafasi ya Mamluki ilikuwa inazidi kupwaya kutokana na wahifadhiwa wao wa Kituruki huko Anatolia kulazimika kuafikiana na Wakiisto ili kuepuka kumezwa na Waottoman. Mapigano baina ya Waottoman na Mamluk yalikuwa hayana budi kutokea. Yalifanyika mara kadhaa, kuanzia wakati wa usultani wa Khayt Bay. Licha ya ujuzi wa kutuonia

bunduki na mizinga ambao Waottoman waliupata kutoka Magharibi, Mamluk waliweza kumudu vita hivyo kutokana na Waturkoman wa Iraqi kuingilia kati, Waottoman kuelekeza nguvu zaidi kwenye vita vya jihadi huko Mediterani na mwisho kujitokeza, mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, kwa mamlaka ya Safavi yaliyowaunganisha Waturkoman na Wairan katika Iran ambayo iliingia chini ya Washia kwa inara ya kwanza, na hivyo kuwa tishio zaidi kwa Waottoman kuliko kwa Mamluk.

Hata hivyo ilikuwa ni upanuzi wa Wareno katika Bahari ya Hindi uliobadilisha mambo kwa kuharibu misingi ya uchumi wa mamlaka ya Mamluk. Tangu wakati wa safari ya Vasco da Gama, Wareno walikuwa wakinunua viungo kutoka India moja kwa moja, na walizingira Bahari ya Shamu. Baada ya kushindwa kwa kikosi cha maji cha Misri huko Diu kwenye pwani ya magharibi ya India mnamo mwaka 1509, himaya ya Mamluk ilibakia kwenye ulinzi wa Bahari ya Shamu tu. Wakati Wasafavi walipowashambulia Waottoman, baada ya kuchochewa na mataifa ya magharibi, Waottoman hawakupewa msaada na Mamluk, licha ya kwamba wao walikuwa wamewasaidia Wamisri huko Bahari ya Shamu. Hata hivyo, kutokana na matumizi ya bunduki, walifaulu, mnamo mwaka 1514 kukomeshea upanuzi wa Washia huko Iran. Mnamo mwaka 1516, katika vita vya Marj Dabik karibu na Aleppo, kwa kutumia silaha za kisasa zilizoangamiza wapanda farasi wa kizamani wa Kisirkassi, Waottoman waliwalazimisha Mamluk kuwatambua kama mamlaka ya Kisunni inayoongoza katika Mediterani na Afrika.

Hitimisho

Mamlaka ya Mamluki yaliyobakia kuwa ya Wasirkassi yalikusisha tabaka dogo la wanasiasa. Yalipopoteza msingi wake wa uchumi katika Bahari ya Hindi, na uhalali wake wa kidini wa utetezi wa Uislamu, yalilazimika kukubali kushindwa na Waottoman ambao walimweka gavana huko Kairo. Hata hivyo kwa muda mrefu baadaye jamii ya Kimisri iliendelea na athari za kisiasa na kitamaduni za Mamluk ambazo zilikuwa adhimu kwa Uislamu na kwa Afrika.

16

Nubia toka mwishoni mwa karne ya kumi na mbili hadi Utamalaki wa Wafunji mwanzoni mwa karne ya kumi na sita

Kudidimia na kutoweka kwa nchi za kinubia za Kikristo


Licha ya kuwepo kwa mikinzano michache midogo midogo, *bakt*, mkataba wa kimataifa baina ya Misri ya Kiislamu na Nubia ya Kikristo uliendelea kuzingatiwa kwa karne sita. Zaidi ya kuwa na mawanda ya kisiasa, kijeshi na kidini, mkataba huu pia ulianzisha kutegemeana kiuchumi.

Msingi huu wa kuvumiliana ulikuwa na uzito hasa chini ya utawala wa Wafatimi waliotaka amani na pia watumwa kwa ajili ya jeshi lao wakati Nubia ilipokuwa ikifikia upeo wa mamlaka yake. Kipindi kinachozungumziwa hapa, yaani kile cha Waayubi (1171-1250) na cha Mamluki (1250-1517), kilishuhudia kuvurugika kwa uhusiano baina ya Misri na Nubia kutokana na kuongezeka kwa shinikizo la Kairo juu ya Nubia iliyokuwa ikidhoofu, na ongezeko la mwingilio haribifu wa makundi ya Wanomadi wa Kiarabu.

Karibu nyaraka zote zinazotudhihirishia harakati hizi ni za Kimisri. Kumbukumbu za mahali hapo, ambazo ni chache na zisizokuwa muhimu sana, zimekuzwa na mabaki ya kiakiolojia yaliyochinibwa mnamo miaka ya 1960 ambayo huwezesha uchanganuzi wa kina wa maendeleo ya ndani. Mpaka baina ya falme mbili kuu za Mukurra huko kaskazini, na makao yake makuu huko Dunkula na Alwa huko kusini, ulipita kati ya maporomoko ya tano na sita katika mto Nili. Kiti cha enzi kilirithishwa kuukeni, mrithi akiwa mwana wa dada wa mtawala aliyetangulia.

Mukurra

Wakati wa Wafatimi, mahusiano ya kibiashara baina ya Misri na Nubia yalikuwa yameshamiri kama inavyoshuhudiwa na athari ya kisanaa ya Wafatimi juu ya watengenezaji bidhaa wa Kinubi. Hii ilikuwa hivyo wakati mkataba wa *bakt* uliporasimishwa kwa msingi wa kuaminiana. Mfalme wa Nubia alikuwa na



16.1 Unubi kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na mbili hadi ushindi wa funj nwanzoni mwa karne ya kumi na sita (L. Kropáček)

maelewano bora kabisa na Askofu Mkuu wa Aleksandria ambaye alikuwa mlinzi wake. Wafatimi wa Kishia, waliokuwa wametengwa katika ulimwengu wa Kiislamu, hasa walithamini nia njema ya Wanubia ambao walipanga mashambulizi kutoka wakati mmoja na majaribio ya Wafatimi ya kuteka nchi ya Wamisri. Wanubia hawakusita kuwarejesha watumwa waliokimbia na wakimbizi wa kisiasa kwa Wafatimi. Wapiganaji wengi kutoka Nubia ndio waliounda kitovu cha jeshi la Wafatimi, hasa baada ya kufaidi ulinzi wa mama ya al-Mustansir, ambaye alikuwa mwcusi, mnamo nusu ya mwisho ya karne ya kumi na moja. Hatimaye, askari wa Kinubia walisukumwa kusini na washindani wao wa Kituruki na Kiberiberi, lakini waliendelea kuiunga mkono kwa dhati nasaba ya Kifatimi dhidi ya Waayubi waliokuwa wakizidi kupata nguvu. Katika kukabiliana na Waarabu, Wafatimi walipata suluhisho makini la kuwatuma Wabanu Hilal kuelekea Maghrib wakati wakikomesha uasi wa Wabanu al-Kanz. Mnamo karne ya kumi na mbili Kanz al-Dawla aliyekimbilia Mukurra alirejeshwa kwa Wamisri ili kuhukumiwa.

Hivyo, kulikuwa na kujumuikiana na mabadilishano yaliyowanufaisha wote. Kwa masharti ya mkataba wa *bakt*, wafanyabiashara walilindwa katika nyendo zao ndani ya Nubia, lakini waliweza tu kukaa karibu na mpaka wa kaskazini wa Nubia. Shughuli zao zilisaidia mno usilimishaji kuliko mawakala rasmi wa Ushia wa Kifatimi.

Kuingia madarakani kwa Waayubi kulizusha shambulizi la Wanubia mnamo mwaka 1172 ambalo lilirudishwa nyuma na shambulizi la Turanshah, kaka ya Salah al-Din, aliyeteka Kasr Ibrim. Kuwafurusha Waarabu waasi wa Banu al-Kanz kuelekea kusini kulichangia kuingiza Uarabu na usilimishaji wa Nubia, ikiwa ni pamoja na kuoana na Wabanu al-Kanz ambao tayari walikuwa mchanganyiko wa Waarabu na Wanubia. Mashambulizi ya mara kwa mara ya Wamisri yakiongozwa na Waayubi na Mamluk dhidi ya makabila ya Wanomadi wa Kibedui yaliwarejesha nyuma Mabedui hawa na kuwafanya wakimbilie Sudan. Lakini kupitia kwao Nubia, kulikoambatana na vitendo vya kinyang'anyi na kidhalimu, kulileta uharibifu mkubwa.

Baada ya kutikiswa na vitendo hivi vyote vya uharibifu na mapinduzi ya ndani, Mukurra haikuweza tena kuwa mwenzi mshitika na ikawa inaingia kwenye hadhi ya utwana ambayo ilishadidiwa na ehokochoko za kivita za Mamluki. Sultani Baybars (1260-77) pengine kutokana na kuchochewa na shaka juu ya usalama wa himaya yake na ukubwa wa nyara alizorudi nazo kutoka kwenye mapambano yake huko Nubia na dhidi ya *Waurbana* wa Misri ya Juu, alimwagiza Mfalme Dawud wa Nubia aanze tena kutoa mchango wake kama inavyotakiwa chini ya mkataba wa *bakt*. Dawud alijibu kwa kufanya mashambulizi ambayo matokeo yake yalikuwa ni kutekwa kwa Aydhab, bandari ya Misri katika Bahari ya Shamu. Baybars alijibu

kwa shambulio lililopelekea kuondolewa madarakani kwa Dawud na nafasi yake kuchukuliwa na binamu yake aitwaye Shakanda ambaye alikubali kwa dhati kuwa kibaraka na mwakilishi wa sultani (*naib*), na vilevile kulipa kodi inayolingana na nusu ya mapato yote ya nchi. Juu ya hayo, alitakiwa pia kutoza kodi ya kichwa kwa wasiokuwa Waarabu, kukubali ushirikiano wa kisiasa na kurejesha wakimbizi wa Kiarabu. Aidha, Misri ilinufaika kwa kuchukua maelfu ya watumwa waliotekwa, miongoni mwao akiwemo Mfalme Dawud ambaye suala lake lilingiliwa kati na *Negus* Yekuno Amlak katika barua (alizomwandikia Baybars).

Utwana haukuhifadhi umoja wa ndani wa Mukurra; kwa hakika, mambo yalikuwenda kinyume. Mamluk, ambao punde tu waliungwa mkono na Waarabu wengi, waliibadilisha Nubia kuwa nchi ya wavamizi.

Mfalme Shamamun wa Nubia alijibu kwa kufukuzwa kikosi cha Mamluk kilichoachwa huko Dunkula. Baadaye, aliona hapana budi kumuomba msamaha Sultani Kalaun mnamo mwaka 1290, na sultani huyo, kwa kuwa alikuwa yumo katika mapambano dhidi ya majeshi ya vita vya msalaba, hakuwa na jingine bali kukubali. Baada ya kipindi cha utulivu, Mfalme Karanbas aliacha kulipa ushuru, kikosi cha kumtia adabu kikatumba kutoka Kairo kikifuatana na mdai Mwislamu wa ufalme wa Mukurra aliyelitwa Sanbu. Kuwekwa kwa mdai huyu huko Dunkula ndiko kulikuwa mwanzo wa kusilimishwa rasmi kwa Mukurra. Kanisa kuu kongwe la gorofa mbili liligeuzwa kuwa msikiti na Sanbu. Lakini punde tu alishindwa na kuuawa na Kanz al-Dawla, ambaye alikuwa na mashabiki miongoni mwa Wanubia na Waarabu. Sultani, kwa kuogopa kuwepo kwa nguvu hii, alijaribu kumrudisha Karanbas, mfalme wa Kinubia aliyesilimu wakati akiwa mateka huko Kairo. Alikuwa ameondolewa na Kanz al-Dawla, ambaye alikuwa binamu yake. Kisha, Wabanu al-Kanz na washirika wao Wabanu al-Ikrima walipigana kila mara na majeshi ya Mamluk waliotumwa kulipiza kisasi. Mukurra iliingia katika machafuko. Ruwaza mpya za kumbari zilikuwa zikianza kuchomoza bila Nubia kutwaliwa. Lakini, kwa kudhoofishwa ndani kwa ndani kutokana na kuingiliwa na makundi mengi na kushambuliwa mara kwa mara, nchi hii ilipoteza nguvu kama dola lenye taratibu za kujicendesha. Ndoa mchanganyiko, ambazo, kulingana na kanuni ya Kinubia ya urithisho, ziliwapa wana wa baba wa Kiarabu na mama wa Kinubi haki kwa mali ya wajomba wa Kinubi, iliongeza kasi ya kuingiza Uarabu na usilimishaji katika hali ambayo ilionekana kuwa vurugu tupu.

Uchunguzi wa kiakiolojia unaonyesha kukua kwa ukosefu wa usalama kuanzia katikati ya karne ya kumi na mbili, hasa kutokana na ongezeko la majengo ya kujihami yaliyonuiwa kulinda maeneo yaliyokuwa na Wakristo wengi.

Mabaki mengi ya jumuiya za Kikristo za baadaye yanapatikana katika visiwa ambako minara ya lindo inatazama kusini kana kwamba adui (ambao pengine walikuwa Wanomadi) alitarajiwa kutokea upande huo. Ingawa kumbukumbu za

Kimisri zinazungumzia vijiji vilivyochomwa moto, magurudumu ya maji yaliyoharibika na watumwa waliotekwa, na vilevile sera ya Wanubia ya uhomaji moto ardhi, yaelekea kwamba pigo la mwisho dhidi ya Wanubia lilitoka kwa makundi ya waporaji kutoka jangwani, kama vile Waberiberi wa Kizaghawa, na hasa Waarabu.

Alwa

Historia ya ufalme huu ni ya vunguvungu mno pamoja na kuwepo kwa maelezo ya Ibn Sulaym (katika karne ya kumi) na Abu Saleh (katika karne ya kumi na tatu) ambayo yanatuonyesha soko la watumwa lenye kushamiri lililokuwa na makanisa 400, likiwemo kanisa kuu la Soba. Tunaambiwa kwamba Adur, mtawala wa al-Abwab, mara nyingi aliwarejesha wafalme wa Kinubi wahalifu ili kuhakikisha kuendeleza uhusiano mvema na masultani wa Kimamluk. Kaina ilivyokuwa huko Mukurra, pengine, wahamiaji wa Kiarabu waliojipenyeza na kuoja humo walidhibiti malisho na hatimaye kudhoofisha mamlaka kuu kwa kukaa karibu na Soba mnamo nusu ya mwisho ya karne ya kumi na tano. Zaidi ya hayo kulikuwa na mashambulizi yaliyofanywa na watu weusi kutoka Sudan ya Kati na ya Mashariki na vilevile kufifia kwa Kanisa.

Majilio ya usultani wa Kifunji wa Sennar si lazima yatazamwe kama ya wakati mmoja na kuanguka kwa Alwa mnamo mwaka 1504. Mapokeo fulani yanakuwekea tarehe ya mapema zaidi kutekwa kwa Soba na Waarabu. Mashambulio hayo yanasemekana yaliongozwa na Abdallah Jamma ("sanyasanya") dhidi ya udhalimu wa wafalme wa Alwa. Ukoo wa akina Abdallah ulishika hatamu juu ya makabila ya kinomadi na ukaanzisha kituo ehake huko Kerri. Lakini tokea mwanzo wa karne ya kumi na sita Wafunji waliokuwa wakimiminikia *Blue Nili* waliikalia Gezira. Hawa walikuwa jumuiya ya dini ya kimapokeo ambao *Tarihi ya Wafunji* inatueleza kwamba walishirikiana na Waarabu, wakati vyanzo vingine vinataja vita baina ya Amara Dunkas na Abdallah Jamma. Hii, kwa hakika, ina maana kwamba baada ya vita, ambapo Wafunji walipata ushindi, Waarabu wafuasi wa Abdallah walishuka hadhi kimamlaka na hii ilihakiksha kuwepo kwa utulivu uliorahisisha usilimishaji wa nchi.

Ushindi wa Uislamu

Kutoweka kwa Ukristo

Uislamu, ambao ulianzishwa mapema kabla ya kipindi tunachokitazama, ulienezwa na wafanyabiashara, kujipenyeza kwa Waarabu au ubarakala wa baadhi ya viongozi wa Kinubia ambao, kama wale wa Dunkula, waliamua kusilimu.

Imani ya Kikristo kwa muda mrefu ilidumu bila kuathiriwa na kupotea kwa wafalme wa Kinubia, kama inavyoonyeshwa na kaburi la Askofu huko Kasr Ibrim linalodhihirisha kwamba alikuwa bado yu katika shughuli zake mnamo mwaka 1372. Kufuatana na maelezo ya kasisi wa Kireno, Fransisco Alvarez, aliyetembelea Ethiopia mnamo mwaka 1520, miongoni mwa Wanubia ambao walitembelea nchi yao, kulikuwa bado kuna makanisa 150 ndani ya ngome kongwe. Watu ambao hawakuwa Wakristo, Waislamu wala Wayahudi, yasemekana walitaka kuwa Wakristo. Yasemekana kuwa walituma ujumbe kwa mfalme wa Ethiopia wakiomba makasisi lakini bila mafanikio. Enco linalozungumziwa pengine lilikuwa Dunkula.

Hapo mwanzoni, Waislamu ambao walikuwa wachache, yaelekea waliishi kwa amani na majirani zao Wakristo. Jefule dhidi ya Ukristo baada ya kuenca kwa Uislamu yaelekea ilikuwa ni matukio ya nasibu tu kuliko udhalimu uliopangwa: kwa mfano, kubadilisha makanisa kuwa misikiti, kumtesa askofu na kuwachinja nguruwe kufuatia kutekwa kwa Kasr Ibrim na Waayubi. Wakiwa wamejikuta kati ya Waislamu wa Kimisri na Waislamu wa Kinomadi ambao walichukiana, Wanubia pengine wangaliweza kuendelea kudumu kwa muda mrefu ila kwa mfululizo wa matukio ya nasibu tu.

Kwa upande mwingine, sababu kadhaa za ndani zinasaidia katika kuelewa kufifia kwa Ukristo wa Kinubia.

Kwanza kabisa yaelekea kwamba, kimsingi, hii ilikuwa dini ya tabaka la juu bila mashiko miongoni mwa umma. Mapadre wa Kikristo wakiwa wamejikita katika utamaduni wa kigeni waliwaabudu watakatifu ambao hata mmoja wao hakuwa Mnubi. Ingawa sanamu za ukutani katika makanisa zinaonyesha nyuso za maaskofu weusi wenyeji, dini hii haikupata kuwa ya wenyeji kama vile Uislamu ulivyokuwa. Hii ndiyo sababu imani za kabla ya Ukristo zimedumu mahali hapo kwa nguvu.

Kanisa la Kinubia ambalo lilikuwa limefungamanishwa na dola lilikuwa limetengwa katika mazingira ya kijiografia ya Kiislamu. Mawasiliano na Ubizenti yanaweza kubainika katika sanaa ya Kinubia, lakini kufikia karne ya kumi na tatu mawasiliano na Askofu mkuu wa Aleksandria yalikuwa yamekatwa, ingawa mahujaji wachache wa Kinubi walikuwa wakionekana bado katika Kanisa la Kaburi Takatifu huko Yerusalemu.

Katika muktadha huu wa udhaifu wa ndani, vituko vya nje vilikuwa na vishindo vya maangamizi; usilimishaji kutoka tabaka la juu la jamii hadi tabaka la chini ukawa dalili mpya ya heshima na muungano mpya.

Uarabishaji

Mawimbi ya uhamiaji wa makabila ya Kiarabu kuingia Nubia na mehanganyiko mkubwa wa jamia mbalimbali uliofuatia, vilifanya lugha na utamaduni wa Kiarabu



16.2 Ukuta wa mji wa Mafara wa Kiarabu, ulikarabatiwa kwa matojali ya zamani (K. Michalowski, 1962)

vikubalike. Ukoloni huu wa kitamaduni ulifidiwa na kugeuzwa kwa maumbile na tabia za wahusika kuwa za Kiafrika.

Idadi kubwa ya vyanzo vilivyoweka kumbukumbu za mchakato huu ni vya mapokeo ya kinasaba (*nisba*), ulivyokusanywa mathalani mnamo kame ya kumi na sita na Wa al-Samarkandi. *Nasaba* hizi lazima zitumiwe kwa uangalifu sana, kwani kwa jumla ziliandaliwa kuunganisha familia kuu za wakati huo na mababu maarufu ili kuzihalalisha; kwa kawaida mababu waliorejelewa walikuwa ni wale wenye asili ya kusini mwa Bara Arabuni (Kahtani) au kaskazini mwa Bara Arabuni *Adnani* au ndugu za Mtume kama vile mjomba wake aitwaye Al-Abbas. Kwa upande mwingine, Wafunji walidai kuwa wa ukoo wa Waummaya. Halikadhalika, familia za waalimu wa dini na wanasharia katika eneo hilo zilitoa madai kama hayo.

Uhamiaji wa makundi ya wachungaji wa Kiarabu uliofanyika kwa kame kadhaa ulibadilika tu kuwa uvamizi mkubwa kuanzia kame ya kumi na mbili na kuendelea. Njia zilizopitiwa na hawa wachungaji wa Kiarabu hubainika kwa kiasi.

Kiambishi tamati – ‘*ab* kinachoambishwa kwenye baadhi ya majina ya kimbari ni mkopo kutoka kwa ukoo wa Tu-Bedawie (Bejawi) na kinaashiria kupitia nchi ya Wabeja. Eneo hili pengine lilikuwa katika njia ya zamani kabisa iliyotumiwa na wahamiaji wa Kiarabu waliotoka Bahari ya Shamu na Misri. Lakini mimea katika

schemu hiyo haikufaa kwa ufugaji ng'ombe, hivyo, pamoja na ndoa mchanganyiko baina ya Waarabu na Wabeja, idadi kubwa ya wale waliokuwa wakifika walilazimika kuendelea na safari yao kuelekea Nili ya katikati na Gezira.

Makundi mengine ya Waarabu yaliendelea kusini kupitia bonde la Nili hadi kusini mwa Dunkula. Wengine walielekea magharibi, pengine kupitia uchochoro wa Wadi al-Milk na Wadi al-Mukaddam au walifuata 'njia ya siku arobaini' (Darb al Arbain) hadi Darfur.

Makundi ya Kinubia yazingumzayo lugha ya Kiarabu yaliunganishwa na *nisba* zao kwenye makundi mawili. Wajaaliyyin na Wajuhayna. Kundi la Wajaaliyyin lilikuwa na koo zenye makazi ya kudumu kama vile Wajawabra na Wajamaiya zinazoishi katika bonde la kati la Nili na huko Kordofan. Zilidai kuwa ni za nasaba ya babu mmoja wa kukisia tu aliyejulikana kama Abbasid Ibrahim Jaal. Kwa hakika, majina ya kimbari Jama Siya na Jamaab yanadokeza mzizi wa kitenzi cha Kiarabu *Jamaa* chenye maana ya "kukusanya." Kiashirio hiki cha kisemantiki kinarejelea mchanganyiko mwingi na wa muda mrefu baina ya Wanubia na Waarabu ambao waliwaoa kwa hiyari yao binti za wastahiki kutoka Nubia hadi Bornu kupitia Darfur na Wadai. Hivyo, Wanussabbaat wa Kordofan wanadai unasaba wa Jaali.

Wajuhayna walikuwa na asili ya Kiarabu zaidi. Waliendelea kuishi maisha ya kinomadi ambayo yalistawi katika malisho ya mbuga za ufalme wa Alwa, uliokuwa ukiporomoka. Lakini si Wanomadi wote katika kanda hii walikuwa Wajuhayna, kulikuwa pia na Washuriyya, Wakinana na Waarabu wa Kikababishi. Aidha kulikuwa pia na Wabakkara walioko kusini mwa njia ya mashariki-magharibi kuvuka Sudan kwenye ukanda usiofaa kwa kondoo wala ngamia ambao uliwafanya wachague kufuga madume ya ng'ombe. Rangi yao nyeusi sana ni ushahidi wa mchanganyiko mkubwa na Wanubia. Baadhi yao wanadai kwamba babu zao walitoka Tunis na Fezzan. Ama kwa hakika, Wabakkara wanaelekea kuwa matokeo ya mchanganyiko wa Wajudham wa Kinilo na makundi ya kutoka Fezzan na Chad. Mapokeo yanayoelezea uhusiano baina yao na Wabanu Hilal yanaashiria pia kwamba baadhi yao walitoka Afrika Kaskazini.

Pamoja na Waarabu, ni lazima pia kutaja kufika katika ukanda huu kwa Waberiberi asilia au walioathiriwa na Uarabu kama vile Wahowara ambao kuanzia karne ya kumi na kuendelea walitoka Misri na kuingia Kordofan na Darfur.

Mabadiliko ya kijamii na kitamaduni

Tangu zama za kale, Nubia imekuwa makutano ya staarabu za tropiki na Mediterania. Kurithiana kwa dini za kimapokeo, Kikristo na Kiislamu kunasisitiza tu dhima hii ya kalibu hii ambayo inaendelea kuifanya Sudan leo hii kuwa ulimwengu ndogo mahsusi wa Kiarabu na Kiafrika. Kupotea kwa mamlaka kuu ya

madola ya Kikristo lazima kulisababisha umaskini na kutokuwepo usalama kama inavyoshuhudiwa na mapokeo, pasi kutaja kwamba akiolojia ilibaini kupungua kwa kina cha maji katika mto Nili, kukiashiria kuvurugika kwa hali ya hewa.

Ni kweli kwamba mnamo karne ya kumi na mbili mjumbe wa Kiayubi alieleza juu ya nchi iliyokwajuka ikilima tu mtama na tende; lakini karibu wakati huohuo msafiri wa Kiarmenia anazungumzia ustaarabu wa mjini ulioshamiri. Hii inathibitishwa na mabaki ya kiakiolojia yanayoshuhudia kwamba uchoraji ulikuwa wa Kibizenti na ufinyanzi wa jadi ya Kimeroe.

Kati ya kuharibiwa kwa Dunkula na kuwckwa kwa vikosi vya Ottoman mwanzoni mwa karne ya kumi na sita kulikuwa na kipindi cha giza kwa Nubia halisi (yaani Mukurra na Maris). Akiolojia na Isimu vinaweza kusaidia kutoa mwanga kuhusu kipindi hiki. Tatizo la msingi ni kueleza tofauti isiyo ya kawaida baina ya lahaja za Kinubia (Mahasi) zinazosemwa na Wamaha katikati mwa Nubia na zile zinazosemwa kaskazini zaidi na Wakenuz (Kenzi) na kusini zaidi na Wadanakla. Hata hivyo, sifa ya jumla ya kipindi hiki ni kwamba sehemu kubwa ya watu waliokuwa na makazi ya kudumu walibadilika kuwa wanomadi/au nusu wanomadi. Ibn Khaldun ambaye alishii katika kipindi cha mabadiliko, aliona ndani yake uthibitisho wa mpango wake wa kielimu jamii ambao kwao uloweaji ni hatua ya uoza katika mduara wa mageuko ya jamii. Tofauti yake na uchangamfu wa Wanomadi waliokuwa jirani huchochea uvamizi wa Wanomadi kwenye maskani ya kudumu na kuanzisha duara jipya.

Akizungumzia kuvunjwa kwa ufalme na makabila ya Kibedui, hasa Wajuhayna, Ibn Khaldun anaandika: "Hakuna chochote kilichobakia cha mamlaka makuu (*mulk*) katika nchi yao kwa sababu ya mabadiliko yaliyoletwa kwao na athari ya ubedui wa Kiarabu kupitia ndoa mchanganyiko na ushirikiano." Hata hivyo, hatupaswi kurahisisha mno hali hii changamano na kudai kwamba kulikuwa na mtengano wa pande mbili na ujenzi wa unomadi kwa jumla.

Jambo moja la hakiika ni kwamba uigizaji Uarabu ulileta mabadiliko ya kitamaduni wa polepole lakini ya msingi, mathalan, mabadiliko kutoka urithishaji kakeni kwenda urithishaji kuumeni. Vivyo hivyo, kukubalika kwa lugha ya Kiarabu na utafutaji wa Uarabu yalikuwa mambo ya jumla, ingawaje kati ya Nili na Bornu Uarabu huu uliandamana na athari ya wazi ya lugha za Kiafrika juu ya lahaja za Kiarabu hata kama katika Nubia yenyewe (kutoka Assuan hadi Dunkula) usemaji wa lugha mbili ulikuwa umeenea sana.

Wanawake waliondoshwa katika shughuli za hadhara, na desturi mpya za kijamii zilizoongozwa na sharia za Kiislamu zilianzishwa polepole.

Wakati ambapo sanaa na usanifu majenzi wa Kikristo vilitoweka, sanaa ndogo za kienyeji ziliendelea kuwepo katika vifaa vya kiufundi, lakini aonavyo Ibn Khaldun, Mabedui washenzi walioshika madaraka Nubia hawakuleta ufundi wala

usanii aali, ambao wakati huo, ulibainisha nchi za kati za Kiislamu. Katika jambo hili, Nubia ilitolekezwa pembezoni.

Ibn Khaldun pia anataja kwamba usilimishwaji uliwaondolea Wanubia ulipaji kodi (*jizya*). Lakini kama ilivyokuwa wakati wa mkataba wa *bakt*, upungufu wa watumwa mara nyingi ulifanya watumwa washikwe ndani ya Nubia yenyewe na kwa namna hiyo uenezi wa Uislamu ulisogeza maeneo ya kuwawinda na kuwanunua watumwa kusini zaidi kwa hasara ya watu weusi walioishi kati ya Nili ya Juu na kusini mwa Ziwa Chad. Kuoza kwa dola hatimaye kuliishia katika kuimarisha miundo ya kimbari, umaskini uliofungamana na kuzagaa kwa unomadi, na hivyo kurudi nyuma kijamii kwa muda.

Nubia katika Afrika

Wanahistoria leo hii wanafikiri kwamba hapo zamani kigezo cha mtu wa kaskazini au Mwarabu katika historia ya Nubia kilisisitizwa kupita kiasi, dhidi ya maendeleo huru ya ndani na mahusiano na tamaduni za Waafrika weusi. Kigezo hiki kilitokana na kukoskana kwa uwiano katika vyanzo vya historia hii kwa kupendelea nyaraka za Kiarabu, kwani kazi za kiakiolojia, zikiandamana na mapokeo simulizi, ndio kwanza zinaanza kushughulikiwa, zikiwa na matokeo ya kuvutia hasa kufuata mhimili wa mashariki-magharibi wa Sudan na hata ndani kabisa mwa jangwa la Wabeja, ambao baadhi yao, kulingana na maelezo ya Ibn Khaldun, waliupokea Ukristo. Ni muhimu kusisitiza uasilia wa ubunifu wa utamaduni wenyewe wa Kinubia kuhusiana na jumuiya za Kikhufu ambazo watawa wake walikimbilia Nubia nyakati za mateso. Nubia, kwa upande mwingine, iliwasilisha nyaraka zilizopatikana katika nyumba za watawa za Misri ya Juu na kusafirisha bidhaa za Dunkula nje.

Ama kuhusu biashara kupitia Bahari ya Shamu, yajulikana ilikuwa imeshamiri sana hadi karne ya kumi na sita na kuwasili kwa Wareno. Ama kwa hakika, Wafatimi walikuwa wamechagua Nubia kama kiungo cha biashara hiyo na Bahari ya Hindi kupitia bandari za Aydhab, alikokaa Ibn Battuta, na Sawakin. Waarabu na Wabeja walihusika katika misafara hiyo kupitia mikataba. Aydhab, ambayo ilipata ufanisi wake mkubwa kutokana na kufifia kwa njia ya Sinai kulikosababishwa na kuwepo kwa majeshi ya vita vya msalaba hako Palestina, ilififia mwishoni mwa karne ya kumi na nne, Jeddali ilipojitokeza katika ufuko wa Asia. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tano, kufifia kwa mji huu kulisababishwa na uamuzi wa Sultani Barsbay wa kuuangamiza kama hatua ya ulipizaji kisasi dhidi ya Waarabu walioishi hapo na Wabeja walioathiriwa na Uarabu. Sawakin, iliyokuwa kusini zaidi, ilipata umaarufu, ingawa ilikuwa imeshambuliwa na Sultani Baybars kabla ya kutambuliwa na Mamluk waliodai malipo ya mwaka ya watumwa, ngamia na meno

ya tembo. Udhhibiti wa Mamluk uliimarishwa mnamo katikati ya karne ya kumi na tano.

Itabidi tusubiri ushahidi zaidi kabla ya kuweza kusema kama mahusiano baina ya Nubia na Ethiopia ya Kikristo yalikuwa ya karibu zaidi kuliko inavyodokezwa na ushahidi mdogo tulio nao wakati huu.

Ama kuhusu mahusiano na kusini, ni wazi kwamba ni vigumu zaidi kuwa na hakika nao. Ncha ya kusini kabisa ya Alwa ilikuwa karibu na Wad Medani. Waandishi wa Kiarabu, ambao wanawabainisha Wanubia na weusi wengine, wanatoa majina machache ya kimbari kama vile Wakersa na Wabakunna. Ibn Abd al-Zahir anaripoti shambulio dhidi ya Alwa mnamo mwaka 1290, ambalo pengine lilifanywa na mababu wa Wafunji, waliokuwa wamefika Gezira kutoka kusini kwa kufuata *Blue Nili*. Lakini yawezekana washambuliaji walitoka Kanem au Darfur.

Kwa upande wa magharibi, lazima tuwe waangalifu kutofikiria Nubia kama kituo cha kuenca kwa Ukristo hadi Afrika Magharibi kupitia Sudan ya Kati. Wala hatupaswi kukubali bila kuhoji tasnifu ya ueneaji wa mbinu za uyeyushaji chuma ndani ya Afrika kutoka Meroe. Si lazima athari zote za Kikristo au Kiislamu zihusishwe na nchi za bonde la Nili, ingawaje mapokeo simulizi ya Afrika Magharibi mara nyingi hutaja asili za mashariki. Lakini athari kama hizo, ikiwa zilikuwepo, lazima zilitoka kwa Wanubia wa enzi za Kati kuliko kwa Wameroc.

Mabaki kadhaa ya vitu, kwa hakika, yanaelekeza kwenye athari ya utamaduni wa Kinubi katika njia za Sudan kutoka Zenkor na Abu Sufyan huko Kordofan hadi Nguru (Nigeria) kupitia Darfur na Borno. Vifinyange kutoka Zenkor vinafanana na vile vya Soba. Huko Ayn Farah kaskazini mwa Darfur, magofu ya majengo ya matofali mekundu, yaliyobainishwa kama nyumba ya watawa na makanisa, yana magae ya asili ya Nubia ya kati ya karne ya nane na ya kumi na moja, yakiwa yanepambwa na ishara za Kikristo. Katika msururu wa maeneo kama hayo, kuna Birmin Gazargamo ya tarehe ya walau karne ya kumi na sita, wakati maeneo ya Chad huko Koro Toro na Bochianga ya umbali wa kilomita 1450 kutoka Nili yana vifinyange vya tarehe ya kuanzia mwaka 1000 wa enzi ya Kikristo.

Eneo la Darfur huenda lilikuwa na dhima kubwa kuhusiana na Afrika Magharibi, lakini historia yake bado haijawa wazi sana. Yaelekea kwamba kulikuwa na uhamishaji wa mamlaka kutoka kwa Wadaju wa huko kusini hadi kwa Watunjur wa huko kaskazini (pengine mnamo karne ya tisa?) na hatimaye kwa Wafur.

Karibu na mwaka 1240, kwa mujibu wa maelezo ya Arkell, Darfur ilitakwa na Dunama, mfalme mkuu wa Kanem, ambaye mamlaka yake yalienea hadi Nili, huko Maris, katika sehemu iliyo karibu sana na njia inayojulikana kama Darb al-Arbain.

Athari ya Borno juu ya Darfur ilidumu kwa karne nne hasa chini ya utawala wa *Mai Idris* mnamo karne ya kumi na sita. Kwa hakika, mamlaka ya kitamaduni ya Borno yaliyobainika kutoka Nili hadi nchi ya Wahausa au pia hata Gao katika mitindo ya utawala, usanifu majenzi na dhima ya mama malkia, hayaashirii utawala wa kisiasa.

Kwa mujibu wa Arkell, Uri iliyoko kaskazini mwa Darfur, ilikuwa jiji la Watunjur na baadaye la Kanem. Inawezekana lilikuwa jiji muhimu la biashara katika njia-panda ya Darb al-Arbain na njia ya savanna ya mashariki-magharibi inayojulikana kama *tarik al-Sudan*. Haeleweki kama njia hiyo ilitumiwa na misafara ya hija kabla ya karne ya kumi na sita. Hadi wakati huo, njia ya kawaida kutoka Sudan hadi sehemu takatifu, ikiwa ni pamoja na zile za watawala, ilipitia pwani ya Afrika Kaskazini, Misri na Aydhhab. Mnamo karne ya kumi na sita, uvamizi wa Moroko huko Gao na kupungua kwa usalama kulikofuatia, vilikuwa na athari chanya kwa ustawi wa njia ya magharibi kabisa kufuata upwa wa Atlantiki, na pia njia inayopitia bonde la Nili, iliyokuwa matokeo ya kubomolewa kwa utawala wa Kikristo huko Nubia na kuimarishwa kwa mamlaka ya Kiislamu huko Sennar, Darfur na Wadai. Aidha, Uislamu, mwanzoni, zaidi ya yote ulikuwa dini ya kifalme chini ya Watunjur na ulienea tu kwa umma chini ya Kayra Fur mnamo karne ya kumi na saba.

Hapa, kama ilivyokuwa huko Nubia, uingizaji wa Uarabu hatimaye ulileta mabadiliko ya msingi ya kitamaduni, kidini, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mnamo mwaka 1391, Sultani Barkuk huko Kairo alipokea barua kutoka kwa mfalme wa Borno ikilalamikia udhalimu wa Wajudham na Waarabu wengine ambao walikuwa wakivateka watu wake hata kama walikuwa Waislamu, kuwafanya watumwa na kuwauza kwa wafanyabiashara kutoka Misri, Shamu na kwingineko. Tukio kama hili linaonyesha mabadiliko yanayovuka kabisa kipindi kinachoshughulikiwa katika juzuu hili.

17


Pembe ya Afrika: Wasulemani katika Ethiopia na Madola ya Pembe ya Afrika

Jiografia ya Kisiasa ya Pembe ya Afrika toka karne ya 13 hadi ya 16

Hali ya kisiasa ilikuwa changamano mno. Dola lililojulikana sana katika nyanda za juu za kaskazini za Ethiopia, lilikuwa ni Ufalme wa Kikristo ambao, mnamo mwaka 1270, ulitoka mikononi mwa Wazagwe na kutwaliwa na ukoo tawala uliodai kuwa wa kizazi cha Mfalme Sulemani. Ufalme huu ulienea hadi Shoa huko kusini na hadi kwenye fuko za Ziwa Tana na *Blue Nili* ya juu huko magharibi. Huko kaskazini-magharibi kulikuwa na ufalme wa Mafalasia (wajulikanao pia kama Wayahudi wa Ethiopia) na huko Kusini-Magharibi kulikuwa na ufalme wa Gojam na vile vile dola lenye nguvu la Damot ambalo liliwakilisha imani ya kijadi dhidi ya tawala za Kikristo na Kiislamu, na ambalo lilikuwa na mamlaka juu ya ukanda mzima ya nyanda za juu za Shoa. Kuhusu maamiri ya Kiislamu, haya yalienea kwenye upwa wa Bahari ya Shamu kutoka Ghuba ya Aden na Bahari ya Hindi kupitia Zeila, Berbera, Mogadishu na Marka na pia ndani ya nchi huko mashariki chini ya vilima vya nyanda za juu za Ethiopia, Bali, Ifat, Adal, n.k. Hivyo mamlaka hizi zilifaidi nafasi muhimu katika sehemu hii ya kiini kwenye njia ya viungo ya kimataifa.

Watu na Lugha

Pembe ya Afrika ni "makumbusho ya watu". Makundi kadha ya lugha za Kiafrika yanawakilishwa hapo, kukianza kundi la Kongo-Kordofani na la Afrika-Asia lenye matawi matatu yafuatayo: Kikushi (kama vile Kibeja, Kiagew, Kiburgi Sidamo, Kigalla na Kiomo katika bonde la Omo, n.k.); Kisemiti (k.v. Kiharari katika Harar iliyotekwa na wanamfalme wa Kiislamu waliokimbilia hapa kutoka Ifat; Kiamhara.



17.1 Ethiopia na Pembe ya Afrika (Tadesse Tamrat)

lugha ya watu wa ukoo tawala wa Kisulemani, Kigurage na Kigeez). Hii iliyotajwa mwisho ilikuwa lugha ya maandishi ya Kanisa la Ethiopia tangu karne ya nne, na imeendelea hivyo hadi leo hii. Ama kuhusu Kitigre na Kitigrinya, zote zinazungumzwa huko Eritrea na Tigre. Kiarabu kilikuwa lugha ya dini na biashara kote katika sehemu ya mashariki ya ukanda huu.

Tawala za Kiislamu za Pwani

Madola kongwe ya Kiafrika (Falasha, Gojam na Damot) yanajulikana kwetu kupitia tarikhi za falme za Kikristo na Kiislamu, na hata hivyo kwa baadaye sana; na hizo Tarihi zinayaonyesha tu pale yanaposhindwa vitani. Ni utafiti wa kiakiolojia na kiisimu tu utakaotuwzesha kupata maarifa ya kina ya historia ya watu hawa. Kwa upande mwingine, mamlaka za Kiislamu zinajulikana vizuri zaidi.

Huko kaskazini zaidi, Visiwa vya Dahlak, ambavyo pamoja na Visiwa vya Farasan kwenye musoma wa Bara Arabu ni kivuko kati ya Yemen na Eritrea, vinadhiti misafara katika sehemu ya kusini ya Bahari ya Shamu. Wakati fulani visiwa hivi vilidhibitiwa na Yemen lakini vikajikomboa mnamo karne ya kumi na tatu; vilikuwa na utawala uliotegemea biashara na uharamia, na vilifaulu kuhifadhi uhuru wake dhidi ya majaribio ya kuvitawala yaliyofanywa kwa ushindani na Mamluk wa Misri, na watawala wa Yemen na wa Ethiopia.

Kusini zaidi, chini ya Ghuba ya Aden, Ibn Battuta ambaye alisafiri kupitia eneo hili mnamo karne ya kumi na nne, anautaja Zeila, mji uliokaliwa na "Waberbera" weusi (Wasomali), waliojijhusisha na ufugaji wa ngamia na kondoo, uvuvi na biashara.

Makdishu (Mogadishu) ulikuwa pia kituo kikubwa cha biashara ambacho, kwa mujibu wa Ibn Battuta, kilisafirisha nje nguo zisizo kifani; aidha Mogadishu ililima kiasi kikubwa cha mpunga, matunda (ndizi na maembe) na mboga. Mji huu ulikuwa chini ya mamlaka ya shehe akisaidiwa na mawaziri. Ulitawaliwa na umvinyi wa wafanyabiashara, wanasharia na watumishi, na ulipata sifa kubwa za kimataifa kwa hali yake ya kimji na ukarimu mkubwa wa watu wake.

Uislamu na mafunzo ya Kurani tukufu yaliendelezwa sana humo, lakini lugha asili ya Kiafrika na miundo ya kijamii na kitamaduni iliyohusiana nayo viliendelea kutumika.

Wanajiografia wa Kiarabu pia wanatueleza juu ya miji mingine mitatu ya biashara katika ukanda huo. Kwanza kulikuwa na Berbera, ambao ulikwishatajwa na Ptolemy na katika *Periplus of the Erythraean Sea*. Jina la mji huu lilitumika kuita Ghuba ya Aden ambayo wanajiografia wa Kiarabu waliita Bahari au Ghuba ya Barbara; na walibainisha wakazi wake kwa uangalifu kama Waberabir na Waberberi, Waswahili na Wahabeshi. Hawa pengine walikuwa Wasomali.

Ikiwa kwenye pwani ya kusini ya Pembe, miji ya Merka na Brava ilikuwa ndani ya mzunguko na mtandao biashara wa Mogadishu, ambayo ilipakana na sehemu ya bara iliyokuwa tajiri na changamfu.

Madola ya Kikristo na Kiislamu kuhusiana na jamii zilizoamini dini za jadi za Kiafrika

Kuanzia karne ya kumi, utanuzi wa mtandao wa biashara wa pwani hadi bara kwa kupanua njia za ndani ulikuwa jambo kuu ambalo lilileta mapambano makali baina ya tawala za kanda hiyo. Katika njia hizi mlipita athari nyingi za kitamaduni na za kidini. Kutoka katikati ya karne ya kumi na tatu, hata ufalme wa Kikristo wa Zagwe huko kaskazini mwa Ethiopia ulikuwa ukitumia kama lango la kutokea sio tu usultani wa Dahlak bali pia bandari ya kusini ya Zeila. Maendeleo ya bandari hii ya Zeila pengine yataelezeka kutokana na utamalaki wa dola ya Kiislamu ya Ifat iliyoko kati ya Ghuba na nyanda za juu za Shoa; lakini pia na uhamisho wa kitovu cha kisiasa cha Ethiopia ya Kikristo kuelekea kusini na majilio ya ukoo tawala wa Kisulemani¹.

Yekuno-Amlak, mmojawapo wa viongozi wenyeji huko Amhara, anaelezwa na mapokeo kama mtu aliyekomesha ukoo tawala wa Zagwe mnamo mwaka 1270, na, kulingana na mapokeo hayo, akarejesha ukoo tawala wa kale wa Kisulemani wa Aksuni. Kwa yakini, kwa muda mrefu makazi ya Kikristo katika majimbo ya kusini mwa Ethiopia yalikuwa yanahusika katika mtandao wa mahusiano ya kibiashara ulioenea kutoka Ghuba ya Aden hadi nyanda za juu za Shoa, ukielekea hasa katika bonde la Avwash, na kuingiliana sana na Waislamu na wafuasi wa dini za jadi.

Mmoja wa watawala anayejulikana sana wa jamii zilizofuata dini za jadi ni mfalme wa Damot anayetajwa na Ibn Khaldun. Alitawala eneo hili mnamo karne ya kumi na tatu na makazi ya Kikristo na Kiislamu yakateseka wakati wa utawala wake. Kufikia karne ya kumi na mbili, Wakristo tayari walikuwa wamenza kujiamini kwani linatajwa shambulio lililoshindwa la Zagwe dhidi ya Damot ambamo mfalme wa Zagwe aliuliwa. Lakini polepole mamlaka ya Zagwe yalichukua nafasi ya yale ya Damot hadi kufikia hatua ambapo Wakristo walijihesabu kuma raia wa Wafalme wa Zagwe. Baadhi yao walidhibiti njia za biashara kati ya Shoa kwa upande wa Kusini na Tigre kwa upande wa kaskazini ambako walileta chumvi waliyobadilishana na farasi na nyumbu. Wakristo hawa pia walijihusisha na kilimo mchanganyiko kiliehoshamiri sana na kilichotegemea familia

¹ Huitwa hivyo kwa sababu ulidai kuwa kizazi cha mfalme Suleman

kubwa na kazi ya watumwa wengi. Makazi yao, ambayo yalikuwa na fahiwa thabiti kuanza kutii ufalme wa Zagwe, utii uliofidiwa kwa athari halisi ya kiuchumi ya utambulisho wa Kikristo, yaliacha kulipa ushuru kwa wafalme wa Damot na iliyotegemezwa kwenye nafasi yao kama wafanyabiashara wa kati.

Jamii za Kiislamu nazo zilianza kutawaliwa na wafalme wa jadi wa Kiafrika. Nao pia walikuwa na fahiwa thabiti ya kuwa asili yao ni Meka. Walishindana wenyewe kwa wenyewe na polepole walijiondoa Damot. Nyakati fulani tawala zao ziliungana kuunda mamlaka kubwa zaidi kama vile "Usultani wa Shoa" au Ifat. Walisema lugha za Kiethiopia-Kisemiti, na kuishi kwao kwa raha, kulitegemezwa, kwa kiasi kikubwa, kwenye biashara ya masafa marefu, wakishirikiana, pale inapolazimu na majirani zao Wakristo wa Shoa na Amhara. Bandari ya Zeila, lango la biashara kutoka Ethiopia ya Kati, ilinufaika mno na ushirikiano huu kwa moyo wa uvumilivu. Yaelekea kwamba, kabla ya kunyakua madaraka, Yekuno-Amlak alikuwa amekwishajenga mashirikiano na jamii za Kiislamu na za Kikristo huko Shoa. Katika barua aliyoituma kwa Baybars wa Misri (karne ya kumi na tatu) alijigamba kwa kuwa na Waislamu wengi wapanda farasi katika jeshi lake.

Hivyo, wakati ikidai utukufu wa kale, hapo nasaba ya Kisulemani ilitegemea nguvu za kiuchumi na kijeshi katika majimbo ya kusini, na kwa hiyo iliamisha makao makuu ya himaya ya Ethiopia kuelekea Amhara na Shoa.

Ufalme wa Ethiopia chini ya mamlaka ya Wasulemani

Mwanzo wa utawala wa Kisulemani ulikuwa mgumu ndani na nje. Moja ya matatizo makubwa ya kutafutiwa ufumbuzi lilikuwa ni lile la kurithi kiti cha enzi. Suluhisho lifuatalo lilitumiwa: ndugu wote wa Yekuno-Amlak isipokuwa vizalia vyake, waliwekewa pamoja katika vilele visivyofikika' vya Mlima Geshen, na kuwekwa ulinzi mkali. Wanamfalme waliozuiliwa majumbani huko walinyimwa mawasiliano yote na sehemu za nje, lakini walihudumiwa vizuri. Walianza kupata mafunzo ya sanaa yenye mchomo wa kidini. Na ni pale tu alipofariki mtawala bila kuwa na mrithi ndipo mmoja wa hawa waliopelekwa uhamishoni alipochaguliwa kuwa kiongozi wa nchi. Hii ilizusha jina la "mlima wa wafalme" lililotumika kuita kasri hii ambayo pia ilikuwa jela asilia uliyogezwa kuwa asasi ya dola.

Lakini hatari kutoka nje ilikuwa ya kutisha zaidi: hii ilihusu mahusiano na tawala za Kiislamu zilizokuwa zikizidi kupata nguvu kati ya Ghuba ya Aden na bonde la Awash. Lakini wakati wa kutawazwa madarakani Amde-Siyon (mnamo 1314-44), mjukuu wa Yekuno-Amlak, nguvu ya Wasulemani iliyokuwa imefia, ikiwa imepunguzwa eneo lake hadi kulingana na mipaka ya nchi kongwe ya Zagwe,

ililazimika kukabiliwa na uchochezi wa jamii za Kiyahudi (Wafalasha) na wafuasi wa dini za jadi, pasi ya kutaja ya kujipanua kwa Waislamu. Mapambano ya ushindi yaliyoongozwa na Amde-Siyon dhidi ya Damot na Gojam, yaliishia katika kutamalakiwa kwa eneo la kaskazini mwa Ziwa Tana, na udhibiti wa vituo vya mwisho vya misafara ya biashara kutoka Ghuba ya Aden.

Kushindwa huku kiuchumi na kisiasa kulisababisha hasira na chuki katika duru za Kiislamu kuchukua nafasi ya uvumilivu uliokuwepo hapo kabla.

Akitumia kisingizio cha kutekwa na kutiwa utumwani mmoja wa raia wake na mwana mfalme Akl Din wa Ifat, Mwislamu aliyekuwa na nguvu nyingi kupita wote katika kanda hii, Amde-Siyon aliteka Ifat ambayo, baada ya kifo cha kiongozi wake mwanamfalme, katika vita, ilifanywa dola kibaraka chini ya Ethiopia. Mamlaka nyingine kama Dawaro zililazimika kuingia mikataba ya urafiki. Tukiongezca katika haya, utamalaki wa awali wa nchi za jamii zilizofuata dini za jadi kama vile Damot na Gojam, ni dhahiri kwamba Ethiopia ya Amde-Siyon ilikuwa imelimbikiza rasilimali kubwa ya watu na bidhaa. Maasi yaliendelea kuwa sugu, kama yale ya mwaka 1320 yaliyolitia msukosuko jimbo la Kikristo la Tigre, na yale ya mwaka 1332, wakati maasi ya sawia yalipoitikisa mamlaka ya Kikristo, lakini ikaibuka ikiwa imeimarika zaidi. Sifa za ujasiri wa Amde-Siyon zilienea sana Mashariki ya Kati, kwa kiasi kwamba al-Umari, aliyeishi wakati wa matukio haya, alimwelezea Maliki wa Ethiopia kwa maneno haya: "Yasemwa kwamba ana wafalme tisini na tisa chini yake na kwamba yeye ni wa mnia moja."

Ingawa idadi hii imekuzwa mno, bado ni ya kuvutia, kwani mwanahistoria huyu wa Kiarabu alijumuisha miongoni mwazo "falme saba za Kiislamu za Ethiopia."

Madola ya Kiislamu na Ethiopia

Himaya iliyoundwa na Amde-Siyon haikuwa na umoja wa kidini, kimbari na kiisimu. Kwa hakika, kama anavyosisitiza al-Umari, ingawa mamlaka yalirithiwa katika falme zilizotekwa, hakuna hata mmoja miongoni mwazo uliokuwa na mamlaka thabiti bila ya kubarikiwa na mfalme wa Amhara."

Udhibiti huu wa kisiasa wa madola yaliyotawaliwa ulifanya iwe lazima kuwa na jeshi kubwa la kudhibiti majimbo na nchi zilizotekwa. Majeshi yaliyowekwa katika eneo moja yalitokana na watu wa eneo jingine la mbari tofauti ili kuhakikisha utii wa askari. Hii ndiyo ilikuwa gharama ya kudumisha himaya, kukusanya ushuru na kuhakikisha usalama wa njia kuu za biashara. Askari wa ziada kutoka nchi jirani walipelekwa walipohitajika, na hali ilipokuwa mbaya, kama ilivyokuwa mwaka wa 1332, mtawala mwenyewe aliongoza jeshi kwenda kuzima uasi. Ama kwa hakika, upanuzi uliokuwa ukiendelea daima uliwalazimisha wafalme kuweka ufalme katika hali ya vita, na kutokuwa na makazi maalum katika mji mkuu kwa sababu ya haja ya kuonyesha nguvu za serikali katika kila mkoa.

Muundo wa himaya ya Ethiopia

Kwa hiyo, kambi lenye kuhamahama la Wafalme wa Kisulemani ndilo lilikuwa kituo cha utawala na kitovu cha kiuchumi na kisiasa cha himaya, na pia subu ambamo mbari kuu na tamaduni mbalimbali ziliendelea kuunganishwa. Kambi hilo lilikuwa na walenzi wa mfalme na vikosi vya askari, makasisi waliohudumia makanisa ya kifalme, na wafanyabiashara na mafundi wa Kikristo na Kiislamu ambao walikuta, ndani ya kambi hilo, mahitaji na soko lenye faida kubwa kuliko yote katika himaya. Wakati wa kiangazi, idadi ya watu waliosongamana hapo ilikuwa ni pamoja na ile ya wanamfalme mateka, magavana waliopeleka zawadi na raia waliokuja kutafuta maamuzi ya mfalme na ya watumishi wake. Hii ilifanya lilingane na mji wa wastani ambao uhamahamaji wake ulifanikisha shughuli zake, kwani tofauti na makazi ya kudumu, lilipelekwa miongoni mwa wakazi wa vijijini. Kwa namna hii lilitia uhai zaidi katika mahusiano na mikoa yote na hivyo kukuza mchanganyiko wa kitamaduni na muunganiko wa kisiasa. Hii ilikuwa kweli hasa kwa wafungwa ambao waliingizwa kwa wingi katika jeshi la Kikristo na kupewa kazi katika jumba la mfalme, wakati wanamfalme wa nchi zilizotekwa walizuliwa katika kasri kama wageni au mateka, mara nyingi wakiteuliwa baadaye kushika nyadhifa za juu na hivyo kujitoa kwa dhati kuitumikia himaya.

Hata hivyo, ni muhimu kutofumbia macho ukandamizaji ulioambatana na hatua zilizosababisha mahitaji makubwa ya wafanya kazi na bidhaa. Kwa hakika, umbo la kawaida la manlaka ya kisiasa katika himaya lilikuwa la utawala usiokuwa dhahiri (wa kupitia wengine), uliodumisha mila za mahali fulani. Kwa hiyo, kwa namna fulani, uhamaji wa makao ya mfalme ulikuwa ni hatua za udhibiti wa kati ulionuiwa kupunguza tofauti za kikanda. Hili lajitokeza juu ya yote kwenye ongezeko katika ukubwa wa baraza la mfalme na jeshi wakati wa Amde-Siyon. Tokea wakati huo, kutolipa ushuru kulilingana na tendo la uhaini. Kuwapatia mashamba raia wengi ilikuwa zawadi kwa huduma na wakati huo huo kichocheo cha kutoa huduma zaidi. Udhibiti wa kijeshi wa ndani ya nchi ulioleta watumwa wa *kihabasha*, ambao walikuwa wakitafutwa sana Mashariki ya Karibu, wakinunuliwa na kuuzwa na Waislamu, ulileta mapato zaidi yaliyohifadhiwa kama dhahabu na meno ya tembo, ambazo ndizo zilikuwa bidhaa kuu za biashara katika ukanda. Zaidi ya hayo ardhi zenye rutuba za nyanda za juu za Ethiopia ziliipelekea miji ya pwani nafaka na matunda. Watawala wa Ethiopia walinufaika mno na shughuli hii ya kiuchumi kwa namna mbili: kwanza, kwa namna isiyo ya moja kwa moja kwa kutoza ushuru bidhaa zilizoingia na kutoka nchini; lakini, zaidi ya yote, kwa kuwekeza raslimali moja kwa moja kwenye biashara ya masafa marefu. Lakini, hatimaye, upanuzi wa kijeshi, kisiasa na kiuchumi wa Wasulemani uliishia tu kuchochea, na kama jibu lake, ushirikiano zaidi baina ya manlaka za Kiislamu katika eneo hilo, hasa chini ya


uongozi wa tawi lililojitenga la ukoo wa Umar Walasma ambao, ukiendesha shughuli zake kutokea nyanda za juu za Harar, ulijenga mtandao madhubuti wa mashirikiano katika eneo kati ya Visiwa vya Dahlak na pwani ya Somalia katika Bahari ya Hindi. Hapa palikuwa kimbilio la upinzani wa Kiislamu dhidi ya utawala wa Ethiopia hadi *Jihad* ya Imam Gragn katika karne ya kumi na sita.

Ufufuaji wa Kanisa la Ethiopia

Kipindi kuanzia karne ya kumi na tatu hadi ya kumi na sita pia kilishuhudia ufufuaji wa nguvu wa Kanisa la Ethiopia. Mwanzoni, Kanisa lilikuwa limeimarika tu huko kaskazini, katika majimbo ya kale ya Eritrea, Tigre, Lasta (chimbuko la Wazagwe na mji wa maaskofu) na Amhara. Na hata katika eneo hili la mwisho, ni mnamo tu wakati wa kutawazwa mamlakani kwa Wasulemani ndipo taasisi maarufu ya watawa ilipoanzishwa na mtawa mashuhuri kutokea Lasta aitwaye Iyesus-Moa. Kadri himaya ilivyopanaka kuelekea kusini, Waamhara na Washoa walianza kujiundia mtandao wa asasi kubwa za kidini ambazo zilikuwa vituo vya kueneza imani ya Kikristo kuelekea pande zote. Mambo mawili makuu yanaelezea uenezi huu mkubwa: kwanza ni vuguvugu la ndani katika Kanisa lenyewe, na pili ni sera ya makusudi ya Wasulemani ambao walijihusisha zaidi na mahubiri kuliko wafalme wa Zagwe, wakiwa na raslimali kubwa zaidi.

Hivyo nyumba ya watawa iliyoanzishwa na Iyesus-Mo'a huko Amhara katika kisiwa kwenye Ziwa Hayk ilifuatwa na nyingine nyingi kote kusini mwa nchi. Lakini kanuni katika asasi hizi ziliendeleza jadi kongwe ya waasisi wa maisha ya kitawa, wajulikanao kama Watakaifu Anthonio na Pakomio. Mwanzoni, nia ya waasisi wa Ethiopia, kama ilivyokuwa ya mifano yao ya Misri, haikuwa kueneza imani, bali kutafuta wokovu binafsi kwa kuiacha dunia na kuishi maisha ya kusali kimoyomoyo na kutoa kafara katika sehemu zisizofikika, kama vile, majangwani, milimani, mapangoni, visiwani, n.k. Lakini maisha haya ya kujitiisha pekee au katika jumuiya yenye wafuasi wachache lazima yaliwavutia wenyeji ambao punde tu walianza kueneza sifa za watawa na ujasiri wao wa kiroho.

Polepole, wacha Mungu kutoka miongoni mwa watu wa kawaida au hata kutoka miongoni mwa familia za kifalme walikuja kujiunga na watawa. Taratibu zake zikawa changamano zaidi. Kwa mfano, jumuiya ilipata wakfu wa ardhi ikajijengea kanisa, shule na hospitali na ikaanzisha mfumo wa uzalishaji na ugawaji kutosheleza mahitaji ya kiroho na kimwili. Mafukara, wakongwe na mayatima walichanganyika na mahujaji. Mfumo msonge wa watawa waliochaguliwa kidemokrasia uliishi kwa kanuni thabiti zenye ingawanyo wa kazi kama vile usanii wa hati za maandishi, uchoraji picha za kidini, muziki na ualimu. Nyumba kuu za kitawa nchini zilishindana baina yao kuwavutia mabingwa wakubwa walioshehenezwa sifa nyingi



17.2. Lalibela: Kanisa la Mtakatifu George, picha ya juu ya kanisa Lililofukuliwa (Picha: G. Geister/Agence Rapho, Paris, 1979)

na fedha. Wanafunzi hodari lakini maskini walipata msaada na mara nyingi waliingia katika maisha ya kidini ama kama watawa waliojiwekea nadhiri ya kutooa, au kama makasisi waliooa. Hata hivyo, shule za kitawa hazikutengwa kwa ajili ya watumishi wa baadaye wa kanisa tu. Zikiwa ndizo zenye ukiritimba katika masuala ya ufundishaji, shule hizi ziliwavutia vijana wote ambao walikuwa na tamaa ya kujiunga na tabaka la juu la Wakristo na serikali ya nchi.

Hii ilikuwa kweli hasa kuhusiana na wanamfalme waliozuliwa katika Mlima Geshen.

Kanisa lilikuwa na udhibiti huu wa ufundishaji tokea wakati wa ufalme wa Kikristo wa Aksum hadi karne ya kumi na nne na wakati wa kuenea kwa nyumba za watawa huko Amhara na Shoa; na hii inaelezea nafasi muhimu ya watumishi wa kanisa katika vyombo vya dola.

Hivyo, Ethiopia nzima ilienca nyumba za kitawa kutokana na juhudi za waumini wa kwanza kutoka nyumba za kitawa ambazo ndizo zilikuwa za kifahari nno. Hizi ni kama vile Debre Asbo (ambayo baadaye iliitwa Debre Libanos), iliyoanzishwa huko Shoa na Tekle-Haymanot (katika karne ya kumi na tatu), Debre Gol huko Amhara iliyoanzishwa na Abba Anorewos na Daga katika kisiwa kwenye Ziwa Tana. Katika sehemu ya kaskazini kabisa ya nchi, ikiwa ni pamoja na Eritrea ya

sasa, mwamko wa kitawa uliwezekana mno kutokana na uchangamfu mkubwa wa Mtakatifu Abba Ewostatewos.

Kwa kibali cha maliki Amde-Seyon, Askofu mkuu wa Kimisri (*abunna*) wa Kanisa la Ethiopia, Askofu Yakob, alizipanga nyumba za kitawa katika madaraja yaliyoongozwa na kanuni na dayosisi. Mfalme ambaye alikuwa akianzisha ngome za kijeshi nchi nzima, alikuwa na shauku kusaidia kueneza nyumba za kitawa miongoni mwa Wafalasha huko Gojam (Gojam) katika Damot na hata katika mashamba ya Kiislamu ya Ifat, Bali, n.k. Watawala ambao walitoa ardhi kubwa kwa nyumba za watawa, walitaka wenyeji wazilinde, na hawukusita kumwadhibu vikali yeyote aliyeshindwa kufanya hivyo. Hivyo, katika nyoyo za watu waliokuwa wafuasi wa dini za jadi au ya Kiislamu, taswira ya Kanisa la Ethiopia ilikuwa imefungamanishwa mno na ubeberu wa Kiethiopia. Aidha, nyumba za kitawa zilizodekezwa sana zilishindwa kudhihirisha uhuru wao wa uadilifu. Hii ndiyo huelezea kwa nini taathira zake halisi katika nchi zilikoanzishwa, ilikuwa ndogo, na kwa hakika athari hiyo iliyeyuka mwanzoni tu mwa mashambulizi ya Waislamu mnamo karne ya kumi na sita.

Zaidi ya hayo, Kanisa hili, kiroho, lilitegemea Askofu mkuu wa Kikhufu wa Aleksandria ambaye aliwateuwa maaskofu wa Misri kuongoza ngazi za kidini katika himaya. Daraja mbili za kitawa au “nyumba” zilikuwa na hadhi zaidi katika Kanisa la Ethiopia. ‘Nyumba’ ya Tekle-Haymanot, na nyumba mama yake, huko Debre Libanos, ilihusiana kwa karibu sana na jumba la mfalme jambo ambalo liliipatia utii wa jumuiya nyingi za kidini. Ama kuhusu nyumba ya Ewostatewos, tangu karne ya kumi na nne iliwakilisha kundi dogo kali ambalo lilianzisha nyumba za watawa toka Tigre hadi Eritrea ambako ndiko nyumba kuu ya kitawa ya Debre Bizen ilianzishwa.

Lazima itambuliwe kuwa Kanisa hili la Ethiopia pia lilikuwa limegawanywa sana kimadaraka. Jamii ya maaskofu ya Kimisri na mfalme walifanya kila waliloweza kupunguza mgawanyo huu wa madaraka ili kukita mamlaka yao. Walifaulu kwenye makanisa ya kawaida yaliyokuwa na makasisi waliooa ambao hadhi yao ilitegemea matakwa ya walei. Kwa upande mwingine, nyumba kuu za kitawa zililinda uhuru wao kwa uchu. Maskanini mwa maaskofu wa Kimisri na katika jumba la mfalme, kulikuwa na maofisa wa kidini. Aliyekuwa na hadhi kubwa zaidi miongoni mwao katika msafara wa kifalme alikuwa *akabe-seat* aliyechaguliwa awali kutokana na watawa wa nyumba ya watawa ya kisiwa cha Hayk kabla ya maaboti wa Debre Libanos kuanza kufanya kazi hii kutokana na nyadhifa zao.

Kipindi cha kati ya karne ya kumi na tatu na karne ya kumi na sita, kwa hakika, kilikuwa cha neema mno katika historia ya Kanisa la Ethiopia. Japokuwa kulikuweko na ushindani wa kila mara baina ya mashirika ya watawa ya Tekle-Haymanot na ya Ewostatewos, harakati za kitawa zilifanya kazi kubwa katika



17.3 Mswada ya Kiethiopia wa karne ya kumi na tano, ukionyesha Upastaji Habari za Duni (UNESCO/New York Graphic Society, Ethiopia 1961)

upanuzi wa Kanisa na vilevile katika ufufuaji wa utamaduni, kama Guidi na Cerulli walivyodhihirisha kuhusu mchango wake kuhusiana na fasihi. Sanaa hazikuachwa nyuma katika kipindi hiki, kama inavyoonyeshwa na miswada iliyonakshiwa, michoro ya kwenye kuta za kanisa na misalaba na fimbo za maaskofu zilivyopambwa mno sanaa ambazo zimedumu kwa karne nyingi hadi leo hii. Wafalme wakuu walikuwa wadhamini wenye ujuzi, kwani aliyekuwa maarufu mno miongoni mwao, Zera-Yakob (1434 - 68), inasemekana aliandika tasnifu kadhaa za kidini. Vuguvugu la shughuli za kidini lazima nyakati fulani zilizusha mitarafuku mikubwa juu ya masuala ya kimadhehebu na ya kiliturjia. Katika hali hii, mafundisho ya maaskofu wa Kimisri yalizidi kupingwa na mapadre wakaidi wa Kiethiopia ambao, hadi kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tano, walikaribia kutengana kabisa na Uaskofu mkuu wa Aleksandria.

Mapambano baina ya Wakristo na Waislamu: kutokea kwa Wareno

Uaskofu wa Aleksandria huenda, hasa, ulikuwa kama namna ya pingu kwa Kanisa la Ethiopia, lakini pia ndio uliokuwa kivuko muhimu kwenda kwa Wakristo wa Nchi Takatifu na nchi nyingine za Kikristo. Kwa maneno mengine, ndio uliokuwa kiungo na tegemeo kuu.

Mamlaka ya Kiethiopia yalikuwa yanaelewa fika jambo hili. Hii ndiyo sababu mivutano na Kanisa la Kikhufu la Misri haikutoka kuwa mfarakano wa wazi. Ama kwa hakika, Ethiopia ilijikuta katika ukinzani mkubwa: ilitaka kutumia nafasi yake kama dola la Kikristo kuanzisha mahusiano ya kiuchumi na kijeshi na nchi za Ulaya na wakati huo huo, ilikuwa na shauku ya kulinda mahusiano ya amani na majirani zake wa Kiislamu walioishi pande zote mbili za Bahari ya Shamu, hasa Yemen. Hii ilikuwa lazima kwa kuwa Misri ya Mamluk ambayo ilidhibiti njia zote hadi Mediterania na Bahari ya Hindi, ilizuia karibu njia zote zilizokuwa muhimu kwa diplomasia ya Ethiopia. Hali hii inasaidia kuelewa kwa nini viongozi wa Ethiopia waliendelea kupeleka watumwa na dhahabu na zawadi nyingine kwa sultani huko Kairo kila walipokuwa wakijadiliana kuhusu kutculiwa kwa askofu mpya wa Kimisri au kupita kwa mahujaji wa Kiethiopia kwenda katika Sehemu Takatifu. Lakini wakati wa utawala wa Amde-Seyon, himaya ya Ethiopia ilipotanda hadi katika maeneo ya Kiislamu ambayo kimsingi yalikuwa chini ya ulinzi wa Sultani wa Misri, madai ya wafalme wa Kikristo yalikuwa dhahiri zaidi. Hivyo, Seyfe-Arad, mriti wa Amde-Seyon, aliongoza jeshi lake hadi bonde la Nili katika jaribio la kuimarisha kuzingirwa kwa Aleksandria na mfalme wa Kupros mnamo 1365. Al-

Makrizi anaripoti kuhusu ushindi wa Dawit I (1380-1412) juu ya Waarabu katika eneo la Aswan na juhudi za Mfalme Yishak (1413-30) kuunda ushirika na Ulaya ya Kikristo ili kukomesha utawala wa Kiislamu Mashariki ya Karibu. Ujumbe wa kisiri ambao Yishak alituma Ulaya ulizuiwa na utawala wa Misri wakati wa kurudi na kiongozi wake akanyongwa. Wakhufu walipoteswa huko Misri, Zera-Yakob (1438-68) alilalamika vikali na akamfunga balozi wa Misri kwa miaka minne aliporudisha majibu ya kejele kutoka kwa sultani. Yalikuwa ni mabadiliko makubwa toka wakati ambapo, mnamo karne ya kumi na tatu, Yekuno-Amlak wa Ethiopia alijieleza kuwa ni "mtumishi mnyenyekevu kuliko watumishi wote" wa Sultani Baybars.


Tangu karne ya kumi na nne hadi ya kumi na sita, watawa wa Ethiopia wakilindwa na nguvu mpya za wanamfalme wao, waliunda msururu wa jumuiya ndogondogo zilizoenea hadi Roma, Florensi na Venisi, kwa kupitia bonde la Nili, Nehi Takatifu na Visiwa vya Kupros na Rhodes. Maelezo ya nguvu za ajabu mno za wafalme wa nchi yao tangu enzi za Amde-Siyon, yaliwafanya wazungu wengi kuwafananisha watawala hawa wa Kikristo na "Presta Yohana" wa hadithini; hasa pale uamuzi wa Mamluk kukata mawasiliano yote baina ya Ulaya na Ethiopia ulipowafanya Waethiopia kupeleka ujumbe zaidi kaskazini mwa Mediterania.

Mnamo mwaka 1450, ujumbe mmojawapo ulitembelea Roma na Naples na kurudi na mafundi na wasanii kadhaa wa Kizungu. Baadhi ya wanamikakati hata walifikiria kwamba Waethiopia wangeshiriki katika vita vya msalaba vya mwisho. Lakini, hatimaye, siasa ya kilinwengu ilikuwa dhidi ya Ethiopia. Njia za kufika Mediterania zilidhibitiwa kutoka pande zote na Mamluk; na kwa kupitia kwa askofu mkuu wa Aleksandria mwenyewe ambaye alidhibiti Kanisa la Ethiopia, walikuwa na karata ya turufu iliyotishia misingi yenyewe ya mfumo wa wafalme wakuu wa Ethiopia. Hivyo wafalme hawa wa Ethiopia, walilazimika mwishowe kukubaliana na matakwa ya Kairo.

Sultan Jakmak, wakati akijibu vitendo vya Zera-Yakob, alifanya askofu mkuu wa Aleksandria apigwe na kumlazimisha amwombe mfalme wa Ethiopia kumfungulia balozi-wake; sasa askofu mkuu mwenyewe ilibidi apate ruhusa ya kuwasiliana na Ethiopia kutoka kwa sultani. Matokeo yake yalikuwa kwamba ilichukua miaka thelathini kabla ya askofu mpya kutawazwa - miaka thelathini ambamo Waethiopia walianza tena kujinyenyekeza na kupeleka zawadi kwa sultani. Ni baada ya hapo tu ndipo "makasisi waliongezeka, Makanisa yakarudishiwa hadhi yake na nchi ikajaa furaha." Hivyo hali ya Ethiopia ilishawishi kuwepo utegemezi kwenye mambo ya kiroho na hii ilipeleka kuwepo kwa utegemezi katika mambo mengine mengi.

Kupea na kudidimia kwa Ethiopia

Mwishoni mwa karne ya kumi na tano, baada ya upeo wa utamalaki wa Wakristo katika utawala wa Zera-Yakob, nchi ilianza kuporomoka. Maliki huyu alikuwa amerekebisha na kulisafisha Kanisa la Ethiopia. Alikwisha patanisha kundi la watawa wenye msimamo mkali la Ewosatawos na "nyumba" nyingine za watawa na hivyo kuondoa tishio kubwa kwa utulivu kwenye mfumo. Alikwisha ondoa pia mabaki ya imani na matendo ya kidini ya jadi, kabla ya Ukristo. Mwenyewe akiwa mwanazuoni wa kidini, alikwisha watesa watawa wapinzani na kuanzisha huko Debre Berhan (Shoa), makao makuu yenye utawala unganifu. Hii ilimwezesha kuzima mashambulizi ya kila mara ya ufalme wa Adal uliokuwa kwenye majimbo ya mashariki na kukomesha juhudi za sultani wa Hadya za kufanya maasi. Katika sehemu ambayo leo hii ni nyanda ya juu ya Eritrea alianzisha ngome ya askari jasiri wa Maya waliohamishwa kutoka Shoa. Huu ulikuwa ndio upeo, lakini gharama yake ilikuwa kubwa. Njama kubwa zilizimwa kikatili. Hii ndiyo sababu mwana na mrithi wa Zera-Yakob, Beide-Maryam (1468-78), alianza kwa kuwasamehe wafungwa na kulegeza maovu ya utawala wa kuhodhi madaraka. Lakini hii ilipelekea tu kuongezeka kwa milipuko ya maasi ambayo Beide-Maryam alipata taabu kubwa kuyadhibiti hadi kifo chake. Aliwaacha wana wadogo wawili na hivyo makundi mawili ya wafuasi yaliyopigana yenyewe kwa yenyewe. Si ajabu kwamba kushindwa kwa dhati kwa mara ya kwanza kwa jeshi la Ethiopia na majeshi ya Adal kulitokea wakati wa utawala wa Beide-Maryam. Kuporomoka huku kuliendelea bila kusita hadi anguko la mwisho kabla ya jihad ya Imam Gagn.



Maendeleo ya Ustaarabu wa Waswahili

Kipindi baina ya karne ya kumi na mbili na kumi na tano kilikuwa ni cha maendeleo wenye visiwa na pwani ya Afrika Mashariki ya watu waitwao "Waswahili" na madola yao, yaliyojulikana tangu karne ya kumi. Kuwasili ghafla kwa watekaji wa Kireno katika karne ya kumi na sita kuliashiria na kukatisha kilele cha ustaarabu wa Waswahili.

Hadi karne ya kumi na mbili, hakukuwa na jumuiya ya aina moja. Katika mbari, watu wa pwani walishuhudia kuingia kwa watu kutoka bara na ng'ambo ya bahari: Waarabu, Waajemi na Wahindi. Kijamii, umma wa watu wa kawaida ulitawaliwa na tabaka la watawala waliofanya shughuli za kijadi, na tabaka la wafanya biashara, lililokuwa na nguvu za kiuchumi. Watumwa walikuwa bado hawajawa wengi wa kutosha kustahili kutajwa kwenye Tarehe, lakini ilipofika mwisho wa karne ya kumi na tano, taarifa ya Wareno inaeleza juu ya watumwa waliofanya kazi za shamba huko Kilwa. Kwa hiyo, kulikuwa na tofauti kubwa za kijamii ambazo kwa bahati mbaya hazijulikani sana kutokana na ukosefu wa nyaraka.

Uchumi na Biashara

Kilimo na uvuvi

Hizi ndizo zilizokuwa shughuli kuu mbili za uzalishaji mali. Al-Masudi (karne ya kumi) anaorodhesha mazao ya chakula yafuatayo: ndizi, *dura* (aina ya mtama mweupe), viazi vikuu na nazi. Waandishi wengine wanataja ukwaju na miwa. Katika karne ya kumi na tano, Mreno mmoja anataja machungwa, malimau, kunde za aina mbalimbali, pamba na ng'ombe huko Kilwa. Pia za kusokotea zilizokutwa kwenye magofu zinathibitisha kuwa watu hawa walisokota nyuzi na kufuma nguo.

Uvuvi, ambao Al-Idrisi anasema kuwa ulikuwa ndio shughuli kuu ya Malindi, umeelezwa mara nyingi na waandishi wa Kiarabu ambao wameeleza pia kwamba lulu, simbi na magamba ya kasa yalikusanywa na kuuzwa. Simbi zilitumiwa

kutengeneza vidani, vijiko, sahani, n.k.

Utaalamu wa ubaharia ulikuwa wa aina mbili: uundaji wa vyombo vya bahari, iwe mitumbwi au mitepe, na kutokana na taarifa za Mreno yuleyule ambaye hakutajwa jina, waliunda hata *jahazi* la tani 50. Aina hizo mbalimbali za vyombo zinadhihirishwa na majina mengi ya vyombo yaliyomo kwenye lugha ya Kiswahili. Aidha, uchunguzi wa elimu ya falaki waliyonayo watu wa eneo hili unaonyesha kwamba maarifa hayo yasingekuwa na maana na yasingeweza kupatikana kama si safari za kibiashara za Bahari ya Hindi.

Biashara na Ukaaji Mijini

Waandishi wanaeleza makazi ya aina mbili: vijiji na miji. Vijiji vilijengwa kwa matofali ya udongo, mianzi na makuti pamoja na paa za nyasi na makuti. Wanakijiji waliwinda chui (mara nyingine chui hao walipunguzwa ukali kwa matambiko) na walifua chuma. Ngoma kubwa ilitumiwa katika ibada zao za kijadi. Miji tayari ilikuwa na majengo ya mawe ambayo ndiyo yalikuwa makazi ya watu mashuhuri na wafanya biashara wa jamii ya Waswahili pamoja na wanazuoni wa Kiislamu. Biashara ilileta faida sana kutokana na makadirio ya thamani ya bidhaa ambayo hayakuwa na viwango maalumu. Kwa hali hiyo, vifaa kutoka nje vilichukuliwa kuwa ni vya anasa kutokana na uadimu wake, na vilibadilishwa kwa dhahabu na pembe za ndovu ambazo zilipatikana kwa wingi huko bara na hivyo kupewa thamani ndogo.

Katika karne ya kumi na mbili bidhaa nyingi zilipitia Zanzibar na visiwa vya Lamu. Lakini ufukuaji wa kiakiolojia unaonyesha pia kuwa mji wa Manda, ulio kwenye kisiwa chenye jina hilohilo, ulikuwa muhimu kuanzia karne ya tisa, na kwamba uliendelea kuwa muhimu hadi karne ya kumi na tatu, ambapo umaarufu ulichukuliwa na Kilwa, kama ilivyodhihirishwa na mabaki ya vyungu vya Kisasani-Kiislamu, kauri za Song kutoka China, marundo ya simbi, shanga za vioo, n.k. Huko Gedi viliingizwa vyungu vya Kiislamu vya "rangi nyeusi na njano".

Baada ya nyaraka nyingine za Kiarabu kueleza juu ya usafirishaji nje wa dhahabu kutoka Sofala, al-Idrisi anaeleza juu ya mlolongo wa miji ya pwani na visiwani ambapo meli zilitia nanga, kama vile Brava, Mombasa, Pangani na Unguja (baadaye ulijulikana kama Zanzibar). Alieleza ifuatavyo juu ya Malindi: "Chuma ndio chanzo chao kikubwa cha mapato na bidhaa kuu ya biashara." Aidha, mavi ya chuma yamegunduliwa. Pia, kulikuwa na ngozi za chui na samaki.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tatu, Yakut anaandika pia juu ya Mogadishu iliyokuwa na watu mchanganyiko, wakiwemo Waarabu Waislamu. Ulikuwa ni mmoja kati ya miji mizuri ya Afrika ya Mashariki, iliyosafirisha nje mpingo, sandali,

pembe za ndovu na ambari.


Pia, Yakut ndiye wa kwanza kuitaja Kilwa kwa jina hilo. Kilwa ilitawaliwa na wale walioitwa wa nasaba ya Washirazi ambao walipata ushindani kwa muda kutoka kwa Wasanje (labda kutoka kisiwa cha Sanje ya Kati). Inaelekea kilichogombewa ni kumiliki njia za biashara. Kutokana na *Tarihi ya Kilwa*, Kilwa hatimaye ilitawala, na kukuza ustaarabu wa Waswahili chini ya mfalme mkuu mpya, Abu Mawahib. Kiasi cha bidhaa zilizoingizwa Kilwa kiliongezeka: vyungu vya grafito, kauri, chupa za manukato na wanja. Vifaa vya aina hiyohiyo, ambavyo vilitoka hasa Iran na Irak, vimegunduliwa huko Gedi.

Hata hivyo, biashara hiyo ilifikia kilele chake katika karne ya kumi na nne, kama anavyoeleza Ibn Battuta, ambaye alitembelea eneo hili mnamo 1332. Anataeleza kuwa Mogadishu ilikuwa kituo kikuu cha biashara, ambapo kila mfanyabiashara wa kigeni angeweza kupata mwenzi au wakala wa kuendesha biashara zake. Mji huo ulisafirisha nje *makdashi* (kitambaa cha Mogadishu), ambayo iliuza hadi Misri ambako nguo nyingine zilitoka, kama vile zilivyotoka Yerusalemu.


Ufukuaji wa hivi karibuni unedhihirisha kukua kwa mji wa Pate, kwenye kisiwa chenye jina hilohilo, katika kipindi hichohicho. Kauri za kijani za Kiislamu zilizong'arishwa kwa monokromi ya kijani, na idadi kubwa ya vipande vya kauri za bluu za Kichina zenye umbo la fimbo zilionekana kwa mara ya kwanza mnamo kipindi cha pili cha karne ya kumi na nne.

Kauri zenye rangi ya bluu na nyeupe za Ming zilifika Gedi kwa mara ya kwanza mnamo karne ya kumi na tano. Hata hivyo, katika kipindi hichohicho Kilwa ilielekea kuanguka kutokana na migongano baina ya vikundi vilivyogombania madaraka. Hata hivyo, bidhaa kutoka nje ziliendelea kuongezeka na kulikuwa na kauri maradufu kutoka China ikilinganishwa na vyungu vilivyotoka nchi za Kiislamu.

Zaidi ya ongezeko la usafirishaji nje wa dhahabu, pembe za ndovu, vipusa, ambari, n.k. kuliongezeka pia watumwa na nguo zilizoingizwa kutoka nje na zile zilizosafirishwa nje katika biashara iliyozunguka baina ya Mombasa, Kilwa na Sofala. Zaidi ya hayo, kulingana na *Tarehe ya Kilwa*, kisiwa hicho kilinunuliwa kwa nguo iliyokuwa na urefu sawa na mzingo wake. Bandari za Afrika Mashariki zilikuwa ni vituo tu vya mapumziko katika safari iliyunganisha mabara ya Asia na yale ya magharibi kupitia Bukini na Bahari ya Shamu. Aidha, vituo vya uzalishaji mali vilivyokuwa bara, kama vile migodi ya dhahabu karibu na Ziwa Nyasa, na ile ya Sofala, viliingia mikononi mwa watawala wa Kilwa mnamo karne ya kumi na nne. Ugunduzi wa kiakiolojia, kama vile shanga za njano zilizofukuliwa Zimbabwe ambazo zilifanana na bidhaa za vioo zilizoenea India katika karne ya kumi na tatu, ulionyesha wazi mahusiano yaliyokuwepo baina ya pwani na wamiliki migodi ya bara, kuanzia bonde la Zambezi, kama inavyoonyeshwa na simbi zilizotumiwa



18.1 Biashara ya ndani na ya kuvuka bahari kwenye pwani za Afrika Mashariki kati ya karne ya kumi na mbili nanya kumi na tano (V.V. Matveiev)



18.1 Inuendelea

kubadilishana na dhahabu na pembe za ndovu huko Gokomere na Kolomo. Vilevile, huko Engaruka, iliyoko Tanzania ya hivi sasa, simbi na shanga za vioo za tangu karne ya kumi na tano na kumi na sita na ambazo zinafanana na zile zilizokutwa Kilwa zinaonyesha biashara zinazofanana na zilizotumia mbinu zinazoelezwa na al-Idrisi (karne ya kumi na mbili): "Wao wenyewe husafirisha mizigo yao kwa vile hawana wanyama wa kubeba mizigo. Hujitwika bidhaa kichwani au kuzibeba mgongoni kwenda miji miwili - Mombasa na Malindi. Huko huuza na kununua."

Zaidi ya simbi, walitumia shanga za vioo na kauri kama sarafu, na mwishowe, katika miji mikubwa kama vile Kisiwani, Mafia, Zanzibar, Pemba, na zaidi ya yote Kilwa baada ya kuibuka kwa Ufalme mkuu wa Shirazi, walitumia sarafu za shaba na fedha. Kuwepo kwa sarafu zilizokuwa na thamani kubwa ya kubadilishana kuliko simbi kunaonyesha ukubwa wa biashara iliyofanyika na thamani ya bidhaa zilizofanyiwa biashara. Kuwepo kwa dhahabu nyingi Kilwa kuliifanya isitumiwe kama njia ya malipo. Lakini kutokuwepo sarafu za metali zilizoonyesha mahali, tarehe na thamani yake Mchoro 18.1 *Biashara ya ndani na ya kuvuka bahari kwenye miji ya Afrika Mashariki kati ya karne za 12 na 15*, kuna weza kuashiria kwamba kitu kilichokuwa muhimu hapa kufuatia utamaduni wa kutumia simbi ambao ulipokuwepo, ilikuwa ni idadi ya sarafu zilizohusika.

Biashara, ikiwa chanzo cha faida kubwa, ilikuwa pia muhimu katika maendeleo ya jamii na utamaduni, hasa kutokana na mabadilishano yaliyohusisha ulimwengu wa Kiarabu, Kiajemi, Kihindi na Kichina. Wachina waliingia tu katika shughuli hizi moja kwa moja kuanzia karne ya kumi na tano, wakati jeshi lililoongozwa na Cheng-Ho lilipofika katika maceo haya. Hadi kufikia karne ya kumi na moja, vyombo vya biashara vya China havikwenda kusini au magharibi zaidi ya Java na Sumatra.

Ustaarabu wa Waswahili kuanzia karne ya kumi na tatu hadi kumi na tano

Kadiri biashara ilivyogeuka kuwa ya kati ya mabara ndivyo vijiji vilivyogeuzwa kuwa miji mikubwa. Tabaka maarufu la wafanyabiashara liligombea madaraka na koo mashuhuri za jadi zilizopata madaraka yao kutokana na kutimiza shughuli maalumu za kijamii. Tabaka hili jipya lilijijenga na itikadi mpya ya Kiislamu, iliyoletwa na Waarabu na Waajemi, na hivyo kuwa washirika wao. Dini hii ilikubaliwa kwa urahisi na wafanyabiashara hawa hata kabla ya karne ya nane. Mnamo karne ya kumi, Al-Masudi anaripoti juu ya kuwepo kwa Waislamu wanaoongea lugha ya Kiafrika kwenye kisiwa cha Kambala. Kufikia karne ya kumi na tatu, eneo la pwani lilikuwa limeathirika sana. Lakini Uislamu huu haukufanana

na ule wa nchi za Kiarabu, kwani uliingiza mila nyingi. Kilichokuwa muhimu ni kuonekana kuwa muumini wa Kiislamu, na hivyo kukubali imani hiyo mpya. Dini hiyo mpya ilikubalika na wengi na kupata waumini zaidi kadiri muda ulivyopita, na kusababisha ujenzi wa misikiti mingi.

Mnamo Karne ya kumi na nne, Ibn Battuta aliieleza Mogadishu kuwa mji ulio wa Kiislamu sana. Ameeleza pia kuwa kwa wakazi wa Kilwa "imani na haki ni sifa zilizothaminiwa sana." Wakati huo, kulikuwa na misikiti Gedi, Sanje, Magoma na kwingineko. Kusilimu kuliandamana na ishara nyingine dhahiri kama vile mavazi ya Kiislamu na vyeo ambavyo polepole vilibadili ufahamu wa watu. Hata hivyo, kulikuwa na kipindi cha kuwepo pamoja kwa tamaduni zote mbili, kwa mfano baina ya cheo cha *sultani* na kile cha *mfalme*. Kama ilivyokuwa kwingineko, watu wa kwanza kuikubali imani hiyo mpya walikuwa ni wafanyabiashara matajiri, baadaye watu mashuhuri na kisha watu wa kawaida ambao waliiga tu. Kilichofuata ni kukubali vipengee vingi vya mfumo wa sharia za Kiislamu. Ibn Battuta anagusia juu ya kuwepo makadhi Mogadishu na Kilwa. Hatimaye, maneno kadhaa ya kisimu yalikopwa kutoka Kiarabu kwa ajili ya mahitaji ya biashara, uhasibu, dini, haki na upendeleo maalumu. Lugha ya Kiswahili iliibuka polepole kutokana na mahitaji hayo muhimu na iliandikwa kwa hati za Kiarabu, ambazo zilirekebisliwa kufuatana na mantiki na misingi ya Kiswahili chenyewe.

Ukuaji wa miji na usanifu majengo

Kuenea kwa Uislamu kuliambatana na maendeleo katika ujenzi wa mawe na misikiti. Kulingana na Kirkman na Chittick, mwanzo wa aina hii ya ujenzi ulikuwa karne ya kumi na mbili huko Gedi, Zanzibar na Kilwa. Mwanzoni wahiridhika kujenga vipande vya matumbawe kwa udongo wa mfinyazi kama walivyojenga msikiti wa Kilwa. Mnamo karne ya kumi na tatu, ufundi mpya unaonekana katika baadhi ya misikiti ya Kisimani: matumbawe yenye umbo la tofali yalishikizwa na mchanganyiko wa chokaa na udongo, chokaa ambayo ilitokana na kuchomwa kwa matumbawe.

Katika karne ya kumi na nne, huko Kilwa, mji ambao ulikwishakuwa kituo kikuu cha biashara wakati huo, mabadiliko mapya ya mbinu za ujenzi wa kutumia mawe yalitokea: lakini ujenzi huo ulitumiwa tu katika kumalizia mihirabu na kuzungushia madirisha na milango. Vitu vipya vilionekana: makuba, nguzo na misingi iliyorembwa, zege zenye umbo la nusu mcheduara, n.k. Yote haya yalionekana Kilwa tu, kwenye kasri iliyotumiwa kama ngome na kituo cha biashara cha Husuni Kubwa. Inawezekana jengo hilo lilijengwa karne ya kumi na nne na inawezekana pia kuwa lilitumiwa kama mfano wa makazi ya watu mashuhuri. Wakati wa kujenga

majengo sehemu ya mbele ya majengo haya ilitokea kwenye uga wenye mlango mmoja ulioingia kwenye chumba cha kwanza. Vyumba vilikuwa virefu na vyembamba vilivyotazamana, na karibu vyote vilikuwa giza kwa vile havikuelekea kwenye uga. Kwenye pembe moja, nyuma ya jengo, kulikuwa na vyoo. Nyumba kama hizo zilikuwepo Gedi, Kisimani Mafia na Kilwa.

Husuni Kubwa haina mfano na ni upeo wa ujenzi, ingawa matumizi yake hayajajulikana kabisa. Ikiwa na makazi kadhaa, ina sehemu wazi ambayo bila shaka ilitumiwa kama bwawa.

Kwenye karne ya kumi na nne, Kilwa ikawa mji mkubwa wenye nyumba za mawe. Karne ya kumi na tano ilileta maendeleo zaidi katika njia za ujenzi. Kuanzia wakati huu, zege ilimiminwa kwenye chonibo na kifusi kikaongezwa, hata makuba yalijengwa kwa namna hiyo. Nguzo, ambazo zilikuwa za moja kwa moja zilianza kujengwa kwa kumimina zege la mehanganyiko wa mawe na udongo. Majumba ya ghorofa moja au mbili yalijengwa kwa njia hiyo, yakiwa na vyumba vya chini kwa chini na makuba yaliyorembwa kwa majagi ya kauri kutoka China na Uajemi yaliyowekwa ndani ya kuta za jengo. Msikiti Mkuu wa Kilwa uliomalizwa wakati wa utawala wa Sultan Sulayman al-Adil (1412-42) unabakia kuwa moja ya maajabu ya ujenzi wa Kiswahili.

Mawazo juu ya asili ya majengo haya yanatofautiana. Baadhí, kama Freeman-Grenville, baada ya kulinganisha majengo haya na nyumba za kawaida zenye kuta za udongo, wanasema kuwa yanatokana na ujenzi wa wenyeji, na hali wengine wanadhani kiwa yanatokana na Waarabu na Waajemi. Baadhi ya usanifu unaojitokeza haulingani na ujenzi unaotokana na Uislamu: kwa mfano, kuwepo nakshi ya kigumba kwenye msikiti wa Gedi. Lakini karibu waandishi wote wanakubaliana kuwa "ujenzi wa pwani ya Waswahili umeendelea kuwa wa aina yake na kuwa na jadi zilizodumu karne nyingi na kuutenganisha na ule wa Arabuni, Uajemi na nchi nyingine za Kiislamu." Hata kama waliiga mifano kutoka nje, waliurekebisha kufuatana na hali ya maeneo yao, kwa mfano kwa kutumia vifaa vinavyo patikana hapohapo.

Kufuatana na taarifa za Wareno, mitaa ya Kilwa ilikuwa myembamba yenye nyumba za udongo zilizozekwa kwa makuti, na nyumba za mawe zenye vibaraza kwa upande wa mtaani. Kasri ndiyo iliyokuwa kivutio kikubwa. Majengo yalikuwa na milango ya mbao iliyochongwa na kurembwa kifahari, kama inavyoonekana Bagamoyo na Zanzibar. Majengo hayo hayakuwa ya hali ya chini zaidi ya yale ya Ureno, walisema wasafiri wa kwanza wa Kizungu, ambao walivutiwa na utajiri wa wakazi wa maeneo haya, na utanashati wao kutokana na nguo za pamba na hariri zilizotarizwa kwa dhahabu. Wanawake walivaa hariri na vikuku vya dhahabu, fedha au vito vya thamani. Taa za udongo na mishumaa iliyokutwa kwenye ufukuaji



18.2 *Mihrab ya Msikiti Mkuu wa Gedi (S. Unwin)*

inaelekea ilitumiwa kutoa mwanga kwenye sehemu za giza za nyumba hasa kwa ajili ya kusoma, kuandika au kuhesabu.

Samani zilikuwa ni mazulia, mikeka, vigoda, vitanda vikubwa vya anasa vilivyopambwa kwa pembe za ndovu, lulumizi, fedha na dhahabu. Vyombo kutoka nje vilitumiwa kwenye nyumba za watu mashuhuri: vyungu na kauri kutoka Iran, Irak, China, Misri na Shamu. Vyungu vya maenco haya vilivyotumiwa na watu wa kawaida ni pamoja na majagi yenye kitako cha duara ama kilicho chongoka kwa ajili ya kuinjikwa na vyombo vya kupakulia chakula visivyvo na kina.

Miundo ya madaraka

Miji ya Kiswahili haikuwa tu vituo vya biashara na Uislamu bali pia miji mikuu ya falme kuu za kienyeji za Kiislamu. Kilwa ni mfano dhahiri. *Tarihi* yake ambayo imetujia katika fasili mbili; inatueleza kuwa ufalme mkuu ulikuwa na asili ya Uajemi na ulitoka Shiraz. Asili hizo za kubuni ni nyingi katika pwani ya Afrika Mashariki

na kwinginckokwenye bara hili. Uchunguzi wake utatuwezesha kusuluhisha kwa uhakika tatizo la asili ya ustaarabu wa Waswahili.

Kutoka visasili hadi kuwa uhakika wa kihistoria

Kuna nadharia mbili juu ya mada hii. Kufuatana na nadharia moja, ni Waajemi na Waarabu ndio waliojenga miji, kuingiza Uislamu na kuendeleza utamaduni wa hali ya juu pwani, wenyeji wa Kiafrika wakiwa wasaidizi wasio na hadhi, kama watumishi, mahawara na wateja. Lakini mchango huu kutoka nje ulipungua polepole na, bila mchango huo, historia ya maeneo haya ingekwama. Fasili hii, iliyotolewa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na Justrandes, inatokana na nadharia ya Hegel inayowagawa watu wa dunia hii katika mafungu mawili, wale wanaounda historia na wale walio nje ya historia na wanaoteseka kimyakimya kutokana na vitendo vya kikundi hicho cha awali. Nadharia hii bado inatawala wanahistoria na wanaakiolojia kadhaa. Nadharia nyingine, iliyobuniwa na mwanaakiolojia wa Kiingereza, Chittick, na wa Kirusi, Misiugin, inafanana na mawazo yaliyoasisiwa na wanahistoria wa Kiafrika, Joseph Ki-Zerbo na Cheikh Anta Diop, ambayo ni kuwa Waafrika walishiriki kikamilifu kwenye historia yao. Uchunguzi zaidi unaendelea kuonyesha kuwa falme kuu za mijini na watu mashuhuri wa maeneo haya walikuwa na asili ya Kiafrika.

Mfumo wa kukabidhi madaraka

Kazi ya Misiugin kuhusu *Tarihi ya Pate* inaonyesha kuwa kabla ya kutokea kwa ufalme mkuu wa Nabhani kulikuwa na dola iliyotawaliwa na Wapate waliokuwa na cheo cha *mfalme*. Zaidi ya hayo, ufalme huu mkuu ulibakisha mfumo wake wa makundi yaliyoundwa chini ya misingi ya undugu na marika. Cheo cha *mfalme* kilikuwa ni cha pamoja na hakikukabidhiwa mtu mmoja bali wanandugu ambao walijumuisha baadhi ya koo za Wapate. Hivyo cheo cha *mfalme* hakikuwa cha maisha, bali kilirithishwa kutoka kwa ndugu mmoja hadi mwingine mara anapooa mke anayetokana na ukoo wa Kipate wa rika linalotawala. Kwa ufupi, kila mwanamume wa ukoo alikuwa na cheo cha *mfalme*, mali ya ukoo isiyogawika, na alishika cheo hicho kwa muda, wakati wanawake ndio waliochukuliwa kuwa ndio watanzaji wa haki hii. Ilikuwa ni kwa kumwoa mwanamke wa Kipate ndipo Sulayman, mwanzilishi wa ufalme mkuu wa Nabhani, alipopata cheo cha mwanamfalme wa Pate. Hukupata cheo hicho kwa kuwa mkewe alikuwa binti wa mfalme wa wakati ule bali kwa kuwa alikuwa kwenye kizazi cha ndugu ambao walikuwa washike cheo hicho. Hata hivyo, haikuwa na maana kuwa jamii ya Waswahili ilibakia kuwa jamii iliyofuata koo tu. Kufuatana na Misiugin, ina maana kuwa Wapate, ambao walikuwa na nguvu za kiuchumi, walihodhi madaraka ya siasa ufuatana na mifumo ya undugu iliyokuwepo. Lakini Sulayman alihusika na

ukoo wa kifalme kupitia kwa mkewe tu. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza kulikuwa na hatari ya cheo cha *mfalme* kutoka nje ya ukoo kwani kutokana na mfumo wa *undugu* cheo hicho kilirithishwa ndugu wa kiume wa mfalme. Mke wa mwanamfalme alikuwa ni mtunzaji wa haki ya kidhahania ya cheo cha mwanamfalme, cheo ambacho kilishikwa na mumewe.

Kwa kutumia fasili hii kuangalia *Tarihi ya Kilwa*, imewezekana kuonyesha kuwa mfumo wa *undugu* ulitumiwa hapa pia katika kukabidhi madaraka. Kwenye sura ya kwanza ya maandiko hayo, tunaona kwamba mtawala wa kwanza, Muhammad, alirithiwa na nduguye wa kiume, Baskhat, na kisha mtoto mmojawapo wa Baskhat. Lakini huyo mtoto alikuwa amenyang'anya madaraka kutoka kwa ami zake. Hii ni kufuatana na haki ya kijadi ya *undugu* ambapo madaraka hukabidhiwa kwa shemeji wa arayeshikilia ubinti mfalme. Kwenye sura ya tatu ya *Tarihi*, kisa kingine kinathibitisha fasili hii. Lakini fasili ya Kiswahili ya *Tarihi ya Kilwa na Tarihi ya Pate* inawafanya masultani wa kwanza kuwa ni Waajemi waliooa mabinti wa machifu wa maeneo yanayohusika. Hivyo ndivyo ilivyotokea kwenye miji mingi mingine. Hivyo, ufuataji wa kanuni za wenyeji katika kukabidhi madaraka unatuwezesha tuhitimisha kwamba mfumo wa dola ulitokana na wenyeji, licha ya utamalaki, rasmi na wa kuhusika, wa Uislamu na mila zake.

Uislamu na itikadi ya madaraka

Inawezekana athari hii ya Uislamu iliakisi kuibuka kwa waumini katika jamii ya Waswahili waliotajirika kwa biashara. Ili kudhibiti nguvu hii, watawala wa maeneo haya wakaamua waungwe mkono na Waislamu, kwa kuwaoza binti zao kwa wafanyabiashara matajiri, kwa mfano, ambao kwa upande wao walijipachika asili za Kiarabu au Kiajemi ili kujipa hadhi sawa na watawala. Hivyo, visakale vya mfululizo wa vikundi vya wahamiaji wa Kiislamu baina ya karne ya saba na ya kumi kwenye miji iliyokuwepo, vilibadilishwa kuwa ngano zilizoeleza juu ya kuwasili kwa wahenga waanzilishi kutoka Arabuni na Uajemi. Visasili vya aina hiyo havikuwa vya maeneo haya pekee. Kwani ufalme mkuu wa Ethiopia haukudai kuwa unatokana na Mfalme Sulemani na Malkia Sheba? Isitoshe, watu wa Sudan Mashariki hudai kuwa wanatokana na machifu wa kabila la Kiarabu; na mwanzilishi wa ufalme wa Kanem, Sefe, hutambuliwa kuwa ndiye mfalme Sayf wa Yemen. Na Keita wa Mali hujinasibisha na masahaba wa Mtume Muhammad, na asili ya baadhi ya Wayoruba hurudishwa nyuma hadi kwa Wakaanani wa Palestina ya kale. Inasemekana kuwa falme kuu nyingi za Kiafrika ziliundwa na wageni wahamiaji wcupe. Mwelekeo huu wa jumla unalingana na wakati ambapo tabaka mashuhuri katika jamii huibuka na kutaka kujitenga kabisa na asili ya watu wa kawaida.

Hitimisho

Ingawa ustaarabu wa Waswahili ni wa asili ya Kiafrika, maendeleo yake yanatokana na biashara, hali ambayo ilikuwa na faida zake na hasara zake hasa kwa vile ustaarabu huu haukujengwa na nguvu za uzalishaji mali, ambazo zinaelekea zilivia. Jamii ya Waswahili haikuunda masoko ya ndani kwa ajili ya mazao yake yaliyotokana na uwindaji, ama uchimbaji wa dhahabu na chuma; ilitegemea nchi za nje kwa ajili ya maendeleo yake, kama maelezo kuhusu kuanguka kwake yanavyodhihirisha.

Baadhi ya mambo yanayodaiwa kuuangusha ustaarabu huu (kwa mfano, ukame na mashambulizi ya Wazimba) si chochote yakilinganishwa na kuanguka kwa biashara ya ng'anibo ya bahari iliyoharibiwa na Wazungu. Mahabaria wa Kireno waliokuwa na mizinga walishikilia vyombo kadhaa vilivyoshehenczwa kwa bidhaa, wakazamisha vyombo vingi vya Zanzibar na kushambulia na kuharibu miji ambayo hapo awali ilijaa uhai, hasa Kilwa. Hili ndilo tukio lililoua ustaarabu wa Waswahili.

19

Kati ya pwani na Maziwa Makuu

Mwanzoni mwa kame ya kumi na mbili, sura ya Afrika Mashariki iliyotokana na vipindi vilivyotangulia ilikuwa ni ile ya uhusiano wa karibu baina ya mazingira na mbari. Idadi ya watu ilikuwa bado ndogo licha ya uhamiaji wa Wabantu ambao walijikusanya kwenye maeneo yenye maji mengi yenye angalau mvua za mm1,000 kwa mwaka. Kwenye maeneo hayo, upandaji wa nafaka na ufugaji wa baadhi ya mifugo haukuondosha aula iliyowekwa tangu zamani katika upandaji wa mazao ya mizizi. Kwa upande mwingine, kwenye miinuko ya Kenya na Tanzania, kilimo mchanganyiko, kilichojumuisha ulimaji wa nafaka na ufugaji mkubwa, kilitawala. Hapa, waliishi watu waliozungumza lugha za Kinilo, ambapo kusini waliishi Wakushi wa Kusini.

Bara ya Afrika Mashariki

Katika pwani ya mashariki, inawezekana kuainisha makundi makuu matatu ya Wabantu: wazungumzaji wa Kisabaki, wazungumzaji wa Kiseuta na wazungumzaji wa Kiruvu.

Kisabaki

Kisabaki kilikuwa na lahaja tatu katika pwani ya Kenya: Kimiji-Kenda cha zamani, Kipokomo na Kiswahili cha kale ambacho kilizungumzwa pwani kwenyewe.

Jamii hizi za Wasabaki ziliondolewa na watu wenye aina nyingine ya maisha, kama vile wazungumzaji wa aina za mwanzo za Kisomali na Wanilo wa Kusini. Mfumo wa marika ambao ni wa utamaduni wa Kisabaki hasa unaweza kuwa umetokana na mahusiano baina ya Wabantu na Wanilo wa Kusini hata kabla ya 1600. Kwa kweli, wafugaji wa bara na Wabantu wa pwani walishirikiana na watu waliokuwa wawindaji na wahameaji, kama vile Waboni waliokaa Kaskazini nwa

Mto Tana, ingawa walikwisha chukua lugha ya wafugaji wa Kisomali ambao ndio waliokuwa wengi kwenye eneo hili. Vilevile, Wadahalo, ambao ni wazungumzaji wa Kikushi cha Kusini, walikuwa na msamiati wenye maneno ya mkopo ambayo yalidhihirisha mahusiano yaliyoendelea baina yao na Wapokomo waliokuwa wengi na Waswahili.

Waseuta

Waseuta waliishi kusini mwa Wasabaki. Hadi mwaka wa 1100 wa kipindi cha Kikristo, Waseuta wa kale walikwishaongeza mimea yenye asili ya Indonesia kama vile majimbi na ndizi kwenye mimea ya Kiafrika. Miaka 500 iliyofuatia, Waseuta wa kale walijigawa kwenye makundi matatu: wale walioongea lahaja za Kishambala, na jamii za wazungumzaji wa Kizigula-Ngulu cha kale, na mwishowe kikundi kilichozungumza Kibondei cha kale.

Wabantu wa Ruvu

Mwisho, kusini mwa Waseuta, kulikuwa na Wabantu wa Ruvu walioishi kwenye bonde la Wami. Mnamo kame ya kumi na mbili, walikuwa katika jamii mbili kila moja ikiwa na mtindo wake wa ukulima. Jamii za Ruvu mashariki, ambazo zilitoa Wakutu, Wazaramo na Wakami, zilitamakani kwenye mabonde yaliyo na maji mengi na zilishiriki kwenye kilimo chenye asili ya Kiafrika na Kiindonesia. Waruvu wa magharibi, kwa upande mwingine, ambao lugha yao inazaa Kigogo cha leo, waliishi kwenye maeneo ya juu, na walichagua kilimo cha nafaka na kufuga.

Kutoka kwa Ziwa Nyasa hadi Ziwa Viktoria

Mnamo kame ya kumi na mbili, eneo kubwa la makazi lilikuwa ni lile la kaskazini mashariki mwa Ziwa Nyasa ambako watu waliozungumza Kinjombe cha kale waliishi. Hao ndio waliokuwa wahenga wa wazungumzaji wa Kihehe, Kisangu na wengineo. Magharibi zaidi, kulikuwa na kundi la watu waliozungumza aina ya Kinyakyusa. Kwenye eneo la miinuko baina ya Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika walikuwepo Wanyiha na Walapwa wa kale, ambapo kwenye maeneo baina ya Ziwa Nyasa na pwani ya Bahari ya Hindi kandoni mwa mto wote wa Ruvuma kulikuwa na Wapogoro na Wayao-Wamakonde wa kale.

Katika pande zote mbili za kaskazini mwa Ziwa Nyasa, kulikuwa na uhamiaji wa kiwango kikubwa, kama ule wa Walapwa, magharibi mwa Ziwa na Wasongea wa kale upande wa magharibi hadi sehemu ya juu ya Mto Ruvuma. Lakini pia kulikuwa na safari za humohumo katika maeneo ya Njombe, kwa mfano Wakinga walioingilia nchi ya Songea, na hata kwenye kame ya kumi na sita wakawa watawala wa Wangonde waliozungumza Kinyakyusa.

Kwa jumla, uhamaji wa Wabantu, hasa magharibi na kusini magharibi, unaelekea kuwa ulikatiza mifumo ya kijima iliyokuwepo na hivyo kusababisha hali ya kuundwa viunzi vipya vya uchifu ambamo wageni walishika nafasi muhimu.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili, eneo la tatu la makazi ya Wabantu linaweza kuonekana kandokando mwa Ziwa Viktoria kuanzia Mara, upande wa kusini na Ghuba ya Kavirondo kwa kaskazini na kusini mashariki mwa Mlima Elgon.

Ingawa kulikuwa na mahusiano na Wabantu hawa wa Ziwa, jamii zilizokuwa mashariki zilibaki kuwa tofauti, na tofauti hizo zilionyeshwa karne kadhaa za athari za kitamaduni baina ya Wabantu na wasio Wabantu. Hivyo, katika karne ya kumi na mbili, Wabantu wa mashariki ya Viktoria walitahiri wanawake na wanaume, mila mbili ambazo hazikujulikana kwa Wabantu wa Ziwa, lakini zilizotekelezwa na Wanilo na Wakushi wote walioishi jirani na Wabantu wa mashariki mwa Ziwa Viktoria. Zaidi ya hayo, mahusiano hayo ni alama muhimu ya maendeleo ya kihistoria kwenye maeneo haya. Kwa mfano, kwa watu waliozungumza Kimara, ongezeko la watu lililotokana na kuwaingiza Wanilo wa Kusini (kama vile ilivyokuwa kwa wahenga wa Wakurya) mwishowe lilisababisha kuwepo mfumo wa marika ambao ni wa Wanilo wa Kusini, uliobandikizwa kwenye mfumo uliokuwepo wa ukoo, na Kimara kikaendelea kuwa lugha ya mchanganyiko huu mpya.

Aidha, kwa kikundi cha Wagusii ambao walikuwa kundi dogo la Wamara, haikuwa tena Wanilo wa Kusini ambao waliwaathiri bali Wakushi wa Kusini. Jumuiya za Wagusii ziliwaingiza Wanilo wa Kusini kwa makundi madogomadogo, kiasi kwamba mfumo wa marika wa Wanilo wa Kusini haukuigwa, badala yake, hadi kufikia 1600, Wanilo wa Kipsigis walijinasibisha na Wagusii na walifuata mfumo wa Kibantu wa kuongoza jumuiya zao. Kulikuwa na mahusiano makubwa ya kiutamaduni. Hivyo kupungua kwa tohara na mifumo ya marika ya moja kwa moja kwa Waluyia inawezekana kunatokana na maingiliano ya muda kutoka kwenye maeneo ya wazungumzaji wa lugha za Maziwa ambao hawakuwa na mifumo hiyo. Hali kadhalika, wazungumzaji wa Kibantu walianza kutamakani kwa wingi huko Busoga na Buganda labda kuanzia karne ya kumi na nne, tukio ambalo masimulizi hugusia wakati wa kuzungumzia kipindi cha Kintu. Masimulizi hayo yanaclezea pia juu ya athari za lugha za Kibantu, pamoja na kuongezeka kwa ulimaji wa migomba wa Wabantu hao, ambao walikwisha anza kilimo hicho kuzunguka Mlima Elgon.

Lakini katika mseto huu wa watu wa kaskazini-mashariki mwa ziwa Viktoria, maingiliano na Wanilo yalikuwa mengi zaidi, na hivyo kusababisha ufugaji ng'ombe kupewa umuhimu mkubwa. Vilevile, mnao karne ya kumi na sita na baadaye, mahusiano baina ya Waluyia na Wakalenjin, ambao ni Wanilo wa Kusini, yalisababisha uundaji wa jumuiya zilizofuata mfumo wa ukoo katika shughuli zao,

lakini ukiwepo pia mfumo wa marika wenye asili ya Kikalenjin. Baadaye, wahamiaji wa Kiluo walioelekea kusini zaidi walileta mabadiliko makubwa kwenye maeneo haya.

Kanda za Bara ya Kenya na Tanzania

Ilipofika karne ya kumi na moja, baadhi ya jumuiya za Kibantu zilikwishatamakani katika maeneo makavu, kama vile Watakama wa kale, kama uchambuzi wa kuenea lugha za sasa za Kitakama, yaani Kinyamwezi, Kisukuma, Kikimbu, n.k. unavyoelekea kuelekeza. Watakama wa kale walikwishaanza kulima nafaka kuhakikisha kupatikana kwa chakula cha kuaminika. Kwenye maeneo mengine ya bara ya Kenya na Tanzania, Wanilo na Wakushi wa Kusini walipendelea zaidi kufuga na walilima nafaka kujikimu. Hata hivyo, kwenye maeneo machache yasiyokuwa na mvua za kuaminika, kama vile nyanda za Wamasai na sehemu kubwa ya kaskazini mashariki ya Kenya, inawezekana kuwa ufugaji ulichukua nafasi ya kilimo.

Tofauti kubwa kati ya makazi ya kikwi (milenia) cha kwanza na hali ya sasa ni kuenea kwa makazi ya Wakushi wa Kusini, kama vile watu wa Mashariki ya Bonde la Ufa, kutoka Kilimanjaro na Milima ya Upare hadi mkoa wa Dodoma wa Tanzania ya leo: walichunga ng'ombe, kondoo, mbuzi na walipanda uwele, mtama, na ilipowezekana, ulezi. Mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili, Wanilo kama vile Wadadog na Waongamo waliingia na kukatiza umoja uliokuwepo kwenye makazi, licha ya upinzani mkubwa kutoka kwenye jumuiya kama vile za Waasaki, Wakwadza na Wakushi wa Kusini mwa Iringa.

Ukame wa nchi uliendelea kwa karne kadhaa baada ya karne ya kumi na mbili. Matokeo yake ni kuwepo kilimo cha mchanganyiko, ambacho kilifanywa na jumuiya nyingi za Wabantu waliofika maeneo hayo, kama vile Wanjombe, Waruvu wa Magharibi na Watakama. Ingawa kuingia kwao kulichelewa, waliingia mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Wakwadza waliendelea kuwa muhimu katika historia ya Tanzania ya Kati. Lakini Watakama walienea zaidi magharibi mwa Tanzania kuanzia mwaka 1000. Kuenea huko kulikoendelea katika karne kadhaa kuliwagawa Watakama wa kale katika jumuiya tatu: jamii ya Wawembere, na majirani zao, Wanyamwezi wa kale na Wasukuma waliokuwa schemu ya juu ya Mto Wembere. Tofauti nyingi za kilahaja zinazoonekana Usukuma zinamaanisha kuwa eneo hili ndilo lililokuwa makazi ya awali ya kundi la Wanyamwezi na Wasukuma wa kale. Zaidi ya hayo, kuwepo kwa maneno mengi ya Kikushi cha Kusini kwenye msamiati wa Kinyamwezi na Kisukuma kunaashiria kuwepo kwa maingiliano baina ya wazungumzaji wa Kitakama na wazungumzaji wa Kikushi. Kuenea kwa Wanyamwezi na Wasukuma kuliongezeka kwa kiasi kikubwa; ilipofika kama

mwaka 1600 walikuwa wamefika kusini mwa Ziwa Viktoria.

Maeneo ya milima: Kilimanjaro na Kenya

Kaskazini mwa Umasai, kwenye miteremko ya Mlima Kilimanjaro, jumuiya kadhaa za Wakushi wa Kusini ya Bonde la Ufa la Mashariki walilima nafaka kwa kumwagilia na kutumia mbolea. Kilimo hiki shadidi cha milimani kilikuwa ni tukio muhimu la kihistoria. Wabantu walichukua njia za kilimo za Wakushi na kuongeza migomba iliyotoka Indonesia, na bidaa hii muhimu inaelekea ilitokana na jumuiya za Wabantu wa Kilimanjaro, Mlima Kenya na Milima ya Upare, kuanzia karne ya kumi na moja. Kuingizwa kwa mila za watu wa milimani kuliwezesha kuanzishwa kwa makazi ya Washambaa kwenye mfululizo wa milima ya Usambara mnamo mwaka 1500.

Mnamo karne ya kumi na mbili, vikundi vya milimani mashariki mwa Bonde la Ufa vilizuiwa kwenye maeneo ya milimani kutokana na kuingia kwa Waongamo kwenye mabonde ya Kaputic. Msamiati wa Waongamo unafanana sana na ule wa Kimaasai cha kale, ikiashiria kwamba watu hawa walifuga na kupanda uwele na ulezi.

Mnamo 1100, Wachaga wa kale huenda walitamakani kwenye miteremko ya kusini mashariki mwa Kilimanjaro. Uzalishaji mkubwa uliotokana na kilimo shadidi uliwezesha Wachaga kuenea haraka katika karne tano zilizofuata, wakiingiza jumuiya za Mashariki mwa Bonde la Ufa na zile za Waongamo. Kwa njia hii, Wachaga wa Rombo walisambaa katika makundi kadhaa mashariki mwa mlima, ambapo Wachaga wa Magharibi walikwenda kwenye miteremko yenye misitu ya Mlima Meru.

Historia ya Vilima vya Taita baina ya mwaka 1100 na 1600, ilitawaliwa zaidi na kuungana kwa watu wa Mashariki mwa Bonde la Ufa na Wabantu kupita hata ile ya Kilimanjaro. Watu wa Bonde la Ufa Mashariki walimezwa na Wabantu jinsi karne zilivyoendelea.

Mchakacho huu ulifanywa kuwa tata zaidi kwa Wasagala kutokana na kuingiliwa na Wabantu kutoka Milima ya Upare na vikundi vya Wazungumzaji wa Kisabaki kutoka pwani mnamo karne ya kumi na sita. Maneno mengi ya mkopo kutoka Kisabaki yamo katika Kisagala.

Uingiaji huu wa makundi ya Wasabaki katika vilima vya Taita ulikuwa muhimu katika kuleta mshikamano na kujitambua kwa Wakamba waliokaa kaskazini mwa vilima hivyo mnamo karne ya kumi na sita.

Hadi kufikia mwaka 1100, Wathagichu wa kale waliunda jumuiya ndogondogo za Kibantu kusini mwa Mlima Kenya. Kama ilivyokuwa kwa Wachaga wa kale, walisongana na Wakushi wa Kusini na Wanilo wa Kusini. Lakini Wamaasai walianza kuwaathiri baada ya 1600 tu. Kabla ya hapo, Wathagichu walieneza

makazi yao ya kilimo kwa kukata misitu, na kuzaa makundi makuu mawili: Wakikuyu (waliokuwa baina ya mfululizo wa milima ya Nyandarua na Mlima Kenya) na Wameru, mashariki mwa Mlima Kenya.


Wakati huohuo, wahamiaji wa Kisabaki walishirikiana na Wathagichu wa Ukambani, wakiunda kundi ambalo ligha yake ilikuwa Kithagichu lakini utamaduni ukafanana na ule wa Wataita au Wabantu wa pwani. Hivyo, Wakamba wakawa na upinde na mshale badala ya mkuki kama silaha yao ya kawaida na wakaacha mfumo wa marika.

Magharibi mwa nchi baina ya Mlima Kenya na Kilimanjaro kulikuwa na eneo kubwa ambamo Ubantu haukushika katika kipindi cha miaka 1100 - 1600. Waliotamalaki hadi baada ya 1500, walikuwa Wanilo wa Kusini, hasa Wakalenjin na Wadadog, walioenea kwenye mbuga za Jasingishu na mashariki na kusini-mashariki hadi kati na kusini mwa Bonde la Ufa. Kuenea huku kwa Wakalenjin kulikengeua utaratibu wa kawaida wa Wakalenjin wa kuwashirikisha Wabantu. Wakalenjin wa Elgon, walioishi kusini mashariki mwa Mlima Elgon, walikengeuka kwa kuwaingiza Wabantu. Kwa mfano, mfumo wa koo za maeneo ulitawala ule wa marika ya vipindi na walianza kilimo kilichotegemea migomba.


Mashariki mwa Mlima, ilipofika mwaka 1500, wakati wahenga wa Wapokot walitawaliwa na Waitunga, Wanandi wa kale waliwaingiza Wukushi na waliingiza mtindo hahi wa Kikushi wa kilimo cha umwagiliaji kwa vizalia vyao vya Kikalenjin, kilimo ambacho kinaonekana kwa wazungumzaji wa Kinandi, kama vile Wakcyo. Halafu, mnamo 1500, kuenea kwa Wanandi kulielekea kusini katika misitu na mbuga za Mto Nyando; kutokana na wahamiaji hao wa Kinandi ndipo kulitokea jumuiya za Wanandi na Wakipsigis.

Lakini ueneaji uliokuwa mashuhuri sana ni ule wa Wakalenjin wa Kusini. Ilipofika 1500, walikuwa wamekwenda Kusini kufikia nchi ya Ruvu Magharibi. Wakalenjin hawa wa Kusini waliwaondosha Wadadog waliokuwa Umaasai ya kati na kaskazini; na waliwafukuza au kuwameza Wakivadza wa Umaasai ya kusini. Walisimamishwa na genge la Bonde la Ufa kaskazini mwa Tanzania, kwani Wadadog waliendelea kudhibiti miinuko ya Loita na Ngorongoro, pamoja na mbuga za Serengeti na Mara zilizokuwa magharibi. Kutamalaki huko kwa Wadadog kulimalizwa na wavamizi wa Wamasai mnamo karne ya kumi na saba.

Kwenye miinuko ya Kondoa na Mbulu, Wakushi wa Kusini wahoishi magharibi mwa Bonde la Ufa na Wabantu wa Irangi ya kale hawakuathiriwa na kuenea kwa Wakalenjin wa Kusini. Makundi mawili ya watu yalitamakani kwenye genge la Bonde la Ufa: Wasonjo waliozungumza Kibantu na Wairaqw ambao waliiga makazi ya Wabantu hao kwa kuwa na makazi madogomadogo ambapo umwagiliaji uliwezekana; wao ndio waliowatangulia Wasonjo wa sasa kuishi juu ya Ziwa



19.1 Makisio ya makazi ya watu wa bara ya Afrika Mashariki kwenye karne ya kumi na mbili (C. Ehret)



A	Ongamo	F	Sandawe	Wabantu	△ Vilele vya milima
B	Dawida	G	Irangi	Wakushiti wa Kusini	//// Bonde la Ufa
C	Sagala	H	Burungi (West Rift)	Wamiloti	
D	Dahalo	J	Alagwa (West Rift)	Wakushiti wa Mashariki	
E	Hatsa	K	Asax		
		L	Sonjo		

19.2 Makisio ya Makazi ya watu wa bara ya Afrika Mashariki
-kwenye karne ya kumi na sita (C. Ehret)

Natron, labda kwenye eneo maarufu la kiakiolojia la Engaruka.

Upande mwingine wa mbali wa Wakalenjin, Baringo, Wamaasai wa kale walijigawa kwenye makundi matatu: Wasamburu, Watiamu na Wamaasai; kati ya makundi hayo matatu, Wamaasai, wakiwa ndio wa kusini zaidi, walianza kuingia kwenye nchi ya Wakalenjin iliyoambaa Bonde la Ufa mapema kwenye karne ya kumi na sita na walienea hadi kaskazini mwa Tanzania, wakitishia utawala wa Wadadog na Wakalenjin wa kusini.

Hajira ya watu na mabadilishano ya kiutamaduni

Baina ya miaka ya 1100 na 1600, bara ya Kenya na Tanzania ilikuwa ni mahali pa hajira za watu zilizoambatana na migongano na mahusiano ya kiutamaduni na kibioolojia ambayo yaliunda makundi inapya ya kijamii na kisiasa. Jambo muhimu katika sakata yote likiwa ni mabadiliko katika mbinu za kilimo. Kwa hivyo, Wabantu ambao walizoea mazao ya mizizi walikubali kubadili na kulima uwele na mtama uliopendwa na Wakushi na Wanilo ambao waliweza kukaa nao na baadaye kuwameza. Kwenye maeneo mengine, hata hivyo, ilikuwa ni kilimo cha milimani kilichowashawishi Wabantu kusambaa.

Mojawapo ya matokeo yake yalikuwa ni kuanzishwa kwa maeneo mapya ambayo hapo awali yalikalwa na jumuiya za wawindaji na wahemeaji. Yaelekea hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Wachaga wa Kilimanjaro waliokata misitu iliyoambaa mlima juu ya maeneo ya wenyeji ambao waliwameza polepole. Ilikuwa ni kwenye eneo hili la Mlima Kenya na Kilimanjaro ambako kilimo shadidi kiliwezesha kuwepo kwa ziada ya kutosha iliyosababisha kuundwa kwa masoko rasmi. Kilimo hiki kilikwenda sambamba na ufugaji wa ng'ombe ambao ulizalisha ngozi za ziada zilizotumiwa kutengenezea nguo za ngozi zilizopendwa na wakulima wa milimani. Wakulima wa milimani nao walikuwa na mbaao, mali ghafi ya kutengenezea vyombo, mizinga na hori za maji. Walipanda pia vibuyu ambavyo vilitumiwa kama vyombo, pamoja na mazao ya ziada ambayo walibadilishana wakati wa uhaba wa chakula uliowapata wafugaji wahoishi kwenye maeneo makame zaidi. Mwisho, wawindaji-wahemeaji waliweza kushiriki kwenye biashara hii ya pande tatu kwa kuchuuza asali na ngozi. Upatikanaji usio sawa wa migodi ya metali ulifanya mahusiano yawe tata zaidi. Hivyo Wagweno wa Upare kaskazini waliunganika kwenye mfumo wa biashara ya milimani na mabondeni kwa mchango wao kama watengenezaji na wasambazaji wa chuma na vifaa vya chuma, nafasi waliyokuwa nayo Wathagichu kuzunguka Mlima Kenya.

Masoko ya namna hiyo yalianza kuibuka kwingineko baada ya 1600.

20

Eneo la Maziwa Makubwa

Mwanahistoria anayeshughulikia eneo la maziwa anakabiliwa na matatizo makuu manne. Kwanza, kuna data chache za masimulizi, lugha na akiolojia. Kwa mfano, inapokeo huwaonyesha wahenga wa koo kuwa ndio walioleta mazao ya chakula na ng'ombe. Ndiyo maana baadhi ya wanahistoria wanawaainisha kuwa ni viumbe vya kubuni, vilivyochukuliwa na visasili kama vile vya Wachwezi, kuwa ni mizimu myema.

Pili, mada kuu kuhusu mahusiano baina ya wafugaji na wukulima ina matatizo. Waandishi wengi wanawaonyesha wafugaji kama washindi walioleta ustaarabu na wakulima kama umma ulio mpole na usiotenda. Mwelekeo huu unaonyeshwa na A. Kagame anapocleza juu ya Rwanda, ambaye anaonyesha wasiwasi juu ya mchango wa Wahutu katika kuleta ustaarabu, kitu ambacho anaona kuwa ilikuwa ni kazi ya Watutsi peke yao. Kwa upande mwingine, tunaona kwamba dola ziliundwa baina ya wakulima kabla ya kuja kwa wafugaji ambao walihusiana na wenyeji na kushadidia miundo ya dola kwa misingi ya matabaka na nasaba. Kwa hiyo, maneno "wafugaji" na "wakulima" yanaonyesha kazi kuliko kabila; yanaonyesha jinsi watu walivyoishi. Wafugaji walipokuwa hawana ng'ombe wakawa wakulima, na kinyume chake.

Tatizo jingine kubwa ni kronolojia ya Wabantu na Wanilo. Jitihada za kuiunda zimefanywa kwa kutumia misingi ya marika, marejeo yanayofungamana nayo, na kupatwa kwa mwezi na jua kunakoelezwa kwenye mapokeo. Lakini bado kuna shaka kubwa juu ya ukweli wake. Kwa mfano, kizazi cha Wabito wa Bunyoro kimetiliwa shaka na Henige. A. Kagame anaeleza kuwa mwanzo wa dola la Rwanda ulikuwa karne ya kuni, ambapo Jan Vansina anasema kuwa ni kipindi cha mwisho cha karne ya kumi na tano. Hata kama utatuzi ungepatikana juu ya kronolojia ya kila dola, vipimo hivi tofauti vya muda vinghitaji kuunganishwa kwa ajili ya

vikundi kadhaa na kwa karne nyingi.

Tatizo la mwisho linatokana na ukweli kwamba, mpaka hivi karibuni, nyaraka za kihistoria zilizochapishwa zilitoa habari za watawala, zikizingatia dola kuu na kutozingatia sana sehemu kubwa ya jamii.

Tutaangalia kwa mfululizo makundi manne ya makabila mbalimbali tukitilia maanani matatizo yaliyotajwa hapo juu: utanzo za Kitara, Kintu, Ruhinda na Rwanda.

Utanzo wa Kitara

Utanzo wa Kitara unajumuisha Bunyoro, Toro na sehemu za jirani za Nkore na Buganda; hili ndilo dola la zamani zaidi kwenye maeneo ya maziwa, na historia yake inaashiriwa na maingilio ya makundi matatu: Watembuzi, Wachwezi na Wabito. Lakini awamu hizo tatu zinazohusiana na wageni zinawaacha Wabantu, wengi wao wakiwa ndio wenyeji, ambao lugha zao ndizo zilizotawala eneo hili. Je, wao walikuwa watazamaji tu? Kulingana na Buchanan, hajira za mwanzo kabisa zilitokea baina ya 722 na 1200. Waliofika mwanzo, hata kabla ya Wabantu, kutokana na ushahidi wa lugha, ni watu kutoka Sudan ya kati. Kutokana na ushahidi wa kiakiolojia, hiyo ilitokea kabla ya karne ya nne. Koo za kwanza za wazungumzaji wa Kibantu zinaelekea zilitoka magharibi ya Ziwa Mobutu (Albert) na kuingia kwenye maeneo ya kusini mwa mto Nili. Walilima mtama na ulenzi. Walifika kwenye maeneo haya mnamo karne ya kumi na kumi na moja. Baadhi ya koo hizo ziliunda madola madogo ya wakulima, ambayo hayakupata mchango wowote kutoka kwa wahamiaji wafugaji, bali ilikuwa kazi ya makundi ya awali ya wazungumzaji wa Kibantu. Mwanzoni, waandishi walikiita kipindi cha Watembuzi kuwa "utawala wa miungu," kipindi kilichokuwa cha visasili kuliko kuwa cha kihistoria, ambacho kilikuwa na wafalme watangulizi (*Abakama Abatembuzi*) kumi na tisa kufuatana na mapokeo ya Kinyoro au wanne kufuatana na mapokeo ya Kinyankore. C. Buchanan ameiunda upya historia hii kwa kufuatilia maendeleo ya koo hizo. Hivyo, uchifu wa Bugangaizi ulianzishwa na ukoo wa Wagabu, na kiongozi wao alikuwa Hangi. Wayaga, ukoo mwingine uliokuweco kabla ya Wachwezi, wanahusishwa na kuja kwa ng'ombe (labda wasio na pembe ndefu) na machimbo ya chumvi huko Kibiro. Ukoo wa tatu, Wasita (unaotambuliwa kutokana na mwanzilishi wake, Sitta), unajitokeza sana kwenye ngano za madola ya Nkore, Kiziba na Buhaya kama kundi lililopata nguvu zake kutokana na uhunzi. Majina ya mahali kama *Mbale au Kabale* yaliyo kwenye eneo hili yanahusishwa na kuwepo kwa Wasita.

Hadi mwaka 1250, kulikwisha kuwa na tawala kadhaa za machifu wa Kibantu mashariki mwa Milima ya Ruwenzori, zilizotokana na Watembuzi na zilizoundwa

sambamba; kwa mfano, mfalme wa kwanza wa Kiziba alitawala 1236-63.

Ukoo wa Bukuku ulipata jina lake kutokana na mwanzilishi wake, ambaye inasemekana alikuwa "kabwela" na alikuwa ameajiriwa na Baraza la Isaza (k. 1301-28), "mfalme wa mwisho wa watangulizi", ambaye alitawala kabla ya kumpokea na kumlea Ndahura (k. 1344-71), mtawala mkuu wa kipindi cha Wachwezi. Kizimu cha ukoo wa Bukuku kilikuwa panzi na fungo, ambacho ni muhimu katika historia ya Busoga. Bukuku, ambaye inasemekana kuwa alikuwa mfinyanzi, anatuonyesha kwamba kukua kwa dola unganifu hakukutokana na wafugaji wageni pekee. Hata hivyo, ilibidi Bukuku avunje upinzani wa machifu waliopinga kutawaliwa na kabwela. Kuenea kwa upinzani huu kulimwezesha Ndahura, mwanzilishi wa ustaarabu wa Wachwezi, kushika madaraka.

Kufuatana na mapokeo ya Bunyoro na Nkore (Ankole), ufalme mkuu huu mpya ulikuwa na wafalme wawili (Ndahura na Wamara) na Mfalme-Kaimu aliyelitwa Murindwa. Wanahistoria wengi wanakubali kuwepo kwa nasaba tawala ya Wachwezi kihistoria: mmoja wao anawahusisha wa Wasidana wa Ethiopia; wengine wanahusisha ufalme wao na ule wa Waganda, wa Wachwa na wa Wahima. Ni takriban Wringley pekee anayedai kuwa Wachwezi ni "mkusanyiko wa miungu iliyopewa majina na nafsi, iliyobuniwa kama watu wa aila moja waliopewa utukufu."

Hata hivyo, kwa maoni yetu, hili lilikuwa tukio halisi katikahistoria ya Afrika Mashariki lilitokea kwenye utanzo wa Kitara kuanzia 1350 hadi 1500. Kuna nadharia kuu mbili za maendeleo haya. Baadhi, kama Oliver, wanadai kuwa Wachwezi walikuwa wafugaji wa Kihima waliokuja kutoka kaskazini mashariki au kusini. Nadharia hii ya kuwa wametoka kusini inatetewa na Ehret, anayependekeza kwamba Watutsi na Wahima wa sasa wanatokana na Wakushi wa Kusini, ambao anaona kuwa walitoka mashariki, na wakaingia kwenye eneo la maziwa kutoka kusini mnamo karne ya kumi na tatu au mwanzoni mwa karne ya kumi na nne, ambapo walishirikiana na marafiki zao waliokuwa miongoni mwa wenyeji kuunda tabaka la kifalme na dola kuwatawala wakulima.

Nadharia nyingine, ambayo inapata mashiko haraka, ni ile ya kuwa Wachwezi walikuwa watawala wenyeji walioibuka kutokana na mabadiliko ya uchumi na demografia. Kilicho dhahiri ni kwamba himaya ya Kitara iliundwa na Ndahura (1344-71), ambaye alieneza uchifu mdogo wa Bugangaizi kwenye eneo kubwa ambalo lilijumuisha Bunyoro, Toro, Buganda magharibi, Ankole (Nkore), Kiziba, Karagwe, Visiwa vya Sese, sehemu ya Rwanda, n.k.

Kwa vile hakuwa na jeshi wala maafisa wa watawala, alitegemea mawakala aliowateua kwenye maeneno mbalimbali ambao waliongoza uchumi wa himaya uliotegemea chumvi, ng'ombe na chuma. Alikamatwa wakati wa vita ambapo

kupatwa kwa jua kulitia majeshi yake hofu kubwa. Aliachiwa lakini akaamua kuhamia magharibi mbali na mji wake mkuu uliokuwa Mwenge. Mwanawe Wamara (1371-98), alikuwa na utawala uliokuwa na fujo zaidi. Alihamishia mji wake mkuu Bwera lakini ilibidi ashughulikie vikundi kadhaa vya wahamiaji, zikiwemo koo za wazungumzaji wa Kibantu waliohusishwa na utanzo wa Kintu, Wajooma, Washambo kutoka kusini, na Waluo kutoka kaskazini. Inawezekana Wajooma walikuwa ni watawala waliozungunza Kibantu waliotoka Uganda magharibi katika karne ya 14 na 15. Mfalme Wamara alijaribu kuwaingiza wahamiaji hao kwenye makundi yake kwa kuwapa vyeo vya juu vya siasa. Kwa mfano, Ruhinda, ambaye ni Mhima, aliwekwa kuangalia mifugo ya mfalme. Wamara alichanjiana damu na Kintu, kiongozi wa koo za Wabantu zilizotoka mashariki. Lakini vitendo hivyo vilifasiriwa na wale walionufaika navyo kuwa ni kuwapoza tu. Njaa kubwa iliyofuatiwa na ugonjwa wa ng'ombe, vilitosha kuleta manung'uniko yaliyoenea kote. Kagoro, amiri jeshi, alitumia fursa hiyo kufanya mapinduzi na mauaji ya watawala wa Kichwezi. Miungano miwili ya madola ilitokea kutokana na kuanguka kwa madaraka ya Wachwezi: madola ya Waluo-Wabito ya Bunyoro-Kitara, na kusini zaidi, madola ya Wahinda. Kwa hiyo kulikuwa na mapambano baina ya Waluo na Wahima.

Ili kuelewa mabadiliko kwenye dola za Waluo, ni muhimu kusisitiza kwamba maendeleo ya kihistoria ya Uganda magharibi hayawezi kuchukuliwa tu kama athari za mfuatano wa vipindi vya ushindi wa wafugaji kama waleta ustaarabu. Waluo kutoka Sudan kusini walifika wakati wa Wamara. Hawa ni Waluo wa kusini na kati ambao walitengana na wale wa koo za kaskazini mnamo miaka ya 670 hadi 1070, na ambao walijigawa makundi mawili baina ya 1170 na 1470. Ilipofika mwishoni mwa karne ya kumi na nne, jumuiya nne za Waluo ziliibuka, mojawapo ikaishi karibu na Mlima Agoro. Huko walifuatwa na Wajooma (Wahima). Waluo hawa, ambao hadi sasa walikuwa wawindaji na wakulima, walijifunza kufuga ng'ombe kutoka kwa Waliima. Walivuka mto Nili na kuingia kwenye himaya ya Wachwezi wakati wa Mfalme Wamara, kufuatia kulipuka kwa ugonjwa wa ng'ombe, wakiacha nyuma makundi machache yaliyoongozwa na Owinyi I (1409-36), aliyeanzisha ufalme wa Tekidi, inoja ya dola za mwanzo za Waluo. Owinyi alimwoa msichana wa Kihima, aliyezaa naye mtoto wa kiume, Rukidi ambaye alimkimbia baba yake. Alikaribishwa na Waluo waliohamia kwa Wachwezi na kuanzisha ufalme mpya wa Wabito wa Kitara. Mfano wa Rukidi unaonyesha kuwa kulikuwa na kuchanganyika sana baina ya Waluo na Wahima, kiasi kwamba baadhi ya waandishi huzungumzia Wahima waliozungunza Kiluo.

Mwingiliano wa makabila wa aina hiyohiyo ulikuwa ukiendelea kaskazini zaidi huko Uchwezi baina ya Waluo na Wamadi. Wanyimur na Wapatiko, ambao baadhi

yao baadaye waliongozana na Rukidi kwenda Kitara ambako Waluo-Wakwonga nao walikwenda, walitokana na mchanganyiko huu. Kwa hiyo halikuwa jeshi kubwa la Waluo lililoingia Kitara, bali makundi madogomadogo yaliyoingia kwa vipindi, wengine wakielekea Sudani, Zaire (Kongo) ya leo au Ethiopia.


Kutokana na mapokeo ya Bunyoro, Kiziba, Nkore na Karagwe, ni dhahiri kwamba, ingawa Wabito na Wahima ambao walimwangusha Wamara walivumisha uzushi juu ya kupotea kwa Wachwezi, huku wakisisitiza kuwa wana uhusiano nao, walishindwa kuwashawisli raia wao hao wapya. Ni mchanganyiko wa nguvu na ujanja ndivyo vilivyowaletea ushindi. Kwa mfano, huko Kiziba, ilichukua umri wa kizazi kizima kabla Kibi (tk. 1417-44), mwindaji wa Kiluo, hajaweza kuunda utawala wake kwa kugawa nyama pori na kutumia mbinu za kisiasa. Mapambano yalikuwa ya muda mrefu zaidi huko Bunyoro-Kitara. Kagoro, mwanzilishi wa mapinduzi ya serikali, hakuweza kuendeleza umoja wa dola ya Wachwezi ambayo alikuwa ameharibu. Hata hivyo, alihakikisha kuwa nembo za kifalme kama vile ngoma zilibakishwa. Rukidi, ambaye aliingia kwenye eneo hili lililokuwa na watu wa kila aina na lililokwishavurugwa, alipata tabu kupata mji mkuu, na mvishowe alikaa Bugangaizi, kituo kikuu cha dola ya zamani ya Watembuzi. Hali hiyo haikutulia hadi baada ya 1500, Bunyoro ilipoanza kupanuka kuelekea dola za Wahinda na Rwanda.

Utanzo wa Ruhinda

Kitovu cha kijiografia cha utanzo huu kilienea sehemu za Ankole (Uganda), Tanzania, Rwanda na Burundi. Dola kuu zilizohusika ni Nkore, Karagwe na Buzinza. Utanzo huu ulikuwa na mslukamano mkubwa ulioonyeshwa na wafugaji wa Kihima na Kitutsi, pamoja na koo kongwe za Wasiita, Wazigaba, Wakimbiri, Washambo, na wengine. Kila ukoo uliwakilisha uchifu uliokuwa na watu mchanganyiko: Wahima wakijumuishwa kwenye koo za "Kibantu", na Wabantu kwenye koo za Watwa na kinyume chake. Ushahidi wa ziada unaonyesha kuwa lahaja walizotumia wote (Kikiga, Kinyakore, Kinyarwanda) zilihusiana sana.

Mapokeo yanaonyesha kuwa Watwa walikuwa wawindaji na wahemeaji; walizurura kwenye ukanda wa misitu ambao ulikuwa umecnea zaidi kuliko ilivyo sasa. Misitu hiyo ilifyekwa na wakulima wa Kibantu walioingia kutoka kusini na magharibi. Zaidi ya kulima mtama na uwele, walikuwa wawindaji na wahunzi. Hivyo ndivyo walivyokuwa watu wa ukoo wa Barongo na Basinga, kwa mfano.

Mwanzoni, wazungumzaji wa Kibantu walijiunda kwa misingi ya familia pana, wakiwa na wazee wa baraza wa kutatua matatizo ya kawaida. Lakini kutokana na kuingia wahamiaji kwa wingi, walijiunda kwenye koo. Koo hizo hazikutokana tu na vizazi vya mhenga mmoja: mila ya undugu wa kuchanjia damu ilivawezesha wageni



20.1 Uhamaji wa mwanzo wa Waluo (B.A. Ogot)

kuungana na koo kongwe. Na ilikuwa jambo la kawaida mtu kubadili ukoo. Kwa njia hiyo, koo zilikuwa ni vitengo vya maeneo ya ardhi vilivyochukua jina la familia iliyokuwa mashuhuri (k.m. Wasigi walikuwa mashuhuri Usigi). Koo kubwa zilikuwa na mfalme au chifu (*mwami*), ambaye alikuwa mkuu wa kidini na kisiasa, alikuwa pia mganga wa mvua na alikuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wa mifugo na upatikanaji wa mazao. Hivyo ndivyo walivyoishi Wagahe huko Ndorwa na Wasigi huko Usigi.

Inaelekea kuwa ilipofikia mwanzoni mwa kame ya kumi na tano, baadhi ya koo hizo za Kibantu zilikwishaunda nasaba za kifalme, kama vile Wasita, waliotawala Nkore na Karagwe. Ukoo wa Barengeye, waliotengeneza majembe makubwa, ulitoa familia zilizotawala makundi kadhaa yaliyoenea Rwanda ya leo na kusini magharibi mwa Uganda.


Wazigaba nao walikuwa ni ukoo mashuhuri sana wa wakulima. Kwa kweli waliunda utanzo wa kibubusa uliokuwa na koo kadhaa zilizoenea Rwanda, Ankole na Kigezi zilizokuwa na vizimu mbalimbali (chui, swala n.k.), chini ya dola ya Mubari na mfalme wake (*Kabeija*), na ngoma ya kifalme (*sera*). Watu wake walisambaa na kupoteza haki zao za kisiasa lakini walibaki na jina lao kama ainisho la kijamii, na koo zao zilizotambulishwa kwa vizimu.

Ukoo mwingine uliotamkani katika nchi kadhaa, Waishekatwa wako Rwanda, Kigezi (ambako ndio wakazi wa zamani zaidi wa Bujumbura), Toro na Ankole.

Koo hizi kuu za wazungumzaji wa Kibantu ndizo zilizotamalaki maeneo haya ilipofikia mwishoni mwa kame ya kumi na tano.

Kuhusu wafugaji, ni lazima ielezwa hapa kwamba hakuna uthibitisho wa kuwa walitoka kaskazini; tusikatae kuwa asili yao inawezekana kuwa ni ya hapahapa na labda karibu na Karagwe. Isitoshe, dhana kuwa wafugaji walikuwa washindi ambao kila wakati waliwatawala wenyeji ambao walikuwa wakulima inahitaji irekebishwe. Kuishi pamoja kwa amani kulikuwa na mafanikio na, hadi kame ya kumi na tano, dola kadhaa za wafugaji zilipoibuka kwenye maeneo mbalimbali, koo za wakulima ndizo zilizounda nasaba za watawala.

Kundi kama la Wariisa, kwa mfano, linachukuliwa kuwa miongoni mwa koo za zamani zaidi za wafugaji. Kufuatana na mapokeo yao, walihama kutoka kaskazini (Bunyoro) hadi Karagwe. Baadaye waliamia tena kaskazini kupitia Kigezi na Ankole kisha wakasambaa. Mwanamume mmoja aliyelitwa Kateizi alibaki njiani na kutamakani Buhweju, ambapo alioa wanawake wa hapo, akawa mkulima na kuanzisha ukoo mdogo wa Wateizi. Dada yake, Iremera, aliolewa na Mfalme Wamara na Wachwezi walimpa kaka yake mmoja nchi atawale na mwingine alipewa cheo cha kiutawala na kundi la ng'ombe. Kutokana na mapokeo haya, ni



dhahiri kwamba wafugaji hawakutwaa madaraka mara moja na kuwa, kama majaaaliwa ya Baitezi yanavyoonyesha, wengine hawakufanikiwa kabisa. Kati ya wahamiaji wafugaji waliokuja baadaye zilikuwepo na koo tatu zilizoongoza kwa umashuhuri huko Nkore, Karagwe na Kiziba. Koo hizo zilikuwa Washambo, Wasiita na Wahinda. Kuna mabishano makubwa kuhusu asili ya kundi la mwisho. Mapokeo ya Nkore yanadai kwamba walitokana na Wachwezi. Wengine wanadai kuwa ni Wanilo wanaotokana na Waluo. Karugire hakubaliani na nadharia hii. Denoon anamwona Ruhinda ni Mugyesera aliyetoka Gisaka, ambaye alishika madaraka ya eneo na kuunda Rugyesera, ambayo inatambuliwa kuwa Nkore na baadhi ya vikundi vya sehemu hii. Zaidi ya hayo, Wagyesera na Wahinda wanachangia kizimu kilekile cha nyani. Lakini hoja hizi hazionyeshi uhusiano wa kihistoria baina ya Ruhinda na Wagyesera.

Mapokeo ya Bunyoro yanaonekana kuwa thabiti zaidi. Ruhinda alikuwa mfugaji tajiri aliyekuwepo wakati wa Wamara na aliteuliwa kuwa mchungaji mkuu wa baraza la Wachwezi. Kagoro alipofanya mapinduzi ya utawala, Ruhinda aliwakimbiza baadhi ya ng'ombe wa kifalme kwenda Karagwe na kuingiza ng'ombe wenye pembe ndefu huko. Nono, ambaye alikuwa Msiita, alikuwa akitawala wakati huo. Ruhinda alitumia utajiri wake mwingi kumwondoa kwenye madaraka. Baadaye alikwenda kaskazini na kuingia Nkore ambako alitwaa madaraka kwa kufanya urafiki na ukoo wa Wanyangwe. Kama ilivyokuwa kwa Rukidi, Ruhinda alijaribu kuwashawishi raia wake kuwa alikuwa anatokana na Wachwezi. Aliwaweka watoto wake wa kiume kutawala maeneo mbalimbali (Nkore, Uzinza n.k.), alitumia hata sumu ilipobidi, na alipiga maeneo yote ya karibu na kisha aliwaweka watoto wake badala ya wawakilishi wa Wachwezi. Hesabu za miaka zinazotokana na mapokeo dola nne (Uzinza, Kyamutwara, Karagwe na Nkore) ambazo watawala wake wakuu wanadai kutokana naye, zinaonyesha kuwa alitawala mnamo tk. 1405-47. Hadi alipofariki, alikwishaunda dola ya Wahinda upande wa kusini iliyofanana na ile ya Wabito upande wa kaskazini au dola ya Rwanda. Lakini dola hii haikudumu baada ya kifo chake, na dola huru za Waliinda ziliingia katika mkumbo mmoja na dola nyingine kama vile za Rwanda, Ndorwa, Buganda n.k. ambazo zilibaka kutokana na mabaki ya utanzo wa Wachwezi na ambazo karibu zote (isipokuwa labda ile ya Buganda) zilikuwa za wafugaji hasa.

Utanzo wa Rwanda

Nadharia inayotolewa na A. Kagame na *Mapadre Weupe* kuhusu historia ya Rwanda ina makosa makubwa. Inaweza kufupishwa ifuatavyo. Kuanzia kame ya kumi, kundi la wafugaji lililoshikamana la "Wahamiti wa Kitutsi" waliotoka kaskazini liliwaletea Wabantu wakulima (Wahutu) ufugaji, uhunzi, dhana ya ufalme, jamii iliyogawanyika kiamali, na dola ya Rwanda, ambayo ilikua kuwa

Rwanda ya leo. Wahutu, waliotwezwa kuwa watwana, walipewa ng'ombe kama malipo ya huduma walizotoa na uaminifu wao kwa watawala. Historia hiyo imezingatia sana falme kuu na mabaraza kuanzia wakati wa Gihanga, mhenga wao, na kuacha umma wa watu nje ya historia hiyo. J. Vansina na J.K. Rennie wameandika historia ya Rwanda iliyo na urari zaidi na isyopendelea upande wowote.

Inabidi turudi nyuma zaidi, kabla ya wakati wa dola na jamii za Nyiginya. Wakazi wa awali walikuwa Watwa ambao walikuwa wawindaji, wafinyanzi na watengenezaji wa vikapu. Walipokea intama, asali, ng'ombe, vifaa vya chuma, na chumvi, toka kwa wazungumzaji wa Kibantu wakulima waliofika baada yao, na kubadilishana na ngozi za wanyama, nyama, vikapu, n.k. Ilipofika karne ya kumi na tano, wazungumzaji wengi wa Kibantu walikwisha jiunda kwenye madola madogomadogo yaliyomilikiwa na koo za kitawala za chifu au mfalme (*mwami*) ambaye alikuwa chifu wa nchi na kiongozi wa dini. Baadhi, kama vile koo za Singa na Zigaba, walikuwa na ng'ombe hata kabla ya kufika kwa ukoo wa Wanyiginya. Madola ya Singa, Zigaba, Gesera, Banda n.k. ndiyo yaliyomiliki kwa asili ardhi ya Rwanda. Kufuatana na ngano za Kitutsi, dola la zamani zaidi liliundwa na aila ya Renge wa ukoo wa Singa. Ilipofika karne ya kumi na sita, walikuwa na ufalme changamano wa kimila uliohudumiwa na wataalamu wa miviga waliojulikana kama Watege. Gihanga, mwanzilishi wa koo za Watutsi, anaaminiwa kuwa alichukua wazo la ngoma ya kifalme na kanuni za miviga ya kifalme kutoka kwa mhenga wao Nyabutege. Ilipofika katikati ya karne ya kumi na saba, madola yote za Renge yalimezwa na dola la Rwanda.

Mashariki mwa Rwanda kulikuwa na dola la Mubari la ukoo wa Wazigaba. Ukoo wa Wanyiginya unatajwa kwa mara ya kwanza kwenye mapokeo kuwa ulipewa kilima cha Gasabo na ukoo wa Zigaba. Makundi hayo mawili yalioleana bila vikwazo wakati wa kipindi hiki. Hata baada ya kunyanganywa ngoma na mtawala wa Rwanda mwishoni mwa karne ya kumi na sita, nasaba hii ya kifalme iliendelea kuwepo hadi kipindi cha mwisho cha karne ya kumi na nane.

Waliokuwa wanahusiana kwa karibu sana na Wazigaba walikuwa Wagesera, ambao walitawala dola yenye nguvu ya Gisaka hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Busigi hakuingizwa Rwanda hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini. Hivyo kulikuwa na muda mrefu ambapo inifumo miwili ya dola, ule wa wenyeji na ule wa wageni, iliendelea kuwepo kwa pamoja, na miviga ya kifalme ya Rwanda ilifanikiwa kisiasa kwa sababu ilijumuisha miviga ya wakulima na wafugaji na wakulima kadhaa walipewa vyeo vya kimila, hivyo kuwafanya watake mfumo huo uendelee.

Ingawa labda mwanzoni wafugaji walikuwa "wateja" wa wukulima, walibadilika baada ya karne ya kumi na tano, kutokana na ndugu zao kuingia kwa wingi, na kuwa koo kubwa na mnamo karne ya kumi na sita wakawa mabwana. Maisha ya

mwanzo ya amani yakageuka kuwa mapigano. Mnamo karne ya kumi na tano, koo mbili za wafugaji zilifanikiwa kuanzisha dola huru. Wakondogo, waliotamakani kusini kuzunguka Ziwa Mugesera, na Wanyiginya waliokaa Gasabo katikati ya Rwanda. Asasi za dola hizi kuu zilijumuisha wafugaji na wakulima.

Eneo la Buganda, Busoga na Milima ya Elgon

Kati ya karne ya kumi na mbili na ya kumi na sita, koo kadhaa za wazungumzaji wa Kibantu (hasa koo za Kintu) zilihama kutoka eneo la Mlima Elgon na kutamakani mwambao wa kaskazini wa Ziwa Viktoria. Uhamaji huu haukuchochewa na wahamiaji wa Kiluo walioelekea kusini mashariki; ulifanyika angalau karne moja mapema zaidi, na ulikuwa msingi wa dola kadhaa ndogondogo, ikiwemo Buganda. Huenda Kintu alikuwa mtu wa kubuni, lakini mapokeo yanamwelezca kama kiongozi wa koo ambazo vizimu vyake ni chui na simba. Walisimama mahali mbalimbali walipokuwa njiani. Kulikuwa na koo nyingine za Kibantu kabla ya hapo zilizokuwa na vizimu mbalimbali, kama vile vichozi na paa. Ukoo huu wa mwisho uliotawaliwa na aila ya Abaiseigulu, ambao walitegemea ufinyanzi wa mitungi uliofanywa kwenye ziara muhimu, ulianzisha uchifu wa Bugulu, Busoga. Walikuwa ni wa koo enyeji za *banansagwa* au "wale waliokutwa mahali hapo". Ukoo wa kambare ulikuwa ni mmoja wa koo hizi; walikuwa wavuvi na wahunzi mashuhuri. Baadhi yao, ambao waliongozwa na Walumbe, walikutana na kundi la Kintu kusini mwa Busoga na wakaunga urafiki naye kwa kumwoza binti ya Walumbe. Kintu alielekea magharibi hadi Buswikira ambako aliungana na kundi la wakweze lililoongozwa na Walumbe. Ugomvi wa ugawaji wa ardhi ulitokea na Walumbe akaenda magharibi zaidi hadi Buyanirwa.

Kutoka Busoga, Kintu alikwenda magharibi hadi kwenye nchi ambako, akiwa na koo rafiki (koo za tembo na funo), waliweza kupambana na Bemba, mtawala wa ufalme mkubwa wa Buddu, ambaye alipigwa na kuuawa. Kisha Kintu akaanzisha kiini cha dola iliyokuja kuwa Buganda.

Hivyo wakulima, ambao ni wazungumzaji wa Kibantu, walianzisha dola ndogondogo Buganda Busoga, Uganda mashariki, na Kenya magharibi ambako shughuli za wafugaji zilikuwa si za muhimu hadi karne ya kumi na nne. Miundo ya matabaka na mifumo ya kiamali ilianza kujitokeza kwa wenyeji.

Baada ya kifo cha Kintu, aliyekuwa mtawala kutoka mashariki kwenye Ziwa Wamara, koo kadhaa zikahamia kwenye nisisitu ya Ikweta iliyo kaskazini mwa Ziwa Viktoria. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa utano wa Kimera. Inasemekana Kimera alitawala baina ya 1344 na 1374. Simulizi moja inaelekea kuelezea kuwa kizimu cha ukoo wake kinaonyesha kuwa alikuwa na asili ya Kiluo. Masimulizi mengine

humhusisha na ukoo tofauti na kudai kuwa alikuwa ni wa nasaba ya Wasonga ambao walifika kabla ya kuja kwa watawala wa kwanza wa Wabito huko Bunyoro. Jambo muhimu ni kwamba, ili kuepuka mapigano ya Ndahura, makundi ya watu yaliukimbia ufalme wa Wachwezi na kutamakani kwenye misitu ya Ikweta ambapo wengine walihamia Nkore na Buganda. Kufuatana na mapokeo ya Buganda, utanzo wa Kimera ulijumuisha koo zifuatazo, nyati, pongo, senene, kindi n.k. Kimera anaweza kusemwa kuwa ana asili ya Kiluo au Kihima, kutokana na ukoo unaoangaliwa.

Kwa vile watu hawa walikuwa wanazikimbia tawala mbalimbali, ni dhahiri kwamba itikadi zao zilipingana na zile za Wachwezi, Wabito na Wahima. Ndio maana mapokeo yanayohusisha Buganda na kundi lolote kati ya hayo matatu yalizimwa, hata kama kuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha uhusiano. Kile kihichotokea kwa kweli kinaweza kupatikana tu kwa kulinganisha mapokeo mbalimbali.

Ingawa walihamia kwa nyakati mbalimbali, wengi wa wanaodai walihama pamoja na Kimera kwa sababu alifanikiwa waliingizwa kwenye koo thelathini na tano zilizotawaliwa na nasaba mpya ya kifalme aliyoianzisha. Kila ukoo, kwa kuwa ulitaka ushiriki kwenye utawala na kujipa fursa ya kutoa mfalme (*Kabaka*) siku moja, ulikimbilia kumpatia *Kabaka* wake.


21

*Mabonde ya Zambezi
na Limpopo
1100 - 1500*

Tamaduni za Jamii za Zama za Chuma Mnamo mwaka wa 1000

Kilipomalizika kipindi cha miaka elfu moja ya kwanza ya enzi ya Ukristo, aina mbili za vikundi vya binadamu zilikuwa zikiishi katika zile nyanda pana sana za nyika baina ya mto Zambezi na Limpopo katika enco lililoanzia Kalahari na kuishia Bahari ya Hindi. Kikundi cha kwanza kilikuwa cha wakulima waliokuwa wakilima mtama pamoja na kuendeleza shughuli za ufugaji na huku wakiwinda na kuhemea ili kuongezea chukula kilichoweza kupatikana. Watu hawa walikwishajipatia ubingwa katika fani ya kufua vyuma. Vijikundi vya watu wa kipindi cha mwisho cha Zama za Mawe vilivyoishi kwa kuwinda na kuhemea bado vilibakia miongoni mwa watu hawa, hasa katika sehemu wazi na tambarare za eneo la Kalahari.

Kuna ushahidi unaonyesha kuwako kwa makazi ya watu wa Zama za Chuma katika sehemu za Kusini ya Afrika ya Kati mapema kabisa mnamo mwaka wa 200 wa enzi za Ukristo, na jamii za wakulima zilizokuwa zikiongezeka kidogo kidogo na kutawanyika sana katika maeneo yalionusurika na ndorobo, ambayo yalikuwa na idadi ndogo kabisa ya wakazi. Kusambaa kwa kanda zenye ndorobo kuliathiriwa na mfumo wa kilimo ambao nao uliathiri kukua na kusambaa kwa idadi ya watu. Lakini shughuli za usafishaji wa misitu ziliathiriwa na hali ya tekuolojia ambayo hapo mwanzoni ilikuwa duni kabisa. Kulikuwa na ufinyanzi usionakishiwa lakini uliotengenezwa vizuri, ufuaji wa shaba nyekundu kwa ajili ya kutengenezea mapambo na baadaye nyaya, yote haya yakitendeka kwa misingi ya kujitosheleza huku biashara ikibaki ya aina ya kubadilishana bidhaa au ya mitaani tu. Mila hizi za kitamaduni zilizokuwepo mapema kabisa ambazo maendeleo yake yameweza kufuatiliwa kwa kutazama mitindo ya ufinyanzi na kwa kutumia mbinu za



21.1 Maeneo na mapoko ya kiakiojia yaliyotajwa kwenye matini (B.M. Fagan)

radiokaboni za kutambulia tarehe, ziliendelea hadi ndani ya milenia ya pili, pamoja na mbinu za kilimo zilizotumia majembe ya chuma na vilevile mipango yao ya kijamii na kisiasa katika vijiji vidogovidogo.

Hicho kinachojulikana kwa jina la utamaduni wa Kalomo ndicho kilicho kuwa chanzo cha Zama za Chuma katika sehemu za juu za bonde la Zambezi kwenye uwanda wa juu wa Batoka, ambapo sehemu za misitu ya savana ziliishia na kuanza ardhi ya malisho isiyokuwa na ndorobo na kwa hivyo kufaa kwa shughuli za ufugaji. Katika sehemu hizo, huko Isamu Pati, yamegunduliwa masalio ya utamaduni wenye aina mpya ya ufinyanzi (wa) baada ya karne za mwanzo za makazi yaliyoanza karne ya saba. Kijiji ambacho kiliamwa katika karne ya kumi na tatu kilikuwa na vibanda vilivyojengwa kuzunguka zizi la ng'ombe. Kilimo cha nafaka na utengenezaji wa zana rahisi za chuma au silaha ndizo shughuli kubwa zilizokuwa zikifanyika. Lakini dalili pia zimeonekana za kuwepo biashara za mitaani na masafa ya mbali ya kubadilishana bidhaa, vikiwemo vipande vya shaba nyekundu, na shanga kutoka migodi iliyokuwa kilomita mamia kadhaa kutoka hapa, na pia shanga za kigae na simbi kutoka mwambao wa mashariki. Lakini mabadilishano haya ya nadra hayakutosheleza kuleta mabadiliko makubwa katika mfumo wa jamii. Mara kwa mara kulitokeza kugawika kwa vijiji ili kupunguza shinikizo juu ya ardhi ya kilimo na malisho. Kwa namna hii utamaduni wa Kalomo inaonekana kwamba uhendelea mpaka kufikia mwaka 1450, lakini haukuweza kuifikia sehemu za kaskazini za uwanda wa juu wa Batoka.

Sehemu nyingine, kama zile za Sebanzi ukingoni mwa tambarare za Kafue na za Kangila, zinaonekana kuashiria utamaduni wa kileo wa Waila-Tonga ambao ni miongoni mwa vikundi vya kikabila vya zamani kabisa sehemu ya kaskazini ya Zambezi.

Historia ya baadaye imegubikwa na harakati kubwa za kuhama kwa makundi ya watu na mehanganyiko wa kijamii na kisiasa ambao unatokana zaidi na mehangano wa sehemu za bonde la Mto Kongo. Kwa upande wa ufinyanzi, mapokeo ya mitindo ya Zana za Chuma za Awali yalitoweka kufuatia kuibuka kwa aina mbili muhimu za ufinyanzi zilizotambuliwa na Philipson: aina ya Luangwa huko Zambia ya kati na ya kusini na kuendelea mpaka Malawi; na aina ya Lungwebungu huko Zambia magharibi.

Mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika karne za kumi na moja na kumi na mbili

Mfano wa awali wa jamii mpya zilizojitokeza katika jimbo hili katika karne za kumi na moja na kumi na mbili ni ule wa kile kitwacho Jadi ya Kilima cha Chui (*Leopard*

Kopje Tradition) ambayo inajitawanya kuanzia bonde la Limpopo kwa upande wa Kaskazini mpaka kwenye jimbo la Bulawayo na sehemu za kati za eneo lililoko kati ya mito ya Limpopo na Zambezi. Hapa vijiji ni vidogo zaidi kuliko makazi ya kipindi kilichopita, ambapo makundi ya ng'ombe yalionekana kuwa makubwa zaidi. Visanamu vya mafahali na masalia mengine yanayoonyesha kuachana na mitindo iliyotangulia vinaonyesha kwamba *Kopje* walikuwa wahamiaji ingawa kilimo cha mtama na uwele pamoja na uwindaji uliendelea katika kipindi hiki.

Katika karne ya kumi na mbili idadi ya watu iliongezeka, wakaanza kulima ile ardhi iliyokuwa na rutuba zaidi lakini yenye udongo mzito kwenye ukanda wa dhahabu wa Matabele. Vijiji vilikaliwa kwa muda mrefu zaidi, tukio ambalo luenda lilitokea sambamba na uchimbaji na ufuaji wa kwanza wa dhahabu. Sehemu hizi za makazi vilevile zilikuwa kubwa zaidi.

Kwenye kilima cha Mapela, kwa mfano, kuna kilima ambacho kiliwekewa matuta kwa kutumia mawe yaliyorundikwarundikwa, jambo ambalo linaonyesha kuweko kwa jamii kubwa iliyokuwa na nidhamu. Pia mkusanyiko wa vibanda juu ya kilima hiki ulikuwa mkubwa na wa maana zaidi kuliko ule wa vibanda vya chini. Labda hizo zilikuwa nyumba za watu muhimu. Kwa hivyo kulikuwa na kutofautiana na pia madaraja katika jamii. Shanga za vioo na vifaa vingine vya kutoka nchi za mbali vilijaa kama kwamba harakati za biashara na sehemu za mbali ziliongezeka sana. Jambo hili liliendelea kama makazi ya baadaye ya utamaduni huu yanavyoonyesha: madaraka na utajiri vilizidi kuhodhiwa mahali pamoja kama inavyoonekana katika magofu ya Mapungubuwe, ambapo katika karne ya kumi na tano kikundi kidogo cha watawala matajiri kilikikalia kilele cha kilima kilichotazama bonde la Limpopo, na kuonekana kama wanakitawala kijiji kikubwa. Shanga na vipande vyembamba vya dhahabu vinaonyesha kwamba watukufu hawa, ambao mamlaka yao yalikuwa ya kidini kama yalivyokuwa ya kisiasa, walitajirika kutokana na mashapo mengi sana ya shaba nyekundu ya bonde la Limpopo.

Katika sehemu nyingine, makazi mengine kama vile Musengezi katika ukingo wa kulia wa bonde la Zambezi, yamekaa katika hali hasa ya Jadi ya Kilima cha Chui lakini yenye madoido zaidi. Na hali iko hivi hivi katika jimbo la Inyanga. Kwa hakika Jadi ya Kilima cha Chui iligawanyika katika matawi ya kaskazini na ya kusini, na tawi la kusini liliboreshwa na kuweza kunusurika hadi karne ya kumi na tisa. Je, ruwaza hii inawezaje kuoanishwa na ramani ya lugha na makabila ya jimbo hili? Kishona na mkusanyiko wa lahaja zake (Kikaranga, Kimanyika, Kikorekore n.k.), ndilo kundi kubwa kabisa la lugha za kienyeji. Lugha nyingine zilizoingia kutoka nje ya eneo hili, kama vile, Kindebele, Kitongo na Kivenda zilingizwa katika karne ya kumi na tisa. Desturi za kitamaduni ambazo tumezielezea hapa ni dhahiri sehemu ya maendeleo ya watu wasemao Kishona.

Asili ya utamaduni wa Zimbabwe

Yale magofu mashuhuri ya Zimbabwe Kuu yaliyopo karibu na mji wa kisasa wa Masvingo yamechochea mawazo ya uzushi ya waandishi ambao walitafuta asili ya magofu hayo nje ya Afrika. Ukweli wa mambo ni kwamba magofu haya kwa yakini yalikuwa ni maendeleo ya Kiafrika, yalijengwa kwa kutumia mali ghafi ya kienyeji na kwa misingi ya usanifu majengo wa kale. Lakini sababu za msingi za kujitokeza kwa utaratibu wa kiuchumi, kijamii na kisiasa zilizoweza mafanikio haya na menginyo kama haya bado zinajadiliwa sana na wana historia.

Uvumbuzi wa kiakiolojia na makazi ya kale kabisa

Matabaka ya chini kabisa, ambayo tarehe zake zinafikia karne ya nne, ya msururu mrefu wa kitamaduni katika hicho kinachoitwa Kilima cha Akropolis kinachoukabili Uwa Mkubwa wa Zimbabwe, pamoja na vipande vichache vya vifinyange vilivyotawanyika katika bonde kwa chini, vyote hivi ni vya Zama za Chuma za Awali.

Wakati huo pahala hapo labda hapakuwa pakubwa sana: kilimo na uwindaji ndizo zilizokuwa shughuli kuu. Mpaka karne ya kumi ilipofika, ndipo watu wa Zama za Chuma za Baadaye walipofanya maskani katika Zimbabwe Kuu. Mpaka sasa karibu hapajulikani chochote kuhusu utamaduni uliokuwepo katikati baina ya utamaduni wa Kilima cha Chui na wa Zimbabwe Kuu. Utamaduni huu wa Gumanye ni wa mapema zaidi kuliko ule wa ujenzi wa zile kuta kubwa.

Ilipofika karne ya kumi na mbili, mabadiliko makubwa yalikuwatokea: ufinyanzi ulifanywa kwa ustadi zaidi, visanamu vya binadamu vilifinyangwa, shanga nyingi zaidi za kioo na vifaa kutoka nje vilijitokeza, kadhalika vitu vya kienyeji vilivyotengenezwa kwa shaba nyekundu na nyeusi, na vya dhahabu. Nyumba za udongo na fito zikawa madhubuti zaidi na majumba ya mawe kuanza kutumika. Kwingineko, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kilima cha Chui kama yale yaliyoko Mapela, maendeleo ya aina hiyohiyo yanaweza kuonekana katika jimbo lote ambamo kuna ishara za utamaduni wa aina moja ambao labda ulitiwa mweka na Kishona. Ni wazi kwamba mlimbiko wa kiuchumi na ubozezi katika shughuli za kijamii ulioambatana nao ulikuwa umeshaanza kujitokeza. Lakini ule msukumo wa awali ulitokea wapi? Kuna nadharia tete mbili kuu.

Donald Abraham anawaona Washona kama wahamiaji wa kipindi cha mwisho cha kikwi cha mwanzo ambao walianzisha ufundi maalum, hasa ule wa uchimbaji migodi, pamoja na madhehebu ya kuenzi mizimu. Walianzisha maziwara (madhabahu matakatifu); ziyara kuu ilijengwa kwenye kilima kilichoitwa *Dzimba*

dzemabwe (yaani nyumba za mawe). Abraham anaamini kwamba kwa kutumia mbinu za kijanja Washona waliimarisha uongozi wao juu ya muungano legelege iliokuwepo, na machifu wake kuwageuza vibaraka ambao waliwafanyia matambiko kwa wahenga na kwa *Mwari*, na machifu waliwapa pembe za ndovu na vumbi la dhahabu kama ushuru. Bidhaa hizi ziliwavutia wafanyabiashara wa Kiarabu kutoka mwambao wa Afrika Mashariki, na kwa njia hii biashara ikapanuka. Nadharia hii ya kwanza ambayo iliitwa nadharia tete ya kidini inafanya kigezo cha utamaduni kuwa ndio kiini cha msukumo katika maendeleo yote kwa jumla.

Kinyume chake, ile nadharia tete juu ya kuimarika kwa shughuli za biashara, inachukulia kwamba katika jani ya kinasaba chifu huwa ndiye tajiri kuliko watu wote, lakini utajiri wake hutumiwa katika kutekeleza shughuli kadha za kijamii. Kwa upande mwingine, kadiri hali ya kukutana kibiashara inayoimarika, ndivyo utajiri na madaraka vinavyolimbikizwa mikononi mwa wachache ambao punde huweza kuwalazimisha wakazi kufanya kazi za dola kama walivyofanya Walozi wa Zambia. Hivi ndivyo ilivyotokea kuhusu kuta kubwa za Zimbabwe Kuu, na kuhusu asili ya dola la Karanga, ambapo, katika karne ya kumi na nne, biashara ilifikia kilele kutokana na kuwepo kwa vioo kutoka Syria, fenza (vyombo vya udongo vilivyonakshiwa) kutoka Uajemi, na seladoni za Kichina ambazo zililipiwa kwa vifaa vya dhahabu na vya shaba nyekundu ambavyo pia vilizagaa huko Zimbabwe Kuu.

Pia huu ndio uliokuwa wakati wa kilele cha ustawi wa Kilwa ulionasibishwa na dhahabu na pembe za ndovu za jimbo la Sofala, ambalo ndilo lililokuwa kituo cha biashara cha Afrika ya Kati. Kwa mujibu wa Ibn Batuta, ambaye aliizuru Kilwa mwaka 1331, dhahabu ya Sofala ilitoka "Yufi katika nchi ya Limis", ambayo ilifikiwa baada ya safari ya mwezi mzima bara. Nadharia hii tete ya biashara ni madhubuti katika mambo fulani, lakini si madhubuti vya kutosha pale inapochukulia kwamba nguvu za kiuchumi moja kwa moja huwa sawa na madaraka ya kisiasa, au pale inapochukulia kwamba kundi kubwa la vibarua lilihitajika kwa ajili ya kujenga kuta za mawe, jambo ambalo huenda ikawa si kweli.

**Madaraka ya kisiasa na kiuchumi
katika kuunda dola la Zimbabwe Kuu**

Nadharia zote mbili zilizozungumzwa hazikutia maanani vilivyo hali halisi ilivyokuwa kuhusu kilimo cha kujikimu na zile tamtibu changamano zilizotumika katika kufikia maamuzi. Hakika ilipofika karne ya kumi na tatu jadi za Kilima cha Chui na Gumanye zilionesha dalili za maendeleo makubwa katika biashara na

katika kuyakusanya pamoja mamlaka ya kisiasa. Pia ukuaji wa idadi ya watu na macndeleo katika taratibu za kilimo huenda yaliruhusu kuweko vipindi virefu vya kupumzisha makonde baina ya kipindi kimoja cha kilimo na kipindi kingine. Lakini wengi sana miongoni mwa wale walioweza kujitoshleleza walikuwa wametawanyika vijijini na walivutiwa tu kuendesha biashara ya masafa marefu kutokana na sababu nzito za kidini au za kiuchumi. Na hata hivyo ilihitaji kuweko mamlaka ya juu zaidi ya kuidhibiti biashara ya aina hiyo ili iweze kustawi. Lakini mahitaji ya mali ghafi na vifaa vilivyokwisha tengenezwa peke yake hayakutosha kuweza kuchocha kujitokeza kwa mamlaka ya aina hiyo. Kilichohitajika ni kwa kikundi fulani kuchukua hatua ya kwanza ya kisiasa au ya kidini, ihyo lazima, na kikundi kikubwa cha vijiji (ambao kwa kweli vilikuwa tayari vinazo fursa nyingine) viukubali mfumo mpya wa matabaka ambao fidia yake ilikuwa kuongezeka kwa fursa za kujinufaisha.

Hapa kama kwingineko, sababu za kidini na za kibiashara pekee hazitoshi kueleza kuibaka kwa dola.

Kwa ufupi, Zimbabwe Kuu ni jengo la kuvutia mno lililotawaliwa na Akropolis ambalo limefunikwa na miamba mikubwa iliyoungwa na kuta zilizo jengwa kwa kame nyingi, na kutenga nyuwa mbalimbali, uwa ulio mkubwa kabisa ni ule ulio upande wa magharibi kabisa. Elimu ya mpangilio mawe, stratigrafia, imewezesha kufuatilia maendeleo ambayo kwa uchache yalikuwa ya awamu tatu.

Makazi ya dhati yalianza katika kame ya kumi na moja tu, lakini hakuna kuta za mawe zilizo jengwa mpaka kame ya kumi na tatu wakati pahala pa vibanda vidogo vidogo palichakuliwa na nyumba kubwa zaidi za udongo. Kujengwa kwa ukuta kwa ajili ya uwa wa upande wa magharibi kulitokea wakati ule ule zilipomiminika bidhaa kutoka nje. Kipindi cha mwisho cha ujenzi kilikuwa pale majengo ya kwanza yalipojengwa bondeni. Uwa Mkuu ulijengwa kwa kipindi kilichozidi kame moja; ule ukuta mkubwa wenye kuzunguka una wastani wa urefu wa mita 7.3 na unene wa mita 5.5 sehemu ya chini na kati ya mita 1.3 na 3.6 sehemu ya juu. Uwa huu unauzunguka ukuta mwingine wa mzunguko. Baina ya kuta mbili hizi kuna ujia mwembamba unaoenda kwenye mnara wa pia uliyojengwa kwa ustadi. Kutokana na muundo wake, ni dhahiri kuwa Uwa Mkuu ulikuwa ndiyo makazi ya watawala wa Zimbabwe Kuu. Katika matabaka ya juu ya Akropolis na katika Uwa Mkuu mapambo mengi ya dhahabu na shaba nyekundu, mabakuli mazuri na vifaa vya kuchonga vya mawe laini, chungu ya shanga za kioo kutoka nje, na vyombo vya kauri vya Kichina, Kiajemi na Kiarabu vya tangu kame ya kumi na nne vimepatikana. Hiki ndicho kipindi alichokuwepo Afrika Mashariki Ibn Battuta na wakati wa biashara kubwa ambayo watawala wa wakati huo bila ya shaka


waliidhibiti peke yao, jambo ambalo liliwafaa pamoja na kuhakikisha usalama na faida ya juu kabisa kwa wafanya biashara kutoka mwambao na pia uhakika wa kisiasa. Hii ilikuwa hasa hivi kwa vile dhahabu na pembe walizozitafuta zilienguliwa na watawala kwa njia ya dini na malipo ya kodi. Hakuna chochote cha kuonyesha kwamba wakati huu Waarabu kutoka mwambao walileta bara taathira zozote za kisiasa au za kitekuolojia. Kulinganisha mnara wa mviringo wenye ncha na misikiti ya Afrika Mashariki ni uzushi tu. Ukweli ni kwamba usanifu majengo wa Zimbabwe Kuu kimantiki ndiyo kilele kilichofikiwa katika ujenzi wa nyuwa kubwa na makazi ya machifu ambayo hapo kale yakijengwa kwa majani na tope na hivi sasa kwa mawe kwa sababu mbinu mpya ziliwezesha haya kufanyika. Kwani jamii iliundwa ili iweze kufanya hivyo, na mawe ya matale ya kujengea ambayo yalikuwepo kwa wingi yalichimbuliwa katika matabaka ya kawaida yenye unene wa kiasi cha sentimita 50 mpaka 100, na kupata mapande ya mawe ilikuwa shughuli iliyoweza kuharakishwa kwa matumizi ya moto na maji. Mbali ya mnara wenye umbo la pia, hapana chochote katika Zimbabwe Kuu kilichokuwa kigeni katika shughuli za Kiafrika. Hasahasa taathira za Kiarabu za hakika ni muhali kuzigundua.

Kipengee nyeti cha utamaduni, kama vile makazi kisingeweza kubadilishwa kutokana na biashara ya rasharasha ya masafa marefu iliyofanywa na Waarabu wachache au wakala wa biashara ambao pengine walifanya makazi ndani ya mipaka ya Zimbabwe Kuu.

Upanuzi wa Zimbabwe Kuu na utawazi wake kikanda

Zimbabwe Kuu ni pahala pa aina ya pekee kwa sababu tu ya ukubwa wake ikilinganishwa na magofu 150 madogo madogo yaliyotawanyika katika nchi ya mawe ya matale iliyoko kati ya mto wa Zambezi na mto wa Limpopo, ambayo mara chache huwa na vifaa vya dhahabu au shaba nyekundu na shanga za kioo. Kwa upande wa kronolojia, yanachukua kipindi cha kuanzia karne ya kumi na nne mpaka ya kumi na tano. Miundo ya magofu hayo inaonyesha umuhimu ambao mara nyingine ng'ombe walikuwa nao, na kwa kawaida ngome hizo za mawe zilikuwa ndogo, jambo linaloonyesha kwamba sehemu zilikuwa na idadi ndogo kabisa ya watu na hazikuweza kustawi kiuchumi, ingawa labda zilipokea malipo na mchango wa kikazi kutoka vijiji vya jirani vilivyokuwa vikiendeleza kilimo cha kuhamahama.

Katika magofu ya Nhunguza, kulikuwa na jengo moja tu kubwa sana, lililogawanywa katika vyumba vitatu: kimoja kilikuwa kikubwa sana (kwa ajili ya kupokelea wageni), cha pili kilikuwa na kiti kimoja tu, na cha tatu kilikuwa kimetengwa kabisa na lazima kilikuwa na vitu vya thamani au vya kidini.



21.2 Ukuta wa Wigo Mkuu huko Zimbabwe Kuu (P.S. Garlake, 1973)



21.3 Sanamu ya ndege iliyochongwa kwa juwe laini iliyopatikana kwenye magofu ya Philip kwenye bonde la Zimbabwe Kuu (P.S. Garlake, 1973)



21.4 Muara pia wa Zimbabwe Kuu (Idara ya Habari, Zimbabwe)

Tulichonacho hapa kwa mara nyingine tena ni mfumo wa mamlaka ya kisiasa au kidini ambao pekee ndio ulikuwa kiungo kilichounganisha jamii pamoja. Mipaka ya dola la Zimbabwe Kuu, hata katika karne ya kumi na nne haikutengwa wazi kabisa, lakini makao makuu yake yalikuwa sehemu za kati za nchi ya Washona.

Baadhi ya magofu ya aina ile ile katika sehemu ambayo sasa ni nchi ya Wandebele yamejitokeza kuwa vituo vinavyoonyesha taathira ya Zimbabwe Kuu kwenye eneo la Kilima cha Chui.


Mahusiano ya kibiashara na mwambao wa Afrika Mashariki

Tusihadaike na uchache wa bidhaa zilizokuwa zikibadilishwa kati ya vituo vya ndani katika bara la Afrika na mwambao wa Afrika Mashariki: bidhaa hizi zilikuwa ni vitu vya thamani. Ikiwa Ibn Batuta aliweza kuandika kwamba Kilwa ilikuwa miongoni mwa nchi za kupendeza kabisa ulimwenguni, mji huu ulipata sifa hii hasa kutokana na biashara ya dhahabu ya Sofala. Kwa namna hiyo hiyo, utajiri wa watawala wa Zimbabwe Kuu uliambatana na neema ya biashara ya mwambao ambayo ilikuwa njia pekce ya kutoa dhahabu, shaba nyekundu, na pembe za ndovu — ambavyo ilionekana kwamba Waafrika waliweza kuvitoka kwa wingi mno. Lakini biashara hii ilianza kupungua kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na tano, na walipowasili Wareno, biashara hii ilibaki kama kivuli tu cha ile ya hapo awali.

Uporaji wa magofu katika eneo hili umeifanya iwe taabu kudurusu taratibu na masharti ya biashara iliyoendelezwa na mwambao wa mashariki. Lakini katika sehemu za kaskazini magharibi ya mbali ya nchi ya Mashona, na katika bonde la kati la Zambezi sehemu kama Chedzugwe iliyojitawanya kwenye eneo la hekta 24 za majani mazuri, inaonyesha, kwa wingi wake wa mifupa ya ng'ombe na wanyama pori, umuhimu wa uchungaji na uwindaji. Ufuaji wa vyuma na shaba nyekundu pia ulistawi, shaba nyekundu ikiumbwa katika mikuo ya viwango viwili tofauti vya nzito. vikuku vya waya vilivyotengenezwa kwa shaba nyekundu na bati vilikuwa vitu vya kawaida. Vitambaa na vifinyange vilivyotengenezwa kwa ustadi kabisa na kunakishiwa kwa uzuri sana vinakamilisha sura ya uchumi ulioandaliwa vizuri kabisa kwa wakati huo.

Akiologia na mipaka ya taathira ya Zimbabwe

Chedzugwe ilikuwa na mahusiano sio tu na Zimbabwe Kuu bali pia na sehemu iliyojitenga ya Igombe Ilede (Zambia). Hili linathibitishwa na kuwepo kwa mikuo mizuri ya shaba nyekundu na vyombo vyepesi vilivyofinyangwa kwenye kilele cha kilima ambako makaburi kumi na moja yaliyopambwa kwa fahari na kuzungukwa na uzio wa vifaa vya kupendeza kabisa kutoka nchini na nchi za ng'ambo yaligunduliwa. Moja kati ya mifupa ya binadamu ilikuwa imevaa kidani cha kombe



21.5 Kibongetofali cha shaba iliyokalibiwa Katoka Ingombe Iledu, Zambia
(hacada ya karne ya kumi na moja) (B.M. Fagan)

za pwani, ambazo kijadi zilinasibishwa na uchifu, na pia nyuzi za chuma, shanga za shaba nyekundu na kioo zilizokuwa zikivaliwa shingoni na kiunoni. Mikuo ya shaba nyekundu yenye umbo la msalaba, patu za chuma, majembe ya sherehe na zana za kuvutia nyaya zilipangwa pia kuzunguka hiyo mifupa. Aidha masalia ya mavazi yamegunduliwa, na pia mabaki ya vigurudumu vya kusokotea uzi vinavyoonyesha kwamba vilifanywa na wenyeji.

Karibu vitu vyote hivi vinatokana na slughuli za biashara ya masafa marefu. Hakuna migodi ya shaba nyekundu, dhahabu au chuma ya haja, ingawa chumvi na pembe za ndovu ziliweza kupatikana mumo humo. Kwa hivyo inafikiriwa kwamba ile migodi mingi ya chumvi ya Mto Lusitu huenda ikawa ndiyo iliyowapa watu wa Ingombe Ilede "sarafu" ya kuwawezesha kupata madini ya thamani kutoka mikoa mingine upande wa kaskazini na kusini mwa Zambezi, ambayo waliweza kuyabadilisha na bidhaa za anasa kutoka mwambao wa mashariki. Bila ya shaka watukufu wa Ingombe huenda pia waliweza kupata bidhaa za nje moja kwa moja kutoka Zimbabwe Kuu kwa kubadilishana na chumvi. Kijiji cha Ingombe Ilede, ambacho huenda kilikaliwa tangu karne ya saba, kilikuwa kimchamwa na wakulima wa kujikimu ambao waliishi humo mwanzoni. Hivyo hakikuwa kituo cha biashara hapo awali. Lakini kilikaliwa tena kama mwaka 1400, na hapo tena makaburi yalitengenezwa kwenye mirundiko ya jivu laini kileleni mwa mlima. Huu ulikuwa ndio wakati wa kilele cha ustawi wa Zimbabwe Kuu. Hivyo panafahamika wazi. Ila bidhaa za thamani kama hizo ziliishia kwa watukufu wachache tu. Matabaka ya kijamii, kwa hivyo, yalikuwepo hapa kwenye mpaka wa kaskazini kabisa wa harakati za biashara kati ya mabonde ya Limpopo na Zambezi. Wakati, Valentin Fernandes alipofanya safari ya mwanzo kabisa katika sehemu za bara, mbele zaidi ya Sofala, katika mwaka 1514, alisikia hadithi za mto mkubwa upande wa kaskazini mwa Mwenemutapa ambapo watu wa "Mobara" walibadilishana shaba nyekundu kwa vitambaa. Inawezekana kuwa "Wambara" hawa ndio walikuwa wakazi wa Ingombe Ilede.


Kipeo kikuu cha karne ya kumi na tano

Karibu na mwisho wa karne ya kumi na tano Zimbabwe ilianza kuhamwa. Madaraka yalihamia upande wa kusini na wa magharibi chini ya kabila lililokuwa na nguvu la Rozwi. Mtawala wa kwanza, *Mwenemutapa* (mporaji mkuu) alikuwa Mutota, ambaye mwanawe Mutope aliutanuwa utawala huo na kuhamishia makao yake makuu upande wa kaskazini mbali na Zimbabwe Kuu. Kiasi cha mwaka 1490, sehemu za kusini ya utawala huo zilijitenga chini ya Changamire. Mwenemutapa, madaraka yake sasa yakiwa yamepungua, aliangukia moja kwa moja chini ya

udhibiti wa Wareno katika karne za kumi na sita na kumi na saba.

Lakini suala la kwa nini Zimbabwe Kuu iliamwa bado linabaki. Mashamba yaliyoizunguka huenda yakawa hayakuweza tena kuvikimu vijiji sambuse mfurno ghali wa Zimbabwe Kuu. Kutokana na kutoweka kwa taratibu za matumizi ya mbolea bandia au kilimo cha umwagiliaji maji, ambacho kisingeliwezekana hapa, uchovu wa ardhi uliwalazimisha watu wahamie kwenye sehemu mpya za nyika.

Juu ya sifa zake za utukufu na kutotikisika, Mwenamutapa ilibidi ahame. Misukosuko ya kisiasa ya mwishoni mwa karne ya kumi na tano huenda ikawa imetokana hasa na sababu za kimazingira na kiuchumi. Pale tu nguzo mbili za ustawi, yaani kilimo chenye nguvu na mtandao wa biashara ulizochangamka, zilipochoka Zimbabwe Kuu na mrithi wake (dola la Rozwe) zilitikiswa na kusambaratika.



*Afrika ya Ikweta na Angola:
Uhamiaji na kujitokeza
kwa Madola ya Awali*


Hali ya maarifa ya hivi sasa

Baina ya mwaka 1100 na mwaka 1500 jimbo hili limeguswa kidogo sana katika maandishi ya wakati huo ambayo yameshughulikia zaidi ufalme mmoja tu wa Kongo. Uchimbuzi wa kiakiolojia katika majimbo ya Shaba na Bas-Zaire hautoi sura kamili ya kikronolojia. Kwa hivyo simulizi za jadi zinabakia kuwa chimbuko muhimu la taarifa, hadi wakati ambapo taarifa za kiisimu zitakuwa zimeshaweza kutumika kikamilifu kwa ajili ya kuichunguza jamii ya awali ya Kibantu, kufarakana kwa lugha, na mchakato wa kuundwa kwa madola. Hapo ndipo itakapowezekana kuzitumia kikamilifu taarifa za kianthropolojia. Lakini pingamizi linabakia kuwa ni kutokuwepo kwa kronolojia kamili na ya kuaminika.

Katika hali hii jambo la kufanya ni kujaribu kukielewa kipindi hiki kwa kutumia taarifa za kiakiolojia na za kiisimu pamoja na simulizi za mapokeo kuanzia kipindi kilichotangulia mpaka kipindi cha baada ya mwaka 1500; na kwa njia hii kupata picha inayounganisha taarifa za mapema kabisa na za karibuni kabisa. Lakini picha inayojitokeza kimsingi ni ya nadharia tete tu.

Ikiwa kupanuka kwa lugha za Kibantu kunaonyesha uhamaji mkubwa, basi uhamaji huu ulimalizika kipindi kirefu kabla ya mwaka 1100. Ni kweli - kwa mujibu wa Oliver na Guthrie - kwamba chanzo cha asili cha Wabantu ni katika jimbo la Shaba. Huko ndiko mwenendo halisi wa maislia yao ambayo yalitegemea matumizi ya chuma na kilimo cha nafaka ulikoanzia, na kusababisha kukua kwa idadi ya watu na uhamahamaji wa kufuata mito, mwambao wa bahari, na hata misitu, ambako katika mwaka 1000, baadhi ya vikundi vya wawindaji na wakusanyaji bado vilikuwa vikiishi (Mbilikuno na wakulima waliowatangulia Wabantu). Isitoshe, watu hawa bado walibakia baada ya mwaka 1500, kipindi ambapo hajira za Wabantu zilikwisha malizika.

Nadharia hii inakataliwa na wanaisimu wengi wanaomfuata Greenberg na



22.1 Afrika ya Kati, 1500 (J. Vansina)

kukiweka chanzo cha asili cha upanuzi wa Wabantu baina ya Mto Benue na Mto Cross (Nigeria). Inasemekana kwamba watu wasemao Kibantu walitawanyika kutoka pale kuelekea Afrika ya Ikweta katika Ukanda wa Sanaga na Ogowe, kwa upande mmoja, na katika Ukanda wa Ubangi-M'Bomu kwa upande mwingine. Katika kipindi cha pili kulikuwa na "mlipuko" wa lugha kutoka Shaba au maenco ya Maziwa Makuu. Matukio haya yote kwa vyovyote vile yalimalizika kabla ya mwaka 1000. Katika bonde la Ubangi, ambalo ni eneo la mapambano ya lugha na mbari, zile lugha za kale kabisa zilizotumiwa na kikundi cha mashariki cha Adamawa ya Mashariki zilidhoofishwa na lugha za Kibantu au za Kisudan ambazo zenyewe zilikuwa katika mapambano ambayo matokeo yake hayakuweza kuamuliwa kwa karne kadha.

Kwingineko, Wabantu walianzisha matumizi ya lugha zao, huku wakikopa sifa nyingine za kitamaduni kutoka kwa wenyeji na kwa hivyo kuweza kuwa na ustaarabu ulionona na wenye sifa za aina nyingi.

Sura ya nje ya mbari za awali ilikwisha anza kuwepo kipindi kirefu kabla ya mwaka 1500, kama mfano wa Waimbangala unavyoonyesha ambao walikuwa mchanganyiko wa Waluba, Walunda, Waovimbundu na Waambundu. Mchanganyiko huu pia ulitokana na mgawanyo wa kazi kati ya wakulima, wawindaji na wavuvi, na kusaidiana kulikohitajika kati yao.

Maingiliano ya watu ndani ya bonde la kati yanaelezea kwa nini lugha za Kimongo zimebaki kuwa za aina moja. Kwa upande mwingine katika eneo kama lile la Manyema, msitu na ardhi ya milima ilihifadhi sifa maalum za sehemu hii, lakini hata huko makundi mawili makubwa, yaani kundi la Lega na kundi la Korno, yalitamalaki.

Athari ya mawasiliano katika lile eneo muhimu kati ya mito ya Zaire na Ubangi-M'bomu, bado ingali katika hali ya dhana dhana. Kwa mujibu wa Ehrct, mwanaisimu, Wasudan wa sehemu ya kati waliikalia sio tu sehemu ya kaskazini-mashariki, bali pia nchi yote upande wa mashariki ya Lualaba ambapo walikwisha gawika katika makundi mbali mbali ya kilugha kabla ya kuwasili kwa watu wasemao lugha za Kibantu. Lakini lazima ikumbukwe kwamba sura ya makazi ya watu ilibadilika sana kutokana na uhamahamaji mkubwa wa baadaye ulioanza karne ya kumi na saba mpaka karne ya kumi na tisa. Kwa hivyo uhamiaji wa Wabanda kutoka Sudan ya kusini ili kuepuka mashambulio ya wateka watumwa uliwasukuma kando Wasabanga ambao walisalia katika hali ya vikundi vidogo vidogo miongoni mwa umati wa Wabanda. Ni ufalme wenye nguvu wa Nzakara tu ndio ulioweza kulipinga wimbi hili na kuendelea kubakia; lakini kwa upande wa magharibi mashambulio kutoka Adamawa yaliyasukuma makundi ya Gbaya upande wa

mashariki.

Historia na ustaarabu

Kilimo

Taarifa ya kiekolojia na kiakiolojia zinaonyesha kwamba hata kabla ya mwaka wa 1100 kilimo kilikuwa kikiendelezwa kila mahala isipokuwa kusini mwa Angola karibu na jangwa la Kalahari, na kwenye baadhi ya maeneo ya misitu. Mtama mwekundu na mtama wa kawaida (hasa kwenye sehemu za nyika), viazi vikuu, majimbi, ndizi na miwa ya asili ya Kiasia (hasa msituni), njugu nyasa na kunde za aina mbalimbali zililimwa sana kwa kutumia vifaa vya chuma. Uvuvi, uwindaji na ukusanyaji wa viwavi na mafunza pamoja na ufugaji wa wanyama wadogo (wakiwemo nguruwe na ng'ombe wenye pembe katika sehemu za chini za mto) ulisaidia kupatikana kwa chakula cha kuridhisha. Na pia tusinghai sehemu za nyika za hapa na pale mwituni. Na ilikuwa hasa katika kingo za kando kando za nyika kama hizi, kando kando mwa msitu ambamo makundi ya binadamu yanayofaidika na mazingira ya aina zote mbili yaliweza kuongezeka kwa haraka. Hali kama hii ilijitokeza pia katika yale maeneo membamba yenye miti kando kando ya mito mingi iliyojaa samaki.

Sanaa za ufundi na biashara

Ilipofika mwaka 1100 mbinu za sanaa za ufundi ambazo wasafiri wageni walivutiwa nazo mwishoni mwa kipindi hicho zilikuwa tayari zinajulikana: ufinyanzi, usukaji vikapu, usukaji majamvi, utengenezaji makasiki, utengenezaji wa chumvi ya mawe na ya bahari, utoaji chumvi kwenye mimea na kwenye sehemu za matope ya chumvi, na ufuaji wa madini kama inavyoonekana kwenye machimbo ya Buar, Sanga na, labda, Munza (Shaba).

Ishara za mwanzo za mzunguko wa mikuo ya shaba nyekundu ya aina ya msalaba kama pesa zimejitokeza kauka ukanda wa shaba nyekundu kama mwaka 1000, na zinaweza kuonekana kuanzia Zambezi mpaka Lualaba kabla ya mwaka 1450. Simbi, vipande vya majamvi, chumvi ya mawe kutoka Kisama, vyote vilitumika kama pesa. Wachukuzi wa mwanzo labda walikuwa wavuvi waliokuwa kwenye sehemu za mito zilizoweza kupitika na wafanya biashara waliobadilishana vyuma, shaba nyekundu na chumvi, hususan na nyama ya pori kutoka kwa wawindaji wa msituni.

Jamii na upangaji wa madaraka

Mukundi haya yaliishi kwenye vijiji vyenye msongamano na katika nasaba za

kuumeni. Lakini kuna ukanda wa jamii zenye kuzingatia nasaba za kuukeni kwenye eneo linaloanzia Namibia mpaka Zambezi, na kuanzia Ogowe mpaka Ziwa Tanganyika. Murdock anadai kwamba hali ilikuwa vivyo hivyo miongoni mwa wakazi wote wa misituni upande wa magharibi ya Lualaba. Jambo la uhakika ni kwamba katika karne ya kumi na tano, mbali ya Waluba wa Kasai na Shaba, ambao pia walikuja kubadilika baada ya mwaka 1500, wakazi wote wa msituni walichukua nasaba za kuumeni. Mabadiliko ya hatua kwa hatua yalipendelea mfumo huu. Kwa hakika ndani ya mfumo wa kuukeni wa Kibantu, ile fikra kwamba wanaume walikuwa na mamlaka juu ya wanawake ilitambuliwa na hii, kwa mfano, ilisababisha makazi kutawaliwa kiume. Hii ilisababisha kudhoofika kwa nasaba za kuukeni, na kupendelea zaidi kuwepo kwa mamlaka ya maeneo, na kwa hivyo ya kisiasa, kijijini. Wadhifa wa uchifu, kwa hivyo, ulikuwepo tangu mwanzo.

Miongoni mwa makundi ya nasaba kuumeni yasiyozungumza Kibantu, hali ilitofautiana. Upande wa kaskazini baadhi yao waligawanyika katika vijiji vidogo vidogo visivyokuwa na machifu, wakati katika sehemu za Ubangi na Chari, kulikuwa na vijiji vikubwa vilivyokuwa na nasaba tawala chini ya mamlaka ya machifu.

Katika sehemu za nyika upande wa kusini, wakuu wa nchi ambao pia walikuwa wakuu wa mizimu ya nchi, walishika madaraka ambayo kwa kweli yalikuwa mamlaka ya kisiasa juu ya mkusanyiko wa vijiji ambavyo vilikuwa ndio chanzo cha falme. Katika hali halisi, wakuu wa koo zilizokuwa kubwa na tajiri kabisa walikuwa ndio mabwana wa nchi, na baadaye wakawa wafalme ama kwa kuzimeza koo nyingine au kwa kutumia mabavu. Uzalishaji wa ziada wa mazao uliwanusuru machifu na washauri wao na kazi za mikono, na kwa hivyo wakaweza kupanda mbegu ya madaraka ya kidola. Haya yalikuwa yakitokea katika mawanda ya eneo ambamo kila mtu alitambua mamlaka moja tu. Hapo mwanzo mamlaka hayo yalibaki na sifa zake za kidini, jambo ambalo linaelezea sifa ya utukufu ya mamlaka hayo. Baadaye kuongezeka kwa ziada kuliwchezha mgawo mpya wa mali na hadhi kwa wateule wengi zaidi, na hivyo kupanua mfumo wa washauri, mahakimu, na kadhalika. Mfumo wa uteja ulizuka na kuendelezwa kwa kugawa tembo la mnazi au pombe. Miviga maalum iliyoambatana na kinywaji cha mfalme iliudhihirisha mfumo huu kwa vitendo. Ili kutosheleza mahitaji ambayo yaliongezeka kufuatana na wingi wa wateja, na kwa ukosefu wa maendeleo muhimu ya teknolojia, wafanyakazi zaidi walihitajika. Kuanza kwa utunzi wa majumbani kulikidhi haja hii, watumwa wa mwanzo wakiwa labda mateka wa vita au wahalifu ambao hukumu zao za kifo zilikuwa zimebadilishwa. Hawa waliongezwa kwenye kikundi cha wafanyakazi ambao, kwa jamla, walikuwa wanawake. Vita vya mara kwa mara vilivyoongezeka vikiambatana na kukua kwa madola viliuchochea mfumo huu udumu.

Juu ya hivyo, ingawa hali ya uchumi ilikuwa nzuri, baadhi ya koo zilipinga

ujenzi wa dola. Kupenda usawa na haja ya kujijengea nguvu yalikuwa matakwa mawili yaliyopingana ambayo yalisuluhishwa kwa kukua kwa muungano wa koo zenye misingi ya jumuiya zenye miviga maalum. Mfano ni Wangbandi ambao bado walitoa nasaba za watawala wa sehemu nyingine, na pia Wagbaya ambao walikuwa majirani za Wambum ambao jamii yao iliundwa kidola. Hatimaye, Wasara walisaidia kuunda ufalme wa Bagirmi, lakini walihifadhi koo zao.

Kwa upande wa dini kulikuwa na hali ya kufanana kwa kuwepo kwa sihiri, ramli, miviga ya rutuba na tiba, na vile vile madhehebu ya wahenga na mizimu ya kienyeji. Aina zote za mamlaka yakiwemo yale ya mkuu wa familia, yalikuwa na sifa zilizopindakia zile za kibinaadamu, ambazo kwa harakaharaka zilipewa jina la "ufalme mmkufu" na juhudi zilifanywa kutafuta asili moja tu yenye kujumuisha tarche na mahali ya mila hizi. Lakini kuna tofauti muhimu katika ruwaza liizi, kwa mfano katika falme za Luba au kwenye mwambao wa bahari ya Atlantiki, jambo ambalo linapinga unasibishaji wa mila hizi.

Sehemu za savana kaskazini

Mapokeo simulizi ya Wangbandi wanaochukua nasaba kuumeni ambao walitoka katika ile sehemu ambayo sasa ndiyo Jamhuri ya Sudan kusini mwa Bahr-al-Arab, yanatuwezesha kusema kwamba labda walifukuzwa kutoka kwao na Waarabu wa Kinomadi wa Bakkara yapata mwaka 1300. Visasili vyao vyaelezea juu ya watu weupe waliokuwa na mikuki, pinde na mishale, visu, vishale, na hata bundaki, ambao walianzisha uhamaji ulioendelea kwa kame mbili na ukawapeleka Wangbandi mnamo mwaka 1500 hadi kwenye eneo baina ya Katto na Dar Runga, ambalo wakati huo lilikaliwa na Wamanja-Ngbaka upande wa magharibi na wasemaji lugha ya Kibantu upande wa mashariki. Watu wa Sudan ya kati walikwisha gawanyika kwa uchache katika makundi mawili, kundi mojawapo likijumuisha Wasara na Wabagirmi wa baadaye.

Katika kame ya kumi na sita nasaba moja ya Wangbandi ilianzisha ufalme wa Nzakara ambao raia wake walitumia lugha ya Kizande, wakati Wangbandi wengine walianzisha nasaba kubwa chini ya malodi. Labda liuu ulikuwa ni mfano numoja tu kati ya harakati ngumu sana za hajira za vikundi vya kikabila na vya kiisimu ambavyo havikuhama kwa mawimbi bali kwa kujipenyeza huku vikiathiri kitamadum baadhi ya mambo.

Mbilikimo, kwa mfano, walichukua lugha za Sudan ya Kati. Jambo ambalo wanaakiolojia wanaliona hapa ni kule kubaki kwa muda mrefu kwa vifaa vya Zama za Mawe sambamba na vile vya chuma, kama huko Misri ya Kale. Mawe yaliyotumika ni ya aina ya mtapo chuma (hacmatite), yenye sehemu kubwa ya chuma, hata ikawa kwamba kule kuzidi kidogo kwa uwezo wa zana za chuma wa



22.2 *Kengele Pacha ya Chuma kutoka Mangbetu (Zaire Musée Royale de l'Afrique Centrale)*

kutekeleza shughuli zake haku kulingana na kazi kubwa sana ya ziada iliyohitajika kuyafua mawe hayo ya mtapo chuma.

Msitu mkuu wa ikweta

Msitu haukuwa uzio wa kijani usiopenyeka bali chunjio lililopitika kwa njia mbili maalumu: moja kando kando na mwambao na nyingine kutoka Kadei Sangha kupitia Ubangi na Kongo/Zaire mpaka Ziwa Malebo. Safari za baharini zilianza kabla ya mwaka 1,000, kama inavyoonekana kutokana na kuwepo kwa watu wa Bubi huko Fernando Po na kwa kufanywa kwa sanamu za mbao za rangirangi kuanzia nchi ya Yoruba mpaka Lwango.

Mwisho, makutano ya mito ya Ubangi, Sangha na Zaire/Kongo yalisababisha kuwepo kwa eneo kubwa la matope la msitu wenye mafuriko lililoweza kupitwa na wavuvi tu.

Kwa njia hii kengele moja moja zisizokuwa na kilimi na baadaye kengele pacha zilivuka msitu kutoka kaskazini mpaka kusini, zikisafiri kutoka Ife wakati wa utukufu wake mpaka Zimbabwe ilipofika karne ya kumi na tano. Utengenezaji wa kengele hizi ulihitaji ujuzi wa kufua mabamba ya chuma na wa kuyachomea. Pia zile kengele pacha zilitumiwa kuigiza toni za lugha inayoscmwa (kwa upande wa lugha za Kibantu) mbali ya kengele hizo kutumika kama alama ya madaraka ya kisiasa, kuanzia Nigeria mpaka Zambia. Kwa njia hiyo hiyo visu vya kurusha na ngoma ndogo za mgambo pia zilitokea upande wa kaskazini (zikithubitisha nadharia ihusuyo upanuzi wa Wabantu uliotajwa hapo juu). Ni wazi kwamba fikra na mila pia ziliweza kufafanua pamoja na vifaa hivi. Miongoni mwa fikra hizi ni ile fikra muhimu ya kuwa na chifu wa kisiasa. Kwa mfano lugha za Kimongo zinatofautisha baina ya haki ya mahusiano ya damu iliyokuwa ikiitwa kwa jina *mpifo* na haki ya mkazi wa kwanza mwinyi wa nchi, *okofo*. Ni hawa mamwinyi wa kwanza ambao, kwa kutumia taratibu za uteja zilizotajwa hapo juu, walikuja kuwa machifu wakuu wa kwanza na baadaye wafalme.

Utaratibu wa kijamii msituni na sehemu za wazi

Kabla ya mwaka 1500 kulikuwa na msambao mkubwa sana lakini wa taratibu wa watu waliozungumza lugha za Kimongo katika sehemu ya kusini-magharibi ya mbali ya Sankuru na Kasai. Tawala ndogo ndogo za machifu au *nkumu* zilizoanzishwa wakati wa kuhuma haku zilikuwa na sifa zifuatazo: kijiji kiliwakilishwa na wasemaji wawili: mmoja kwa kila moja ya makazi mawili katika kila upande wa mtaa mkuu. Mahusiano na Mbilikimo yalikuwa ya kigeugeu: mara nyingine waliishi kwa mashirikiano, mara nyingine walipigana. Madaraka

yalifuatana na umri katika mfumo wa erontokrasia, uliowapa madaraka wazee. Upande wa kusini wa jimbo hili, mahusiano ya ndoa yaliimarisha madaraka ya maeneo. Jambo la kuvutia hapa ni ule uwezo wa watu wa msituni wa kufua vyuma. Wasongye wamekiri kwamba Waluba, amabao walitoka msituni, waliwafundisha jinsi ya kufua vyuma. Kwa kuchoma miti yenye mbao ngumu, watu wa msituni waliweza kutoa hali ya joto kubwa na hata walivumbua jinsi ya kutengeneza chuma cha pua.

Habari kidogo tu inajulikana ya historia ya msitu unaoanzia Gabon mpaka Jamhuri ya Kongo wakati huu. Kuhama kwa Wapahvin kulikuwa kwa taratibu kulioanza kabla ya mwaka 1500, na pengine kwa miundo ya aina ya *nkumu*. Huko Manyema wazazi wa jadi wa Walega pengine walikuwa tayari wakiishi katika jumuiya za kijamii na kisiasa zijulikanazo kama *bwami*, pamoja na mfumo wao changamano wa madaraja ya kijamii ambamo daraja la juu kabisa liliwakilisha maadili ya jumla na madaraka ya kisiasa. Inaaminika kwamba watu wa sehemu ya magharibi ya Ziwa Kivu na Ziwa Tanganyika waliendeleza dhana za uchifu na ufalme kutokana na msingi huu wa *bwami*.

Mchakato kama huu pengine ndio ulioleta ulodi wa kuchaguliwa miongoni mwa Wasongye wa kusini. Kwa ufupi, kinyume na ilivyotarajiwa, msitu ulikuwa ndiyo chimbuko la maendeleo makubwa ya ufundi na ya kijamii na kisiasa.

Sehemu za nyika za Shaba

Ni lazima kupambanua baina ya jadi ya mashariki (iliyogawika katika utanzo wa Kiluba na utanzo wa sehemu ya juu ya Kasai Shaba) na jadi ya magharibi kwenye mwambao wa Atlantiki. Kwa hali hii hadithi kuhusu asili ya tawala za Waluba na Walunda haziwezi kudhaniwa kuwa ni visasili tu.

Kituo kikubwa kuhusiana na mbinu za kufua chuma ni kile kilichoko Sanga. Kuhusiana na maendeleo haya, tofauti za kijamii lazima zilichipuka baina ya Zambezi ya kati na Limpopo. Isitoshe, jimbo hili liliungana na maziwa ya Luahaba kwa biashara ya kipindi kirefu ya misalaba ya shaba nyekundu, ambayo ilikuwa sehemu ya mtandao wa biashara ulioenea hadi Bahari ya Hindi.

Falme za Luba na Lunda

Mapokeo ya mdomo yanaelezea habari za machifu wa "Kiluba" huko Malawi na Zambia. Dola la Kilunda linajulikana kwamba lilikuwepo kabla ya mwaka 1450. Kwa kweli, hali zote za kuwezesha kukua mapema kwa tawala za kichifu zenye nguvu zilikuwepo hapo: yaani migodi ya shaba nyekundu ya huko Shaba, ardhi zenye rutuba, na urahisi wa kusafiri kupitia sehemu za nyika — yote haya

yalihamasisha shughuli za biashara.

Utawala wa Kiluba labda ulianzishwa kabla ya mwaka 1500 na mtu aitwaye Kongolo, karibu na Kalongo, kwa kuchanganya koo kadha zenye nasaba za kuumeni. Kila ukoo, ambao uliongozwa na chifu au *kiloto*, yaani "mmilikaji watumwa," liliyatambua mamlaka ya mfalme. Mfalme alizungukwa na si chini ya watukufu wawili: Mtunzaji wa nembo za mamlaka aliyeitwa *inabanza*, na mkuu wa jeshi au *twite*. Utukufu wa ufalme au *bulopwe* ulirithiwa ndani ya damu ya nasaba tawala kwa msingi wa *mpifo*.

Maliasili ya chumvi, madini na shaba nyekundu, mchanganyiko wa watu, na biashara vilifanikiwa kuchochea kuchipaka kwa miji mikubwa, kuongezeka kwa ziada ya bidhaa, na kukua kwa asasi za kisiasa. Kuhusu suala hilo la mwisho, Wasongye wanatafautiana sana na Waluba kwa vile wao wana ufalme wa kuchaguliwa ambao kigezo cha utajiri kilikuwa na uzito mkubwa: mara nyingi huu ulikuwa ni ufalme wa muda maalumu na uliotegemea ushauri wa jumuiya ya siri, iitwayo *bukinshi*. Srikali ya nasaba ya kuukeni ya Luba mashariki ilitegemea jumuiya za kisirisiri kama hizi.

Kwa upande wa Walunda, kuanzia sehemu za juu za Kwango mpaka sehemu za juu za Kasai na mipaka ya Zambia, walikuwa wakiendelea kufuata misingi ya ufalme wa milele kiitikadi na kisiasa. Mfumo huu haukutambua kupita kwa wakati ili kuhakikisha kutovunjika kwa mshikamano wa nasaba tawala, na waliamini kwamba mrithi wa ufalme hakika alikuwa ndiye yuleyule aliyemtangulia, na alichukua jina lake, mahusiano yake ya ukoo, kazi na haki zake, na hivyo kuendeleza milele mtandao wa makubaliano "ya kidugu", mashirikiano na miungano. Hiki ndicho chombo cha kiitikadi ambacho ufalme mkubwa wa Lunda ulikiunda baada ya mwaka 1500.

Sehemu ya magharibi ya jimbo hili ilikuwa kidogo maskini, lakini ilikuwa na migodi ya chumvi na mashapo ya shaba nyekundu kati ya Lualaba na Luapula. Dola la Lozi, ambalo lilijitokeza katika bonde la juu la Zambezi, labda lilifuata mfano wa Lunda.

Angola

Bonde la Lui, ambao ni kijito cha mto Kwango, lilishuhudia kuzuka mapema kwa tawala za machifu zilizotawaliwa na Wapende. Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, upande wa kusini wa Libolo, dola moja la Kulembe lilijitokeza ambalo msingi wake ulikuwa ni jumuiya za kufunda mambo ya kijeshi, yaani *kilombo*. Labda ilikuwa moja kati ya madola ya mwanzo ya Ovimbundu ambayo alama yake hasa ilikuwa makaburi ya mawe. Waovimbundu ambao wanatumia lugha ya Kibantu ya sehemu za kusini magharibi, walihusika na uasisi wa dola ya *Humbe*, kusini mwa

Angola, kwa msingi wa *kilombo* ambacho huenda kilikwisha anzishwa hapo na Waimbangala. Baadhi ya madola kumi na nne ya Ovimbundu, ambayo kijamii na kitamaduni yameungana na Angola kusini, huenda yalizuka kabla ya karne ya kumi na sita.

Watu waliozungumza Kibantu wa Angola Kaskazini na Namibia waligawanyika katika matawi matatu makubwa: Wanyanyeka-Humbe, Waambo na Waherero. Miongoni mwa kundi la mwanzo, Wahumbe tu ndio waliounda utawala wa kichifu wenye nguvu, ambapo ilipofika karne ya kumi na tisa Waambo walikwisha unda madola kumi na mawili yenye miji mikuu yenye ngome imara, urithi wa kuukeni na madataka ambayo alama yake ilikuwa moto mtakatifu, na muundo wa kiuchumi uliotegemea umilikaji wa ng'ombe. Waherero walikuwa wanomadi waliokuwa wafugaji ng'ombe, wawindaji na wakusanyaji kama majirani zao wa Kikhoi huko Namibia.

Wanyanyeka-Humbe walidai kuwa ni wazawa. Matawi mengine yanaonyesha kwamba yametoka eneo la Zambezi, kuelekea upande wa mashariki. Makundi yote haya yanaonekana kuwa yaliingiza idadi kubwa ya wawindaji (watwa).

Inaelekea kuwa Wabantu waliolikalia eneo la kati la nyanda za juu la Angola na mabonde ya Angola Mashariki walizungukwa na wawindaji weusi wenye utamaduni wa Kisan katika sehemu za mwambao, na Wakhoi na Wasan kusini katika nchi iliyokuwa kati ya mito.

Upande wa kaskazini ambao ulikuwa na maji zaidi makundi ambayo kilugha yalikusika na kundi la Lunda - Guangella-Chokwe yalikuwa yakicndeleza kilimo cha Zama za Chuma.

Nyika za Kusini Magharibi

Wareno walipowasili, walikuta falme tatu, kuanzia kaskazini mpaka kusini: ufalme wa Makoko Kuu au Tio/Bateke ndani bara, Lwango na Kongo, zilizoanzishwa moja baada ya nyingine katika karne za kumi na tatu na kumi na nne. Inawezekana, ikiwa kweli watu hawa walikuwa na asili moja kaskazini, kwamba jamii ya awali kando kando mwa msitu wa Mayombe ilikuweco mnamo mwaka 1000.

Kwanza walilizoea eneo la nyika au sehemu ya nyanda za juu ya Bateke. Baadaye Wakongo walijitawanya upande wa kusini, nao Wavili wa Lwango wakalowea kando kando mwa mwambao, wakati Wabateke walizikalia nyanda za juu za kusini, mapori ya Gabon.

Mfumo wa maendeleo kama ule uliotokea mwituni unaweza kufikiriwa kuwa ndio uliotokea hapa: vijiji vikubwa vya nasaba za kuukeni vyenye machifu wa kisiasa na kidini, pamoja na washauri, ushirikiano na miungano, madhehebu ya

kuenzi wahenga na mizimu, na tabaka za kijamii zilisababisha kuwepo kwa mamwinyi, na mateka walioshughulikia kazi za kilimo; na biashara iliyofanywa kwa mujibu wa mfumo bayana wa fedha.

Ufalme wa Kongo kabla ya mwaka 1500

Maelezo ya Wareno yameufanya utawala huu ujulikane zaidi ya tawala nyingine. Lukeni Nimi ndiye aliyefunga safari kutoka Mayombe akavuka mto na kuanzisha ufalme kwa kuushinda utawala wa kichifu wa Ambundu wa Mbanza Kongo. Baadaye wegani walichanganyika na wenyeji. Kwa mujibu wa Pigafetta na Lopes (1591):

"Utawala huu umegawanyika katika majimbo sita: Bamba, Sogno, Sundi, Pango, Batla na Pemba. Bamba, iliyo tajiri na kubwa kabisa, inatawaliwa na Dom Sebastiao Mani Mamba, mtoto wa mjomba wa Mfalme Dom Alvaro, aliyekufa karibuni ... wako malodi wengi wanaomtegemea .. Neno *Mani* maana yeke ni "Lodi" na sehemu ya pili ya jina inamaanisha nchi. Kwa mfano, Mani Bamba, maana yake ni "Lodi wa jimbo la Bamba". Baniba ... ndiyo ufunguo wa ufalme ngao yake na upanga wake ... wananchi wake siku zote ni mashujaa na wako tayari kutwaa silaha, kuwafukuza maadui kutoka Angola ... pakihitajika jeshi la askari laki nne linaweza kukusanywa.

Hii idadi ya mwisho bila ya shaka imetiwa chumvi lakini inatoa picha ya ukubwa wa idadi ya watu nchini.

Mfalme wa Kongo, pasi na kuwa mtawala wa mabavu, alikuwa na mamlaka mukubwa. Alitcua magavana, isipokuwa gavana wa Mbata, ambaye "alichaguliwa na watu na watukufu wa familia ya Nsaku na kupata uthibitisho wa mfalme". Katika jimbo la Soyo, gavana wake alikuwa wa kurithi. Pia inaonesha kwamba kabla ya mwaka 1500 ufalme wa Kongo ulikuwa mkubwa zaidi kwa vile uhiendelea kuweka madai ya utawala juu ya Kakongo, Lwango, ufalme wa Teke, na kadhalika.

Magavana walikusanya kodi na malipo mengine yaliyofanywa kwa bidhaa: mtama, tembo la mnazi, ng'ombe, pembe za ndovu, ngozi za chui, lakini zaidi kuliko vyote hivi, vipande vya majamvi na simbi ya kiishara (*nzimbu*, zikitumika kama pesa). Ngozi za chui na simba zilikuwa na thamani ya kiishara zikiwa ni alama ya uchifu.

Utawala mkuu, ambao uliweza kuondolewa, uliwajumuisha mkubwa wa ikulu ambaye alikuwa ndiye mwakilishi wa mfalme, jaji mkuu, mpokea kodi pamoja na wasaidizi wake, mkuu wa polisi, huduma za utarishi, na kadhalika.

Lodi *kabungu*, aliyetokana na wazawa wa eneo hilo, hapa kama kwingineko

Afrika, alikuwa kama kuhani mkuu na mkubwa wa nchi. Magavana walikuwa jamaa wa karibu wa mfalme waliokabidhi Nsundi na Mpangu kwa wanawe. wapenzi. Kwa hiyo walikuwa na msingi madhubuti wa kupigania urithi wa utawala Magavana waliwachagua malodi wadogowadogo ambao nao waliwatawala *wankuluntu*, machifu kwa kurithi wa vijiji. Makaburi ya wazee, ambayo yalikuwa karibu na mji mkuu, yalihusishwa na ibada za kidini. Ingawa mfalme akiitwa *nzambi mpungu* au "mzimu mutukufu", yeye mwenyewe binafsi hakuwa mtukufu: madaraka tu ndiyo yalikuwa mmkufu. Kwa kumnajisi dada yake, mtawala alijitenga mbali na wanadamu wa kawaida, na kwa kubaki "bila familia" aliweza kuzitawala familia zote kwa haki. Kwa kitendo hiki na kwa mafundo maalum ya kutawazwa alijipatia uwezo mkubwa juu ya matalasimu kutokana na nguvu maalum za sihiri. Nembo zake za utukufu zilikuwa ni pamoja na vazi la kichwani, ngoma, kikuku cha shaba nyekundu au pembe, na kigoda cha mti. Alizungukwa na taratibu za itifaki mithili ya zile za kidini, ambazo Wareno wamezielezea vizuri kama walivyoelezea mji mkuu na maisha ya nyumbani kwa mtawala katika karne ya kumi na tano.

Banza (ambayo maana yake ni nyumba ya mfalme au bwana mkubwa), yalikuwa makao makuu yaliyozungushiwa kuta za mawe. Kutoka kuta hizi msaada uliweza kupelekwa mara moja kwenye majimbo mbali mbali ya ufalme. Makao haya yalikuwa ndiyo mji mkuu wa biashara, na makutano ya njia kuu; Wareno waliupa jina la San Salvador.

Baraza la watu tisa au kumi na wawili lilikuwa na wajibu wa kumchagua mrithi wa mfalme na kumshauri. Gavana wa Mbata, ambaye alikuwa havezi kurithi ufalme, alikuwa mjumbe kutokana na wadhifa wake, na Lodi *Kabunga*, mkuu wa nchi, alikuwa na haki ya turufu. Washauri hawa wachaguzi, waliotoka nje ya ukoo wa kifalme, mara nyingi walithibitisha tu mizani ya madaraka iliyokuweco kwa kumchagua yule aliyekuwa na nguvu zaidi. Pia, wakati wa utawala, baraza la dola lililojumuisha pia watu wenye vyeo vikubwa, lilikuwa na haki ya kumsimamia mfalme, hasa katika mambo ya vita, kuchagua na kufukuza magavana na biashara (ufunguaji wa njia za biashara).

Dola lilisimamia utoaji wa simbi na ulipaji mishahara. Biashara iliendelea katika vifaa vya chuma na vya kufinyanga, mikeka, vikapu na chumvi, na pia katika bidhaa za msingi kama vile shaba nyekundu, mapambo ya pembe, vitambaa na kadhalika. Hakukuwa na desturi ya ubobezi katika sanaa ya aina moja tu, ila ucyeyushaji wa chuma na shughuli za usukaji wa majamvi zilifanywa na makabaila tu.


Simbi zilifika kwa kupitia njia inayoanzia Luanda: chumvi ya baharini, samaki, vifaa vya kufinyanga na vya henzirani kutoka Bas Zaire; shaba nyekundu ilitokea Bamba na kadhalika. Ni habari chache tu zinajulikana kuhusu watu walio wengi katika jamii. Mfumo wa nasaba ya kuukeni hauonyeshwi kwa uwazi. Kwa mfano,

kwenye jina la mfalme wa kwanza mlikuwemo jina linalomnasibisha na baba yake na jingine linalomnasibisha na baba wa mama yake. Jamii iligawanywa katika daraja tatu: makabaila waliooana wenyewe kwa wenyewe, watu luru na watumwa. Ndoa ziliimarisha ushirikiano kati ya koo. Mabwana wa zamani wa nchi (*kitomi*) walikuwa sehemu ya makabaila.

Hitimisho

Jambo kuu la kwanza linalojitokeza katika mapitio haya ya historia ya Afrika ya Ikweta tangu karne ya kumi na mbili hadi ya kumi na sita, ni mchango muhimu wa msitu katika maendeleo ya teknolojia (kufua vyuma) na mifumo ya kijamii, ikiwemo mifumo ya dola, vitu viwili hivi vikiwa vimefungamana. Ingawa mchango huu haukuwa wa pkee (kwa mfano tunafikiria mchango wa mwanzo wa kituo cha mapema kabisa cha Luba), kwa jinsi ulivyopotoshwa kwa muda mrefu imebidi sasa usisitizwe.

Lakini bado kumbaki maeneo makubwa yaliyo kizani ambayo utafiti wa isimu na akiolojia utayapa mwangaza.



*Kusini mwa Afrika:
Watu wake
na Muundo wa Jamii*

*Uandikaji wa historia na tatizo la vyanzo vya taarifa**

Siasa ya ubaguzi wa rangi ya Afrika Kusini ya hivi sasa imezuia kupatikana kwa taarifa sahihi kuhusu Afrika ya nyakati za kale. Historia, kama mali zote za thamani na amali zote za jamii, pia ilihifadhiwa kwa ajili ya weupe wachache. Ule mwelekeo wa kushughulikia historia ya watawala weupe walio wachache umeimarishwa na msimamao mkali uliochukuliwa na vyyo vikuu vya Afrika Kusini na wachapishaji wa Afrika Kusini kwa jumla ambao wanakataa kukubali uthabiti wa taarifa zisizoandikwa katika kuiunda upya historia (UNESCO 1980).

Sayansi kama vile akiolojia, anthropolojia na isimu hazikubaliwi kama chimbuko la taarifa za kihistoria, na ni historia ya watu weupe tu, ambayo ipo katika taarifa za kimaandishi, ndiyo inayostahiki kushughulikiwa. Vile vile chimbuko la taarifa za Kireno limepuuzwa makusudi na kwa dhati. Mapokeo ya mdomo yamepuuzwa na hata baadhi ya chimbuko za maandishi zimeachwa kando kwa sababu ya siasa ya ubaguzi wa rangi. Kwa ufupi, Waafrika wamecondolewa katika historia ya watu weupe, ambayo inaonyesha tangu nyakati zilizopita ile itikadi ya utawala wa watu weupe. Juu ya haya yote, uhuru wa Angola na Msumbiji, pia ule wa Zimbabwe mwaka 1980, umefungua mawanda mapana ya utafiti.

Hali ya maarifa

Matatizo mawili yanautawala utafiti wa kihistoria: kwanza ni ile tarehe ambayo jamii mbali mbali zilifanya makazi yao huko, yaani uhamiaji, na pili, miundo ya madaraka. Kwanza kabisa lazima tusisitize kwamba ni zama gani Wakhoikhoi

*Tanbihi ya UNESCO: Mtini haya yaliandikwa kabla ya kufutwa kwa siasa ya ubaguzi wa rangi huko Afrika Kusini, hivyo hayazingatii mageuzi yaliyotokea katika historiografia ya Afrika Kusini tangu 1994.

walilikalia jimbo hili. Zama za Chuma za Awali, ambazo ziliamalizika karibu na mwaka 1100, zilianza kiasi cha karne moja kabla ya Enzi ya Ukristo katika eneo lililoko baina ya Zambezi na Limpopo. Huko Lydenburg, katika Transvaal, vichwa vya vyombo vya kufinyanga vimefukuliwa pamoja na ushahidi wa kuwepo shughuli za kilimo.

Karibu na mwaka 1100, Zama za Chuma za Kati zilianza. Kikundi cha watafiti kikiwa na mwanaisimu Ehret kilitumia mkusanyiko wa maneno 90 kuchunguza uwiano kati ya vikundi viwili vya lugha katika jimbo hili: lahaja za Kishona na lahaja za Kisotho, Kinguni, Kivenda na nyinginezo. Wazungumzaji wa Kishona inasemekana walifanya maskani mahali ambapo sasa ni Zimbabwe, ambapo watu wa kundi la pili walilikalia eneo la kusini zaidi.

Baina ya mwaka 1000 na 1500 kulitokea maendeleo muhimu: Wakhoikhoi waligetika kuwa wachungaji na kutawanyika kwenye eneo kubwa sana. Mila maalum zilijitokeza zilizowanasisibisha Wasotho, Watswana na Wanguni kwenye takriban mwaka 1500, waliosema lugha ya Kibantu.

Mabadiliko haya yaliathiri sana maisha ya jamii za wavuvi wa schemu za mwambao wa Atlantiki na wachungaji karibu na Rasi. Kwa vile ushahidi wa maandishi au simulizi kwa kipindi hiki ni adimu kabisa kupatikana, ni muhimu kukusanya na kuzipanga kwa wingi izezekanavyo taarifa kama vile za kiakiolojia, anthropolojia linganishi na isimu. Hasa tunahitaji kuudurusu msamiati wa Kinguni na Kisotho cha awali na kuchunguza maneno ya mkopo ya Kikhoisan katika lugha za Kibantu na kinyume chake.

Kuibuka kwa lugha za Kibantu za upande wa kusini

Utafiti wa isimu wa karibuni kabisa umeonyesha kwamba Kishona na lahaja za Kibantu za kusini-mashariki ni vijikundi maalum chini ya kundi la lugha ileile. Uwiano wenye nguvu kabisa ni kati ya Kivenda na Kishona (asilimia 55), halafu kati ya Kitsonga na Kishona (asilimia 41) zikifuatiwa na Kichopi (asilimia 38), Kisotho (asilimia 37) na Kinguni (asilimia 35).

Kishona, kwa upande mmoja, na zile lugha nyingine kwa upande mwingine, zilikuwa ndio vitovu vya kuenezea lugha za kibantu upesi upesi kupitia kusini mashariki:- Kisotho, Kichopi na Kitsonga, kwa mfano, zikitumika kwenye bonde la chini la Limpopo, wakati Kinguni na Kisotho-Tswana zimeenea sana katika miteremko yote miwili ya Drakensberg. Kutofautiana kwa vikundi vya lugha ya Kisotho na ya Kinguni ni wa karibu zaidi kuliko kutofautiana kwa lugha nyinginezo. Utofauti huu, ambao unaakisi au kushawishi mtindo maalum wa makazi, ulikwishanza kutokea kati ya mwaka 1500 na mwaka 1600, jambo ambalo litakubaliana na mapokeo ya mdomo yanayoelezea nasabu zinazorejca nyuma mpaka karne ya kumi na tano na kumi na sita.

Nadharia inayokubalika sana iliunganisha upanuzi wa Wabantu na ule wa kilimo na ufuaji vyuma mwanzoni mwa kipindi cha Kikristo. Kwa kweli hakuna uhakika kama kila pahala Wabantu walileta mbinu na zana mpya na bora za kilimo, bali walileta mabadiliko yaliyosaidia kukua kwa uchumi na idadi ya watu na pia makazi ya aina mpya. Kwa hiyo hakukuwa na mapinduzi makubwa sana ya kihistoria bali kujipenyezapenyeza tu kulikoendelea kwa mfululizo.

Washona, Wavenda na Watsonga na lugha zao wanaelekea waliishi bega kwa bega kwa muda mrefu katika jimbo baina ya Zambezi na Limpopo; hii inaweza kuelezea kule kushabihiana kwingi kwa desturi za kijamii (kurithi upande wa kuumeni, kutahiri, na ndoa ya mitala). Pia Wanguni ndio kabila pekee lisilo na vizimu vya ukoo.

Kaskazini mwa Ukhahlamba

Huko Olefantspoort, Melville Koppies na Platberg, kulipatikana meno ya ng'ombe, kondoo na mbuzi, vifaa vya chuma, na mbegu za mtama za Zama za Kati za Chuma ambavyo bila ya shaka ni vya Wasotho-Tswana. Pahala pekee ambapo daraja mbali mbali za maendeleo ya pole pole ya Zama za Awali za Chuma zinaonekana kwa wazi ni kule Eiland katika Transvaal ya kati ambako chumvi ilichimbuliwa katika kipindi chote hiki. Kuanzia karne ya kumi na moja, vifaa vya kufinyanga vya Zama za Chuma za Awali vilipotewa na kuvipisha vifaa vya Mapungubwe na baadaye vifinyange vya Phalaborwa.

Sehemu hii ilikuwa miongoni mwa vituo vikubwa vya kuzalisha shaba nyekundu vya Transvaal wakati luo. Sehemu hii ipo karibu na kijito cha mto Limpopo kütwacho Olifants, ambacho Vasco da Gama alikiita "mto wa shaba" mwaka 1498. Shughuli za uchimbaji migodi ziliendelea hapo angalao tangu karne ya nane. Mtindo wa vifaa vya kufinyanga ni kama ule wa Walobedu masafa kidogo upande wa kaskazini; Walobedu waliweza kutofautishwa hasa kutokana na malkia wao wa mvua.

Katika mabadiliko yaliyotokea katika jimbo hili, inaonekana kwamba wachimba migodi na wafinyanzi wa kienyeji, ambao pia walikuwa wafanya biashara, waliweza kudumisha mtindo wa jadi wa maisha; labda walikuwa Wasonghai ambao ilibidi kupambana na washambuliaji wa Kivenda.

Kwa ufupi, baina ya mwaka 1100 na mwaka 1500 katika nyika za chini za Transvaal, wakazi wa makazi ya kilimo lazima waliendesha biashara kati yao na kubadilishana bidhaa zao za sanaa za ufundi. Migodi ya Phalaborwa ilikuwa chimbuko la vifaa vya chuma katika mzingo wa kilometa dazeni chache, na pia chimbuko la shaba nyekundu kwa masafa makubwa zaidi, kufikia Limpopo na sehemu za mwambao. Ufuaji wa vyuma na biashara huenda zikawa ndizo

zilizosababisha kuweko kwa tawala kubwa za kwanza za machifu, ambazo ziligongana na tawala jirani za machifu na makundi ya wawindaji wazururaji hadi karne ya kumi na saba, wakati zilipomezwa katika ufalme mmoja wa Wavenda.

Kaskazini mwa Vaal, karibu na Johannesburg, zimekutwa dalili za vijiji ambavyo majumba yake ya duara yalikuwa na majukwaa na sakafu za plasta, wakati kuta zilikuwa za zana zisizodumu, nyumba zote zilijengwa kuzunguka nafasi yenye umbo la yai au duara ambayo labda ilikuwa zizi la ng'ombe.

Makazi ya aina hii yalitangulia ujenzi wa kutumia mawe ambao ulianza karne ya kumi na tano au kumi na sita. Sehemu za aina hii kaskazini na kusini kando ya mto wa Vaal ya juu kufikia Drakensberg, katika eneo linalopata mvua nyingi na lenye nyasi zilizostawi, zenye majumba, ghala za nafaka na mazizi ya ng'ombe na kuzungushiwa ukuta, ni ushahidi wa uchumi uliochanganya ukulima na ufugaji.

Kama makazi ya kabla, na yale ya wakati wa ujenzi wa kutumia mawe yanaweza kunasibishwa na mfumo wa maisha ya Wasotho, kama ilivyosemwa, na kama baadhi ya mitindo ya ufinyanzi katika vijiji hivi inaweza kunasibishwa na vikundi vya Kitswana, ni masuala yanayohitaji kufanyiwa utafiti hapo baadaye.

Asili ya ujenzi wa majumba ya mawe huenda ikawa ya kienyeji, kwa mfano kwenye maeneo ambamo malisho ni mazuri lakini mbao ni adimu, au yanaweza kuwa yameigizwa kutoka majumba yaliyojengwa na watawala katika jimbo la Zambezi.

Sehemu za makazi kaskazini mwa Drakensberg zinaonyesha mabadiliko makubwa baada ya mwaka 1100, pamoja na kuongezeka kwa ukubwa wa makazi na kuongezeka kwa mchango wa ufugaji ng'ombe katika uchumi. Hali hii iliyopelekea kuanzishwa kwa madola mbali mbali katika karne ya kumi na sita.

Botswana inatoa muhtasari mzuri zaidi wa maendeleo katika kipindi hiki hiki. Huko zaidi ya sehemu 150 zimechimbuliwa, kuanzia mwaka 800 mpaka mwaka 1800, ambazo zinaonyesha maendeleo katika ufanyanzi wa vifaa vya Kigokomere (Zama za Chuma za Awali). Sehemu hizi zina ushahidi wa ufugaji mkubwa wa ng'ombe, jambo ambalo halishangazi, hasa ukizingatia malisho matamu na majani ya aina ya *mopane* yanayoifunika mbuga hii. Ni hapa, na wala sio Natal, ambapo inaonekana kuwa kuzaliana kwingi kwa mifugo kumetokea. Baada ya mwaka 1000, kuna ushahidi mehache wa kuweko kwa biashara kati ya sehemu hizi na mwambao wa Afrika Mashariki, labda kwa sababu Zimbabwe ilikuwa inaanza kudhibiti biashara yote ya ndani. Baada ya mwaka 1300, idadi ya makazi sehemu hizi ilizidi kupungua labda kwa sababu ya kunyemelewa na jangwa (Kalahari haikuwa mbali), au kwa sababu ya kusogea kwa ukanda wa mbung'o.

Kwa upande mwingine, huu ulikuwa wakati wa kuongezeka kwa idadi ya watu kwenye sehemu za magharibi za Transvaal, karibu na Vaal, na ushahidi wa ufugaji

kabambe wa ng'ombe huko; labda kwa sababu ya uhamiaji wa makundi ya watu uliotajwa hapo juu, au watu walikuwa wanavutiwa na mila za kijamii zilizohusishwa na ufugaji ng'ombe, kama vile *lobola* (mahari yanayolipwa kwa ng'ombe) na mikataba ya uteja kwa ajili ya ng'ombe. Pamoja na ulipaji wa kodi kwa njia ya kutoa ng'ombe, mila hizi ni sifa hasa za utamaduni wa Wasotho na Watswana wa baadaye. Ukamuaji wa maziwa umelekea kuwa umeanza baada ya kuvuka hiyo Vaal.

Kusini mwa Ukhalilamba


Huko kusini mwa Drakensberg, ambayo sasa inakaliwa na Wanguni ambao maisha yao yanategemea ng'ombe, sehemu nyingi zinathibitisha athari za Zama za Chuma za Baadaye.

Huko Blackburn, karibu na Durban, nyumba zilizojengwa kwa plani ya msonge zenye fremu ambazo labda zilitengenezwa kwa matawi ya miti na mapaa yaliyoczekwa kwa nyasi ambamo vipande vya chuma, mifupa ya wanyama wa kuwinda na miiba michache ya samaki imepatikana, ni vitu ambavyo vinaonyesha moja kwa moja mfumo wa maisha ya Kinguni, isipokuwa ule mwiko wa kula samaki miongoni mwa Wanguni. Lakini labda mwiko huu ulianza na kuendelea baada ya karne ya kumi na moja, au masalia haya yalikuwa ya wawindaji Wakhoikhoi wa pwani. Makazi ya Park Moor yameanza karne ya kumi na tatu au kumi na nne. Kwa vile yalikuwa kwenye rasi na kuzungukwa na ukuta, yalikuwa pahala madhubuti pa kujilinda.

Pasi na kutarajiwa, ramani ya sakafu inaonekana kuwa ya mstatili. Wukazi walitumia chuma, waliwinda wanyama na kufuga ng'ombe. Mbali ya sakafu za mstatili, mahala hapa panakubaliana zaidi na shughuli za Wanguni.

Mkusanyiko wa mwisho wa makazi umepatikana Transkei, na umehusisha kila kipindi cha Zama za Chuma. Lakini kwa mujibu wa mapokeo ya mdomo hadi kufikia karne ya kumi na tano, Transkei ilikaliwa na Wakhosa wakiwa katiku tawala ndogo ndogo za kiekifu.

Kufika mwaka 1500, Wanguni walikwishakalia eneo lote ambamo walikuwa wakiishi katika mwaka 1800, ingawa katika sehemu za magharibi walichanganyika na Wakhoikhoi ambao kidogo kidogo waliwameza. Wakhoikhoi nao waliacha athari kubwa katika lugha za Kinguni za mashariki na magharibi, ingawa athari hii ilikuja baadaye, baada ya mwaka 1600, yaani baada ya mkusanyiko wa lugha za Kikhosa na Kizulu kuanza kugawanyika. Kwa vile taathira ya Kikhoikhoi juu ya Kizulu ilikuwa asilimia 14 na juu ya Kikhosa asilimia 20 ya misamiati ya lugha mbili hizi, taathira za Kikhoikhoi ziliubadilisha mfumo wa fonctiki ya Kikhosa. Wakhoikhoi



23.1 Maeneo ya kiakalojia ya kusini mwa Afrika 1100-1500 (J. Vansina)

lazima walizikalia sehemu za ardhi ndani kabisa za Natal, maana hata lugha za Kinguni za mashariki kabisa ziliathiriwa.

Ile hali ya ufugaji kutawala kilimo miongoni mwa Wanguni ilikuwa ni matokeo ya athari ya Kikhoikhoi, ingawa ng'ombe wa Kisanga wa Wanguni walitofautiana na aina ya ng'ombe wa Afrika Kusini wa Wakhoikhoi; hawa Wakhoikhoi pia waliyafundisha makabila mengi kukamua wanyama maziwa, na waliwafundisha Wakhosa kutumia mafahali kubebea mizigo.

Mwishoni, Wakhoikhoi waliwaathiri pia Wakhosa katika mambo ya kidini, katika mpango wa makazi na katika desturi ya kunyofoa sehemu ya kidole kidogo.


Wanguni wa leo ni mchanganyiko wa "Wanegro" na Wakhoikhoi. Kuwoko huku kwa idadi kubwa ya jeni (viini vya urithi) ya aina moja pia kunajitokeza kati ya Wakhoikhoi na Watswana. Ukichukuliwa ushahidi wa kiisimu na wa kibiolojia kwa pamoja, lazima mtu afikie hitimisho kwamba ama wakati fulani Wakhoikhoi wengi walikuwa na mahusiano ya karibu na Wanguni huko Natal au kabla ya kuhamia katika jimbo hili. Kwa ufupi athari ya Wakhoikhoi juu ya historia ya watu wa sehemu za kusini za Afrika ilikuwa kubwa zaidi kuliko wanahistoria walivyokiri mpaka sasa.

Wakhoikhoi

Haiba ya Wakhoikhoi ilijitokeza tangu mwanzo wa kukutana kwao na Wareno walioongozwa na Bartholomew Dias mwaka 1488 na Vasco da Gama mwaka 1497. Katika mwaka 1510 waliwaua Wareno sitini (akiwemo Don Francis D'Almeida, Mwakilishi — Mtawala wa India), katika mapigano ya Table Bay, ingawa Wareno walikuwa na bunduki. Karne moja na nusu baadaye, Waholanzi, wakiwa na hamu ya kujipatia jimbo la Rasi (Cape), walianza kuwauwa wenyepi. Kikhoikhoi, katika lahaja zake mbalimbali kilikuwa miongoni mwa lugha ziliyozungumzwa zaidi ya nyingine katika jimbo lililoanzia Namibia Kaskazini mpaka kwenye Ras, na upande wa mashariki, katika vipindi fulani, mpaka Natal.

Umoja huu wa kiisimu au lugha unaonyesha kwamba kutawanyika kwa Wakhoikhoi ni kwa hivi karibuni na kwamba kulitokea haraka. Walifuga ng'ombe na kondoo wenye mikia minene, na walipanda ng'ombe ambao pia walibebeshwa vitu vyao pamoja na boriti kwa ajili ya nyumba zao. Hii iliwapa uwezo mkubwa wa kusafiri, jambo ambalo linaclezea kule kusambaa kwa lugha yao. Lugha hii imo katika kundi la "Kikhoisan"¹ walilomo wao wenyewe kwa upande wa sifa za maumbo yao, licha ya tofauti chache kutokana na kutumia maziwa katika chakula chao. Wareno walipofika, Wakhoikhoi tayari walikuwa wapo kwenye eneo la Rasi.

¹ Khoisan ni sawa na makundi mawili ambayo awali yaliitwa Hottentot na Bushinan



23.2 Upanukaji wa Wakhoikhoi (J. Vansina)

Walikuwa wamekwishajipatia ng'ombe kwa wingi huko Botswana ya kaskazini, wamekwisha acha kuwinda na kukusanya, wamekwisha jifunza ufuaji lakini siyo uyeyushaji wa metali. Kupungua kwa idadi ya watu huko Botswana baada ya mwaka 1300 kunaonekana kusadifiana na kuhama kwa makundi makubwa siyo tu ya wale waliozungumza Kibantu bali pia Wakhoikhoi.

Wakifuata mabonde kwa kiasi walichoweza, Wakhoikhoi walikwenda upande wa kusini mpaka kufikia makutano ya Mto Vaal na Mto Orange. Kutoka hapa tawi moja lilielekea magharibi na kuingia Namibia na la pili kuendelea upande wa kusini na kugawanyika katika matawi mawili, moja likaelkea magharibi na kuingia kwenye sehemu za malisho mazuri kabisa kwenye enco la Rasi. Ni kweli kwamba masalia ya karne ya kumi na moja yamegunduliwa huko Middledrift, pamoja na mabaki ya ng'ombe, vifaa vya kufinyanga na zana za mawe, ingawa hakukuwa na alama ya chuma. Ikiwa Middledrift ni makazi ya Wakhoikhoi, ile nadharia iliyoenezewa hapo juu kuhusu uhamaji haiwezi tena kufaa. Lakini masalia haya yanaweza sana kuwa yametokana na wawindaji wa zamani zaidi waiokwishajipatia ng'ombe.

Ueneaji wa Wakhoikhoi uliathiri sana maisha ya wakazi wote wa Afrika ya Kusini. Ile dhana kuwa Wanguni hawakuwakuta Wakhoikhoi huko Natal ili uwongo. Kinyume cha haya, inaelekea kwamba Wakhoikhoi waliwatawala wakulima waliowakuta huko Transkei na Natal. Ilikuwa baadaye ndipo mizani ya mamlaka ilipobadilika na kuwa upande wa Wakhosa, hasa katika karne ya kumi na sita. Upande wa magharibi pia, Waherero walikalia sehemu za mbali zaidi upande wa kaskazini na bila kutumia lugha ya Wakhoikhoi, waliiga mtindo wa maisha ya Kikhoikhoi wa ufugaji na utaratibu wao wa kiukoo. Ng'ombe wao walipoongezeka, waliunda tawala kubwa zaidi za kisiasa chini ya uongozi wa machifu wa kurithi, zenye mfumo wa kodi, walau ilipofikia karne ya kumi na saba. Msisimko fulani wa mabadiliko uliathiri jamii ya Kikhoikhoi. Kwa mfano, ingawa uongozi wa kisiasa ulinasibishwa na utajiri wa binafsi, lakini mfumo wa urithi na mfumo wa kuchukua nasaba kuukeni uliwapa warithi sehemu tu ya mali hiyo. Kwa hivyo mabadiliko ya kipato yaliweza kutokea; na wakati wa mwambo baadhi ya watu walirjea maisha ya kuwinda na kusanya. Lakini ushirika wa watu maskini uliweza kukamata makundi makubwa ya mifugo na kujipatia uongozi wa jamii. Nyakati za neema, hali ilitulia zaidi, lakini palipotokezea ukame au milipuko ya maradhi fulani, wizi wa ng'ombe na mizozo vilishamiri. Kwa hivyo, wakati Wakhoikhoi hapo wanzoni waliwapiku wakulima kutokana na wepesi wao wa kuhamahama na namna alivyoji -cndesha, mwishoni, mabadiliko ya hali ya hewa na mngongano ya wenyewe kwa wenyewe yaliwanufaisha wakulima, walau katika majimbo ya mashariki. Kuweko kwa Wakhoikhoi pia kulileta machafuko pia kwa wawindaji wenyewe na wafugaji

kondoo ambao walikuwa wakiwania raslimali ileile. Wafuga kondoo walinyang'anywa mali yao na Wakhoikhoi au kuwekwa kwenye daraja la uteja. Hali kama hiyo iliwakumba wawindaji wa sehemu ya mwambao. Lakini wawindaji wa sehemu za ndani waliowaona Wakhoikhoi kama majangili, wakati wao wenyewe wakionekana kama ni majambazi, walijitetea kwa kipindi kirefu. Waliweza kudhibitiwa nyakati za kawaida, lakini alifaulu tena mara tu hali ya mazingira ilipokuwa mbaya, jambo ambalo lilikuza idadi yao, kwani Wakhoikhoi waliofukarika na kurejea maisha ya uwindaji walijiunga nao. Lakini maisha ya Kikhoikhoi yalianza kidogo kidogo kutawala na ilipofika karne ya kumi na saba lugha yao ilikwishakuwa lugha ya mawasiliano ya eneo zima la Rasi.

Hitimisho

Mambo mawili makuu yanajitokeza: kuenea kwa lugha ya Kibantu na kupanuka kwa Wakhoikhoi kutoka Botswana. Kuanzia Zimbabwe na katika mbuga ya juu, wakulima wa jamii ya Wasotho na Watswana wa kale walianzisha tawala za kichifu sehemu ya kaskazini ya Drakensberg. Wanguni walipokutana na Wakhoikhoi walijikita zaidi katika ufugaji wa ng'ombe. Lakini lini waliachana na Wasotho na kuuvuka mto wa Limpopo ni jambo ambalo mpuka sasa limo kizani. Pia ni shida kuelewa kwa nini, baina ya kama mwaka 800 na mwaka 1000 maisha ya ufugaji yalitia mizizi huko kaskazini mwa Botswana. Maendeleo haya hayaonekani kwamba yalikuwa kazi ya wale wanaotumia lugha ya Kibantu, kwani lugha zao zina uchache wa msamiati wa ufugaji wa ng'ombe; aidha, hayukutokana na wale wanaodhaniwa kuwa ni wahamiaji kutoka Sudan ya Kati. Inafaa zaidi kuwafikiria wahenga wa Wakhoikhoi wenyewe ambao, kwa zaidi ya miaka mia tano, waliukamilisha ustaarabu wao bila ya kuzitupa kabisa mila zao za kinomadi na uwindaji.

24

*Bukini na visiwa vya
jirani kuanzia karne ya kumi
na mbili hadi kumi na sita.*

Makundi muhimu ya watu yanayounda jamii ya watu wa Bukini yalikuwapo tayari kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na mbili, ingawa mawimbi ya uhamaji yaliendelea hadi karne ya kumi na sita. Matukio haya yalitokea katika kiunzi cha jumla cha "malusiano ya kihistoria katika Bahari ya Hindi." Tatizo kubwa katika kipindi kinachozungumziwa katika sura hii ni mabadiliko ya polepole na changamano ya mwingiliano wa kibiolojia na kitamaduni wa jamii miongoni mwa Waafrika, Waarabu na Waindonesia ambao hadi karne ya kumi na sita ulishazaa utambulisho asilia wa Kisiwa hiki kikubwa. Huenda vita vilivyoelezwa katika mapokeo baina ya wageni na *Wazimba* ni migongano kati ya wahamiaji kama vile Wamerina na wenyeji ambao yaelekea walikuwa ni Waafrika kwa asili na kwa hivyo waliitwa "wahenga" (*Vazimba*).


Kwa upande wa wahamiaji Waarabu kuna nyaraka zilizoandikwa kwa lugha ya Kiantemoro lakini kwa herufi za Kiarabu zinazoitwa *sorabe*.

Lakini falme ambazo Wareno walipofika walikuta tayari zimeshaanzishwa katika karne ya kumi na sita ziliundwa kwa mchakato gani? Ingawa Waindonesia waliofika baadaye zaidi waliehangia katika kuzipanga kwa namna imara zaidi, ni wazi kwamba wakati walipofika tayari kisiwa kilishajipanga katika makundi makubwa makubwa ya kitemi na luenda kwa msingi wa wakazi wake wa zamani zaidi, Waafrika na Waarabu.

Chimbuko la falme

Mapokeo kuhusu *Wazimba* yamefasiliwa visivyo kuwa ni ya kugombanisha wageni washindi na wastaarabishaji kutoka ng'ambo ya bahari dhidi ya wenyeji, ambao hawakuwa wamejitayarisha, hasa kama inavyoonyesha taarifa ya Watsileo kwamba walitcua watemi tu wakati wa vita.

Nadharia tete kuhusu asili ni nyingi na zenye kupingana. Ottino anasisitiza mchango wa Waindonesia upande wa utamaduni. Mchango uliohusu maisha ya



24.1 **M** Bukini: mikondo ya uhamaji na kuenea kwa watu.
 Chanzo: F. Essoavelomandroso kwa kushirikiana na T. Rajaona, wakitumia taarifa kutoka katika Atlas de Madagascar ya S. --- Ayache (pl. 20 na 20 bis) na Atlas de peuplement de Madagascar ya F. Ramiandrasoa.

Tanbihi: Mawimbi ya mwisho ya uhamaji wa Waindonesia yalitokea kati ya karne ya kumi na mbili na kumi na tatu. Watu walilosilimishwa (Waswahili na Waarabu) walikuwa na makazi yao makuu katika Visiwa vya Ngazija; kutoka hapo walikizunguka kisiwa kwa kaskazini.

umma ulitokana na wahamiaji na jadi ya Kimalay Kipolinesia na wakati vipengere vya ukabaila na dola viliingizwa katika karne ya kumi na mbili na Uhindu wa Kiindonesia, kama inavyoweza kuonekana kwa kulinganisha sherehe za nasaba tawala za Imerina na zile za majimbo ya watu wanaoishi Kihindu ya Insulindia (Indonesia). Hata hivyo, I. Lombard anaona kwamba uundwaji wa tawala kubwa za kisiasa katika jimbo hili umesaidiwa na makundi yaliyokuwa na athari za Kiarabu yaliyofika kusini na magharibi.

Kwa maneno mengine, jinsi mwingiliano wa kibiolojia na kitamaduni na vilevile wa kisiasa ambao unajionyesha katika athari za Uislamu juu ya taasisi za Imerina ulivyochimbuka haijitokezi waziwazi.

Kwa upande wake, J.P. Domeni chini anasisitiza mchango wa Waafrika. Kwa mfano, iwapo mtu atachanganua talasimu za sihiri au *sampy* walizotumia wafalme ili kuendesha utawala wao, inaweza kufahamika kuwa idadi ndogo tu (tatu kati ya kumi na nne) ni kutoka kusini mashariki, eneo kuu la athari za Kiislamu. Aidha, Ottino anatambua kuwapo kwa falme ndogo ndogo ambazo hazikuwa na kanuni bayana za kurithishana uongozi kabla ya kufika Maroserana. Zaidi ya hayo, anabainisha kati ya falme kabla ya Sakalava ambazo zilikuwa ni juhudi za wahamiaji wa mwanzo wakulima, ambao walikuwa "Wabantu wanaojinasibisha kuukeni"; na falme za Sakalava zilizoundwa na Wabantu wafugaji wanaojinasibisha kuumeni: ni dhahiri kuwa, lazima kisiwa kilipata taathira ya muundo wa kisiasa wa awali uliokuwa ukitumika katika bara jirani.

Lililo muhimu zaidi ya yote ni kubainisha na kufuatilia kwa kipindi kirefu kilichopita michango mbalimbali iliyoishia katika kuunda haiba ya Wamalagasi, ambayo bila shaka ni ya mchanganyiko. Hali hii inahitaji kuitafakari kwa kuzingatia mapokeo ya kitamaduni kuliko taifa au kundi moja moja. Kwa mfano, Raminia, mwanzilishi wa ufalme uliosilimishwa wa kusini-mashariki lazima alitoka kusini magharibi mwa India; na huenda koo tawala za Maroserana na Andrevola zina asili ya Kihindi-Kiarabu. Falme zinazofahamika hivyo hasa zilikuwapo baada ya karne ya kumi na mbili, ingawa mapema zaidi, shirikisho za kitawala msonge za koo tayari zilishaunda temi kubwa.

Hata hivyo, maingiliano ya uhamaji wa ndani yanasababisha ugumu zaidi katika kufafanua majukumu ya kuyapa makundi mbalimbali yanaohusika (kuhusu suala hili, tazama juzuu la III la *Historia Kuu ya Afrika*).

Kuzaliwa kwa ufalme wa Merina

Leo hii nyanda za juu zinakaliwa na Wamerina, Wabetsileo na Wabezanozano, ambao huenda wote wana asili moja; lakini Wamerina wanaunda kundi la watawala, ambalo inadaiwa mhenga wake, Andriantomaza, alifika katika ghuba ya Antongil

moja kwa moja kutoka kusini mashariki mwa Asia, au baada ya kuishi katika bara la Afrika na Visiwa vya Ngazija. Uhamaji polepole wa makundi haya hadi katika nyanda za juu, uliosukumwa na ujio wa makundi madogo madogo ya Waasia katika kipindi cha karne kadha ulikamilika mnamo karne ya kumi na tano. Njia hizi mbalimbali zinafahamika kutokana na makazi walipoishi watu ambayo sasa tayari yametambuliwa.

Nyaraka za Waarabu na Wareno zinathibitisha kuchelewa kufika wahamiaji hawa ambako vilevile kunatajwa katika mapokeo ya Wabetsileo, pamoja na kupanda kwa wahenga wao wa kinasaba, Waiarivo kutoka pwani kuelekea vyanzo vya mto wa Mahatasira.

Kwa kweli hapakuwa na wimbi la utekaji. Kulikuwa na kipindi kirefu ambapo waliishi kwa amani ihyounganisha jamii mbili hizi pamoja. Ni baada ya vipindi viwili vya utawala, ikiwa ni pamoja na kile cha Andriamanelo, wageni walipoanzisha vita dhidi ya wenyeji wao.

Idadi ndogo ya watu iliyokuwapo katika maeneo makubwa ya misitu ilisaidia watu kuishi kwa ujirani mwema usio na migongano na kuoleana kwa kiasi kikubwa hivyo kwamba, katika baadhi ya hadithi hali hiyo inaendelea bila kukoma kuanzia nasaba iliyojulikana kuwa ni ya wafalme wa *Wazimba* (yenye utambulisho wa Ubantu) hadi nasaba ya wafalme wa Merina. Matokco yake ni kwamba wafalme hawa wa baadaye waliweza kujiwasilisha kama warithi halali wa wale waliotangulia. Hivyo inawezekana kwamba wageni walikuta muundo wa dola ambao hapo mwanzo walishirikia na nao na baadaye wakauchakua na kuurckebisha. Migongano ya baadaye baina ya wenye nchi au *tampon-tany* na wageni kuhusu mgawanyo wa ardhi nzuri ilikuwa mikali. Inasemekana kuwa mfalme Andriamanelo alishinda kwa sababu askari wake walikuwa na silaha za chuuna, na "wenye nchi" hawakujua matumizi ya metali hii. Kwa hakika yaelekea chuma kilingizwa Bukini kabla ya mwisho wa milenia ya kwanza enzi za Ukristo. Kwa hiyo kilichotokea ni kwamba washindi walijitwalia tu kitikadi uvumbuzi huu uliotokea mapema.

Kwa mujibu wa Hebert, baina ya wageni hawa na Wasakalava wenyeji, mahusiano ya utani (*ziva*) yalianzishwa, hali inayoonyesha mshikamano, na kubadilishana bidhaa na inatusi ya mizaha, mambo yanayotendeka katika schemu nyingi za Afrika kati ya wenyeji na wahamiaji. *Manazimba* maana yake ni "kutukana", urejeaji unaofanywa kwa asasi hii ukikumbusha Wazimba wenyeji ambao walikuwa wenye asili ya Kiafrika au mchanganyiko wa watu weusi na Waindonesia.

Mapokeo ya Wamerina na Wabatsileo yanaeleza kuhusu kukimbia kwa wenyeji walioshindwa kuelekea magharibi hadi jimbo la Manabe. Baada ya kutimuliwa

kutoka nyanda za juu, wazao wao Wasakalava bado wanakumbuka kisa hiki (kwa mfano miongoni mwa Wamikea katika jimbo la Tulcar). Lakini watu hawakuondoswa kabisa kabisa: wenyeji hawakukubali kukimbia tu waache makaburi ya mababu zao walioheshimiwa. Kusema kweli, kuwapo kwa ukoo wa Antehiroka, unaodai kuwa ni uzao wa Wazimba, katikati ya Imerina kunapingana kabisa na hoja hiyo. Wenyeji wengi walibaki: na Wamerina ambao haja yao ilikuwa kufikia maelewano na "wenye nchi" ili wapate upendeleo wa miungu yao ya "duniani", waliongeza mahusiano ya kuoana na wenyeji, ambao kwa upande wao waliona ni njia ya kushirikishwa na utawala mpya. Hivyo, kwa upande wa magharibi, ushirikiano baina ya wahamiaji na kundi la *tampon-tany* la Waandrambe ukawa chimbuko la mtawala wa kwanza wa nasaba ya kihistoria ya Andriambolamena. Huu ulikuwa ni ufalme wa Menabe. Falme nyingine ziliundwa katika mazingira ya kufanana na hayo na Wamerina, Wabetsileo na wengine. Aidha kulikuwa na michango ya Waislamu waliokuwapo katika jimbo kuanzia mapema sana katika karne ya tisa.

Uislamu katika Bukini na Visiwa vya Ngazija

Katika kuinukia kwa utamaduni wa Kiswahili wa safari za baharini katika pwani ya Afrika ya Mashariki (tazama sura ya 18), mahusiano yaliimarishwa kati ya pande mbili za Mlango Bahari wa Msumbiji. Walowezi wa Kiislamu walitamakani katika visiwa vya Ngazija. Hivyo kaskazini magharibi ya Bukini, kukiwa ni karibu na athari ya makundi haya ya Waislamu, kukapata aina ya utambulisho wa Kiswahili na Kikomoro, kutokana na mila na desturi za mabaharia, ambapo upande wa kisini mashariki ya kisiwa, kulikokuwa mbali na athari hizi, hakukuathirika. Kama ilivyo mahali pengine, napokeo ya kawaida kuhusu asili yenye maudhui yaliyojaa itikadi yanapatikana katika macneo haya. Hivyo *sorabe* za Antemoro zinaeleza ujio wa mhenga Ralitavaratra, katika karne ya kumi na tano, mwangalizi wa kumbukumbu takatifu zilizorithishwa na Musa na kutamaniwa sana na Sultani wa Makka. Baada ya masaibu mengi, aligundua "nchi ya ahadi" katika kingo za Mto Matitanana. Waantanosi vilevile wanaeleza kuhusu kufika kutoka Makka mhenga wao Raminia. Mapokeo ya Kingazija yanaeleza kufika Anzuani kundi la Waislamu wa Sunni katika karne ya kumi na nne ambalo lililazimishwa kuikumbia Ajemi. Ingawa sababu za kidini zinazohusu kakimbia huku ni za muhimu, baadaye zilibadilishwa na sababu mpya za vivutio vya kibiashara vya ulimwengu wa Waswahili ambavyo ni muhimu kuviingiza katika muundo wa safari za magharibi mwa Bahari ya Hindi. Hali hii ilisambaza watu, vitu na amali baina ya pwani ya Afrika, Visiwa vya Ngazija na Bukini.

Vituo vya biashara vya ulimwengu wa Waswahili

Shughuli nyingi za biashara zilizokwisha anzishwa miaka mingi iliyopita ziliunganisha miji na visiwa kuanzia Bukini hadi Sofala tangu zamani za kale. Bandari za Waswahili zinaelekea baharini na zilistawi sana tangu karne ya kumi na mbili na kuendelea, na zikawa ni vituo vya biashara kati ya Arabia na India kwa upande mmoja, na Visiwa vya Ngazija na Bukini kwa upande mwingine.

Waislamu wengi wahofika katika Kisiwa Kikuu walikuwa na utamaduni wa Kiswahili na mara nyingi walikuwa Waislamu weusi. Hivyo athari ya Afrika ilikuwa kubwa, kwa kuwa akiolojia imeonyesha kwamba miji mingi katika pwani ya kaskazini magharibi ilianzishwa na Waafrika, wala si Waarabu.

Kwa kweli kuna mnasaba kati ya vituo hivi vya biashara na miji ya Ngazija na ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na maboma yao, misikiti yao na milango iliyonakshiwa kwa ustadi katika Anzuani, Mutsamudu, Domoni, Sima, Mahilaka, Nosy Boina, Langany, n.k. Wareno wameacha maelezo ya kituo kilichotajwa mwisho yanayosisitiza kwaniba "misikiti yao na nyumba zao zilizo nyingi zinejengwa kwa mawe ya chokaa, zikiwa na roshani za mtindo wa Kilwa na Mombasa." Majahazi yalipakiwa mchele na vifaa vya mazishi vilivyotengenezwa kutokana na mawe laini kutoka Iharana; yalileta katika Kisiwa Kikuu lulu za India, nguo, kauri za China, na vifaa vingine vinavyopatikana katika miji ya Waswahili. Biashara hii iliendelea baada ya karne ya kumi na sita licha ya ushindani toka kwa wageni Wazungu.

Higawa Visiwa vya Ngazija, na hasa kisiwa cha Anzuani, huenda vilipokea wahamiaji Wabantu na Waindonesia, vilijaa makundi ya watu waliosilimishwa kutoka pwani ya mashariki ya Afrika, kila kundi likiwa hufika na mipango yake ya kurekebisha dini na kuihuisha. Kaskazini magharibi mwa Bukini, makundi ya wahamiaji yaliunda kundi la Antalaotse, mabwanyenye wafanyabiashara waliodhibiti madaraka ya kiuchumi na kidini katika vituo vya biashara.

Ustaarabu wa Kimalagasi kuanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita

Pamoja na mapokeo simulizi na maandishi, taarifa nyingi zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa wanaakiolojia, ambao kazi yao ndiyo sasa inanza.

Utamaduni wa vitu

Kilimo cha mpunga, migomba na kakao kilienca kisiwani baada ya karne ya kumi na

mbili. Wanyama wafugwao (ng'ombe na kuku) na viazi vikuu vilikuwa vya asili ya Afrika. Hakika, athari za Kiafrika zilitamalaki kusini, magharibi na sehemu za kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, ngalawa zilizosaidia wenyeji kuitawala bahari, na kilirno eha mpunga, vilikuwa na asili ya Indonesia. Bila shaka vielelezo vya kisiasa na kidini, ni matokeo ya mahusiano baina ya ruwaza za Kiafrika na Kiasia na michango ya Kiislamu.

Koo (*foko*, *troki* au *firazana*), zilizoongozwa na wazee au mzee mkuu, zilisumbuliwa na migongano mingi, iliyosababisha kuenea kwa koo zilizoshinda, na pia mtengano wa kisiasa.

Katika Visiwa vya Ngazija, *Wabeja* walishatoa nafasi kwa watemi wa kwanza waliosilimishwa, *Wafani*. Katika Kisiwa Kikuu, nasaba tawala za magharibi na kusini (Sakalava, Mahalafy, Zafimanara za jimbo la Androy) na zile za kusini mashariki (Zafiraminia wa jimbo la Anosy) zinaonekana kuwa zilihusiana. Mapokeo yanataja Wahamaji wa kutoka mashariki kwenda magharibi, waliotoka nchi ya Antemoro, na katika jimbo la Anosy na kukomea, kwa mfano, katika Menabe.

Ingawa ni vigumu kutenganisha athari za Kiafrika na za Kiindonesia, na hapa bila kuzungumzia zile zinazotokana na vuguvugu la maisha ya wenyeji, kwa kiasi kikubwa ni kweli kwamba madhchebu yanayozingira masalio ya wafalme waliokufa (*dady* katika nchi ya Sakalava) yametokana na mawasiliano kati ya ufalme wa Maroserana Volamena na himaya maarufu ya Mwenemutapa. Akipuza kisasili cha "wafalme weupe" wa asili ya Kiasia, Kent anathubutu kutoa nadharia tete kwamba Waandriana Merina ni watu wenye asili ya kuchanganyika mno, na hivyo kuwa mshabaha wa kibiolojia wa mseto wa kijamii-kisiasa wa wazawa ambao ndio walikuwa "wakuu na nchi" (*tampon-tany*) wenye asili ya Afrika, na wahamiaji waliosharabu Uarabu, Waindonesia na wageni wengine. Jambo jingine dhahiri ni kwamba, baada ya karne ya kumi na nne, dhana mpya zilingizwa, kama vile uundaji wa falme katika vitengo vya maeneo ya watu wa jamii moja.

Dini

Vilevile hapa kuna mchanganyiko dhahiri wa vipengere vya Kiafrika, Kiindonesia na Kiislamu. Katika jumla ya miungu yote iliyoabudiwa, nafasi ya kwanza imewekwa maalum kwa mungu wa asili ya Kiindonesia: Zanahary au Andriananitra (muungu aliyetiwa uturi). Aliumba dunia, akaunda jamii na akaweka mila na desturi. Lakini, kwa mujibu wa imani ya Kiafrika, mungu huyu yuko mbali sana, pote; walio karibu zaidi ni pepo (au majini) wa kila aina, kama vile pepo wa maji, misitu, walienga, Wazimba. Mara nyingi makafara ya nyati au ng'ombe yalitolewa kwao. Iwapo neno "mchawi" lina asili ya Kiasia (*inpamo sary*), hali halisi inakaribiana sana na

matendo ya Kiafrika. Mazishi ya maradufu ni mila ya Indonésia; na miongoni mwa Wabetsileo, wabeba jeneza hucheza kama watu waliopagawa, wakizunguka kwa mtindo wa zigizaga.

Kwa kumalizia, kipindi kinachoanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita kilikuwa awamu muhimu katika uundaji wa Wamalagasi kama walivyo leo. Kongamano la *UNESCO* kuhusu mahusiano ya kihistoria katika Bahari ya Hindi huko Port Louis (1974) yalifanikisha kutoa mwanga kuhusu vipengere kadhaa vya chimbuko changamano la Bukini, ambamo Afrika Arabia, India na Indonesia zimekutana, na kuupatia ulimwengu mfano wa kuisimua wa mchangamano wa kibiojia na kitamaduni, ambao kizazi chake ni chenye sura za kupendeza.

25

Mahusiano na Mabadilishano kati ya Majimbo Mbalimbali

Utangulizi

Afrika ilipata upendeleo katika mahusiano yake na mabara mengine, hasa na "Ulimwengu Mkongwe" baina ya 1100 na 1500. Mabara ya Ulaya na Asia yaliunganishwa pamoja na bara la Afrika kwa biashara iliyoshamiri kuvuka bahari za Hindi na Mediterania ambayo kwa kawaida iliendeshwa na Waislamu. Kwa kiasi kikubwa, hiki kilikuwa kiwango cha juu cha kiuchumi na kibiashara kabla ya kuanzishwa kwa biashara ya watumwa katika ulimwengu wa Magharibi.

Mawimbi makubwa ya mabadilishano ya kitamaduni yaliambatana na mawimbi ya biashara ambayo yaliathiri kila jimbo, bila kujali vizuizi vya misitu wala majangwa.

Sahara na Sahel: maeneo yaliyopendelewa katika mahusiano ya nje

Kwa kipindi kirefu waandishi mbalimbali walihusisha "uduni wa teknolojia" katika Afrika na jangwa la Sahara; yaani Sahara likionekana kuwa ni kikwazo kikuu katika kueneza maarifa na bidhaa mbalimbali. Lakini kwa hakika, kipindi hiki kimeshuhudia kushamiri kwa biashara ya kuvuka Sahara. Kana kwamba lilikuwa ni Mediterania ya mchanga mwingi, jangwa la Sahara liliunganisha nchi zilizopakana nalo na "bandari" za kusini kama vile Timbuktu, Tichit, Walata, Gao na bandari za kaskazini kama vile Sijilmasa, Tilimsan, Wargia na Ghadames. Ngamia, "merikebu" pekee ya jangwani, akawa na umuhimu mkubwa kama yalivyokuwa malisho aliyoyahitaji ili aweze kuishi na ambayo Wanomadi waliyapigania vikali.

Kupitia "bandari" zilizotajwa hapo juu, biashara ya kuvuka Sahara ilipanuka zaidi hadi Ulaya na Mashariki ya Kati kwa upande mmoja, na hadi Ghuba ya Guinea kwa upande mwingine.

Wanomadi walioishi katika njia za misafara hii walinufaika sana. Waliweza kupata nguo, dhahabu, nafaka, pembe za ndovu na watumwa kwa kubadilishana na chumvi na madini mengine, nyama na waongoza safari wa kukodi. Ibn Batuta aliacha taarifa ya kusisimua na yenye thamani kubwa kuhusu biashara hii katika safari yake ndefu ya kuvuka jangwa, ambako mkuu wa msafara "alimwongoza kila mtu aliye katika msafara kama afanyavyo nahodha wa meli." Kutoka Sijilmasa hadi Walata ilikuwa ni safari ya miezi miwili, na msafara ulipumzika Teghazza kwa siku kumi. Mapumziko haya yalikuwa ya lazima kabla ya kuendelea na safari. Waongoza safari wazofu Wamassufa — walilipwa vizuri sana kuhakikisha usalama wa misafara. Hata hivyo, idadi kubwa ya misafara ilianguka jangwani kama ilivyodhihirishwa na malundo ya simbi, mikuo ya shaba nyekundu na vipande vya nguo vilivyogunduliwa na T. Monod huko Mauritania mnamo 1964.

Siku ishirini na nne zaidi zilihitaika kusafiri kutoka Walata hadi Nyani, mji mkuu wa Mali, kwa kutumia njia hii salama ambayo mtu angeweza kusafiri peke yake. Kwa ufupi, misukosuko iliyosababishwa na binadamu katika safari hizi za biashara jangwani ilikuwa muhimu sawa na vikwazo vinavyotokana na mazingira ya asili. Kila mamlaka madhubuti zilipodhibiti njia, misafara ilifanya safari zao kwa urahisi. Mara tu mamlaka zilipodhoofika, visima vya maji vilivyotumika kama alama za njia za kupita humo jangwani vilizibika na wasiwasi kujitokeza. Wakati huo Wanomadi walilihama jangwa na kunyemelea miji.

Machimbo ya dhahabu

Kwa mujibu wa Ibn Hawkal, katika karne ya kumi mfalme wa Ghana ndiye aliyekuwa mtawala tajiri kuliko wote hapa duniani kutokana na dhahabu iliyolimbikizwa na nasaba yake iliyotokana na ukiritimba wa kifalme wa mikuo ya dhahabu. Machimbo haya ya dhahabu katika Galam, Bure na Bambuk yalikuwa muhimu kiasi kwamba wafanya biashara Waarabu Waberiberi walipigwa marufuku kufika huko. *Mansa* Kanku Musa I alipofanya hiya yake hakutoa maoni yake kuhusu suala hili gumu la machimbo ya dhahabu. Hata hivyo, mara baada ya hiya, mfalme wa Mali akaonekana katika atlas ya Majorka akiwa ameshika mche mkubwa la dhahabu. Pamoja na machimbo yaliyotajwa, dhahabu kutoka Volta, na nchi za Walobi na Waakan pia ilipitishwa katika miji mikubwa ya Sudan kwenda kaskazini ya Sahara na ulimwengu wa Kiislamu au Ulaya. Hata hivyo, sehemu kubwa ya akiba hiyo ya dhahabu ililimbikizwa tu, kwa sababu dhahabu ilikuwa ni kama bidhaa takatifu ambayo matumizi yake yalitawaliwa na miviga kama ya kidini.

Bidhaa nyingine

Chumvi ilikuwa ni bidhaa kuu katika eneo hili na watawala wa Sudan walipenda

kuteremsha bei yake ingawa kodi iliyotokana na bidhaa hii iliingiza kiasi kikubwa cha mapato ya kifalme. Hivyo, chumvi kutoka Teghazza ambayo iliuzwa kwa "mithkal" 10 kwa mzigo mmoja huko Walata, bei yuke ingeweza kuwa mara nne katika Nyani, makao makuu ya Mali.

Gharama za kusafirisha chumvi kutoka Awlil, pwani ya Senegal, zilikuwa za chini, lakini chumvi hiyo ilipofikishwa kwa wakazi wa misituni ilinunuliwa kwa uzito (sawa) wa dhahabu, na ilitumika pia kama fedha ya kununulia kola, watuniwa, pembe za ndovu, n.k. Ulipotokea upungufu wa chumvi, Waafrika walitumia mbinu nyingine: walipata chumvi kutokana na majivu ya mboga fulani fulani. Vivyo hivyo, bidhaa ya shaba nayo ilikuwa muhimu katika mabadilishano ya kibiashara kama alivyosisitiza *Mansa Kanku Musa I* akigusia machimbo ya shaba nyekundu katika Takedda, na shaba iliyoingizwa Nyani katika mikuo na baadaye kuuzwa nchi za kusini (Worodugu) ambako waliuza kwa bei ya uzito wa "mithkal" ya dhahabu. Faida iliyopatikana kutokana na mauzo haya ilikuwa kubwa mno. Kwa mujibu wa Ibn Battuta, Takedda kilikuwa kituo kikubwa cha biashara ambapo dhahabu ilifuliwa katika mikuo minene na myembamba na kuuzwa kwa bei ya jumla katika maeneo ya ndani kabisa ya Sudan. Aidha, shaba iliyokuwa katika vipande vidogo vidogo ilitumiwa kama fedha, na kwa kuipeleka Misri iliwawezesha wafanya biashara kurudi na bidhaa za viwandani zikiwa ni pamoja na nguo laini.

Kwa bahati mbaya, bidhaa ya tatu ya faida kubwa ilikuwa ni watumwa wanaume na wanawake. Wakati Ibn Battuta aliposafiri kuvuka Sahara kutoka Sudan hadi Tuat, katika karne ya kumi na nne, msafara wake ulikuwa na watumwa wanawake 600. Watumwa hawa walihitajika sana katika majumba ya wanamfalme wa Kiarabu na wa Kiberiberi ambako walitumika kama watumishi, askari, masuria na makahaba. Wakati mwingine watumwa hawa waliwaathiri mabwana zao hasa kama walikuwa wameelimika au walikuwa wazuri wa kupindukia.

Kuanzia karne ya kumi na tano, watumwa hawa walitumiwa zaidi katika kazi za kilimo, kwa mfano katika Mashariki ya Kati, lakini zaidi katika Ulaya ya Mediterania. Ni kweli kwamba watawala weusi pia walichukua watumwa kutoka kaskazini, lakini walifanya hivyo kama ishara tu ya ukubwa. Al-Umari aliandika kuwa wakati mansa alipokaa katika kiti chuke cha enzi hadharani, "nyuma yake walisimama mamluki wa Kituruki au mamluki wengine wapatao thelathini walionunuliwa maalum kwa ajili yake kutoka Kairo. Mmoja wao alishika aina ya mvamvuuli wa hariri wenye kikuba juu yake na ndege wa dhahabu aina ya kozi." Inawezekana kwamba waandishi wengine wametoa taarifa zilizotiwa chumvi kuhusu upotevu wa idadi ya watu uliosababishwa na biashara hii ya utumwa iliyofanywa na Waarabu wa Kiberiberi. Raymond Mauny alikadiria upotevu wa watu 20,000 kwa mwaka au milioni mbili katika karne. Kwa mfano, kwa mkataba wa *bakt*, mfalme

wa Nubia alipaswa kuwasilisha Kairo watumwa 442 kila mwaka. Kwa hakika mchango huu ulipatikana hasa kutoka katika jamii zenye kufuata dini za kiasili katika sehemu za kusini.

Bidhaa nyingine zilizohusika katika biashara zilikuwa ni pamoja na pembe za ndovu, kwa sababu pembe za ndovu wa Afrika zilikuwa laini zaidi na rahisi zaidi kuzichonga kuliko zile za ndovu wa India. Vilevile Sudan ilisafirisha nje ngozi, ngozi za choroa, nafaka na nguo. Njia iliyotumiwa zaidi katika karne ya kumi na nne ni ile iliyotumiwa na Ibn Battuta, lakini vilevile ilikuwapo njia nyingine kutoka Timbuktu hadi Kayrawan kupitia Wargla. Kaskazini mwa Sahara kulikuwa na koo za wafanya biashara tajiri, walanguzi kweli kweli waliotayarisha mzigo na kughariniua misafara. Katika wafanya biashara wa aina hiyo walikuwamo wanandugu akina al-Makkari ambao waliaminiwa na watawala wa Mali. Walikuwa na mtandao wa biashara uliochangamana ambao mbali na makao makuu yake yaliyokuwa Tilimsan, ulikuwa na matawi katika Sijilmasa na Sudan.

Kusini mwa jangwa mashirika madhubuti ya wafanya biashara WaJuula na Wahausa yaliimudu biashara kama wafanya biashara wenzao wa kaskazini. Aidha, jamii za Wayahudi zilishiriki katika biashara hizi kama vile huko Tuat, na hata kupenya ndani kabisa ya Sudan, tangu kame ya nane. Pamoja na kutekwa tena Hispania, na haja ya kuuzunguka ulimwengu wa Kiislam kuanzia karne ya kumi na tano, wazungu pia walijasiri kusafiri katika maeneo haya. Mgenoa Antonio Malfante alisafiri hadi Tuat, na Benedetto Dei alisafiri hadi Tumbuktu.

Kiwango cha biashara kuvuka Sahara hakipaswi kudharauliwa. Misafara ya kawaida ilikuwa na ngamia elfu moja, lakini Ibn Khaldun anazungumzia misafara kati ya Sudan na Misri iliyokuwa na ngamia 12,000.

Kuenea kwa fikra na ufundi

Kutangamana kwa Waarabu wa Kiberiberi na wakazi wa Sahel, hasa katika miji, bila shaka kuliwezesha mawasiliano baina ya pande mbili ya mbinu za ufundi, fikra na amali mbalimbali.

Kwa mfano, je, mfumo wa ubaba (wa kujinasibu kuumcni) ulianzishwa na Waislam? Inaelkea sivyo, ingawa kipindi kinachoanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita kilionyesha wazi mabadiliko kutoka mfumo wa umama (wa kujinasibu kuukcni) kuelekea mfumo wa ubaba, kama ilivyokuwa katika ufalme wa Ghana na dola la Gao, ikiwemo Mali, ambayo inatupatia mfumo wa kati (urithiano wa kidugu) ambao umejaa inigongano.

Lakini kuna Waislam Waberiberi na Wasudani kama vile Wabambara ambao wanafuata mfumo wa umama. Zaidi ya hayo, watu wa Kongo wenye mfumo wa

ubaba hawakuwa na uhusiano wowote na Uislamu. Wakati huu Uislamu haukuenezwa kwa kutumia mabavu. Hasa, wakati huu, Waarabu Waberiberi, Wangara na Wahausa ndio waliowasilimisha watu kwa njia ya amani, na kueneza dini hii mpya kusini zaidi. Kwa miaka mingi Uislamu ulivumilia baadhi ya ibada za kale licha ya raghba za mwana mageuzi al-Maghili za kuhimiza matumizi ya taratibu mpya. Ibn Battuta alibaini kuwa Wasudani waliheshimu sana Uislamu lakini pia aliona mkengeuko wa tabia ulioonyesha uvumilivu wa Wasudani.

Katika miji, Kiarabu kikawa lugha ya wanazuoni na kikatumika pia katika mahakama: Mansa Musa alikizungumza kwa ufasaha. Fasihi ya Kiafrika kwa Kiarabu ikaanzishwa, lakini upeo wa mafanikio yake ukaonekana katika karne ya kumi na sita. Mabadilishano ya wataalamu yalifanyika kwa msingi wa usawa baina ya vyuo vikuu mbalimbali katika Sahara. Watawala wa Sudan walizungukwa na washauri, wanasharia na maimaniu ambao aghalabu walikuwa wafuasi wa madhehebu ya Maliki.

Uhusiano baina ya Chadi na Mediterania

Hakuna taarifa nyingi kuhusu biashara ya kuvuka Sahara katika jimbo hili ikilinganishwa na Sudan magharibi. Lakini pia Sudan ya kati ilikuwa na uhusiano wa muda mrefu na Misri, Libya na Maghrib.

Katika karne ya kumi na nne, ufalme wa Kanem ulienca hadi Fezzan kwa upande wa kaskazini na Wadai kwa upande wa mashariki. Njia moja kuu ilianza Kanem kwenda Misri kupitia kwenye *viganga* vya chumvi vya Kavar, Zawila katika Fezzan, Oasisi za Libya na pwani ya Mediterania. Njia ya pili iliunganisha ziwa na Kairo kupitia Tibesti na Aswan. Ya tatu ilikwenda Tunis na Tripoli kupitia Ghadames. Njia hizi zilitumika sana wakati wa kuinukia kwa majimbo ya Hausa. Lakini, shughuli za biashara ya watumwa zilizofanywa na Waarabu katika jimbo la Darfur ziliua njia ya mashariki kuendea Misri.

Sudan ya kati ilisafirisha nje ngozi, watumwa na pembe za ndovu. Katika biashara hii, Wahausa walikuwa wafanya biashara wa kati baina ya Afrika ya Kaskazini na maeneo ya msitu (Ife, Oyo, Benin, Igbo-Ukwu), na pia baina ya madola makubwa ya Sudan magharibi na nchi za Nili.

Eneo la Savana na la msitu

Wafanya biashara wa Sahel walichukua hadhari walipotakiwa kutoa taarifa kuhusu nchi za msitu. Kwa hakika walikuwa wanajaribu kuficha siri, hasa, ili waendeleo kuhodhi mahusiano na ukanda huu ambao ulichangia biashara ya savana kwa bidhaa zake za thamani kama vile dhahabu, kola, viungo, n.k. Bidhaa hizo


zilibadilishwa na shanga, chumvi, zana za chuma, nguo na samaki wakavu kutoka Niger ya kati. Bidhaa ya kola ilikuwa ndiyo lengo la misafara ya biashara ya masafa marefu iliyoandaliwa na vikundi shupavu vya wafanya biashara weledi kutoka Guro, Bete au nchi ya Asante.

Kwa hakika tunda la kola ambalo lilipatikana hata sehemu za mbali sana kama vile Kongo, lilikuwa na dhima muhimu katika masuala ya chakula na mahusiano ya kijamii miongoni mwa watu wengi. Kutokana na haja yao kubwa ya kupata kola na hasa dhahabu, wafanya biashara Wangara walijenga vituo nyikani ambavyo baadaye vikawa vituo vikubwa vya biashara na hata vya siasa. Hivyo, misitu kusini mwa nyika haikuwa kizuizi kwa wafanya biashara, kama ambavyo jangwa halikuwa kizuizi upande wa kaskazini. Kutokana na mabadiliko ya polepole ya makazi, misitu iliingiliwa na watu waliotoka nyikani na kujenga jamii za vijijini zilizostawi au vituo vya kisiasa na kiutamaduni kama vile miji ya Wayoruba.

Afrika ya Mashariki na Kati

Data zilizopo kuhusu eneo hili ni za kuokoteza zikilinganishwa na zile za Sudan ya Magharibi. Ni kwa namna gani bidhaa kutoka bara (pembe za ndovu, ngozi, dhahabu, shaba, chuma, n.k.) zilikusanywa na kusafirishwa hadi pwani ya mashariki na Bahari ya Hindi? Ni kiasi gani cha bidhaa zilizoingizwa kutoka nje (hasa simbi) na kupitishwa katika bandari za pwani zilisambazwa bara? Hakuna majibu ya maswali haya ingawa taarifa zilizokosekana katika siku za nyuma polcpole zimeanza kufahamika. Kwa mfano, biashara iliyofanyika kuanzia Ethiopia hadi Zambezi sasa imeanza kufahamika zaidi. Katika ukanda huu, kama ilivyokuwa huko Awlil Taonden katika Afrika Magharibi, biashara ya chumvi ilifuatiliwa kwa karibu kwa sababu ilikuwa bidhaa muhimu. Chumvi ya Dankali ilisafirishwa nje tangu kale na ufalme wa Aksum. Ingawa uzalishaji ulikuwa chini, kiasi kidogo kilichopatikana angalau kiliuzwa katika nchi jirani. Hata hivyo, kwa mujibu wa Grottanelli, katika sehemu za pwani ya kusini ya Somalia na kaskazini ya Kenya hadi kisiwa cha Pate, kulipatikana chumvi nyingi ya kutoka baharini iliyokusanywa na wanawake na watoto. Aidha ilifahamika kuwa kulikuwa na chumvi nyingi ya mawe iliyochimbwa na kuuzwa. Vasco da Gama, katika taarifa yake, anaeleza kuhusu Waafrika waliobeba vibuyu vya maji ya bahari ili wakayavukize na kupata chumvi. Zipo sababu za kufikiri kwamba njia hii ya kupata chumvi imeanza kutumika miaka mingi iliyopita kwenye pwani ya Atlantiki katika enco la Ghuba ya Guinea. Taarifa kutoka katika mapokco simulizi zinaweza kuthibitisha jambo hili.

Katika sehemu ya magharibi mwa Tanzania, viganga vya chumvi katika eneo la Uvinza bado vinatumika hadi leo na vimesambaa kwa umbali wa km 15. Machimbo ya kiakiolojia yanaonyesha kwamba kazi hii imeanza kufanyika tangu karne ya tano enzi ya Ukristo. Huko Ivuna uzalishaji uliyofanywa baada ya karne ya




25.1 Mzunguko wa watu na ufundi wao mbalimbali katika Afrika ya Magharibi (J. Devisse)

kumi na tatu hapana budi ulihusika na biashara za masafa marefu. Huko Kabiro, Uganda, kama ilivyokuwa huko Bazanga katika Zambia, inaelekea kuwa uzalishaji ulianza mapema sana. Hivi karibuni, huko Burundi, wachunguzi wamepima ubora wa njia za kiasili za kutengeneza chumvi, njia ambazo zimeonyesha kuwa Waafrika wanaweza kupata chumvi ya mboga kutoka katika mimea yenye chumvi. Baadaye shughuli hii ilipigwa marufuku na wakoloni.

Huenda katika machimbo ya chumvi ya Mpinda nchini Kongo, karibu na mlango wa mto wa Zaire (Kongo), na pia huko Ambriz katika Angola, bidhaa ya chumvi ilihodhiwa na wafalme, kama walivyohodhi bidhaa ya kombe na, kwa jumla, bidhaa zote ambazo zingeweza kutumika kama fedha. Katika ukanda huu, kama ilivyokuwa Afrika Magharibi, misitu ilitumika kama njia tu za kupita, njia ambazo zilizidi kupanuka kutokana na hali ya hewa au na shughuli mbalimbali za wanadamu. Hivyo, akichunguza kengele ambazo ni mapambo ya wafalme kuanzia Ife hadi Zambezi, J. Vansina ameonyesha jinsi wafanya biashara walivyovuka na kuvusha bidhaa hii katika misitu ya ikweta kutoka kaskazini hadi kusini. Hapa, kama kwingineko, inito (barabara zinazotembea) ilitumika kwa msaada wa wavuvi, kueneza mawazo na ufundi mbalimbali. Aidha biashara katika pwani ya Atlantiki nayo ilifanya kazi kama hiyo, kwa mfano, kueneza ufundi wa kutengeneza sanamu za rangi rangi ambao ulianza Nigeria na kuenea hadi Angola. Kwa kifupi, fikra nyingi zilizopotoka kuhusu "mkwamo" wa jamii za Kiafrika katika uvumbuzi na maendeleo zingeporomoka iwapo, badala ya kurejea katika karne nyingi za mahusiano na Wazungu (Afrika ilipokuwa imekwisha bomolewa na biashara ya watumwa), watu wangengalia shughuli mbalimbali na uzoefu wa Kiafrika katika kipindi tunachohusika nacho hapa.

Shaba na dhahabu: misingi ya mabadilishano katika Afrika Kusini

Uchimbaji wa shaba nyekundu katika Afrika ya Kusini ulianza katika karne za mwanzo za kipindi cha Ukristo katika jimbo la Shaba na kauka sehemu za kati nyanda za juu kauka Zimbabwe. Shaba iliyokuwa kauka mikuo na umbo la misalaba ilisafirishwa nje katika safari ndefu sana. Wakati huo Wareno wakiwa na hamu ya kujitoa katika kuwategemea Wazungu wazalishaji wa bidhaa hii walitaka kutafuta wenyewe kauka Afrika vyanzo vya metali hii ambayo wakati huo tayari walikuwa wakiisafirisha kwa wingi barani humo. Hivyo mara moja walijihusisha katika kusafirisha bidhaa hiyo kupitia mlango wa mto Limpopo. Shaba ilihitajika sana katika Afrika kwa ajili ya kutengeneza mapambo na kuonyesha sifa za watawala wa kisiasa, na vilevile ilitumika kama fedha ikiwa imefuliwa kauka mikuo



Bidhaa zilizotusika katika biashara ya masafa marefu

Chumvi	● Mahali ilipozalishwa kwa hakika	Dhahabu	■ Mahali ilipopatikana kwa hakika
	○ Mahali ilipokisiwa kuzalishwa		□ Uchunguzi wa kiakiolojia katika kuthitisha matumizi
	--- Njia za biashara	 Njia ya hakika ya biashara
Shaba	▲ Mahali ilipopatikana kwa hakika		..?.. Njia za biashara ambazo zinaweza
	X Uchunguzi wa kiakiolojia kuthibitisha usambazaji wa metali hii na taarifa za maandishi		

25.2 Afrika ya Kati, Mashariki na Kusini karne ya 11-15 (J. Devisse)

midogo midogo. Katika eneo la Shaba, wingi wa madini hayo uliwavutia watu wengi, na kutokana na hali hiyo, ufundi mbalimbali uliohusu metali zenye chuma na zisizo na chuma ulibuniwa na kuendelezwa. Ufundi huu ulichangia katika kuanzishwa kwa falme za Luba na dola ya Lunda katika ukanda huu kabla ya 1500, na katika kuenea kwa athari za kitamaduni za Luba hadi Zimbabwe. Mapema katika karne ya kumi, al-Masudi anasisitiza kuwepo kwa biashara kubwa iliyoleta dhahabu Sofala kutoka bara. Machimbo ya kiakiolojia ya Summers nayo yamedhihirisha kiwango cha uchimbaji dhahabu katika uwanda wa juu wa Shona, na sehemu zilizokuwa na machimbo hayo zimeainishwa kwa uangalifu.

Inaelekea kuwa uchimbaji ulianza kunako karne ya saba karibu na kusini ya Zambezi na ukaenea kati ya karne ya tisa na ya kumi na moja katika uwanda wote wa juu hadi kufika Limpopo katika karne ya kumi na tano. Bidhaa nyingi zilifika Sofala kupitia bonde la Sabi, na vile vile kupitia mito Zambezi na Limpopo. Bila shaka mafanikio ya Zimbabwe na Sofala katika karne za kumi na nne na kumi na tano yalikusishwa na biashara hii ambayo inakisiwa ilifikia tani kumi kwa mwaka ilipofika karne ya kumi na moja. Aidha biashara hiyo ilifika kwenye vituo vingi vya pwani kwa kupitia njia nyingi tofauti. Biashara ya mwambao iliyoendeshwa na Waislamu na kuenea hadi Sofala ilikatizwa na Wareno. Kupitia bandarini, biashara hii iliunganishwa na Aden na ulimwengu wa Waislamu, India na China.

Wareno walipofika, bado tani elfu nyingi zilikuwa zinasafirishwa kutoka Sofala kila mwaka. Machimbo ya Zimbabwe Kuu yameonyesha mabaki ya mahali ambapo metali hiyo ya thamani ilikawa ikiicyushwa.

Hata hivyo, biashara hii haikuwa msingi mkuu wa utajiri wa Zimbabwe. Badala yake shughuli kuu ya uchumi ilikuwa ni ufugaji wa ng'ombe katika maeneo ya nyanda za juu zilizokuwa na mbung'o, shughuli ambayo hapo awali iliwageuza mabwana wa Zimbabwe kuwa wafalme wa matanibiko. Baadaye "wachimba madini" na "wajenzi" waliambatisha mafanikio yao ya kuvutia katika mafanikio ya wafugaji. Inawezekana makundi haya ndiyo yaliyokuwa mababu wa Wasotho na Washona wa wakati huu. Dola la kibaguzi la Afrika ya Kusini lilizuia uchunguzi yakinifu kuhusu mambo ya kale ya kusini mwa Afrika, kwa lengo la kufuta kumbukumbu muhimu za mafanikio ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni ya watu weusi kabla ya kufika kwa Wazungu.

Mwisho, ni muhimu kuthamini mahusiano yaliyokuwapo baina ya Bukini, visiwa vya Ngazija na visiwa vingine jirani na bara hili kwa njia ya bahari. Kwa miaka elfu nyingi, mahusiano haya yalieneza mawazo, ufundi, na miundo mbalimbali ya kijamii katika pande zote mbili za mahusiano (kama inavyodhihirishwa na magudulia ya mawe yaliyoingizwa na Waafrika kutoka Bukini).



26

Afrika katika Mahusiano na Mabara Mengine

Picha ya Afrika katika Ulimwengu

Ni vigumu kueleza namna Waafrika ambao waliwasiliana na ulimwengu kupitia kwa wafanya biashara, watawala na wasomi wao, walivyoutambua ulimwengu. Angalau tunafahamu, kwa mfano, kwamba Wangara walikuwa na muundo maalum wa kutambua mandhari. Kwao kaskazini ilikuwa nchi ya chumvi, (*Kogodugu*), kusini nchi ya kola (*Worodugu*) au *Tukoro* (msitu). "Nchi wazi" (*Gbe Kan*) iliyotanda kuanzia mashariki hadi magharibi ilikuwa ni enco wazi lililofaa kwa biashara. Hii ilikuwa ni jiografia iliyozingatia uzoefu halisi.

Lakini utambuzi huu wa ulimwengu (*imago mundi*) ulipanuka na kujumuisha Afrika Kaskazini na Mashariki ya Karibu kutokana na hija, biashara na balozi kutoka kwa watawala weusi walioishi kusini mwa Sahara. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa pia kwa Wazanji na Waswahili kuhusu nchi zinazopakana au zilizo ng'ambo ya Bahari ya Hindi.

Katika shule za elimu ya juu za Timbuktu, labda jiografia iliyofundishwa ilikuwa ni ya kinadharia zaidi, ambayo iliwapatia watawala kama vile Kanku Musa picha angavu zaidi ya "mfumo" wa kimataifa na nafasi ya Mali katika "mfumo" huo. Je, watu wengine waliifikiriaje Afrika?

Waislamu waliifahamu Afrika, na ujuzi wao kuhusu bara hili uliongezeka na kuboreka katika kame ya kumi na nne kutokana na safari zao za bara. Lakini, maarifa yao yaliendelea kutegemea nadharia tete za kale za Ptolemy au al-Idrisi ambaye Ibn Khaldun aliendelea kumtegemea.

Majimbo ya ikweta na yale ya kusini zaidi yalifikiriwa kuwa hayakuishi watu na hayakustaarabika. Kwa mujibu wa Ibn Khaldun, ukitoa bonde la Mediterania ambalo lilikuwa "kitovu cha ustaarabu" kutokana na hali bora ya hewa, majimbo ya ikweta kama yale ya kaskazini, hayakustaarabika kwa sababu ya hali mbaya sana

ya hewa. Mbali zaidi magharibi, visiwa vya Kanari vilikuwa ndio mpaka wa eneo lenye kuishi watu. Hivyo, katika dhana ya ulimwengu unaoanzia Mediterania, ulimwengu ulizungukwa na bahari isiyo mipaka. Nchi za pembezoni kama Afrika ya watu weusi, zilichukuliwa kuwa ni makazi ya watu "waliofanana zaidi na wanyama kuliko viumbe wenye akili," hali iliyotokana na umbali baina ya nchi hizi na ukanda wenye hali ya hewa ya wastani, ikiwa na "maana kwamba hali ya watu hao inakaribiana kabisa na ile ya hayawani." Lakini polepole, safari za maskanini zilizofanywa baina ya karne ya kumi na kumi na nne zilibadili mtazamo huu. Al-Umari na Ibn Battuta wanapongezwa, kwani licha ya hatua zilizochukuliwa na watawala weusi kulinda ustarabu wao, taarifa za Al-Umari na Ibn Battuta zilivwezsha maarifa mbalimbali yenye kina kuanza kuchukua nafasi ya mafunzo ya kalautala kutoka katika vitabu. Hali hii ilijitokeza katika eneo lote kuanzia Mauritania hadi pwani za Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi. Jimbo la misitu liliendelea kutoingilika hadi walipofika wazungu katika karne ya kumi na sita.

Kwa miaka mingi, kwa upande wa ulimwengu wa magharibi, Afrika iliwavutia wafanyabiashara, watawala na walokole, hasa kwa kuwa ilipakana na ulimwengu wa Kiislamu, waliotaka kuuzunguka na kuushinda. Juhudi za wachora ramani zilikuwa muhimu sana katika kuleta mitazamo mipya. Mnamo 1339 jina la *Rex Melli* (Ufalme wa Mali) katika ramani ya Angelino Dulcert lilitabiri ziara ya Mgenoa Malfante huko Tuat karne moja baadaye. Hii ilikuwa ni ziara ya upelelezi katika "bara lisiloleweka" ambalo halikuweza kuingilika kwa sababu ya kuzibwa kabisa na Moroko kwa upande wa magharibi, na utawala wa Kairo upande wa mashariki. Lakini kuanzia karne ya kumi na tatu, Chuo cha Miramar katika Visiwa vya Balearik na "Taasisi ya Taaluma za Kiarabu ya Ulaya" vilivyokusudia kuwabadili wapagani, vilitoa taarifa zaidi. Kanisa la Kirumi, kupitia makubaliano ya kidiplomasia, lililenga hasa katika kulinda maenco madogo ya Wakristo katika pwani ya kusini ya Mediterania.

Hadi kufikia karne ya kumi na tano, Asia haikujishughulisha sana na bara la Afrika, licha ya wahamiaji wa Kiajemi na Kiindonesia. Ni katika mazingira haya ambapo majilio ya ghafla ya Wareno kusini mwa tropiki yalitangaza mapinduzi dhahiri ya habari na mikakati.

Kutoka kwenye dimplomasia ya Kimediterania hadi mabadilishano kati ya Waafrika na Wazungu

Nchi za Kiislamu zilizo katika pwani ya kusini ya Mediterania, pamoja na al-Andalus, hazikufuata sera madhubuti na ya pamoja kuliko nchi za Kikristo. Licha ya matakwa ya kidini, siku zote Genoa ilitetea maslahi ya Granada dhidi ya Kastile, ambapo Misri, rafiki wa Kastile na Aragon, iliepaka kuunga mkono Granada.

bidhaa zilizoimaliza Afrika yenyewe na kuchochea uchumi wa Kaskazini, yaani Wavenisi na Wagenoa waligombea masoko miongoni mwa Mamluki na Waottomani, wakati ambapo Wahafsi wa Tunis, Wamarini wa Moroko na watawala wa Tilimsan walipambana wenyewe kwa wenyewe na kupigana vita kadhaa, au wakati mwingine walifanya urafiki kati ya nchi mbili au tatu.

Ukweli ni kwamba kiunzi cha mikakati ya mahusiano haya yanayokinzana kipo mahali pengine kabisa. Waislamu, ambao ndio waliokuwa mabwana wa biashara kati ya Asia na Ulaya, waliingiza uchumi wa Sahel katika biashara ya ulimwengu na kupitia biashara hiyo, dhahabu ya Sudan ilichochea mfumo wa fedha wa Waarabu na baadaye ule wa nchi za Magharibi. Kwa kifupi, ulimwengu wa Kiislamu ulinufaika sana kutokana na nafasi yake ya kati baina ya Ulaya na Afrika ya ndani kabisa. Lakini wenzake wawili katika biashara walifanya kila njia kuuvunja ukiritimba huu. Modola ya Kisudani yalipanga mfumo bora wa kudhibiti bidhaa zinazotoka nchini na kodi ya bidhaa zinazoingia, kuchepua njia za biashara na kutafuta wateja wapya huku yakiingilia kati mahusiano ya Waarabu na Waafrika kwa njia za kidiplomasia. Vilevile yalitumia hali ya uchumi kudhoofisha nasaba tawala za Wamarini, Wattasi na Wasadi.

Madola ya Kikristo yalijaribu kutingisha hali iliyopo kwa kutumia mikataba ya biashara ambayo kwa hakika ilizidisha mashindano baina yao, na polepole wakaanza kutumia mikakati ya kisiasa na kidini. Kwa mfano, Venisi ililenga Misri na bonde la Mediterania Mashariki, ambako ilitilia mkazo ununuzi wa viungo kutoka Asia, na kuhodhi biashara ya sukari kutoka Mashariki, Kupros na Krete. Mara chache ilibadilisha vico na nguo zake katika Tunis na Tripoli, kwa dhahabu kutoka Sudan. Katika karne ya kumi na nne, Wagenoa walijishughulisha na ngano, watumwa na sufu ya Kiingereza.

Ushindi wa Waottomani uliwatimua Wagenoa kutoka bonde la Mediterania mashariki, na wakaishia Afrika Kaskazini, wakileta sukari kwa wingi katika soko kusliindana na Wavenisi. Hali hii iliwafanya waone haja ya kudhibiti maeneo yaliyozalisha sukari kwa kujiunga na Wahispania waliokuwa wanaanza kuizalisha, wakiunga mkono sera ya Warcno ya uvumbuzi na ya mashamba ya miwa katika visiwa vya bahari ya Atlantiki (Madeira, Kanari). Shughuli hizi ziliwaingiza Waitaliani katika Bahari ya Atlantiki na ulimwengu wa Afrika na Marekani, na katika mlipuko wa ujenzi wa meli uliofanyika ili kukidhi haja mpya za "ndoto za kishujaa na za kikatili." Aidha Wakatalani walikodisha meli zao kwa Waislamu wakijaribu kujipatia faida kutokana na misafara hii ya meli, ila biashara yao ilikuwa ndogo ikilinganishwa na Venisi na Genoa — miamba mawili katika biashara wakati huo.

Mchango wa Afrika katika mapambano haya ya kiuchumi ulikuwa hasa ni

dhahabu na watumwa. Katika karne ya kumi na moja na kumi na mbili, dhahabu ya Afrika ilichangia katika kujenga umaarufu wa sarafu za Wafatimi, Waumayya, Wamoravi, Wamohadi na Wahafsi. Hadi karne ya kumi na tano, bidhaa hizi ziliendelea kuchangia na kuimarisha uchumi wa watu hao, usitawi wa ustarabu wao na anasa katika majumba yao ya kifalme—mambo yanayoelezwa vizuri na waandishi wa Kiarabu.

Kwa kupitia biashara yao na Afrika Kaskazini, polepole kuanzia karne ya kumi na mbili na kuendelea, nchi za Kikristo zilishika sehemu ya dhahabu ya Sudan katika masoko ya Kairo, Tunis, Bijiya, Tilimsan, n.k. Faida ilikua kutokana na kuongezeka kwa ukubwa wa meli. Katika karne ya kumi na tano, mapato ya mwaka kutokana na biashara ya Katalani na Maghrib yanakisiwa kufikia kiwango cha dinari 120,000. Katika hali hii, matumizi ya dhahabu kama fedha ambayo yaliachwa kwa karne nyingi katika nchi za Magharibi, yalianza tena katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tatu, na bila shaka, kwa kiasi fulani yalitokana na dhahabu ya Afrika. Huko Magharibi, kiu ya dhahabu iliendelea kukua na hivyo kusababisha juhudi za awali za wafanya biashara kama Malfante na wengine za kutafuta njia ilimopita dhahabu ng'ambo ya Sahara.

Pamoja na faida zilizotokana na biashara, watawala walitajirika kutokana na ushuru waliotozwa Waislamu baada ya ushindi wa Wakristo. Katika karne ya kumi na mbili, wafalme wa Tunis waliilipa Sisilia "bezant" za dhahabu 33,000 kwa mwaka. Masultani wa Granada, ambao walipokea kiasi fulani cha dhahabu ya Afrika, kwa mwaka walipeleka Kastile kati ya dinari 10,000 na 40,000. Mwishoni mwa karne ya kumi na tatu, Tilimsan ilimlipa mfalme wa Aragon kati ya dinari 2,000 na 6,000 kwa mwaka. Njia mojawapo ya kupata dhahabu hii ilikuwa ni kukodisha meli, ambazo gharama za ujenzi wake zingelilipwa kidogo kidogo katika miezi minne, au kukodisha mamluki kulikofanywa na Wakristo (kwa mfano, kwa Moroko). Kutokana na njia hizi mbalimbali, mfalme wa Aragon aliweza kupata mapato yaliyofikia asilimia 10 ya mapato yake ya mwaka. Lakini vilevile falme za Afrika Kaskazini zilinufaika, angalau kwa muda mfupi, na biashara hii isiyolingana kwa sababu ya ushuru wa forodha (asilimia 10) uliotozwa kwa bidhaa zilizoiingizwa toka Ulaya. Katika karne ya kumi na tano ofisi ya forodha ya Wahafsi ilijipatia mapato ya mwaka ya dinari 150,000. Watawala wa Maghrib wenye kuona mbali zaidi waliona madhara ya muda mrefu ambayo yangetokana na ukoloni huu wa kibiashara.

Tangu karne ya saba mapambano baina ya Waislamu na Wakristo yalimalizika kwa kuchukua watumwa miongoni mwa wale walioshindwa. Katika karne ya kumi na kumi na moja, "soko" hili liliwafaa zaidi Waislamu. Kuanzia karne ya kumi na mbili na kuendelea, mambo yalibadilika kutokana na shinikizo la ushindi wa Wakristo. Vilevile, idadi kubwa zaidi ya watu weusi ilionekana miongoni mwa

makundi ya watumwa ambao hapo awali waliletwa kutoka Sudan au Nubia. Kulikuwa na "watu weusi" katika majeshi ya Hispania ya Waislamu ambayo yalipigana dhidi ya Wakristo. Katika karne ya kumi na nne na kumi na tano, wafanya biashara walitawala soko. Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tano, katika Naples, asilimia 83 ya watumwa walikuwa weusi. Vilevile kulikuwa na watumwa wengi huko Sisilia. Nguvu kazi hii ilikuwa ni ya aina mpya, na hasa kwa sababu idadi kubwa ilitokana na watumwa kutoka "Guinea". Wareno walishambulia pwani ya Mauritania kwa ajili ya kupata watumwa tangu mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Kuanzia 1494 na kuendelea, soko la Valensia lilikuwa na watumwa wengi ambao miongoni mwao walikuwa wa asili ya Kisenegali. Mfumuko huu wa watumwa ulisababisha bei yao kuanguka. Watumwa weusi wakauzwa kwa bei rahisi sana, na wakatumwa katika kazi ngumu za kilimo na migodi. Mkabala wa kuwadharau watu weusi miongoni mwa jamii za Mediterania umecanzia wakati huo. Ni wakati huu ambapo kukua kwa uehumi wa bara la Afrika kulikotokea katika karne ya kumi na nne kulipoathirika sana. Huku inapambano ya kudhibiti Bahari ya Hindi na kujipanua kwa Waottomani yakiwa yanaendelea upande wa mashariki, na vituo vya Wazungu vya biashara ya watumwa vikiwa vinaanzishwa katika mwambao wa Atlantiki kwa upande wa magharibi, Afrika ilijikuta imenaswa kwa karne kadhaa katika uovu ambao uliua maendeleo na ustawi ulioanza kuchipua karne ya kumi na nne.

Afrika, Asia na Bahari ya Hindi

Njia kuu za biashara, za nchi kavu na za bahari, zilisafirisha bidhaa maridhawa za Asia kwenda Asia magharibi. Njia hizo zilidhibitiwa na Waislamu tangu karne ya saba. Lakini kulikuwa na mashindano makali kati ya njia iliyokomea katika Ghuba ya Arabia/Uajemi, ambayo iliimarisha biashara ya Mesopotamia na Shamu, na ile iliyokomea Bahari ya Shamu, ambayo ilipitia Nili hadi kwenye bandari za delta. Hivyo vilikuwa vituo viwili vyenye ushindani mkubwa. Katika kipindi tunachoshughulika nacho, mageuzi makubwa yaliyotokea Asia, na kuanguka kwa utawala wa Kiislamu katika Mesopotania, vilipa mwanya Misri kuanzia wakati wa Wafatimi na Wamamluki, na kuifikisha Kairo kwenye upeo wa ustawi wake.

Mediterania ilitetekezwa kwa Wakristo baada ya 1100, lakini jitihada zao za kijeshi na kibiashara za kufikia njia iendayo Bahari ya Shamu kupitia Misri hazikufanikiwa. Hao Wamisri wenyewe walitegemea Aden, kitovu cha biashara hii. Kutoka hapo, wafanya biashara Wakarimi walidhibiti biashara ya viungo, dhahabu, vito vya thamani, pembe za ndovu, kati ya Asia, Afrika na Misri n.k. Ustawi wa utajiri wao ulifika hadi Aleksandria ambako wafanya biashara wa Magharibi

walikuja kununua bidhaa walizozihitaji.

Mnamo kame ya kumi na tatu, Aydhab ikawa mojawapo ya bandari zenye shughuli nyingi sana duniani. Lakini hapakuwa na utawala wowote ulioweza kudhibiti kila tawi la biashara hii. Wakarimi wakawa wafanya biashara wa kati ambao hawakuweza kuepukika, na walilindwa na uhuru wa kidiplomasia katika kujadili mikataba baina ya Wamisri na Waasia. Mamluki walitwaa madaraka ya bandari katika pwani ya magharibi ya Bahari ya Shamu: Sawakin, Massawa na Assab. Lakini kiu ya dhahabu waliyokuwa nayo Wamisri katika kame ya kumi na mbili, kabla ya mmiminiko wa dhahabu kutoka Sudan, ilichochea hamu ya Wafatimi kupata dhahabu ya Sofala na kuipata njia inayoelekea huko. Lakini ni kutokea hapohapo Sofala, chuma cha Afrika kilichokuwa bora sana kama ilivyochezwa na al-Idrisi, kilisafirishwa India pamoja na pembe za ndovu, ngozi za wanyama, mbao, n.k. Imekadiriwa kwamba tani kumi za dhahabu safi ya Sofala ziliuzwa Kilwa, kiasi ambacho ni sawa na dhahabu iliyozwa kutoka Afrika ya Magharibi. Waafrika walipata aina mpya za mimea, shanga za kioo, simbi, na nguo. Katika kame ya kumi na tatu, asilimia 60 ya ushuru wa forodha uliotozwa Kilwa ulitokana na bidhaa za pamba zilizoingizwa nchini, na kupelekwa hadi mwishoni mwa "nchi ya ajabu" ya Afrika kupitia Sofala kwa njia ya mlango bahari wa Msumbiji.

Meli zilianza safari yake ya kwenda Asia kutoka bandari za Mombasa na Malindi. Safari za meli zilifanikishwa na unajimu na matumizi ya dira, taaluma zilizopatikana kutoka China. Aidha ujuzi wa pepo, mikondo ya maji, mimea na wanyama wa baharini uliofungamana na safari hizi ulikuwa ni mchango mkubwa katika hazina ya sayansi na teknolojia. Vituo vya biashara na makazi vilizagaa huko India, Afrika na Arabia ya kusini. Zaidi ya miji hamsini kuanzia Rasi ya Gardafui hadi Sofala ilikuwa imeshasitawi hata kabla ya kuja kwa Waarabu. Katika miji hii, tabaka jipya la kikabaila na kibwanyenye likazaliwa kwenye chungu cha kikabaila, kitamaduni na kiislamu cha ustaarabu wa Kiswahili. Uchunguzi wa kiakiolojia umegundua mabaki ya kustaajabisha ya misikiti mizuri ya mawe na majumba ya wafalme, vyombo vizuri vya kioo vilivyoingizwa kutoka Uajemi, vyombo vya udongo vya China na vifaa vya udongo kutoka India, mapambo ya shaba na mazulia kutoka Mashariki ya Kati. Utajiri huu ulitofautiana kabisa na maisha ya taabu ya wakazi wenyeji ambao wakati mwingine walichukuliwa utumwani.

Taarifa zinazotokana na Wachina zinaeleza kuhusu nyumba za ghorofa nne au tano katika mji wa Kilwa, "mji mmojawapo kati ya miji mizuri kabisa ulimwenguni" katika kame ya kumi na tano. Huo ni wakati Wachina walipofika kwa wingi katika ukanda huu, ingawa kuna taarifa pia kuhusu Waafrika waliofika China mapema sana kwenye kame ya saba. Hata hivyo, mnamo 1402, ramani ya Kikorea ilionyesha mchoro wa kusini mwa Afrika ambao haakuwa wa ki-Ptolemi. Katika kame ya kumi na tano, meli kubwa kubwa, mara tano ya vyombo vya Kireno, zilizoongozwa

na Cheng Ho, zilibeba bidhaa tunu za Kiafrika kupeleka China, ambazo ni dhahabu, pembe za ndovu, na watumwa. Cheng Ho alirejea kutoka Malindi, akifuatana na ujumbe uliowasilisha kwa mfalme wa Beijing zawadi ya twiga. Baadaye ghafla, safari hizi za kigunduzi za Wachina zilikoma kutokana na matatizo ya ndani.

Wakati huu ndipo, katika 1488, Bartolomeo Diaz aliposafiri kuzunguka ncha ya kusini kabisa mwa Afrika na kugundua umbo la kijiografia tofauti na lile lilionyeshwa katika 'ramani' ya Ptolemy. Hatimaye sasa, Ulaya ikaingia katika Bahari ya Hindi. Mnamo 1498, Vasco da Gama alishuhudia kidogo utukufu wa dola za Kiafrika katika nyanda za juu za Zambezi, na akavutiwa sana na ubora wa mavazi ya "mabwanyenye" wa Kiswahili. Alikirimiwa vizuri na sultani wa Mombasa, na akaondoka mara moja kuelekea India, safari iliyoongozwa na mwandishi Mwarabu wa chati za baharini, Ibn Masjid. Haya yalikuwa mapambazuko ya kipindi kipya.

Kuishika Atlantiki na athari zake kwa Afrika

Waarabu na Wazungu hawakufahamu sana Madeira, Azores na Visiwa vya Kanari. Katika karne ya kumi na moja, Al-Bakri anaeleza kuhusu uzalishaji wa kaharabu katika pwani ya Atlantiki ya Ghana, na Al-Idrisi anaeleza kuhusu biashara ya chumvi baina ya Awlil na Senegal. Sababu hasa za ushindi wa Wazungu katika Atlantiki hazitokani na uhodari wao wa kiteknolojia. Katika karne ya kumi na mbili, msafara wa meli za kivita wa Wamohadi ulisifika na kumfanya hata Salah al-Din atake msaada wa msafara huo dhidi ya vyombo vya Wakristo. Lakini mwishoni mwa karne ya kumi na tatu, baada ya ushindi wa Wazungu katika vita vya Jibraltar na kutwaliwa mabepari kwa maeneo yaliyokuwa muhimu katika uzalishaji wa mbao za kutengenezea meli kwa ajili ya viwanda vya kuundia meli, uwiano na nguvu ya utawala ukabadilika. Wafadhili wahogharimia ujenzi wa meli walikuwa mabepari binafsi waliofaidika kutokana na kukua kwa uchumi kuanzia 1200 hadi 1600. Misafara ya meli ya Wagenoa, na baadaye Wavenisi, iliunganisha biashara za Italia na viwanda vya Filandia na Uingereza. Waislamu hawakuitikia changamoto hii, huenda kwa sababu ya udhaifu wa wafalme za Maghrib, au kwa sababu misafara yao ilishaleta dhahabu nyingi zaidi kuliko ile ambayo ingeweza kuletwa na meli ndogo. Hivyo, Waarabu hawakuwa na motisha, jambo lililowawezesha Wazungu kupiga hatua hadi Rasi ya Bojador kwenye mwambao wa Sahara magharibi, baada ya jitihada nyingi sana. Kilichowavutia zaidi kuliko dhahabu ya Sudan kilikuwa ni nchi mpya zenye joto la kutosha kwa uzalishaji mkubwa wa ngano, zabibu na miwa. kumi na tano, meli kubwa kubwa, mara tano ya vyombo vya Kireno, zilizoongozwa

kumi na tano, meli kubwa kubwa, mara tano ya vyombo vya Kireno, zilizoongozwa na Venisi. Lakini hapakuwa na taratibu za uwekezaji na za mauzo, na baada ya mafanikio makubwa, Moroko ya Saad ikashindwa kuendelea. Wenyeji wa Visiwa vya Kanari walifanywa watumwa na Wazungu, ambao polepole walichukua nafasi ya Moroko.

Kusini ya Rasi ya Bojador

Hili ni eneo la Atlantiki lenye pepo za msimu na lisilo na vimbunga. Vipingamizi vingi vilikwamisha jitihada za kuelekea kusini zaidi ya rasi hii. Kutoka hapa hadi Kongo ilichukua miaka hamsini. Vilevile ilikuwa vigumu kwa meli zilizosafiri zaidi ya Rasi ya Bajador kurejea. Izingatiwe kwamba majaribio mengi ya kugundua njia hii ya bahari yaliishia katika maafa na kujitoa muhanga. Utafiti wa kisayansi na kifundi ambao mara nyingi uliegemezwa katika mafanikio ya Waarabu, ulikuwa wa lazima ili kutengeneza majahazi madogo na rahisi kuongoza yaliyofaa katika njia hii. Baadaye merikebu zilitumika badala ya majahazi haya kabla hazijabadiliwa na majahazi makubwa. Wareno, wakiwa wamekasirika kwa kushindwa kugundua chungu ya dhahabu, waliyokiota kwa muda mrefu, wakadunisha bara hili kwa kulifanya mgavi wa "nguvu kazi nyeusi" iliyopelekwa Amerika, mabara yaliyoonekana kuwa yana dalili njema za kuwaletea faida. Vilevile wakati huu Asia ilizidi Afrika kwa umaarufu.

Kwa mujibu wa Al-Umar, mtawala wa Mali, Mansa Kanku Musa aliarifu kwamba, mtawala aliyemtangulia hakuamini kwamba bahari haivukiki. Akaunda na kupelcka vyombo 200. Haya yalikuwa maafa makubwa ambayo hatimaye yalimwangamiza yeye mwenyewe. Je, kutokana na taarifa hizi, tunaweza kuhitimisha kwamba katika karne ya kumi na nne Wamali waligundua Marckani kabla ya Kolumba. Labda hili si kweli, ingawa kuna madai hayo, na Waafrika walilijua sana eneo fulani la bahari, angalau kwa ajili ya biashara ya mwambao. Lakini ukubwa wenyewe wa bara hili na hali halisi ya mazingira ya pwani havikuwaruhusu Waafrika kuitamani bahari. Vituo vikuu vya utawala vilikuwa bara, isipokuwa katika Afrika Kaskazini, pwani ya mashariki na pengine Kongo. Ni muhimu basi, kutambua shauku hii ya mtawala wa Mali, yenye kuakisi mtazamo wa kisayansi, sawasawa na juhudi zilizofanywa na Wazungu wakati huo, lakini ambayo haikuwa na nyenzo wala jadi ya kuiendeleza.

Upanuzi, kutoridhika, matumizi ya mali asili

Wareno walipofahamu mbinu za kurejea kwa kupitia Azores, walitumia miaka hamsini na nne kufika kwenye Rasi ambayo waliipa jina la *Good Hope* (Matumaini

Mema). Rasi hiyo waliizunguka na kuingia katika Bahari ya Hindi. Mwanzoni walifanya ukatili, wakateka nyara pamoja na kukamata watumwa, lakini baadaye upanuzi ukafanyika katika vituo vya biashara vilivyoshughulika na bidhaa za gundi, ngozi na kaharabu. Baadaye wafalme wakaruhusu wafanya biashara binafsi kushiriki katika biashara hiyo, huku wakijaribu kupambana na ushindani wa nchi nyingine za Ulaya.

Kutoridhika kukaongezeka: Meli chache na ndogo kutoka katika nchi ndogo hazingeweza kupata faida kubwa. Jitihada za kuingia ndani zaidi ya nchi zilikwamia mapindi ya Felou katika mto Senegal, maporomoko ya Yelada katika mto Zaire au kwa kukabiliwa na upinzani wa wenyeji, kama ilivyotokea Wadane; au pia kutokana na vikundi vya wafanya biashara vilivyokuwapo kama kule Kantor, huko Gambia, walipokutana na wafanya biashara Wajuula. Msako wao wa dhahabu ilikuwa kazi bure. Meli ndogo zilisafirisha kama moja ya tano na hata pengine moja ya saba ya dhahabu iliyoendelea kubebwa na ngamia kuvuka Sahara. Mara "malagueta" na pilipili manga kutoka Benin zikaingia katika ushindani na pilipili zitokazo Asia. Ni mauzo ya fedha, nguo, farasi na shaba tu yaliyofanya mizania ya biashara iendeleo bila kuyumba.

Aidha katika kiwango cha kisiasa na kidini, Wareno walimtafuta bila mafanikio Presta Yohana, wakifikiri kwanza kwamba wangempata huko Mossi, baadaye Kongo... Lakini hapakuwa na alama yoyote ya utawala wa Kikristo hadi mbali kabisa Ethiopia.

Kwa upande mwingine, katika kiwango cha sayansi, mafanikio maridhawa yalipatikana kutokana na uchunguzi wa manahodha wa meli, wafanya biashara au wamisionari waliochunguza kuhusu mvua za majira ya joto, ruwaza za pepo, hasa pepo za msimu, na uchunguzi wa awali wa kiethnografia na kianthropolojia. Wakati mwingine taarifa zao zilianiinika, kama vile katika Kongo, wakati mwingine taarifa hizo zilionyesha upendeleo wa wachunguzi; kwa mfano, uchunguzi uliofanyika kuhusu "miungu iliyoabudiwa" na wenyeji.

Kwa upande wa kilimo, matumaini ya kuanzisha makoloni pamoja na kuhamisha watu, mbinu za kilimo na mimea ambayo ingezozwa mazingira mapya, yalikuwenda kinyume na mazingira halisi ambayo yalisabisha vifo na kujenga hofu miongoni mwa watu. Wazo la "kutengeneza sukari" lilitokea Sao Tome, eneo lililokaliwa mnamo 1472. Ilihujika kupeleka watumwa weusi huko na baadaye kuwahamishia katika visiwa vingine vya "Mediterrania ya Atlantiki" ili kufanikisha azma hiyo.

Kuanzia 1440 na kuendelea, Zurara katika kitabu chake kitwacho *Tarihi ya Uvumbuzi na Utiishaji wa Guinea*, alirejelca laana la Nuhu kwa mwanawe Ham, ambaye anadaiwa kuwa ni chimbuko la watu weusi. Hata hivyo aliongeza kuwa, licha ya mambo yote, watu hawa weusi walikuwa na roho na hawakuwa Waislamu, hivyo "ingekuwa rahisi kuwaongoza katika njia ya wokovu." Kwa ufupi, hizo

zikawa sababu mbili za wazi za kuanzisha biashara ya watumwa na dhamira safi kabisa.

Mnamo 1444, ilianzishwa kampuni katika Lagos na Ureno kufanikisha biashara ya watumwa na kuanzisha kituo katika Arguin, ambacho kilianza mara moja kutoa watumwa mia kadhaa kwa mwaka. Baada ya 1460, watumwa wapatao 1,000 kwa mwaka walichukuliwa kutoka maeneo kati ya Cape Verde na Sine Salum (Senegal). Huo ulikuwa mwanzo wa mzunguko wa jahanamu. Wakati huu Kastile ilitambua ukiritimba wa Ureno katika biashara hii. Hata hivyo, kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tano utaratibu wa biashara ulitengemaa, hali kadhalika bei: watumwa sita waliuzwa kwa farasi mmoja, bei ambayo polepole ilibadilishwa kwa mikuo ya shaba. Kwa karne kadhaa, biashara ya watumwa Waafrika, iliyochukua nafasi ya biashara ya kinjozi ya dhahabu, ikawa ni biashara iliyowapatia wazungu faida kubwa kabisa katika Afrika.

Katika kipindi chote cha karne ya kumi na tano, Afrika ilijitenga na vituo vya biashara ya watumwa vilivyosimamiwa na mawakala Waafrika wenyeji, walioitwa "wafalme". Kulikuwa na hali mbalimbali zilizoonyesha kujitoa katika biashara hii: Haikuwezekana kuwa na mawasiliano na Mansa wa Mali; uhusiano na Mfalme Nkuwu wa Kongo uliendelea kuwa na utata hadi alipoikana imani ya Ukristo baada ya kupokea maseremala wachache, waashi na wafugaji kwa muda mfupi. Dini ya asili ilitoa upinzani mkubwa.

Hata hivyo, matokeo mabaya ya biashara hii ya wanadamu yalikuwa na madhara ya muda mrefu katika miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ya Afrika. Kwa mfano, hadi wakati huo, kwa kupiga marufuku biashara ya chuma ya Senegambia, Mali ilijihakikishia uhibititi wa pwani ya Gambia na Kasamansi, na kuacha jimbo la kaskazini zaidi chini ya mamlaka ya Jolof. Lakini mauzo makubwa ya chuma yaliyofanywa na Wareno kwa Jolof yalibadili uwiano huu wa biashara. Kwa upande mwingine, Burba (mtawala) wa Jolof, aliyetambuliwa na madola ya Kajor na Baol, aliacha biashara ya ndani ambayo hapo awali aliitegemea na kununua farasi pwani kwa kubadilishana na watu. Lakini kwa msingi huu, Kajor na Baol ziliweza kuitumia haraka hali ya kijiografia kuuangusha utawala wa Jolof.

Kijamii, biashara ya watumwa ilirahisisha na kuchochea mifarakano ambayo hapo awali jamii zilijitahidi kuisawazisha. Mamlaka yakahodhiwa na mtu mmoja, na hata kuegemezwa katika mahusiano ya kitumwa, ambapo hapo awali mateka wa vita, wa madeni na njaa, waliingizwa katika mtindo wa uzalishaji ambao haukucndeshwa katika mahusiano hayo. Utawala katika dola, ambao hapo awali ulikuwa na sifa ya utukufu, sasa ukadharauliwa kijamii na kimaadili. Katika Senegambia, hali hiyo ndiyo inayoeleza jinsi watu walivyofuata Uislamu, kama njia ya kuzishutumu tawala zilizokosa uelekeo, tawala ambazo punde zingeanza kupigana zenyewe kwa zenyewe katika vita vya kugombea watumwa.

Juzuu hili linamalizikia wakati ambapo upanuzi na ushindi wa Ulaya ulimwenguni unaanza, na hivyo kufungua sura mpya katika historia. Mbinu mpya zilikuwa zinafungua milango ya Bahari kubwa ya Atlantiki kwa harakati za Ulaya, haya yakiwa matokeo ya kulinyonya bara la Afrika. Historia ilionekana kuipa mgongo Mediterania, ziwa la kale lililo katika kitovu cha Ulimwengu Mkongwe. Waitalia, ambao walijaribu kwa woga kufika Sudan kwa kuvuka jangwa walitwaliwa nafasi na jirani zao Wahispania na Wareno "waliovumbua" Amerika na kuzunguka Afrika hadi kufika Asia. Haikuwa miujiza kwamba wagunduzi hawa walikuwa ndio wale wale waliopata urithi wa kisayansi wa zamani za kale, uliojengwa na Waarabu Waberiberi na kuvushwa Afrika kwenda Ulaya wakati bara hilo lilipoanza kuzinduka.

Kuanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita, Afrika iliongoza katika uchumi wa ulimwengu. Marekani ilipogunduliwa Afrika ikasukumwa kando na kutumiwa tu kama chombo. Katika kipindi kinachojadiliwa katika juzuu hili, ni muhimu kuisisitiza mambo makuu matatu.

Vipengere vya kidini na kisiasa

Afrika ya watu weusi ilionyesha haiba kubwa katika kipindi hiki. Kwanza, kuhusiana na mifumo ya kidini na kisiasa iliyokuwa ikienea katika eneo hilo. Uislamu uliweza tu kupokewa na umma baada ya kufanyiwa marckebisho, vinginevyo ungebaki kama pambo tu kwa ajili ya wafalme, wasomi na wafanya biashara. Vilevile, Ukristo ukaingiza Uafrika, kama vile katika Ethiopia; ambapo pia ulipata upinzani kama ilivyokuwa katika Kongo. Katika karne ya kumi na tisa, vita vitakatifu vya Kiislamu na upanuzi wa Ukristo vilikuwa bado vinaendelea. Dini ya asili iliweza kuendelea kuwa na nguvu, hata katika asasi na miviga iliyohusiana na

utawala katika Kumbi, Nyani, na Yatenga, Kanem na Mwenemutapa. Lakini uvumilivu ulikuwa ndiyo sheria iliyowezesha Mali na Ethiopia kuchanganya watu tofauti wenye dini mbalimbali.

Kanuni hii hii ilifaa kutumiwa katika miundo ya kisiasa iliyounganisha koo na makundi ya kiamali katika mfumo wa uhusiano huenda haukuwa imara lakini ulikuwa umerasimishwa. Katika Aftika Kaskazini hata falme zenyewe zilikuwa ni nukusanyiko ya "makabila" chini ya "kabila" la mtawala. Vivyo hivyo, katika Mali, Mossi na Rwanda, Afrika iliunganisha watu waliogawanyika mno katika maeneo makubwa. Zaidi ya yote hayo ilikuwa katika karne ya kumi na saba ambapo tabia ya kujitawanya na kuzuka kwa falme za makundi ya kikabila zilijitokeza. Tabia hii iliendelezwa zaidi katika Aftika Kaskazini baada ya jitihada kubwa za kuunganisha watu zilizofanywa na Wamohadi. Zaidi ya hayo, katika kipindi hiki, Uislamu, ambao hapo awali ulikuwa ukiendeleza ushindi, ukabakia kujilinda mbele ya ushindi wa Wakristo. Wakristo wakashikilia Mediterania kusini, na kuzunguka eneo la Waislamu kupitia Atlantiki na baadaye kuingia katika Bahari ya Hindi, njia ambayo hapo awali ilizibwa na Waayubi na Mamluki. Ni kweli kwamba katika Nubia Ukristo ulifutwa baada ya mapambano ya muda mrefu. Lakini hali hiyo ilitokea hasa kwa sababu Ukristo ulikuwa ni dini ya wateule waliohusiana na viongozi wa kanisa wa Kikhufu na utamaduni wa kigeni ambao haukuwa na watakatifu au mashahidi wenyeji, ingawa sanamu katika makanisa zinaonyesha sura nyeusi za maaskofu wa Kinubi. Lakini upinzani uliodumu kwa karne nyingi kutoka katika miviga ya kiasili vilevile ulikuwa ni ukweli wa kihistoria hapa pia. Mwisho, tabia ya vyanzo vya maandishi ya Kiarabu ya kuegemea upande mmoja kuhusu Sudan ya Wanilo, mara nyingi ilisababisha msisitizo mkubwa katika kipengele cha kaskazini kuliko maendeleo ya wenyeji katika eneo la Waafrika weusi. Hata katika majangwa na misitu ambayo ilikuwa haijaguswa, koo na makundi yaliyotofautiana sana yalikuwa yakiishi kwa ushirikiano na watu wa makabila mengine kwa mabadilishano ambayo pengine hayakuwa ya usawa, kama ilivyokuwa kwa Watuaregi, Mbilikimo, Wakhoikhoi na Wasan.

Hivyo kabla ya 1600, Afrika ilikuwa na aina zote za miundo ya kisiasa, kuanzia koo hadi dola, hali inayomaanisha kuwepo uzocfu anuwai na utajiri mwingi wa kisiasa.

Katika Afrika ya kati, na kusini, ambako sera ya ubaguzi wa rangi ilizuia ujuzi wa maarifa ya kale ya Afrika, ushahidi wa kiakiolojia na kūsimu unatoa fununu kuhusu suala hilo. Makaburi makuu yaliyopo Sanga na Katoto, kusini kidogo ya dola la Luba, ni ushahidi wa utaratibu fulani wa kisiasa, mabaki dhahiri ya chombo cha kisiasa kilichofafanuliwa vizuri. Makaburi haya yalikuwepo tangu kabla ya mwaka 1000. Ukale huuwa wa mfumo wa dola, katikati ya bara la Afrika, usioingiza athari zozote zisizo za Kiafrika, unaonekana katika ukanda wa Maziwa

Makuu katika makundi ya Wabantu. Ni kumbukumbu inayoakisi ukale wa tajiriba wa binadamu katika Afrika. Ni ukale wa madola kama ya Luba ambao kwa hakika unahusika katika kuenea kwa lugha nyingi za kundi hili kutoka Kasai mashariki hadi Zambia. Licha ya uporaji katika makaburi ya wafalme wa ustaarabu wa Zimbambwe-Mapungubwe, ubora unaodhihirika katika majengo yao makubwa ya mawe ya mjengo halisi wa kienyeji unafanana na ule wa majengo yaliyoko Manykemi katika Msumbiji au yale ya Transvaal ya kale. Aidha, Mapungubwe ilifanikiwa kuonisha utamaduni wa Kibantu na ule wa Wakhoikhoi ambao haakufahamika sana hapo awali. Uenezi wa chuma hapa ulikamilika mapema kabla ya karne ya kumi, na pengine hata kabla ya kipindi cha Ukristo, na ustaarabu wa Mapungubwe ulisitawi hadi karne ya kumi na tano, wakati ulipoathirika vibaya, na hatimaye kuhasirika, kutokana na pigo la biashara ya watumwa.

Vipengere vya kiuchumi na kitamaduni

